**ANTHROPOSENIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI ZA *BUSTANI YA EDENI, VIPULI VYA FIGO, MAFUTA* NA *WALENISI***

**ANTONY KAGO WAITHIRU**

**Tasnifu hii Imewasilishwa kwa Shule ya Mafuzu ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili na Mawasiliano ya Chuo Kikuu cha Laikipia.**

**OKTOBA, 2025**

## IKIRARI

### IKIRARI YA MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo hiki wala kingine au kutolewa popote kwa mahitaji ya Shahada yoyote ile katika chuo chochote kile.

______________________________ ______________________________

**Antony Kago Waithiru** **Tarehe**

**MDK32/2614/20**

### IKIRARI YA WATAHINI

Tasnifu hii imetolewa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri walioteuliwa rasmi wa chuo hiki.

______________________________ ______________________________

**Prof. Wendo K. Nabea** **Tarehe**

**Chuo Kikuu cha Laikipia**

**Idara ya Usomi wa Lugha, Fasihi na Mawasiliano**

______________________________ ______________________________

**Prof. Sheila Wandera Simwa** **Tarehe**

**Chuo Kikuu cha Laikipia**

**Idara ya Usomi wa Lugha, Fasihi na Mawasiliano**

## HAKI ZA KUHIFADHI UCHAPISHAJI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili au kutoa sehemu ya tasnifu hii au nakala nzima kwa njia yoyote ile bila idhini mahsusi katika maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Laikipia.

# TABARUKU

Utafiti huu na matokeo yake natabaruku kwa babangu mlezi Askofu Charles Mirie Kago na kwa wataalamu – akiwemo Prof Wendo Nabea, Prof James Ogola Onyango na wengine wengi – na wanafunzi wote wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Laikipia na ulimwenguni kwa jumla.

## SHUKRANI

Ningependa kuwashukuru watu wote waliochangia ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine. Siwezi kudai kwamba jitihada zangu pekee zingewezesha kufua dafu bila mchango wa wengine wengi. Tasnifu hii isingekamilika bila ushauri na usaidizi wao.

Kwanza, namshukuru Mungu Muumba Mwenyezi aliyenijalia uhai, siha njema, stahamala na ukakamavu. Pasi ya Mola, kazi hii haingefana kamwe. Pili, nachukua nafasi hii adimu kutoa shukrani kwa usimamizi wa Chuo Kikuu cha Laikipia kwa kunikubali na kunisajili kuwa mwanafunzi wa shahada ya uzamifu. Tatu, namshukuru mkuu wa Idara ya Usomi wa Lugha, Fasihi na Mawasiliano (LITCOM) katika Chuo Kikuu cha Laikipia wakati nilipoanza kazi hii, Prof. Eliud Kirigia kwa kuikubali nia yangu ya kujiendeleza kimasomo katika idara na ushauri alionipa.

Nne, natoa shukrani zangu tumbitumbi kwa wasimamizi wangu, Prof. Wendo K. Nabea na Prof. Sheila Wandera Simwa walionishauri, kunihimiza na kunielekeza tangia mwanzo wa safari hii ya kiakademia. Namshukuru Prof. Ogola kwa kunisaidia kupiga msasa anwani ya utafiti huu na kuhakikisha kuwa malengo ya utafiti huu yanalenga ndipo. Kwa ujumla nawapongeza wasimamizi wangu kwa kulipitia pendekezo la utafiti likiwa bichi sana, ushauri wao ulinifaa kulipiga pendekezo msasa, kulipika hadi likaiva na hatimaye nikalitetea katika idara na kitivo kwa ufanisi. Nawashukuru kwa kusoma miswada ya tasnifu, kuirekebisha huku wakinipa ushauri na mwongozo mwafaka uliofaulisha tasnifu hii. Bila msaada wa wasimamizi hao ningesalia nikitapatapa katika giza na tope la kutojua bila ya kukwamuliwa. Shukrani tele ziwaendee wahadhiri wote wa Idara ya Usomi wa Lugha, Fasihi na Mawasiliano, wakiwemo Prof. Khasandi, Prof. Kamau, Dkt. Mahero, Dkt. Mwithi na Dkt. Nderitu, ambao walinisaidia kwa mawazo mengi yaliyoniongoza katika masomo yangu. Mungu awabariki na awape siha njema, upendo, maarifa mwafaka na hekima.

Kwa wote niliowataja na wengine wengi ambao sijawataja naamba, SHUKRAN BELELE!! Barikiweni nyote!

## IKISIRI

Riwaya ya Kiswahili ni mojawapo wa tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili. Utanzu huu umedhihirisha, kwa njia moja au nyingine, masuala ya bayotiki na ikolojia kimwavuli. Suala la anthroposenia ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Hii ni kwa sababu binadamu anakumbana na masuala mazito ya kiikolojia katika mazingira yake kila siku. Masuala haya ya anthroposenia ni ya kisayari na yanafungamana na ubepari, ubinafsishaji, uhuluti wa tamaduni na upujufu wa mifumo ya kiikolojia. Riwaya ya Kiswahili ilitathminiwa ili kubaini mchango wa anthroposenia katika kukabiliana na changamoto zinazopaliliwa na kuzalishwa na upujufu wa mazingira. Mchango wa riwaya ya Kiswahili katika anthroposenia ungali na mengi yaliyosalia kushughulikiwa. Hivyo, utafiti huu ulichunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule. Hizi ni *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo* zilizotungwa na Emmanuel Mbogo na pia *Mafuta* na *Walenisi* zilizotungwa na Katama Mkangi. Riwaya hizi zilichaguliwa kimakusudi kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Madhumuni hayo yalikuwa ni; kupambanua aina za anthroposenia katika riwaya hizi nne, kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya hizi kisha kutathmini rai za watunzi wao kuhusu mbinu bora za kukabiliana na anthroposenia. Eneo la utafiti lilikuwa maktabani hivyo utafiti ulifanyiwa katika maktaba za umma na ya vyuo vikuu vya umma na vya kibinafsi. Utafiti uliongozwa na nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira iliyoendelezwa na Glotfelty na Fromm, pamoja na Buell. Mihimili ya nadharia hii iliyoongoza uchanganuzi wa data ni kama vile; haki za mazingira, utamaduni na mazingira, maendeleo endelevu, uwezo na kifo, na uongozi mbaya. Muundo wa utafiti ulikuwa ni wa kimaelezo. Data ya utafiti ilikuwa ni maudhui ya kimazingira katika riwaya nne zilizoangaziwa mintarafu ya madhumuni ya utafiti. Njia kuu ya utafiti ilikuwa ya kithamana ambapo matumizi ya upekuzi-changanuzi yalitekelezwa. Mtafiti alisoma riwaya teule, akatongoa yaliyomo kisha kuyachanganua akiongozwa na baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Uhakikimazingira. Uchanganuzi wa data ulihusisha mbinu ya kithamana. Matokeo yalibaini aina za anthroposenia kama zifuatazo: binadamu, mawakala wa anthroposenia, vifaa vinavyotumiwa na binadamu, vurugu za mazingira kutokana na binadamu, jiografia ya binadamu, na mabeberu wa kisasa. Kadhalika, matokeo yalidhihirisha mbinu kadhaa zilizotumika kusawiri anthroposenia kama zifuatazo: Taashira, taswira, ishara, majazi, tashtiti, na tashihisi. Isitoshe, matokeo yalibainisha rai za waandishi kuhusu namna ya kukabiliana na anthroposenia kama zifuatazo: vyombo vya habari na uhamasishaji wa uendelevu, nafasi ya ukakamavu na utu katika ulinzi na uhifadhi wa mazingira, matumizi madhubuti ya rasilmali asilia, nafasi ya mashairi na nyimbo katika kuizindua jamii na matumizi pevu ya akili katika uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu unatarajiwa kuwa na natija kwa kuongeza kanoni ya anthroposenia kwa wasomi, wahakiki na watafiti wa masuala ya anthroposenia. Kadhalika, utafiti huu unaongeza data kuhusu jinsi waandishi wa fasihi ya Kiswahili wamewajibikia mazingira na hivyo ni hazina katika nadharia ya Uhakikimazingira wa Kiafrika.

## ABSTRACT

The Kiswahili novel is one of the genres of written literature. The novel has demonstrated a variety of biotic and ecological issues. Anthropocene is a crucial issue that should be at the core of every human activity. This is as a result of the fact that humanity is facing major ecological issues in multifaceted spheres. These anthropocenic concerns are planetary in scale. They include expansion of global capitalism, eurocentricism, reterritorialization and the degradation of ecosystems. Nonetheless, there is a dearth of literature on the contribution of the Kiswahili novel to anthropocene. This research therefore, set out to examine the representation of anthropocene in selected Kiswahili novels, namely *Bustani ya Edeni* and *Vipuli vya Figo* by Emmanuel Mbogo, as well as *Mafuta* and *Walenisi* by Katama Mkangi. Informed by purposive sampling, this research engaged four literary works whose thematic and contextual significance most effectively advanced its central objectives and interpretive concerns. In particular, the research sought to achieve the following objectives: To demonstrate the typologies of athropocene in the selected novels, to explore the styles employed in portraying anthropocene and to interrogate the authors' narrative perspectives to mitigate the socio-ecological challenges inherent in anthropocene. Through purposive sampling, four literary works were selected for their relevance to the study's objectives and interpretive focus. Primarily library-based, this inquiry adopted a qualitative design to examine the representation of anthropocenic themes in the novels. The research was hinged on the Ecocriticism theory as espoused by Glotfelty, Fromm and Buell. The tenets of the theory that underpinned the research included environmental rights, tradition and environment, sustainable development, power and death, and poor leadership. The findings demonstrated typologies of anthropocene such as: Human beings, agents of anthropocene, tools and technologies used by humans, environmental violence perpetrated by humans, human geography, and modern imperialists. Similarly, they revealed a number of styles that were employed in portraying anthropocene. These included the use of symbolism, imagery, signs, metaphor, satire, and shifting narrative perspectives to depict human-nature entanglements through personification. Further, the study established the authors' perspectives on approaches to addressing the challenges of anthropocene. These comprise promoting media engagement and public awareness on sustainability, fostering resilience and human dignity in environmental protection, ensuring the efficient use of natural resources, harnessing poetry and music to awaken ecological consciousness. and employing knowledge in safeguarding the environment. This investigation is anticipated to contribute to the growing canon of anthropocene, thereby advancing critical conversations on literary representations of ecological and existential transformation. In addition, it will make an invaluable contribution in Kiswahili literature specifically on African ecocriticism.

**YALIYOMO** **UKURASA**


**IKIRARI** …....…………………………..……………………………………………...... i
**HAKI ZA KUHIFADHI UCHAPISHAJI**...………………………….………………… ii
**TABARUKU** ……………………………………………………….……………...... iii
**SHUKRANI** ………………………………………………………………………… iv
**IKISIRI** ………………………………………………………….................………… v
**ABSTRACT** ………………………………………………………………………… vi
**YALIYOMO** ………………………………………………………………………... vii
**VIFUPISHO VYA MANENO** ............................................................................... xi
**UFAFANUZI WA ISTILAHI** ............................................................................... xii
**SURA YA KWANZA**……………………………………………….………………… 1
1.0 **UTANGULIZI** …………………………..…………………………….……….. 1
1.1 Usuli wa Mada ………………………………………………….………………. 1
1.2 Suala la Utafiti ………………………………………………….………………. 6
1.3 Madhumuni ya Utafiti..……………………………………………..…………… 6
1.4 Maswali ya Utafiti ………………………………………….............................. 7
1.5 Umuhimu wa Utafiti ……………………………………………..………... 7
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti …………………………………………..……...... 9
1.6.1 Upeo wa Utafiti ......................................................................................... 9
1.6.2 Mipaka ya Utafiti ....................................................................................... 9
**SURA YA PILI**…………………………………………………………….………... 10
2.0 **MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA NADHARIA** …………….………... 10
2.1 Utangulizi ……………………………………………………………..………… 10
2.1.1 Aina za Anthroposenia …......................................................……..……… 10
2.1.2 Mbinu Zilizotumiwa Kusawiri Anthroposenia …...............………...……... 19
2.1.3 Rai za Waandishi wa Kazi za Fasihi Kuhusu Jinsi ya Kukabiliana na Anthroposenia ...................................................................... 23
2.2 Msingi wa Nadharia ……………………………………………………..……… 27
2.2.1 Nadharia ya Uhakikimazingira ………………………………….................. 29
**SURA YA TATU** ………………………………………………………………….… 40
3.0 **MBINU ZA UTAFITI** ……………………..…...…………………………...…….. 40
3.1 Utangulizi ………………………………..………………………….……... 40
3.2 Muundo wa Utafiti ……………………………..……………………….……. 40

3.3 Njia za Utafiti ……………………………………..……………………………… 40
3.4 Eneo la Utafiti …...………………………………..………………................... 41
3.5 Kikundi Lengwa ……………………………………...…………………………. 41
3.6 Uteuzi wa Sampuli….…………………….……………..……………………… 42
3.7 Mbinu za Kukusanya Data ………………………….…..……………………… 42
3.8 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji ………….……………..….……….…... 43
3.9 Masuala ya Kimaadili ........................................................................................ 44
**SURA YA NNE**……………………………………………………………….…….. 45
4.0 **UCHANGANUZI WA AINA ZA ANTHROPOSENIA** ………...……………….……….. 45
4.1 Utangulizi ……………………………………………………………….……... 45
4.2 Binadamu ……....................…………………………………………………….. 45
4.2.1 Binadamu Kupitia Shughuli za Kiuchumi na Utabaka ………….....……….. 46
i. Uchafuzi wa Mazingira...…………………………………………………… 47
ii. Athari za Mtu kwa Mwenzake ………....…………………………………….. 48
iii. Tamaa na Ubinafsi ……………………………………………………………. 52
4.2.2 Binadamu Kupitia Utovu wa Utu na Maadili ……......………………...… 55
i. Shughuli za Nyumbani ........................................................................ 55
ii. Athari za Ulofa ..................................................................................... 57
iii. Utowajibikaji ........................................................................................ 62
iv. Ukatili .................................................................................................... 67
4.2.3 Binadamu na Maendeleo ............................................................................. 70
4.2.4 Binadamu Kupitia Utumwa wa Kimawazo na Kiutawala ............................. 73
i. Utumwa wa Utawala ............................................................................. 73
ii. Utumwa wa Kimawazo ......................................................................... 75
4.3 Mawakala wa Anthroposenia .............................................................................. 80
i. Wanyama ................................................................................................. 80
ii. Wadudu ................................................................................................... 82
4.4 Matumizi ya Vifaa ................................................................................................ 85
4.4.1 Fedha ................................................................................................................ 90
4.5 Vurugu Dhidi ya Mazingira na Binadamu ............................................................ 92
4.6 Jiografia ya Binadamu ........................................................................................... 95
i. Shughuli za Kiuchumi ..................................................................................... 95
ii. Uongozi na Utawala Dhalimu ......................................................................... 97

iii. Utambulisho Tepetevu ... 102
iv. Uchafuzi wa Hewa ... 103
v. Mahakama na Janibu za Binadamu ... 104
4.7 Wafisadi ... 114
4.8 Mabeberu wa Kisasa ... 118
i. Uharibifu wa Mazingira ... 118
ii. Udhibiti wa Utawala na Uchumi ... 120
iii. Ghashi za Viongozi ... 126
iv. Lugha na Ubaguzi ... 129
4.9 Mabepari ... 132
4.10 Utepetevu wa Binadamu ... 141
i. Dini ... 141
ii. Moto ... 148
iii. Sheria ... 150
4.11 Viongozi Wabaya ... 151
**SURA YA TANO** ... 156
5.0 **UCHANGANUZI WA MBINU ZINAZOSAWIRI ANTHROPOSENIA** ... 156
5.1 Utangulizi ... 156
5.2 Taashira ... 156
5.2.1 Taashira ya Mahali ... 157
5.2.2 Taashira ya Vifaa ... 158
5.2.3 Taashira ya Viumbe ... 168
5.2.4 Taashira ya Udhalimu ... 180
5.2.5 Taashira ya Ulofa na Ndwele ... 185
5.2.6 Taashira ya Hali za Maumbile ... 191
5.3 Taswira ... 197
5.4 Ishara ... 208
5.5 Majazi ... 217
5.6 Tashtiti ... 225
5.7 Tashihisi ... 226
**SURA YA SITA** ... 229
6.0 **UCHANGANUZI WA RAI ZA WAANDISHI WA RIWAYA NNE TEULE** ... 229
6.1 Utangulizi ... 229

6.2 Vyombo vya Habari na Uhamasishaji wa Uendelevu .................................................. 229
6.2.1 Vyombo vya Habari vya Chapa na Ufanisi wa Mazingira .................................... 230
6.2.2 Vyombo vya Habari vya Kielektroniki na Ufanisi wa Mazingira ......................... 235
6.3 Kupambana na Uchafuzi: Nafasi ya Ukakamavu katika Ulinzi wa Mazingira ............ 236
6.4 Nafasi ya Utu katika Uhifadhi wa Mazingira: Sauti ya Mwandishi ............................ 239
6.5 Ushirikiano na Ujasiri katika Uhifadhi wa Mazingira: Mtazamo wa Mwandishi ......... 248
6.6 Matumizi Madhubuti ya Rasilimali Asilia: Mtazamo wa Mwandishi .......................... 253
6.6.1 Thamani ya Maji katika Ustawi wa Mazingira .................................................... 253
6.6.2 Maumbile kama Msingi wa Mazingira Endelevu ................................................ 256
6.7 Nafasi ya Mashairi na Nyimbo katika Kuizindua Jamii ............................................... 256
6.8 Mwandishi na Maandamano: Kutetea Uhifadhi wa Mazingira .................................... 262
6.9 Elimu kama Ala ya Uhifadhi wa Mazingira: Mtazamo wa Mwandishi ....................... 266
i. Elimu ya Utafiti .......................................................................................... 267
ii. Maarifa ya Teknolojia .................................................................................. 272
iii. Elimu ya Haki za Kijinsia ............................................................................ 275
6.10 Matumizi Pevu na Madhubuti ya Akili katika Uhifadhi wa Mazingira: Sauti ya Mwandishi ........................................................................................................... 279
**SURA YA SABA** .......................................................................................................... 284
7.0 **MUHTASARI, MAHITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO** ………..... 284
7.1 Utangulizi …………………………………………………………………..... 284
7.2 Muhtasari wa Tasnifu ……………………………………………………… 284
7.2.1 Aina za Anthroposenia ......................................................................... 284
7.2.2 Mbinu Zilizotumiwa Kusawiri Anthroposenia .............................................. 285
7.2.3 Tathmini ya Rai za Waandishi wa Riwaya Teule Kuhusu Jinsi ya Kukabiliana na Anthroposenia ..................................................................... 287
7.3 Mahitimisho ya Tasnifu …………………..…………………………………… 288
7.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye …………...............…………..………….. 288
**MAREJELEO** ………………………………………………………………………… 289
**KIAMBATISHO 1:** IDHINI YA UTAFITI KUTOKA CHUO KIKUU CHA LAIKIPIA 307
**KIAMBATISHO 2:** IDHINI YA KAMATI YA UKAGUZI WA MAADILI YA KITAALUMA YA KISAYANSI YA CHUO KIKUU CHA LAIKIPIA ........................................................................... 308
**KIAMBATISHO 3:** LESENI YA NACOSTI ................................................................. 310

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| **BAKIZA** | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| **TATAKI** | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| **TUKI** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| **TYM** | Tafsiri Ya Mtafiti |
| **UK** | Ukurasa |

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

Ufafanuzi wa istilahi ulifanywa kwa kuzingatia dhana maalum kama zilivyotumika katika utafiti huu. Ikizingatiwa kwamba utafiti huu ulijishughulisha na uhakiki wa suala la anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni, Vipuli Vya Figo, Mafuta* na *Walenisi,* dhana na istilahi zilizotumiwa ni pamoja na:

**Anthroposenia** Ni kipindi ambacho taathira yake ingalipo na inaendelea kuwanda kiwakati katika maisha ya binadamu, ambacho hutawaliwa na mahitaji na mielekeo ya kimazingira, yanayosheni; ubepari, utandawazi, vurugu dhidi ya mazingira na mabadiliko makuu katika ikolojia yanayozalishwa na shughuli za kila uchao za binadamu; pamoja na jitihada za utunzaji wa mazingira.

**Ikolojia** Ni taaluma inayochunguza uhusiano wa mimea na wanyama katika mazingira yao ya kiasilia na kibayolojia ambayo huhusisha mwangaza na joto, hasa la jua pamoja na unyevunyevu.

**Ishara za kitaashira** Kiurejelezi/kiutamaduni. Ni ishara zinazotambuliwa na kufasiriwa katika misingi ya utamaduni husika.

**Kapitalosenia** Ni dhana inayorejelea ubepari kama mfumo wa utawala, uratibu na uchafuzi wa mazingira ya ulimwengu, ambapo mataifa, viongozi au hata asasi zenye uwezo hushirikiana kuyaharibu mazingira.

**Mazingira** Ni dhana inayotumiwa kuelezea muktadha wa kimaumbile wa tukio, hadithi au tendo katika kazi ya fasihi. Ni neno linalolenga miktadha ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kitamaduni miongoni mwa mingine.

**Najisi** Ni mchakato unaochochewa na mwingiliano wa kibinadamu unaoathiri kwa kiasi kikubwa mfumo wa ikolojia kwa njia za uchafuzi, uharibifu wa rasilimali

asilia pamoja na usambaratishaji wa uhusiano wa kiasili kati ya viumbe na mazingira yao.

**Upujufu wa mazingira** Ni shughuli yoyote ambayo hutekelezwa na mashirika, jamii, viumbe na wanajamii, na inayoathiri kwa njia hasi siha na au mazingira ya binadamu na viumbe katika janibu fulani.

**Utandawazi** Ni dhana inayotumiwa na wakosoaji wa baada ya enzi ya ukoloni kuelekezwa kwa nchi zilizostawi kuingilia maswala ya nchi zinazoendelea, hasa katika mikabala ya kiutamaduni, kimazingira, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ni hali ambapo Mzungu aliondoka na Waafrika walioshika hatamu wakaanza kuendeleza nyenzo zile zile za Mzungu za utawala.

**Utu** Ni hali ya kuwa na sifa njema za uwajibikaji, ukakamavu na upendo dhidi ya uhai wa binadamu na mazingira yake kwa kujikita katika mtazamo wa mwandishi wa riwaya teule.

**Vurugu dhidi ya mazingira** Ni dhana inayorejelea mvutano baina ya wanajamii dhidi ya rasilimali asilia; sera za kimazingira ambazo huzalisha vita baina ya wanajamii; vita dhidi ya binadamu kutoka kwa ulimwengu asilia kama zao la uharibifu wa ulimwengu na wananjamii; na kadhalika uharibifu wa moja kwa moja wa mazingira na wanajamii, ambao hutisha uhai na maisha yao kwa jumla.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi imekuwepo kwa muda mrefu. Kimsingi, imegawika katika matawi mawili makuu; la fasihi andishi na la fasihi simulizi. Ingawa mna mwingiliano kati ya matawi haya mawili, mna tofauti bayana pia. Utafiti huu ulijihusisha na tawi la fasihi andishi hasa riwaya ya Kiswahili. Fasihi huwa haitungwi katika ombwe ila huhusiana na binadamu na mazingira yake. Suala la anthroposenia limeangaziwa sawia katika fasihi simulizi na andishi. Anthroposenia imekuwepo katika hadithi na ngano katika fasihi simulizi ambapo wahusika wanyama kama vile, sungura, ndovu, kuku, chui, simba na wengine hudhihirika wakitunza mazingira na kuzuia anthroposenia. Hili hufanikishwa kupitia mbinu mbalimbali ambazo kando na kujenga fasihi husawiri anthroposenia. Wamitila (2003) na Senkoro (2011), wakishadidia kauli hii wanasema kuwa fasihi hujengwa na vipengele vya kimtindo na kimuundo ambavyo hupatikana katika kazi yoyote ya kifasihi.

Mbatiah (2019) anadokeza kuwa, kimsingi, mwandishi wa kazi ya fasihi ni mwanajamii ambaye huzingatia kwa makini maono, ndoto, na maazimio ya jamii yake na hususan mazingira inamoishi jamii ile. Kwa misingi hii, hawezi kuwa mwasi anayeishi nje ya jamii wala akose kuisikitikia hali ya maisha wanayoishi wanajamii wake. Hivyo, ingawa ana uhuru wa kuandika kile anachotaka, uandishi wake hutawaliwa na mahitaji na haja za jamii yake. Mbatiah (2019: 4) anafafanua kuwa, "... uteuzi wa maudhui na dhamira ni wajibu muhimu kwa mwandishi wa Kiafrika. Lazima maudhui na dhamira ya kazi yake yaendane na mahitaji ya jamii yake. ... hadhira ya mwandishi ni jamii yake." Aidha, Mbatiah anashikilia msimamo kuwa, mwandishi hawezi, mathalan, kuandika kuhusu ndoa wakati ambapo jamii yake inakumbwa na majeraha na makovu ya migogoro na mivutano ya kikabila au ya vita vya baada ya uchaguzi. Hivyo, mlikuwa na haja ya kutafiti kuhusu anthroposenia katika fasihi madhali ni suala msingi  na hatari linalomkabili binadamu kila uchao, ingawa ni zao la shughuli zake mwenyewe za kila siku.

Fasihi ni kioo cha jamii na hutumia mbinu mbalimbali kuwasilisha dhana tofautitofauti kama vile anthroposenia. Fasihi kama sanaa imekuwa ikihusisha anthroposenia katika kazi mbalimbali za kifasihi. Dhana ya kuhusisha anthroposenia

katika fasihi si suala ngeni bali limekuwepo kwa kipindi kirefu. Mathalani, kazi nyingi za fasihi zimejadili mienendo na hulka za binadamu ambazo huzalisha anthroposenia (Garrard, 2007; 2023; Angus, 2016; Alia, 2017; Moore, 2018; Coughlin na Gephart 2020; Reno, 2022; Hujibens, 2023). Wasomi hawa wanaongeza kuwa, mazingira ambayo ni kipengele msingi katika anthroposenia yamekuwa yakihusishwa katika fasihi kwa muda mrefu kijumla, bila kujifunga kwenye anthroposenia ya kijiolojia au ile pendwa. Clark (2015), Moore (2017), Filipova (2023) na Garrard (2023) wanaunga mkono kauli hii kwa kusema kuwa, suala la kuhusisha anthroposenia katika fasihi kimwavuli ni taaluma ambayo iliibuka katika karne ya kumi na nane lakini ikashamiri katika karne ya kumi na tisa. Hivyo, dhana ya kuhusisha anthroposenia katika fasihi ni taaluma kongwe. Fasihi ni asasi ambayo hutumia lugha kwa ufundi katika kuangazia matatizo yanayoikumba jamii. Watunzi wengi wa fasihi ya Kiswahili wamedhihirisha anthroposenia katika kazi zao za kisanaa kwa kutumia mbinu tofautitofauti za kisanaa. Kutokana na hili, kuna haja ya anthroposenia kufanyiwa utafiti mpana na wa kina katika riwaya nne teule kwani halijapata kuchunguzwa na watafiti wengi hususan katika misingi ya kiuhakikimazingira.

Suala la anthroposenia husheheni masuala mbalimbali kama vile, masuala ya mabadiliko ya tabianchi, mabadiliko ya hewa, uchafuzi wa mazingira, ubidhaaishaji wa kibepari ambao huzalisha utumwa aina aina, ongezeko la watu duniani, vurugu dhidi ya mazingira, utandawazi, maangamizi na mengine mengi msingi katika maisha ya binadamu. Masuala haya hudhihirika katika kazi mbalimbali za fasihi na huchukua nafasi kubwa katika maisha ya binadamu katika kazi za kisanaa za fasihi, hasa ya Kiswahili. Mathalani, fasihi ya watoto hudhihirisha masuala haya katika harakati za uhifadhi wa mazingira. Aidha, haja ya maendeleo endelevu katika kazi za kisanaa imempelekea binadamu kupalilia na kuendeleza anthroposenia katika viwango mbalimbali. Hali hii, kama inavyodhihirika katika kazi za fasihi humsukuma binadamu kujiangamiza mwenyewe kutokana na shughuli zake za kila siku. Wakishadidia kauli hii, Nayar (2010), Bladow na Ladino (2018), Ballard (2023) na LaMothe (2024) wanashikilia kauli kuwa, kama binadamu, tunaendelea kudidimiza ulimwengu katika bahari la uchafu, najisi na kemikali zitokanazo na viwanda, hali ambayo hupalilia anthroposenia kwa kiwango kikubwa. Kupitia kazi ya kisanaa wanatahadharisha kuwa, leo hii hakuna anayefaa kukuzuia kusema kuwa binadamu

amefanikiwa kujiua kimazingira na hivyo kufanya sayari mahali pasipofaa uhai wa kiumbe chochote kile. Hata hivyo, maangamizi yanayorejelewa na mtafiti ni yale ambayo hudhihirika katika kazi za kifasihi.

Hivyo, kuna haja ya kushughulikia kwa kina anthroposenia katika riwaya teule za Kiswahili. Katika utafiti huu, mtafiti alinuia kutafiti anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili katika misingi ya uhakikimazingira. Anthroposenia huzalisha upujufu wa mazingira pamoja na athari zingine hasi kwa binadamu. Uchafuzi na uharibifu wa mazingira huwa tishio kubwa kwa binadamu na pia wanyama wengine wanaomzingira. Ongarora (2017) na Waithiru (2022d) wakiunga mkono kauli hii wanakariri kuwa, uchafuzi na uharibifu wa mazingira hutokea kupitia kwa uchafuzi wa maji na hewa, mmomonyoko wa udongo, ufyekaji miti kiholela na ufugaji wa wanyama wengi bila mikakati kabambe miongoni mwa njia nyingine nyingi. Aidha, kwa kuzuia au kuchangia anthroposenia, binadamu huingiliana na mazingira yake katika kazi za kifasihi. Maingiliano haya husababisha athari hasi zinazozalishwa na anthroposenia katika kazi za kisanaa hasa za Kiswahili. Claser (2002) akishadidia kauli hii anasisitiza kuwa, binadamu anapoendelea kuhitilafiana na mazingira yake katika kazi za kifasihi, huathiri maendeleo yake ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ambayo huchipuka kila uchao, hasa katika karne ya ishirini na moja.

Matini nyingi za fasihi zinadhihirisha kuwa, jinsi binadamu anavyoendeleza anthroposenia ndivyo anavyodidimiza maisha yake ulimwenguni kutokana na maradhi na ukame. Coughlin na Gephart (2020) wanabisha kuwa, athari za anthroposenia zinaathiri idadi ya miaka mwanadamu anayoivuruga sayari. Kadhalika, tofauti za kitabaka zinazodhihirika katika matini mbalimbali za kifasihi huzalishwa na anthroposenia. Hii ni kwa sababu, anthroposenia hupalilia ulofa na kuchipuza utegemezi wa mtu kwa mwingine badala ya ujitegemezi wa mtu mwenyewe. Hali hii hupelekea kufifia kwa mojayazo ya mhimili wa Nadharia ya Uhakikimazingira wa maendeleo endelevu. Ukosefu wa usawa na utabaka katika jamii huchangiwa pakubwa na anthroposenia. Robert na Battista (2016) wanaunga mkono kauli hii wanaporai kuwa, utabaka baina ya wanajamii huathiri uzoefu walonao katika harakati zao za kila siku zinazoathiri mazingira. Mathalani, wanashadidia kuwa, anthroposenia husheheni uchafuzi wa hewa ambao hutekelezwa na kuchangiwa pakubwa na wanajamii wa tabaka la juu ilhali wanaoathiriwa ni wale wa tabaka la chini. Hii ni kwa sababu, wale wa tabaka la juu huepuka madhara ya uchafuzi wa hewa kwa

kutumia vifaa vya kusafisha hewa kama vile viyoyozi. Tofauti hizi hudhihirika katika kazi mbalimbali za fasihi kupitia wahusika. Hivyo, ubaguzi wa kitabaka hupelekea ubaguzi wa mazingira katika matini za kifasihi.

Binadamu katika aushi yake hukumbana na mambo tofautitofauti ambayo hana budi kupambana nayo ili aweze kuyamudu mazingira anamoishi. Mambo ambayo binadamu hukutana nayo katika maisha ni mengi na yanaweza kuainishwa kwa kutumia utanzu wa fasihi andishi, hasa wa riwaya ya Kiswahili. Mtunzi kupitia utanzu wa riwaya huiumba na kuifinyanga hadithi yake kwa kutumia usanii unaotawaliwa na haja na mahitaji ya kuzuia anthroposenia kwa kiwango kikubwa. Hivyo, wahusika katika riwaya ya Kiswahili kama vile binadamu, hutekeleza shughuli zao za kibinafsi zinazopelekea maangamizi ya mazingira kwa jumla. Shughuli hizi katika kazi za kifasihi ni kama vile, kutupa taka ovyo, kukata miti ovyo, kujenga vyumba na kulima katika maeneo oevu na karibu na mito, kuongezeka kwa teknolojia inayochangia kushamiri kwa anthroposenia na uadimikaji wa uongozi adilifu katika anthroposenia. Coughlin na Gephart (2020) wanafafanua kuwa, shughuli zinazotekelezwa na viumbe mbalimbali zimesababisha mitandao ya viungauhai kuharibika. Anthroposenia husheheni athari na mabadiliko hasi dhidi ya mazingira katika kazi nyingi za kifasihi. Wahusika katika kazi za kifasihi hudhihirishwa na watunzi wakizuia uharibifu wa mazingira kupitia njia mbalimbali.

Jinsi miaka inavyosonga ndivyo watu wameanza kuwajibikia na kusikitikia mazingira. Hii ni kwa sababu baadhi ya wasomi kama vile Clark (2015), Moore (2016; 2017), Coughlin na Gephart (2020), Harvey (2020), Feder (2021), Sklair (2022), Sritama (2022) na wengine wengi wanaonyesha kwamba anthroposenia isipotunzwa vyema mwanadamu anaweza akaathirika na kusababisha maangamizi. Kwa upande wa fasihi, watunzi wa fasihi wamekuwa wakishughulikia suala la anthroposenia, hususan upande wa riwaya ya Kiswahili lakini data iliyopo kuhusiana na anthroposenia ni haba na ndiposa kazi za watunzi Mkangi na Mbogo zilitafitiwa. Waandishi wengi wa fasihi wameandika kuhusu athari za anthroposenia zinazozalishwa na shughuli za kila siku za binadamu. Baadhi ya athari ambazo wanataja ni kama vile kuongezeka kwa jotohewa na kuvuguta mazingira, ndwele zitokanazo na anthroposenia, mauti na kupungua au kuongezeka mvua zaidi. Bladow na Ladino (2018) wakishadidia kauli hii wanakiri kuwa, upungufu wa mvua husababisha janga la ukame na hatimaye maangamizi, hususani katika kipindi cha

utandawazi na ubidhaaishaji wa kibepari. Wanaongeza kuwa, athari hizi za anthroposenia huathiri maisha ya binadamu na huweza kutinga maendeleo endelevu katika jamii na hivyo kuchangia ulofa. Utandawazi na maendeleo endelevu ni baadhi ya mihimili ya nadharia ya Uhakikimazingira iliyoongoza uchanganuzi wa data ya utafiti huu kwa minajili ya kuchunguza anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Kiuamilifu, fasihi hunuia kufikia jamii ili iikosoe, iielimishe, iiburudishe na pia iitahadharishe kuhusu athari za matendo mabovu ya wanajamii. Kilele cha dhima hizi za kazi za fasihi ni kusuluhisha matatizo yanayochipuka katika jamii na yanayotishia uhai wa viumbe wote wenye uhai. Katika misingi hii hii, fasihi ina mchango mkubwa wa kuhamasisha jamii kuhusu suala la anthroposenia, hasa sana kuhusu aina za anthroposenia kama vile binadamu, dini, uongozi mbaya, ukoloni mamboleo, ufisadi, wanyama, wadudu na nyingine nyingi. Hii ndiyo sababu wataalamu na waandishi wa fasihi wamejitosa uwanjani na kulivalia njuga suala la anthroposenia katika kazi za fasihi. Baadhi ya wasomi ambao wamelivalia njuga suala hili ni Clark (2015), Moore (2016), Demos (2017), Bladow na Ladino (2018), Simon na Mark (2018), Coughlin na Gephart (2020), Vermeulen (2020), Feder (2021), Mostafanezhad na Norum (2021) pamoja na Butler (2024).

Kadri binadamu anavyoendelea kuingiliana na mazingira katika anthroposenia, ndivyo anavyoendelea kuyanajisi. Maingiliano haya huzalishwa na sababu kuwa, katika anthroposenia, binadamu hujibunia mazingira yake tofauti na yale ya kiasili. Anthroposenia hupelekea upujufu wa kitamaduni na kihistoria, hali ambayo huathiri maisha ya binadamu kwa kiwango kikubwa. Huggan na Tiffin (2010) wanataja kuwa, wanajamii wanafanikisha anthroposenia kupitia mifumo mipya ya kiteknolojia. Crutzen (2008) anatilia mkazo kauli hii anaposema kuwa, suala la anthroposenia lilianza katika mapinduzi ya kwanza ya viwanda na kuendelea hadi leo, huku likichangiwa na kupaliliwa zaidi na utafiti ambao unaendeshwa kupitia teknolojia mpya ambayo inavumbuliwa na binadamu kila uchao. Hivyo, kuna haja ya kutafiti kuhusu anthroposenia katika riwaya teule za Kiswahili katika misingi ya uhakikimazingira ili kuziba pengo la upungufu wa tahakiki zinazohusu anthroposenia katika kazi za kifasihi.

Hivyo, je, kulikuwa na haja ya kutafiti suala la anthroposenia katika riwaya ya Kiswahili kwa lengo la kuongeza tahakiki zinazohusu anthroposenia katika kazi za fasihi? Ndiyo, na tena pana haja kubwa. Hata hivyo, utafiti huu ulitekelezwa mintarafu madhumuni ya utafiti na uliongozwa na baadhi ya nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira kwa minajili ya kuziba mwanya wa kiakademia. Suala lenyewe lilikuwa kuziba pengo la upungufu wa tahakiki zinazohusu anthroposenia (Hupkes na Durbeck, 2023; Wallenhorst na Wulf, 2023; Smith na Wilson, 2024; Economides, 2025; Dyke, 2025) katika kazi za kifasihi na hususan katika riwaya ya Kiswahili.

### 1.2 Suala la Utafiti

Kiuyakinifu, mazingira mema, safi na yenye viumbehai wenye siha njema ni muhimu sana kwa maisha ya mwanadamu. Ingawa mazingira mema ni mwafaka kwa binadamu, wanajamii wengi hupujua mazingira katika anthroposenia kwa sababu za tamaa, ubinafsi-uchoyo na mahitaji yao binafsi bila kujali jamii wala kizazi cha siku za usoni. Hata hivyo, kuna wale wanaoshikilia kwamba, hata katika anthroposenia mazingira hayawezi kuharibika kiwango cha kuharibu dunia, madhali mazingira yenyewe huweza kujidhibiti. Mwanadamu mwenyewe kama aina ya anthroposenia ni sehemu ya kujidhibiti kwa mazingira. Hivyo, ingawa kazi za fasihi zimetungwa kuhusiana na anthroposenia, kuna upungufu wa tahakiki kuhusiana na jinsi fasihi inashughulikia anthroposenia. Utafiti ulinuia kuziba mwanya huu wa kiakademia. Baadhi ya vigezo bainifu vya utafiti huu vilikuwa mabepari, mabeberu wa kisasa; utepetevu wa binadamu; vurugu dhidi ya mazingira; viongozi wabaya na wafisadi. Hamna tafiti nyingi ambazo zimelishughulikia suala la anthroposenia katika riwaya ya Kiswahili hususani katika misingi ya Uhakikimazingira. Hivyo basi, utafiti huu unahusu anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili mintarafu madhumuni ya utafiti huku ukiongozwa na baadhi ya mihimili mikuu ya nadharia ya Uhakikimazingira.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kutimiza malengo mahsusi yafuatayo:

i. Kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi*.

ii. Kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi*.

iii. Kutathmini rai za waandishi wa riwaya teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi*.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kuyajibu maswali ya utafiti yafuatayo:

i. Je, aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya za *Bustani ya Edeni, Vipuli vya Figo, Mafuta* na *Walenisi* ni zipi?

ii. Je, mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo, Mafuta* na *Walenisi* ni zipi?

iii. Je, rai za waandishi wa riwaya teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi* ni zipi?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Suala la anthroposenia linahusu kila mja na hivyo ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Utafiti huu ni wa kifasihi na hivyo ulinuia kuchochea tafiti za halafu kuhusu anthroposenia katika fasihi. Ilitarajiwa kuwa utafiti huu utasaidia kwa kiwango kikubwa kuimarisha njia za maingiliano baina ya aina mbalimbali za anthroposenia kisanaa. Kimsingi, utafiti huu ulinuia kuwa utakuwa na natija kwa wasomi, wahakiki na watafiti katika fani ya anthroposenia katika fasihi hususan ya riwaya ya Kiswahili kwa kuwa sehemu ya kurejelewa. Kiuyakinifu, utafiti huu ulilenga kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya teule za Kiswahili. Baadhi ya aina za anthroposenia zilizoangaziwa katika utafiti huu ni pamoja na binadamu; mabeberu wa kisasa; wakala wa anthroposenia kama vile, wadudu na wanyama; wafisadi; mabepari na viongozi wabaya. Ilitarajiwa kuwa wasomi na wahakiki wa halafu watanufaika na tahakiki ya aina za anthroposenia katika riwaya ya Kiswahili.

Kadhalika, utafiti huu uliangaza mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia kama vile taswira, majazi, taashira na tashbihi katika riwaya za *Bustani ya Edeni, Vipuli vya Figo, Mafuta* na *Walenisi*. Mbinu katika uandishi si kile kinachosemwa au kuandikwa, bali ni namna kinavyosemwa au kuandikwa. Ilitarajiwa kuwa wahakiki wa siku za usoni watanufaika na uchanganuzi wa mbinu za mwandishi wa kazi za fasihi, hasa za kusawiri anthroposenia katika kuzuia vurugu dhidi ya mazingira. Mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya teule za Kiswahili,

zilihakikiwa kwa kina na kwa upana katika misingi ya uhakikimazingira. Utafiti huu ulitarajiwa kuwa utakuwa wa manufaa kwa waandishi wa siku za usoni watakaotumia mbinu zinazosawiri anthroposenia kama vile, taashira, ishara na taswira kueleza kuhusu vitu, watu, matukio au janibu katika kuimarisha na kuendeleza vita dhidi ya siasa za mazingira. Kadhalika, ilitarajiwa kuwa utawahami na stadi za jinsi ya kuchagua msamiati ambao huchangia kuwasilisha ujumbe lengwa kwa hadhira lengwa. Hili liliafikiwa kupitia uchanganuzi wa kina wa wahusika, kinaya, toni, mikakati ya kibalagha, mbinu za kisanaa, na mbinu za uandishi.

Hatimaye, ilitarajiwa kuwa utafiti huu utawanufaisha wasomi kwa jumla hasa katika harakati za kudhibiti anthroposenia kupitia rai za waandishi wa kazi za fasihi hasa riwaya za *Bustani ya Edeni, Vipuli vya Figo, Mafuta* na *Walenisi*. Hata hivyo, si rahisi kudhibiti anthroposenia bila kumaizi jinsi ya kukabiliana na anthroposenia hasa katika kazi za fasihi. Hivyo basi, usomi huu ulitarajiwa kuwa utasaidia kuwahamasisha watafiti, wahakiki na wasomi kuhusu njia mbalimbali za kukabiliana na anthroposenia katika misingi ya Uhakikimazingira, kwa kujikita katika riwaya nne teule za Kiswahili zilizotajwa. Hivyo, utafiti huu ulitarajiwa kuwa utachangia pakubwa katika kumulika na kufafanua kuhusu uchafuzi wa mazingira, na majanga mengine ya anthroposenia ambayo huvamia janibu nyingi ulimwenguni kila uchao. Kwa jumla, utafiti huu ulinuiwa kuwa utawasaidia watafiti na wasomi wa siku za usoni katika kufafanua haja ya kushughulikia changamoto za anthroposenia zinazokuzwa na kupaliliwa na aina mbalimbali za anthroposenia kama vile, wanadamu na wanyama. Hili lilisaidia kuangaza changamoto za kimazingira kiwingi-idadi na kithamana.

Kwa misingi hii, kazi hii ilitarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kusaidia wasomi kuchunga anthroposenia kwa kutoa dhana na suluhu kutoka kwenye riwaya ya Kiswahili. Hili ni muhimu kuangaza kwa sababu, unajisi wa mazingira ni mojawapo ya baadhi ya matatizo makubwa yanayomkumba binadamu katika anthroposenia kwa mujibu wa kazi za fasihi. Shughuli nyingi za mwanadamu zinachangia anthroposenia kwa kiwango kikubwa. Kulingana na kazi nyingi za fasihi, mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea yanakumbana na changamoto chungu nzima zinazozalishwa na anthroposenia. Hata hivyo, yale yanaendelea yanakumbana na matatizo makubwa na changamano zaidi yakilinganishwa na yanayoyakumba mataifa yaliyoendelea. Hii ni kutokana na harakati za kudumisha maendeleo endelevu kama vile, upanuzi wa miji, uchimbaji wa madini na mafuta, pamoja na mashirika ya kigeni

yanayokuza maua katika mataifa mengi barani Afrika. Maendeleo endelevu ni mojawapo ya nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira zilizoongoza uchanganuzi wa data ya utafiti huu na hivyo hali hii ya kudumisha maendeleo endelevu inafungamana moja kwa moja na utafiti huu. Anthroposenia ina uwezo wa kusambaratisha mataifa, jamii na boma ikiwa itapuuzwa na hivyo kuna haja ya kuiangaza na kuisuluhisha madhubuti kwa kuikita katika riwaya ya Kiswahili.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

### 1.6.1 Upeo wa Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti aliangaza riwaya ya Kiswahili na alijishughulisha na vitabu vinne – *Bustani ya Edeni* (2002), *Vipuli vya Figo* (1996), *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data, mtafiti aliongozwa na mihimili mikuu ya nadharia ya Uhakikimazingira ili kukidhia malengo ya utafiti. Mtafiti alisoma riwaya nne teule kisha alitongoa na kuchanganua data ya kategoria aliyoikusanya, mintarafu madhumuni ya utafiti. Alitumia mbinu ya kimaelezo ya utafiti. Kwanza alizichunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule, kisha alihakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili na hatimaye alitathmini rai za waandishi wa riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi* kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia.

### 1.6.2 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulinuiwa kufanywa kwa muda wa miaka mitatu. Ingawa ulihusisha riwaya ya Kiswahili, ulijifunga katika riwaya nne teule. Ulitekelezwa maktabani na kwenye tovuti tofautitofauti. Hivyo, mtafiti alichunguza namna Katama Mkangi na Emmanuel Mbogo walivyozisawiri aina mbalimbali za anthroposenia kama vile; binadamu, wakala wa anthroposenia kama vile, wanyama na wadudu, wafisadi, viongozi wabaya, utepetevu wa binadamu, mabeberu wa kisasa, jiografia ya binadamu, matumizi ya vifaa na mabepari katika riwaya nne teule za Kiswahili. Pia aliangaza mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia kama vile taashira, taswira, ishara, majazi, tashtiti na nyingine nyingi katika riwaya nne teule. Hatimaye, alitathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule za Kiswahili kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia. Mathalani, rai kuhusu vyombo vya habari na uhamasishaji wa uendelevu, nafasi ya ukakamavu katika ulinzi wa mazingira, nafasi ya utu pamoja na ushirikiano na ujasiri katika uhifadhi wa mazingira kupitia lensi ya mwandishi, na mengine mengi katika anthroposenia katika misingi ya Uhakikimazingira.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliangazia maandishi muhimu kuhusu mada ya utafiti na pia alichambua nguzo muhimu za Nadharia ya Uhakikimazingira mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu. Kazi alizoangazia za watafiti wengine alidhihirisha mchango wao kwa kazi hii na pia tofauti iliyopo baina ya utafiti huu na kazi aliyoipitia. Lengo lake kuu lilikuwa kudhihirisha kinaganaga pengo la kiusomi linalonuiwa kujazwa na utafiti huu. Ikizingatiwa kwamba mna upungufu wa tahakiki kuhusiana na jinsi fasihi imelishughulikia suala la anthroposenia, mtafiti alipitia kazi za wasomi wa hapo kabla pamoja na tovuti na makavazi mbalimbali kwa lengo la kuongeza data husika, mintarafu ya madhumuni ya utafiti.

### 2.1.1 Aina za Anthroposenia

Katika kuangaza athari za uongozi mbaya katika jamii, Kobia (2007) anadhihirisha namna viongozi waliochaguliwa na kutunukiwa wajibu wa kuhifadhi mazingira wanavyoyanajisi. Anatoa sababu kuwa kisababishi kikubwa cha najisi hii ni tamaa, ubinafsi na ufisadi wa mwanadamu. Mawaziri ambao wana jukumu la kulinda na kutunza miti, hasa ya kiasili wako mstari wa mbele katika ufyekaji wa misitu. Miti hii ndiyo huwapa wanajamii hewa safi, husaidia kuvuta mvua na pia kuzuia mmomonyoko wa udongo. Mawaziri kama aina ya anthroposenia wakihongwa na baadhi ya wananchi, wanawapa leseni ya kukata miti shaghalabaghala ambayo pia ni aina ya anthroposenia. Miti inayokatwa inachomwa makaa na mingine kupasuliwa kutengeneza mbao za ujenzi. Hali hii inachangia ufyekaji wa miti ya kiasili. Jambo hili linasababisha mito na maziwa kukauka na mvua kupungua kwa kiasi kikubwa, kando na ongezeko la joto kutokana na kuraruka kwa ozoni. Kadhalika, ukame unashamiri na maafa ya mifugo na mimea yanachipuka na kunawiri na hili linazalisha uzorotaji wa uchumi na hatimaye, maafa ya wanajamii kutokana na njaa kama zao la aina za anthroposenia. Kazi hii ilichangia utafiti huu hasa katika uchanganuzi wa data kwa kutumia mihimili ya kifo na uongozi mbaya, katika kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili. Lakini, tofauti na Kobia ambaye ameangaza ‘Tumbombele Mla Misitu’, utafiti huu uliangazia aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili katika misingi ya Uhakikimazingira.

Morton (2007) anajadili kuwa, kizingiti kikuu kinachozuia mawazo kuhusu anthroposenia ni taswira ya ulimwengu yenyewe. Waandishi wa kianthroposenia wanapendekeza kuwa muono mpya wa ulimwengu unahitajika, lakini kuziba kwao wenyewe katika harakati za kuthibiti anthroposenia katika ulimwengu asilia huwaongoza wao wenyewe mbali na ulimwengu ambao wameuona. Tatizo kubwa ni dalili za maangamizi ya kiikolojia ambayo huukumba ulimwengu kila uchao. Morton anaweka kweli kinzani kuwa, ili kupata muono mwafaka wa anthroposenia, ni lazima wanadamu waache tabia na dhana ya uulimwengu kabisa. Matini hii ya Morton ilichangia utafiti huu wa mtafiti katika kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule. Hata hivyo, tofauti naye, mtafiti alitathmini aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili za fasihi kwa kujikita katika mtazamo wa Uhakikimazingira bali si kiulimwengu wala kisayansi.

Ufisadi hujidhihirisha katika viwango na namna tofautitofauti. Mathalani, katika msongamano wa magari mjini, madereva wa magari ya kibinafsi pamoja na wale wa magari ya usafiri wa umma hujipata katika bahari ya ufisadi wanapokiuka sheria za trafiki. Ingawa ufisadi ni mchakato ambao ni changamono zaidi kuliko tukio la ukiukaji wa sheria za trafiki barabarani, kushiriki hongo, kulaghai kimapenzi baina ya mengine mengi huchangia pakubwa katika uzorotaji; wa afya, wa huduma za umma, utu, mazingira na uhai kwa jumla. Hivyo, ufisadi sio tu suala la dharura, hatari na la maangamizi kwa taifa la Nigeria ila pia kwa ulimwengu kwa jumla (Smith, 2007). Tofauti na kazi ya Smith ambayo imeangaza mila na desturi ya ufisadi katika shughuli za kila siku za binadamu, mtafiti katika utafiti huu aliangaza mafisadi kama aina ya anthroposenia na athari zake hasi kwa jumla, mintarafu ya madhumuni ya kwanza ya utafiti. Hata hivyo, utafiti wake ulichangia huu wa mtafiti katika kuchunguza ufisadi kama aina ya anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Kazi za fasihi zimeweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uhifadhi wa mazingira (Kezilahabi, 2008). Kulingana na Kezilahabi, mafuriko kwa mfano, huwa na athari hasi kwa jamii, hasa kiuchumi. Hili huwa kizingiti katika maendeleo endelevu ambao ni mhimili utakaotumika katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Katika kazi yake anadhihirisha hasara kubwa inayosababishwa na mafuriko dhidi ya wakulima ambao wanalima kwa bidii kisha mimea yao kuharibiwa na mafuriko.

Kadhalika, nyumba kongwe zilizoko mabondeni zinabebwa hobelahobela na mafuriko kutokana na ukosefu wa nguvu ya kujisetiri. Wanajamii wanakumbwa na maangamizi na kulazimika kuhamia kwenye janibu salama. Maeneo mengi yanafunikwa na giza kutokana ukosefu wa nguvu za umeme. Ukosefu huu unazalishwa na kuanguka kwa vikingi vya nyaya za umeme. Zaidi ya hayo, nyaya hizi zinahatarisha maisha ya wajamii na wanyama wanaoishi katika maeneo yale. Baada ya mafuriko, upepo mkali unabisha na kusababisha maafa. Maafa haya yanasababishwa na miti inayoangukia vyumba wenyeji wakiwemo kutokana na upepo mkali. Wengine wanakimbia makwao uvumapo kwa kuhofia usalama na uhai wao. Kuanguka kwa miti kunachangia mmomonyoko wa udongo kwa kiwango kikubwa katika maeneo yale. Kezilahabi amedhihirisha athari za aina za anthroposenia kupitia kazi ya fasihi kwa jamii. Kazi yake ilichangia hii ya mtafiti katika kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili. Tofauti na Kezilahabi, mtafiti aliongozwa na nguzo za Nadharia ya Uhakikimazingira kama vile, binadamu dhidi ya maumbile na maumbile.

Pana dhana mpya inayosisitiza kuwa binadamu wote huwa sehemu kubwa na ya hadhi katika uhusiano ambapo jamii huwa na uhusiano wa kisimbiotiki baina yake na mazingira anamoishi (Morton, 2012; Head, 2018; Vermeulen, 2020; Butler, 2024, 2024; Smith na Wilson, 2024). Wataalamu hawa wanazidi kufafanua kuwa kuna ushirikiano na muungano wa msingi dhidi ya ikolojia pamoja na historia ya mazingira. Ushirikiano huu wanauangazia katika uhusiano unaotawaliwa na mahitaji katika kipindi kinachosheni athari hasi dhidi ya mazingira. Wanatambua anthroposenia kama ulimwengu ambapo shughuli za binadamu zinaendelea kuathiri mifumo ya dunia. Mifumo hii ni pamoja na hali ya anga, ozoni, ongezeko la joto na uharibifu wa hewa pamoja na uharibifu wa chemchemi za maji. Morton (2013), Moore (2017), White na Whitlock (2021) wanarejelea, anthroposenia kama sadfa ya historia ya binadamu na jiolojia ya kiterestria. Kwamba, ni msimu mpya wa historia ambapo viumbe visivyo binadamu na maumbile huhusishwa na kujumlishwa katika vita dhidi ya uharibifu wa mazingira. Kazi za watafiti hawa zilichangia utafiti huu katika kuchunguza aina za anthroposenia. Hata hivyo, kazi zao zilitofautiana nah ii ya mtafiti kimadhumuni na kinadharia.

Clark (2015) anasema kuwa, aina mbalimbali za anthroposenia huzalisha athari za kisaikolojia na shani za jazba. Baadhi ya athari hizi ni sera zinazoyumba na zisizo tekelezi za kimazingira na udunishaji wa masuala mazito ya mazingira. Akinukuu mwongozo wa Greenpeace, *How to Save the Climate,* anaongeza kuwa msomaji wa kazi ya fasihi ambaye ni binadamu, anafaa kuoga kwa kutumia bafu ya manyunyu ila sio kwa kujitumbukiza kwenye hamamu, na pia aweze kukadiria na kupima muda anaotumia kuoga huku akiimba wimbo mfupi. Kimsingi, Clark anapendekeza aina za anthroposenia ziweze kukamilishana katika harakati za uhifadhi wa mazingira bunifu na asilia. Aidha, kupitia aina za anthroposenia anakemea mifumo ya siasa inayotawala mahitaji ya ubepari wa kimataifa. Ingawa utafiti wake ulichangia huu wa mtafiti katika shughuli za kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili, unatofautiana na huu. Tofauti zenyewe zipo kwenye nadharia na lengo. Tofauti na Clark pia, utafiti huu ulijifunga kwenye fasihi pekee. Kadhalika, Clark alitumia mseto wa nadharia mbalimbali na alinuia kuhamasisha ulimwengu kuhusu uhakikimazingira huku akiashiria anthroposenia kama dhana ya kiupeo.

Horacio (2015) anafafanua kuwa, mazingira yanaendelea kubadilika namna muda unavyosonga. Mabadiliko haya nayo humlazimu kiumbe hai kubadili mazingira yake na kuyakarabati ili kuishi na kuendeleza kizazi chake. Mabadiliko haya hutokana na vurugu dhidi ya mazingira ambapo binadamu huhitilafiana na mazingira kutokana na matumizi yake mabaya na ya maangamizi ya mazingira. Matumizi mabaya ya mazingira kutoka kwa binadamu huzalisha utowekaji wa rasilimali asilia ulimwenguni, jambo ambalo husababisha mazingira kupigania haki zake na katika hali hiyo binadamu huwa na mvutano na mazingira asilia. Horacio anasisitiza kuwa, kiwango na mwendo ambao binadamu anavuruga mazingira ni wa kasi na hatari kwa maisha yake mwenyewe, maisha ya mazingira na ya viumbe wengine na maumbile kwa jumla. Hivyo, anasisitiza haja ya binadamu kupunguza vurugu dhidi ya mazingira maadamu uhai uweze kudhibitiwa katika michakato ya uhai wa kawaida duniani. Hatimaye, anahitimisha kuwa bila maarifa mwafaka kuhusu mazingira na matokeo ya vurugu dhidi ya mazingira, tutakuwa spishi nyingine iliyotoweka ulimwenguni hivi karibuni. Kazi yake ilichangia utafiti huu wa mtafiti katika kuchunguza vurugu dhidi ya mazingira kama aina ya anthroposenia kwa jumla. Hata hivyo, tofauti naye, mtafiti alichunguza aina mbalimbali za anthroposenia kwa kuongozwa na nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira.

Mtaalamu Moore (2016, 2017, 2018) anasisitiza kuwa tunaishi katika kipindi ambacho kinashuhudia mabadiliko katika maisha ya sayari, ambayo yana uwezo wa kubadili dunia kwa haraka, kwa njia kuu, na katika hali ambayo haiwezi kurekebishwa milele; katika hali isiyofahamika katika tajriba ya binadamu. Anaongeza kuwa katika tathmini razini hali inaendelea kuzorota. Hii ni kwa sababu, anthroposenia huzalisha maswali ya ukapitalisti, mamlaka na utabaka, anthroposentriki, uratibu wa mazingira na jamii, pamoja na jukumu la himaya na serikali dhidi ya mazingira. Aidha, anataja kuwa kapitalosenia huwa na mchango mkuu katika anthroposenia, madhali huashiria njia za kupanga mazingira katika ulimwengu wa kibepari ndani ya mfumo kamili wa ikolojia. Hili hufanikishwa na nguzo ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya uwezo, ambapo mataifa yenye uwezo huyapujua mazingira ya mataifa fukara. Kulingana na Moore (2017, 2018), anthroposenia katika fasihi ni dhana iliyodokezwa na Paul Crutzen na Eugene Stoermer katika miaka ya 2000, ambayo ilichipuka kutokana na nafasi razini ya janibu za dunia ambapo uhai wawezekana kuwepo na kipindi ambacho kimsingi kimeathiriwa na shughuli za binadamu. Kazi zake zilichangia hii ya mtafiti katika kuchunguza aina za anthroposenia hasa kwa kuongozwa na nguzo ya uwezo ya Nadharia ya Uhakikimazingira. Tofauti naye, mtafiti aliangaza anthroposenia katika riwaya ya Kiswahili.

Dhana ya anthroposenia hukisiwa na baadhi ya wasomi (Bunker na Ciccantell, 2005; Allen, 2011; Cox, 2015; Angus, 2016; Gill, 2016) kuwa inapotosha kutokana na utenganisho wake na kapitalosenia (Moore, 2017). Moore anajadili kuhusu kiini cha mawazo ya kihistoria katika ufahamu na ukubalifu wao wa migogoro ya kiulimwengu ya ubepari katika karne ya ishirini na moja. Tofauti na historia ya hivi majuzi isiyo ya kina ya anthroposenia, anasisitiza kuwa anachagua ile ya kina, upana na ukezo zaidi ya kapitalosenia. Hii ni kwa sababu, kapitalosenia hueleweka kama mfumo wa uwezo, faida na uzalishaji katika utando wa maisha (Moore, 2018). Isitoshe, anatenganisha anthroposenia na mabepari katika misingi ya mawazo na mielekeo ya kapitalosenia katika misingi ya mazingira kiuyakinifu. Hata hivyo, katika utafiti huu, mabepari walichunguzwa kama aina ya anthroposenia na walihusisha kapitalosenia chini ya nguzo ya uwezo ya Nadharia ya Uhakikimazingira. Anthroposenia husisitiza kuwa migogoro ya kimazingira ilichipuka baada ya majilio ya mabadiliko makuu ya viwanda bila kuzingatia mabadiliko ya mazingira yaliyokuwepo hapo kabla kutokana

na ubepari, ambayo yalikuwa makubwa zaidi tangu kuibuka kwa kilimo na miji ya kwanza (Moore, 2017). Ingawa ni kweli kuwa mabadiliko katika mazingira yaliongezeka na kushika kani sana baada ya 1850, na hususan baada ya 1945, ni vyema kutambua namna uwezo, miji na mazingira vilivyochangiana, vilivyohusiana na vilivyoathiriana, karne nne kabla ya 1850. Ingawa kazi yake inatofautiana na hii ya mtafiti, iliweza, hasa maoni kuhusu mchango wa uwezo katika upujufu wa mazingira, kuchangia utafiti huu katika uchunguzi wa aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Kusserow (2018) anashadidia kauli kuwa, uhakikimazingira sio tu mbinu ila pia tabia au sifa ya kimawazo kuhusu namna ya kudhibiti anthroposenia. Kadhalika, kando na kutekeleza uhakikimazingira katika anthroposenia katika karne ya kumi na tisa, watafiti wametumia vifaa, rasilimali, taswira, teknolojia na epistemolojia kama nadharia ya uhakiki na uelekezi na kwa kufanya hivyo fasihi imekuwa ikiimarisha utamaduni wa anthroposenia. Aidha, anthroposenia ni kama mizizi ya mti ambao matawi yake husheheni kapitalosenia, ubepari, njaa, maradhi, utawala dhalimu, ufukara, mazingira machafu, kiangazi, mafuriko na maafa huku yamekita kwenye shina la mti wa anthroposenia. Mti huu huunyonya ulimwengu na hatimaye hudhoofisha siha ya ulimwengu kwa kila namna. Vilevile, Simon na Mark (2018) na Slovic na wenzake (2020) wanapambanua kuwa, athari za shughuli za binadamu kwenye mazingira huwa na athari kubwa zaidi kuliko vile tunavyofahamu. Kwamba, ulimwenguni, shughuli za binadamu husababisha mmomonyoko wa udongo kwa kiwango kikubwa kuliko namna michakato na mifumo mingine yote asilia husababisha ikiwa imejumlishwa pamoja. Kwa mfano, wanataja kuwa binadamu tumetengeneza na kuzalisha plastiki nyingi, kiwango kwamba visehemu vidogo vya ufumwele wake vimezagaa ndani ya karibu kila tone la maji tunalokunywa. Kutokana na haja ya binadamu ya kulima na kufuga mifugo, ameendelea kufyeka miti akisaka mashamba na maeneo ya malisho ya mifugo, hivyo kubadili maisha moja kwa moja ulimwenguni. Hivyo basi, takriban kila kiumbe hai ameathiriwa na shughuli za binadamu. Halafu wanahitimisha kuwa, anthroposenia ni zao la mabadiliko ya mazingira, maisha na tamaduni ulimwenguni yanayozalishwa na shughuli za kila siku za binadamu. Hata hivyo, wanasisitiza kuwa kando na ongezeko la idadi kubwa ya watu ulimwenguni, binadamu amechangia anthroposenia pakubwa kutokana na haja za kiutandawazi. Kazi zao zilichangia hii ya mtafiti katika kuchunguza binadamu

kama aina ya anthroposenia. Ingawa waliangaza uhakikimazingira kama nadharia ya uhakiki hawakuiangaza katika misingi ya uhakiki wa riwaya ya Kiswahili.

Lara na wenzake (2018) wanadokeza kuwa, uhakikimazingira katika mtazamo wa kifeministi huangazia uhusiano uliopo katika dhuluma dhidi ya mwanamke na upujufu wa mazingira. Kadhalika, wanaongeza kuwa mtazamo wa mazingira kwa jumla katika mtazamo wa fasili za kidini ulianza katika kipindi cha miaka ya tisini pamoja na mawazo ya kiikolojia masomo ya kidini. Hata hivyo, athari za kifeministi katika fasili za ikolojia katika misingi ya dini zilikita mizizi katika makala ya kwanza makuu yaliyochipuka katika kipindi cha baada ya elfu mbili (2000). Ingawa wanaangaza mchango wa mwanamke katika mazingira katika msingi wa dini kwa mtazamo wa kifeministi; tofauti na mtafiti aliyeangaza dini katika misingi ya utepetevu wa binadamu kama aina ya anthroposenia, kazi yao ilichangia hii ya mtafiti katika kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili. Kadhalika, tofauti nao, mtafiti hakuongozwa na Nadharia ya Uhakikimazingira kwa mtazamo wa kifeministi ila nguzo kuu za Uhakikimazingira.

Kwa misingi hiyo hiyo, Coughlin na Gephart (2020) wanasisitiza kuwa, mwanafalsafa wa kiuhakikimazingira Timothy Morton anatetea hoja kuwa, kuna haja ya kuwaza kwa kina na upana ili kumaizi changamoto na dhiki za kimazingira ambazo ni kubwa na nzito katika anthroposenia kama vile ongezeko la joto ulimwenguni na mabadiliko hasi ya mifumo ya ikolojia. Kwa upande wa aina za anthroposenia, wanashikilia msimamo kuwa, athari na aina za anthroposenia ulimwenguni zimepokea uhakiki na uchunguzi haba katika kutoa mwanya kuhusu mchango wao katika kupalilia maendeleo endelevu, maliasili na vipengele vya utamaduni vinavyochangia mabadiliko hasi ya ikolojia. Wanasema kuwa baadhi ya vipindi vya runinga vinasifu na kuabudu anthroposenia kupitia uchimbaji wa madini na anthropomofiki zinazopalilia anthroposenia. Kazi yao ilifaa hii ya mtafiti katika kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili. Hata hivyo, tofauti na uchunguzi wao wa kumulika jinsi anthroposenia imeshamiri katika misingi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika sanaa ya muono, utafiti huu ulichunguza aina za anthroposenia katika misingi ya Uhakikimazingira katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Harvey (2020), Sklair (2022), Butler (2024), Dyke (2025) na Maier na wenzake (2025) wanafafanua kuwa, anthroposenia ni kipindi ambacho mabadiliko ya anga yanachangiwa na kusababishwa na shughuli za kila siku za binadamu. Wanasisitiza kuwa, zaidi ya kuwa kipindi ambacho kilichipuka kabla ya karne ya kumi na tisa ni kipindi ambacho kinatawaliwa na ukoloni mamboleo, kushamiri kwa ubidhaaishaji wa ubepari, ongezeko la uchafuzi wa mazingira, pamoja na upujufu wa ulimwengu kama matokeo ya shughuli za binadamu, uhamaji wa wanyama, na umwagaji wa kemikali usiowajibikia mazingira kutoka viwandani. Kipindi hiki hutawaliwa na ubinafsishaji wa Uropa, imani na itikadi ya Ukristo katika utawala na udhibiti wa binadamu ulimwenguni. Hata hivyo, watafiti wengi leo hii, wana mwelekeo wa kimazingira ambao umekuwa ukielekeza na kutawala karne hii, hasa katika fani ya sanaa na fasihi. Hivyo, wanasisitiza kuwa, muono wa anthroposenia kupitia jicho la utamaduni wa ikolojia na ule wa jamii kama viungo sawa vinavyokamilishana. Kazi zao zilichangia hii ya mtafiti katika kuchunguza binadamu, mabepari na mabeberu wa kisasa kama aina za anthroposenia. Hata hivyo, kazi zao zilitofautiana na utafiti huu katika kuzifafanua aina za anthroposenia kwa kuongozwa na nguzo kuu za Uhakikimazingira.

White na Whitlock (2021) wanadokeza kuwa anthroposenia husheheni ubepari wa kiulimwengu, athari hasi za uchafuzi wa mazingira na ukataji miti ovyo miongoni mwa matokeo mengine, ambapo shughuli hizi zimefikisha ulimwengu kiwango cha kujiua kiikolojia. Wanaongeza kuwa mabadiliko ya hali ya hewa ya anthropojeniki ni tatizo ndogo linalofunika suala nzito la ubepari wa kimataifa. Hata hivyo, suala hili kamili huwa halitambulishi ubepari wa kisasa kama wakala wa kipekee wa vurugu dhidi ya mazingira. Hivyo, anthroposenia huhusisha pia shughuli ambazo huwa za kabla ya ujio wa ubepari. Shughuli hizi, kimsingi, ni uvumbuzi wa ukulima, ukataji misitu, ongezeko zaidi la idadi ya watu duniani, mmomonyoko wa udongo, uvuvi zaidi ya kiwango kinachostahili, na kutoweka kwa wanyama wakubwa katika ikolojia (Head, 2018; Chandler na wenzake, 2020; Burdon, 2023). Kazi za wataalamu hawa zilichangia utafiti huu katika uchunguzi wa mabepari kama aina ya anthroposenia. Tofauti nao mtafiti aliangaza ujio wa ubepari katika misingi ya mabepari wenyewe na uharibifu wa mazingira wanaoendelea kupalilia ulimwenguni. Uchunguzi huu uliongozwa na nguzo za uwezo na haki na maadili za mazingira.

Fiedorczuk na wenzake (2023) wanaangazia binadamu kama aina ya anthroposenia kupitia utamaduni huluti unaokiuka utamaduni asili uliohimiza uhifadhi wa mazingira zaidi kuliko upujufu. Wanadai kwamba wakati binadamu wote kwa ujumla wameongeza ushawishi wao katika ikolojia ya sayari inayojulikana kama anthroposenia, uwezo wa mtu binafsi umebadilika kinyume chake, hali wanayoiita agensini. Kufikiria kuhusu anthroposenia yenye fahamu ya kibinafsi haielekei kwenye vionjo vya jiolojia au vipimo vya mabadiliko ya sayari; badala yake, inachunguza mabadiliko ya kitamaduni na kiakili yanayokwenda sambamba na ufahamu mkubwa wa mabadiliko makubwa ya mazingira yanayoonekana wakati wetu. Kulingana nao, utamaduni huluti umechangia mienendo, hulka na tabia zinazopalilia upujufu wa mazingira zaidi kuliko uhifadhi na utunzaji. Kazi yao ilichangia hii ya mtafiti katika kuchunguza binadamu kama aina ya anthroposenia. Hata hivyo, ilitofautiana na utafiti huu wa mtafiti kwa kuwa wao walijikita katika kufafanua maandishi ya kimazingira ilhali utafiti huu ulijikita katika kuchunguza aina za anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili katika misingi ya Uhakikimazingira.

Ong na Whittles (2024) wanasisitiza kuwa binadamu kupitia ubepari amekuwa akichangia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa hiari na wakati mwingine bila hiari ila kutokana na mahitaji msingi. Ingawa wanaojipata wakiyanajisi mazingira bila hiari ni wale wanaosukumwa na ufukara. Kwa ujumla binadamu amekuwa akipalilia unajisi wa mazingira kama zao la shughuli zake za kila siku. Katika kazi yao, akina Ong wanachambua fasihi kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni inayounganisha wasomaji na athari za hali ya hewa na dharura za ikolojia katika maeneo husika. Kitabu chao kinaingiza kuvunjika kwa ikolojia ndani ya historia ya ukapitalisti wa ukoloni, kuchunguza jinsi fasihi inavyotusaidia kutunga na kuumba dunia inayoweza kukalika na yenye haki kwa aina zote za maisha. Kazi yao inawaletea wasomaji dhana ya anthroposenia pamoja na mitazamo inayopinga dhana kwamba mgogoro wa hali ya hewa unasababishwa na binadamu wasio na utofauti. Kazi yao ilichangia utafiti huu wa mtafiti katika kuchunguza mabepari na kapitalosenia kama aina za anthroposenia katika kazi za kifasihi. Hata hivyo, kazi ilitofautiana na utafiti huu pale ambapo wao hawakuongozwa na Nadharia ya Uhakikimazingira wala hawakuchunguza mabepari na kapitalosenia kama aina za anthroposenia ila kama mizizi ya anthroposenia.

Paszkiewicz na wenzake (2025) wanasema kuwa dhana ya anthroposenia imekuwepo tangu kipindi cha 1800. Wanaeleza kuwa anthroposenia ni epoki ambalo linatumiwa kuelezea kipindi na muda wa hivi majuzi katika historia ya ulimwengu, ambapo shughuli za kibinadamu ambazo zimeathiri kwa kiwango kikubwa mifumo ya ulimwengu ya hali ya anga na ya kiikolojia. Dhana ya anthroposenia hivyo basi, imerejelewa kama kipindi cha kijiolojia ulimwenguni. Wasomi wanabisha kuwa anthroposenia ilitambulishwa na ukweli kuwa shughuli za binadamu zimepiku matokeo ya kiulimwengu katika kusukuma dunia kwenye janga la uharibifu wa hewa, upungufu na ukosefu wa mvua, mmomonyoko wa udongo, ufyekaji wa misitu, umwagaji taka zenye kemikali ovyo na mbinu hatari za ukulima. Kuna watafiti ambao huamini kwamba, ukulima na ufyekaji wa misitu ni shughuli ambazo zimeathiri mfumo wa dunia na kutanguliza epoki jipya. Epoki hili hudaiwa kuwa lilianza maelfu ya miaka iliyopita. Kazi yao ilichangia hii ya mtafiti katika uchunguzi wa aina za anthroposenia kwa kumaizi anthroposenia yenyewe. Hata hivyo, mtafiti alipiga hatua na kuchunguza aina zenyewe kama vile binadamu na mabeberu wa kisasa kwa kuongozwa na nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira.

### 2.1.2 Mbinu Zilizotumiwa Kusawiri Anthroposenia

Okuku (2010) anarejelea fani kama vile; taashira, jazanda, sitiari, chuku na majazi kwa lengo la kuonyesha uhusiano wa mbinu za kiisimu na matini za fasihi. Alitumia uchanganuzi wa kiisimu kuchanganua matini ya Said Ahmed Mohamed ya K*iza katika Nuru.* Mtafiti alinufaika kutokana na utafiti wa Okuku katika kuhakiki baadhi ya mbinu za lugha zilizotumika kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule. Hata hivyo, tofauti naye, mtafiti aliangaza mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili katika misingi ya uhakikimazingira. Utafiti wa Okuku ulimfaa mtafiti katika kuchanganua mbinu kama vile za lugha ambazo waandishi wametumia kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule.

Katika kazi yoyote ya fasihi, msomaji anaweza kujifunza kwa kina zaidi na kwa kuyapa maneno au muundo umakini kutegemea namna mwandishi anavyoyachagua na kuyatumia katika kazi yake tofauti na mwandishi mwingine yeyote (Ngugi na Nabea, 2011). Namna ambavyo mwandishi huyatumia maneno katika kazi yake huweza kuipa kazi mnato na upekee katika kuwasilisha ujumbe lengwa kwa hadhira lengwa. Wasomi hawa wanafafanua mbinu kama dhana ambayo hujishughulisha na usomi wa fasihi kwa kutumia isimu elezi. Hivyo, wanasisitiza kuwa mbinu hunuia

kupambanua uhusiano kati ya lugha na uamilifu wa kisanaa katika matini za kifasihi. Kadhalika, wanaongeza kuwa, mbinu ni njia ya kutekeleza usomi wa lugha ambao hutumia uchanganuzi wa maelezo ili kufanikisha uvumbuzi kuhusu muundo na uamilifu wa lugha. Kazi yao ilichangia hii ya mtafiti katika kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili. Hata hivyo, tofauti nao mtafiti alitafiti namna waandishi wa kazi walivyotumia mbinu kusawiri anthroposenia kwa kujikita katika nguzo za nadharia ya uhakikimazingira.

Wahakikimazingira pamoja na wasomi wengine wa fasihi ambao hupendezwa na mazingira wameweza kuegemea kwenye tathmini ya maandishi ambayo moja kwa moja huhusu aina za anthroposenia na huangaza zaidi suala la uelekeo kuliko la usemi (Scott, 2012). Hivyo, Scott katika kazi yake anajadili kuwa ni wakati wa kuchukua hatua nyingine katika uhakikimazingira. Anatoa kauli kuwa, watafiti wanahitaji kutalii uwezo wa lugha wa kusikika na wa kitamathali katika kuamsha ulimwengu asilia kwa njia zenye uwezo. Kazi yake ilichangia utafiti huu katika kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili. Hata hivyo, tofauti na Scott anayependekeza kuwa watafiti waangaze uwezo wa lugha wa kusikika na wa kitamathali katika kuhamasisha jamii kuhusu ulimwengu asilia, mtafiti aliangaza matumizi ya baadhi ya tamathali za lugha kama vile; taashira, tashbihi, uhuishi na mbinu zingine nyingi kama vile anthropomofiki katika kusawiri anthroposenia mbalimbali katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Ufanisi wa mwandishi wa kupitisha ujumbe katika fasihi huchangiwa pakubwa na mbinu na maarifa ya msanii katika kupitisha ujumbe nuiwa kwa hadhira lengwa. Matumizi ya lugha huweza kuangaliwa kama mtindo wa mtu binafsi au mazoea yake katika uandishi wa fasihi. Kimsingi, mwandishi ana uhuru wa kuteua mbinu zake za kuwasilisha ujumbe lengwa (Onchangu, 2013). Onchangu ameangaza matumizi ya mbinu katika riwaya na hadithi fupi za Clara Momanyi. Utafiti wa Onchangu ulichangia huu wa mtafiti katika kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili. Hata hivyo, tofauti na Onchangu aliyetumia Nadharia ya Elimu-Mtindo mtafiti alitumia Nadharia ya Uhakikimazingira na pia badala ya kutafiti kazi za Clara Momanyi alitafiti kazi za Emmanuel Mbogo na Katama Mkangi.

Dhana ya kuhusisha fasihi ya ikolojia katika fasihi ya Kiswahili ilishika kani katika mwanzo wa karne ya ishirini na moja. Kwa mujibu wa Nabeta na Ongutte (2014) riwaya ya *Bustani ya Edeni* (Mbogo, 2002) ambayo ilitafsiriwa na Timothy Arege kutoka *The Garden of Eden* ndiyo kazi ya kwanza ya fasihi ya Kiswahili kuandikwa katika misingi ya kimazingira. Kwa misingi hii, kazi zingine za fasihi ya Kiswahili katika misingi ya kimazingira zilizoandikwa na wasomi kama vile: Mberia (2001), Mohamed (2001), na Momanyi (2009) zilifuata. Waandishi hawa wamechangia kwa kiasi kikubwa usomi katika uwanja wa fasihi-mazingira wa Kiswahili. Kupitia kazi zao, wamebainisha masuala ya kianthroposenia yanayoathiri jamii ya Afrika Mashariki na ulimwengu kwa jumla, moja kwa moja kwa njia chanya na hasi kimwavuli. Mathalani, kupitia kazi zao wanadhihirisha mbinu za lugha zilizotumika kusawiri anthroposenia, ambazo zinazalishwa na maendeleo katika sayansi, teknolojia ya kisasa na utandawazi katika mataifa mengi barani Afrika na duniani kimwavuli. Ingawa mtafiti hakutafiti kazi hizi, mojayazo – *Bustani ya Edeni* – ilitafitiwa katika misingi ya Uhakikimazingira ili kuangaza anthroposenia. Kadhalika, mtafiti aliangaza utanzu wa riwaya ya Kiswahili bila kuchanganya tanzu zingine na kuhusisha riwaya nne teule, huku akihakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia.

Kulingana na Musembi (2019), Katama Mkangi ametumia taswira kimakusudi kama mbinu kwepi, kwa lengo la kuwasilisha ujumbe lengwa kwa hadhira lengwa bila kuweka kazi yake kwenye hatari ya kupigwa marufuku. Kazi yake ililenga na ingali inalenga na kumulika kwa ushabaha uozo katika jamii na hususan katika uongozi. Uozo huu huishia kupalilia anthroposenia kwa kuyachafua na kuyaharibu mazingira. Katama Mkangi alitumia taswira kama kurunzi ya kumulika uozo huu kupitia kazi zake za kifasihi. Baadhi ya masuala muhimu kwa wanajamii yanayosheheni uozo huu ni pamoja na siasa, jamii, uchumi, dini, ufisadi na hasa sana uongozi mbaya chini ya kunga za ukoloni mamboleo. Katama Mkangi katika *Mafuta* na *Walenisi* ametumia taswira kuwashambulia wenye mamlaka bila kuibua hisia kali wala kuwakemea moja kwa moja. Kwa njia hii, mtunzi Mkangi amefanikiwa kuanika upungufu na uozo wa jamii yake na jamii pana ya ulimwengu paruwanja. Ingawa Musembi ameangaza mbinu ya taswira pakee bila kuihusisha moja kwa moja na anthroposenia, makala yake yalifaa utafiti huu katika kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Katama Mkangi na Emmanuel Mbogo. Tofauti naye, mtafiti alihakiki taswira kama ilivyotumiwa kusawiri anthroposenia katika kazi mbili

husika za Mkangi kwa kuongozwa na baadhi ya nguzo za Nadharia ya Uhakikimazingira, mintarafu ya madhumuni ya utafiti.

Kwa upande mwingine, Waithiru (2019) ameangaza matumizi ya taashira katika misingi ya kibaada ukoloni na kimtindo. Anaeleza jinsi taashira kama mbinu inafanikishwa kupitia utandawazi na jiografia katika tamthilia mbili teule za Kiswahili. Utafiti wake utajenga huu wa mtafiti kimbinu. Hii ni kwa sababu, kama Waithiru, mtafiti atahakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili na kwa msingi huu ataangaza tamathali za lugha, mbinu kama vile anthropomofiki na nyingine nyingi. Hata hivyo, tofauti ilidhihirika pale ambapo, tofauti na Nadharia za Baada ya Ukoloni na Umitindo, mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Uhakiki mazingira. Pia, tofauti na mbinu ya taashira, utandawazi na jiografia, mtafiti aliangaza anthroposenia mbalimbali zilizosawiriwa kupitia mbinu mbalimbali katika riwaya nne teule bali si za lugha tu.

Simpson (2021) amedhihirisha kina cha kuridhisha na upana wa haja katika uchunguzi wake wa mbinu za kimtindo, mada na maudhui. Anashikilia msimamo kuwa, mazoezi na usomi wa mbinu, hasa za kifasihi huhusisha uchunguzi wa mbinu husika. Hivyo, kama wasomi, jambo linalotarajiwa kila wakati katika kazi ya maandishi ni uwezo wa kazi yenyewe kuweza kuangaza masuala yanayoathiri jamii moja kwa moja na pia iweze kupasha ujumbe zaidi ya dhana zinazowasilishwa na istilahi zilizotumiwa, mada au suala la utafiti pamoja na kuweza kuwa ya thamani kila siku. Kazi yake inatofautiana na hii ya mtafiti katika misingi kuwa, tofauti na Simpson anayeangaza namna kazi ya fasihi inavyoweza kupitisha ujumbe nuiwa kwa kutumia mbinu za uandishi kuwasilisha dhana pana kuliko maana ya kawaida ya maneno yaliyohusika, mtafiti aliangaza mbinu zilizotumiwa na watunzi Mbogo na Mkangi kusawiri anthroposenia kimwavuli bila kujifunga katika zile za uandishi tu. Hata hivyo, kazi yake ilichangia utafiti huu katika kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Katika kuhakiki taashira za jumba hai la Usher kwa mtazamo wa kiuhakikimazingira, Waithiru (2022a) anaeleza kuwa, Edgar Allan Poe alitumia jumba la Usher kuashiria uhusiano kati ya taifa, viongozi wao, wananchi pamoja na mazingira yanayolizingira ndani na nje. Ingawa Poe hajataja moja kwa moja kuhusu suala la anthroposenia ulimwenguni, ameangaza athari hasi za anthroposenia zinazonyonga ulimwengu kila

kuchao, kama vile, vurugu dhidi ya mazingira, kujiua kimazingira na upujufu jumla wa mazingira. Tofauti naye, mtafiti aliangaza anthroposenia moja kwa moja na hususan alihakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili bila kujifunga katika taashira. Hata hivyo, makala yake yalichangia mtafiti katika kuhakiki suala la mbinu ya taashira kwa kuongozwa na nadharia ya Uhakikimazingira pia. Kwa misingi hiyo hiyo, Waithiru (2022b) ameangaza namna mbinu ya taashira imetumiwa na waandishi katika fasihi ya watoto kusawiri dhana za kimazingira kama vile; rangi, wanyama, ndege, wadudu, pamoja na binadamu, kwa njia nyepesi na inayopendeza watoto. Ametathmini namna waandishi wa fasihi ya watoto hutumia taashira za kimazingira kwa kutumia jicho la mtoto kuashiria dhana pana na msingi, sio tu kwa watoto ila pia kwa jamii kimwavuli. Amehakiki kazi mbili za fasihi ya watoto kwa kuongozwa na nadharia ya Uhakikimazingira. Makala yake pia yalichangia utafiti huu kwa upande wa mbinu na wa nadharia. Lakini tofauti ilidhihirika pale mtafiti alihakiki riwaya nne teule bila kujifunga katika fasihi ya watoto na katika suala ngeni na tofauti na kazi ile ya anthroposenia.

### 2.1.3 Rai za Waandishi wa Kazi za Fasihi Kuhusu Jinsi ya Kukabiliana na Anthroposenia

Katika kupitia matawi yote ya kiusomi, Watson na Watson (2007) wanadhihirisha kuwa tangia kipindi cha kuzaliwa kwa ikolojia ya kisasa na epistemolojia, dhana hizi zimekuwa dhana mbili pacha. Wanasema kuwa, uanzilishi wa miji, ubepari, ukoloni, ufufuaji wa nadharia ya kushuku, ishara za kitaashira, na teknolojia za elimu ya nuru zilichangia njama ya kufakisha watu kutoka duniani na uhalisia wenyewe katika anthroposenia. Fasihi na sanaa za muono zilipeleleza baadhi ya mazao ya vidonda vya kitamaduni, kuashiria dhiki na kupendekeza baadhi ya tiba bunifu katika anthroposenia. Watson na Watson walimulika baadhi ya suluhu dhidi ya anthroposenia katika harakati za maendeleo kwa mazingira kwa kuegemea upande wa binadamu pekee kama aina ya anthroposenia. Tofauti nao, mtafiti aliangaza rai za waandishi wa riwaya nne teule za Kiswahili kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili. Hata hivyo, kazi yao ilichangia hii ya mtafiti katika kutathmini rai za waandishi hawa hususani kuhusu namna ya kudhibiti anthroposenia katika riwaya nne teule katika misingi ya Uhakikimazingira.

Kazi za fasihi zimeweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uhifadhi wa mazingira (Wamitila, 2010). Wamitila anajadili kuhusu namna meli zinazosafirisha mafuta zinavyoharibu maji safi baharini kwa kulinajisi bahari. Tukio hili la kianthropomofiki linazalisha athari hasi kwa mazingira katika anthroposenia. Mafuta haya yanapujua mazingira kwa sababu, yanapoingia majini yanasababisha maafa ya mimea na wanyama wa majini kutokana na ukosefu wa hewa na kemikali sumu. Hili linapelekea kodhoofika kwa baadhi ya chumi kwani baadhi ya wanajamii, hasa wanaoishi karibu na ukingo wa ziwa au bahari, hutegemea uvuvi kama kitega uchumi chao. Hili hutinga maendeleo endelevu katika jamii. Wamitila, anaonyesha pia athari hasi za mabadiliko ya tabia nchi ulimwenguni yanayosababisha upungufu na wakati mwingine ukosefu wa mvua. Mabadiliko ya tabianchi yanasababishwa na ufyekaji wa miti na uchafuzi wa mazingira bila kujali athari zake. Haya yote yanaimarisha anthroposenia. Ingawa kazi yake haijaangaza anthroposenia yenyewe, imetoa mwanga kuhusu namna ya kukabiliana na anthroposenia. Kazi ya Wamitila ilichangia hii ya mtafiti katika kuchanganua data akiongozwa na mhimili wa maendeleo endelevu. Hivyo, ilichangia utafiti huu katika kutathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule za Kiswahili kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika misingi ya Uhakikimazingira. Hata hivyo, kazi yake inatofautiana na hii ya mtafiti kwa sababu mtafiti aliongozwa na nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira, tofauti na Wamitila anayetumia misingi ya uchanganuzi wa fasihi kwa jumla.

Outka (2013), anatathmini suala lililotengwa lakini msingi na muhimu sana katika elimu ya uhakiki wa ubaguzi wa kimbari na uhakikimazingira: suala la ubaguzi wa kimbari wa kimazingira. Suala hili ni sehemu muhimu katika anthroposenia. Katika kazi yake, alitathmini jinsi bonde pana na refu lililopo kati ya tajriba za Wamarekani wa Uropa na Wamarekani Waafrika kuhusu dunia asilia zilivyokuzwa na kuendelezwa na utamaduni na historia ya Wamarekani asili, pamoja na namna tajriba hizo zilivyoumba na kujenga ubaguzi wa kimbari. Ujenzi wenyewe ulifanikishwa na matumizi ya anthropomofiki mbalimbali. Haya aliyaafikia kwa kuchota kutoka Nadharia ya Adhama, ya Kimuyemuye na ya Uhakikimazingira. Outka alitumia nadharia tatu kuangaza athari za tajriba za baadhi ya wanadamu kwa mujibu wa maeneo tofauti, utamaduni na historia ya jamii husika kupitia anthropomofiki tofautitofauti zinazojinasibisha na janibu za Marekani na Uropa. Mtaalamu huyu anahimiza kuwa anthropomofiki za maeneo na utamaduni ni vipengele ambavyo

vinachangia kusuluhisha anthroposenia katika kazi yake. Hili lilichangia utafiti huu wa mtafiti katika kutathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule kuhusu namna ya kukabiliana na anthroposenia katika misingi ya kimazingira. Kadhalika, tofauti naye, mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Uhakikimazingira katika uchanganuzi wa data.

Ong'utte (2014) amehakiki suala la uhifadhi wa mazingira katika ushairi, tamthilia na riwaya kwa kugusia baadhi ya sura na maonyesho kadhaa katika misingi ya uhakiki ki-mazingira. Amejadili hali halisi ya uharibifu wa mazingira kwa kuchanganua uamilifu wa kimaudhui, kijamii, kihistoria, kiitikadi na kimbinu katika mazingira asilia kama unavyohusishwa katika fasihi. Amejikita katika kuzuia uharibifu wa mazingira. Utafiti wake ulichangia huu wa mtafiti katika kuhakiki suala la anthroposenia katika misingi ya Uhakikimazingira, hasa katika uhakiki wa kutathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule za Kiswahili kuhusu namna ya kukabiliana na anthroposenia. Hata hivyo, tofauti na Ong'utte aliyeshughulikia tanzu tatu teule za fasihi na tena kwa kugusia baadhi ya sehemu, mtafiti alishughulikia utanzu mmoja wa riwaya kwa kina na kujikita katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Oliver (2016) anafafanua kuwa, jukumu la Ngugi katika kanoni ya mabadiliko na elimu ya kung'oa ukoloni kwa jumla lilisaidia kukita mizizi ya nidhamu ya mafunzo ya baada ya ukoloni, hata kama halikuondoa idara za Kiingereza katika janibu zilizowahi kumilikiwa na Mbeberu. Kwa kumsawiri Ngugi kitaashira, Oliver anasema kuwa binadamu ana jukumu la kubambua magamba ya athari hasi za ukoloni kimwavuli, hasa katika mataifa yaliyowahi kutawaliwa na Mbeberu, enzi ya ukoloni mkongwe, ili kuweza kukabiliana na changamoto katika mazingira yake. Anasisitiza kuwa elimu ya msomi wa kuasi ukoloni mamboleo ndiyo ala kuu ya kumuongoza na kumwelekeza binadamu katika mazingira yake. Oliver anaongeza kuwa, ingawa mchakato mzima unavumbikwa na changamoto tele, hasa kutoka kwenye himaya zinazonufaika hadi sasa kutokana na mfumo wa utandawazi, hatimaye binadamu atafaulu. Tofauti naye, mtafiti alitathmini rai za waandishi Mbogo na Mkangi kuhusu namna ya kukabiliana na anthroposenia kwa kujifunga katika upeo na mipaka ya riwaya nne teule za Kiswahili. Hata hivyo, kazi yake ilifaidi utafiti huu katika kutathmini elimu kwa jumla kama njia mwafaka na madhubuti ya kukabiliana na anthroposenia.

Kwa mkondo huo, Mwaniki (2019) ameangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ikolojia katika ushairi wa Mberia kwa kutumia Nadharia ya Ikolojia. Aidha, ameeleza njia mwafaka kutoka kwenye kazi za fasihi kuhusu jinsi ya; kuhifadhi misitu, kuzuia uharibifu wa hewa na ongezeko la joto; uchafuzi wa mito na mabwawa; mmomonyoko wa udongo na kuhifadhi milima, mabonde, bahari na maziwa. Kazi yake ilichangia utafiti huu katika kutathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule za Kiswahili kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia. Hata hivyo, tofauti na utafiti wake, mtafiti aliangaza anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili na kuchota suluhu dhidi ya anthroposenia kutoka kwa rai za waandishi wa kazi husika za fasihi. Kadhalika, mtafiti hakuangazia ushairi wa Mberia ila aliangazia riwaya nne teule za Kiswahili na kuongozwa na nguzo saba kuu za Uhakikimazingira badala ya tano zilizomuongoza Mwaniki.

Sabula (2014) ameshughulikia suala la nafasi ya wanawake katika uhifadhi wa mazingira katika misingi ya ufeministi wa kiikolojia. Anaonyesha nafasi na jitihada za mhusika wa kike Nakuruto katika harakati za kuhifadhi mazingira. Njia kuu ambayo Nakuruto anatumia kuhamasisha jamii kuhusu athari za kupalilia anthroposenia ni anthropomofiki, hasa za chemichemi za maji.  Anadhihirisha jinsi ufeministi wa kiikolojia unavyochangia pakubwa katika kuzuia athari hasi za anthroposenia. Isitoshe, Sabula anadhihirisha nafasi ya ufeministi wa kiikolojia katika kuwaamsha wanawake kupigania ukombozi na uhifadhi wa mazingira. Aidha, amedhihirisha namna Nakuruto anavyoelimisha wanajamii kuhusu anthroposenia na namna wanavyoweza kujikomboa kotokana na janga hili. Anaendelea kuonyesha namna mwanamke anavyonyanyaswa na kudhulumiwa anapojaribu kujihusisha na shughuli za uhifadhi wa bayotiki na ikolojia. Amedhihirisha namna dhiki na changamoto kama vile, ulofa, kukauka kwa chemchemi za maji, maradhi na maangamizi yanayozalishwa na anthroposenia. Utafiti wake ulichangia huu wa mtafiti katika kutathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule za Kiswahili kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia. Tofauti na utafiti wa Sabula, utafiti huu ulijikita katika misingi ya Uhakikimazingira na kuhakiki riwaya nne teule za Kiswahili bali si moja.

Kwa mujibu wa Ahmandi (2024), matumizi madhubuti ya vifaa na rasilimali asilia yanaweza kuchangia pakubwa katika kudidimiza madhara ya anthroposenia ulimwenguni. Anachunguza sanaa ya maigizo ya kisasa kupitia lensi ya uchambuzi wa kiuhakikimazingira inayoelezwa katika anthroposenia. Inakadiria jinsi fikra za

anthroposenia zinavyoshirikisha njia tofauti za uwakilishi wa maigizo pamoja na jinsi vifaa vya maigizo na vile asilia vinavyoweza kukabiliana na changamoto za uwakilishi zinazobadilika kati ya binadamu na ulimwengu usiokuwa na ubinadamu. Kazi yake ilichangia hii katika kutathmini matumizi madhubuti ya vifaa na rasilimali asilia yanaweza kuchangia mikakati kabambe ya kukabiliana na anthroposenia ulimwenguni. Hata hivyo, tofauti na kazi yake ambayo haikubainishwa bayana matumizi madhubuti ya vifaa na rasilimali asilia kama mbinu ya kukabiliana na anthroposenia mtafiti alitathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule za Kiswahili katika kukabiliana na anthroposenia katika misingi ya Uhakikimazingira.

Peresen na wenzake (2024) wanasisitiza kuwa, binadamu yu karibu na hatua za mabadiliko ambazo, mara zikifikiwa, zitabadilisha sana maisha duniani katika miongo ijayo. Kazi yao inarekebisha elimu kama isiyoepukika kutoka kwa vitisho vingine vya binadamu na nguvu za asili ambazo zinaonekana kuwa zinaunganishwa zaidi katika uzalishaji wa pamoja wa hali yetu ya sasa. Kulingana nao, elimu ni njia ya kipekee ya kukabiliana na changamoto za kimazingira zinazozalishwa na shughuli za kila siku za binadamu katika harakati zake za kujiendeleza kijamii, kisiasa na kiuchumi. Hivyo, kazi yao ilichangia utafiti huu wa mtafiti katika kuangaza elimu kama namna madhubuti ya kukabiliana na anthroposenia. Hata hivyo, tofauti nao ambapo waliangaza elimu kwa upekee mtafiti aliangaza elimu kama rai iliyotolewa na waandishi wa riwaya nne teule katika kukabiliana na anthroposenia katika misingi ya kiuhakikimazingira.

## 2.2 Msingi wa Nadharia

Uhakikimazingira ni mtindo ambao hutazama viwakilishi vya viumbe vyote na mandhari katika matini zenye; fani zote, imani, mila na desturi kwa kuangaza hasa mielekeo mintarafu ya viumbe vyote pamoja na balagha inayotumika, punde tu ule mtindo unapozungumziwa. Hujinasibisha na uhamasishaji wa mazingira pamoja na nadharia ya jamii kwa kuamini kuwa balagha ya matini zenye fani zote na utamaduni huakisi na hufahamisha nyenzo za utekelezaji mintarafu ya mazingira, huku ukijitahidi kupanua utambuzi kuuhusu na kujihusisha na kazi za fasihi pamoja na sayansi za ikolojia na mitazamo tofauti tofauti (Nayar, 2010). Kwa mujibu wa Howarth (1996), uhakikimazingira ni dhana ambayo etimolojia yake ni ya Kigiriki. Anashikilia kauli kuwa, maneno ‘eco’ na ‘critic’ yanatokana na ‘oikos’ na ‘kritis’.

Neno ‘oikos’ katika Kigiriki linaashiria nyumba na ‘kritis’ linaashiria kuhukumu, kuhakiki, kutathmini na kukosoa makosa ya kitu, jambo au hali fulani pia. Hivyo, kulingana na Howarth, uhakikimazingira ni kuhukumu, kukosoa na kurekebisha hali mbaya ya dunia yetu ambamo ndimo makazi yetu sote. Philips (2003) anaeleza mhakikimazingira kama mja ambaye hujishughulisha na shughuli ya kukarabati, kuurejesha uhai wa mazingira kwa kukashifu anthroposenia, kutathmini ubaya na uzuri wa utamaduni fulani kwa mazingira na hatimaye kuibuka na suluhu mwafaka kusuluhisha matatizo na changamoto zinazoyaguguna mazingira katika anthroposenia.

Akiwanukuu Glotfelty na Fromm (1996) anashikilia msimamo kuwa, uhakikimazingira ni uhusiano baina ya kazi ya kifasihi na mazingira asilia yanayomsheheni mwanadamu. Uhakikimazingira ulichukua mtazamo wa kiardhi kwa masuala ya kifasihi. Larsson (2019) anasema kuwa, uwanja wa fasihi-mazingira ni mpana na wa kina. Anaongeza kuwa upo mintarafu ya wanadamu kuhakiki na kuandika diskosi mbalimbali kuhusu mandhari, sehemu za dunia, spishi za viumbe hai, maliasili na uzuifu wa uchafu wa viwandani. Mkabala huu unanuia kutoa taswira halisi ya jinsi wasanii wanavyoumba na kuashiria taswira na taashira za mazingira asilia katika kazi zao za kisanii. Mwaniki (2019) anaongeza kuwa, mkabala huu huyapa mazingira nafasi kubwa katika kazi yoyote ile ya kifasihi kimwavuli. Uhakikimazingira unashadidia kauli kwamba sio kila mtunzi wa kifasihi anahusisha mazingira asilia katika matini yake bali ni watunzi wa kipekee ambao wamebobea na kuelewa masuala ya kimazingira sio tu katika mazingira yao ila pia katika jamii zao.

Buell (1996) anadokeza kuwa fasihi-mazingira ni mkabala mpya uliochipukia katika fasihi za kilimwengu na chimbuko lake ni Marekani. Ananuia kuepuka uchangamano wa kinadharia kwa jumla kwa kuziba mwanya uliopo kati ya uhusiano wa kazi ya fasihi na mazingira ya ulimwengu anaotamalaki mwanadamu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakikimazingira. Nadharia hii iliendelezwa na Cheryll Glotfelty na Harold Fromm (1996). Baadhi ya mihimili yake ni kama vile; tabia ya mwanadamu, lugha ya msanii kuoana na mazingira, binadamu dhidi ya maumbile, uwezo, kifo, lugha na mazingira, haki za kimazingira, maendeleo endelevu, maumbile, jinsia, utamaduni na mazingira, utandawazi na mingine mingi. Kadhalika, utafiti huu utaangazia jinsi riwaya ya Kiswahili huangazia masuala ibuka na uchafuzi wa

mazingira pamoja na hali zinazoathiri mazingira kupitia maendeleo ya teknolojia mintarafu ya madhumuni ya utafiti.

### 2.2.1 Nadharia ya Uhakikimazingira

Hapo mwanzo, wasomi maalumu walitoa kauli mbalimbali kuhusu anthroposenia ambazo baadhi yazo ziliwekwa kwenye kategoria za maeneo, dini, mazingira na fasihi, maeneo na fasihi na hasa sana usomi wa fasihi ya Marekani. Kila mmoja alitoa sauti lakini iliambulia jangwa la kutosikika na kutotambulika. Waldon (1836) ilikuwa mojayazo ya kazi za mwanzo msingi katika fasihi ya Kimarekani kufungua nadharia ya kimazingira iliyojikita kwenye utanzu wa ushairi. Kazi nyingine iliyoangazwa katika misingi ya uandishi wa kimazingira na kujikita kwenye misingi ya ikolojia, na ambayo ilitumiwa na wasomi wengi kama marejeleo msingi na nguzo ya kipekee katika kuhakiki kazi za kiusomi ni ile ya Walden. Walden (1854) anaweza kuchukuliwa kama baba wa uhakikimazingira. Kwa kufuata misingi ya Walden, kazi ya Norman (1923) iliasisi uwanja mpya wa kiakademia katika fasihi ya Marekani. Katika miaka ya sabini, Rueckert (1978) alitumia dhana ya ikolojia na ki-ikolojia katika kuchanganua kazi za kifasihi. Katika kipindi cha kati cha themanini, wasomi walianza kushiriki katika miradi ya pamoja na hili likapelekea uzalishaji wa uwanja wa usomi wa fasihi-mazingira na katika kipindi cha mwanzo cha tisini, uwanja huu ulikomaa na kuanza kunawiri (Glotfelty na Fromm, 1996). Hivyo, kulingana nao mtazamo wa kuangazia anthroposenia katika kazi za kifasihi ulianza kuibuka katika miaka ya themanini na kushamiri katika miaka ya tisini.

Waage (1985) alihariri makala ya *Teaching Environmental Literature: Materials, Methods and Resources*. Kazi hii ilijumuisha wataalamu kumi na tisa tofauti ambao waliandika kuhusiana na dhana ya mazingira katika fasihi. Mnamo mwaka wa 1989, Alicia Nitecki alianzisha shirika la *The American Nature Writing Newsletter* (A.L.W.N) ambalo kusudi lake lilikuwa ni kuchapisha, makala mafupi, uhakiki na maelezo mafupi ya vitabu, maelezo darasani na taarifa zilizohusiana na usomi wa uandishi kuhusu bayotiki na ikolojia. Shirika hili lilichapisha makala, vitabu na habari zingine kuhusu fasihi ya ikolojia. Katika mwaka wa 1990 Chuo Kikuu cha Neveda, Reno Marekani kilibuni ngazi ya kwanza katika usomi wa uhakikimazingira. Kadhalika, katika mwaka wa 1996, Glotfelty na Fromm walihariri kitabu cha *The Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology* na kuweka msingi madhubuti kuhusiana na fasihi ya mazingira.

Mwaniki na wengine (2019) alimhoji kwa kifupi Glotfelty kupitia kwa barua pepe. Lengo lake kuu lilikuwa kumaizi alikozaliwa Glotfelty, lini na ni kile kilichomchochea na kumpa msukumo kuandika kuhusiana na ikolojia katika kazi za kifasihi. Mwaniki na wengine wakiyanukuu majibu ya Glotfelty walisema kuwa, Glotfelty alizaliwa Julai 5, 1958. Mshawasha wa kuangaza usomi wa fasihi katika misingi ya kimazingira ulitokana na mapenzi ya juu ya mazingira na haja ya kutaka kusuluhisha changamoto zinazoyakumba mazingira. Aliongeza kuwa amekuwa msomi katika uwanja wa Kiingereza kwa muda mrefu na wakati huo wote amekuwa akiandika kuhusu ikolojia katika fasihi kama njia mojawapo ya kuchangia katika sayari yenye buheri ya afya, nadhifu na ya kupendeza. Wakihitimisha, Mwaniki na wengine (2019) wanarai kuwa, kichocheo kikuu kilichomchochea Glotfelty kuandika kuhusiana na mazingira katika fasihi ni kutokana na matatizo yanayoyakumba mazingira. Matatizo haya yasabaishwa na binadamu mwenyewe; jinsi anavyoingiliana na mazingira hasa katika kipindi hiki cha sayansi, teknolojia na utandawazi.

Hivyo basi, nadharia ya uhakikimazingira iliwekewa misingi na Glotfelty na Fromm. Hata hivyo, Buell (1996) pia alichangia pakubwa katika kuipa mizizi na kuiendeleza nadharia hii. Buell anasisitiza kuwa, mwanadamu anafaa kutekeleza shughuli zake za kila siku huku akitawaliwa na kuongozwa na mahitaji na haja za mazingira ila si tamaa, ubinafsi na ubadhirifu wa rasilimali asilia. Nadharia ya Uhakikimazingira ni ngeni na ingali katika kipindi cha ukembe. Kutokana na dhana ya ‘eco’ na ‘criticism’, dhana ‘eco’ humaanisha ikolojia. Kwa mujibu wa Scott (2012), dhana ikolojia hufasiliwa kama; mazingira, yanayotuzingira, ulimwengu, vyenye uhai na visivyo uhai, vinavyoishi na visivyoishi, bayotiki na visivyo bayotiki, na kila kitu kwenye sayari. Anatoa hoja kuwa, kila kitu huwa chini ya mwavuli mmoja uitwao ikolojia. Kulingana naye, ikolojia au mazingira ni dhana pana sana ambayo haiwezi kupambanuliwa kwa urahisi na kwamba binadamu hawezi kuishi bila utegemezi wa mazingira. Outka (2013) akimuunga mkono anakariri kuwa, maumbile yote, viumbe wote na kemikali zote zimo kwenye mashua moja iitwayo ikolojia au mazingira. Anasema kwamba, hii ndiyo sababu, daima mwanadamu amehisi hitaji la; ulimwengu, miti, mimea, matawi, mizizi, maji, jua, mvua, joto, baridi, upepo, wanyama, matunda na kila kitu kilichomo ulimwenguni kikubwa na kidogo. Hivyo basi, mahitaji ya binadamu yalimuongoza hivi kwamba, alipoanza kuandika na kusanii, aliona haja na umuhimu wa kuhusisha mazingira katika kazi yake.

Glotfelty anadokeza kuwa uhakiki wa kimazingira ni taaluma ya usomi inayomulika uhusiano na ugiligili baina ya fasihi na mazingira. Hii ni kwa sababu, namna uhakiki wa ufeministi unavyoangazia mahusiano kati ya lugha na fasihi ukizingatia kigezo cha kijinsia kwa mfano, vivyo hivyo ndivyo uhakiki wa kimazingira huchukua mtazamo wa mazingira katika usomi na uhakiki wa kazi za fasihi. Kwa mujibu wa Glotfelty na Fromm (1996) wahakiki wa nadharia ya uhakikimazingira hujiuliza maswali kadhaa wakati wanaangazia kazi za kifasihi. Maswali haya ni pamoja na: Je, ni vipi maumbile ya kiasili yanavyosawiriwa katika kazi za kifasihi? Je, ni vipi fasihi imeathiri mahusiano baina ya jamii na mazingira ya kiasili? Je, ni vipi mazingira ya kiasili yalivyobadilika kutokana na mapito ya wakati? Ni vipi matatizo yanayokumba mazingira yanavyoathiri fasihi ya kisasa na ni vipi teknolojia na sayansi ya bayotiki na ikolojia inavyoathiri fasihi? Maswali haya yatakuwa muhimu sana katika shughuli za ukusanyaji na uchanganuzi wa data mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu ili kusuluhisha suala la utafiti.

Nadharia hii inashikilia kuwa utamaduni wa wanajamii unaingiliana na ulimwengu halisi. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kuangazia mahusiano na maingiliano kati ya mazingira ya kiasili na binadamu. Ikumbukwe kwamba, binadamu, kutegemea jamii yake huweza kuwa na utamaduni mahususi katika mazingira yake. Nadharia ya uhakikimazingira huchambua kazi za kifasihi kwa kujikita katika vipashio vya uhusiano, ugiligili na pengine utegemeano kati ya binadamu na mazingira anamoishi. Kulingana na nadharia hii, utamaduni wa jamii una nafasi kubwa ya kujenga mtazamo, mielekeo na mienendo inayoathiri matumizi ya mazingira kwa namna tofautitofauti (Mhango na Bulaya, 2022). Utamaduni huwa sehemu muhimu sana na kubwa katika uhifadhi au uchafuzi wa mazingira ya jamii na ni nguzo nyingine ambayo itaongoza uchanganuzi wa data mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu. Kadhalika, mtazamo wa kimazingira kama diskosi huangazia mahusiano baina ya viumbe hai na visivyo hai. Diskosi hii ya mazingira hujumuisha mazingira ya ulimwengu wote kwa jumla kwa sababu kila kiumbe, mmea, maumbile au chombo huhusiana na kingine kwa namna moja au nyingine. Hivyo, fasihi ina jukumu la kupambanua masuala yanayohusiana na mazingira (Mwaniki na wengine, 2019). Wahakiki wa nadharia hii wanakubaliana kwamba binadamu amefikia wakati ambapo matendo yake yameathiri na kuharibu mfumo mzima wa mazingira (Ong'utte, 2014). Hivyo basi, binadamu hana budi ila kubadilisha mienendo yake au akabiliane na

majanga ya kitaifa yanayoharibu uzuri wa mazingira katika anthroposenia pamoja na viumbe vinavyoishi ulimwenguni. Upujufu wa mazingira usipositishwa binadamu atajiangamiza mwenyewe kutokana na jitihada zake potofu na mbovu (Mhango na Bulaya, 2022). Baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Uhakikimazingira ni kama vile:

i. Binadamu dhidi ya maumbile. Mhimili huu umeweza kurejelewa kama mhimili-mama na baadhi ya wasomi na watafiti (Nayar, 2010; Bertens, 2024; Ong na Whittle, 2024). Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa wataalamu hawa, binadamu hawezi kutenganishwa na maumbile katika mazingira anamoishi kwa sababu huwa na maingiliano na mahusiano ya moja kwa moja na tena ya karibu sana. Ni katika harakati za maingiliano na mahusiano haya ambapo binadamu huweza kunawiri au hata kuangamia. Watu wanakufa kila uchao kutokana na binadamu kushindwa kuyalinda na kuyatunza mazingira na hivyo anaangamia kutokana na njaa, nduli, mafuriko, kemikali, na mmomonyoko wa udongo. Robert na Christine (2016) wanasema kuwa, binadamu huweza kuamka kutoka usingizi wa mapuuza ya mazingira punde tu panapotokea janga kutokana na uchafuzi wa mazingira. Mathalani, binadamu atagutuka pale wenzake wanapoaga dunia kutokana na kuwala samaki waliomeza madini sumu kwa mwili wa mwanadamu. Madini haya hutokana na umwagaji taka za viwanda, umwagaji taka pamoja na kemikali kwenye bahari au hata ziwa.

ii. Uwezo na kifo. Kwa mujibu wa Ogude na Mushonga, (2023), Ahmandi (2024), Bertens (2024) na Pedersen na wenzake (2024) nchi zenye nguvu mara nyingi hutumia rasilimali asilia za nchi maskini kupitia njia aina aina kama vile viwanda vya uchimbaji, ukataji miti na uchafuzi wa viwanda. Mataifa haya hufanikisha haya kupitia mashirika ya kimataifa, mikutano ya biashara au shinikizo la kiuchumi. Aidha, mataifa yenye uwezo huweza kuwa na sheria za mazingira zisizokuwa kali, kuruhusu viwanda vyao kupujua kwa uhuru zaidi wanapofanya kazi katika mataifa fukara na dhaifu. Ufisadi huu mara nyingi hufanyika bila kuwajibika kwa mataifa yenye nguvu hivyo kusababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira pamoja na matatizo ya kiafya chungu nzima katika nchi fukara. Uwezo huu hupelekea sio tu unyonyaji wa rasilimali za mataifa fukara na dhaifu ila pia kifo cha viumbe na mazingira ya mataifa fukara, hususan kupitia uchafuzi wa hewa na utupaji taka sumu kwenye maji ukingo wa bahari katika mataifa fukara (Pentreath, 2021; Waithiru, 2022d).

Ukataji huu wa miti ovyo pamoja na uchafuzi wa hewa hupelekea maafa ya mimea, wanyama na watu mtawalia (Filipova, 2023; Garrard, 2023). Maafa haya huendelea kuongezeka katika mifumo ya utawala wa kidhalimu na maonevu kwa kusudi la ukuzaji wa utajiri na uwezo katika kapitalosenia (Moore, 2016; 2017; 2018).

iii. Lugha na mazingira – ambapo jazanda zinatumika kurejelea mazingira. Kulingana na Howarth (1996), mazingira huzua dhana ya lugha kimaeneo hasa kwa mtazamo wa kiuhakikimazingira. Kwa mfano, katika baadhi ya maeneo ya kijiografia kuna shani za kimazingira ambazo hupatikana katika maeneo hayo. Maeneo kama vile Marekani wanamaizi leksia kama vile barafu, dubu na miti fulani ambayo hupatikana katika maeneo baridi. Katika maeneo ya Uarabuni, joto, kiangazi na jangwa hutawala mazingira yao. Aghalabu maumbo ya lugha yao husheheni matumizi ya leksia hizi kama vile katika sitiari, mafumbo na tamathali nyingine za lugha. Kadhalika, jamii ambazo zinaishi karibu na maji ya maziwa, bahari na mito hutawala lugha iliyosheheni misemo inayotokana na leksia hizi za maji. Watunzi wanapotunga kazi zao katika maeneo haya ya kijiografia, hutawaliwa na shani hizi katika lugha zao na hivyo huweza kuathirika na mazingira kiutunzi na kiuandishi (Ong'utte, 2014; Ong na Whittle, 2024).

iv. Haki na maadili ya kimazingira. Licha ya kwamba binadamu tumetunukiwa uwezo wa kusimamia vyote vilivyomo ulimwenguni tusimamie, kama vile wanyama na mimea, mazingira yana haki. Hivi kwamba, umiliki wake ni kama unapigwa vita kwamba haujamruhusu aharibu mazingira kwa sababu tu yeye ndiye ana mamlaka kuhusu vyote vilivyomo ulimwenguni (Alia, 2017). Kwa mujibu wa Howarth (1996), mhimili huu unadai kwamba wanadamu ndio asili ya upujufu wa mazingira na kwamba tamaa yao ya kulimbika mali bila kujali mazingira itathminiwe kwa kusudi la kumfanya mwanadamu ajirudi. Howarth anadai kwamba matumizi ya kemikali na vitu vingine vya kuboresha mazao vifanyiwe utafiti zaidi na hata mwanadamu anapotupa vifaa na taka vilivyosheheni mabaki ya kemikali hizi, atafute jinsi bora na maeneo bora ya kutupa. Kwa mujibu wa Buell (1996), ili fasihi ihakikiwe kama ya kimazingira, lazima uasilia ujidhihirishe kwenye matini, matamanio ya kibinadamu yaoane na ya kimazingira, binadamu awajibike kwa mazingira na

kuwepo maendeleo yanayosababisha upujufu wa mazingira ambao mwandishi hujaribu kuangazia.

v. Maendeleo ya kudumu au maendeleo endelevu, uongozi mbaya na utandawazi. Yaani mazingira huchochea maendeleo endelevu kuwafaidi wanadamu. Hivyo, viumbe na hali zote vina haki ya kuishi kwa namna zao wenyewe, iwe ni wanyama, mimea, wanawake wanaotengwa, au hata makabila. Yaani huwezi hujumu kimoja na kisha ufikiri kwamba unajiendeleza. Kwa upande mwingine, utandawazi ni zao la maendeleo ya kiteknolojia yanayozalishwa na mataifa tajiri ya Ulaya katika mataifa mengi Barani Afrika. Uongozi mbaya na athari zake zinaathiri jinsi wanajamii wanavyohusiana na mazingira asilia. Inaaminika kuwa jamii za Kiafrika ziliheshimu mazingira kabla ya kuja kwa wakoloni. Kuja kwa wakoloni kulisababisha mazingira ya Waafrika kupotea kwa kukatwa misitu, ukulima, itikadi ya kibepari pamoja na haja ya kubadili vijiji kuwa miji na sehemu za viwanda. Mathalani, kuenea na kusambaa kwa tamaduni za kila aina kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuathiri suala la ujitambuzi ni mojayazo ya athari za utandawazi (Waithiru, 2019; Waithiru na wenzake, 2021). Mintarafu ya haya, msukumo wa utandawazi unatazamwa kama unayaathiri mataifa ya kifukara vibaya kwa kuwa yanalazimishwa kupambana na kushindana na mashirika makubwa ya kimataifa, kulazimishwa kuondoa vikwazo vya kiuchumi na kuishia kuathirika kutokana na mfoko wa bidhaa za kila aina kutoka nchi nyingine hasa za kibepari, kama vile, Ulaya, Marekani, Japani na mengine mengi.

vi. Utamaduni na mazingira. Utamaduni wa kila jamii huna budi kuhusishwa katika shughuli za jamii husika mintarafu ya misingi ya kimazingira (Nayar, 2010). Anashikilia msimamo kuwa, kauli hii ilitokana na wazo kwamba kila utamaduni una njia yake ya kipekee ya kuhusisha mazingira na jamii. Tamaduni mbalimbali zimekuwa aghalabu zikilinda mazingira. Philips (2003) anashikilia msimamo kuwa, utamaduni wa kila jamii huna budi kuangazwa katika misingi ya kimazingira, kwa sababu vyote viwili huchangiana na kukamilishana. Aidha, Claser (2002) akishabihiana na kauli hii, anashadidia kuwa uhusiano uliopo baina ya mazingira na utamaduni ni wa kisimbiotiki. Kwa misingi hii, kukazaliwa wazo kwamba kila utamaduni una njia yake maalum ya kuhusisha mazingira na jamii. Mathalani, jamii ya Waafrika katika

nyakati za kale waliheshimu misitu kama sehemu za matambiko na unyago. Mhimili huu utatumika kudhihirisha bayana jinsi watunzi wa riwaya teule wanavyotumia mazingira kuhamasisha hadhira yao kuhusu umuhimu wa uzuiaji wa najisi ya ikolojia pamoja na utunzaji wake mwafaka. Kuna mwingiliano mkubwa kati ya mazingira na binadamu. Nadharia ya Uhakikimazingira humulika mahusiano na mwingiliano kati ya binadamu na mazingira anamoishi (Quick, 2004; Njiru, 2015; Tan, 2019; Mwaniki, 2019). Mhimili huu uliongoza katika uchanganuzi wa data baada ya ukusanyaji wa data.

vii. Maumbile. Wanyama na ndege wote hupamba ulimwengu na kufanya mazingira yapendeze. Kwa hivyo kinachohitajika ni pawe na urari kati ya hali za kimaumbile. Iwe ni milima, miti iliyopo, wanyama waliopo pawe na urari katika mfumo wa ikolojia. Fasihi kwa jumla, watu kama Buell (1996), Quick (2004), Garrard (2007) na  Heise (2016) wanataka kuona kama kweli fasihi inawajibikia mazingira kama vile tunaona katika *Bustani ya Edeni*. Kweli watu wanashughulikia fasihi ama yawezekana kwamba katika kuyashughulikia ni kama inahimiza mazingira yaharibiwe zaidi? Hivyo, watu wasikitikie mazingira, tuwe na mawazo yanayojali na kuyapa mazingira kipaombele (*eco-concsiousness*) badala ya kutunza mazingira yamfaidi binadamu kwa mahitaji yake binafsi (*ego-consciousness*) bila kujali jamii wala kizazi cha kesho.

viii. Jinsia na historia za jamii za mabadiliko ya kimazingira. Kwa kurejelea mtazamo wa Kimagharibi, mojayazo ya mikabala na mitazamo kongwe ni maumbile dhidi ya mila na desturi (Nayar, 2010; Filipova, 2023; Garrard, 2023). Nayar anaongeza kuwa, pande zote mbili – maumbile na utamaduni – husheheni sifa na itikadi za kijinsia: utamaduni hudhihirisha sifa na itikadi za kiume ilhali mazingira hudhihirisha sifa na itikadi za kike hasa katika anthroposenia. Anafafanua kuwa, baadhi ya sifa zinazodhihirishwa na utamaduni wa kiume ni ubongo, uyakinifu, uwezo wa kuwaza vyema na kuweka hadharani kwa umma, ilhali zinazodhihirishwa na mazingira ni mwili au kiwiliwili, kutokuwa na lengo maalum, kutawaliwa na hisia pamoja na kuweka siri. Taswira kama mazingira mame huashiria mazingira kama mwanamke ambaye majukumu yake makuu huwa kuzaa na kutunza. Hili hupelekea mwanamke kuonekana kama uamilifu wake ni ‘asilia’ kwake.

Pamoja, mitazamo hii miwili huepuka wajibu wa utamaduni na jamii katika kulazimisha uamilifu na majukumu kwa mwanamke, jambo ambalo si mwafaka.

Howarth (1996) anafafanua nguzo ya historia za jamii mbalimbali hasa historia za mabadiliko ya kimazingira. Nguzo hii inadai kwamba jamii zetu za kale zilikuwa na mazingira nadhifu, yenye afya na ya kupendeza lakini kwa sababu za kiuchumi, siasa, sayansi na teknolojia wanajamii wa baadaye walianza kuyaharibu mazingira hayo mazuri. Nguzo hii humulika kronolojia ya matendo na shughuli ya binadamu tangu enzi za kale, hadi enzi ya uvindaishaji na jinsi walivyoanza kupujufu janibu za makazi na misitu asilia. Kadhalika, hutathmini athari hasi na chanya za matendo na shughuli hizi za binadamu kwa sayari, binadamu na spishi nyingine za kielimuviumbe.

Kulingana na Heise (2016), fasihi ina nafasi na uwezo wa kujenga utamaduni mwafaka na madhubuti dhidi ya uhifadhi wa mazingira wenye faida kwa mwanadamu na viumbe wengine wanatamalaki ulimwenguni. Tatizo la mabadiliko ya tabianchi litokanalo na uchafuzi na upujufu wa mazingira ni mazao ya hali halisi ya jamii na uelewa wake kuhusu uhifadhi wa bayotiki na ikolojia. Uhakikimazingira ulizalishwa na mabadiliko ya tabianchi yaliyozalishwa na uchafuzi na upujufu wa mazingira katika sehemu nyingi duniani. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa, uchanganuzi wa kimazingira ni mkondo wa uhakiki wa kazi za fasihi unaochunguza na kutathmini uhusiano uliopo baina ya fasihi na mazingira kimwavuli. Hivyo basi, uchanganuzi wa kazi za kifasihi kwa mtazamo wa kimazingira unayachukulia mazingira kama ajenda msingi katika uhakiki wake. Uhakiki wa matini za kifasihi kimazingira unamakinikia ulimwengu kama mada kuu na kuchanganua sifa kuhusu sayari na uhusiano wake na viumbe na maumbile yaliyomo kupitia kazi za kifasihi. Uchambuzi wa matini za kifasihi kwa mtazamo wa nadharia ya uhakikimazingira hupelekea matokeo kwamba, dhana kuu zinazohusu uhusiano baina ya mwanadamu na mazingira asilia ndizo zinazotawala katika matini za fasihi.

Nadharia hii hutilia mkazo dhana kuwa, utamaduni wa mwanadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana (Mhango na Bulaya, 2022). Hii ina maana kuwa uhakikimazingira unahakiki namna mwanadamu, utamaduni na mazingira vinavyohusiana na kuathiriana. Mathalani, maisha ya mwanadamu yanategemea

mimea kwa kuwa ndiyo inayozalisha gesi ya oksijeni ambayo ni muhimu sana katika mfumo wa upumuaji wa mwanadamu. Mimea nayo, kando na kuwa kivutio cha mvua ambayo ni hitaji la msingi kwa ajili ya shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji, humpa mwanadamu kivuli wakati wa jua, dawa na lishe bora. Kwa upande mwingine, mimea inategemea kwa kiwango kikubwa mbolea inayozalishwa na wanyama kama vile, wanadamu, mifugo na wanyama wa porini, ambao huzalisha kiwango kikubwa cha hewa ya ukaa ambayo ni malighafi muhimu kwa mimea katika mchakato wa usanisi wa chakula cha mimea. Ikizingatiwa kwamba utamaduni unahusu jinsi waja waendeshavyo maisha yao ya kila siku, uchanganuzi wa namna hii ni njia kabambe ya kudhihirisha mienendo ya matumizi na uhusiano kati yao na mazingira waishimo. Utamaduni, kando na kuwa njia inayowatofautisha watu kijamii ni njia ya kujitambulisha kutoka katika makundi yao ya kijamii.

Fauka na hayo, nadharia ya Uhakikimazingira inachanganua dhima ya mazingira katika kuukilia utamaduni wa jamii katika kipindi maalum cha kihistoria pamoja na itikadi, mila na desturi zinazonasibishwa au zisizonasibishwa na hali ya mazingira na sababu za kufanya uamuzi huo. Kwa kawaida, matatizo na changamoto za kimazingira zinazowasilishwa katika matini za fasihi zinachukuliwa kuwa ni athari zitokanazo na shughuli za kila uchao za mwanadamu. Kwa mujibu wa Mhango na Bulaya (2022), hali hii inatokea pale ambapo shughuli za kibinadamu zinapopujufu uwezo wa kawaida wa ulimwengu kuwezesha uendelevu wa mifumo ya kimazingira. Uhakiki wa kazi za fasihi kimazingira hunuia kutatua changamoto za upujufu na uchafuzi wa mazingira kama vile, ukame, nduli, maafa, mafuriko, ongezeko la gesijoto na kudidimia na kuadimika kwa baadhi ya bioanuwai na viumbelishe katika uso wa ulimwengu.

Kwa mujibu wa Nayar (2010), Mihimili ya nadharia hii ilitokana na maswali kama vile: Je, ni namna ipi mazingira yamewasilishwa na kusawiriwa katika matini maalum iliyosanwa kisanii? Je, ni jinsi gani mandhari yalivyochipuka katika riwaya fulani? Je, masuala ya mazingira na thamani yake katika tamthilia yanazingatia maadili ya kimazingira? Je, utukuzi na uumbaji wa sitiari katika sanaa unalandana na namna tunavyoyahifadhi au kuyavuruga mazingira? Je, ni kwa njia gani maswala ya mazingira yanavyojipenyeza katika fasihi ya kisasa? Kwa mujibu wa Huggan na Tiffin (2010) wanasema kuwa, maswali hayo yalichipuza mitazamo tofauti tofauti ya

Nadharia ya Uhakikimazingira hasa katika kipindi cha utandawazi. Heise (2016) anawaunga mkono katika kuitaja mitazamo hii ambayo ni; uhakiki mazingira Kinisai, uhakiki mazingira ya Pahali na hatimaye uhakiki mazingira ya Kiafrika. Uhakiki mazingira Kiafrika ni mtazamo uliokuwa umepaliliwa na kuendelezwa hapo kabla na mawazo ya wasomi kama, Estok (2005) na Heise (2008) waliokariri kuwa, kulingana nao haiwezekani kuchanganua matini za fasihi za kimazingira kwa kujikita katika mkabala mmoja. Kulingana nao, kila jamii ina njia zake za kipekee za kusawiri na kuhusiana na mazingira na kwamba upekee huu unahitaji kila jamii kujichunguza kwa kujikita katika upekee wake.

Mathalani, zipo jamii ambazo hutumia misitu kama maeneo ya kafara na unyago wao kama vile tohara, ibada, elimu na uganga ilhali jamii hasa za kimagharibi hufanyia ibada na matibabu katika majengo ya kifahari (Ong'utte, 2014). Hata hivyo, mtazamo wao kuhusu umuhimu wa misitu huenda ukatofautiana kwa sababu ya misingi ya tamaduni zao. Mtazamo huu kwa hivyo unaazimia kuangalia upekee wa jamii ya Kiafrika kuhusiana na mazingira na jinsi walivyokuwa wakiyahifadhi na au kuyapujufu. Hatimaye, kwa kuzingatia nadharia hii utafiti ulilenga; kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya za *Bustani ya Edeni* (2002), *Vipuli vya Fugo* (1996), *Mafuta* (1994) na *Walenisi* (1995), kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya hizi teule na kutathmini rai za waandishi wa riwaya hizo teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya teule taje. Kimsingi, mahusiano kati ya waandishi, kazi na mazingira katika fasihi ya Kiswahili ndiyo shughuli muhimu ambayo huchunguzwa na nadharia hii (Heise, 2016). Nadharia hii inajitoa mhanga kujadili hali halisi ya upujufu wa mazingira kwa kuchanganua matini za fasihi katika nyanja za; uamilifu wa maudhui, usanii, jamii, historia, itikadi, utandawazi, jinsia na mbinu katika mazingira asilia au vipengele vyake kama vilivyohusishwa katika kazi fulani ya fasihi au makala ya kimazingira. Pia, huangaza tanzu za fasihi andishi na simulizi, filamu, sinema pamoja na teknolojia-burudishi. Hata hivyo, mtafiti aliangaza utanzu wa riwaya ya Kiswahili katika riwaya nne teule mintarafu ya madhumuni ya utafiti.

Ingawa nadharia ya Uhakikimazingira ni muhimu katika kuchunguza uhusiano kati ya fasihi na mazingira, imekumbwa na changamoto kadhaa. Wataalamu wa awali wa Uhakikimazingira walikosolewa kwa mtazamo wao wa kiwanadamu, ambapo

mazingira yalizingatiwa kwa kuangalia tu jinsi yanavyomhusu binadamu, jambo lililopunguza utambuzi wa uwezo wa maumbile na viumbe visivyo binadamu. Hili limekabiliwa kupitia ujumuishaji wa mitazamo ya baada ya uanadamu na nyenzo mpya zinazosisitiza utegemeano kati ya binadamu na visivyo binadamu. Pia, nadharia hii ilikosolewa kwa kupendelea fasihi ya Kimagharibi na kupuuza mitazamo ya mazingira kutoka Kusini mwa Dunia na jamii za asili. Hili limesahihishwa kupitia kuzuka kwa mtazamo wa Uhakikimazingira wa baada ya ukoloni, unaojikita katika dhuluma za kimazingira na athari za ikolojia za ukoloni. Aidha, awali, nadharia hii ilielemea kuenzi mandhari ya porini na kupuuza mazingira ya mijini na kiteknolojia. Ili kurekebisha hilo, nadharia ya Uhakikimazingira ya mijini na tafiti za vyombo vya habari vya kimazingira zimeibuka kuchunguza miji, teknolojia za kidijitali, na mazingira ya kisasa. Vilevile, ukosefu wa ushirikiano wa taaluma mbalimbali katika Uhakikimazingira umetatuliwa kupitia ushirikiano na sayansi kama vile ikolojia, jiografia, na tafiti za hali ya hewa, hivyo kuongeza kina cha uchambuzi. Hatimaye, ingawa awali haikujihusisha kwa kina na mabadiliko ya tabianchi, sasa imejumuisha ukosoaji wa tabianchi na tafiti za fasihi ya mabadiliko ya hali ya hewa, ikijumuisha dhana kama vile "hyperobjects" ya Timothy Morton na kazi za Dipesh Chakrabarty kuhusu uhusiano kati ya tabianchi na ubinadamu. Kupitia mageuzi haya, nadharia hii inaendelea kuboresha umuhimu na wigo wake katika kukabiliana na changamoto za mazingira za sasa.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alishughulikia mbinu za utafiti. Hivyo, aliangazia hatua muhimu zilizofuatwa katika shughuli nzima ya utafiti ili kuafikia madhumuni ya utafiti. Utafiti huu ulikuwa wa kifasihi uliozingatia wa fasihi andishi; utanzu wa riwaya. Kimsingi, utafiti huu ulitumia utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika riwaya nne teule katika ukusanyaji wa data. Mintarafu ya haya, mtafiti alitekeleza utafiti wake kwa kupekuapekua riwaya nne teule pamoja na tahakiki zilizoshughulikia masuala yaliyohusu anthroposenia, msingi wa nadharia na mbinu za utafiti zilizohusiana na utafiti huu ili kukusanya data. Riwaya zilizotafitiwa ni pamoja na *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi.* Katika uchanganuzi wa data, mbinu ya kithamana ilitumika kwa kutoa maelezo ya kimakisio kwa mujibu wa elimu na maarifa. Utafiti huu hivyo ulichukua aina ya muundo wa kimaelezo. Isitoshe, sehemu hii ilipambanua eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, kikundi lengwa, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data hiyo na hatimaye masuala ya maadili yalizingatiwa.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Kwa mujibu wa Yin (2014), muundo wa kimaelezo hujihusisha na kuchanganua suala la utafiti pasipo na kubadilisha vibadala. Utafiti huu uliambatana na muundo wa kimaelezo. Yin anafafanua kuwa, muundo huu hutegemea maelezo na fasili za uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishi wake. Aidha, hujifunga kwenye shughuli ya uchanganuzi na ufasili wa data katika kusuluhisha suala maalum la utafiti. Hata hivyo, huongozwa na kutawaliwa na madhumuni ya utafiti husika. Hivyo, katika kujadili anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili, mtafiti alitumia muundo wa kimaelezo kutimiza madhumuni ya utafiti huu. Muundo wa kimaelezo hulenga kupata taarifa mpya kuhusu suala la utafiti husika. Kimsingi, huangaza mambo asilia na yasiyobadilika lakini huweza kuibua data mpya kwa kuyaangaza katika mtazamo tofauti (Cresswell, 2014).

## 3.3 Njia za Utafiti

Njia kuu ya utafiti huu ilikuwa kutumia mbinu ya upekuzi-changanuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji data. Uchanganuzi wa data ulihusisha mbinu ya kithamana. Kwanza riwaya zilizoteuliwa zilisomwa na mtafiti. Kisha mtafiti alidondoa kama data ilidhihirisha; aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili, kisha alihakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya

teule na halafu alitathmini rai za waandishi wa riwaya teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia. Aidha, mtafiti alipitia na kusoma kwa makini kazi za fasihi zinazohusu uchambuzi wa fasihi hususani sehemu zilizodhihirisha anthroposenia katika matini za kifasihi.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Mtafiti alinuia kufanyia utafiti huu maktabani na kuhusisha riwaya nne za Kiswahili: *Bustani ya Edeni, Vipuli Vya Figo, Mafuta* na *Walenisi***.** Data ya utafiti huu ilichimbuka kutoka kwenye riwaya hizo nne na tahakiki za kifasihi kuhusu suala la anthroposenia zilizohifadhiwa mtandaoni na kwenye tovuti mbalimbali. Mtafiti alichanganua riwaya nne teule pamoja na maandishi mengine mengi kwa lengo la kutambua na kuziba mwanya wa kiakademia mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu. Mtafiti alinuia kupata data iliyojibu maswali ya utafiti na suala la utafiti katika tahakiki, kazi na makala yaliyohifadhiwa maktabani. Mtafiti alifanya mapitio na upekuzi wa maandishi tofautitofauti maktabani na kwenye tovuti mbalimbali za vyuo na taasisi aina aina ili kutambua maoni na mchango wa wasomi wengine kuhusiana na suala la anthroposenia. Upekuzi na mapitio hayo ya maandishi yalimsaidia mtafiti kujua mchango wa kila kazi katika kufanikisha utafiti huu wa mtafiti, tofauti za kazi zao na hii na vile vile mapendekezo yao kuhusiana na mada ya utafiti. Majarida, makala, vitabu vya kinadharia na matini zinazoangazia anthroposenia zilisomwa. Kadhalika, tafiti za awali maktabani zilisomwa ili kupanua weledi wa nadharia, mbinu za kukusanya data, uwasilishaji na uchanganuzi wa matokeo ya utafiti. Baadhi ya maktaba aliyoyazuru ili kufanikisha utafiti ni pamoja na maktaba ya umma kadhaa nchini na pia maktaba ya vyuo vikuu mbalimbali vya umma na vya kibinafsi.

### 3.5 Kikundi Lengwa

Kikundi lengwa kilikuwa riwaya za Kiswahili za Katama Mkangi na Emmanuel Mbogo. Mintarafu ya madhumuni ya utafiti, mtafiti alikusudia kutafiti anthroposenia katika riwaya za waandishi hawa wawili za Kiswahili. Riwaya teule zilizofanyiwa utafiti ziliteuliwa kwa kudhamiria. Sababu kuu ya kuchagua waandishi hawa wawili ni kutokana na kuwa wamejikita kwa kina katika mjadala endelevu kuhusu anthroposenia. Isitoshe, umaarufu na mchango wao katika fasihi ya mazingira huwatambulisha. Hivyo kuwapa msingi bora wa kuchunguza kazi zao kitaaluma kutokana na sauti zenye mamlaka katika uwanja huu.

### 3.6 Uteuzi wa Sampuli

Mtafiti alitumia sampuli matilaba katika uteuzi wa sampuli. Riwaya hizi ziliteuliwa kutokana na udurusu wa awali. Kwa mujibu wa Mvumbi na Ngumbi (2015), sampuli matilaba huweza kuwa muhimu sana katika hali ambapo suala la msingi kwa mtafiti ni kufikia sampuli lengwa kwa wepesi ila si ugavi wa sampuli wakilishi. Lengo kuu la kuteua sampuli ni kumwezesha mtafiti kukusanya data anayohitaji kutoka kwa watafitiwa wachache ambao wanawakilisha jamii pana na kusaidia kupatikana kwa data mwafaka na madhubuti ya kufanikisha madhumuni ya utafiti (Palys, 2008; Kumar, 2014). Utafiti huu ulilenga riwaya za *Bustani ya Edeni, Vipuli Vya Figo, Mafuta* na *Walenisi* kama sampuli wakilishi ya jamii pana ya riwaya za Kiswahili za watunzi Mbogo na Mkangi. Mtafiti aliteua riwaya hizi nne kutokana na mseto wao wenye mwelekeo, maudhui yanayohusu anthroposenia, upana ulioweza kudhibitika pamoja na uwakilishi wa muda na muktadha. Sababu kuu ya kuteua riwaya mbili za mtunzi Mkangi na mbili za mwandishi Mbogo ni kuweza kuyajibu maswali ya utafiti na kuziba mwanya wa kiakademia mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu kikamilifu. Kazi hizi za kifasihi ziliandikwa katika vipindi tofauti, kama vile, kile cha themanini, cha tisini na cha elfu mbili hivyo kuwa mwafaka kwa utafiti huu kwa kuzingatia muktadha wa kihistoria na kitamaduni.

### 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu tofautitofauti ili kufanikisha utafiti wake. Kwanza, alizisoma kazi teule kwa kina kwa misingi ya Uhakikimazingira ili aweze kupata mwanga na mihimili ya kufikia upeo mpevu wa kiuchanganuzi na wenye ithibati za kisanaa na kinadharia. Kwa kuzingatia kwamba uchanganuzi wa mtafiti utakuwa wa kimaelezo na wala si wa kitakwimu, mtafiti alijikita katika udurusu wa vitabu, tahakiki na makala maalum kwa lengo la kupanua mawanda ya uelewa. Data ilikusanywa kutokana na matini zilizopo kwa kuangazia uchunguzi wa aina za anthroposenia zilizosawiriwa katika riwaya teule, uhakiki wa mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya hizi teule na utathmini wa rai za waandishi wa riwaya nne teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia. Pili ni kwamba, mtafiti alirejelea makala tofautitofauti pamoja na tasnifu za kiakademia zinazohusu mada hii. Kwa kufanya hivyo, mtafiti aliweza kubainisha pengo ambalo utafiti huu ulinuia kuziba la kiusomi. Hivyo basi, mtafiti alitalii na kurejelea maoni ya wasomi wengine

waliochangia mawazo na maoni kuhusu anthroposenia katika utanzu wa riwaya katika misingi ya Uhakikimazingira, mintarafu madhumuni ya utafiti huu.

### 3.8 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishi

Data iliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa njia ya maelezo. Vifungu vilivyodhihirisha anthroposenia vilidondolewa kutoka riwaya zote nne, kupangwa na kuchanganuliwa. Aidha, mtafiti alijikita katika uchanganuzi wa kithamana, ambapo alipanga data katika dhana, alionyesha uhusiano kati ya kategoria za data kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Hivyo basi, data ilichanganuliwa mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu pamoja na nguzo muhimu za nadharia ya Uhakikimazingira. Uchanganuzi wa yaliyomo ni mbinu ambayo hutumiwa ili kusaidia kufanya mahitimisho kutokana na ufasili na usimbuaji wa misimbo ya matini fulani. Aidha, ni uchanganuzi wa makala na sanaa za mawasiliano, ambazo huweza kuwa katika miundo na mitindo tofauti, picha, michoro, vibonzo, sauti na video. Sifa hii huifanya njia ya maelezo mbinu mwafaka zaidi katika uchanganuzi wa kazi za fasihi (Franklin, 2012; Gee na Handford, 2012). Bernard (2002), Creswell (2014) na Kumar (2014) wakiwaunga mkono wanakariri kuwa, ni mbinu rahisi, nyepesi na madhubuti ya uchanganuzi wa yaliyomo, hasa katika kazi za kifasihi za kithamana na pia za wingi idadi. Ili kurahisisha uchanganuzi na ufasiri wa data, utafiti huu ulinuiwa kugawika katika sura mbalimbali na kila sura iliangazia masuala ya kipekee yanayohusiana na anthroposenia, ambayo yaliibuka kutoka kwa data iliyokusanywa.

Kwanza, mtafiti alichunguza aina za anthroposenia zilizosawiriwa katika riwaya nne teule mintarafu ya madhumuni ya utafiti. Aina kama vile binadamau, maumbile, wafisadi na nyingine nyingi zilinuiwa kuangaziwa katika utafiti huu. Pili, mtafiti alihakiki mbinu kama vile, taashira, tashtiti, majazi, taswira na nyingine nyingi zilizosawiri anthroposenia katika riwaya nne teule. Hatimaye, mtafiti alitathmini rai za waandishi wa riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli Vya Figo*, *Mafuta* na *Walenisi* kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia. Aidha, mtafiti aliangazia masuala yanayohusiana na anthroposenia, kama vile, uharibifu wa hewa, mmomonyoko wa udongo, ujenzi karibu na kingo za mito, umwagaji wa kemikali kwenye bahari na mito, ukataji miti ovyo bila kupanda mingine, ubidhaaishaji wa kibepari, utandawazi, ulaji wa mimea mbalimbali pamoja na wanyama wengine, ongezeko la joto na watu ulimwenguni, na matokeo ya anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili.

Hatimaye, data iliyokusanywa na kuchanganuliwa mintarafu ya madhumuni ya utafiti, iliwasilishwa kwa njia ya maandishi.

### 3.9 Masuala ya Kimaadili

Kwa mujibu wa Kumar (2014), maadili ni dhana inayotumika katika mazingira fulani ambapo jamii imejiwekea itikadi, kaida na desturi maalumu kwa lengo la kuhifadhi, kulinda na kutwaza heshima ya amali zake na kuzuia unajisi na uchafuzi wake. Hivyo, maadili huweza kuchukuliwa kama adhari au tahadhari kuhusu suala fulani linalolindwa kutokana na kuchafuliwa na wanajamii (Roberts, 2015). Katika kuzingatia masuala ya maadili katika utafiti huu, mtafiti alizingatia maadili kabla ya kukusanya data, wakati alipokuwa akikusanya data na baada ya kukusanya data, hasa katika uchanganuzi. Hili liliafikiwa pale ambapo alihakikisha kuwa maelezo na fafanuzi kutoka kwa wasomi wa hapo kabla zilizonukuliwa, zilirejelewa sahihi katika sehemu ya marejeleo. Kunakili kazi ya msomi mwingine bila kumtambulisha kama mwenyewe ni kosa linalofaa kuepukwa kwa kila namna (Kumar, 2014). Ikizingatiwa kwamba data ya kimsingi ilitoka kwenye riwaya nne teule za Kiswahili, mtafiti alipata barua ya utangulizi kutoka Chuo Kikuu Cha Laikipia ili kumwezesha kuomba kibali kutoka Institutional Ethics Review Committee (IERC) pamoja na kibali cha utafiti kutoka National Commission on Science, Technology and Innovation (NACOSTI); ili kutimiza mahitaji ya kimaadili kwa mujibu wa sheria katika kutekeleza shughuli za ukusanyaji wa data katika mitandao na tovuti mbalimbali; vibali ambavyo alivipata.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA AINA ZA ANTHROPOSENIA

## 4.1 Utangulizi

Uchanganuzi wa data ulifanywa mintarafu ya madhumuni ya utafiti na kuongozwa na nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira. Kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza ambayo yalikuwa kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya za *Bustani ya Edeni (2002), Vipuli Vya Figo (1996), Mafuta (1984) na Walenisi (1995)*, mtafiti alichunguza aina za anthroposenia zilizosawiriwa karika riwaya hizi nne teule za Kiswahili. Mintarafu ya Nadharia ya Uhakikimazingira, nguzo kuu kama vile; binadamu dhidi ya mazingira, maendeleo endelevu, uongozi mbaya, utandawazi, uwezo na kifo ziliongoza katika uchunguzi wa aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule. Mathalani, baadhi ya aina za anthroposenia zilizochunguzwa ni pamoja na; binadamu, mawakala wa anthroposenia, vifaa vinavyotumiwa na binadamu, vurugu dhidi ya mazingira kutokana na binadamu, jiografia ya binadamu, mabeberu wa kisasa, mabepari, wafisadi, pamoja na utelekezaji wa binadamu kupitia moto, fedha na sheria. Hivyo basi, data ilikusanywa na kuchanganuliwa kutoka kwenye riwaya nne teule za Emmanuel Mbogo na Katama Mkangi.

## 4.2 Binadamu

Binadamu kama aina ya anthroposenia alichanganuliwa mintarafu ya madhumuni ya kwanza ambayo ni kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule. Kimsingi, binadamu ni mwanamume, mwanamke, au mtoto wa spishi ya *Homo Sapiens*, ambaye hutofautishwa dhidi ya wanyama wengine na uwezo wake mahiri wa kuendelea kimawazo ambao humwezesha kufanya uamuzi wa kirazini, uwezo wa mawasiliano kwa lugha na ishara mbalimbali, pamoja na uwezo wake wa kusimama wima (TUKI, 2006; Ndalu na wenzake, 2014; Wamitila, 2022). Kadhalika, binadamu ni mtu, mwanadamu, au mahuluku (Mdee na wenzake, 2015). Kama aina ya anthroposenia, binadamu amejitia kitanzi kutokana na shughuli zake za kila siku zinazotisha mazingira na uhai wake mwenyewe. Wakishadidia kauli hii, Nayar (2010), Clark (2015), na Coughlin na Gephart (2020) wanasisitiza kuwa binadamu ndiye chanzo kikuu cha anthroposenia kupitia maingiliano na mahusiano yake na mazingira kwa jumla. Binadamu amefanikiwa kuafikia hili kwa kujiponza kiafya, kiuchumi na kijamii. Davis na Heather (2015), pamoja na Moore (2016),

wakikubaliana na hili wanataja kuwa, ingawa kapitalosenia humuondolea binadamu lawama ya kuyaangamiza mazingira asilia ya viumbe hai na visivyo hai katika anthroposenia, hatimaye wote wanakubaliana kuwa hata kama ni binadamu mwenye uwezo anayeyaharibu mazingira huku mnyonge akiathirika pakubwa, bado ni binadamu. Kutokana na maoni, mchango na kauli za wataalamu hawa ni dhahiri kuwa, binadamu kama aina ya anthroposenia hupalilia anthroposenia kupitia shughuli zake za kila siku katika harakati zake za kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa jumla.

### 4.2.1 Binadamu Kupitia Shughuli za Kiuchumi na Utabaka

Kimsingi, shughuli ni dhana inayorejelea jambo ambalo linamfanya mja atumie nguvu, juhudi au jitihada na akili yake ili kuitekeleza; kazi au dimba (TUKI 2006; TUKI, 2013; BAKITA, 2015, 2022; Wamitila, 2022). Katika utafiti huu, istilahi hii ilirejelea jambo, tukio au hali ambayo hutendwa na binadamu, aidha katika kujitafutia riziki, burudani, amani, maendeleo, mahusiano mema, ukulima au hata kupunga upepo katika ufuo wa bahari au kando ya mto huku; kwa kutumia nguvu zake za ubongo na mwili, jitihada au bidii na pia teknolojia na sayansi. Uchumi ni nomino ambayo hurejelea mali iliyopatikana kutokana na amali za nchi au watu. Pia hurejelea mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi au taaluma ya mapato na matumizi ya watu (TUKI, 2014; Ndalu na wenzake, 2014; Mdee na wenzake, 2015; BAKITA, 2022; Wamitila, 2022). Utabaka nao hutokana na hali ambapo kundi la watu wenye hali moja linalotokana na jamii yenye mfumo wa kiuchumi (Kesting na wenzake, 2022; Fuchs, 2023) huwatenga wanajamii mintarafu ya uwezo wao wa kumiliki na kutawala namna za kuzalisha mali kimwavuli (Huggan na Tiffin, 2010; Secretan, 2019; Kesting na wenzake, 2022). Katika utafiti huu, ilibainika na mtafiti kuwa, binadamu hufanikisha jukumu lake kama aina ya anthroposenia kupitia shughuli zake za kila siku za kiuchumi pamoja na hulka yake ya kupalilia utabaka katika jamii. Hili lilidhihirika baada ya uchunguzi wa aina za anthroposenia zinazosawiriwa na watunzi Mbogo na Mkangi katika riwaya zao nne teule. Uchunguzi huu uliongozwa na mihimili ya uwezo, binadamu dhidi ya mazingira, haki na maadili ya kimazingira, na maendeleo endelevu.

#### i. Uchafuzi wa Mazingira

Katika harakati za kujiendeleza kiuchumi, binadamu anazalisha uchafuzi wa mazingira unaomwathiri kwa njia hasi. Mathalani, kupitia mhusika Doricas katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* inadhihirika kuwa uchafuzi wa mazingira husababisha njaa. Doricas akiwa na wasiwasi anampa mwanawe Samsoni ziwa ambalo limechokachoka kwa kukosa maziwa ya kutosha. Ingawa Samsoni analinyonya, njaa inaendelea kumsakama, madhali ziwa la mamake lina maziwa kidogo mno. Binadamu katika harakati zake za kujiendeleza kiuchumi, anajenga viwanda ambavyo vinachangia uchafuzi wa mazingira pakubwa. Kwa mfano, kiwanda cha kemikali cha *Saga Saga Chemical Industry* kinachangia upujufu wa hewa kwa kiwango kikubwa pale eneo la Siza. Uchafuzi huu wa hewa unachangia maradhi baina ya wenyeji ambao wanapungukiwa na nguvu za kupalilia mimea pamoja na kujitafutia riziki kwa njia mbadala.

Hili linadhihirishwa na Doricas anapopiga chafya mfululizo kutokana na maradhi yanayosababishwa na hewa chafu. Analalamika kuhusu mwasho unaotawala pua zake kila anapopiga chafya, hadi inambidi atumbukize kidole ndani ya tundu za pua; moja baada ya nyingine kuzichokonoakonoa, mradi apunguze mwasho na mnyegeo unaomnyima amani na utulivu. Hali hii inashabihiana na kauli ya Sidang' (2023) kuwa, binadamu ameleta uharibifu mwingi duniani. Anasisitiza kuwa binadamu hukata miti ovyo na kuichafua mito hivyo ni dhalimu.

Shughuli za binadamu za kujiendeleza kiuchumi zimechangia uchafuzi wa mazingira. Hii ni kwa sababu, athari zake hasi na matokeo yake hatari kwa viumbe hai zinaendelea kuenea ulimwenguni. Davis na Heather (2015) pamoja na Canty (2025) wanasema kuwa, shughuli na juhudi za binadamu za kujiendeleza kiuchumi, kama vile uundaji wa plastiki, zinaendelea kuzorotesha afya ya binadamu, kufupisha maisha yake kwa vianio kadhaa na kualika kifo kwa haraka. Mtunzi Mbogo akishadidia ukweli huu katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* anamtumia mhusika Eliya kudhihirisha athari hasi za uchafuzi wa mazingira kama zao la juhudi na jitihada za binadamu, hususan za matajiri na viongozi. Mathalani, Eliya, mumewe Doricas alikuwa amekumbwa na kikohozi kisichokwisha pamoja na ugonjwa wa ngozi kuwasha. Maradhi haya yalikuwa yameenea Siza kutokana na kemikali zilizozalishwa na kiwanda cha *Saga Saga Chemical Industry*. Walioathirika zaidi, kando na wenyeji wa Siza ni wafanyakazi katika kiwanda kile. Hili linafungamana na nguzo ya uwezo

ambapo wenye mamlaka na vyeo huyanajisi na kuyachafua mazingira ya waduni. Hili linashabihiana na kauli ya Filipova (2023) kuwa, wanyonge na maskini huathiriwa zaidi na athari hasi za uchafuzi wa mazingira kuliko wenye vyao na nafasi ambao hutumia teknolojia kupunguza na wakati mwingine kukabiliana kikamilifu na athari hasi za mazingira chafu.

**ii. Athari za Mtu kwa Mwenzake**

Binadamu kama aina ya anthroposenia amejiathiri mwenyewe kwa njia hasi sana. Mathalani, Bwana Abdula katika harakati zake za kujiendeleza kiuchumi anawaathiri wenyeji wa Siza kupitia shughuli za kila siku za kiwanda chake. Ingawa mna athari chanya kama vile utoaji nafasi za ajira kwa wenyeji athari hasi zinavimbishwa na ubinafsi-uchoyo wa Bwana Abdula na Wakurugenzi wa *The Trans-American Company* wanaowaona Waafrika kama vifaa vya matumizi na majaribio. Samsoni anamweleza Doricas katika *Bustani* kuwa, kiwanda kile kiliwaathiri wakazi wote wa eneo la Siza. Samsoni anakiri kuwa aidha kila mtu anakohoa au anajikuna ngozi. Ilifikia kiwango kwamba, wenyeji walitania na kuurejelea kama ugonjwa wa kupiga gita ama Franco. Doricas anaongeza kuwa, hata nywele zinanyonyoka na vichwa kushamiri vidonda kama kile cha Baba Mohamed. Doricas anadhihirisha kuwa binadamu anajiponza mwenyewe pamoja na kizazi chake katika anthroposenia. Mathalani, katika *Bustani* Doricas anamlaani mende kuwa: "“Shenzi!” Kwa kasi, alimpiga kofi mende mwingine tena aliyekuwa anacheza na kuking’ong’osa kidonda cha mwanawe kichwani” (uk. 10). Inadhihirika kuwa binadamu mwenye uwezo ndiye anayeyatawala na kuyadhibiti mazingira ya yule duni tena kwa njia hasi. Hali hii inashabihiana na nguzo ya uwezo na kifo, ambapo mwenye nguvu humwangamiza mnyonge bila kujali matokeo yake.

Linalobainika mahakamani katika *Mafuta* ni kuwa binadamu wakati mwingine hana umilisi wa kile akitakacho kando na kuuangamiza ulimwengu na vilivyomo hai na visivyo hai. Hili linawekwa bayana na Dubwasha ambalo linaonekana kuwa halifahamu litakalo, madhali jibu halitoki na pia swali halitoki. Hata hivyo, kutofahamu huku kunadhihirika tu pale linapokabiliana na ukweli. Hivyo, ukweli unaibuka kuwa adui ya wanaoangamiza wenzao na mazingira yao kwa jumla kulingana na mtunzi Mkangi. Mwandishi Mkangi katika *Mafuta* anasisitiza kuwa lile analolifahamu binadamu ni: “... kukera ndilo alilojua tu.” (uk. 44). Binadamu anadhihirisha athari kwa mwenzake kupitia ulinganisho wake yeye na paka

anayemwona panya kama mlo tayari. Hivyo, mtunzi Mkangi anamsawiri binadamu mwenye uwezo kama paka anayemkabili panya tayari kumbadili kitoweo. Kwa misingi hii, panya ni wananchi wachochole ambao huwatumikia watu wenye uwezo, mamlaka na nafsi, kama watumwa kupitia kulipa kodi ya juu zaidi bila huruma, kunyimwa haki za binadamu na kufanyishwa ajira za sulubu chache zisizopatikana kwa wepesi na mishahara duni pamoja na dhiki na dhuluma chungu nzima wakumbanazo nazo. Hili linafungamana na nguzo ya uwezo. Hii ndiyo sababu uso wa Dubwana unachanuka kwa furaha baada ya kuwashika Ti na Mtue wakicheka mahakamani kwa kupata nafasi ya kuwadhalilisha na hatimaye kuwaangamiza.

Familia inayoelezewa na Mbeyu inaendeleza athari za mtu kwa mwenzake kupitia ajira ya baba na ya mama pamoja na nafsi zao. Baba watoto anafanya kazi ya kuwatesa wafungwa kwa kuwadunga pini vidoleni, kuwachoma na moto wa sigara na pia anawachoma na moto wa spaki kwenye viungo vyao vya uzazi. Hili linaashiria maangamizi kwa kizazi kizima. Filipova (2023) na Garrard (2023)wanasisitiza kuwa mazao ya nguzo ya uwezo na kifo ni maangamizi ya viumbe hai na visivyo hai mtawalia. Hili hutokana na haja ya walalahai kuyadhibiti na kuyatawala maisha ya walalahoi katika mataifa mengi ulimwenguni, hususani katika bara la Afrika. Hii ni kwa sababu, baada ya mkoloni kuondoka mamlakani, aliwapa visesere vyake nafasi za uongozi ili aweze kuwatumia kuwatawala wananchi pamoja na mazingira yao.

Emmanuel Mbogo katika riwaya ya *Vipuli Vya Figo* anamsawiri Profesa Williams akiathiri wenzake kama vile Dkt Matoga na Dkt Charles. Profesa Williams ni daktari maarufu sana Ughaibuni. Anaimarisha athari zake kwa wenzake kupitia shughuli zake za kila siku. Kama fundi mwingine yeyote ambaye hukarabati vifaa, mahali au vitu mbalimbali, Profesa Williams anatafuta vipuli vya figo na mioyo duniani kote kwa minajili ya kuvipachika wagonjwa wake ambao wanamlipa pesa taslimu. Wengi wa wagonjwa wake walikuwa wameathirika na athari hasi za matumizi ya kemikali sumu katika ukulima na kuugua maradhi tofautitofauti. Maradhi haya yasiyokuwa na tiba yanaathiri figo au mioyo ya wateja wa Profesa Williams. Chanzo kikuu cha maradhi haya ni athari hasi za ulaji wa vyakula vinavyokuzwa kwa kutumia kemikali sumu. Hivyo, Profesa Williams anaathiri wenzake kwa kuvitumia viungo vya mwili vya wanyonge kama vifaa vya kumfaidi kifedha na matajiri kwa mkupuo mmoja. Hali hii inashabihiana na mhimili wa uwezo na kifo ambapo waduni hunyanyaswa na matajiri kisha huangamizwa.

Kadhalika, Nyau, Kipanga na Shipe wanadhihirisha athari kwa binadamu wenzao. Kando na wao kushirikiana na Dkt Matoga katika mradi wa uwindaji, upasuaji na usafirishaji wa vipuli vya figo na mioyo wanawaua viwete, maskini na wanawake wanaoshiriki ukahaba usiku. Uaminifu wao wote na utu wao kwa jumla unanunuliwa na pesa. Mkuu wa Magereza anadhihirisha hili katika *Vipuli* anapotaja kuwa, “Tunategemea pesa kununua uaminifu wao.” (uk. 103). Vilevile anashirikiana na Dkt Matoga kuiba kwa kuzoa viungo vya figo na mioyo kutoka kwa wafungwa wanaonyongwa. Hakika hili linafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile ambapo baada ya binadamu kushindwa kuyalinda na kuyatunza mazingira, anaangamia kutokana na athari zake mwenyewe katika harakati za kutaka kujitajirisha. Bergthaller na Horn (2020) wanataja kuwa, athari za binadamu kwa mazingira husababishwa na athari za binadamu kwa mwenzake katika harakati za kujiendeleza kiuchumi. Kigezo kikuu cha uharibifu huwa woga. Hili linathibitishwa na Dkt Matoga anayefafanuliwa na mwandishi Mbogo katika *Vipuli* kuwa, “... alishusha sauti na kusema kwa woga ... “Wale wanaonyongwa.” (uk. 104). Woga unatumiwa na binadamu kumwaathiri na kumdhibiti mwenzake.

Rais Gorbachev anaashiria athari za binadamu kwa mwenzake kupitia msimamo na mfumo wake wa kisiasa na kiuchumi wa kibepari na soko huru. Hili linawekwa bayana na Dkt Matoga anayeweka furaha ya ndani kwa ndani baada ya kusoma maelezo kwenye gazeti la *Daily Echo* yanayosema kuwa, Rais Gorbachev amerejeshwa madarakani baada ya waasi – viongozi wa Kirusi – wakomunisti kushindwa kumuondoa mamlakani, yeye na ubepari wake. Kulingana na mwandishi Mbogo, Waasi hawa ni tisho kwa mabepari kama Rais Gorbachev kupitia msimamo wao wa siasa ya ujamaa na itikadi za Kimaksi na Kilenini. Rais Gorbachev anapalilia ubepari kupitia mfumo wa uchumi wa kikapitalisti unaojikita kwenye mhimili wa uongozi mbaya wa nadharia ya Uhakikimazingira. Dkt Matoga anatetea ubepari kwa kusisitiza kuwa, ni mfumo mzuri kwa sababu hata malaika wote hawako sawa; majini pia yana daraja zao tofauti; binadamu nao wana matabaka na ubaguzi wa aina aina ambao hupalilia uongozi mbaya.

Mtunzi Mbogo anawalinganisha nyuki na ubepari kwa kusisitiza kuwa, mzingani, kuna wale nyuki ambao ni walinzi, kuna wenye hukaa tu wakalishwa, kuna wenye hufanya kazi kwa bidii, kuna wenye kazi yao ni kufanya mahaba na malkia pia kuna wale hufanya vibarua kwa kuwatumia nyuki wenye hadhi. Hakika hili linasawiri hali

ambazo huendeleza athari za binadamu kwa wenzake. Dkt Matoga anashadidia hili kupitia misingi ya dini na kukariri katika *Vipuli* kuwa, "... hiyo hali kaiumba mungu. Sijui binadamu wanashindwaje kuelewa mambo haya ya kawaida." (uk. 108). Balozi Suprano anadhihirisha athari za mtu kwa mwenzake kupitia majukumu yake kama Balozi. Balozi Suprano anamuuliza Dkt Matoga ikiwa alipokea vyombo vyote vya upasuaji na vya kuhifadhi vipuli ili kuwahakikishia biashara shwari. Anatumia mamlaka yake kutoa kinga ya kibalozi ili kuifanikisha biashara yao. Hali hii inalandana na nguzo ya uongozi mbaya.

Hili linadhihirisha kuwa Balozi Suprano anatumia mamlaka yake kuulinda na kuuendeleza uongozi mbaya mjini Daluta. Ikizingatiwa kwamba Balozi Suprano anaashiria viongozi wa mataifa tajiri ya Ughaibuni ilhali Dkt Matoga anaashiria viongozi wa mataifa fukara ya Afrika, basi ni dhahiri kuwa, viongozi wa mataifa tajiri ya Ughaibuni huukuza, huupalilia na huuimarisha uongozi mbaya katika mataifa fukara ya Afrika na kuyanufaisha mataifa na wananchi wao, huku wakiwatumia wananchi wa mataifa ya Afrika kama vifaa au shashi ila sio kama binadamu. Hivyo, mataifa ya Afrika huendelea kufifia na kukaushwa na uongozi mbaya huku yale ya Ughaibuni yakifaidi na kunenepa kwa raha. Ingawa hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya pia linafungamana na nguzo ya uwezo na kifo mtawalia.

Mwandishi Mkangi anakiri kuwa hamna tofauti ya umati wa watu na ule wa ng'ombe wanaosubiri kuchinjwa na madhara ya vitendo vya binadamu. Kwa misingi hii, binadamu anazalisha mauti kupitia utafiti. *Sayari* ni chombo kinachozaliwa kama zao la utafiti wa binadamu. Pia binadamu hana tatizo kumtoa binadamu mwenzake kafara. Dzombo baada ya kuhukumiwa kifo anatiwa kwenye *Sayari* inayorejelewa na mnyongaji kama halali. Woga ni mojawapo ya athari za mtu kwa mwingine unaopigiwa upatu na binadamu. Kwa mfano, mtawala katika taifa la Dzombo anapata furaha kutokana na kifo cha Dzombo. Kwa upande mwingine, Dzombo kutokana na kunyanyaswa na athari za mtu kwa mwenzake anaishia kuendeleza athari zile zile hasi bila hiari yake. Baada ya kufutwa kazi na tajiri wake, anaamua kujiajiri mwenyewe. Katika bidii zake za kuingilia ukulima kwa dhati anakata vichaka na kufyeka misitu. Jambo hili linachangia uharibifu wa rasilimali asilia pakubwa. Hakika hili linadhihirisha kuwa athari za binadamu kwa mazingira huwa hasi kwa binadamu mwenyewe hasa katika mazingira yanayotawaliwa na ufukara.

Dkt Charles kutokana na athari za Profesa Williams anapalilia uharibifu wa mazingira kupitia taaluma ya upachuaji na upachikaji wa vipuli vya mioyo na figo, na pia ule wa ubongo. Anashirikiana na Profesa Williams, Dkt Matoga na Balozi Suprano katika mradi wa vipuli vya mioyo na figo ambao wote wanaufanikisha. Profesa Williams akidhihirisha namna biashara na mradi huu kwa jumla unavyouangamiza uhai wa watu wengi katika *Vipuli* anaeleza kuwa, "Mchango wake ni katika kunusuru maisha, kazi na hadhi yake katika mradi huu wa kuchezea moto." (uk. 135). Kwa mujibu wa mwandishi Mbogo, maisha yanayolindwa na Balozi Suprano ni yale ya anthroposenia kwa jumla ambayo imeashiriwa na moto ilhali mradi wenyewe kwa jumla unazalisha athari chungu nzima hasi za anthroposenia dhidi ya ulimwengu, hususani katika maisha ya binadamu kimwavuli.

**iii. Tamaa na Ubinafsi**

Binadamu anapojiendeleza kiuchumi, vitendo vyake vinavyoongozwa na tamaa, ubinafsi na unajisi dhidi ya mazingira vinachangia kuendeleza uharibifu wa mazingira na hivyo vinahatarisha uhai wa viumbe vyote. Mathalani, mtunzi Mbogo katika *Bustani* anafafanua kuwa, Mto Zamala ulikuwa umepungua sana samaki tofauti na kitambo ambapo walikuwa wengi. Upungufu huu umezalishwa na kiwanda cha Saga Saga. Takataka na mafutamafuta ya kiwanda hiki yalielekezwa ndani ya Mto Zamala. Kutokana na sumu ya takataka na mafutamafuta, maisha ya viumbe na mimea yaliweza kuhatarishwa pakubwa. Binadamu baada ya kuimeza ile sumu kupitia maji au samaki, huweza kupatwa na maradhi na hatimaye huweza kuangamia. Mimea nayo huweza kukauka na hili huvisababishia viumbe hai njaa ambayo mara nyingi husababisha maafa. Hili linafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile, ambapo watu wanakufa kila uchao kama zao la binadamu kushindwa kuyatunza mazingira. Hili linawiana na kauli ya Nayar (2010) kuwa, tamaa na ubinafsi wa binadamu humzalishia maangamizi kutokana na njaa, ndwele, mafuriko, kemikali, na mmomonyoko wa udongo.

Mjomba wake Dkt Matoga anadhihirisha tamaa na ubinafsi. Kama Mkuu wa Magereza, anapalilia tamaa na ubinafsi anapomshauri Dkt Matoga kushiriki mradi wa vipuli vya binadamu, hususani figo na mioyo. Kwa mujibu wa Wamitila (2022), Mdee na wenzake (2015), BAKITA (2015; 2022) na TUKI (2013), figo ni kiungo kilicho ndani ya mwili wa binadamu au wa mnyama au wa ndege, ambacho hufanya kazi ya kusafisha damu na kutoa uchafu mwilini. Kwa upande mwingine,

wanafafanua kuwa, moyo ni kiungo kilicho katika mwili wa viumbe hai kama vile binadamu au wanyama, ambacho husukuma damu na kuieneza mwilini kote. Suala la msingi linalodhihirika katika *Vipuli* ni kuwa, kando na majukumu muhimu yanayotekelezwa na viungo hivi viwili – figo na moyo – mwilini, ukosefu au tatizo la viungo hivi huweza kusababisha maafa kwa binadamu au mnyama. Howarth (1996) anadokeza kuwa, tamaa ya binadamu ya kujilimbikizia mali bila kujali binadamu mwenzake pamoja na mazingira yake imemfanya afikie kiwango cha kujiangamiza mwenyewe. Hakika hili linafungamana na mhimili wa haki na maadili ya kimazingira.

Hivyo, mtunzi Mbogo kusawiri shughuli ya uwindaji na uuzaji wa vipuli vya figo na moyo kama zao la tamaa na ubinafsi ni suala linalohalisi na linalolandana na baadhi ya nguzo kuu za anthroposenia, ambazo lengo kuu huwa maangamizi ya kila aina na hali. Shughuli hii ni hatari na ndiyo sababu Mkuu wa Magereza anamshauri Dkt Matoga na kumsisitizia haja ya kuweka siri kubwa kadiri iwezekanavyo ili afanikiwe. Kwa misingi hii hii, Banko – Bosi wa Bandari – amesawiriwa kama mwenye tamaa na ubinafsi kutokana na hulka yake ya ufisadi unaopalilia biashara ya uuzaji wa vipuli vya figo na mioyo. Kando na hilo huipotezea serikali kiwango kikubwa cha ushuru wa bandari. Kutokana na tamaa na ubinafsi wa Banko mashine za kuhifadhia figo na mioyo zinaingia mjini Daluta bila kizingiti chochote. Mashine hizi zinafanikisha mauaji ya maskini, viwete na makahaba kwa lengo la kuvuna vipuli vya figo na mioyo. Ufanisi huu unapaliliwa na kurutubishwa na nguzo ya uongozi mbaya ambapo ufisadi unashamiri kama zao la tamaa na ubinafsi wa walalahai.

Magamba na Dkt Matoga wanaendeleza tamaa na ubinafsi wanapohimizana katika njama ya kuiba maiti kutoka mle Mochware anakofanya kazi Magamba kama mhudumu. Baada ya zao la tamaa na ubinafsi kwa binadamu ambalo ni kifo kutokana na athari hasi zao, Magamba na Dkt Matoga wanadumisha tamaa na ubinafsi kwa kuvuna vipuli vya figo na mioyo kutoka kwenye wafu. Siri na kazi wanayoshirikiana zinadumisha na kuendeleza tamaa na ubinafsi. Magamba anakiri kuwa ile ni kazi inayobidi wawe na ujasiri na moyo wa kuitunza siri ya mauti. Dkt Matoga katika *Vipuli* anataja kuwa, "... siri hiyo ni maiti." (uk. 77). Hili linathibitisha kuwa tamaa na ubinafsi kupitia shughuli ya kiuchumi huzalisha mauti. Hali hii inashabihiana na mhimili wa kifo ambapo baada ya binadamu kujilundikizia kila kitu hatimaye hujiangamiza mwenyewe baada ya kuyaangamiza mazingira yake.

Isitoshe, Magamba anaendeleza tamaa na ubinafsi kupitia msaada wa maiti na viungo vya maiti anaowapa wachawi, waganga, wafanya biashara, wanasiasa na viongozi tofautitofauti. Sanaa ya sihiri na kiza anayoshiriki Magamba na kubobea imejikita katika mizizi ya tamaa na ubinafsi. Kigezo kikuu kinachowaongoza Dkt Matoga na Magamba kupalilia tamaa na ubinafsi ni pesa. Dkt Matoga anapokumbuka namna mradi wa vipuli vya figo na mioyo utakavyofungua mikoba ya hazina, woga unamkimbi, nguvu na ujasiri vinamvamia na anabadili sauti. Kwa ujasiri anafafanua katika *Vipuli* kuwa, “Nitahitaji maiti - ... kila siku: wake, waume kwa watoto wa aina na sampuli zote.” (uk. 78). Hili linathibitisha kuwa, ikizingatiwa kuwa wote wawili wanaongozwa na tamaa na ubinafsi na shughuli yao ya kiuchumi inatawaliwa na maiti, basi hatima kuu ya tamaa na ubinafsi ni maafa. Hali hii inafungamana na nguzo ya kifo.

Maafa haya hutokana na tamaa na ubinafsi wa binadamu kama anayosawiri Dkt Matoga. Dkt Matoga analiweka hili wazi anapoeleza kuwa, watu wengi huaga kutokana na ajali, ujambazi au hata maradhi mengi ya kawaida kutokana na udhoofu wa huduma za afya. Hili linashadidia ukweli kwamba, kutokana na tamaa na ubinafsi wa viongozi wengi uongozi hudorora na huduma nyingi hutiwa doa. Lakini, hata Magamba mwenyewe anatishwa na mradi huu ambao umejaa mizungu na vizungumkuti asivyowahi kukumbana navyo na kijasho kinamtoka kwapani. Hili linadhihirisha kuwa mauti hutisha hata wale wanaoyapalilia na kuyalinda. Hata hivyo, tamaa ya kutajirika, ubinafsi na uchoyo vinawapa Magamba na Dkt Matoga ujasiri wa kuvuna vipuli vya figo na mioyo kutoka kwenye maiti.

Tamaa na ubinafsi huzalisha uongozi mbaya na hatimaye uharibifu wa mali ya umma. Dkt Matoga anadhihirisha kuwa alikuwa kiongozi mbaya kupitia ufisadi na ubadhirifu wa mali ya umma anapomwambia Bruno kuwa awe mwangalifu katika kazi yake pale zahanatini. Sababu kuu ikiwa, hataki kupata hasara. Anasisitiza kuwa ingekuwa wakati alikuwa waziri, hangejali hasara kwa kuwa Wizara ama serikali ingepata hasara ila siye, lakini kwa sasa Bruno awe makini ili pasitokee hasara yoyote. Kwa misingi hii ya uongozi mbaya, Mkuu wa Magereza anasawiriwa na mwandishi kama mwenye tamaa na ubinafsi baada ya kumruhusu Dkt Matoga na wafanyakazi wake wavune vipuli vya figo na mioyo, kutoka kwenye maiti ya wafungwa waliouawa baada ya hukumu yao ya kunyongwa kutimia. Hivyo, ubinafsi na tamaa zinaimarisha uongozi mbaya. Hali hii inafungamana na nguzo za uongozi mbaya na kifo.

Hakimu anayemhukumu Dzombo anadhihirisha tamaa na ubinafsi. Katika nchi ya akina Dzombo mahakimu hawana huruma kwa sababu wanapalilia anthroposenia kupitia ubinafsi, tamaa na ufisadi vinavyowatawala. Ndiposa anaingia kama malaika wa mauti pale mahakamani kutokana na uraibu wake wa kuishi akiipalilia na kuiendeleza ubinafsi-uchoyo. Katika *Walenisi,* inadhihirika kuwa, katika anthroposenia mahakama hazifuati sheria kwa mujibu wa kuzilinda au kuzitetea wala kuzidumisha haki za binadamu. Hii ni kwa sababu, anthroposenia hushamiri watu wanapopalilia ubinafsi, tamaa na ufisadi. Anadhihirisha hili katika *Walenisi* anapofafanua kuwa, "Kazi yake kubwa ilikuwa ni kumtia hatiani yeyote yule aliyekuwa amepatwa na kisirani cha kushtakiwa." (uk. 1). Katika anthroposenia binadamu anashabikia na kuzoea kifo kinachosababishwa na binadamu kwa binadamu mwenzake kama jambo la kawaida katika jamii kutokana na desturi ya ubinafsi. Aidha ubinafsi na tamaa vinamnyima mtu uwezo wa kudadisi athari za matokeo ya vitendo vyake kwa binadamu mwenzake na mazingira yake.

### 4.2.2 Binadamu Kupitia Utovu wa Utu na Maadili

Binadamu kupitia hali ya kutokuwa na au hali ya kukosa hulka zinazolandana na hadhi ya mtu, mwenendo mwema unaokubalika na wanajamii wengi katika mazingira yao au katika taaluma au maisha yao kwa jumla (Kumar, 2014; Roberts, 2015; Carvalho na Gavioli, 2020), amechangia pakubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira ulimwenguni. Hili lilibainika baada ya uchunguzi wa binadamu kama aina ya anthroposenia katika riwaya nne teule lililodhihirishwa na kuwekwa wazi na waandishi wa kazi hizo teule. Kiuyakinifu, dhihirisho la binadamu kukosa ubinadamu na tabia njema vilionyesha namna binadamu anavyopalilia anthroposenia katika mazingira yake mwenyewe. Nguzo zilizoongoza uchunguzi huu ni pamoja na binadamu dhidi ya maumbile, uongozi mbaya, na utamaduni na mazingira. Binadamu anachangia pakubwa kupujua mazingira katika kuhifadhi anthroposenia kupitia shughuli zake za kila siku za nyumbani, kama vile kufua nguo na kuosha vifaa vingine kama vile mashine au magari, kuosha vyombo na kukoga mwili.

#### i. Shughuli za Nyumbani

Kwa jumla, shughuli za nyumbani huhusisha maswala kama vile; kupamba nyumba, kukata majani ya mifugo, kukata nyasi, kupiga nguo pasi, kufagia, kusoma, kutupa taka, kupika, kusafisha vyombo, kusafisha nyumba, kufua nguo, kulima bustani na kulisha wanyama. Kwa misingi ya nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile, Nayar

(2010) anatahadharisha kuwa, jinsi binadamu anavyotagusana na mazingira katika shughuli zake za nyumbani huweza kuzalisha aidha upujufu au uhifadhi wa mazingira kutegemea uwajibikaji wake. Mathalani, wananchi wa Siza katika *Bustani ya Edeni,* wake kwa waume, watoto kwa wakubwa, wanahatarisha afya zao kupitia shughuli za nyumbani. Hili linazidisha uchafuzi unaotokana na kiwanda cha kemikali cha Saga Saga. Hili linadhihirika pale ambapo wanaonekana wakifua, wakioga na kisha wakiyanywa maji yale yale yaliyokuwa na uwezekano wa kusababisha maradhi yasiyo na tiba, kama vile saratani. Ikizingatiwa kwamba maradhi yasiyotibika huhitaji fedha nyingi kudhibitika, wakazi wa Siza walikodolewa macho na ulofa kutokana na changamoto chungu nzima katika kuhifadhi anthroposenia bila hiari yao huku ikiwanyonya uhai wao. Maathai (2009) akikubaliana na mawazo ya mtafiti anaeleza kuwa, kando na huduma za afya kuwa ghali sana katika nchi za Afrika, Waafrika wanazidi kupalilia hulka na tamaduni zinazonajisi mazingira, ambayo huzalisha virusi kutokana na uchafu, na kutokana na kiwango cha juu cha ufukara baina ya wananchi. Hatimaye, maradhi haya ambayo ni zao la binadamu la shughuli zake zinazohifadhi anthroposenia huwaangamiza watu wengi. Hali hii inafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile.

Katika *Walenisi* Uchuna ulisisitiza haja ya kuwepo na baadhi ya watu wa kuwafulia Wachuna chupi zao, kuwaosha na kuwatunza watoto wao, kuyasafisha magari yao na pia watu wa kuwachimbulia thangari na ndago zao Wachuna. Hali hii inadhihirisha kiwango anachodunishiwa utu wake mnyonge na tajiri. Hivyo, Uchuna ulisisitiza kuwa elimu kwa wote na tena bora ingezalisha mafahali wengi ambao daima hawakai zizi moja. Wananchi ambao hawakuwa na uwezo waliendelea kunyanyaswa na wenye uwezo na mamlaka. Wachuna waliwafanya wenzao kuwa watumwa waaminifu na watiifu, hadi walipogutuka na kujenga taifa la Walenisi lililopalilia na kuuhimiza utu na maadili paruwanja baina ya Wawalenisi. Kutokana na utovu wa utu baina ya Wachuna, maradhi yanayowaangamiza ni yale ya kuwanenepesha kuliko nguruwe ilhali wananchi fukara udhia wao ni njaa. Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anadhihirisha hili anapotaja kuwa, "... waja na vijakazi wao. Hawa, waliachwa kuokota masazo, kurambaramba masahani, kukomba vyungu na kuguguna mifupa – makombo ya Wachuna." (uk. 173). Hakika hili linadhihirisha kiwango cha unyama ambao huwepo baina ya matajiri na maskini hususani katika mataifa fukara ulimwenguni. Kutokana na tofauti kubwa iliyopo baina ya matajiri na maskini katika

mataifa mengi, utu wa maskini hukandamizwa na badala yake maskini hutumikishwa kama kifaa na matajiri. Katika hali hii, mazingira ya maskini hutumiwa kama jaa la kutupia taka na matajiri wenye uwezo. Hali hii inawiana na nguzo ya uwezo.

**ii. Athari za Ulofa**

Ulofa unamsukuma binadamu kuuuza na kuusaliti utu wake. Matajiri wengi wanachukua fursa hii kuwatisha walalahoi bila kuyajali mazingira yao kwa jumla. Kwa mfano, pale hospitalini ingawa Pasta Yona anafanikiwa kumwona Samsoni, kwa wananchi wanaoamini lile wanaloambiwa, inadhihirika kuwa matajiri wasio na maadili wanaweza kuipalilia anthroposenia kwa kuununua utu wa watu na kuwanyima wengi huduma katika maeneo mbalimbali. Hii ni kwa sababu, baadhi ya watu, kutokana na ulofa huyavua maadili na utu na kujivika unyama, ufisadi, tamaa na ubinafsi. Mtunzi Mbogo anataja kuwa, binadamu katika harakati za kupambana na ulofa amejipata katika bahari la ubinafsi na tamaa unaosababisha upujufu wa mazingira kwa kiwango kikubwa. Pasta Yona anakiri kuwa matajiri wa kiwanda cha *Sagasaga Chemical Industry Limited* wanaabudu fedha na utajiri kuliko uhai wa binadamu. Hali hii inamfanya binadamu kutisha uhai wake mwenyewe pamoja na mazingira anamoishi. Mathalani, katika kiwanda cha Sagasaga, wafanyakazi wanapakia maboksi ya madawa na makemikali ndani ya lori bila wao kuvaa sare wala mipira ya kujikinga na ajali mikononi mwao.

Utepetevu huu huchangia sio tu uharibifu wa mazingira bali maradhi ambayo yanaweza kuepukika ambayo hatima yake huwa kifo. Katika mataifa mengi barani Afrika wafanyakazi katika viwanda mbalimbali hupuuzwa na waajiri na hunyimwa vifaa vya kimsingi vya kujikinga kutokana na hatari aina aina. Horacio (2015) anapendekeza kuwa utepetevu huu udhibitiwe kikamilifu ili kuzuia vurugu dhidi ya mazingira na hatimaye kupunguza maangamizi ya mazingira. Moore (2018) anadokeza kuwa utepetevu huu hunawiri kutokana na haja ya kuimarisha kapitalosenia dhidi ya ulimwengu wa tatu kutoka kwa viongozi wa ulimwengu wa kwanza. Mtafiti naye anashadidia kauli kuwa, utepetevu huu husababishwa na ubinafsi na tamaa ya wenye nafasi katika harakati za kuulinda utajiri wao kwa kuendelea kuwafilisisha zaidi wanyonge na mazingira yao. Filipova (2023) na Garrard (2023) wakikubaliana na mawazo ya mtafiti wanasisitiza kuwa, ulofa huchangia pakubwa katika uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika mataifa ya ulimwengu wa tatu. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo na kifo ambapo wenye

nafasi hutumia uwezo wao kuyanajisi mazingira ya wanyonge halafu husababisha kifo.

Hivyo, binadamu kutokana na tamaa na ubinafsi anauimarisha ulofa na kwa wakati huo huo anajitia kitanzi kiafya. Mathalani, Yusuf anamweleza Jonalisti kwa dhati na uchungu kuwa, maisha yake pamoja na ya wafanyakazi wenzake mle kiwandani yalikuwa ya taabu. Anasisitiza kuwa kazi yenyewe ilikuwa hatari na kuthibitisha kauli hii anapovua kofia yake ya kibaragashia, kisha anainama na kumwonyesha Jonalisti vidonda vilivyotapakaa kichwani mwake. Anamuuliza Jonalisti katika *Bustani* kibalagha kuwa, "Unaona? Vidonda." (uk. 20). Yale yanayomsukuma binadamu kufanya kazi katika mazingira hatari yanayosababisha maradhi ni ulofa. Hili linawiana na kauli ya Smith (2007) kuwa, ulofa huchangia uharibifu na uchafuzi wa mazingira kupitia ufisadi.

Aidha, binadamu mwenye uwezo na nafasi hutumia vitisho kumkandamiza maskini. Binadamu anaimarisha ulofa kupitia vitisho dhidi ya wanadamu wenzake. Mathalani, viongozi wa kiwanda cha Sagasaga wanawatisha wafanyakazi pamoja na Jonalisti. Ndiposa Yusuf anaposikia mtu akija anavaa kofia yake harakaharaka ili isibainike kuwa ameonyesha mtu mwingine vidonda alivyonavyo kichwani. Hili linaashiria kwamba wenye kiwanda hawataki kuwapa wafanyakazi vifaa vinavyohitajika kwa minajili ya usalama wao dhidi ya madawa ya sumu na wanawatisha waduni. Hili linashabihiana na nguzo ya uwezo na ya uongozi mbaya ambapo wenye mamlaka na uwezo huwakandamiza wanyonge kwa kutumia mamlaka vibaya. Tan (2019) anaeleza kuwa, wenye uwezo hutumia ulofa kama ala ya kuwadhibiti na kuwadhulumu waduni. Hili hufungamana na nguzo ya uongozi mbaya ambao hupalilia ulofa kwa kiwango kikubwa. Hili linafungamana na kauli ya Reno (2022) kuwa, mizizi ya ulofa unaosababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya mwanadamu ni uongozi dhoofu.

Chandler na wenzake (2020) wanafafanua kuwa, binadamu huusaliti utu na maadili yake kutokana na changamoto zitokanazo na ulofa maishani. Mathalani, Pasta Yona wa Yona anaketi pale kwenye *Equator Hotel* akimngoja mgeni wake, Mama Esnati. Alimtarajia afike pale mwendo wa saa tisa jioni. Mmoja wa wafanyakazi katika hoteli ile anashika bomba na kupuliza dawa ya kuulia nzi na wadudu wengine. Baada ya kuipuliza harufu inaenea kila pahali. Hili linaashiria uharibifu wa hewa mle ndani

kutokana na kitendo cha mfanyakazi kupuliza dawa ya kuulia nzi na wadudu ilhali mlikuwa na watu kadhaa waliokuwa kwenye meza nyingine wakila na kunywa. Kutokana na ulofa, ingawa binadamu anaishi katika mazingira chafu na anatumia vifaa vyenye kemikali zinazotishia uhai wa wanyama, wadudu, mimea na hata wake mwenyewe, unyama ndio unaomfanya kuyaharibu mazingira yake. Unyama huu husababishwa na ukosefu wa mahitaji msingi hasa baina ya wachochole ulimwenguni kama zao la ulofa. Hali hii huchangia pakubwa katika utovu wa maadili ya binadamu na hatimaye ukiukaji wa maadili ya mazingira. Alia (2017) katika ufafanuzi wa nguzo ya haki na maadili ya kimazingira anasema kuwa, uhitaji wa binadamu humfanya kuyazika maadili yake na ya mazingira katika kaburi la sahau.

Hili linadhihirishwa na mtunzi Mbogo anapoisawiri hoteli ya *Equator Hotel* ambayo haikuwa ya haja. Aidha hali yake ya usafi haikupendeza kamwe na nzi pamoja na wadudu kama mende waliruka na kutua kila pahali ovyo. Mfanyakazi anapopuliza ile dawa huku yeye mwenyewe akipiga mluzi, harufu ilienea kila eneo na kusababishia wateja kupiga chafya. Kutokana na ulofa binadamu anajisahau pamoja na utu wake na kusababisha uharibifu wa hewa bila kuwajali binadamu wenzake. Hakika hili ni kweli kwa mujibu wa nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile ambayo hushadidia kuwa, binadamu anaangamia kila siku kutokana na kushindwa kwake kuyalinda na kuyatunza mazingira yake. Hata hivyo, ni vyema kutambua kuwa kushindwa huku husababishwa na ulofa ambao humnyima binadamu uwezo wa kuyalinda na kuyatunza mazingira na badala yake kuyakausha katika harakati za ushindani uliogubikwa na manyanyaso na maonevu kati ya walalahai na walalahoi. Hili humpelekea binadamu kujiponza mwenyewe na kudhuru afya yake kutokana na uoga wa kuogopa kukabiliana na uharibifu wa hewa.

Mwandishi katika *Bustani* anaeleza kuwa, “Walaji chakula walipiga chafya lakini ama waliogopa kusema au (katika ujinga wao) walifikiri kitendo kile kilikuwa hasa ndiyo sehemu ya usafi, wenyewe.” (uk. 55). Hili linadhihirisha kuwa binadamu anapalilia uchafuzi wa hewa na mazingira kwa jumla kupitia ujinga unaozalishwa na ulofa na utovu wa utu anaouendeleza mwenyewe kwa kutodadisi mambo, hali na matendo katika mazingira alimo. Hata hivyo, ufukara pia unachangia pakubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira hasa katika nchi za Afrika ambamo uongozi dhalimu unatawala. Hali hii inafungamana na mhimili wa uongozi mbaya. Kutokana na ulofa watu wanakosa kudadisi kemikali zinazotumika

katika maeneo wanamoishi. Mathalani, Pasta Yona anakumbuka katika *Bustani* kuwa: ‘Yote haya ni madawa yanayozalishwa na Sagasaga. Na wao ndugu zangu akina yakhe hawana hili wala lile.’ (uk. 55). Kadhalika, kutokana na uongozi mbaya unaopaliliwa na binadamu, viwanda vinavyoendeleza uchafuzi wa hewa na mazingira kwa jumla katika janibu za Afrika vinashamiri.

Kupitia mazungumzo baina ya Pasta Yona na Mfanyakazi pale kwenye hoteli ya *Equator Hotel,* inabainika kuwa uchafuzi wa hewa husababisha ubishi, swintofahamu na migogoro baina ya wanajamii. Hii ndiyo sababu vijana wanaomsaidia Pasta Yona pamoja na Mama Esnati kubeba mizigo wanazozania nafasi ya kubeba mizigo ile angaa wapate riziki. Ufukara huu unazalisha mgogoro baada ya Pasta Yona kuwaachia mia mbili wagawane. Pasta Yona anapomuomba mfanyakazi awaruhusu wateja wale kwanza kabla ya kupuliza dawa hamsikilizi wala hamjibu ila anaendelea tu kupuliza. Pasta Yona anabisha kuwa kando na harufu tele dawa ile ilisababisha matone yaloweza kuingia ndani ya chakula. Hata hivyo, mfanyakazi yule anasita kidogo tu kupulizia na kwa kejeli anamjibu Pasta Yona katika *Bustani* kuwa, “Kama unajifanya mtaalamu na mtanashati sana – nenda huko *Hilton* au *Embassy*. Umefuata nini hapa?” (uk. 55). Katika anthroposenia, wanajamii wanashangilia na kushabikia vurugu baina ya watu na dhidi ya mazingira kuliko mchezo wa burudani. Hali hii inalandana na mhimili wa uongozi mbaya ambapo viongozi huwapofusha na kuwatumia wananchi kama shisha. Hii ni kwa sababu, baada ya Pasta Yona kutetea haki za wanajamii na yule mfanyakazi kumkejeli, baadhi ya watu wanamcheka kweli. Hakika hili linadhihirisha kuwa uchafuzi wa hewa hushamiri katika mazingira yenye ulofa.

Kwa mujibu wa Omolo (2002), wabunge katika mataifa mengi fukara hasa barani Afrika wanamvua mwananchi utu. Wabunge Wachuna katika *Walenisi* wanawahurumia watu duni na kupitisha mswada bungeni. Mswada wenyewe unamaanisha kuwa, baada ya Wachuna kuwaosha paka na mbwa wao, maji hayo yatiwe mapipani na watu duni watunukiwe kama msaada. Hii ni baada ya watu duni kukosa hata tone la kupikia ama kunywa. Magazeti na wakuu wa dini za Wachuna wanasifu umaskini kwa sababu wanasifu kitendo hiki cha ukarimu mkuu cha Wabunge wao. Ikizingatiwa kwamba maji ni uhai (Maathai, 2009), ukosefu wa maji kwa walalahoi unaashiria maangamizi kwa yahe wote. Kando na kukosa maji, akina yahe wanaishi maeneo sawa na makaburini. Mwandishi Mkangi anaeleza katika

*Walenisi* kuwa, "... kwa ujasiri wa matumaini, waliyaita makaburi haya yaliyopwaya kama madungu, ama vibanda hivi vilivyopeperushwa kama ndifu – nyumba." (uk. 176). Alia (2017) anapendekeza kuwa utovu wa utu huchangia ulofa ulimwenguni. Burdon (2023) anashadidia kuwa ulofa umepelekea uchafuzi na unajisi wa mazingira ya binadamu. Burdon na Martel (2025) wanadokeza kuwa, baadhi ya athari za ulofa ulimwenguni ni unajisi wa mazingira safi kutoka kwa viongozi wenye uwezo na mamlaka. Mtafiti naye anashadidia kauli kuwa, asili ya uharibifu wa mazingira ulimwenguni ni ulofa ambao huwa ala ya matajiri na kijisababu chao tosha cha kuyachafua na kuyaharibu mazingira ya wanyonge. Ingawa wanyonge hushuhudia uchafuzi na uharibifu huu huwa hawana uwezo wa kuuzuia wala kuuthibiti.

Zuka na wenziwe wanasawiriwa na mwandishi katika *Mafuta* kama vijana fukara katika mataifa fukara barani Afrika. Hii ni kwa sababu, ingawa mwenye mkunazi aliwapatia fungu moja la kunazi kila siku alipoamka, akina Zuka na wenziwe walikuwa wanamwendea kinyume kwa kuukwea mkunazi kwa haraka na kujitundia kunazi wenyewe bila idhini. Halaiki ya watu wenye sura za furaha katika jumba kubwa wanaometameta kwa mafuta waliyojipaka wanasawiri viongozi na matajiri wenye uwezo na mamlaka katika mataifa fukara. Pande la mtu linalowajibikia mguu mmoja wa kitanda linasawiri waziri katika mataifa fukara. Kitanda chenyewe kinaashiria ulaghai ambao hunawiri katika maeneo fukara. Mtunzi Mkangi ni mithili ya Njogu na Mazrui (2006) wanaashiria kitanda kama gereza la utumwa, najisi, maonevu, ulofa, ukandamizaji wa haki kwa jumla na utumwa wa mataifa. Hivyo, ulofa huukausha utu wa binadamu kiwango kwamba binadamu hugeuka kuwa aidha kiongozi mbaya au mwananchi dhoofu. Hali hii inafungamana na nguzo za kifo na uongozi mbaya.

Moore (2016) na Watson na Watson (2007) wanataja kuwa, kutokana na athari hasi za ulofa, binadamu ameuvua utu na kuvaa unyama. Kwa mfano, mtu yeyote angemwonyesha Waziri wa Mguu wa Kulia ya Mbele ya kitanda ufedhuli wowote, angenyongwa. Mtue anasisitiza hili anaposhangaa katika *Mafuta* kuwa, "Lahaula! Kweli huyu ni nyoka mkoko!" (uk. 18). Nyoka mkoko ni mnyama anayeashiria matajiri wenye unyama badala ya utu. Wasaidizi chungu nzima wa Waziri huyu pia wanaashiria watumwa kutokana na ulofa maadamu madaraka na mamlaka yote ni ya Waziri. Lile jukumu la Waziri wa Mguu wa Kulia ya Mbele la kuhakikisha kuwa kitanda hakitingishiki au kupwaya au kuwa mregumregu linamsawiri kama mnyama

mwenyewe, madhali ana jukumu la kuulinda na kuupa uhai ufukara. Kitanda chenyewe kina vikwazo na ubaguzi tele na kinadumisha utawala dhalimu, ufukara, utabaka na vurugu dhidi ya mazingira. Mafuta yanayohitajika mtu ajipake angaa aweze kukilalia yanasababisha vurugu dhidi ya mazingira, utabaka, ulofa halafu maafa, kama vile mumewe mama Fofi katika *Mafuta*. Mafuta yenyewe yanaashiria ulaghai ambao humsababishia binadamu ulofa.

Kipanga katika *Vipuli* anasawiri athari za ulofa kupitia tamaa ya utajiri mwingi. Tamaa ya utajiri inamfanya Kipanga kuwateka nyara watoto wadogo wa umri wa kati ya mwaka mmoja hadi miaka sita na kuwauzia akina mama matajiri wa nchi jirani, ambao licha ya kuwa na utajiri mwingi hawakujaliwa kupata watoto. Akina mama hawa walikuwa tayari kununua watoto mahali popote kwa fedha nyingi zaidi, na hili linamsukuma Kipanga kuwauza watoto wa wenyewe. Hali hii inadhihirisha namna athari hasi za ulofa huchangia sio tu dhiki na changamoto tele maishani mwa binadamu ila hunawirisha utovu wa maadili na utu.

#### iii. Utowajibikaji

Halikadhalika, katika anthroposenia binadamu anaendeleza uharibifu wa mali, uchafuzi wa mazingira na hata mauaji ya binadamu wenzao kutokana na kutoyawajibikia maisha na mazingira yao wenyewe na binadamu wenzao. Mtunzi Mbogo katika *Bustani* anaeleza kuwa, kikundi cha waandamanaji vijana kilikwenda palipokuwa na kibao cha Halmashauri ya Jiji kilichoonya dhidi ya umwagaji taka ovyo katika dampu la Siza. Nguvu walizodhihirisha kuing'oa mihimili ya kibao kile zilikuwa za ajabu. Baada ya kuking'oa na kukitupa chini mtu mmoja anachukua kiberiti na kukiwasha. Vijana wengine waliingia mle ndani ya dampu wakiwa na fimbo mikononi wakawafukuza nguruwe na ng'ombe waliokuwa wanabugia taka kwa raha zao. Hili linaashiria utowajibikaji wa binadamu katika anthroposenia. Waandamanaji walionekana wamelewa na kupagawa bila kujali yeyote wala chochote. Wanasahau utu na nidhamu na wanaingiwa na jazba ya kupiga, kubomoa, kuangamiza, kuteketeza kila kitu walichokikuta njiani. Hali hii inafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile ambapo binadamu anakosa kuyawajibikia wala kuyasikitikia mazingira yake. Hakika hili hupelekea mazingira kunajisiwa kwa kiwango kikubwa, hali ambayo husababishwa na viumbe hai kutokana na maradhi, ukame na majanga mengine mengi ambayo hutokana na utowajibikaji wa binadamu.

Kuna wale wanakwenda madukani wakati wa maandamano, wanavunja na kuiba mali ya wenzao. Wengine wanaingia sokoni na wanapora maembe, ndizi, minofu ya nyama iliyoachwa na wauzaji waliojitosa kwenye umati wa maandamano. Pia wanazuilia gari moja la Halmashauri ya Jiji na lingine la kiwanda cha kemikali cha Sagasaga pale barabarani na wanayatia moto. Pamela ambaye ni shujaa wa kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa maliasili na rasilimali asili anaghadhabishwa na wendawazimu ule wa wananchi. Jonalisti anafadhaishwa na namna wananchi walivyokuwa waharibifu mali na mazingira kwa wakati ule. Mwandishi katika *Bustani* anadhihirisha hili kupitia maelezo kuwa, "Naye pia alikuwa ametiwa hofu na uharibifu wa mali uliokuwa unafanywa na baadhi ya waandamanaji." (uk. 92). Hili linathibitisha kuwa, binadamu anaweza akapigana na uharibifu wa mazingira ila si kuyanajisi kama baadhi ya wananchi pale Siza wanaowakilisha ulimwengu mpana kimwavuli. Hili linawiana na kauli ya Head (2018) kuwa binadamu ana uwezo na nafasi kabambe ya kuyanadhifisha na kuyahifadhi mazingira bila kujishughulisha na mwenzake ambaye anaweza kuwa mbioni kuyanajisi mazingira yale yale. Uhifadhi huu utafanikishwa na binadamu mwenye kuyawajibikia na kuyasikitikia mazingira yake.

Kutokana na kutowajibika kwa binadamu, anajihami kuyachafua mazingira na kumwangamiza binadamu mwenzake badala ya kuyatunza na kumlinda. Kwa mfano, askari lukuki waliokuwa na hasira na silaha za kila aina walisimama kidete tayari kukabiliana na hali yoyote ile. Walisimama wakiwa wamekizunguka kiwanda cha Sagasaga. Walikaa tayari wakisubiri amri ya kamanda wao ili wamwangamize adui wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Wanapoamrishwa wasonge mbele wananyemelea taratibu bila kupepesa macho. Mwandishi wa *Bustani* anasema kuwa, "Walikuwa wamepania kuwalinda akina Bwana Abdula, akina Trans-Chemi na matajiri wengine wa aina hiyo." (uk. 93). Bila tashwishi waliwakabili wazazi wao, shangazi zao, dada na kaka zao, binamu zao, rafiki, adui na watoto wao.

Utowajibikaji unawaharibu wanadamu kiwango kwamba wanawalinda mawakala wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira bila kuyajali maisha ya wenzao. Pale nje ya kiwanda cha Siza, askari wanawalinda wachafuzi wa mazingira pamoja na kiwanda kinavyosababisha uchafuzi wa mazingira, hewa na maji kwa jumla dhidi ya wananchi. Kwa wakati huo huo matajiri wenye kiwanda kile wako majumbani mwao wakitizama runinga na video huku wengine wakiogelea na kuota jua ufuoni mwa bahari. Kwa upande mwingine, wananchi wa Siza waliokuwa wanakabiliana na

vyanzo vya uchafuzi na uharibifu wa mazingira waliangamizwa na askari waliokuwa wakikilinda kiwanda cha kemikali cha Sagasaga. Hili linawekwa bayana na mwandishi wa *Bustani* anapoeleza kuwa, bunduki zilitapika risasi na kutoa sauti kubwa na kisha moshi. Hakika pafukapo moshi pana jambo. Utowajibikaji huzalisha maangamizi yanayoashiriwa katika hali hii na moshi wa bunduki baada ya maangamizi. Mtunzi Mbogo katika *Bustani* anasawiri hali hii kwa kueleza kuwa:

> Bunduki:
> Tatatatatatatatatatatataaaaa!!!
> Tratratratratratratratratratraaa!!
> Bumbumbumbumbumbumbum!!!
> Moshi! Moshi! Moshi!
>
> Wananchi;
> Yoweeeee
> Yalaa!
> Mamaanguweeee!
> Tunakufa jamani! ... (uk. 93).

Damu ya watu ilimwagika katika vurumai ile na mazingira yakabadilika mekundu na kutapakaa maiti ya watu. Baadhi ya walioaga ni Doricas huku Samsoni akishikilia ziwa la mauti akilinyonya; Pamela naye alizimwa ubishi wake milele na risasi tatu, na kwa jumla, takriban watu hamsini walipoteza maisha yao. Hili linadhihirisha kuwa, binadamu anaghasi mazingira ya jana, leo na kesho kutokana na tamaa na uchu wake wa kupalilia utowajibikaji wake huku nguvu zake zikiuumbua ulimwengu, jambo ambalo hakika ni mkongoto maishani mwa binadamu na ulimwengu kwa jumla. Hali hii inafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile na ile ya haki ya mazingira ambapo binadamu ingawa amepewa uwezo wa kuyamiliki na kuyatawala mazingira, yenyewe yana haki ya kutoharibiwa na kuchafuliwa. Hakika hili linawiana na kauli ya Issberner na Lena (2018) kuwa, utowajibikaji wa binadamu umempelekea kujiangamiza mwenyewe pamoja na mazingira yake kwa juhudi zake binafsi.

Nyau kwa mfano anadhihirisha utowajibikaji kupitia unyama anaomtendea Eliza. Nyau anaashiria mataifa yenye uwezo ambayo huyapa mataifa changa na duni ya Afrika misaada. Anadhihirisha dhuluma, mateso na maonevu mataifa tajiri huyatendea mataifa changa na duni ulimwenguni, na hasa sana barani Afrika kama

zao la utowajibikaji. Hali hii inafungamana na nguzo ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya uwezo, ambapo mataifa yenye uwezo huyanajisi mazingira ya mataifa duni na changa. Eliza bintiye mama Eliza, mwenye umri wa miaka sita ananyanyaswa na kudhulumiwa na Nyau. Mtoto huyu mdogo, kama mataifa changa ya Afrika ni mchangamfu na anapendwa na kila mpangaji kwenye eneo wanaloishi na mamake linaloashiria ulimwengu uliojaa mateso, unyama na dhiki tele. Eliza ni wa darasa la kwanza kuashiria kiwango cha chini cha elimu katika mataifa duni na changa ya Afrika. Anapotoka shuleni ana madaftari mawili ndani ya mfuko wa plastiki, kuashiria umilisi na utaalamu pungufu katika mataifa ya Afrika pamoja na uharibifu wa mazingira ambao hunyonga nchi za Afrika unaoashiriwa na mfuko wa plastiki. Plastiki huchangia kiwango kikubwa cha uharibifu na uchafuzi wa mashamba, mabomba ya maji, mito, maziwa na mabahari aina aina ulimwenguni. Hili linawiana na kauli ya Mostafanezhad na Norum (2021) wanaoshadidia kuwa, plastiki huchangia zaidi ya asilimia sitini na saba ya ajenti za uharibifu wa mazingira na rasilimali asilia ulimwenguni.

Nyau anampa Eliza chai na mkate na mtoto huyu anakunywa huku wakiongea na mjombake Nyau bila taarifa kuhusu hatari inayomkabili mle chumbani mwa Nyau. Hali hii inaashiria uhusiano wa mataifa duni ya Afrika na yale tajiri ya Ughaibuni ambao huwa wa maonevu, mateso, manyanyaso na dhuluma za aina zote bila utu. Hili linawiana na kauli ya akina Mwirabua (2014) na Waithiru (2019; 2020) kuwa, hata baada ya Mbeberu kuondoka bado huwa anadhibiti uongozi, siasa, uchumi na utamaduni wa Mwafrika kupitia ukoloni mamboleo, hivyo kulifanya bara la Afrika kwa jumla kumtegemea Mbeberu kwa njia mbalimbali. Baadhi ya utegemezi huu hufanikishwa kupitia misaada ya chakula, chanjo tofautitofauti dhidi ya maradhi yasababishwayo na Mbeberu yule yule, usalama, taaluma na mikopo ya riba ya juu yenye masharti ya utumwa. Hili linafungamana na kauli ya Thiong'o (1987) kuwa, mataifa ya ulimwengu wa kwanza huyakopesha mataifa ya ulimwengu wa tatu mikopo yenye riba ya juu ambayo huyafanya mataifa fukara kuwa kama watumwa. Nyau anambaka Eliza na kumharibia mwili wake na maisha yake ya hapo baadaye akayatia doa na kovu la daima.

Kadhalika, Kipanga na Nyau wanadhihirisha utowajibikaji kupitia uvutaji wa sigara. Kwa mujibu wa mwandishi Mbogo katika riwaya ya *Bustani*, moshi wa sigara kutoka kwa Bwana Abdula unamsababishia Zaituni saratani. Maradhi haya huchangiwa

pakubwa na uchafuzi wa mazingira na binadamu hasa uchafuzi wa hewa na maji. Hili linashabihiana na mhimili wa binadamu dhidi ya maumbile wa Nadharia ya Uhakikimazingira, ambapo binadamu kutokana na kutowajibika kwake kwa mazingira huzalisha maradhi aina aina. Saratani ni zao la seli ambazo hulishwa na seli zipatikanazo kwenye sukari. Hivyo, punde tu zinazopitishwa kutoka kwenye moshi wa sigara hadi kwenye koo na mapafu, mwili wa binadamu nao hutoa mazingira mwafaka kwa seli zile kunawiri kutegemea aina cha chakula anachokila sana.

Mtunzi Mbogo anaeleza katika *Vipuli* kuwa, "Nyau na Kipanga walisimama kwa furaha ... walipokea sigara zile kila mtu paketi moja ... mate yamejaa mdomoni." (uk. 125). Nyau na Kipanga wanaendeleza uchafuzi wa hewa wanapovuta sigara wanazopewa pakiti kila mmoja na Dkt Matoga pale nje. Dkt Matoga anaokota kiberiti mezani na Nyau anakipokea. Baada ya Nyau kukipokea wanawasha sigara na wote wawili – Nyau na Kipanga – wanaanza kuvuta. Hili linashabihiana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile na ile ya uongozi mbaya, ambapo viongozi ndio wanaowapa vijana sigara kama njia ya kuwahonga na kuwapumbaza. Hili linawiana na kauli ya Waithiru (2022a) kuwa, viongozi wengi katika mataifa duni barani Afrika huwapumbaza vijana kwa kuwapa dawa za kulevya na pombe haramu ili waweze kuwadhibiti na kuwatumia kama shisha.

Wakili wa Dkt Matoga, Premji pamoja na mganga wa Dkt Matoga, Mzee Makolokoza ni baadhi ya wahusika wanaosawiri utowajibikaji na ubinafsi-uchoyo. Hawajali matokeo wala athari ya matendo yao mradi wao wajitajirishe tu. Baada ya Waziri wa Afya – Dkt Matoga – kukumbwa na kesi ya ubadhirifu wa mali ya umma, anamkimbilia mganga wake ili aimarishe ngome yake halafu ampe ushindi dhidi ya mashtaka. Mzee Makolokoza hajali umma unaokosa huduma kutokana na utumizi mbaya wa mali ya umma na Dkt Matoga madhali anabatilisha haki na ukweli. Ngome ya Dkt Matoga inaashiria hulka ya matumizi mabaya ya mali ya umma ilhali ushindi wake ni ushindi wa matajiri na viongozi dhoofu dhidi ya chumi duni katika nchi za Afrika na ulimwenguni kwa jumla. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo. Mganga anafanikiwa kuizika kesi kwa kuwafunga midomo mashahidi na kumtia hakimu giza kuu. Unyamazishaji pamoja na giza ni baadhi ya mbinu ambazo matajiri na viongozi badhirifu hutumia kujitajirisha ulimwenguni kote, hasa katika mataifa ambayo yanadhibitiwa na kutawaliwa na ukoloni mamboleo. Hili linawiana na kauli ya Bergthaller na Horn (2020), Vermeulen (2020), Feder (2021) na Reno (2022)

kuwa, ukoloni mamboleo imekuwa ala mwafaka ya kutumiwa na viongozi wa mataifa tajiri dhidi ya mataifa fukara kuyanajisi na kuyafanya tasa mazingira yao katika misingi ya uwezo. Hivyo, hili linafungamana moja kwa moja na nguzo ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya uwezo na kifo.

**iv. Ukatili**

Ukatili ni hali ambapo binadamu hukosa huruma, mapenzi na utu kwa jumla dhidi ya binadamu wenzake na mazingira yake mwenyewe. Mathalani, Nyau katika *Vipuli* anadhihirisha ukatili wake kwa kuwaangamiza binadamu kupitia ushauri wake na maelezo kwa Shipe na Kipanga. Nyau anawashauri kuwa wapite katika kila kibanda kwanza, huku wakipulizia sumu nusukaputi ili kuhakikisha kuwa waduni wote wamezimia. Anasisitiza kuwa hilo likifanikiwa, Kipanga atasongeza gari karibu kabisa na vibanda ili wapakie mizigo yao haraka na kwa wepesi. Isitoshe, Nyau kwa sauti inayodhihirisha unyama na ukatili uliopevuka anasisitiza kuwa watawapanga wanyonge wale kama kuni. Mtunzi Mbogo anathibisha hili katika *Vipuli* anapotaja kuwa, "... sauti yake ikionyesha ukatili na kukomaa kwa roho ya mauaji kuliko wenzake." (uk. 165). Binadamu mwenye ukatili huukosea uhai wa binadamu heshima na huwaona watu kama vifaa visivyostahili heshima. Hii ndiyo sababu Nyau anapendekeza kuwa wawapange waduni wale kama kuni. Ikizingatiwa kwamba dhima kuu ya kuni huwa kuchomwa moto kwa kusudi fulani, inadhihirika kuwa kwake Nyau, maskini wale hatima yao ni maangamizi kwa lengo la kuwanufaisha matajiri kama akina Dkt Matoga. Hili linafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile. Ukatili unamfanya Dkt Matoga kwa ushirikiano na Agnes na kutokana na tamaa ya utajiri wanamdondoa mgonjwa figo moja katika harakati za kumtoa kidole tumboni. Hali inayompelekea mgonjwa yule kumeza kidole inaashiria njaa ilivyoshamiri ulimwenguni kiwango kwamba binadamu anakula viungo vyake vya mwili akiwa hai.

Kwa upande mwingine, Nyau na Shipe wanadhihirisha ukatili mkomavu zaidi ukilinganishwa na unaodhihirishwa na Kipanga katika kuuangamiza uhai wa mtu. Mwandishi Mbogo anadhihirisha hili katika *Vipuli* anapofafanua kuwa, "Walilenga kwenye matundu na nafasi nyingi za vibanda vile na kuwafusha wale 'mbu maskini' ili kuzidisha usingizi wao." (uk. 165). Nyau na Shipe wanawalinganisha waduni na mbu. Ikizingatiwa kwamba mbu ni mdudu mdogo na mwembamba ambaye hufyonza damu ya watu au wanyama na kuwaambukiza maradhi kama vile malaria au matende

(Waithiru, 2022b), ni dhahiri kuwa Nyau na Shipe wanaudharau uhai wa watu maskini. Aidha wanawaona watu duni kama ajenti wa maambukizi ya maradhi hatari kwa watu ama uchafu unaofaa kuondolewa ulimwenguni. Hili linafungamana na nguzo ya kifo ambapo binadamu hujiangamiza yeye mwenyewe, mazingira yake pamoja na viumbe hai vilivyomo.

Baada ya Nyau na Shipe kuhitimisha mikoromo ya waduni, wanasaidiana na Kipanga kuwapakia waduni wale ambao kwao akina Nyau, ni vipuli ila si watu. Baada ya kupakia maskini wa mwisho kwenye gari, Nyau anapiga tochi kila mahali kuhakikisha kuwa hakuna maskini hata mmoja aliyesalia. Mtunzi Mbogo katika *Vipuli* anaeleza kuwa waliondoka pale baada ya kuhakikisha kuwa usafishaji takataka zile ulikuwa umefanyika vyema. Katika mfumo wa ukoloni mamboleo na uongozi dhoofu ambapo ukatili unashamiri; maskini, viwete, vipofu, viziwi, na walemavu wa aina aina wanachukuliwa kama takataka na matajiri wenye uwezo, mamlaka, nafasi na sauti katika jamii. Aidha wanaonekana kama mbu ambao wanafaa kuangamizwa kwa kupuliziwa sumu. Hali hii inawiana na kauli ya Gregory (2021) kuwa, ingawa ukoloni mamboleo unafungamana na unajisi kama aina ya burudani katika filamu za ufuska za Magharibi, huunajisi utamaduni na mazingira ya mataifa yanayoathiriwa nao moja kwa moja kwa njia hasi sana. Hili linalandana na nguzo ya uongozi mbaya.

Hata hivyo, hatima na mazao ya ukatili huwa kifo. Kwa mfano, Kipanga anadhihirisha dhahiri kuwa shughuli ya uwindaji wa binadamu wenzake na biashara nzima kwa jumla inawaongoza katika hatima ya maangamizi. Linalompa uhakika huu ni thibitisho kuwa, uhuru wao ni wa uongo kabisa madhali wangali watumwa wa Dkt Matoga. Hatima hii huwa sawa kwa maskini na tajiri. Mathalani, mwandishi Mbogo analiweka hili bayana katika *Vipuli* kupitia maelezo yanayodhihirisha mkongoto dhidi ya Dkt Matoga kuwa:

> "Uso wa Dkt Matoga ulikuwa umekatwa vipande viwili, ... mkono wa kushoto begani umekaribia kunyofoka; kifuani ... donda kubwa, minyama imechanuwa kwa hasira na huzuni, ikawacha moyo wa Dkt Matoga wazi. Tumbo ... limechanika na kuyafanya matumbo na figo zichungulie nje kwa shingo upande." (uk. 261).

Hivyo, inadhihirika kuwa, ingawa binadamu humwangamiza binadamu mwenzake na mazingira yake kama zao la ukatili, hatimaye huangamizwa na mazingira yale yale

kama njia ya mazingira kujidhibiti. Hili linawekwa wazi na hali inayosawiriwa na sehemu za mwili wa Dkt Matoga baada ya ajali pale barabarani. Hali hii inafungamana na mhimili wa haki na maadili ya mazingira ambapo ingawa binadamu ametunukiwa uwezo wa kusimamia vyote vilivyomo ulimwenguni (Alia, 2017), hajaruhusiwa kuviharibu na kuvichafua. Mintarafu ya mhimili huu, binadamu anafaa kutathminiwa ikiwa jinsi anavyohusiana na kuingiliana na mazingira yake na viumbe vilivyomo hai na visivyo hai anahusiana kwa hadhari na maadili au kwa ukatili.

Baada ya Nyau na Kipanga kuwakusanya na kuwaangamiza waduni pale mjini Daluta na kurejea Mtoni Clinic, Dkt Matoga akisaidiana na watu wake wa mikono, anazitoa figo zote na mioyo na kuzihifadhi kwenye vyombo spesheli. Dkt Matoga anadhihirisha ukatili kupitia shughuli zake za usiku. Usiku, kwa kuwatumia Nyau, Kipanga na Shipe, Dkt Matoga analisafisha jiji la Daluta. Analisafisha kwa kuwaangamiza viwete, maskini, vipofu, makahaba, vichaa na vilema na kisha kuvuna viungo vya figo na mioyo yao. Hili analithibitisha Dkt Matoga mwenyewe katika riwaya ya *Vipuli* anapoapa na kusisitiza kuwa:

> “Ni jiji zuri lakini watazame: wamevaa mararu, funza wamewang’ong’osoa miguuni, matongotongo yametapakaa usoni. Ni aibu kwa nchi – hasa watalii wanapotembelea jiji letu. Nitausafisha!” (uk. 161).

Hivyo basi, anthroposenia kupitia ukatili inawafaidi matajiri na viongozi huku ikiwatambariza wanyonge na walemavu wanaoonekana kama uchafu, hasa katika nchi fukara za Afrika. Utovu wa utu na maadili unawafanya watu wakose ubinadamu na badala yake kushirai unyama katika nafsi zao. Funza wanaowang’ong’osoa wanyonge na walemavu miguuni ni zao la athari hasi za anthroposenia katika mataifa duni ulimwenguni. Watalii wanaoabudiwa na kuheshimika wanaashiria mataifa tajiri ambayo kwa uwezo wao wa kiuchumi huyatumikisha mataifa duni katika mfumo wa uchumi wa kibepari ambao huuangamiza utu, maadili na uhuru wa kujieleza. Hili linawekwa bayana na mwandishi wa *Vipuli* anapotaja kuwa, “... hawa hawa ... maskini waliochafuka, walionekana mbele ya macho yake kama tunu, lulu, dhahabu, almasi, manemane.” (uk. 161). Hii ndiyo sababu, ingawa Dkt Matoga anawaona kama uchafu, kwa wakati huo huo anawaona kama rutuba ya kuurutubisha unyama na maangamizi. Baada ya binadamu kukosa utu anaingiliana na watu, wanyama na

mazingira yake kwa ukatili bila kujali matokeo yake kwa ulimwengu kwa jumla. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo.

### 4.2.3 Binadamu na Maendeleo

Binadamu kupitia maarifa ya sayansi na matumizi yake katika mitambo, vyombo na zana katika viwanda, kilimo, ufundi au njia za mawasiliano pamoja na hali inayomtawala binadamu ya kupata ustawi (TUKI, 2014; Ndalu na wengine, 2014; BAKITA, 2022; Wamitila, 2022) amefanikiwa kuikuuza na kuiendeleza anthroposenia bila hiari wala fahamu (Ballard, 2023; Hujibens, 2023; LaMothe, 2024). Upofu unaotokana na tamaa ya kujiendeleza unamfanya ayanajisi mazingira yake bila tahadhari wala uwajibikaji. Hili lilipambanuliwa paruwanja na data iliyochanganuliwa baada ya kuchunguza aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule za Kiswahili. Nguzo zilizoongoza uchunguzi huu ni pamoja na ile ya maendeleo endelevu ambapo kutokana na haja ya binadamu kujiendeleza kila uchao hujipalia mwenyewe makaa ya athari za mazingira chafu na dhoofu; uongozi mbaya ambapo viongozi wenyewe huulinda uchafuzi na uharibifu wa mazingira kutokana na tamaa, ubinafsi-uchoyo na utowajikaji; na utandawazi ambapo viongozi wa mataifa tajiri huyadhibiti na huyatawala mazingira ya mataifa fukara kupitia vikaragosi vyao ambao huwa visesere ila si viongozi wazalendo hasa.

Mathalani, kupitia Baba Adamu na Mama Hawa, mtunzi Mbogo anafafanua jinsi binadamu amepalilia uchafuzi wa mazingira kupitia uzinduzi na ubunifu wake. Kutokana na teknolojia na maendeleo katika nyanja za sayansi na nyuklia, binadamu amesababisha uharibifu wa mazingira kupitia uchafuzi wa hewa, utupaji taka hatari ovyo na uchafuzi wa mito, maziwa na mabahari. Uharibifu na uchafuzi huu unasababisha madhara tele sio tu katika maisha ya binadamu ila pia kwa viumbe vingine hai na maumbile kwa jumla. Kwa mfano, uharibifu wa mazingira, hususan unajisi wa rasilimali asilia kupitia juhudi za binadamu za kujiendeleza kimaendeleo, umemeza mito miwili ya Havala iliyotiririka huku ikiyakumba mawe ya dhahabu kuelekea baharini katika *Bustani*. Aidha umemeza Mto Gihoni uliosafiri ukibeba tope na udongo wenye rutuba. Binadamu baada ya kukata miti ovyo na kulima kwenye mbavu za mito, mito Gihoni wakati wa masika ilipotea. Mbolea iliyokuwa inamwagwa na mto huu kandokando ya mabonde ya Edeni imetoweka na mahala pake mbolea zenye kemikali hatari kwa wanyama na binadamu zimechukua nafasi ile.

Hali hii inawiana na nguzo ya maendeleo endelevu ambapo binadamu katika harakati za kujiendeleza mbele anajirejesha nyuma kimaendeleo na hatimaye kujitia kitanzi mwenyewe. Hili linafungamana na kauli ya Nayar (2010), Albert na Lawanson (2019) na Waithiru (2022d) inayoeleza kuwa, juhudi za binadamu za kujiangamiza mwenyewe zisipositishwa au kupunguzwa mwendo basi binadamu atayaangamiza mazingira yake halafu atajiangamiza kwa haraka sana. Katika juhudi za kujiendeleza, binadamu anasababisha kukauka kwa mito hususani katika mataifa yanayojiendeleza ulimwenguni. Utowekaji wa mito huzalisha ukame, njaa na hatimaye baada ya mimea kukauka maafa huwa ibada kwa watu, mifugo na wanyama. Hakika hili ni kweli, madhali binadamu aliyewahi kushiba tumbo, macho na hisia anaangamia kutokana na janga la njaa katika *Bustani*. Mimea ya matunda, miti, maua na vyakula vilivyokuwa vikinawiri kwenye mabonde ya Edeni vimekauka. Ikizingatiwa kwamba Edeni inaashiria ulimwengu na akina Baba Adamu na Mama Hawa ambao wanaashiria binadamu duniani, inadhihirika kwamba binadamu anateseka na hatimaye kuangamia kutokana na uharibifu anaosababisha mwenyewe kama zao la harakati za maendeleo endelevu.

Mto Hedekeli uliowahi kutembea kwa madaha na kupita mbele ya Ashuru huku ukinyonga kiuno chake kizuri ulikaushwa na shughuli za binadamu za kuendeleza maendeleo endelevu. Tamaa na ubinafsi wa binadamu ulimpelekea kuharibu fuko na pwani zilizotandikiwa mchanga wa fedha za mto ule. Aidha, binadamu amebadili rangi ya nyasi iliyowahi kuwa ya kijani kibichi kutokana na umwagaji taka zenye kemikali ovyo. Hali inalandana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo kando na viongozi kupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira huhalalisha sera ambazo huchangia pakubwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika maeneo yao. Barani Afrika, hali huwa ya kawaida na hivyo mna haja ya wananchi kulidadisi suala la uongozi na viongozi kwa lengo la kuyahifadhi mazingira yao wenyewe. Hili linawiana na kauli ya Maathai (2009), Waithiru (2023) na Hujibens (2023) kuwa, viongozi na wananchi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu wasiposhirikiana kuzitatua changamoto zinazoyakumba mazingira yao wenyewe bila kuwaruhusu viongozi wa ulimwengu wa kwanza kuwadhibiti na kuwatawala kimawazo na kielimu, basi wataendelea kuangamiza mazingira yao na kutapatapa katika ulofa.

Maua ya kila rangi yaliyowahi kuwakumbatia wanadamu kwa uturi na manukato yasiyomithilika yameadimika na nafasi yake kuchukuliwa na harufu mbaya, uozo wa

taka na moshi wa kila aina. Binadamu waliowahi kulala juu ya mchanga wa fedha kabla ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira asilia, huku wakiwa wamekumbatiana kwa undugu, umoja na upendo, wakilitazama jua likisafiri kuelekea magharibi walitamauka katika mazingira chafu na tasa, na kutawaliwa na ufisadi, ubinafsi, tamaa na chuki. Mazingira chafu na dhoofu yanalea chuki, tamaa, ubinafsi na ufisadi kutokana na ulofa, maendeleo ya teknolojia, na nyuklia. Uwezo wa mazingira kuyalea mambo hasi namna hii unapaliliwa na haja ya binadamu kujitajirisha na kujiendeleza maishani bila kuyajali wala kuyasikitikia mazingira yake ya leo na kesho. Ingawa jana ya binadamu ilikuwa safi, ya kupendeza na isiyotawaliwa na maradhi aina aina, mazingira ya leo yamenajisiwa na taka, kemikali, moshi, uozo wa; mawazo, maadili na tamaduni mbalimbali, unajisi wa; chemchemi za maji, rasilimali asilia, mito, maziwa na bahari, ukataji miti ovyo, na ulimaji usiowajibikia mazingira. Hali hii inaambatana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo viongozi na utawala huruhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira huku ukiomba misaada ya kiutumwa kutoka kwa mataifa tajiri ya Ulaya, Uropa na Marekani pamoja na Shirika la Fedha Ulimwenguni kusaidia kuyahifadhi na kuyasafisha mazingira yale yale.

Hili linawekwa bayana na mwandishi Mbogo katika *Bustani* anapoeleza kuwa, nyuso za binadamu zimezungukwa na harufu mbaya, uozo na taka, uozo wa maadili, moshi kutoka kwenye viwanda na vyombo vya usafiri, kiangazi na maradhi ya aina aina hususani katika janibu fukara. Aidha, katika mataifa maskini binadamu amebadili mazingira kwa njia hasi. Kwa mfano, mtunzi Mbogo anaeleza kuwa, binadamu amesababisha kutoweka kwa Mto Frati. Mto huu uliwahi kukimbia kwa kasi na kuvuka milima, huku ukiparamia milima ya mawe, kabla ya kuweza kusababisha mungurumo wa maanguko makuu ya maji. Badala ya mungurumo wa aina hii, kama ilivyotajwa awali binadamu amezalisha uchafuzi wa hewa kupitia mashine za viwanda, magari ya usafiri na mashine zingine tofautitofauti unaochafua hewa.

Mwandishi Mbogo anaeleza kuwa binadamu amejiponza mwenyewe. Mathalani, kupitia Baba Adamu analalamika katika *Bustani* kuwa, “Watu wamekata miti, majangwa yameingia. Tulipouliza, tukaambiwa ni shauri ya mashine, maendeleo. Kweli, watu hawaendi kwa miguu tena, wana magari, ndege na roketi. Watu hawapigani vita kwa mikuki wana mabomubomu, wana nyuklia.” (uk. 38). Hakika haya yanarutubisha shughuli zinazozalisha anthroposenia ulimwenguni kupitia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa jumla. Mashine nyingi zimerahisisha kazi ya

ukataji miti. Ndege, roketi na magari hutoa hewa mkaa ambayo huchangia asilimia kubwa ya uchafuzi wa hewa ulimwenguni. Mabomu ya nyuklia husababisha mazingira tasa, huangamiza viumbe hai vyote na huhakikisha kuwa hamna viumbe vinavyoweza kuishi pale na kuzaana bila ulemavu wa kipekee kwa karne kadhaa. Hili linawiana na kauli ya LaMothe (2024) kuwa, nyuklia huwa na madhara kali, hatari zaidi na ya muda mrefu kwa mazingira kuliko kemikali nyingine yoyote na hivyo huongoza katika kuyahasi mazingira pamoja na watu, wanyama na mifugo waliomo. Hatimaye, hali hii husababisha kifo ambacho ni nguzo ya Nadharia ya Uhakikimazingira iliyoongoza uchanganuzi huu.

### 4.2.4 Binadamu Kupitia Utumwa wa Kimawazo na Kiutawala

Binadamu kupitia mfumo katika jamii wa kumtumia mja fulani kama chombo cha biashara na kumfanyisha kazi bila malipo (TUKI, 2014; Mdee na wenzake, 2015; Wamitila, 2022) kwa kumpangia na kumpangulia mambo ndani ya ubongo wake (Ndalu na wenzake, 2014; BAKITA, 2022), ameimarisha anthroposenia kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, anautumia mfumo uu huu katika kuzidhibiti njia za kuendesha shughuli za kutawala za serikali, mamlaka na uongozi kwa jumla (Ndalu na wenzake, 2014; TUKI, 2014) kuiendeleza na kuilinda anthroposenia. Hata hivyo, kiuyakinifu, utumwa huu wa kiutawala na wa kimawazo hutekelezwa na viongozi kwa kupalilia ujinga kupitia elimu dhoofu pamoja na mataifa tajiri dhidi ya mataifa fukara, hasa barani Afrika ambapo viongozi wengi huwa vikaragosi vya viongozi wa mataifa kwasi ya Ughaibuni (Waithiru, 2022c; 2022d), hasa ya Kimagharibi. Utumwa huu wa kimawazo na kiutawala ulidhihirika baada ya uchunguzi wa binadamu kama aina ya anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili kwa kuongozwa na baadhi ya mihimili mikuu ya nadharia ya Uhakikimazingira. Mihimili iliyoongoza uchunguzi huu ni pamoja na uwezo na kifo, binadamu dhidi ya maumbile, na uongozi mbaya na utandawazi.

#### i. Utumwa wa Utawala

Baada ya kudungwa na miiba, kuchomwa na jua mgongoni, kunyeshewa na mvua mgongoni na umande kupata makao mgongoni mwake na kumpa nyungunyungu, Dzombo katika *Walenisi* anashuhudia mahindi yakitoa punga. Harufu ya shibe ilikuwa imeshaanza kumkosesha amani aliposhuhudia jioni moja, madereva na matingatinga yakiingia shambani mwake na kuyafyeka mahindi yote shambani. Jambo hili linapalilia ulofa kwa jumla kupitia upaliliaji wa njaa ambayo huzalisha maafa. Mataifa mengi barani Afrika huishi katika kivuli cha utumwa wa masharti ya

mataifa tajiri na mashirika mbalimbali ya misaada hasa ya fedha. Hali hii inawiana na kauli ya Thiong'o (1987) kuwa, mataifa tajiri ya Magharibi pamoja na Shirika la Fedha Ulimwenguni huyafanya mataifa fukara ya Afrika fukara zaidi kwa kuyafunga katika minyororo ya mikopo na misaada ya kulemaza maendeleo. Hakika mataifa mengi barani Afrika yanaendelea kupapatika katika baa la njaa na utegemezi wa misaada kutoka Ughaibuni. Utegemezi husababishwa na utumwa wa kimawazo na kiutawala ambao hulindwa na kuimarishwa na viongozi wa mataifa tajiri ya Ulaya na Marekani dhidi ya mataifa fukara ulimwenguni.

Dzombo kwa uchungu na lawama bila kikomo anajieleza kwa mrasimu ambaye ni mkubwa wa ukulima. Ingawa Dzombo aliendeleza vurugu dhidi ya mazingira kwa kufyeka misitu na hivyo kuchangiza ukataji miti ovyo, mrasimu alichangia uharibifu zaidi alipowatuma madereva na matingatinga kuyafyeka mahindi aliyokuwa ameyapanda Dzombo. Mrasimu anamlaumu Dzombo kwa kupanda mahindi katika sehemu isiyoruhusiwa na hivyo kukiuka kanuni za ukulima kwa mujibu wa wakubwa wa ukulima. Viongozi barani Afrika wanaimarisha ulofa kwa kuendeleza baa la njaa ili watu waendelee kufukarika kupitia ubepari na ubidhaaishaji wa kibepari, ubinafsishaji wa Uropa, na ukoloni mamboleo. Ingawa hili huwahakikishia mamlaka dhidi ya wananchi maskini na wenye njaa, hufukarisha mataifa husika zaidi. Hili linawekwa bayana na mrasimu katika *Walenisi* anapofoka na kumjuza Dzombo kuwa, "Ungekuwa umepanda *kahawa, kakao, pareto* – ama hata *maua ya waridi au katani,* haingekuwa neno, lakini si mahindi!" (uk. 17). Linalowaongoza viongozi katika mataifa mengi fukara ni tamaa, ubinafsi na ukoloni mamboleo. Mrasimu anadhihirisha hili anapomwambia Dzombo kuwa, kupatwa na njaa kwake sio muhimu, ila muhimu ni kuwa angelima mimea ya pareto, kahawa, maua ya waridi au katani badala ya mahindi, basi taifa lingenufaika kwa kupata fedha za kigeni. Fedha zinazoelezwa na mrasimu hazina manufaa yoyote kwa taifa. Aidha zinawahakikishia kuendelea kuwa watumwa wa ukoloni mamboleo kama zao la ubidhaaishaji wa Uropa.

Katika *Walenisi*, mtunzi Mkangi kupitia mhusika Mtu-Dzombo anamsawiri binadamu kama aina ya anthroposenia katika ulimwengu wa Wawalenisi ingawa ulimwengu huu na wenyeji wao hatimaye wanamgeuza nia na utambulisho pia. Jambo hili linadhihirishwa na Mama Mtu-Maanani anaposhiriki majadiliano na mumewe Mzee Mtu-Mwenzio. Mzee Mtu-Mwenzio anaeleza kuwa, Mtu-Dzombo alidhihirisha

ubinafsi baada ya safari yake ya utu. Hii ni kwa sababu, aliubinafsisha utu na kuwanyima wenzake kutokana na imani yake kuwa bahati ndiyo imwongozayo binadamu badala ya juhudi na uvumilivu. Kutokana na utumwa wa kimawazo, watu wengi maskini huamini kuwa maisha mema ni bahati ila sio zao la juhudi na uvumilivu. Imani hii hutokana na utapeli wa kidini na imani ambapo wahubiri wengi huwatisha na kuwateka waumini mawazo na hatimaye huwatawala kama visesere. Hakika hili hunoga sana barani Afrika. Utumwa huu ni zao la mkoloni ambaye kando na kumfanya Mwafrika kuamini kuwa dini yake na utamaduni wake ni duni alimpa elimu iliyoendeleza itikadi, desturi na imani za utumwa wa kimawazo na utegemezi kwa mkoloni badala ya uvumbuzi na ubunifu.

Kwa mujibu wa mtunzi Mkangi, kusudi la ajira huwa kuufifisha uhai wa binadamu pamoja na kukitukuza na kukiimarisha kifo. Mathalani, mwandishi anataja katika *Walenisi* kuwa, "Nao Wachuna kwa kusisitiza kuwa kazi ni bahati ya wachache, wakafaulu kumvua binadamu utu wake na kumpiga bei kama andazi. Na kama andazi basi, si ajabu wengi wakavia." (uk. 174). Ile hali ya kuvuliwa utu inamfanya binadamu kukumbatia maangamizi, hasa ya mazingira yake na ya uhai wake mwenyewe kwa jumla. Hili hulifanikisha kupitia njaa ambayo hupaliliwa na mazingira chafu na yenye maradhi tele. Binadamu huendelea kuangamia katika mazingira chafu na tasa hususani barani Afrika kama zao la utumwa wa utawala. Hakika hili linawiana na nguzo ya uwezo na kifo ambapo wenye uwezo huwadidimiza wanyonge kwenye maangamizi ya uchumi wao, mazingira yao na hatimaye uhai wao.

**ii. Utumwa wa Kimawazo**

Wachuna wanasawiri utumwa wa kimawazo na kiutawala kikamilifu kupitia hulka na utamaduni wao wa Uchuna. Wachuna wanadhihirisha kuwa Uchuna sio tu uhusiano unaopalilia ubaguzi, maonevu na manyanyaso baina ya watu wawili ila baina ya mtu binafsi na mahitaji yake muhimu. Kwa mfano, Uchuna unasema kuwa sio lazima mtu ale na ashibe madhali kula kwenyewe kwategemea bahati ya mungu. Wachuna wanatumia dini kuhalalisha utumwa wa kimawazo. Wanasisitiza katika *Walenisi* kuwa, "Binadamu hataishi kwa mkate tu peke yake." (uk. 172). Pia, Uchuna unasema kuwa si lazima mtu ajitumikishe kwa juhudi zake ila lazima apate wa kumwajiri kutegemea bahati yake. Kwa misingi hii, kazi inakuwa bahati nasibu wala sio ya kuadhimisha utu. Uchuna unaendelea kutaja kuwa, matibabu hayawezekani kwa kila

mwananchi kwa sababu huduma za matibabu zilitegemea uwezo wa kifedha wa mtu binafsi. Zaidi ya hayo, Uchuna unaongeza kuwa, nyumba si ibada kwa kila mtu ila uwepo wake ungetegemea bahati ya kuzinunua. Hakika hili linadhihirisha kuwa utumwa wa kimawazo hudidimiza sio tu uwezo wa kubuni na kuzindua ila pia haki za kimsingi kwa binadamu. Hivyo, wanyonge kutokana na utumwa wa kimawazo wanategemea matajiri kupata lishe, mavazi na makazi. Ikizingatiwa kwamba haya ni mahitaji msingi kwa binadamu, inadhihirika kuwa utumwa wa kimawazo hupalilia ulofa.

Utegemezi huu ulichangia kuwepo kwa familia zinazoishi vichochoroni mijini leo hii, hasa katika mataifa fukara ulimwenguni. Smith (2007) anadokeza kuwa, katika mataifa mengi barani Afrika kama vile, Nigeria ufisadi kando na kuchangia umaskini, maradhi, njaa na vifo vinavyoweza kuepukika, umepalilia waasi na mayatima wengi ambao huishia kuishi kando ya vichochoro mijini tofautitofauti. Isitoshe, Uchuna unasisitiza kuwa, hamna binadamu aliyezaliwa na mamake akiwa amevaa mavazi, na hivyo, jinsi alivyotoka tumboni mwa mamake, vivyo hivyo anafaa kuendelea kuishi uchi, madhali uchi ni maumbile ambayo kubadilika kwake ni bahati tu. Haya yote yanafanikisha utumwa wa kimawazo na kiutawala kupitia binadamu ambaye kando na kuizalisha, ndiye injini ya filosofia hii yenye dhuluma, maonevu, maradhi, maangamizi na ubaguzi ulimwenguni. Kutokana na haja ya kuendeleza utumwa wa kimawazo na wa kiutawala, vikaragosi wa mataifa fukara, hasa yaliyowahi kutawaliwa na mbeberu hupigia upatu elimu inayoendelea kupalilia utumwa huu hasa. Hili linawiana na kauli ya Filipova (2023) kuwa, ingawa mkoloni aliondoka katika janibu alizowahi kutawala hapo kabla, elimu aliyoyarithisha mataifa husika huendelea kuyadidimiza mataifa haya katika bahari la ulofa, utegemezi na unajisi wa mazingira yao asilia.

Wachuna wanawafanya watu fukara zaidi ya nusu wanyama. Wanawageuza fukara na kuwafanya tarakimu katika hesabu ya vitu vinavyochafua mazingira yao ‘safi’. Hali hii inawafanya Wachuna kuwaguguna wananchi na kisha kuwatupa wakiwa hindi lenye uvundo na kusahaulika. Hivyo, watu wakaacha kuchukuliwa kama binadamu ambao huweza kuhisi njaa, kuugua, kuburudika kufanya mapenzi na mengine mengi msingi na muhimu kwa maisha na uhai wa binadamu. Katika mataifa mengi barani Afrika mbinu hii ya kuwafanya watu fukara zaidi ya nusu wanyama hutumiwa sana na viongozi ambao huchaguliwa ili kuendeleza siasa za ulofa kwa kuwanyima watu

utu wao. Mazingira ya wananchi huchafuliwa kupitia utupaji taka ovyo kutoka kwa viwanda, ufyekaji misitu na uchomaji makaa, uchafuzi wa mito na bahari, na utoaji kaboni zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa na Shirika la Afya Ulimwenguni. Hili hufanikishwa na vingozi ambao huudidimiza utu wa wananchi.

Katama Mkangi anaendelea kudhihirisha kuwa binadamu ni aina ya anthroposenia kupitia utumwa wa kimawazo. Hili analifanikisha kupitia namna anavyomdhihirisha binadamu akizalisha maafa na ubaguzi wa kila hali. Kwa mfano, Medza alipokuwa akimsikia Tabu akikata roho mgongoni mwake na pia mwili wake Tabu kuanza kuganda kuliko barafu, Furaha mwanawe Chihenyo alikuwa anarejeshwa kwa mamake na daktari baada ya kutibiwa. Tofauti zinazodhihirika kati ya mapacha – Medza na Chihenyo – za kiuchumi na katika hali ya maisha kwa jumla ni zao la utumwa wa kimawazo na kiutawala. Hali hii inawiana na kauli ya Ellis (2018) kuwa, shughuli za binadamu za kiuchumi kama vile mabadiliko ya viwanda, katika utumwa wa kimawazo na utawala dhalimu, zimezalisha sio tu mabadiliko katika mifumo ya ulimwengu ila pia mabadiliko katika mifumo ya tamaduni za binadamu kimwavuli. Ingawa hili linafungamana na nguzo ya utamaduni na mazingira ina uhusiano na ugiligili wa karibu sana na nguzo ya uongozi mbaya. Hii ndiyo sababu mwandishi Mkangi anadhihirisha zao la utumwa wa kimawazo unaosababisha ubaguzi kwa kueleza kuwa, hatimaye, Furaha alihitimu na akawa daktari maarufu ilhali Tabu alisahaulika mara moja. Aidha, kaburi lake Tabu halikubainika pale lilipokuwa wala maeneo lililowahi kuwa.

Wawalenisi wanashikilia msimamo kuwa, binadamu kama aina ya anthroposenia huipalilia na kuiimarisha anthroposenia kupitia maamuzi yake mwenyewe ya kuuambaa uadilifu huku akipalilia utumwa wa kimawazo. Hivyo, wanasisitiza kuwa suala la ukosefu wa uadilifu kiuyakinifu si tukio la kuzaliwa au hata bahati mbaya ila ni zao la uhusiano wa kijamii unaodumishwa na sheria za utumwa wa kimawazo, na utumwa wa uongozi mbaya. Dzombo anafafanua kuwa, binadamu hupalilia na kuendeleza utumwa wa kimawazo kupitia njia tofautitofauti. Kwa mfano, kupitia elimu isiyo na usawa na haki, kaida zisizo za haki zinazosheheni ufisadi, maonevu na maangamizi ambazo kutokana na utumwa wa kimawazo, binadamu hufeli kuyadadisi masuala kwa njia ya haki, wazi na tena madhubuti kwa maisha bora ya binadamu. Hali hii inafungamana na nguzo ya uongozi mbaya ya nadharia ya Uhakikimazingira. Kupitia uchumi wa ubaguzi, utabaka na maonevu pamoja na siasa za ulaghai na

uharibifu wa mali ya umma, utumwa wa kimawazo na wa utawala unaendelea kupalilia anthroposenia katika maisha ya binadamu. Hili linawiana na kauli ya Ellis (2018) kuwa, baadhi ya madini ambayo hurutubisha anthroposenia ni elimu dhoofu, sheria zinazonyima haki badala ya kuzilinda, chumi zinazopalilia ubepari pamoja na siasa zinazopalilia ufukara na kudumisha utegemezi badala ya ujitegemezi kama zao la utumwa wa kimawazo.

Dzombo anaongeza kuwa, njia zingine anazotumia mwanadamu kuimarisha utumwa wa kimawazo ni mawasiliano potofu; hasa ya umma, maendeleo ya kudidimiza maendeleo; utamaduni ulionajisiwa na hivyo kukosa dhamira, imani, wala desturi; pamoja na uhusiano wa kinyama baina ya viongozi na wananchi wanaotawaliwa. Haya yote yanafanikishwa na utumwa wa kimawazo. Hili linafungamana na kauli ya Kobia (2007) na Maathai (2009) kuwa, mara nyingi katika mataifa fukara barani Afrika, uhusiano kati ya watawala na watawaliwa huwa ni wa chui na mbuzi, ambapo punde tu chui anapohisi njaa humla mbuzi hadi mkia. Katama Mkangi anazidi kusisitiza kuwa, uhusiano wa kinyama kati ya mke na mume, kati ya mnyonge na mwenye uwezo na kati ya binadamu na mazingira, hasa katika utumwa wa kimawazo, ni baadhi ya njia zinazorutubisha anthroposenia katika hulka za binadamu. Hali hii inafungamana na nguzo ya uongozi mbaya.

Utumwa wa kimawazo unamnyima binadamu uhuru wa kujieleza. Mathalani, mhusika Dubwasha katika *Mafuta* anadhihirisha hili kupitia kauli zake na tuhuma dhidi ya Ti na Mtue. Anawakumbusha kuwa kucheka hadharani, achilia mbali mahakamani ni jambo linalomlazimu mtu hata kama ni mteule kupewa ruhusa kwanza. Sheria hizi za utumwa zinapaliliwa na utumwa wa kimawazo. Dubwasha anathibitisha hili anapowauliza akina Ti na Mtue katika *Mafuta* kuwa, “Leo hii, nyinyi mwajicheka si mahakamani tu bali hadharani pia? Nyinyi nani ...?” (uk. 48). Binadamu anabuni sheria na masharti kali kutokana na utumwa wa kimawazo. Ingawa sheria zenyewe ni za kiutumwa zinapofusha binadamu dhidi ya udadisi wa mambo, ukweli na haki. Isitoshe, binadamu kutokana na utumwa wa kimawazo anazalisha utumwa wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ulimwenguni mwake. Mhusika Dubwasha anadhihirisha hili anapomkumbusha Ti kuwa kitendo cha kukilalia kitanda kinamfunga kwa kumtia pingu. Hili linafungamana na kauli ya Mwirabua (2014) na Nkonge (2014) kuwa, pingu zinaashiria kuta za utumwa, ulaghai, ujinga, ubinafsi, ufisadi, ubaguzi, uonevu na dhuluma za aina zote. Hali hii inafungamana na nguzo ya

uongozi mbaya ambapo wenye nguvu huwanyanyasa waduni pamoja na mazingira yao.

Hii ndiyo sababu, Dubwasha katika *Mafuta* anakariri kuwa, “Kucheka ... kitendo cha nadra sana na ... fursa rasmi tu kwa wateule na si kwa akina yakhe.” (uk. 48 – 9). Matajiri wanawadharau maskini kiwango kwamba ni wao pekee wanaoruhusiwa kucheka. Wachochole hawaruhusiwi kuuliza swali, kujibu chochote wala kutoa wazo lolote katika mazingira yanayotawaliwa na utumwa wa kimawazo. Kutokana na kosa la kucheka hadharani, Dubwasha anamhukumia kifo Mtue na kuondoka. Ukungu unaomficha baada ya uamuzi wake unathibitisha kuwa yeye anasawiri utumwa na mateso. Kama ilivyoelezwa awali, ukunge unaashiria giza, utumwa na dhiki chungu nzima. Mwandishi Mkangi anadhihirisha hali hii anapoeleza katika *Mafuta* kuwa, “Ukungu ulienea kwa haraka na kumficha alipomaliza kutoa hukumu aliyoiita haki.” (uk. 49). Chini ya udhibiti na utawala unaotawaliwa na kuongozwa na utumwa wa kimawazo, haki na ukweli hubatilishwa na kubatizwa kinyume. Hatimaye, baada ya hukumu, Mtue hata bila nafasi ya kumuaga Ti anamezwa na ukungu huku Ti akibwagwa nje kwenye jua kali na tarishi. Hali hii inadhihirisha ubaguzi na uonevu unaodhihirika paruwanja kama zao la utumwa wa kimawazo na utawala dhalimu. Hili linawiana na nguzo ya uongozi mbaya.

Dkt Matoga kwa usaidizi wa mganga wake, Mzee Makolokoza katika *Vipuli* anaendeleza utumwa wa kimawazo kupitia udhibiti wa akili na matashi ya Nyau, Kipanga na Shipe. Linalodhihirika ni kuwa utumwa wa kimawazo una uwezo wa kuiponda mishipa ya fahamu inayotangulia kutoka ndani ya ubongo na kutambaa kwa kufuata uti wa mgongo hadi tamati. Mzee Makolokoza katika *Vipuli*, anataja kuwa, “Huyo ndiye mtu. Huo ndio uhai wa mwanandamu.” (uk. 156). Hivyo basi, mintarafu ya usemi wa Mzee Makolokoza, utumwa wa kimawazo hushamiri pale uhai wa mwanadamu unapodhibitiwa katika misingi ya utumwa na ulemavu wa kimawazo. Udhibiti ule unarejelewa kama sanaa ya fahamu. Hatua ya kwanza na msingi inayotimiza utumwa wa kimawazo ili kumdhibiti mwanadamu ni kumfanya mtumwa wa chakula, hivi kwamba lazima maskini amtegemee tajiri ili kupata tonge. Hili likifanikiwa, tonge lenyewe hutiwa kemikali ili kumlewesha na kumpumbaza maskini. Hali hii inawiana na kauli ya Waithiru (2019) na Thiong’o (1987) kuwa, mataifa tajiri pamoja na mashirika ya kimataifa hudhibiti chumi duni za Afrika kupitia mikopo ya riba ya juu pamoja na kuwadhibiti viongozi vikaragosi ambao huendeleza

ulaguzi wa dawa za kulevya, pombe haramu na mbolea zenye kemikali sumu; pamoja na chakula cha misaada na hivyo kuyafanya mataifa haya duni yawe malemavu kiuchumi, kisiasa na kijamii kimwavuli. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo.

Hata hivyo, kwa jumla, ili binadamu afanikishe na kuendeleza utumwa wa kimawazo, hutawaliwa na ujinga kwanza. Mtunzi Mbogo analiweka hili bayana kupitia maelezo yake katika *Vipuli* kuwa, "Waafrika tunazo akili zetu. Tunayo maarifa sisi. Lakini wamekuja wageni, nasi kwa ujinga wetu, tumeacha utamaduni wetu na kukumbatia mambo tusiyoyajua asili wala maana." (uk. 157). Mtunzi Mbogo katika *Vipuli*, sawa na mwandishi Mkangi katika *Walenisi* wanashabihiana kuwa, ujinga huunawirisha utumwa wa kimawazo pakubwa. Hili humpelekea binadamu kupumbazika na kukosa kudadisi masuala kwa kina na makini. Kwa misingi hii hii, Magamba, Nyau na Kipanga wanadhihirisha utumwa wa kimawazo nyakati za mchana katika hospitali ya Lumumba. Wote wanasaidiana kulitwaa sanduku kubwa kutoka ndani ya mochware hadi kwenye gari lililopakiwa mlangoni. Sanduku lenyewe lina maiti za watu wazima sita na za watoto kadhaa. Ingawa baada ya kufungwa na kupakiwa kwenye gari linanyunyizwa mafuta ya kunukia, hali hii inaashiria hila na njama zinazokamafleji utumwa wa kimawazo ulimwenguni.

### 4.3 Mawakala wa Anthroposenia

#### i. Wanyama

Kwa kawaida mnyama ni kiumbe-hai ambaye huwa na miguu minne. Hata hivyo, katika utafiti huu, istilahi hii ilikuwa na dhana pana ambayo ilijumlisha wanyama wasio na miguu minne kama vile samaki; ambaye ni kiumbe wa majini aliye na mapezi na mkia ambavyo humwezesha kuogelea na mashavu yanayomwezesha kupumua akiwa majini (Wamitila, 2022; BAKITA, 2022; 2015; Mdee na wenzake, 2015; Mdee na wenzake, 2009). Mifugo katika kupalilia anthroposenia wanamega na kumeza takataka za kila aina zenye sumu nyingi na hatari kwao na kwa binadamu pia. Mathalani, mwandishi Mbogo anadhirisha hili katika *Bustani* anapotaja kuwa, "Nguruwe kama zilivyo tabia za uchafu na ulafi wa kula ovyo, walipendelea zile takataka zilizovunda." (uk. 25 – 26). Mhusika Jonalisti kutoka pale jaani, aliwaona ng'ombe, nguruwe na mbuzi wakila takataka za kila aina. Wanyama kama nguruwe, mbuzi na ng'ombe wanachangia ndwele na halafu wanazalisha maafa kama aina ya anthroposenia. Hili linafanikishwa na ukweli kuwa, baada ya wanyama hawa kubugia,

kutafuna na kumeza kemikali mbalimbali, wanachinjwa, na nyama ile ile iliyosheheni kemikali inauziwa watu wanaoila kwa bashasha. Hili linadhihirisha haja ya namna ambavyo binadamu huingiliana na mazingira yake na viumbe vilivyomo kutathminiwa katika misingi ya nguzo ya haki na maadili ya kimazingira.

Mtunzi Mbogo katika *Bustani* anaeleza kuwa, baada ya Jonalisti kupiga picha tatu ule mkono wa mtu waliouona pale kwenye lundo la pamba na mabendiji yaliyochanganyika na damu, akiwa na wale watu sita, aligeuka na kuondoka huku akikohoa. Alipokuwa akiondoka, aliwaona ng'ombe, mbuzi na nguruwe wameinama wakila na kutafuna takataka za kila aina bila kubagua. Nguruwe kwa mfano, walibugia na kumeza kwa ulafi takataka zilizovunda na kuozeana. Walitafuna na kumeza ovyo na walionekana kufurahia miozo ya mabaki ya nyama iliyotoa mijifunza mikubwa, matambara ya sodo pamoja na mizoga ya watoto walioingia duniani kabla ya wakati wao. Hivyo, katika kupalilia anthroposenia, wanyama, hasa mifugo ni maajenti wa kusambaza kemikali sumu kwa binadamu, ambazo hatimaye husababisha maradhi mbalimbali. Hili linawiana na nguzo ya haki na maadili ya kimazingira ambapo baada ya binadamu kuingiliana na kutagusana na mazingira yake kwa njia za kuyaharibu na kuyachafua hatimaye hujiponza mwenyewe kwa kuathirika na madhara ya mazingira dhoofu.

Kwa mfano, katika duka la nyama, mwuza nyama anadhihirisha kuwa nyama ya nguruwe inaliwa kwa kiwango kikubwa. Mama mmoja aliinunua nyama ile, kisha mtanashati mwingine alifungiwa nyama kilo tano ya nguruwe na maini kilo tatu halafu Jonalisti akakatiwa kilo moja, sehemu ya mkia iliyonona. Athari ya wanachokula wanyama na jinsi kinavyoishia kuingia ndani ya mwili wa binadamu inawekwa bayana kupitia mawazo ya Jonalisti. Pale kwenye duka la nyama, inapowadia zamu ya Jonalisti kukatiwa nyama, anasita kidogo na kuwaza. Mwandishi anafafanua kuwa, ndani ya mawazo ya Jonalisti, kanda ya video ilizunguka taratibu naye akaona ng'ombe na nguruwe huku mapua na midomo imebenjuka wazi; wakikoroma na wakila kwa pupa vyakula vilivyoozeshwa kwa mabaki ya taka za sumu zilizomwagwa na wafanyakazi wa Sagasaga Chemical Industry. Aidha, Jonalisti aliutazama mguu na nyama ya ng'ombe lakini kwenye mawazo yake aliona ukigeuka na kuwa mkono wa binadamu wenye vidole vitatu. Ingawa haya yalikuwa yanatokea ubongoni mwake, ukweli ni kwamba yalikuwa yametokea katika nyakati tofautitofauti ile siku, pale kwenye dampu la Siza. Hivyo, uhalisia ni kuwa katika

anthroposenia watu wanaokula nyama ya mifugo wanakula madini na kemikali chungu nzima. Athari ya kemikali hizi inadhihirika kupitia maradhi hatari wanayougua binadamu kila uchao.

Ndege ni neno linalorejelea kiumbe mwenye mabawa na manyoya anayeruka angani, pia huitwa nyuni (TUKI, 2013; Mdee na wengine, 2015). Katika *Bustani*, ndege wanaonyeshwa kama mawakala wa anthroposenia kwa namna aina aina. Jonalisti alipokuwa akipiga picha pale jaani alitazama juu na kuwaona kunguru, tai, mwewe na kipanga wakielea hewani na minofu yao ya nyama. Katika kuendeleza anthroposenia ndege wanakula nyama ya binadamu, ya wanyama na pia ya ndege wenzao. Hili linadhihirika pale ndege wanaelea hewani na nyama za binadamu, wengine wakiwa na nyama za wanyama na wengine wakiwa na nyama za ndege wenzao. Ingawa haya ni matokeo ya shughuli za binadamu, ndege wanachangia pakubwa katika kuyasambaza maradhi na uchafuzi wa mazingira kwa kiwango kikubwa. Nyuni wanaodonoa kumbikumbi warukapo wanasawiri anthroposenia kupitia mataifa tajiri ya Uropa, Marekani, Ulaya na Magharibi ambayo huyanyonya mataifa fukara ya Afrika kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hali hii hupalilia anthroposenia zaidi kwa kuimarisha ulofa, utegemezi na uombaji uliogubikwa na unafiki wa maangamizi. Hivyo, wanyama wanasawiri na kuwakilisha uzoefu wao kama sehemu ya changamoto za kimaadili na ukosefu wa usawa katika mazingira yanayotawaliwa na uonevu na machukizo. Kiuyakinifu, hali hii inashabihiana na mhimili wa uwezo ambao huyasawiri mataifa yenye uwezo yakiyadhulumu yale duni kwa kila hali ulimwenguni kote. Mhimili huu pamoja na ule wa maumbile ndiyo iliyoongoza uchunguzi wa wanyama kama aina ya anthroposenia.

### ii. Wadudu

Wadudu ni viumbe wadogo walio na miguu sita kwa kila mmoja, ambao huruka kwa kutumia mabawa au wanaotambaa (BAKITA, 2022; Wamitila, 2022; Mdee na wengine, 2015; Ndalu na wengine, 2014; TUKI, 2014). Mabadiliko katoka idadi ya wadudu huweza kudhihirisha mabadiliko katika afya ya mazingira kwa jumla. Upungufu au mabadiliko ya wadudu huashiria ukosefu wa usawa katika mifumo ya ikolojia kama zao la shughuli za binadamu. Wadudu hutoa huduma muhimu katika mfumo wa ikolojia kama vile uchavushaji wa maua, kuoza kwa vitu na udhibiti wa

wadudu waharibifu. Nafasi zao katika mchakato huu huchangia kwa ujumla kwenye utendaji na imara wa mifumo ya ikolojia.

Mwandishi Mbogo anadhihirisha kuwa, ingawa aina tofautitofauti za anthroposenia hukamilishana na kuchangiana kupitia njia mbalimbali, wakati mwingine hufarakana kabisa. Binadamu ambaye ni aina ya anthroposenia anahitilafiana na wadudu. Kwa mfano, Doricas katika *Bustani* anamwogopa mende na wanazozana pale chumbani. Hata hivyo, uhusiano kati ya mende na binadamu ni wa maonevu, kwa sababu ingawa mende hunufaika kutokana na uchafuzi wa binadamu, binadamu hukirihika na uwepo wa mende. Bila binadamu kuchafua mazingira mende hangepata kuishi maadamu yeye hutegemea uchafu ule kama lishe yake bora. Hivyo, wote wanapalilia anthroposenia kupitia uchafuzi wa mazingira. Doricas anamwangamiza mende, si kwa sababu ya kunuia kudhibiti uchafuzi wa mazingira ila ni kutokana na woga. Hili linadhihirika pale ambapo mende mkubwa wa kahawia anapomtambaa mguuni huku akielekea kwa paja. Doricas anapiga ukelele na kuusuka mguu wake. Mende badala ya kuanguka anaruka kwa mbawa zake na kutua barabara kwenye pua lake. Inambidi Doricas ajipanguse uso na kumrusha mende juu ya sanduku na kisha kwa kutumia ndala, akamgonga mende na kumwangamiza.

Kutokana na umwagaji taka ovyo na maingiliano yasiyo na uwajibikaji kati ya binadamu na mazingira yake, wadudu wanaoudhi binadamu wananawiri kutokana na uchafuzi wa mazingira. Doricas anajaribu kumwangamiza mende anayeking’ong’osa na kukichezea kidonda cha mwanawe kichwani bila mafanikio. Doricas anaapa kusaka mbinu za kuwaangamiza mende. Hili linadhihirisha kuwa binadamu na wadudu kama aina za anthroposenia hawatangamani na wanazozana, hata kama mchango wao katika kukuza na kuendeleza uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni sawa. Nzi na wadudu wengine wanashamiri katika harakati za kuendeleza na kukuza uchafuzi wa mazingira. Mtunzi Mbogo anadhihirisha hili katika *Bustani* anapoeleza kuwa, “Nzi wawili wakubwa walitua juu ya hilo donda na kunyonya usaha. Kisha waliruka wakatua juu ya futa la kamasi lililokuwa juu ya kifua cha mtoto aliyekuwa anapiga Franco.” (uk. 24). Mwandishi Mbogo anafafanua kuwa wadudu hawajasazwa katika kuendeleza uchafuzi wa mazingira na vilivyomo. Ingawa wadudu husaidia pakubwa katika uzalishaji wa mimea na maua katika harakati za kuendeleza uchafuzi wa mazingira wanaangamizwa ulimwenguni kote.

Kwa mfano, Baba Adamu anaeleza kuwa, “Wadudu kama vipepeo, panzi, nyuki ... walionekana kwa pamoja kati na ndani ya Bustani ile ...” (uk. 37). Wadudu hawa hawapo tena kutokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Kutokana na matumizi ya kemikali kali na sumu katika dawa zinazonyunyiziwa mimea na binadamu, wadudu wanaangamia. Kupitia mhusika Baba Adamu, mwandishi anasikitika kuwa, kutokana na uharibifu wa mazingira maumbile kama vile miti iliyokuwa ikileta hewa safi na iliyokuwa ikizaa; matunda, maua, mito na maziwa pia, hayapo tena. Mwandishi Mbogo anawasawiri wadudu kama wakala ya uharibifu wa mazingira, hasa kupitia uwezo wao wa kueneza viini vya virusi ila si ule wa kusaidia usambazaji wa chavuo za mimea mbalimbali katika harakati za uzalishaji mimea tofautitofauti.

Katama Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* anadhihirisha kuwa, binadamu, siafu, na nyuki wanafanana katika jitihada zao za kuchangia vurugu dhidi ya mazingira. Mwandishi anawasawiri wadudu kama ajenti wa uharibifu wa mazingira ambapo shughuli zao zinachangia mabadiliko makuu katika mazingira ya binadamu na ulimwenguni kwa jumla. Wafanyakazi pale kiwandani wanasisitiza ya kwamba tofauti za kijamii na asili zao zipo kwenye sheria za kimaumbile. Hakika sheria hizi hudumisha ulofa, utabaka na utumwa baina ya wanadamu na wanyama mtawalia kwa kuzingatia msingi wao kuwa, baadhi ya binadamu na wanyama wanaishi maisha yenye afya, usalama na furaha kuu; huku wengine wakiishi kwa kubahatika kupata tone la maji au hata kopo la uji. Dzombo anathibitisha hili katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, juhudi za nyuki na siafu zinamkumbusha kuhusu juhudi za wanyonge katika kujitafutia riziki na kuwafurahisha matajiri duniani ambapo mazingira hunajisiwa bila kujali kwa lengo la kuwafurahisha wakwasi. Mmoja wa wafanyakazi mle kiwandani katika *Walenisi* anaeleza kuwa, “Wachuna walikuwa hawaachi kusisitiza kuwa jamii za binadamu, siafu na nyuki zinafanana.” (uk. 102). Ulinganishi huu wa moja kwa moja unaashiria sifa sawia kati ya utabaka, ubaguzi na dhuluma kati ya watu na nyuki sambamba. Katika mataifa mengi, hususani ya Afrika, utawala, serikali na maskini hujitahidi kuwafurahisha na kuwapendeza matajiri kwa kiwango kikubwa. Hili husababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika harakati za kuwatajirisha matajiri zaidi kama vile kunyunyizia mimea dawa zisizokubalika kwa afya ya binadamu na hewa, uchomaji makaa ovyo, mmomonyoko wa udongo, ongezeko la asidi kwenye mchanga pamoja na ujenzi wa viwanda vya kemikali sumu bila kuwajali wafanyakazi, mazingira yao wala madhara ya kudumu kwa wenyeji. Sklair (2022)

anadokeza kuwa, katika jitihada za kupata uwekezaji, baadhi ya mataifa fukara huweza kujihusisha na mazoea yanayochangia uharibifu na uchafuzi wa mazingira, kama vile kuwa na sheria dhaifu za ulinzi wa mazingira, usimamizi na udhibiti dhoofu wa taka, viwanda bila mazoea endelevu pamoja na uchimbaji mkubwa wa rasilimali asilia.

Ikumbukwe kwamba, Wachuna wanaashiria unajisi wa mazingira na utu katika mazingira ya *Sayari* ya akina Mtu-Bint Fikirini. Uhusiano wa binadamu, siafu na nyuki umejikita katika misingi ya uharibifu, maonevu na ubaguzi. Kwa mfano, mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anafafanua kuwa, "... msafara wa siafu ulikuwa ukipita na nyuki wakifyonza asali kutoka katika maua ya mihepe na mishomoro." (uk. 102). Mtu-Bint Fikirini anasisitiza kuwa, Wachuna waliendeleza na kudumisha ubaguzi na manyanyaso enzi yao kwa kutumia uhusiano wa kizandiki, dhuluma na unyanyasaji mkubwa baina ya jamii za binadamu, siafu na nyuki.

Kumbikumbi ni wadudu kama siafu wakubwa wanaoota mbawa kwa muda mfupi tu wakati wa mvua nyingi (BAKITA, 2022). Katama Mkangi anawatumia kumbikumbi kusawiri utabaka na ubaguzi kati ya chumi duni na chumi imara katika riwaya ya *Mafuta*. Kumbikumbi wanadhihirisha chumi duni, ubaguzi na mifumo dhaifu ya utawala, kijamii na kisiasa. Kwa misingi hii, mbawa za kumbikumbi zinathibitisha chumi na mifumo hafifu na dhaifu. Mama Fofi anadhihirisha hali hii anapotaja kuwa, "... mbawa za kumbikumbi zilivyo hafifu na dhaifu." (uk. 31). Hali hii ni mithili ya ile inayosawiriwa na mwandishi Mbogo katika *Vipuli vya Figo* ambapo sungura anayeashiria chumi duni anakondolewa macho na kifo, pale chatu – anayeashiria chumi imara na kuu – anapomlenga shabaha tayari kumfanya kitoweo chake, sawa na vile mataifa tajiri ya Ughaibuni huyanyonyoa mataifa ya Afrika rasilimali asilia, madini, pamoja na wafanyakazi kwa lengo la kuyanufaisha yao pekee huku yakiyaharibu ya Afrika. Hali hii inafungamana moja kwa moja na mhimili wa uwezo wa nadharia ya uhakikimazingira iliyoongoza utafiti huu.

### 4.4 Matumizi ya Vifaa

Kifaa ni kitu chochote kinachotumika kwa ajili ya kufanyia shughuli fulani (BAKITA, 2022; Wamitila, 2022; TUKI, 2006; 2013; 2014). Samsoni anaeleza kuwa, katika kiwanda cha kemikali cha *Saga Saga Chemical Industry*, vifaa vinavyotumiwa vinapalilia uharibifu na uchafuzi wa mazingira na hatimaye maangamizi. Wafanyikazi

walipokuwa wakiendelea na kazi wakidhani kuwa mambo yote yalikuwa shwari, bomba la gesi na jingine la asidi yalikuwa yanavuja kidogokidogo. Kwa mujibu wa Wamitila (2022), Mdee na wengine (2015), Ndalu na wengine (2014) na TUKI, (2014), gesi ni kitu kama hewa ambacho kikiwashwa huwaka na huweza kutumiwa kupikia au kwa shughuli nyingine. Kadhalika, wanaeleza kuwa tindikali ni kemikali chungu na kali. Samsoni katika *Bustani* anadokeza kuwa, hakufahamu lililosibu ila nati moja ilifyatuka na papo hapo mtambo ukafunguka. Punde tu baada ya nati kufyatuka gesi na asidi vikatoka kwa kishindo. Asidi huyeyusha viumbe vyenye uhai na visivyo hai. Mathalani, watu watatu katika kiwanda cha kemikali cha Saga Saga waliliwa ngozi na asidi miguuni. Watu wengine waliathirika kutokana na gesi. Ingawa waliosalia hawakupata majeraha makubwa, vikohozi na mafua viliwasomba wote. Hili ni zao la matumizi ya vifaa bila kuvitunza wala kuvifanyia marekebisho ya muda kwa muda. Utepetevu huu hutokana na kutafuta usawa kati ya maendeleo ya kiuchumi na uhifadhi wa mazingira. Ushirikiano wa kimataifa, mazoea ya maendeleo endelevu na uwekezaji wa kudumu vinaweza kusaidia kukabiliana na hatari ya matumizi mabaya ya vifaa katika mataifa ya ulimwengu wa tatu.

Doricas na Mama Mohamed walipoliacha daraja wakielekea hospitali ya serikali ya Wilaya ya Siza katika *Bustani*, walilikaribia jaa kuu la taka la Mji wa Siza. Upepo nao ulivuma kuelekea kwao na kuwapulizia harufu mbaya ambayo haikuvumilika. Kwa mujibu wa Tuki (2013; 2014), jaa ni mahali maalum palipotengwa kutupa taka. Wote wawili waliziba pua na midomo yao kwa kanga zao na wakaongeza mwendo kupotelea shombo. Matumizi mabaya ya vifaa kama vile jaa la taka yanachangia pakubwa kuchafua mazingira na kusababisha ufukara na nduli kwa binadamu na wanyama kwa jumla. Butler (2024) anasisitiza kuwa, matumizi mabaya ya mashine na teknolojia yanaweza kuchangia uchafuzi wa mazingira na maafa kupitia uzalishaji na uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa maji, uharibifu wa udongo, kelele, uzalishaji wa taka, uharibifu wa misitu na makazi, uzalishaji wa gesi chafuzi na kutumia rasilimali asilia kupita kiwango.

Uchafuzi wa mazingira kupitia matumizi mabaya ya vifaa husababisha ufukara, ukame kutokana na kiangazi na mvua ya asidi, maradhi kutokana na uchafuzi wa maeneo na hewa, na hatimaye maafa. Kwa mfano, Doricas na Mama Mohamed walipolikaribia jaa lile, waliwaona watu wa kila umri wakichakurachakura kwa lengo la kupata kipato chao cha siku. Hili linadhihirisha ufukara unaopaliliwa na utegemezi

wa taka na baadhi ya wananchi. Isitoshe, wanyama pia wanaokosa lishe wanageukia taka katika mazingira dhoofu kama lishe ya pekee. Mwandishi Mbogo anadhihirisha hali hii katika *Bustani* anapoeleza kuwa, "Ng'ombe, mbuzi na hasa nguruwe pia walikuwa wameinama wakifaidi takataka zile za chachu, za chumvichumvi, za ugwadu, za uchungu, zilizooza na kadhalika." (uk. 12). Hakika umaskini unaozalishwa na mazingira chafu unawaathiri wanadamu na wanyama mtawalia katika mataifa mengi fukara ulimwenguni. Hili linawiana na kauli ya Howarth (1996) na Slovic na wenzake (2020) kuwa, umaskini unaotokana na namna ambavyo binadamu huwa anatagusana na mazingira huweza kuchangia uchafuzi wa mazingira kupitia uchche katika upatikanaji wa teknolojia safi; ufyekaji wa miti; usimamizi duni wa taka; kuwa tegemezi kwa vyanzo vya nishati vinavyochafua; elimu finyu kuhusu mazingira; uzazi kwa mabadiliko ya tabianchi pamoja na ujenzi wa viwanda visivyo rasmi na vyenye uchafuzi.

Jaa la taka katika *Bustani* linatembelewa na watoto wanaoathirika kiafya na kijamii. Katika maeneo chafu, hususani barani Afrika watoto huwa mstari wa mbele wa kuathirika na maradhi, njaa na maafa kuliko watu wazima. Bergthaller na Horn (2020) wanasisitiza kuwa, watoto wanaoishi katika mazingira yaliyochafuliwa hukumbana na madhara aina aina kama vile; matatizo ya pumzi, maradhi yatokanayo na maji chafu na ya kuambukiza, ukosefu wa lishe bora, athari za mishipa, maendeleo duni ya kufikiri, huwa hatarini zaidi kwa mabadiliko ya tabianchi pamoja na upungufu na au ukosefu wa upatikanaji wa huduma za afya. Watoto wa miaka minane hivi wanabarizi uvundo wa jaa lile. Nguo zao zilikuwa chafu na zilizochakaa. Miili yao iliepuka maji kwa muda mrefu na kupelekea kupata uchafu. Mmoja wa vijana wale alikuwa na donda moja kichwani lililoonekana kutoa usaha na majimaji. Donda lenyewe lilikuwa na rangi ya zambarau. Uchafu waliookota mle jaani ulizorotesha hali zao za kiafya.

Mwenye kidonda kwa mfano, alishika chupa ya dawa mkononi mwake wa kulia na sindano za kutibia wagonjwa hospitali kwa ule wa kushoto. Kijana wa pili naye anatokwa na kamasi kila wakati na mwili wake unamwasha vikali. Kadhalika, alikuwa na maradhi ya kujikuna mwilini. Ndiposa alipangusa kamasi kwa mkono mmoja na wa pili akautumia kujikwangua kwa makucha yake meusi na marefu. Kwa wakati mmoja alijikuna ubavuni, kisha tumboni na kadhalika mgongoni, kichwa na sehemu zingine za mwili. Haya yalizalishwa na uchafu wa jaa la taka la Siza. Hivyo, ni vyema kupunguza athari za uchafuzi ili kuboresha ustawi wa watoto na mazingira

kwa kuboresha sheria za mazingira, kukuza vyanzo vya nishati safi, kutoa upatikanaji wa maji safi na huduma za kujisafi, kuboresha miundombinu ya afya na kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira kwa afya ya watoto.

Hata hivyo, ingawa wengi wanateseka kutokana na athari hasi za mazingira yenye uchafuzi kuna matajiri wanaotajirika zaidi. Mathalani, lile jaa la taka lilisheheni vinono, mabaki na mapochopocho yaliyooza na yenye kemikali sumu kwa binadamu lakini yaliyowafaa nguruwe pakubwa. Jonalisti anapoliangalia kundi la nguruwe likipiga mbio kuelekea katikati ya lile jaa la taka, anakiri kuwa walikuwa wachafu lakini walionona kupindukia. Tunaelezwa na mwandishi wa *Bustani* kuwa, "... hapa jaani nguruwe wamepata uhondo. Mwenyewe tajiri atajipatia fedha nyingi." (uk. 23). Hivyo kutokana na ubaguzi na utabaka matajiri hunufaika huku maskini wakiteseka na kuangamia. Quick (2004) na Garrard (2007; 2023) wanaongeza kuwa, wenye uwezo huyapujua mazingira zaidi kuliko wanyonge ulimwenguni hususani katika maeneo yanayotawaliwa na dhuluma za kila aina.

Kulingana na Jonalisti katika *Bustani*, katika gazeti la *New Era* anafafanua kuwa, kiwanda cha kemikali cha Sagasaga kinaendeleza uchafuzi na uharibifu wa mazingira na hatimaye maafa. Anapambanua kuwa, katika eneo la Siza mabati ya nyumba na mageti ya chuma yameliwa na yanaendelea kutobolewa kwa hewa ya sumu na mvua za asidi zinazotokana na kiwanda cha kemikali cha Sagasaga. Waithiru (2022a) anasisitiza kuwa, katika mataifa mengi barani Afrika, hali ya hewa imedorora na imesheheni huzuni, maradhi na maafa kutokana na kemikali nyingi hatari zinazoachiliwa hewani na viwanda visivyojali be wala te afya na uhai wa wanjamii. Ingawa mataifa mengi ulimwenguni hujiendeleza kupitia uvumbuzi na uzalishaji wa rasilimali katika viwanda, maendeleo haya huja kwa kuyagharimu mazingira uhai wao na hatimaye uhai wa binadamu ambao hufungamana moja kwa moja na mazingira hayo hukauka. Hali hii inafungamana na mhimili wa nadharia ya Uhakikimazingira ya maendeleo endelevu kwamba binadamu huyanajisi mazingira yake katika juhudi zake za kujiendeleza kiuchumi. Chandler na wenzake (2020) wanasisitiza kuwa, ukosefu wa usawa kati ya shughuli za maendeleo ya kiuchumi, uekezaji na uhifadhi wa mazingira ndilo tatizo kuu linalosababisha bonde pana na refu linaloendelea kuudidimiza ulimwengu katika mauaji ya mazingira yake kwa juhudi zake mwenyewe.

Ingawa mvua na matope huashiria shibe, amani na utulivu katika jamii,  Katama Mkangi amevitumia kuusawiri umaskini kutokana na uwezo wao wa kukwamiza na kuzorotesha chumi tofautitofauti ulimwenguni. Hiki ni kinyume na matarajio ya kawaida, ambapo binadamu hunufaika na mvua kwa kupata maji, mimea kunawiri na hivyo chakula kupatikana kwa wingi. Wanyama nao hupata majani ya kutosha na hili huimarisha usawa katika kiwango cha wanyama katika ikolojia. Hili linafungamana na mhimili wa maumbile ambao husisitiza haja ya urari kati ya hali za kimaumbile (Nayar, 2010). Kwa mujibu wa mtunzi Mkangi kupitia mhusika mama Fofi, maumbile yanapalilia ulofa kutokana na athari za shughuli za kila siku za binadamu. Kwa mfano, anataja katika *Mafuta* kuwa, mvua na matope ni vikwazo vya kuzorotesha juhudi za binadamu za kukabiliana na ufukara. Binadamu anapopalilia na kuhifadhi mbawa za kumbikumbi ananuia kuziimarisha na hivyo kuimarisha uchumi wake, mifumo yake ya kijamii na kisiasa kimwavuli. Mama Fofi anasisitiza kuwa, mbawa zinazoanguka matopeni huzidi kunyeshewa na kupeperushwa matopeni na upepo unapovuma. Hili linaashiria athari za maumbile katika maisha ya binadamu zinazochangia ufukara. Mama Fofi anasisitiza katika *Mafuta* kuwa maumbile yalikuwa kizingiti katika jitihada za binadamu za kujiendeleza kiuchumi. (uk. 31).

Vyombo spesheli vinavyopatikana kwenye chumba cha kuhifadhi vipuli vya figo na mioyo kabla ya kusafirishwa Ughaibuni vinaashiria maangamizi kupitia dhima yavyo. Profesa Williams na Dkt Charles katika *Vipuli* wanadhihirisha hili kupitia kupendezwa kwao na namna vyombo vile spesheli vya kuhifadhia vipuli vilivyowekwa kwa ustadi. Hili linaashiria namna maafa hufanikishwa na kupaliliwa kwa vifaa. Mathalani, baada ya kujaribu swichi moja ya chombo kimojayacho cha vyombo vile, wote wanafurahishwa na namna chombo chenyewe kinadhihirisha nyuzi zinazotakiwa kwa uhifadhi bora wa vipuli. Ubora huu unahakikishwa na zebaki inayopanda kwenye glasi nyembamba kisha inasimama sambamba na mshale wa mita unaoashiria nyuzi mwafaka za joto kwenye chombo kile.

Ingawa kifaa hiki ni zao la uvumbuzi wa binadamu, kinaashiria juhudi za binadamu za kupalilia maafa na kujifaidi na vifo vya wenzake kupitia jukumu kinachotekeleza, sio tu kwa mwanadamu mwenye kukitengeneza ila pia kwa mazingira yanayokizingira. Hili linawiana na mhimili wa binadamu dhidi ya maumbile. Hakika, mashine na mitambo aina aina huzalisha vichafuzi vya hewa kama vile, oksidi za nitrojeni, kaboni na chembechembe. Hili husababisha uchafuzi wa hewa na

mabadiliko ya hali ya hewa. Ingawa binadamu amepiga hatua katika uvumbuzi wa mashine mbalimbali, mna haja ya kupunguza athari za mazingira zinazosababishwa na mashine kwa kuanzisha teknolojia safi, kukuza mazoea endelevu na kuelekea vyanzo vya nishati mbadala. Kanuni kali mazingira na kampeni za kuwahamasisha watu kuhusu haja ya uhifadhi wa mazingira ni muhimu.

### 4.4.1 Fedha

Fedha ni nomino ambayo hurejelea madini ya rangi ya bati (Wamitila, 2022; TUKI, 2014; Mdee na wengine, 2015) ambayo hurejelewa pia kama; sarafu, pesa, fulusi, dirhamu, faranga au hata ndarama (Ndalu na wengine, 2014; BAKITA, 2022), kutegemea mazingira na matumizi ya lugha ya eneo husika pamoja na wenyeji wao. Pia huweza kurejelea midia ya kubadilishana huduma au bidhaa inayokubalika na sheria. Fedha katika *Bustani* ni kifaa kinachotumiwa na binadamu ambacho kando na kusawiriwa kama aina ya anthroposenia kinafadhili aina zingine kadhaa za anthroposenia. Kutokana na fedha, Bwana Abdula katika *Bustani* ananunua sigara zinazopelekea uzorotaji wa afya ya Zaituni. Ingawa Zaituni ni taashira ya wanajamii wanaoathirika kiafya na hewa chafu anafaidi uchafuzi wa hewa na mazingira kwa ujumla kwa mpigo huo huo. Mathalani, anaishi bila ufukara na anazalia Bwana Abdula watoto sita ambao baadhi yao wanachangia uchafuzi na uharibifu wa mazingira, kama vile Lyakati anayetumia sheria kuuendeleza na kuulinda.

Kutokana na fedha, Dkt Silika anamhakikishia Bwana Abdula kuwa hamkuwa na la kumshtua hata kabla ya kumpima Zaituni na kupata matokeo. Anataja katika *Bustani* kuwa, "*In any case, you don't have to worry very much*." (uk. 46). Dawa za usingizi anazotumia Zaituni ili alale hadi asubuhi zinanunuliwa kwa kutumia fedha. Tumbaku itokanayo na sigara avutazo Bwana Abdula hugharimu fedha. Ikumbukwe kwamba, tumbaku inachangia uchafuzi wa mazingira pakubwa. Zaituni anaeleza kuwa, mumewe alipoinama kumbusu shavuni aliihisi harufu ya tumbaku aliyoizoea. Hili linaonyesha kuwa fedha zinapalilia uchafuzi na uharibifu sio tu wa mazingira ila wa afya ya binadamu kila wakati. Ndiposa Zaituni anaeleza kuwa alikuwa ameizoea ile harufu ya tumbaku. Hakika fedha huchangia pakubwa katika uchafuzi wa mazingira kupitia njia mbalimbali. Kwa mfano, viwanda vinavyolenga faida vinaweza kuweka kipaumbele kwa kupunguza gharama kuliko kuzingatia mazoea mwafaka na ya manufaa kwa mazingira. Hata hivyo, matumizi yenye dhamana ya rasilimali za kifedha yanaweza kusaidia mazoea endelevu na miradi ya kupunguza uchafuzi.

Aidha, vita dhidi ya uchafuzi wa mazingira vinatingwa na kukwamizwa na fedha. Mathalani, Bwana Abdula anaeleza katika *Bustani* kuwa vita vya kwanza dhidi ya watu walioupinga ujenzi wa kiwanda cha Sagasaga pale Siza vilididimizwa kwa kutumia fedha. Baadhi ya viongozi wa siasa, wananchi pamoja na viongozi wa dini walipinga ujenzi ule na walipiga kelele kweli. Hata hivyo, fedha zilipotumiwa katika mazingira ambamo uongozi na utawala mbovu ulishamiri, tamaa na ubinafsi-uchoyo yaliimarika na kudhihirika kupitia ujenzi wa kiwanda kile cha kemikali cha Sagasaga. Kelele za wale viongozi zilikuwa bure kwa sababu fedha zilizizima mara moja. Mtunzi Mbogo anafafanua katika *Bustani* kuwa, "Adui zake walitumia maneno, naye Bwana Abdula akayajibu mapigo hayo kwa silaha yake ya fedha. Aliuzoea msemo wake maarufu: 'penye udhia, penyeza rupia'. (uk. 47). Bwana Abdula alielewa fika kuwa fedha zilikuwa na uwezo wa kubatilisha haki na kutoa leseni hadi pasipofaa na hivyo kupalilia unajisi wa mazingira na maadili ya binadamu. Katika mataifa mengi fukara barani Afrika, matajiri huchangia uchafuzi wa mazingira kwa kuwekeza kwenye viwanda na biashara zinazoweka faida mbele ya ustawi wa mazingira.

Mhusika Bwana Abdula anaeleza kuwa tatizo na udhaifu wa viongozi waliokuwa na madaraka ya kutoa leseni lilikuwa la kutatuliwa kwa fedha. Aidha, vurugu dhidi ya mazingira linafadhiliwa na kupaliliwa na fedha. Kujengwa kwa kiwanda cha kemikali kulizalisha vurugu dhidi ya mazingira na ndiposa baadhi ya viongozi wa siasa, wananchi na viongozi wa dini walikuwa wanapinga ujenzi ule. Fedha huweza kutumiwa kukemea ufukara. Hata hivyo, tamaa, ubinafsi na ufisadi husababisha uzalishaji na uhifadhi wa mazingira chafu. Uchafuzi na uharibifu wa mazingira hushamiri sana katika mazingira yenye utajiri na yanayotawaliwa na umaskini ingawa hukita mizizi zaidi katika yale yanayodhibitiwa na ulofa na athari zake huwa kubwa na hasi dhidi ya wanajamii hohehahe. Wanasiasa na viongozi wengi barani Afrika hukulia katika mazingira ya kimaskini na hili hupelekea wengi wao kuwa na tamaa ya utajiri. Katika hali hii mazingira hunajisiwa pakubwa.

Bwana Abdula alipojua kamati ya kutoa leseni alijibidiisha na kubaini tatizo lililomsumbua kila mmoja au kilichompendeza sana kila mwanakamati. Mathalani, alifanya utafiti na kutambua kuwa mwenyekiti wa kamati ya kutia leseni alikuwa na mradi wa ujenzi wa nyumba ya ghorofa moja lakini alikuwa amekwama kutokana na upungufu wa fedha. Aidha, viongozi wenye ubinafsi, tamaa na ufisadi barani Afrika mara nyingi huchangia uchafuzi wa mazingira kwa kutoa kipaumbele kwa faida

binafsi badala ya sera endelevu. Huweza kutoa leseni kwa viwanda vinavyozalisha uharibifu na uchafuzi wa mazingira kufanya kazi bila kanuni za kutosha. Hivyo, viwanda hivi kutokana na fedha nyingi husababisha uchafuzi wa hewa, maji na ardhi, ukichochea athari kwa mazingira na afya ya jamii. Kutatua matatizo haya kunahitaji kuimarisha utawala wenye uwajibikaji na kukuza sera zinazothamini mazingira.

Bwana Abdula alitumia upungufu ule na kujaza lori tatu za matofali na kuyamwaga kwenye uwanja wa nyumba aliyokuwa anajenga mwenyekiti wa kamati ya kutoa leseni na kabla ya jua kutua siku ile, Bwana Abdula alikuwa na leseni. Kwa upande mwingine aliwatafutia watoto wa ujumbe ufadhili wa masomo na wengine aliwapatia fedha taslimu na haya yalitosha kumpa leseni. Hili linaashiria kuwa mazingira chafu hushamiri katika mazingira yenye ulofa na waduni na hasa sana katika uongozi mbaya. Uongozi mbaya ni mojayazo ya nguzo zilizoongoza utafiti huu. Fedha nazo kama ala zinatumika kupalilia na kunawirisha uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika mataifa tofautitofauti barani Afrika. Kwa kuongozwa na mhimili wa uwezo katika uchunguzi wa aina za anthroposenia, fedha zilidhihirika kama kifaa kinachotumiwa na mataifa yenye uwezo kuyadhibiti na kuyatumikisha yale duni, hasa ya Afrika kwa kufifisha thamana ya sarafu yao ili yaendelee kuyatumikia yale kwasi ambayo sarafu yao huwa ya dhamana ya juu zaidi kila wakati. Utawala huu wa sarafu hupelekea utawala wa viongozi wa Afrika kutoka kwa wale wa Ughaibuni katika istilahi ya kitafsida ya utandawazi. Vilevile utandawazi ni mojayazo ya nguzo zilizoongoza uchunguzi wa data ya vifaa kama aina ya anthroposenia.

### 4.5 Vurugu Dhidi ya Mazingira na Binadamu

Vurugu dhidi ya mazingira ni dhana inayorejelea mvutano baina ya wanajamii dhidi ya rasilimali asilia; sera za kimazingira ambazo huzalisha vita baina ya wanajamii; vita dhidi ya binadamu kutoka kwa ulimwengu asilia kutokana na uharibifu wa mazingira na wanajamii na pia uharibifu wa moja kwa moja wa mazingira na wanajamii ambao hutishia uhai wao na maisha yao na ya viumbe wengine kwa jumla (TYM). Hivyo, vurugu dhidi ya mazingira ni dhana pana. Hata hivyo, kama ilivyofafanuliwa katika sehemu hii, ni dhana inayohusisha vita baina ya watu wakizozania rasilimali asilia; sera za kiikolojia zinazoweza kuwa na mgogoro kati yazo na wanadamu na vita vya kisekondari kutoka kwa ulimwengu asilia kama zao la uharibifu wa dunia na binadamu. Kupitia magazeti, mwandishi katika *Bustani*

anaeleza kuwa, vurugu dhidi ya mazingira inadhihirika katika Vita Vya Ghuba. Ikizingatiwa kwamba vurugu dhidi ya mazingira hupalili uharibifu wa mazingira hakafu maangamizi, basi ni bayana kuwa uharibifu wa mazingira na maafa yanashamiri jinsi Vita Vya Ghuba vinavyoendelea kuchacha.

Mathalani, kila siku magazeti yalitoa uzito kwa Vita Vya Ghuba na hasa sana kuhusu visima vingi vya mafuta vilivyokuwa vinawaka moto. Kadhalika, iliripotiwa kuwa, mamilioni kwa mabilioni ya mapipa ya mafuta yalikuwa yanatiririka kila uchao na kutumbukia kwenye Bahari ya Shamu na Bahari ya Hindi. Hili linadhihirisha kuwa, vita hupalilia uchafuzi wa hewa na maji kupitia vurugu dhidi ya mazingira. Kwa mfano, magazeti katika *Bustani* yanaeleza kuwa, "Iliripotiwa kuwa samaki, viumbe wengine na mimea ya majini vilikuwa vimeathirika vibaya sana." (uk. 72). Hili linadhihirishwa na mtaalamu mmoja wa masuala ya hali ya hewa anapofafanua kuwa, hewa ilikuwa inachafuliwa kiwango kwamba ilikuwa inaathiri afya za watu kwa njia tofautitofauti hasi kuanzia nchi za Ghuba hadi mataifa yote barani Afrika. Hili linafungamana na nguzo mojawapo ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya uwezo ambayo hudokeza kuwa, mataifa tajiri yenye uwezo hueneza uchafuzi wa mazingira katika mataifa fukara yasiyojiweza ya Afrika. Nguzo hii ya uwezo inadhihirika pale ambapo mataifa tajiri kama Ghuba yanazalisha uchafuzi wa hewa lakini badala ya yao yenyewe kuathirika bara zima la Afrika linaathirika.

Halikadhalika, mtaalamu anaendelea kudandavua katika *Bustani* kuwa, baa la njaa lingeendelea kushamiri barani Afrika kutokana na kubadilisha mwelekeo kwa mawingu na pepo ziletazo mvua. Hapa anadhihirisha nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile na ile ya uwezo ambapo Vita Vya Ghuba vinaathiri hadi kiwango cha mvua barani Afrika kiwango kwamba njaa na hatimaye maafa vinashamiri, kama zao la uchafuzi wa hewa. Hakika, uchafuzi wa hewa unachangia sana maafa kwa kiwango cha dunia. Ongezeko la uzalishaji wa gesi chafu kutokana na shughuli za kibinadamu, kama vile kuchoma mafuta ya visukuku na michakato ya viwanda, limeleta mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la joto duniani. Haya, kwa upande mwingine, yana athari kubwa kwenye mfumo wa ikolojia, mienendo ya hali ya hewa na viwango vya bahari.

Gazeti la *New Era* la Kiswahili na la Kiingereza linalototolewa na Jonalisti linadhihirisha vurugu dhidi ya mazingira, hasa kwenye bahari. Mathalani, la

Kiingereza limeandikwa katika *Bustani* kuwa, "OIL IN GULF WAR CAUSES ERNOMOUS POLLUTION IN RED SEA AND INDIAN OCEAN/VITA VYA GHUBA." (uk. 73). Nalo la Kiswahili katika *Bustani* limeandikwa kuwa, "MAFUTA YAFANYA UHARIBIFU MKUBWA WA MAZINGIRA." (uk. 73). Kwa mujibu wa maelezo katika gazeti hili, inabainikia kuwa vurugu dhidi ya mazingira huathiri viumbe vilivyo hai na maumbile kwa jumla. Pasta Yona katika *Bustani* analalamika kuwa, ingawa kwa upande mmoja, wao wanapigana na Cel ilhali Ghuba wanapigana na uchafuzi wa mazingira, mataifa yote husika yanajitahidi kukabiliana na uchafuzi wa mazingira katika janibu zao. Hili linadhihirisha kuwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira hushamiri katika maeneo yenye vita dhidi ya mazingira. Pasta Yona anahuzunika katika *Bustani* anapotaja kuwa, "Haya tazama; wakati sisi tunapigana na Cel huko Ghuba uchafuzi wa mazingira ni wa kutisha zaidi." (uk. 73). Hakika, uchafuzi wa mazingira, hususan wa hewa unatishia moja kwa moja siha ya binadamu, kusababisha maradhi ya kupumua na matatizo mengine ya kiafya. Uvurugaji wa ubora wa hewa unaunganishwa na vipengele mbalimbali vya anthroposenia, ikiw ni pamoja na miji kuongezeka, viwanda kuendelea na matumizi makubwa ya nishati.

Pasta Yona wa Yona anawakumbusha waumini pale kanisani kuwa vita baina ya wanadamu huzalisha vita dhidi ya mazingira. Anasema kuwa, vita vya Ghuba vimesababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira kupita umwagaji wa mafuta ovyo. Anafafanua kuwa wataalamu duniani kote wanakutana ili waone namna watakavyouzuia uharibifu ule na kuulemaza. Uharibifu unaorejelewa unazalisha na kupalilia maafa ulimwenguni. Ingawa ananena kwa sauti ya kicheko anadhihaki yanayoendelea pale Siza yanayochangia maangamizi kwa kiwango kikubwa. Baada ya kimya kidogo katika *Bustani* anasema kuwa, "Na hapa kwetu Siza tukisema. Jamaniee tunaumiaa! Jamaniee hapa magesi ya kemikali ya Cel yanatuumiza: tunapiga chafya, tunapiga magita kama Franco!" (uk. 76). Pasta Yona anadhihirisha kuwa mazingira chafu, kwa jumla yanasababisha maumivu, manyanyaso na dhiki baina ya wanajamii kwa kusababisha maradhi ya kupiga chafya na yale ya kujikuna na hatimaye kutokwa na upele. Zaidi ya hayo, anatoa mifano zaidi kuhusu athari hasi za hewa chafu kama zao la vurugu dhidi ya mazingira, kama vile, watu kuota mapele na vidonda. Kimsingi, mchango wa uchafuzi wa hewa unazidisha maafa kwa kushawishi mabadiliko ya hali ya hewa, kuvuruga mifumo ya ikolojia na kuleta hatari za kiafya kwa kiwango cha dunia.

Kwa misingi hii hii, hewa chafu inasababisha watu kujikuna kwa watu kama vingedere. Kutokana na uongozi mbaya, viongozi kama vile waziri wa viwanda anadidimiza vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kimwavuli kwa kuzalisha vurugu dhidi ya mazingira. Hali hii inafungamana na nguzo ya Uhakikimazingira ya uongozi mbaya ambao hupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya viumbe hai na visivyohai ulimwenguni. Waziri katika *Bustani* anafanikisha hili kupitia kutoa ripoti ya uongo kuhusu hali ya uhifadhi wa mazingira katika eneo la Nomila na hasa sana la Siza. Kadhalika, anawanyamazisha wananchi wazalendo wanaofifisha vurugu dhidi ya mazingira pia anawaita wachochezi ilhali maandamano yao ni mbinu kabambe ya kukabiliana na hulka za uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Kushughulikia changamoto zinazotokana na uchafuzi wa hewa katika muktadha wa anthroposenia kunahitaji njia anuwai aina aina. Kuweka na kutekeleza sheria kali za mazingira ili kudhibiti uzalishaji, kuhamasisha matumizi ya vyanzo vya nishati endelevu na mazoea endelevu katika viwanda ni hatua muhimu. Baadhi ya njia mwafaka na madhubuti za kukabiliana na ukatili wa mazingira ni pamoja na matumizi bora ya ralimali asilia, elimu ya mazingira, sera na sheria kali za mazingira, ulinzi wa bioanuai na ushirikishwaji wa jamii. Hili linawiana na kauli ya Head (2018) kuwa, binadamu anahitaji kuhakikisha suluhu endelevu na lenye usawa katika kukabiliana na unajisi wa mazingira.

## 4.6 Jiografia ya Binadamu

Jiografia ni leksia ambayo ilirejelea eneo analoishi binadamu kama aina ya anthroposenia katika makala haya. Jiografia ya binadamu inawakilisha janibu anazoishi na kuzitawala binadamu. Mihimili iliyoongoza uchunguzi wa jiografia ya binadamu kama mtaimbo endeshi wa anthroposenia ni pamoja na, kifo na uwezo, uongozi mbaya, maendeleo endelevu, na utandawazi. Uchanganuzi huu ulijikita katika vigezo vya shughuli za kiuchumi, uongozi na utawala dhalimu, utambulisho tepetevu na uchafuzi wa hewa.

### i. Shughuli za Kiuchumi

Katika jamii yoyote ile suala la uchumi huwa nyeti na muhimu sana katika maisha ya jamii. Shughuli za kiuchumi za jamii zinazofafanuliwa na watunzi wa riwaya nne teule za Kiswahili zilizotafitiwa katika makala haya zilidhihirisha madhara ya mazingira chafu kwa wanajamii wenyewe. Kwa mfano, katika janibu zinazopalilia mmomonyoko wa udongo wakulima wadogowadogo hulima kandokando ya barabara.

Kando na kuhatarisha maisha yao na wale wanaotumia barabara, wao hupumua hewa yenye gesi ya kaboni itokayo kwenye moshi wa magari yapitayo barabarani.

Kwa mfano, Bilali wakitoka jijini Nomila kuelekea Mji wa Siza katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* waliwapita wanawake na wanaume walioonekana wakivuna mahindi huku miili yao ikipigwa kwa manyunyu na ubaridi wa kipupwe kandokando ya barabara. Benzi lile linapishana na magari mengine mengi yanayopita kwa kasi kuelekea jijini Nomila. Kwa mujibu wa mwandishi Mbogo katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* kupitia mhusika Bwana Abdula pamoja na Mkurugenzi wa *The Trans-American Chemical Products* anadhihirisha kuwa, bara la Afrika ni eneo linalotumiwa na mataifa tajiri ya Marekani na Uropa kuendeleza na kukuza uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Mkurugenzi wa Trans-Chemi kama wanavyofupisha katika maongezi yao pamoja na Bwana Abdula anaeleza kuwa, matayarisho kabambe yalikuwa yamefanywa kabla ya Bwana Abdula kukijenga kiwanda kile cha kemikali cha Sagasaga. Hii ni idhibati tosha kuwa, kabla ya mataifa tajiri ya Marekani na Uropa kuyanajisi mazingira barani Afrika, Asia na Latini Amerika kupitia shughuli zao za kiuchumi huwa wanafanya utafiti kabambe. Utafiti huu huwahakikishia kuwa janibu hizi ni mwafaka kwa kupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla. Hali hii hufungamana na nguzo ya uwezo. Hakika mataifa tajiri huyatumia mazingira ya mataifa duni kwa manufaa yao huku yakiyapujua mazingira ya mataifa hayo kwa vipimo na viwango vya kiulimwengu.

Maeneo duni kama vile barani Afrika matajiri huekeza bila kuzingatia madhara ya bishara zao kwa wenyeji na mazingira ya Afrika. Kwa mfano, Mkurugenzi anafafanua kuwa, katika nchi za Afrika udhalimu, uchafuzi na uharibifu wa mazingira hushamiri kwa gharama ndogo na bila vikwazo vyovyote. Anataja kuwa faida ambayo wangeipata ingekuwa kubwa sana, hasa ikizingatiwa kuwa wangetumia fedha chache kuwalipa wafanyakazi bila kuzingatia sheria na itikadi za viwanda. Anadhihirisha hili anaposema katika *Bustani ya Edeni* kuwa, "*In fact*, kwa kutumia *cheap labour*, huko Afrika tutakuwa tunatengeneza fedha nyingi zaidi." (uk. 49). Katika nchi za Afrika hasa, serikali, uongozi na utawala huzembea na hutawaliwa na ubinafsi, tamaa, ufisadi na utowajibikaji na haya hupelekea kuumia kwa wananchi kutokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika maeneo yenye ulofa wa hali ya juu. Hali hii inalandana na nguzo ya uongozi mbaya. Ingawa inawiana na nguzo ya maendeleo

endelevu moja kwa moja, hatimaye inadidimiza maendeleo hayo kwa mkupuo mmoja.

### ii. Uongozi na Utawala Dhalimu

Uongozi na utawala dhalimu hushamiri sana katika janibu fukara zinazoongozwa na kutawaliwa kupitia mifumo ya udikteta na inayokiuka haki na usawa. Mataifa mengi barani Afrika huongozwa na kutawaliwa na viongozi ambao ni vikaragosi wa viongozi wa mataifa tajiri yenye uwezo. Kwa jumla, sehemu hii iliongozwa na nguzo ya uongozi mbaya ya nadharia ya Uhakikimazingira. Mkurugenzi wa *The Trans-American Chemical Products* katika *Bustani* anadhihirisha hili anapoeleza kuwa, "... serikali za kule viongozi wake bado wamelala. Si kama hapa kwetu. ... Hapa kwetu tunalazimika kufuata sheria zote za WHO ... *And that is damn expensive*." (uk. 49). Hili linadhihirisha kuwa viongozi wa mataifa tajiri ya Uropa, Marekani na kwingineko huwawajibikia na kuwasikitikia wananchi wao na hukemea kila mtu, kitu ama au hali inayoweza kuchangia uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Hii ni kwa sababu, katika mataifa haya tajiri, tofauti na yale fukara ya Afrika, waekezaji katika viwanda hubidiika kufuata sheria zote za Shirika la Afya Ulimwenguni kama vile, usalama wa wafanyakazi, bima zao, mishahara au malipo sawa na mikubwa bila ubaguzi, pamoja na kuweka mitambo maalum ya kuzuia ajali kwenye viwanda. Isitoshe, Mkurugenzi anaongeza kuwa katika janibu za Afrika, hamna sheria ambazo hufuatwa wala kuzingatiwa na hivyo kupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya Afrika kwa jumla. Anashikilia msimamo kuwa, faida inayoweza kupatikana katika mataifa fukara ya Afrika ni tele sana sana. Hakika ni tele lakini unajisi wa mazingira unakita mizizi na kushamiri kote kupitia uchafuzi na uharibifu wa mazingira wenye madhara ya kiwango na kipimo cha kiulimwengu.

Uongozi na utawala dhalimu hutoa leseni za ujenzi wa viwanda vya maangamizi kwa watu na mazingira yao. Mathalani, baada ya kamati ya kutoa leseni za ujenzi pale mjini Siza kutoa leseni ya ujenzi wa kiwanda cha *Sagasaga Chemical Industry* katika *Bustani*, walalahoi wachache waliopata fursa ya kupata ajira mle kiwandani waliumia na kuhatarisha maisha yao kutokana na ukosefu wa vifaa vya kujilinda wakipakia na kutayarisha kemikali aina aina. Mfano mwema ni pale Yusuf anapokutana na Jonalisti mle kiwandani, analalamika kuwa maisha yao kama wafanyakazi yalikuwa ya taabu na kazi yenyewe ilikuwa hatari. Alipotoa kofia yake ya kibaraghashia na kuinama, alimwonyesha Jonalisti vidonda alivyokuwa navyo kichwani na punde tu aliposikia

mtu akija alivaa tena kofia yake harakaharaka. Yusuf anamweleza Jonalisti katika *Bustani* kuwa, “Sisi wanyonge tunawategemea nyinyi vijana mliosoma. Hawa watu hawajali kutupa vifaa vinavyohitajika kwa usalama wetu dhidi ya madawa ya sumu.” (uk. 20). Hapa inadhihirika kuwa elimu bora ni ala nzuri ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira kutoka kwa viongozi, matajiri na wananchi mtawalia. Hakika hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo viongozi hupandisha gharama ya elimu hivi kwamba idadi kubwa ya wananchi hushindwa kumudu elimu msingi na hili huwafanya watu watumwa wa serikali na matajiri kwa jumla. Hii ndiyo sababu Yusuf anategemea Jonalisti aliyesoma kuwatetea kupitia gazeti.

Mkurugenzi wa Trans-Chemi anakiri kuwa nchi za Afrika, Asia, Latini Amerika na hata Urusi uongozi huwa hafifu na hupalilia uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Anasisitiza kuwa viongozi wa mataifa haya ni bure tu na hawana nia wala mikakati ya kufifisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Hili analidhihirisha paruwanja anapomweleza Bwana Abdula kuwa, “Hata huko tunaweza kufungua matawi ya Trans-Chem tukapata *super profits*.” (uk. 49). Aidha, alimsisitizia Bwana Abdula haja ya kukamilisha mipango yote ya ujenzi na upanuzi wa kiwanda cha kemikali cha Sagasaga. Bila tashwishi wala shauku katika sauti yake anamweleza Bwana Abdula katika *Bustani ya Edeni* kuwa, “Kama ana tatizo-*fax me any time*. Lakini Siza, kufuatana na ripoti ya wataalamu wangu, *is the best place*.” (uk. 49). Hivyo, kwa mujibu wa Mkurugenzi na wataalamu wake, mataifa ya Afrika, hasa mji wa Siza, ni eneo mwafaka la kukuza na kuendeleza uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla. Hali hii inawiana na kauli ya De Cristofaro na Cordle (2018) kuwa, anthroposenia hushamiri sana katika mataifa fukara ya Afrika kuliko mataifa tajiri ya Uropa, Japani, Ujerumani, Urusi na Marekani. Wasomi hawa wanaongeza kuwa, shughuli za kila siku za Waafrika na viongozi dhalimu ndizo zinazopalilia anthroposenia kila uchao.

Hata hivyo, ni vyema kutambua kuwa mielekeo na uelewa wetu Waafrika dhidi ya anthroposenia huchangia pakubwa ukuaji wa anthroposenia katika maeneo yetu, ambao hukiuka ukuaji katika maeneo mengi. Vita dhidi ya anthroposenia katika janibu za Afrika vinafeli na kugonga mwamba kutokana na ukweli kuwa, viongozi katika mataifa ya Afrika huwa vikaragosi vya mataifa tajiri ya Uropa, Marekani na mengine mengi, ambayo huzalisha na kulea sio tu uchafuzi na uharibifu wa mazingira ila pia mabadiliko hasi ya kudumu ya hali ya hewa na tabianchi. Kutokana na kunakili

utamaduni wa Mzungu na kuupuuza wa Waafrika, bara la Afrika linakosa kujitambua na hivyo kurutubisha anthroposenia. Uigaji bubu huu huchangia madhara ya tabianchi na mabadiliko ya hali ya hewa kama vile ongezeko la joto duniani, mafuriko, ukame, kuongezeka kwa nguvu na ukubwa wa dhoruba, kupotea kwa spishi za mimea na wanyama, kuharibika kwa mazingira ya bahari na mbadiliko ya mifumo ya ikolojia. Hili linawiana na kauli ya Head (2018) kuwa, madhara ya tabianchi na mabadiliko ya hali ya hewa huweza kusababisha madhara makubwa kwa afya ya binadamu, uchumi na mifumo ya ikolojia.

Katika janibu za Afrika sheria hutumiwa kupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira na kwa wakati huo huo kukabiliana nao. Kutokana na uongozi na utawala dhalimu, viongozi huratibu na kuhalalisha sheria za utumwa barani Afrika. Mara nyingi sheria hizi zinazotegemewa kuwalinda wananchi dhidi ya madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa huishia kuyapalilia, kuyakuza na kuyahifadhi madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa. Mathalani, katika kuendeleza uchafuzi wa mazingira, Wakili Lyakati anatumia sheria kukabiliana na adui wa unajisi wa mazingira ambao ni wananchi wa Siza kupitia akina Pasta Yona wa Yona. Bwana Abdula anamweleza Lyakati katika *Bustani ya Edeni* kuwa, "Najua itabidi Lyakati upambane naye mahakamani." (uk. 51). Mwenye kurejelewa kama wa kukabiliwana naye ni Wakili Mwaka ambaye hutumia sheria kuwatetea wanyonge na mazingira yao mahakamani. Kwa mfano, anawatetea wafanyakazi na wakulima wa kawaida na hivyo kwa njia hii huweza kukabiliana na wakala wa uharibifu wa mazingira mahakamani. Hivyo, ingawa sheria inatumiwa kuulinda na kuupalilia uchafuzi wa hewa na mazingira kwa ujumla, mara chache inatumiwa kuufifisha. Hili linadhihirisha kuwa mna matumaini ya bara la Afrika kukomaa kiuongozi na kiutawala siku za hapo baadaye.

Isitoshe, Jonalisti anafafanua uenezaji wa athari za mazingira chafu kwa viumbe kwa jumla katika janibu za Afrika katika *Bustani ya Edeni* kupitia kumbukumbu yake kuwa, Wajerumani wanawaona Waafrika kama nguruwe. Nguruwe ni mnyama mnene na mfupi afugwaye mwenye pua kubwa na ndefu, miguu mifupi na mkia mfupi ambaye Waislamu hawali nyama yake kwa kuwa ni haramu (Mdee na wengine, 2015; TUKI, 2013 na 2014; Wamitila, 2022; BAKITA, 2022). Hivyo, kutokana na uongozi na utawala dhalimu, Wajerumani wanawadhalilisha na kuudunisha utu wa Waafrika wanapowachukulia Waafrika katika nchi za Afrika kama nguruwe. Jonalisti anaongeza kuwa, Wajerumani wanalichukulia Bara la Afrika kama dampu la

kumwaga taka za nyuklia kutokana na ufanifu wa kuyaharibu na kuyachafua mazingira kwa wepesi barani Afrika. Ndiposa wananchi wa Siza wanashangaa jinsi Wajerumani wanawachukulia Waafrika kama funza tu ila si binadamu. Kwa mujibu wa BAKITA (2015), funza ni mdudu mdogo ambaye huingia katika vidole vya miguu ya watu au viluwiluwi vya nzi ambavyo huonekana katika uchafu hasa vitu vilivyooza.

Funza hupatikana sana katika maeneo ya Afrika. Hivyo, Wajerumani wanalichukulia bara la Afrika kama uchafu katika mazingira dhoofu. Aidha, kudhihirisha kuwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira hushamiri katika janibu za Afrika na hufadhiliwa na mataifa tajiri ya Ulaya, Uropa, Marekani na kwingineko, Bwana Abdula na familia yake wanakimbilia nchi jirani wakiwa safarini kuelekea nchini Marekani baada ya kusababisha maafa. Madhara ya tabianchi na mabadiliko ya hali ya hewa barani Afrika yanadhihirika paruwanja pale ambapo usafi unajifunika na uchafu unajifunua. Kwa upande mwingine, maji hayanyweki; hewa haivutiki; chakula hakiliki – yote kutokana na madhara ya tabianchi na mabadiliko ya hali ya hewa. Madhara ya tabianchi na mabadiliko ya hali ya hewa yanashamiri katika mazingira yenye ufisadi, tamaa na ubinafsi-uchoyo. Baadhi ya waliokuwa wanashuhudia hukumu ya kifo ya Dzombo katika *Walenisi* wanashikilia msimamo kuwa, shetani pia hapendi watu wakijieleza sawa na viongozi wao katika mazingira yao ambao hupalilia uozo na maovu ya kijamii.

*Jabali la Ujinga* katika *Walenisi* linasawiri utumwa katika mataifa fukara ya Afrika kama zao la uongozi na utawala dhalimu. Mwandishi Mkangi anafafanua kuwa, maeneo alikotoka Dzombo, ujinga ulikuwa wa matofali ya sampuli nyingi tofauti. Ujinga unachangia uharibifu na uchafuzi wa mazingira pakubwa, hasa katika nchi za Afrika. Dzombo katika riwaya ya *Walenisi* anapambanua kuwa, kulikuwako na ujinga ambao chimbuko lake lilitokana na maumbile kimwavuli, katika janibu za Afrika. Anasisitiza kuwa ulikuwa wa asilia na hivyo kila mwananchi alilazimika kuwa nao kwa kipindi fulani maishani mwake. Ujinga huu ni ule wa utegemezi wa kumtegemea binadamu mwingine. Katika bara la Afrika, mataifa mengi ni changa yakilinganishwa na yale tajiri ya Ughaibuni tangu yapate uhuru. Kutokana na ujinga na ulofa, mataifa mengi ya Afrika hutegemea mataifa yaliyokomaa, tajiri na yenye uwezo ya Ulaya, Uropa, Marekani na mengine mengi kiuchumi, kisiasa na hata kijamii.

Aidha, hukopa na hutegemea misaada ya chakula kutoka kwenye mataifa kwasi. Ingawa Dzombo anabaini kuwa taifa haliwezi kupevuka au kuendelea kwa njia yoyote bila kukabiliana na kulikwepa jabali hili, anasadiki kuwa jabali hili linapalilia utumwa barani Afrika zaidi likilinganishwa na mabara mengine. Hii ni kwa sababu, punde tu mataifa fukara yanapojinasua na jabali la ukopaji na utegemeaji kutoka kwa mataifa kwasi ya Ulaya, hujipata likisongwa papo kwa hapo na changamoto za uhusiano wao na mataifa tajiri. Uhusiano wa kidiplomasia huwa muhimu sana katika kuchangia maendeleo endelevu, amani, uundaji na utekelezaji wa sera mwafaka, miundo msingi na ukuzaji wa chakula cha kutosha.

Hakika, ujinga huimarisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira kupitia matumizi haramu ya rasilimali, kutokuwa na ufahamu wa athari za shughuli za kila siku na kukosa uelewa wa mbinu endelevu za kilimo, ufugaji na matumizi ya rasilimali asilia. Kwa upande mmoja, hili linafungamana na nguzo mojawapo kuu ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya maendeleo endelevu. Hivyo, uchafuzi na uharibifu wa mazingira unarutubishwa kupitia njia tofautitofauti barani Afrika. Kupitia mhusika Dzombo, mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anaeleza kuwa, "Alilokuwa akijua lilikuwa ni kwamba kila wakati binadamu alipojinasua kutoka kwenye ujinga wa maumbile, alijikuta akisongwa papo kwa hapo na ujinga uliotokana na uhusiano wa kijamii." (uk. 13). Hili linafungamana na kauli ya Oliver (2016) kuwa, mataifa tajiri huweza kudhalilisha na kuyanyonya mataifa fukara kupitia ushindani wa kiuchumi usio wa haki, udhibiti wa raslimali, uwekezaji wa kimataifa na kuingilia mifumo ya kisiasa na kijamii.

Duniani, tofauti na kwa Wawalenisi kunasawiriwa kama eneo lenye ubaguzi, utabaka, manyanyaso na dhuluma tele kama zao la uongozi na utawala dhalimu. Mwandishi Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* anaeleza kuwa baadhi ya mambo ambayo huzalisha dhuluma duniani ni kama vile; ukosefu wa ajira, utafutaji wa ajira adimu, uajiri wa vibarua vya sulubu kama vile ajira kwa watoto barani Afrika (Maathai, 2009); na kufutwa kazi ovyo. Mtu-Wazo anafafanua kuwa jambo la kujidharau na la kutia aibu lilikuwepo wakati wa enzi ya Wachuna. Katika *Walenisi* anaongeza kuwa, "Ni wakati wa enzi ya Wachuna tu ndipo uchafu huu ulipochochewa." (uk. 111). Uchafu unaorejelewa hupalilia na kuendeleza uongozi mbaya katika mataifa mengi barani Afrika (Waithiru, 2019). Uchafu huu hupatikana sana katika janibu za Afrika. Ingawa uchafu wa uongozi na utawala huwaathiri viongozi moja kwa moja, wananchi

na mazingira yao hunajisiwa pakubwa. Viongozi hutoa leseni za kuruhusu ufyekaji misitu na ujenzi wa viwanda ambavyo huzalisha kemikali sumu kwa watu na mazingira yao.

**iii. Utambulisho Tepetevu**

Kutokana na wananchi wengi katika mataifa fukara, kama vile ya Afrika kusheheni ukabila, utabaka na utamaduni ulionajisiwa na ule wa Ughaibuni, wao hukosa utambulisho thabiti na badala yake huwa na utambulisho tepetevu. Ingawa si rahisi binadamu kujipa utambulisho maalumu kwa wepesi, upekee wa kila mja humsaidia pakubwa kujitambua na kujizuzua kutoka bahari la kutojijua na kutojielewa (Nabea na Ngugi, 2012). Ndiposa, Bwana Abdula anafanikiwa kupata leseni, mahali na wafanyakazi pale mjini Siza bila vikwazo. Hili linadhihirishwa na mwandishi anapoeleza katika *Bustani* kuwa, "Kweli, Bwana Abdula alishinda vita, na leo Sagasaga inasafirisha na kusambaza madawa kote nchini na nchi za jirani." (uk. 49). Madawa haya yanachangia uharibifu wa hali ya hewa pamoja na kusababisha athari kubwa kwa mifumo ya ikolojia na huduma za mazingira katika utengenezaji wao, hususan katika mataifa ya Afrika. Mwandishi anaeleza kuwa, takriban asilimia hamsini ya maduka ya madawa ya *Sagasaga Chemist Shop* katika jiji la Nomila ni mali ya Trans-Chem na Bwana Abdula. Madawa haya yanauziwa wenyeji bila kuzingatia afya yao. Hili huchangia kuyahatarisha maisha ya wenyeji kwa kiwango kikubwa. Hali hii hufungamana na nguzo ya kifo ambapo baada ya binadamu kuyaangamiza mazingira yake hupelekea maangamizi yake mwenyewe. Hakika mabadiliko ya hali ya hewa yanaweza kuathiri uzalishaji wa chakula na kusababisha upungufu wa chakula na kupanda kwa bei ya vyakula.

Kutokana na utambulisho tepetevu, uchafuzi na uharibifu wa mazingira huabudiwa katika mataifa ya Afrika kutokana na viwango vikubwa vya ufukara wa; mali, utambulisho, umoja, mawazo, dhana na mengine mengi yanayoweza kuepukika. Kupitia Sekretari wake Bwana Abdula, Magarita, inadhihirika kuwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira hushamiri, hukaribishwa na hushangiliwa katika nchi za Afrika. Katika kiwanda cha Sagasaga, kwenye ofisi ya Bwana Abdula – inayoashiria ukoloni mamboleo barani Afrika – pesa nyingi zilikuwa zimetumiwa ili kuitia nakshi kwa samani za thamani kubwakubwa; masofa, mazulia, mapazia, meza, vimeza, makabati, sanamu, maua na vitambaa tofautitofauti. Kadhalika, inadhihirika kuwa, wanaozalisha mabadiliko ya hali ya hewa hujilinda dhidi yake kikamilifu katika

janibu za Afrika. Mathalan, mwandishi anapambanua katika *Bustani ya Edeni* kuwa, "Na lililo muhimu zaidi; mitambo maalum iliyozuia sumu za kemikali kuingia mle ndani." (uk. 50). Bwana Abdula ana mitambo ya kuzuia sumu za kemikali kuingia ofisini mwake ilhali wafanyakazi wake hawana vifaa vinavyofaa kwa usalama wao dhidi ya madawa yale ya sumu. Matajiri wanaoekeza katika mataifa ya Afrika hujilinda dhidi ya kemikali na sumu itokanayo na viwanda vyao huku wakiyaharibu na kuyachafua mazingira ya Afrika bila kujali madhara yake kwa wenyeji wala kizazi cha halafu. Hili linashabihiana na nguzo ya uwezo na kifo. Hakika matajiri huendeleza shughuli katika viwanda vyao ambazo huwasababishia Waafrika maafa kutokana na kuongezeka kwa magonjwa yanayohusiana na joto kama vile kiharusi cha joto. Aidha, mafuriko na ukame huweza kusababisha matatizo ya kiafya kutokana na upungufu wa maji safi na magonjwa yanayoenea kwa maji.

**iv. Uchafuzi wa Hewa**

Uchafuzi wa hewa huwa kigezo kikuu katika upaliliaji wa anthroposenia. Katika janibu ambazo viwanda hukiuka sheria za uhifadhi na utunzaji wa mazingira uchafuzi wa hewa huwa jambo la kawaida. Madhara yatokanayo na uchafuzi huu huwa makuu na hasi mno. Uzalishaji wa dawa katika kiwanda cha Saga Saga husababisha uharibifu wa mazingira hususani majengo marefu na mafupi ya Sagasaga. Kwa mfano, geti la kiwanda cha Sagasaga limeliwa na asidi kutokana na uharibifu wa hewa ya asidi inayochafua hewa na kuyaharibu mazingira. Uchafuzi wa hali ya hewa una madhara tele kwa mazingira na afya ya binadamu. Baadhi ya madhara hayo ni pamoja na matatizo ya kupumua, mvua ya asidi, kupungua kwa ozone na mabadiliko ya hali ya hewa. Matokeo ya madhara haya huwa kifo.

Kando na kifo kuwa mojawapo ya nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira, ni nguzo kuu ya mazingira chafu na dhoofu, madhali bila kifo kushamiri; aidha kupitia ubaguzi, ulofa, maradhi, njaa, vita vya wenyewe kwa wenyewe, uongozi mbaya, vurugu dhidi ya mazingira, unyama na njia nyingine nyingi, uchafuzi na uharibifu wa mazingira hufifia. Mfano mzuri ni mle nchini Walenisi katika riwaya ya *Walenisi*. Hili linadhihirika kupitia mhusika Dzombo – ambaye kando na kuashiria taifa anaashiria umma unaonyanyaswa na kudhulumiwa – anayefanya safari ya kimawazo ya kujitathmini na kujihakiki na hatimaye anajivumbua upya kwa kutambua siri ya utu. Pale anamaizi asili ya jina *Mtu* kabla ya jina la kila mmoja mle Walenisi. wimbo unaoimbwa na kila Mwalenisi unamfanya Mtu-Dzombo kulengwalengwa na machozi

kwa furaha na uhuru wa kikweli aliokuwa akiuhisi moyoni mwake. Dhana kwamba wimbo ule unaimbwa na kila Mwalenisi kwa kushikana mikono wakiwa katika duara inaashiria ukamilifu wa utu wao dhidi ya unyama nchini Walenisi.

Maeneo alimozaliwa baba Fofi yanasawiri athari za mazingira chafu na dhoofu kupitia ukame. Ukame wenyewe ni zao la mabadiliko ya hali ya hewa. Jamii inayoishi kwenye mazingira haya imegubikwa na uchochole na kwa karne nyingi sasa, ukame umekuwa ushindi mkuu wanaojivunia wenyeji katika istilahi ya kitafsida ya anthroposenia. Mama Fofi anathibitisha hili katika *Mafuta* anapotaja kuwa, “Ukame ... ulionekana ukienea jamii nzima na kurithika kama ufalme!” (uk. 26). Ufalme unaorejelewa unaashiria ngome na nguzo za anthroposenia.

Barabara wanayoipitia Dkt Matoga na mwanawe Bruno kutoka uwanja wa ndege imezagaa vijumba vya makuti vilivyokuwa vimechipuka mle kando kando mwa barabara ili kuashiria uchipuzi wa wanyonge fukara mjini Daluta. Hili linasababishwa sio tu na uhamiaji wa watu kutoka sehemu za mashambani hadi mijini ila pia na ongezeko kubwa la idadi ya watu duniani kwa jumla. Ongezeko la watu duniani huathiri hali ya hewa kwa njia kadhaa. Baadhi yazo ni ongezeko la matumizi ya nishati, kupanda kwa mahitaji ya chakula, ukuaji wa makazi na miundombinu pamoja na ongezeko la taka. Hivyo, ni muhimu kwa binadamu kuchukua hatua za kupunguza ongezeko la idadi ya watu, kuboresha teknolojia za uzalishaji wa nishati na kilimo na kukuza mbinu za maisha endelevu ili kupunguza athari za ongezeko la idadi ya watu kwa mabadiliko ya hali ya hewa.

**v. Mahakama na Janibu za Binadamu**

Kwa mujibu wa Ndalu na wengine (2014), Mdee na wengine (2015), BAKITA (2015) na Moseley na Otiso (2023), mahakama ni eneo ambapo kesi au migogoro husikilizwa na hakimu au jaji na kuyatolea maamuzi. Maamuzi yanayotolewa mahakamani, hutarajiwa na kuaminiwa na watu kuwa ya haki na usawa. Hata hivyo, mtunzi Mkangi katika *Mafuta* anayasawiri mahakama kama eneo linalosawiri; linalohifadhi; linalopalilia; linaloendeleza na kuukuza udhalimu kwa kuwaogofya, kuwahangaisha, kuwaonea na kuwahini washtakiwa na washtaki wote kwa jumla – haki. Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa mahakama yenye miraba ya kitabaka yanazindikwa na sheria za kuulinda udhalimu. Hili linafanikishwa na uongozi wa mahakimu na mawakili wenye uzandiki, ulafi, ufisadi na ulaghai wa hali ya juu. Jumba lenyewe linalohifadhi madhalimu katika istilahi ya kitafsida ya mahakama ni

la mawe na tena la kutisha ili kuwaogofya wanyonge. Hii ni kwa sababu, matajiri hawangepata muda wala fursa ya kubabaishwa na mahakama maadamu yenyewe yapo kuyalinda maslahi ya Wakwasi.

Mwandishi Mkangi katika *Mafuta* anaeleza kuwa, "Mahakama yaliyokaa kama ngome isiyosikia vilio vya watu walioko nje; na yenye lengo la kuwaogofya walionaswa tumboni mwake." (uk. 21). Hali hii ni sawia na iliyo kwenye *Walenisi* wakati Dzombo anahukumiwa kifo. Hakimu anaingia mahakamani mithili ya malaika wa mauti na kutekeleza jukumu lake kuu. Katama Mkangi anathibitisha hili anapoeleza kuwa, hakimu alipoketi aliegemeza miwani yake ya nusu glasi puani kwake, akamtazama Dzombo kwa ile sehemu iliyosalia na kumwamrisha asiseme. Ingawa nyakati zile mahakama hazikuwa zikizingatia kaida kwa lengo la kulinda au kutetea, wala kudumisha haki na uhuru wa binadamu, Dzombo anapigwa na butwaa la bumbuazi baada ya hakimu kumhukumia Dzombo kifo.

Mwandishi Mkangi anaeleza katika *Walenisi* kuwa, "... akatanabahi ... katika Ulimwengu mzima wa Walenisi ... Yeye tu ndiye aliyekuwa amesimama peke yake! ... bila kusita kupatoka mbio pale alipokuwa amesimama mpaka jukwaani." (uk. 215). Katika mahakamani, dhuluma inapaliliwa kupitia ulaghai. Mtue anashuhudia katika *Mafuta* na kueleza kuwa, mahakama yenyewe ni ya kibedhahu na itishayo kuliko mizimu. Ikizingatiwa kwamba mizimu hutumiwa na tamaduni mbalimbali, hasa baina ya jamii za Afrika kuhifadhi historia, utamaduni na mazingira yao (Howarth, 1996), janibu za mahakamani zinazoelezewa basi zinaasi desturi hii na kuinajisi kwa kuitumia kuendeleza woga na maangamizi kwa uhai wa binadamu. Ni maeneo ambapo, Mtue anakiri katika *Mafuta* kuwa, ni Mahakama ya uongo ambao punde tu unapojidhihirisha ukweli aghalabu hujitenga. (uk. 21). Uongo unakuza na kuendeleza udhalimu.

Katika misingi hii ya uzandiki wa ulaghai, udhalimu na maangamizi yanashamiri. Tofauti na *Walenisi* ambapo Wawalenisi wanadumisha utu katika miduara kupitia wimbo na hivyo kuufifisha udhalimu, katika mahakamani katika *Mafuta*, watu wanadumisha utabaka, ubaguzi na udhalimu kupitia kukaa kwao katika miduara ya unafiki, utabaka na unyanyasaji uliogubikwa na unafiki. Hivyo, anthroposenia inashamiri kwa kukamafleji katika unafiki, uongo na upofu. Ukweli huu unathibitishwa na mtunzi Mkangi katika riwaya ya *Mafuta* anapoeleza kuwa, "...

kisehemu kidogo katikati ya mduara huu [palikuwa wazi] ... kukikaa wazee wa kike na wa kiume [safu ya kwanza]. Walijibagua kwa kufuatiana na tofauti zao za maumbile kwa jinsi walivyokaa: kuangaliana kwa kuketi nusu mduara." (uk. 22). Hakika, maeneo ya mahakamani yanatumiwa na wenye uwezo kuwadhalilisha wanyonge.

Kwenye mahakamani, kimya kinatanda na kuzagaa kama ukungu. Ukungu unaorejelewa na mwandishi unaashiria kutanda na kutapakaa kwa maonevu na unyanyasaji, hasa katika mataifa fukara ya Afrika. Mdee na wengine (2015), na TUKI (2014), wanaeleza kuwa ukungu ni mawingu mazito meupe – lakini yazalishayo utandu wa giza maishani kijazanda na kitaashira (BAKITA, 2015) – yanayotanda angani na kusababisha giza; vundevunde au hali ya kuwa na hewa ya majimaji au unyevu. Kadhalika, ukungu ni vijani vyembamba au viyoga vinavyoota mahali au kwenye kitu chenye unyevu; yaani kitu kuvu. Mna ukungu wa kimawazo pia, ambapo mtu hupatwa na wazo. Katika riwaya ya *Mafuta* ukungu unaotawala na kuhanikiza kote unaashiria anthroposenia katika istilahi ya kitafsida ya ukoloni mamboleo au utandawazi. Hili linadhihirishwa na mwandishi katika *Mafuta* anapoeleza kuwa, "... kimya kilitanda na kutapakaa kama ukungu. Watu walionekana wakipumua taratibu kana kwamba walikuwa wakichelea kuudhi hewa!" (uk. 22). Hivyo, anthroposenia inashamiri watu wanaponyamaza na kuzivumilia athari hasi kwao kwa kuogopa kuangamizwa na walinzi wa anthroposenia – matajiri, viongozi na wenye vyeo.

Kizindani wanakoenda wateule kujivimbisha pamoja na mahakamani ni janibu zinazosawiri maangamizi katika riwaya ya *Mafuta*. Mazingira yanayosawiri maangamizi yanazidi kudhihirishwa na mwandishi kupitia mazingira anamoishi Msati. Chanzo cha mwangaza ni kibatali kinachoashiria ulofa. Moshi wa kibatali wa mafuta ya taa umetapakaa mle ndani mwote. Paa lililoezekwa ni la matambara ya plastiki, mabati mabovu na mabaki ya makadibodi linalowasitiri akina Msati dhidi ya mvua na baridi kali. Besera inayogawa chumba au kibanda kile inahusisha matambaratambara yanayoning'inia juu ya ulingo. Hali hii inamithili ile ya nyumbani kwake Dzombo kule duniani katika riwaya ya *Walenisi*. Mwandishi Mbogo katika riwaya ya *Vipuli vya Figo*, sawa na mtunzi Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* na ya *Mafuta*, wameusawiri mzinga wa nyuki kama eneo la Afrika ambapo binadamu hupalilia anthroposenia kwa hiari kutokana na kupumbazwa na mataifa ya Ughaibuni. Viongozi hawa wanaashiriwa na Profesa Williams. Mwandishi Mbogo anataja katika

*Vipuli vya Figo* kuwa, “Profesa hakuchelewa kumshawishi Dkt Matoga ili awe ajenti wa kusafirisha vipuli vya figo na moyo kwa malipo makubwa.” (uk. 18).

Pesa zinaibuka kama mbolea ya kuinawirisha na kuinenepesha anthroposenia. Zahanati ya Mtoni Clinic inaashiria janibu zinazoyahifadhi, kuyakuza na kuyaendeleza maangamizi. Jengo hili la gorofa moja linaendelea kujengwa na wataalamu tofautitofauti, kama vile; wanaochanganya sementi, mchanga na maji; mna wanaoshughulikia zege; mna seremala wakiwa na misumeno yao; wa lipu nao na miko yao na wengine waliofanya shughuli aina aina alimradi jengo likamilike kwa ufanisi. Mtunzi Mbogo akieleza kuhusu juhudi za binadamu kuyahifadhi na kuyabuni mazingira unamokulia uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika *Vipuli vya Figo* anasema kuwa, “... ilikuwa kama kundi la nyuki mzingani.” (uk. 19). Pesa zinafanikisha ujenzi wa jumba hili. Baada ya maiti kuzolewa figo na mioyo hutupwa mtoni ili mamba wapate lishe. Huu ni uchafuzi wa maji wa kiwango cha juu.

Mandhari anamoishi Magamba yanasawiri ulofa na ubaguzi wa hali ya juu kupitia hali yake duni. Kwa mfano, Dkt Matoga anazuru eneo lile wakiwa na Magamba, anatahadhari mashimo makubwa, mifereji na vidimbwi vya maji machafu. Mkweche wa Dkt Matoga unayumba na kugonga chini ndani ya shimo na unazimika hapo hapo. Hili linadhihirisha kuwa maafa hushamiri katika maeneo yenye ulofa. Kwa mfano, wanakijiji wana utamaduni wa kujiburudisha kwa nyimbo, ngoma na pombe haramu zinazopikwa na wao wenyewe. Eneo la African Bush katika hoteli ya Village Inn linaashiria mataifa ambayo huimarisha ubaguzi na maangamizi kwa ujumla kwa kuunajisi utamaduni asili na kuwaangamiza wanyama wa porini. Mathalani, ingawa sehemu hii imejengwa kwa majani, nyasi, makuti, viti vya miti vilivyosukwa kwa ngozi za ng’ombe na meza za matete na mianzi, inapalilia maangamizi ya wanyama wa porini kwa kiwango kikubwa kupitia chakula wanachotayarisha na mavazi ya wafanyakazi. Kadhalika, ingawa meza na viti vinamkumbusha mtu utamaduni wa asili, ule unaozingatiwa mle ni wa kisasa unaodumisha maangamizi.

Hili linadhihirishwa na Makasi na mhudumu wanapomfafanulia Angela kuhusu chakula kinachopatikana mle, kama vile nyama ya nyati, swara na nyama ya kanga inayopatikana mle. Makasi katika *Vipuli vya Figo* anasisitiza kuwa, “Hapa African Bush nyama zote ni za porini.” (uk. 65). Mtangazaji wa ngoma pia anadhihirisha hatua yanayofuata maangamizi ulimwenguni kote, ambapo huwalaghai watu kuwa

yana raha kupitia dalili za arusi, kisha hujinasibisha na utamaduni wa eneo fulani halafu yakikomaa hujidhihirisha yenyewe na huzalisha maafa. Hili linawekwa bayana na mtangazaji katika *Vipuli vya Figo* anapoeleza kuwa, "... ya kwanza ya arusi, ya pili ngoma ya jando na ya tatu ... ya mazishi." (uk. 67). Isitoshe, mtangazaji anathibitisha hili anapohitimisha kuwa kilele kitakuwa kibwagizo cha mchawi wa wachawi, kinachoashiria maangamizi kweli.

Maeneo ambamo maangamizi hushamiri ni yaliyovumbikwa na lindi la ulofa. Mathalani, Mabatini mna vijumba chafu; barabara zilizogubikwa vumbi; uchafu wa maji yanayonyiririka ama kusita pahala ovyo; miti iliyoangukia njia; vitoto vinavyojijambia ovyo vikitembea nusu uchi na vinavyodhihirisha utapiamlo na marasmasi pamoja na ishara nyingine nyingi za uchwara. Kadhalika, mna waume kwa wake wanaopika na kuuza mihogo barabarani; taka za kila aina; maganda ya ndizi, miwa, viazi, ukoko, marundo ya majivu, mabaki ya vyakula, michuzi na taka zingine nyingi. Mtunzi Mbogo katika *Vipuli vya Figo* anadhihirisha hali hii anapotaja kuwa, "... taka za kila aina ... vyote vilitupwa katika vifusi ... vikahinikiza uvundo, harufu totolo, funza na wadudu wengine." (uk. 85). Katika mazingira yaya haya, watoto wanachakurachakura kila siku, kwenye majalala na madampu haya wakifuata miozo ya chakula na mara kadhaa wanabahatika uozo, maradhi na shibe sampuli sampuli. Mazingira chafu hupelekea watoto kukumbwa na maradhi ya ngozi, ya mfumo wa neva na matatizo mengine ya kiafya pamoja na changamoto katika kupata huduma za afya bora.

Kitengo kipya cha upasuaji mle kwenye zahanati ya Mtoni Clinic pamoja na chumba kikubwa chenye majokofu makubwa sana ya kuhifadhi maiti ni eneo linalosawiri ukuaji wa maangamizi. Kwa mfano, jokofu moja lina uwezo wa kuhifadhi takriban maiti kumi ya watu wazima. Hili linawiana na kauli ya akina Waithiru (2022), Frantzen na Bjering (2020) na DeLoughrey (2019) kuwa, mataifa tajiri ya Ughaibuni huyanyonya mataifa fukara ya Afrika rasilimali na uhai wao bila kujali kesho ya bara la Afrika. Mtunzi Mbogo anathibitisha hili anapofafanua katika *Vipuli vya Figo* kuwa, "... chombo maalumu kilichofanya kazi kama friji ... kuhifadhi mioyo na figo, kabla vipuli hivi havijasafirishwa kwenda Ughaibuni kwa Profesa Williams." (uk. 98). Pia masanduku maalum yanayotumiwa kusafirishia vipuli yanaashiria vifaa vinavyofanikisha maangamizi katika zahanati ya Mtoni Clinic.

Ubalozi wa Osantonio, ofisini mwa Balozi Suprano ni eneo linalopalilia uharibifu kupitia maangamizi ya wanyama wa porini. Hili linadhihirishwa na Dkt Matoga anapolisawiri eneo lile likiwa na chungu kikubwa kilichoshonewa ngozi ya chui kukizunguka. Eneo la gereza linaloongozwa na kutawaliwa na Mkuu wa Magereza linasawiri utumwa kupitia uwezo wake wa kuwanyima wafungwa uhuru na utu wao kama binadamu. Hali hii ni mithili ya ile inayosawiriwa na mwandishi Mkangi katika riwaya ya *Walenisi*, ambapo Wachuna walijenga magereza kama njia ya kuwatawala wananchi kwa udhalimu bila pingamizi. Wote waliojaribu kuwadadisi Wachuna walitiwa gerezani au kuuliwa. Emmanuel Mbogo anasawiri seli tofautitofauti pale gerezani kama janibu za kuendeleza maradhi, ubaguzi, mateso na hatimaye maafa.

Ili anthroposenia ishamiri, kitu cha kwanza muhimu na msingi ambacho humwondolea mtu ni utu au ubinadamu na kumvisha unyama. Hili linawekwa bayana na Katama Mkangi kupitia jamii ya Wawalenisi katika riwaya ya *Walenisi*. Kwa mfano, kando na walinzi wenye bunduki kulinda seli, zinaundwa kwa vyuma imara na hata sehemu inayoachwa ya hewa kupitia mnatandikwa nondo imara za chuma. Kwenye lango kuna kufuli kubwa zenye uzito wa zaidi ya robo kilo ambazo zimefungwa moja juu, nyingine katikati na ya tatu chini ya lango la chuma. Gereza lenyewe limezungukwa na ukuta tofauti mrefu wenye seng'enge kama futi kumi na mbili. Ukuta huu umejengwa kwa mawe. Emmanuel Mbogo katika *Vipuli vya Figo* anaeleza kuhusu ukuta huu kuwa, "... ulikuwa ngome madhubuti iliyosimama kwa kiburi ikitimiza wajibu wa kuwalinda wafungwa." (uk. 116). Ingawa wafungwa wanafaa kuadhibiwa, Alia (2017) akiyaunga mkono mawazo ya mtafiti anasisitiza kuwa mna haja ya kumrekebisha binadamu katika misingi ya utu na ila si kwa lengo la kumlemaza kwa njia yoyote wala kumwangamiza. Mbogo anathibitisha kuwa gereza lile linapalilia ufukara na utumwa kwa sababu baadhi ya wafungwa kama Shipe walipatikana katika harakati za kupigana na ulofa lakini badala ya serikali kumpa njia za ukweli za kuchuma wanamtia gerezani. Mwandishi anadhihirisha hali hii katika *Vipuli vya Figo* kupitia kauli kuwa, "... ng'ombe wa maskini hazai, maskini akiokota huambiwa mwizi." (uk. 117). Wafungwa wengi wanaosawiriwa na waandishi wa kazi teule wanavunja sheria katika juhudi zao za kukabiliana na ufukara katika mazingira yao.

Baharini na hasa pale kando ya Mto Rasi unapoingia baharini mna mamba wengi. Ikizingatiwa kwamba mamba ni taashira ya maangamizi kwa binadamu, basi eneo lile

karibu na bahari, kando mwa mto, linasawiri eneo linalopalilia na kuhifadhi ajenti wa maangamizi. Baada ya Dkt Matoga na wenzake kuzoa vipuli vya figo na mioyo kutoka kwenye maiti ya maskini, viwete na makahaba, mabaki yanarushwa kwenye mto huo na mamba wanapata mavuno. Huu ni uchafuzi wa maji. Kwa mujibu wa TUKI (2006), Mdee na wengine (2015) na BAKITA (2022), mamba ni mnyama wa jamii ya kenge lakini mkubwa zaidi ambaye ana magamba na huishi kwenye maji. Pia mamba hurejelea nyoka wa rangi nyeusi au kijani mwenye sumu kali sana. Katama Mkangi katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi* na mtunzi Mbogo katika *Bustani ya Edeni* na *Vipuli vya Figo* wakikubaliana na maelezo haya wanaisawiri anthroposenia kupitia bafe na majoka makubwa makubwa. Hata hivyo, kutokana na kuishi kwa muda mrefu katika mazingira yanayotawaliwa na kifo, wenyeji wa Daluta, hasa wanaoishi karibu na Mto Rasi wamezoea athari hasi za maangamizi ingawa wanaangamia tu. Si kawaida binadamu kuyazoea maafa, na ndiposa Dkt Charles anatetemesha mabega anapowaona mamba.

Hili linaonyesha kwamba wenyeji wa sehemu zile wameizoea anthroposenia na athari zake hasi na hatari kwa binadamu. Aidha, maeneo anamoishi Mzee Makolokoza yanasawiri utumwa kupitia ufukara unaoyatawala maeneo haya. Mwandishi Mbogo anafafanua kuwa, eneo lile limesheheni vibanda vya nyasi pamoja na vitoto vilivyo uchi vinavyotapakaa makamasi na nzi vifuani. Hali hii kando na kuusawiri utumwa kupitia ulofa unaashiria uchafu na maradhi ya homa ya mapafu kwa vijana katika mataifa duni ya Afrika. Hali hii ni sawa na taswira ya nyumbani kwake Mzee Makolokoza. Dkt Matoga anapofika wanaambatana pamoja na Mzee Makolokoza hadi kwenye kibanda kidogo cha mabati ya madebe.

Mtaa wa Freedom Avenue, mjini Daluta ni eneo linalosawiri utabaka na maangamizi na pia linayaendeleza kupitia shughuli za Nyau, Kipanga na Shipe. Mtaa wenyewe uko kimya ingawa kinatubuliwa hapa na pale na mikoromo ya fukara waliolala kwenye baraza za majumba kadhaa. Katika kile kimya, kitoto chenye njaa kinapasua hewa kwa kilio baada ya kuzabwa kofi na mamake. Kitoto chenyewe kinalia kutokana na njaa lakini mamake ambaye hana mbele wala nyuma na anayetafunwa na njaa pia anakitusi kitoto na kukizaba kofi. Kipanga anavutiwa na kilio kile cha kitoto kile kidogo pamoja na kauli ya mama yule mzazi anayemlaani mwanawe katika *Vipuli vya Figo* kuwa, “Lala! Shenzi we!” (uk. 163). Kitoto kile kinaendelea kulia kwa sauti ya chini lakini kinanyamaza baada ya babake kukipatia kipande kidogo cha mkate.

Babake ni kipofu. Kando na kitoto kinachopewa kipande cha mkate na babake, mna vijana wawili, ndugu za kitoto kile, wa umri kati ya miaka kumi na kumi na mitano.

Wamelala kwenye vigunia kwa amani, huku wakikoroma. Umaskini, ulemavu na njaa vinatawala familia hii ya mzee ambaye ni kipofu. Mtoto baada ya kupewa kipande cha mkate na babake, anaketi na kuumega kiasi kwa meno yake na kuutafuna kwa muda mrefu kutokana na upungufu wa mate mdomoni ya kuulainisha ili aumeze. Utafunaji huu ukiendelea, kifua chake kilicho wazi kinapigwa na baridi pamoja na mbavu zake za matete zinazolala kwa unyonge. Baridi inampiga kutoka mgongoni hadi tumboni. Kwa mtoto mdogo kama huyu, hali hii kando na kumnyima haki zake za kimsingi inamzorotesha kiafya na kiukuaji. Hivyo, ufukara kando na kuathiri afya na mahusiano ya binadamu, hudidimiza kizazi kwa lengo la kukikausha. Kutokana na ukosefu wa chakula, mtoto yule anapomeza kile kipande cha mkate, uchungu unaompata unalifanya chozi la uchungu na maumivu kooni linyinyirike mashavuni yake laini na dhaifu.

Nyau na Shipe wakiwa na pamba lililolowa sumu, wanaisongea familia ile na kuwakandamiza pua zao. Wanatangulia na mama watoto, kisha mtoto ambaye hata hakutoa sauti, na hatimaye wakahitimisha na vijana waliolala pamoja na baba watoto. Kipanga anasogesha gari na kwa ushirikiano na Nyau na Shipe, wanapakia kwenye gari na kisha kuondoka mbio. Shughuli wanaitekeleza bila yeyote kuwaona wala kujua. Hata baada ya familia hii kutoweka, hakuna anayetambua, kulalamika wala kudadisi mabadiliko yale. Hivyo, mazingira yenyewe yanafanikisha na kuimarisha utumwa ndiposa tukio lenyewe si mkongoto kwa yeyote. Bila tatizo lolote, Nyau, Shipe na Kipanga wanafika na kupakua familia ile ambayo ilikuwa bado imelala na kuimwaga ndani ya jokofu. Lango wanalopitia kuingia linarejelewa na mwandishi wa *Vipuli vya Figo* kama, "... geti la Machinjioni ..." (uk. 164), kudhihirisha eneo linaloendeleza maangamizi.

Baada ya kuipakia familia ile kwenye friji, Nyau anachukua msumeno wa umeme na kwa ushabaha anaulenga meno yake juu ya kila kichwa kwa zamu na kuvipasua vichwa vyao. Mwandishi anadhihirisha hali hii anapoeleza katika *Vipuli vya Figo* kuwa, 'Alichungulia kidogo mle ndani akaona damu na ubongo vinafoka; akafunga lango la friji." (uk. 164). Eneo la Nkrumah Street pia linasawiriwa kama eneo linalopalilia ulofa na halafu mauti. Nyau, Shipe na Kipanga wanafika sehemu yenye

vibanda vya makaratasi na vipande vya mabati na wanaliegesha gari karibu na vibanda hivi. Sehemu hii ni uwanja katikati ya supamaketi na posta. Ni sehemu ambayo wanyonge wengi walijenga vibanda vya makaratasi usiku kwa minajili ya kujipa lepe la usingizi. Asubuhi ilipobisha walikuwa wanavibomoa na kuyaweka makaratasi yale kwenye maboksi na kuyahifadhi maboksi yenyewe kwenye maeneo ambapo yasingenyeshewa na mvua wala kukojolewa na walevi.

Ingawa halmashauri ya jiji la Daluta ilikuwa imejaribu mara nyingi kuwakanya na kuwafukuza kina yahe hao wasije wakajenga wala kulala uwanjani ule, wanyonge walibakia pale pale na hata kuongezeka. Mwandishi Mbogo anataja kuwa baada ya muda vibanda vile viliibuka tena kwa wingi kama uyoga. Chumba kinachohifadhi friji katika zahanati ya Mtoni Clinic kinasawiri maangamizi kupitia shughuli zinazofanikishwa mle na maiti zinazohifadhiwa mle baada ya mauaji ya kikatili. Ikumbukwe kwamba, kabla ya Nyau kuwapasua vichwa maskini huwa bado wako hai ingawa wakiwa wamezirai kutokana na dhiki na dhuluma aina aina. Baada ya Nyau, Shipe na Kipanga kuwapakua wanyonge kutoka Nkrumah Street, Nyau anazika msumeno vichwani mwao na kuwaangamiza, na kisha kulifunga friji.

Emmanuel Mbogo anasawiri uhalisia wa mauti chumbani humu kupitia maelezo yake ya moja kwa moja katika *Vipuli vya Figo* kuwa, “Harufu ya damu, uozo na fukuto la mabaki ya nyama ya maiti waliopasuliwa jana lilikuwa limehanikiza mle ndani – halivumiliki.” (uk. 165). Hali hii inaashiria kuwa maafa huzalisha athari ambazo huwa hazivumiliki. Maiti zinazotoa uozo na uvundo ni zile za familia ya mtoto, vijana wawili, baba na mama waliokuwa wametoka kwenye viambaza vya majumba yaliyojengwa kando ya barabara ya Freedom Avenue mjini Daluta. Kwa ujumla, mji wa Daluta ni eneo linalopalilia maangamizi pakubwa. Mathalani, kutokana na ule uozo na uvundo kwenye friji, Nyau anawakumbusha wenzake haja ya kutupa ile mizoga ya maiti iliyosalia baada ya kudondolewa vipuli vya figo na mioyo, mtoni Rasi kwa kufuata agizo la Dkt Matoga.

Baada ya kuungwa mkono na Shipe, na kisha Kipanga, wanasaidiana kubeba mfuko imara wa plastiki wenye nyamanyama tele na mifupa kibao ya mabaki ya maiti na kuiingiza ndani ya gari. Halafu wanaondoka Mtoni Clinic na kuelekea kwenye daraja kuu la Mto Rasi. Wanapofika katikati mwa daraja, Kipanga anapiga gari breki na kisha kulirejesha nyuma karibu na ukingo wa daraja ili kurahisisha upakuaji wa

mifuko. Hatimaye, Nyau na Shipe wanashuka na kuusukuma mtumba ule wa plastiki hadi ndani ya Mto Rasi, ambapo mamba wakubwa wanafurahia minofu yao ya hisani ambayo hawajui inatokana na hisani ya Dkt Matoga.

Eneo lingine linalofanikisha ufukara na utumwa katika riwa ya *Vipuli vya Figo* ni lile la Sokota. Eneo hili linasheheni mabanda ya malaya wa jiji la Daluta. Kutokana na utepetevu wa serikali wa kutoendeleza eneo la Sokota, linazagaa vibanda vya mbavu za mbwa vilivyoezekwa madebe na makaratasi ya plastiki, wanamoishi malaya wa jiji na kuendeleza shughuli za ukahaba mle vibandani. Mintarafu ya mwandishi Mbogo, plastiki ni ishara ya anthroposenia katika mazingira duni kutokana na ishara kwamba zinatumiwa aidha kuhifadhi mabaki ya maiti au kuezeka mabanda ya waduni. Usiku, vibanda hivi hujitambulisha kwa mwangaza hafifu kutoka kwa vikoroboi ambavyo hupangwa mstari, katika kila kibanda. Wanawake kutokana na ulofa hujibanza, kila mmoja mlangoni mwake akisubiri wanaume wenye haja ili awape huduma. Anthroposenia inazidi kudhihirishwa na mwandishi pale anapomsawiri mwanamke kama kifaa kinachopangwa kwenye gwaride na kukaguliwa na mwanamume.

Watson na Watson (2007) wanaeleza kuwa, udhalilishaji na ubidhaaishaji wa mwanamke katika biashara ya utumwa ni suala lililomnyima sio tu binadamu utu, ila jamii nzima. Kwa mujibu wa waandishi Mbogo na Mkangi katika riwaya nne teule, wanapendekeza utu kama mbinu mwafaka na madhubuti ya kukabiliana na anthroposenia. Akina Nyau wanakubaliana kuwa eneo nzuri la kufanya uwindaji wa vifaa ni eneo hili la Sokota. Wanawarejelea wanawake kama vifaa na hivyo kuwanyima utu. Hivyo, katika maeneo ambayo hudidimiza utu au hata shughuli ambazo hudhoofisha utu, maafa hushamiri. Mtunzi Mbogo kwa mfano, anadhihirisha anthroposenia kupitia biashara ya ukahaba katika *Vipuli vya Figo* anapoeleza kuwa, "... bei za maduka haya ilikuwa moja – si ya "nipunguzie tafadhali", mnunuzi alilipa na kumaliza haja yake, basi!" (uk. 166). Ingawa hili linaashiria uozo wa maadili linasisitiza madhara ya ufukara katika jamii.

Katika eneo hili akina Nyau wanasimamisha gari lao karibu na shule ya sekondari na kisha wanashuka na baadaye wanatembea taratibu kuelekea kwenye vibanda. Shughuli hii inafanikishwa na mazingira yenyewe kuwa na giza na nyakati ambazo ni za saa saba za usiku. Nyau anapita kila mlango wa kibanda akipuliza sumu kwenye nyufa za milango na madirisha hadi tamati. Baada ya Shipe na Nyau kuwapulizia

wanawake wote kumi na wawili nusukaputi, wanawakusanya na kuwatia kwenye gari. Hatimaye, wanalipeleka windo lao la vipuli kwenye zahanati ya Mtoni Clinic. Gereza la Tanulo linaloongozwa na Mkuu wa Magereza pia linasawiri maangamizi kwa kumpa Dkt Matoga maiti za kuvuna vipuli vya figo na mioyo baada ya baadhi ya wafungwa kunyongwa. Mathalani, katika Pango la Kunyongea pale gerezani, Mkuu wa Magereza anawapeleka Dkt Matoga, Nyau na Kipanga na kuwaongoza hadi kwenye majeneza sita ya mbao, ambamo wanapata maiti sita waliokuwa wamenyongwa siku ile asubuhi.

Pamoja wanazitoa maiti zile, moja baada ya nyingine viungo vya figo na mioyo, huku wakiitumbukiza kwenye chombo maalum walichokuwa wamekuja nacho. MaAngela hata kama hana habari kuwa mumewe anashiriki mauaji na usafirishaji wa vipuli vya figo na mioyo huko Ughaibuni kwa akina Profesa Williams, anafaidi uhondo wa anthroposenia. Hata hivyo, ingawa vipuli vinasafirishwa Ughaibuni, asili ya vipuli vyenyewe ni mjini Daluta. Hivyo, jiji la Daluta linafanikisha anthroposenia. Uzunguni anakohamia Dkt Matoga na familia yake ni eneo linaloilinda na kuikuza anthroposenia. Alice anadhihirisha hili katika *Vipuli vya Figo* anapofafanua kuwa, "... Uzunguni. Kila jumba limezungushiwa wigo wa waya, michongoma, mageti na polisi – taabu! Mtu hana uhuru wala nafasi ..." (uk. 227). Mhusika Juma naye anaongeza kuwa Uzunguni mnaishi Wazungu, mapolisi na majibwa yao, ambao mwandishi anawasawiri kama walinzi na wapaliliaji wa anthroposenia, hasa katika nchi za Afrika tofautitofauti.

### 4.7 Wafisadi

Ufisadi kwa kawaida hurejelea aidha utumiaji mbaya wa rasilimali na mali ya umma, shirika, serikali au tabia ya kufanya uasherati na mke au mume wa mtu; utoaji na upokeaji wa chirimiri au hata utoaji wa maneno au vitendo vya chokocho au shari vinavyoweza kuharibu unyumba baina ya mke na mume (Wamitila, 2022; Ndalu na wengine, 2014; TUKI, 2014; Mdee na wengine, 2015; BAKITA, 2015). Kwa misingi hii, wafisadi ni watu ambao hushiriki hulka hii dhoofu. Mintarafu ya maelezo haya, wafisadi walidhihirika kama aina ya anthroposenia kupitia shughuli za kila siku za binadamu katika riwaya nne teule. Wafisadi hupalilia unajisi wa mazingira kwa kukuza ubinafsishaji wa mali ya umma katika mataifa mengi ulimwenguni, hasa barani Afrika. Ukuzaji huu huzalisha ongezeko la gharama ya maisha katika jamii.

Hata hivyo, ingawa wafisadi huathiri jamii kwa jumla, wachochole hupokea ncha kali ya upanga huu ilhali matajiri hulalia upande wenye kanda la usufi. Hivyo, wafisadi huwaathiri waduni kwa kiwango kikubwa na mara nyingi, ambao huwa wamepungukiwa na uwezo wa kiuchumi na huishi katika mazingira chafu na hatari kwa uhai wao (Smith, 2007). Wafisadi hupalilia uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa njia nyingi. Mathalani, huchangia ukiukaji wa sheria zilizowekwa kwa lengo la kuyalinda na kuyahifadhi mazingira katika mataifa tofautitofauti (Bardhan, 2017). Katika uchunguzi huu, mtafiti alibaini kwamba wafisadi hupalilia unajisi wa mazingira kama wanavyosawiriwa na waandishi wa riwaya nne teule. Nguzo zilizoongoza uchunguzi huu ni kama vile uwezo na kifo, haki na maadili ya kimazingira, uongozi mbaya, maendeleo endelevu na utandawazi.

Unajisi wa mazingira hushamiri katika mazingira yenye ufisadi, tamaa na ubinafsi-uchoyo. Kwa mujibu wa Lyakati katika *Bustani*, ufisadi unapalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Anamshauri babake kuwa afanye mahojiano na waandishi wa habari ili atangaze msimamo wa kiwanda cha kemikali cha Sagasaga kwa kukanusha maneno yote kuhusiana na mchango wa kiwanda katika uchafuzi wa hewa na mazingira ya Siza. Kadhalika, anasisitiza umuhimu wa babake kumwona Mhariri Mkuu wa gazeti la *New Era* na pia Jonalisti kwa lengo la kuwahonga waache kukemea uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya Siza wala kukabiliana na kiwanda cha kemikali. Kama alivyotaja Mkurugenzi wa *The Trans-American Chemical Products* kuwa viongozi wa nchi za Afrika ni bure tu na kuwa sheria za Shirika la Afya Ulimwenguni hutiwa kwenye kaburi la sahau, alikuwa sahihi kabisa. Hili linathibitishwa na Bwana Abdula anapomhonga mwenyekiti wa kamati ya kutoa leseni kwa kuyamwaga matofali lori tatu kwenye nyumba ya ghorofa moja.

Hatimaye, Bwana Abdula aliwatega na kuwanasa wajumbe kwa kuwatafutia watoto wao ufadhili wa kwenda kusoma nchi za Ughaibuni na wengine akawapa pesa taslimu. Kwa misingi hii hii, Bwana Abdula anapanga kuwahonga Mhariri Mkuu pamoja na Waziri wa Viwanda ili waunge mkono shughuli zinazosababisha uchafuzi wa mazingira. Mathalani, Bwana Omondo Kimondo kwa sauti nzito katika *Bustani* anaeleza kuwa, "Hakuna la maana kuhusu Mhariri Mkuu. Kubwa ni njaa tu. Na kila mtu ana bei yake." (uk. 52). Lyakati anapiga muhuri kauli hii kwa kusisitiza katika *Bustani* kuwa, "Mhariri Mkuu na Waziri wa Viwanda – wote sawa. Dawa yao moja. Itabidi uwaone." (uk. 52). Haya yanadhihirisha kuwa wafisadi hupalilia na kuchangia

kukua kwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Lyakati ni mwanasheria mwenye ufisadi na anautumia kuwalinda wachafuzi wa mazingira. Mwandishi anadhihirisha ukweli huu katika Bustani anapoeleza kuwa, "... Lyakati, mwanasheria aliyechanganya sarakasi za sheria na pesa ili kuwapiga mweleka mawakili wengine waliolumbana mara kwa mara mahakamani." (uk. 52).

Kwa misingi hii hii ya kupalilia wafisadi, Bwana Abdula, Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda cha Sagasaga hakutaka kashfa ya ajali iliyotokea kiwandani ivuje na kuvifikia vyombo vya habari. Hivyo, anatumia ufisadi kama ala ya kupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Ili kuhakikisha kuwa hakuna angethubutu kuzungumzia ajali ile, alikwenda hospitalini na mfuko wa pesa na akafanikiwa kuwahonga wote ambao wangetoa ushahidi au maoni kuihusu ajali ile. Hali hii ya binadamu kutumia wafisadi kama ala ya kupalilia unajisi wa mazingira bila kuufanya ufisadi wenyewe kuuendeleza unajisi huo, tofauti na aina iliyojadiliwa katika sehemu hii ya aina za anthroposenia ya wafisadi, inafafanuliwa na malalamishi ya Pasta Yona. Pasta Yona haridhishwi na kauli ya mmoja wa wafanyakazi kuwa, hamna wagonjwa waliokuwa wamepata ajali huko Sagasaga waliofikishwa pale hospitalini. Hili linamfanya akaripie vikali karani wa Mapokezi. Katika *Bustani*, Pasta Yona kwa hamaki anamwamrisha karani wa Mapokezi kuwa, "Mnakaa mnanunuliwa kwa visenti viwili vitatu ili kuuza damu na maisha ya ndugu zenu. Leta hilo buku upesi!" (uk. 13). Hili linadhihirisha kuwa binadamu anauza utu wake na kuutumikia uharibifu wa mazingira. Hali hii inawiana na kauli ya Nabea (2021) kuwa, kupitia ufisadi, hulka inayoendelea kudhuru nchi nyingi ulimwenguni, wafisadi wanaendelea kuvuruga uaminifu na kustawisha upotovu, hivyo kusababisha kutoweka kwa maadili ya watu punde tu viongozi wanapochukua kiti cha uongozi.

Wafisadi wanachangia upujufu wa mazingira pakubwa. Wafisadi kama aina ya anthroposenia wanawatatiza binadamu wengine katika shughuli zao za kila siku. Mathalani, Dzombo katika *Walenisi* anatatizika namna wafisadi waliweza kuonekana wazalendo katika mazingira chafu huku wazalendo wakionekana fisadi. Kwa upande mwingine, watu waliopalilia unajisi wa mazingira walionekana mashujaa ilhali waliokabiliana nao walionekana wasaliti wa wale fisadi. Katika mazingira chafu na dhoofu wauaji wanaonekana kama walinda usalama na wasema ukweli waonekana kama wehu. Aidha wasaliti wa mataifa mengi barani Afrika wanaonekana kama wenye busara na hekima. Hili linadhihirishwa na Dzombo katika *Walenisi* anaposema

kuwa, "...mjinga kuonekana mwerevu na mwerevu kuonekana mjinga; mwehu kuonekana timamu; muuaji kuonekana mlinda usalama; msema ukweli kuwa mwenda wazimu; na busara kutoka kwa wasaliti!" (uk. 13). Hivyo basi, wafisadi wanarutubisha upujufu wa mazingira na ufukara kwa kupofusha watu wengi na kuzalisha unajisi wa mazingira. Wafisadi, hususan viongozi fisadi huchangia pakubwa katika uvamizi wa rasilimali asilia kama vile misitu, madini na maji bila kuzingatia athari za muda mrefu kwa mazingira.

Dkt Matoga anapoendea vifaa vilivyotumwa na Profesa Williams vya kutumika katika upasuaji na uhifadhi wa vipuli vya figo na mioyo, kutoka Ughaibuni, Banko anamsaidia Dkt Matoga baada ya kupokea hongo ya shilingi sitini elfu. Anazigawa mara tatu; elfu ishirini zinaenda upande wa serikali, ishirini nyingine zinapewa michuzi na vijana na zinazosalia zinamfaa Banko mwenyewe. Banko anakiri kuwa alikuwa ameshazoea ufisadi. Mbogo anathibitisha hili katika *Vipuli* anaposema kuwa, "Baada ya miaka mingi ya tabia hii, sasa yamekuwa maradhi ambayo hayawezi kutibika ila kwa kustaafu ama kwa pingu mikononi." (uk. 56). Ufisadi wake Banko unaitia hadi serikali hasara kutokana na gharama ndogo ya kulipia vifaa vya Dkt Matoga, pale bandarini. Hili linaathiri uwezo wa serikali wa kutoa huduma kwa wananchi. Hivyo, wafisadi husababisha udhaifu katika mfumo wa sheria na udhibiti, kuruhusu shughuli za uchafuzi wa mazingira kufanyika bila kushughulikiwa ipasavyo au kuepuka adhabu.

Vilevile, ufisadi unakamilisha mchakato wa upaliliaji wa upujufu wa mazingira kupitia zawadi anayoitoa Dkt Matoga ya shilingi elfu sita kwa Mzee Makolokoza kama hongo inayobatizwa shukrani. Ushindi wa ajenti za unajisi wa mazingira hupatikani bila maafa kwa binadamu. Hili linadhihirishwa na Mzee Makolokoza anayemjuza Dkt Matoga kuwa ushindi wao utahitaji chombo cha kutengenezea kazi ile. Chombo chenyewe kitapatikana tu baada ya janadume kuaga dunia. Kifo cha janadume na ukataji wa sehemu zake za siri vinaashiria athari hasi za ufisadi ambazo hutishia uhai wa jamii yote kwa jumla. Mtunzi Mbogo anathibitisha hali hii katika Vipuli anapotaja kuwa, "Tutahitaji sehemu ya siri ya janadume." (uk. 151). Kwa kweli wafisadi hujali nafsi zao na mahitaji yao pekee bila kuwajali wengine. Hili hupelekea mapuuza ya maendeleo endelevu katika eneo husika. Hii inaweza kusababisha uwekezaji katika miradi isiyofaa kwa muda mrefu.

### 4.8 Mabeberu wa Kisasa

Mabeberu wa kisasa ni kisawe cha hali na udhibiti wa kiutandawazi; ambapo ni hali ambapo mbeberu alipoondoka na kuondokea mamlaka chini ya mfumo wa ukoloni mkongwe, Waafrika walioshika hatamu ya uongozi wakaanza kuendeleza nyenzo zile za mbeberu za uongozi na utawala kijumla kwa kutumiwa kama vikaragosi na viongozi wa mataifa yale yale yaliyowahi kuyamiliki na kuyatawala pamoja na mengine tajiri yenye uwezo (Mwirabua, 2014, Nkonge, 2014 na Waithiru, 2019). Wasomi hawa wanasisitiza kuwa mabeberu wa kisasa hushabikia na kupalilia mfumo unaoyapendelea mataifa ya ulimwengu wa kwanza huku ukiyadhulumu yale ya ulimwengu wa tatu. Hii ndiyo sababu, jamii nyingi duniani huupinga mfumo unaowazalisha mabeberu wa kisasa na kwa misingi hiyo kupinga utandawazi (Thiong'o, 1987). Hata hivyo, katika utafiti huu, mtafiti aliwaangaza mabeberu wa kisasa kama wanavyosawiriwa na Katama Mkangi na Emmanuel Mbogo katika riwaya zao nne teule za Kiswahili kama aina ya anthroposenia. Mabeberu wa kisasa wanazalisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira kijumla. Waandishi wa kazi za fasihi wamefanikiwa kuihamasisha jamii kuhusu haja ya kukabiliana na mabeberu wa kisasa kama aina ya anthroposenia ulimwenguni, hususani katika bara la Afrika. Katika sehemu hii mtafiti alichunguza mabeberu wa kisasa kama aina ya anthroposenia kwa kujijita katika vigezo vinne vikuu: uharibifu wa mazingira; udhibiti wa utawala na uchumi; ghashi za viongozi; na lugha na ubaguzi. Uchunguzi huu ulijifunga katika mipaka ya riwaya nne teule na kuongozwa na nguzo za uwezo na kifo, haki na maadili ya kimazingira, maendeleo endelevu na uongozi mbaya na utandawazi.

#### i. Uharibifu wa Mazingira

Uharibifu wa mazingira umedhihirishwa kama zao la mabeberu wa kisasa katika kazi nne teule za Katama Mkangi na Emmanuel Mbogo. Uharibifu wa mazingira katika anthroposenia huhusu shughuli za binadamu zinazosababisha mabadiliko hasi na ya kudumu kwenye mazingira na kwa maumbile kwa jumla (Ballard, 2023; Filipova, 2023; na Garrard, 2023). Matajiri wengi katika mataifa ya ulimwengu wa tatu hukiuka sheria na masharti ya kuyalinda mazingira yaliyowekwa na Wizara za Mazingira katika mataifa husika kwa lengo la kupunguza fedha za matumizi na badala yake kuongeza faida maradufu. Ingawa wanalielewa hili bayana huwalaghai wafanyakazi na wananchi kwa jumla wa nchi husika. Mathalani, ingawa Bwana Abdula anamaizi ukweli, anamweleza Pasta Yona wa Yona kuwa kampuni ya Cel ilikuwa inazingatia kaida na masharti yote ya Shirika la Afya Ulimwenguni kuhusu viwanda na uhifadhi

na utunzaji wa mazingira. Huu ni uongo unaofanikishwa na mabeberu wa kisasa katika kuendeleza unajisi wa mazingira. Ingawa Abdula analalamika kuwa kilichotokea katika kiwanda cha kemikali cha Sagasaga ilikuwa ajali, ukweli ni kuwa lilikuwa zao la utepetevu, utowajibikaji na uvunjaji wa kanuni zilizowekwa na Shirika la Afya Ulimwenguni za kumlinda mfanyakazi dhidi ya matukio hatari, kemikali sumu, vifaa hatari na masuala mengine mengi hatari.

Viongozi wengi barani Afrika wanachangia uharibifu wa mazingira kwa kutumia mamlaka na mali ya umma isivyofaa. Baada ya maafa ya watu hamsini mjini Siza wakati wa maandamano dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika *Bustani*, rais anaamuru kufungwa kwa kiwanda cha kemikali cha Cel. Ukweli ni kwamba, wakati kiwanda hiki kilikuwa kinasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, rais hakuwa anafanya chochote. Alikuwepo wakati akina Waziri, kamati ya leseni ya ujenzi wa viwanda, Bwana Abdula, Mkurugenzi wa The *Trans-American Chemical Products* na wengine walipokuwa wakiimarisha uharibifu wa mazingira kupitia ujenzi wa viwanda vya kemikali. Anthroposenia inanawiri nchini Siza na kusababisha mateso, dhuluma na maafa kwa wananchi waliowachagua viongozi wale. Kwa mujibu wa gazeti la *New Era*, agizo la kufungwa kwa kiwanda cha kemikali cha kampuni ya Cel kilichoko Siza lilitolewa baada ya maandamano makubwa yaliyofanyika kupinga uchafuzi na uharibifu wa mazingira hapo Siza. Kwa muda mrefu, anthroposenia imekuwa ikipaliliwa na kuzalisha madhara chungu nzima. Mathalani, kiwanda cha Sagasaga kinazalisha kemikali tofautitofauti bila kuzingatia sheria na masharti ya Shirika la Afya Ulimwenguni zinazohusu ulinzi dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Hakika hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo viongozi huruhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kuhalalisha sera na sheria zinazochangiz uchafuzi na uharibifu wa mazingira, hususani barani Afrika.

Baadhi ya athari hasi za unajisi wa mazingira ambazo zimepaliliwa na mabeberu wa kisasa ni pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira ya sehemu za Siza, hali mbaya ya hewa, maradhi ya ngozi, kifua, saratani, mvua za asidi na mito ya maji safi kuingia sumu baina ya nyingine nyingi. Chini ya mabeberu wa kisasa, wanaokabiliana na anthroposenia wanaangamizwa. Kwa mfano, Pasta Yona wa Yona katika *Bustani* anauawa na maiti yake kutupwa bondeni. Dhihirisho kuwa serikali ilihusika katika kifo chake ni habari zilizojaa utata zilizokuwa zimetolewa na msemaji wa Ikulu. Aidha, serikali yenyewe kupitia msemaji wa Ikulu inasema kwamba Mheshimiwa

Rais ameunda tume inayotarajiwa kuchunguza vifo vya wale wanaodaiwa kuwa waliuawa katika maandamano yaliyokuwa yamefanywa jijini Siza. Ukweli ni kwamba wanadaiwa kuuawa bali walikuwa wamepigwa risasi paruwanja na askari waliotarajiwa kuwalinda lakini wakachagua kukilinda kiwanda cha kemikali cha Saga Saga na kuwaangamiza wananchi wenzao. Hali hii inawiana na uongozi mbaya ambapo vitengo vya usalama hutumiwa na viongozi dhoofu kujilinda, kuwalinda wanaoyachafua na kuyaharibu mazingira, na kuwaangamiza wanaolalamika uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Chini ya mabeberu wa kisasa uchafuzi na uharibifu wa mazingira unasababishia wananchi wa Siza kuchubuka ngozi, vichwa vyao kuwauma kutokana na upele, miti kukauka na serikali inafumba jicho na kudidimiza jitihada za wananchi za kukabiliana na uharibifu ule. Wananchi kama vile, akina Jonalisti, Pasta Yona wa Yona, Pamela, Doricas, Wakili Mwaka na wengine wengi wanaaga dunia katika vita vya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika *Bustani*. Serikali inatumia propaganda kwa kuikoleza magazetini, redioni, vikaoni kanisani, na kwingineko kwa lengo la kuufumba umma macho usibainikiwe na athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira hata kama wanaendelea kuteseka kutokana na uharibifu ule. Hili linawiana na kauli ya Thiong'o (1987) kuwa, mabeberu wa kisasa wameendelea kutumiwa na Mbeberu kumpotosha Mwafrika kuhusu fasiri ya uhalisi wa Uafrika ambao vyombo vya habari vya Magharibi vimepepeta na kuupa umaarufu na kupelekea upotoshaji wa lengo kuu la kukabiliana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira pamoja na ufukara. Hili linaziba ukweli na kuwapofusha Waafrika ili wasibaini kuwa mabepari wa kisasa ndio chanzo cha matatizo mengi katika nchi za Afrika. Anapendekeza kuwa, suluhu mwafaka ni kuangaza mabeberu wa kisasa kwa kumulika utamaduni unaopalilia hali ya kukubali mambo yalivyo bila kuyatathmini wala kuyabadilisha.

**ii. Udhibiti wa Utawala na Uchumi**

Udhibiti wa kiutawala na kiuchumi ni hali ambapo utawala na uchumi huwa chini ya mamlaka ya watu maalum aidha moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja (Waithiru, 2022b). Kwa misingi hii, udhibiti wa kiutawala na kiuchumi ulirejelea hali ambapo ingawa mkoloni aliondoka mamlakani bado angali anatawala mataifa mbalimbali kupitia viongozi ambao ni vikaragosi na visesere vya wakoloni. Hivyo, kutokana na uwezo wa mataifa tajiri, huendelea kuyadhibiti yale fukara kwa kila namna (Thiong'o, 1987; Falola, 2024a). Mathalani, hili linadhihirika kupitia ubishi

unaohusu Sadam Hussein na Vita vya Ghuba pale nyumbani kwa Sheikh Ali katika *Bustani*. Kwa upande mmoja, mhusika Jonalisti anashikilia msimamo kuwa Sadam Hussein alikosea kuivamia Kuweiti. Kwa upande mwingine, Pamela anabisha kuwa wale watu wa Kuweiti wamenyonya na kuiba mafuta ya Iraq. Ingawa mgogoro kati ya Iraq na Kuweiti unajikita katika rasilimali, kila upande unanuia kutawala mwingine kiuchumi, kisiasa na pia kijamii. Ndiposa Kuweiti walifanya wizi wa kufyonza mafuta ya Sadam Hussein chini kwa chini na kisha kushusha chini kabisa bei ya petroli. Hakika hili linafungamana na nguzo ya uwezo ambapo mataifa tajiri yenye uwezo huyadhibiti mataifa fukara kiuchumi.

Kwa mujibu wa Sheikh Ali katika *Bustani*, Mfalme wa Kuweiti ni kibaraka wa Marekani anayeongozwa na tamaa, upumbavu na ubinafsi-uchoyo bila kujali matokeo yake. Viongozi wengi wanaoashiriwa na Mfalme wa Kuweiti hujali nafasi na nafsi zao bila kuzingatia uhai wa taifa lao. Hulka hii hurithiwa kutoka kwenye mbeberu kutokana na haja yake ya kutaka kumiliki na kutawala vyote bila kuwajibikia yeyote wala chochote. Katika anthroposenia, mataifa tajiri ya Ulaya, Marekani na mengine mengi yanafifisha yale fukara, hasa ya Afrika kiuchumi. Mathalani, Sheikh anasema katika *Bustani* kuwa, "Bush anatoka mbali huko kilomita maelfu kwa maelfu kuja kujitumbukiza katika mambo yasiyomhusu!" (uk. 59). Anaongeza kuwa Mfalme wa Kuweiti aliiba mafuta ya Iraq kwa sababu alikuwa ametumwa na Mmarekani. Wizi ule ndio uliosababisha Sadam Hussein na taifa lake kulivamia lile la Kuweiti. Huu ni udhibiti wa kiutawala na kiuchumi ambapo Mmarekani anataka kulitawala taifa la Iraq bila kuonekana kama analivamia kwa kutumia Kuweiti kama kikaragosi na chambo kwa Iraq. Hali hii inafungamana na nguzo ya utandawazi na ya uongozi mbaya. Kutokana na utajiri na uwezo – unaofungamana na nguzo ya uwezo – viongozi wa mataifa kwasi husababisha na kufadhili vita vya wenyewe kwa wenyewe na vile vya baada ya uchaguzi ili kuyafukarisha zaidi na kuyasukuma mataifa fukara kwenye bahari ya utegemezi kwa yale tajiri. Kwa mfano, zana za vita za nyuklia ambavyo ni hatari kwa ulimwengu zinaundwa na taasisi za serikali za mataifa kwasi ulimwenguni. Mwandishi Mbogo katika *Bustani* anaeleza kuwa, "CIA inajua fika kuwa Sadam yumo katika kuunda bomu la nyuklia." (uk. 60). Hali hii huambatanishwa na majaribio ya zana hatari za vita pamoja na chanjo zenye madhara makubwa hatari na ya kudumu kwa mwanadamu hususani baina ya Waafrika na mazingira yao.

Kimsingi, udhibiti wa visima vya mafuta vya Iraq unamaanisha kuwa Iraq inadhibitiwa kiuchumi madhali biashara ya mafuta huwa uti wa mgongo wa uchumi wao. Hivyo, katika anthroposenia mataifa tajiri yanatawala mengine kiuchumi na kutumia mbinu zozote zile kuhakikisha kuwa hakuna mengine yanayoyatisha yale tajiri. Jonalisti anaeleza kuwa, Mmarekani na Myahudi walijua dawa ya Iraq ni kuwatenga Waarabu ili kila wakati wazozane wenyewe kwa wenyewe, na kwa njia hii hawangepata muda wa kujiendeleza kiuchumi wala kijamii. Anadhihirisha hili katika *Bustani* anaposema kuwa:

> "... Mmarekani na Myahudi wakajiuliza: tufanye nini! Dawa ni kuwatenga Waarabu. Tuwafanye siku zote wagombane; kwa njia hii hawatakuwa tishio kwa taifa la Waisraeli. Hawatakuwa tishio kwa maslahi ya Wamarekani kwani wanataka siku zote wavidhibiti visima vya mafuta." (uk. 60).

Aidha, Jonalisti anadokeza kuwa si mara ya kwanza Marekani kukomesha mataifa yanayojiinua kiuchumi wala kujaribu kuyatawala na kuyaamulia juu ya uchumi na siasa zao. Anadhihirisha hili katika *Bustani* anapotaja kuwa, "Walimmaliza Ayatola na Iran, sasa wamepata mwanya wa kummaliza na kumpondaponda Sadam na Iraq." (uk. 60). Hakika hili linathibitisha kuwa mataifa tajiri huutumia uwezo wao kuyadidimiza mataifa duni kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa jumla. Hili linawiana na kauli ya LaMothe (2024) kuwa, mataifa yenye uwezo hunuia kuyatawala na kuyamiliki mataifa duni ili kuyatumia kama dampu la kemikali, chanzo cha wafanyakazi wa gharama ya chini, maabara ya majaribio ya dawa, chanjo na zana hatari za vita. Hivyo, kwa kuyafanya mataifa fukara daima yaishi yakizozana, viongozi wa mataifa tajiri hufanikiwa kuyadhibiti na kuyatawala mataifa yanayoendelea. Udhibiti na utawala huu hudidimiza maendeleo endelevu katika mataifa ya ulimwengu wa tatu na kuyasukuma kwenye dimbwi la lawama, chuki, njaa, utegemezi, maradhi na maafa kutikana na mambo yanayoweza kutatuli kwa wepesi na upesi.

Katika nchi za ulimwengu wa tatu, matajiri hawana imani na mbinu, mashine na madaktari wa nchi zao. Ndiposa Bwana Abdula anasisitiza kuwa bila tashwishi Zaituni atapelekwa Marekani kupata matibabu baada ya kuugua saratani kutokana na moshi wa sigara anazovuta mumewe, Bwana Abdula. Baada ya matajiri kuichafua hewa ya wananchi duni huishia kuichafua hewa yao wenyewe na kujisababishia

maradhi. Hali hii huchangia usawa katika maafa baina ya matajiri na maskini. Ingawa usawa katika kifo si jambo la kuvutia linadhihirisha kuwa, watu wasipoyajibikia na kuyasikitikia mazingira, wenyewe ndio wataangamia na kuyaacha mazingira. Hali hii inafungamana na nguzo ya maadili ya mazingira ambapo binadamu huhitajika kutathmini mbinu anazotumia kuingiliana na kutagusana na mazingira au aangamie. Aidha huhitajika kuimarisha nafsi inayoyajali mazingira kwa kila hali.

Katama Mkangi anadhihirisha kuwa mabeberu wa kisasa hunawirishwa zaidi na udhibiti wa utawala na uchumi. Dzombo anapotoka pale anapoabiri *Sayari* amesheheni athari hasi za udhibiti wa utawala na uchumi. Athari hizi zinasawiriwa kupitia mabeberu wa kisasa waziwazi bila hata kujaribu kuzibatiza. Kwa mfano, mwandishi wa *Walenisi* anaeleza kuwa, marubani ambao ni viongozi barani Afrika huwa kweli hawana uwezo wa kuumiliki usukani au uongozi kutokana na kudhibitiwa kwa kila hali na viongozi wa mataifa tajiri ya ulimwengu wa kwanza. Maadamu wao huwa viongozi au marubani bandia. Rubani kwa misingi hii anaashiria kiongozi na usukani unaashiria uongozi. Kwa misingi hii hii, marubani bandia wanaashiria viongozi wa mataifa fukara ya Afrika ambao hutawaliwa na viongozi wa mataifa tajiri ya Ulaya na Marekani. Viongozi wengi barani Afrika hufurahikia tu kuitwa viongozi pasipo hata kumaizi uongozi wenyewe uko wapi. Hali hii inafungamana na nguzo ya uongozi mbaya. Viongozi hawa pamoja na mataifa ya Afrika yanayorejelewa kama vyombo hutekwa nyara na viongozi wa mataifa tajiri ya Ulaya, Marekani na kwingineko na kutawaliwa bila hiari yao. Udhibiti huu huchangia ulofa na utegemezi dhidi ya mataifa tajiri ya ulimwengu wa kwanza.

Kwa mujibu wa nguzo ya uongozi mbaya na utandawazi, viongozi wa mataifa tajiri ya Ughaibuni hujificha nyuma ya ukoloni mamboleo kupitia utandawazi na kuwatumia viongozi wa nchi za Afrika kama wanasesere ama kifaa tu cha kuonekana kama kinyago. Katama Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* anataja kuwa, "Lau, washindwapo kuviegesha hivyo vyombo vyao kule waambiwako wavielekeze, basi hujikuta wakivurumishwa maporomokoni na miambani kwa makusudi, huku wakiachiwa kupiga mayowe." (uk. 8). Uegeshaji unaorejelewa na Katama Mkangi ni uongozi unaotawaliwa na Wakoloni kupitia viongozi wa Afrika. Vyombo navyo vinaashiria mataifa fukara ambayo viongozi wao wasipotii huwa yanatozwa riba ya juu ya mikopo yanayopewa mataifa haya na hivyo kutawaliwa kiuchumi. Aidha, mataifa haya fukara hunyimwa msaada na huteseka kutokana na ulofa katika

anthroposenia. Hivyo basi, anthroposenia hunawiri kupitia juhudi na jitihada za mabeberu wa kisasa.

Mara tu inapodhihirika kuwa mataifa haya fukara huenda yakajiangamiza kupitia vita vya kikabila, uraibu wa pombe haramu, maradhi, ukame na njaa, viongozi wa mataifa tajiri huwaondoa viongozi wa Afrika ambao ni wanasesere wao na mahali pao hupewa wanasesere wengine wenye asili ya Afrika. Hili huendeleza na kuwaimarisha mabeberu wa kisasa barani Afrika bila kikomo na hivyo kuendeleza anthroposenia. Hata hivyo, mataifa tajiri huepuka na kuambaa anthroposenia hata kama huwafaidi wao pakubwa. Mathalani, Dzombo katika *Walenisi* anajisemea kuwa, "Umpaye uwezo huu, basi yake yatakuwa ya kwanza; na yako ni ya kuning'inia ukingoni mwa viganja vyake yakingojea kutupiliwa mbali vishindo vidogo tu vizukapo." (uk. 8). Hakika hili linadhihirisha utumwa wa utegemezi wa mataifa ya Afrika kwa yale tajiri ya Ughaibuni. Hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya ambao hupalilia ulofa na hatimaye maafa.

Hali hii inawiana na kauli ya Thiong'o (1987) kuwa, mataifa mengi barani Afrika yamepigwa mnada na kuuzwa kwa Shirika la Kimataifa la Fedha analolirejelea kama Wizara mpya ya Kimataifa ya Fedha. Kadhalika, anasisitiza kuwa, kwa upande mmoja ni Ubeberu katika misingi ya ukoloni mkongwe na mabeberu wa kisasa ambao wanaendelea kumsukuma Mwafrika katika imani potovu kuwa; suluhu dhidi ya anthroposenia inaweza tu kupatikana katika njia inayoweza kufunguliwa tu na M-beberu ambaye amejihami na Biblia kwa mkono mmoja na bunduki kwa mkono mwingine. Hivyo, anasema kuwa, mabeberu wa kisasa na m-beberu wanaendelea kudhibiti utawala, uchumi, siasa, na tamaduni za Afrika katika anthroposenia. Mathalani, mrasimu anakiri kuwa udhibiti wa utawala na uchumi unawapalilia na kuwaimarisha mabeberu wa kisasa. Anadhihirisha ukweli huu anapomjuza Dzombo katika *Walenisi* kuwa wakubwa wa ukulima walifyeka mahindi yake kwa kufuata ushauri na uelekezi wa Benki ya Dunia. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo ambapo mataifa yenye uwezo huyadhibiti yale duni.

Mrasimu anafafanua kuwa, Benki ya Dunia yenyewe ndiyo iliyowashauri kuwa sehemu ile aliyokuwa amepanda mahindi Dzombo inapaswa kupandwa mazao ya kuliletea taifa fedha za kigeni. Hivyo, wakubwa wa ukulima na viongozi kwa jumla hawana tatizo kufyeka misitu lakini wana tatizo na mahindi yanayoweza kushibisha

wananchi. Hili linaashiria udhibiti wa utawala na uchumi wa mataifa ya Afrika kupitia mabeberu wa kisasa. Ndiposa mrasimu kwa fedheha anamwambia Dzombo kuwa, ushauri wa Benki ya Dunia ni wa kiutaalamu na unafaa kutiliwa maanani ila si kupuuzwa kwa kuwajali wananchi wanaoangamia kutokana na janga la njaa. Utawala unapodhibitiwa kupitia mabeberu wa kisasa unajijali bila kuwajali wananchi. Kwa mfano, mrasimu anamfukuza Dzombo kutoka kwenye ofisi yake kwa kugonga meza kwa nguvu. Ingawa Dzombo hakati tamaa anaendelea kudhulumiwa kupitia mabeberu wa kisasa. Hili linawiana na nguzo ya uwezo.

Dzombo anaporudi nyumbani anazingatia kanuni zote za wakuu wa ukulima. Anatayarisha shamba, analigawa na kupanda katani katika sehemu moja, majani katika sehemu nyingine, na miwa na pareto kwa nyingine. Anapalilia na kuitunza mimea yake. Muda huo wote hakujali kupiga foleni ndefu kwa kibaba cha unga wa chachu na maharagwe yenye vidudu. Hili linadhihirisha ulofa na utegemezi barani Afrika, ambapo serikali hushabikia kuwapa wananchi chakula kisichofaa cha misaada badala ya kuwapa mbegu bora, mbolea na mbinu za kisasa za ukulima ili kuijtegemea kama taifa. Kutokana na mabeberu wa kisasa mataifa ya Afrika yanategemea mataifa tajiri ya Ulaya, Marekani na mengine mengi na pia misaada na mikopo kutoka kwenye mashirika ya kimataifa mbalimbali na Benki ya Dunia. Hakika huu ni utumwa chini ya utawala na udhibiti wa mabeberu wa kisasa.

Udhibiti wa utawala na uchumi huendelea kuyadididimiza mataifa fukara kwenye bahari ya ulofa zaidi kila uchao. Mathalani, ingawa Dzombo anaambiwa na mkuu wa kilimo kuwa atafaidika sana kutokana na mazao yake, kwa sababu bei ya ulimwengu ilikuwa juu sana kwa wakati huo, bwana Karani anamtamausha anapomfahamisha kinyume cha mambo. Bwana Karani katika *Walenisi* anaeleza kuwa serikali inamdai Dzombo kwa sababu ya chakula alichokila – hata kama kilikuwa na vidudu – mbolea aliyotumia pamoja na mbegu alizopanda. Linalomtumbua Dzombo zaidi ni kufahamishwa kuwa tofauti na bei ya ulimwengu ilivyokuwa juu sana akipalilia, kwa wakati huo, kati ya kuyavuna na kabla ya kuyapeleka mazao kwa idara ya serikali, bei za ulimwengu ziliteremka kwa ghafla. Hili linaashiria udhibiti wa uchumi kupitia mabeberu wa kisasa. Dzombo anastaajabu namna udhibiti wa uchumi wao unatekelezwa paruwanja anapomuuliza Karani kwa hasira katika *Walenisi* kuwa, "Mbona basi watufanya wajinga hivi?" (uk. 20). Hali hii inaambatana na mihimili ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya uongozi mbaya na uwezo. Karani anamjuza

Dzombo kuwa bei ya mazao hutolewa na mataifa tajiri ya Ulaya, Uropa, Marekani na mengine mengi ulimwenguni pamoja na mashirika ya kimataifa yanayonufaika kutokana na udhibiti wa utawala na uchumi wa mataifa fukara, hususani ya Afrika.

Dzombo anafafanua kuwa, baada ya mahindi yake kufyekwa na akazingatia ushauri wa wakuu wa ukulima alilima mimea aliyoamini kuwa ingemletea pesa za kigeni. Hata hivyo, serikali iliyomshauri imemgeuza mwombaji wa hata chakula chenyewe. Zaidi na kuwa mwombaji, Dzombo anajipata ndani ya deni ambalo hakulifaidi kwa vyovyote. Hili linaashiria utumwa wa mabeberu wa kisasa katika nchi za Afrika. Karani anadhibitisha hili anapopambanua kuwa zile pesa za kigeni chache walizozipata watazitumia kulipia chakula walichowapa wananchi kama Dzombo. Dzombo katika *Walenisi* huku pumzi zikimnyonga anaongeza kuwa, "...sasa nijuacho ni kwamba niko maskini zaidi kuliko nilivyokuwa kabla ya kupanda mimea hii yenu!" (uk. 20). Karani anasisitiza kuwa watapewa mkopo na mataifa tajiri ya Magharibi ili waweze kuwakopesha wakulima ili nao wawalipe. Hakika hili linawiana na nguzo ya uongozi mbaya na ile ya uwezo. Kutokana na uongozi mbaya, mataifa fukara huendelea kufukarishwa na mataifa tajiri kupitia udhibiti wa uchumi na utawala.

Mzunguko huu unapalilia udhibiti wa uchumi na utawala. Kutokana na dhuluma za mabeberu wa kisasa wananchi wanasisitiziwa haja ya kulima mimea inayowatumbukiza kwenye bahari la umaskini. Kwa mfano, Karani katika *Walenisi* anasema kuwa, "Haya ndiyo maendeleo siku hizi, Bwana Dzombo." (uk. 21). Ukweli ni kwamba, katika anthroposenia, dhuluma na mateso kupitia mabeberu wa kisasa yanarejelewa kama maendeleo ya siku hizi. Dzombo kupitia kumbukumbu ya matukio mbalimbali, anadhihirisha kuwa vyombo vya dola kama vile polisi, wanatumiwa kulinda maslahi ya tabaka la juu. Hili linapalilia anthroposenia kwa sababu wale fukara wa tabaka la chini ndio ambao huathirika zaidi kutokana na utawala wa kibeberu. Kutokana na mabeberu wa kisasa udhibiti wa utawala inasawiriwa kupitia wafalme, marais, madikiteta na watawala aina aina ambao wanalinganishwa na mbari ya Wachuna katika *Walenisi*. Dzombo anasisitiza kuwa, kisababishi kikuu cha anthroposenia ni pesa ulimwenguni kote. Hili linafungamana na mhimili wa uwezo.

**iii. Ghashi za Viongozi**

Kiuyakinifu, ghashi za viongozi hususani katika mataifa fukara zinapalilia na kuendeleza mabeberu wa kisasa. Uongozi na utawala wa Siza unakuza na

kuwaendeleza mabeberu wa kisasa kupitia hadaa aina aina. Mathalani, Pasta Yona wa Yona anatibuliwa akili na ripoti ya serikali, ambayo inawaimarisha mabeberu wa kisasa badala ya kuwalinda wananchi kutokana na athari na matokeo hasi ya ghashi za viongozi. Hivyo, viongozi serikalini wanawaabudu na kuwasherehekea mabeberu wa kisasa kutokana na ubinafsi, tamaa na ufisadi wao kwa lengo la kudumisha anthroposenia ili kuimarisha siasa za ulofa na uongozi mbaya. Mhusika Pasta Yona anashangaa hadi anakatiza shughuli ya kufunga baada ya siku moja ili ahifadhi nguvu za kutosha kuandaa maandamano dhidi ya Cel na vilevile dhidi ya tamko la serikali lililowatamausha wengi na lililolinda na kuilea anthroposenia. Kupitia magazeti ya *New Era* na *Our Society* serikali ilikuwa imetoa tamko lililoandikwa kama vichwa vya kuhuzunisha. Gazeti la *New Era* liliandikwa kwa herufi kubwa zilizokolezwa rangi katika *Bustani ya Edeni* kuwa: *FEARS OF GAS IN SIZA UNFOUNDED – MINISTER* ilhali la Kiswahili lilitaja kuwa: WAKAZI WA SIZA HAWANA HAJA YA KUHOFIA AFYA ZAO! – WAZIRI (uk. 70).

Jambo hili linawatamausha wengi waliokuwa wanakabiliana na mabepari wa kisasa waliokuwa wanachafua mazingira kila uchao. Kwa upande mwingine, gazeti la *Our Society* katika *Bustani* lilitoa kauli kuwa: *FATHER YONA WA YONA SHOULD STOP INCITING WANANCHI – MINISTER* (uk. 70*)*. Hili lilimtamausha Pasta Yona wa Yona zaidi na likamtia mshawasha na motisha zaidi kuwa ghashi za viongozi zilizokuwa zikiimarishwa kupitia mabeberu wa kisasa zilihitaji ukakamavu na ujasiri zaidi. Lile la Kiswahili nalo katika *Bustani* liliandikwa kuwa: 'PASTA YONA WA YONA AACHE KUWACHOCHEA WANANCHI' – WAZIRI (uk. 70). Hata hivyo, Pasta Yona wa Yona anaelewa bayana kuwa haya ni matokeo ya ghashi za viongozi yanayozalisha mabeberu wa kisasa zaidi. Lengo kuu la ghashi za viongozi huwa kuwatisha au kuwapumbaza wananchi wenye hamaki katika utawala wa mabeberu wa kisasa, hususani katika mataifa ya Afrika. Hakika hili hufungamana na nguzo ya uongozi mbaya na utandawazi ya Nadharia ua Uhakikimazingira. Viongozi wengi barani Afrika huzitumia ghashi kuwarai wananchi wawapigie kura kipindi chao cha utawala kifikapo hatima. Ingawa wananchi wengi huishia kuingia kwenye mtego huu wote hulia na kuteseka kwa pamoja. Muhimu ni kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuwachagua viongozi mintarafu ya uchapakazi wao, sera na kauli mbiu zinazoshabihiana na uhalisi wa changamoto zinazoyakumba mataifa haya fukara.

Baada ya Pasta Yona kuyasoma magazeti yote mawili anazipigia mistari aya zote zinazomkera. Kwa mfano, anapigia mistari aya iliyosema kuwa; uchunguzi uliofanywa na mtaalamu wa serikali ulikuwa umethibitisha kuwa mvujo wa diyoksaidi ya Salfa uliotokana na asidi katika kiwanda cha Cel ulikuwa chini ya sehemu 0.001 kwa kila *ppm* milioni moja, kiwango ambacho kwa mujibu wa kile kinachopendekezwa na Shirika la Afya Duniani cha *ppm* 2 kilikuwa kiwango kidogo zaidi. Ripoti hii ilikuwa ya uongo baada ya Waziri wa Mazingira kuhongwa na Bwana Abdul. Halikadhalika, alipigia mistari aya katika *Bustani ya Edeni* iliyofafanua kuwa; uchunguzi wa wataalamu wa serikali ulikuwa umeonyesha kuwa hata wale walioishi nje ya Siza kwa wakati ule walikuwa wanaugua maradhi yaliyofanana na yale waliyokuwa wanaugua wananchi wa Siza. Ulaghai huu hupalilia uchafuzi wa hewa na hatimaye maradhi ambayo husababisha maafa baina ya wananchi katika duni ulimwenguni.

Waziri alitumia hila kuwatahadharisha wananchi dhidi ya uzushi wa Pasta Yona uliohitaji kupuuziliwa mbali. Hizi ni mbinu za utawala wa kimabavu na za kudhulumu wananchi kupitia ulaghai wa mabeberu wa kisasa katika anthroposenia. Waziri anadhihirisha kuwa mmoja wa mabeberu wa kisasa wazi anapotaja kibalagha kuwa Pasta Yona wa Yona angemtaja wazi yule bwana aliyekuwa amemwaga pesa mifukoni mwake Pasta Yona. Ingawa anamkumbusha kuwa kazi yake Pasta Yona wa Yona ni kuhubiri Neno la Mungu, anapalilia uongozi mbaya na kwa wakati huo huo kudai kuwa nchi ya Siza ilihitaji amani bali si fujo. Alimsuta Pasta Yona wa Yona kuwa aache kazi ya siasa na ikiwa alitamani siasa avue kola shingoni walumbane na waziri kwenye ulingo wa siasa.

Bwana Abdula katika *Bustani ya Edeni* anadai kuwa, “Ajali inaweza kutokea mahali popote na kwa mtu yeyote. Hata kwenye madhabahu anakosimama Pasta Yona wa Yona na kuhubiri ajali inaweza ikamtokea ...” (uk. 71). Hili linaashiria kuwa, kupitia mabeberu wa kisasa anthroposenia inatisha adui zake hadharani, ikizingatiwa kwamba Bwana Abdula anaashiria anthroposenia na adui wake anaashiria adui wa anthroposenia – Pasta Yona wa Yona. Bwana Abdula anashikilia msimamo kuwa hana mpango wowote wa kukifunga wala kukiondoa kiwanda cha Cel pale eneo la Siza. Bila woga mabepari wa kisasa wanaipa anthroposenia uthabiti na uhakika kuwa ikiwa mna cha kuhamishwa ni Parishi ya Pasta Yona wa Yona ila si Cel kwa kuwa sehemu ile ilikuwa imetengewa viwanda zamani kabla ya Parishi kujengwa. Ukweli

ni kwamba huu ni uongo unaoendelezwa na kusambazwa na watawala fisadi na wenye ubinafsi na tamaa. Hila hizi huwaimarisha mabeberu wa kisasa katika mataifa mengi barani Afrika, jambo ambalo hunawirisha ulofa na maafa ya watu kutokana na maradhi yanayoweza kuepukika. Hali hii huwiana na nguzo ya uongozi mbaya na utandawazi.

Baada ya Pasta Yona kuona ishara za ajabu na kupumzika pale vesteri katika *Bustani*, anafungua mlango na katika kasi ya umeme ananyakuliwa, anatekwa nyara na kuingizwa ndani ya gari aina ya *Range Rover* ya rangi nyeupe. Tukio hili linadhihirisha ghashi za viongozi hususani katika mataifa ya Afrika katika kuwalinda na kuwadumisha mabeberu wa kisasa. Makachero wale wanne wanaovurumisha gari wananuia kumnyamazisha Pasta Yona wa Yona ili akome kukabiliana na anthroposenia. Bwimbwi la vumbi lililopaa juu hewani kabla ya kutua juu ya vichwa na kope za macho ya waumini linaashiria anthroposenia katika maeneo ya ulimwengu wa tatu yanayotawaliwa na mabepari wa kisasa. Hali hii husababisha upofu baina ya wananchi ambao husababishwa na ghashi za viongozi kupitia mabeberu wa kisasa.

### iv. Lugha na Ubaguzi

Kupitia Mtu-Bint Hekima inadhihirika kuwa ubaguzi hupalilia anthroposenia kupitia mabeberu wa kisasa. Ubaguzi ni zao la mabeberu wa kisasa ambapo uhusiano wa kiubaguzi kati ya tajiri na walalahoi hudhihirika. Ubaguzi unadhihirika kupitia mbinu zilizo ndani ya mifumo ya uchumi-siasa wa wale wachache wenye nguvu, uwezo na mamlaka – walalahai – katika kila jamii. Lugha kama chombo cha mawasiliano na kitambulisho cha jamii inatumiwa kufanikisha mabeberu wa kisasa katika harakati za kuimarisha anthroposenia katika riwaya mbili teule. Mathalani, Mtu-Bint Hekima katika *Walenisi* anasisitiza kuwa, “Aghalabu, mifumo mingi huruhusu wachache kuwalaghai wengi kwa ujanja. Na wafanyavyo hivyo huweza kujirundikia mali ama utajiri wa kibinafsi na kuufanya ni urithi wa aila yao tu.” (uk. 84). Mtu-Wazo anaongeza kuwa ubaguzi huzalisha watu wenye ubinafsi, hivyo huwa na wake wengi, ng’ombe wengi, mashamba mengi na makubwa, viwanda, majumba tele, malaki ya pesa kwenye maghala, mivunguni na mafichoni, ilhali wanyonge wengi hawana hata chembe. Mabebeberu wa kisasa wanaimarika na huwepo kudumisha na kupalilia Kabila Tajiri na Kabila Maskini. Hili linadhihirishwa na Mtu-Bint Fikirini anapoeleza kuwa, anthroposenia katika mataifa mengi duniani hugubikwa na miondoko iliyo kwenye mazingaombwe ya siasa, mila, desturi, dini na falsafa ya watawala ama

mtawala au kiongozi wa taifa husika. Hali hii hufanikishwa na ubaguzi na lugha inayowapigia upatu mabeberu wa kisasa.

Kwa misingi hii hii, mabeberu wa kisasa wanadhihirishwa na kuimarishwa na lugha ya Kiingereza. Mzee Mtu-Mwenzio anafafanua kuwa, lugha hii ni *Iblish* ambayo ndiyo lugha ya kiutawala mle Jehanamu. Kauli hii inafungamana na maelezo ya Oliver (2016) anayefafanua kuwa, kwa mujibu wa Ngugi, lugha ya Kiingereza ni mojayazo ya ala alizotumia na bado anatumia kumdhibiti Mwafrika chini ya utawala wa mabeberu wa kisasa. Mwandishi anathibitisha ukweli huu katika *Walenisi* anapofafanua kuwa, "... huyu huyu Dzombo aliyetokomezwa kutoka duniani na tawala za dhuluma zilizojitia utukufu, ukweli, haki na usawa?" (uk. 89). Mabeberu wa kisasa wanaendelea kusawiri anthroposenia kupitia sheria za kiuchumi zilizozalisha fukara wengi. Shetani kwa misingi hii anaashiria viongozi dhalimu ambao hushamiri kupitia ulinzi na uhifadhi wa mabeberu wa kisasa katika mataifa mengi barani Afrika na hupalilia anthroposenia. Dunia inasawiriwa kama Jehanamu, ambapo athari hasi za anthroposenia hutatiza watu kila uchao. Hakika hili liwiana na nguzo za uongozi mbaya na utandawazi.

Katika mataifa mengi barani Afrika, pombe haramu, dawa za kulevya, kemikali sumu pamoja na chanjo hatari zinazofanyiwa majaribio hutawala na hatimaye huzalisha anthroposenia katika misingi ya ubaguzi (Waithiru, 2022a). Mtunzi Mkangi anadhihirisha hili kupitia wahusika Dzombo, Mzee Matingasi na Maskini Jeuri. Mzee Matingasi anadhihirisha ubaguzi na ulofa unaonawirisha anthroposenia anaposhiriki ugema na kula vya walevi fukara waliobaguliwa. Mangwe ni taashira ya mataifa mengi fukara na machafu barani Afrika. Mangwe yenyewe hayakuwa na leseni na hivyo hayakuwa halali. Hili linawiana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo viongozi huruhusu biashara haramu na uharibifu wa mazingira mradi tumbo zao zishibe. Mabeberu wa kisasa hupalilia biashara haramu, ambapo fukara huwa hawana anayewajali hata wakibugia sumu kwa pupa, kama vile pombe haramu (Smith, 2007). Linalohakikishia Mzee Matingasi biashara bila usumbufu kutoka kwa serikali ni wepesi wake wa kuwapa mlungula kuwanyamazisha. Mwandishi anaeleza katika *Walenisi* kuwa, "Kwa yeyote yule askari mpekuzi mja-wa-njaa, mlungula ulimkomesha." (uk. 91). Hili linaashiria kuwa, ulofa unapalilia ubaguzi na hatimaye mabeberu wa kisasa pakubwa. Mzee Matingasi alikuwa anahepa mkono mrefu wa serikali kwa ukarimu wake wa hongo ya aidha, chupa mbili au tatu za chang'aa au

hata wakati mwingine pesa taslimu kuwahonga askari. Ufisadi unamhakikishia Mzee Matingasi biashara shwari kila jioni, unaopaliliwa na mabeberu wa kisasa na kwa jumla hali hii inazalisha na kudumisha ubaguzi.

Anthroposenia inasawiriwa kupitia mabeberu wa kisasa pale ambapo wananchi wanakengeushwa na uongozi na utawala kimwavuli. Kijana Mtu-Wazo katika *Walenisi* anaeleza kuwa, katika enzi ya Wachuna, uongozi ulikuwa dhalimu na vijana hawakuwa na faida kubwa kwa jamii. Hili lilipelekea wao kuchukuliwa kama wazushi wa bughudha hasa kiuchumi na wanajamii wengine kwa kubaguliwa. Sababu kuu ya wao kuwa vimelea ni jitihada za mabeberu wa kisasa katika misingi ya uongozi mbaya na ubaguzi, ambapo anthroposenia hunawiri (Mukherjee, 2010). Kijana Mtu-Wazo katika *Walenisi* anasisitiza kuwa, katika anthroposenia, wanaume hupoteza nguvu zao kwa kushiriki uasherati ilhali wasichana nao humaliza nguvu zao wakijibidiisha na umalaya. Asili ya hali hii ni ukosefu wa fursa ya kuzalisha mali, jambo ambalo huwafanya vijana wengi kupevuka kuwa majangili, wakora na kuishia kuwa gerezani na hatimaye hufia mle gerezani. Hivyo, gereza na uongozi mbaya huzalishwa na mabeberu wa kisasa ambao nao huzalishwa na ubaguzi katika janibu zinazoimarisha ghashi za viongozi. Hili linawiana na nguzo ya uongozi mbaya.

Katama Mkangi anaashiria hili katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, "... watawala hawakujali uele wa hali hii ambayo iliwageuza hawa nzige kuwa sawa na makapi tu." (uk. 108). Hata hivyo, Katama Mkangi anadhihirisha kuwa ubaguzi unaweza kudidimizwa na halafu mabeberu wa kisasa wanaweza kuangamizwa. Mtu-Wazo anadhihirisha kuwa ubaguzi hudidimizwa na uzinduzi wa vijana kutoka kwenye lepe lisababishwalo na mabeberu wa kisasa. Hili hufanikishwa na uongozi bora unaokijali kizazi cha leo na cha kesho kwa wakati mmoja. Mathalani, katika Walenisi waliochukua hatamu za utawala baada ya Wachuna ni Wawalenisi. Jamii ya Wawalenisi iliwapa vijana fursa ya kuzalisha uchumi. Kijana Mtu-Wazo katika *Walenisi* anataja kuwa, "Sasa njoo ushuhudie mwenyewe uwezo wa vijana-chipukizi waliozinduka kwa kukubali kutorudi nyuma ili wawe magugu ya wengine wachache wenye nguvu." (uk. 108). Hakika vijana wakizinduka kutoka kwenye giza la ujinga, dawa za kulevya, pombe haramu na ulofa unaopaliliwa na viongozi wabaguzi wanaotumia lugha ya kuwafanya vijana watamauke maishani, wanaweza kuzalisha usawa, haki na maendeleo endelevu kwa upesi na wepesi. Ingawa hili linakiuka

misingi ya nguzo ya uwezo ambapo wenye uwezo huwatumikisha waduni, linatoa suluhu kwa janga la anthroposenia linaloshamiri kupitia mabeberu wa kisasa.

**4.9 Mabepari**

Wamitila (2022), BAKITA (2015), Mdee na wengine (2015) na Ndalu na wengine (2014) wanaeleza kuwa, ubepari ni hali ya uchumi wa kuwezesha watu wachache kuwa na mali nyingi na kumiliki uchumi wa nchi. Mabepari kupitia ubepari ni mojawapo ya aina za anthroposenia. Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 243), anaeleza ubepari kama: Dhana hii hutumiwa kuelezea aina ya mfumo wa uchumi au jamii ambapo sifa ya ubidhaaishaji wa mali, nguvukazi na maarifa huchukua nafasi kubwa sana. Wamitila (2003: 244) anafafanua ubidhaaishaji katika ukurasa huo kuwa: Hii ni dhana muhimu katika uhakiki wa kimarx. Karl Marx aliitumia dhana hii kuelezea kitu ambacho kinazalishwa katika jamii, lakini sio kwa nia ya kutumiwa na waliokizalisha bali kwa kukibadilisha katika mfumo wa kibepari wa soko. Andermahr, Lovell na Wolkowitz (1997: 29) wanaeleza dhana ya ubepari kama: “Aina ya uchumi au jamii ambayo ina sifa za ubidhaaishaji wa rasilimali, nguvu-kazi na maarifa ... mfumo ambao una sifa kuu ya unyanyasaji.” Hivyo, mabepari kupitia ubepari husawiri anthroposenia moja kwa moja. Ubepari, kando na kuzalisha ushindani uliogubikwa na ubinafsi-uchoyo dhidi ya rasilimali, huwasilishwa kama unaowapokonya watu uwezo wao wa kudadisi na kutathmini masuala yanayohusiana na maadili, utamaduni na sanaa (Siundu, 2011). Mihimili iliyoongoza uchunguzi wa aina hii ya anthroposenia ni pamoja na uongozi mbaya, kifo na uwezo, na utamaduni na mazingira.

Katama Mkangi anasawiri dhuluma katika *Walenisi* kupitia wahusika kadhaa wanaoashiria mabepari. Kwa mfano, nduguye Dzombo anaenda kumuomba mwajiri wake akubali kunyonywa naye ili nduguye Dzombo aweze kuishi sawa kama tajiri. Katika anthroposenia, mataifa tajiri yanayanyanyasa mataifa fukara, hasa barani Afrika na kunufaika yao yenyewe huku Afrika yakifukarika zaidi kutokana na unyonyaji wa kiuchumi, kijamii, kisiasa, kieliemu na pia kunyonya rasilimali za wataalamu aina aina. Hali hii inafungamana na nguzo za uwezo na utandawazi za nadharia ya Uhakikimazingira. Ingawa nduguye Dzombo haelewi maana ya kunyanyaswa, Dzombo hajakosea kumwambia kuwa, hali yao ya ulofa inazalishwa na unyanyasaji wa walalahai dhidi yao walalahoi. Hivyo, mabepari wanapalilia maangamizi pakubwa.

Kwa misingi hii, tajiri wa nduguye Dzombo anawanyonya wafanyakazi wake kimwili, kimawazo na kiuchumi. Unyonyaji huu unampa utajiri mwingi kwa kupata wafanyakazi wasiogharimu fedha nyingi kuwalipa mishahara lakini wanaofanya kazi nyingi, kwa muda mrefu, ngumu na kwa njia madhubuti. Hakika anawanyanyasa wafanyakazi fukara kama alivyotaja Dzombo madhali nduguye Dzombo anapouliza maana ya kunyanyasa, kwa haraka tajiri katika *Walenisi* anajibu kuwa, "Haina maana yoyote, na hakuna neno kama hilo." (uk. 15). Tajiri anawakemea na kuwafukuza Dzombo na nduguye ili aendelee kufaidi kutojua kwao na aendelee kunufaika na huduma zao kwa kuwatapeli. Ndiposa anamwonya nduguye Dzombo asimsikilize nduguye tena ili tajiri aendelee kupalilia dhuluma na maonevu kupitia matunda ya ubepari.

Ili tajiri huyu aweze kuendeleza dhuluma kupitia mabepari, anamfuta kazi Dzombo siku hiyo hiyo kwa tuhuma za kuwachochea wafanyakazi watiifu. Ukweli ni kwamba Dzombo alikuwa anamwambia nduguye ukweli kuhusu maangamizi na hila ambazo hutumia kujiendeleza yenyewe ila si kuwachochea wafanyakazi kupitia nduguye. Aidha, wafanyakazi wanaorejelewa kama watiifu wanatii kutokana na ukosefu wa elimu baina yao. Hawajui haki zao na hivyo inakuwa rahisi kwa tajiri kuwatumia kupalilia ubaguzi na dhuluma. Punde tu Dzombo anapotisha mbepari anafutwa bila hata onyo wala ilani. Maadamu siku iliyofuata asubuhi Dzombo hakuruhusiwa hata kuvuka kizingiti cha mlango. Madhali askari mlinda zamu wa siku hiyo alimpa kijibarua kilichomjuza Dzombo kuwa alikuwa amefutwa kazi. Mabepari wanaopalilia ubepari ili kuimarisha maonevu na maangamizi, wanaburudika wakiona jinsi wananchi fukara wanavyonyenyekea mbele ya mabepari ikizingatiwa kuwa tajiri ni taashira ya bepari halisi. Kwa mfano, tajiri anafurahia kumuona nduguye Dzombo akizungumza kwa unyenyekevu mbele yake, anapomuuliza Dzombo katika *Walenisi* kuwa, "Umesahau pale juzi uliponiambia kuwa ufukara wetu unatokana na kunyanyaswa kwetu?" (uk. 15). Mabepari kando na kuwaogofya watawaliwa huendesha shughuli za uzalishaji na utumiaji zinazotegemea matumizi makubwa ya nishati, malighafi na bidhaa, bila kujali athari zake kwa mazingira na afya ya binadamu na viumbe hai wengine.

Mwandishi Mkangi katika *Walenisi* anaeleza kuwa, Dzombo anazuiliwa kulima mahindi na kuhimizwa apande mimea inayoletea taifa fedha za kigeni. Kama mwananchi mzalendo Dzombo anazingatia na kuufuata ushauri wa wakuu wa kilimo

na kulima kahawa, kakao, pareto, na maua ya waridi, lakini akitarajia kunufaika anapata kuwa mawakala wa mabepari, kupitia ubepari ndio wanaonufaika. Jambo hili linamfilisisha Dzombo kiuchumi na kumbadili kutoka mkulima mdogo hadi mwombaji. Anakiri hili anapolalamika katika *Walenisi* kuwa, “Hii leo mwaniambia licha ya kukosa pesa, pia niko ndani ya deni ambalo sikulilalia ...” (uk. 20). Hili linathibitisha kuwa, kando na mabepari kushamiri katika mataifa fukara, hurutubisha ulofa nao ufukara huyakuza mauti. Hivyo, ufanisi wa mabepari na ufukara huwa na uhusiano wa kisimbiotiki.

Mathalani, Dzombo anafilisika zaidi kiuchumi akiwa Duniani mwao ambapo dhuluma na maonevu ya kimazingira hutawala. Nyumbani kwake Dzombo kunadhihirisha ulofa hupalilia mauti kama zao la ubepari. Baada ya muuza duka kukataa kumuuzia mafuta ya taa, anarejea nyumbani akiwa na hasira na huzuni tele. Giza linaloashiria maangamizi linamdhihirishia mianya chungu nzima katika paa lake. Kuta za udongo za kibanda kile chake zilikuwa na viraka vya kanja, makuti mabovu, na makaratasi ya makatoni. Chumba hiki ni kidogo, kiwango kwamba, pale walipokuwa wameketi yeye na Maskini Jeuri, ndipo palipokuwa pa kulala, kupikia, kuzungumzia na pa kila kitu ambacho nyumba ya kawaida ya binadamu mwenye akili razini yapaswa kuhifadhi na kusitiri kwa heshima ya utu. Nyuma ya kijumba kile ndiko kulikokuwa kwa haja ndogo ilhali kubwa iliachiliwa msituni. Ikizingatiwa kwamba haya yote yanambainikia Maskini Jeuri, hili linadhihirisha kuwa mabepari huzalisha ufukara kutokana na ubepari. Utupaji wa kinyesi msituni huchangia uchafuzi wa mazingira. Sahani za plastiki, sufuria za viraka, vikombe vya mapengo, makopo ya kubonyeka na kukwajuka, vifaa vya kazi kama vile; mundu, panga, jembe, koleo, nyundo na karai; ndivyo vifaa vya thamani walivyomiliki Dzombo na familia yake, mvunguni mwa kitanda kilichotandikwa matandiko ya mchwaramchwara.

Mabepari hupinga juhudi za kuanzisha au kutekeleza sera na sheria za kulinda na kuboresha mazingira, kama vile kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, kudhibiti uchafuzi wa hewa, maji na ardhi, na kuhifadhi bayoanuwai na rasilimali asilia. Aidha, hutumia ushawishi wao wa kisiasa na kiuchumi kwa kushirikiana na serikali, mashirika na vyombo vya habari kwa kutoa taarifa potofu, kuficha ukweli kudhoofisha hoja za wale wanaotetea maslahi ya mazingira na jamii. Mabepari hufaidika na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na wengine, kama vile kwa kuuza bidhaa au huduma zinazotatua au kupunguza madhara ya uharibifu huo, au kwa

kuchukua fursa za kiuchumi zinazotokana na mabadiliko ya mazingira. Hivyo, mabepari huwa chanzo cha utepetevu wa binadamu kwa kuendeleza mfumo wa kiuchumi na kijamii unaotilia mkazo faida na ukuaji bila kujali gharama na madhara kwa mazingira na viumbe wengine.

Nguo zote za familia ya Dzombo zilihifadhiwa kwenye kabati la ukambaa uliokuwa umefungwa fitoni kuta mpaka kuta. Kadhalika, ukambaa huu ndio uliokuwa ukuta uliogawa chumba cha malazi na sebuleni. Matajiri ambao hupalilia ujeuri hunufaika ilhali fukara huendelea kunyanyaswa jinsi tu manyanyaso yanavyonawiri. Mwandishi anasawiri kuwa, unyonge hudhihirika hadi kwenye giza – taashira ya anthroposenia. Hii ndiyo sababu Maskini Jeuri anaweza kuyashuhudia yote chumbani mwa Dzombo kukiwa na giza, baada ya kibatali kulipuka. Mwandishi anasema katika *Walenisi* kuwa, "Umasikini ni ung'arie gizani usije ukapofusha waungwana!" (uk. 73). Ingawa hii ni tashtiti ya uduni, ukweli ni kwamba mabepari huwanyonya wanyonge huku wakiwanufaisha matajiri wenzao. Aidha huwanenepesha matajiri huku wakiwakondesha maskini kuliko unyasi. Mabepari ni wanyonyaji wa rasilimali na nguvu kazi na huchangia ongezeko la ulofa kwa kudhibiti na kugawa mapato na mali kwa manufaa yao wenyewe.

Ubepari unadhihirika paruwanja ndani ya msafara wa siafu na mazingira yake. Katika riwaya ya *Walenisi*, mhusika Mtu-Bint Fikirini anafafanua kuwa, uhusiano na ushirikiano wa siafu unaashiria ubepari ambao unasawiri shughuli za kawaida za mabepari. Mle ndani katikati kabisa mwa msafara wa siafu mna siafu wadogo wadogo wengi sana ambao wanaenda nyuma na mbele bila kupumzika. Wanajikakamua kubeba mizigo. Hali hii inaashiria hali halisi katika mataifa mengi fukara barani Afrika, ambapo wananchi fukara hufanya kazi ngumu za sulubu na kulipa ushuru kwa meno na ukucha ilhali wananchi matajiri hunufaika tu bila hata kutoa ushuru. (Moseley na Otiso, 2023). Hali hii hudumisha mabepari katika mataifa mengi barani Afrika. Siafu hawa wadogo wadogo wanapoendelea na ubebaji mizigo bila kikomo, kuta zinazowazingira kwenye barabara wanayoipitia zimejengwa na siafu wenzao wakubwa. Siafu wakubwa wanaashiria asasi, wizara na idara za serikali ambazo hutumiwa katika misingi ya ubepari kuendeleza anthroposenia. Hili linawiana na kauli ya wasomi wengi kuwa, vyombo vya dola kama vile polisi, hutumiwa na viongozi dhalimu barani Afrika kuilinda na kuikuza anthroposenia (De Cristofaro na Cordle, 2018).

Kadhalika, juu ya siafu hawa wakubwa wanaojenga kuta za barabara, mna wale siafu wenye kiuno chembamba na tumbo dogo, ambao huwa na kichwa kilicho machonge tu. Hawa nao wameshikana meno kwa meno wakimenyana na kuitutumua mori bila kuwajali wala kuwasikitikia wengine. Napo pale nje ya msafara huo mna siafu wale wakubwa kabisa ambao machonge yao yamekaa kama makoleo makubwa ambayo wanayapitisha huku na huku jinsi askari makachero barani Afrika wafanyavyo. Siafu wenye kiuno chembamba, tumbo ndogo pamoja na kichwa kilicho machonge wanaashiria wananchi wa tabaka la kati barani Afrika. Wananchi hawa huzozania mali na vita vya wenyewe kwa wenyewe hujikita katika migogoro ya kiuchumi. Migogoro hii hupalilia anthroposenia kupitia ubepari ambao hunawiri kutokana na migogoro hii. Hili linawiana na kauli ya Clark (2015) kuwa, wananchi hawa huendeleza vurugu dhidi ya mazingira na kwa njia hii hupalilia unajisi wa mazingira.

Kwa upande mwingine, siafu wale wakubwa kabisa wenye machonge yaliyokaa kama makoleo makubwa wanaashiria viongozi katika wizara tofautitofauti katika nchi za Afrika, ambao hutumiwa na viongozi na watawala vikarogosi wa mataifa fukara ya Afrika kuendeleza na kupalilia mabepari. Watson na Watson (2007) wakikubaliana na mawazo ya mtafiti wanaeleza kuwa utabaka huzalisha utumwa, ambao huzalisha mabepari. Mtu-Bint Fikirini anafafanua kuwa, Wachuna waligeresha watu kwa kuwafananisha sawa na vidudu. Walishikilia msimamo kuwa akili ya binadamu ni sawa tu na ile ya siafu, nyuki au hata mchwa. Ingawa waliwadunisha wananchi wenzao hata wao walijitusi katika harakati za kujitajirisha kutokana na tamaa, ubinafsi na unafiki wao wa kutaka kuhakikisha ubepari kupitia mabepari machoni mwa wale siafu, nyuki na mchwa wadogo. Mtunzi Mkangi kupitia mhusika Dzombo katika *Walenisi* anayasawiri mataifa fukara ya Afrika kama chanzo cha mabepari kupitia mizinga ya nyuki na vichuguu vya mchwa. Anadhihirisha hili anapotaja katika *Walenisi* kuwa, "... mizinga ya nyuki na vichuguu vya mchwa viko namna hii." (uk. 103). Hii ni kwa sababu, katika mizinga na vichuguu, wafanyakazi, wasimamizi na nokoa hudhihirishwa bayana kupitia majukumu yao. Utabaka hupaliliwa ambao huzalisha ubepari kama zao la mabepari. Mtu-Bint Fikirini anakiri kuwa, katika mazingira chafu, wataalamu bandia wa elimu-jamii na viongozi fisadi hushamiri kama zao la ubepari. Wakati wa utawala wa Wachuna, ubepari ulisawiriwa kinagaubaga. Utawala wao ulijikita katika misingi ya unyanyasaji wa watu na propaganda. Vijana na wanajamii kwa jumla waliteseka kutokana na shughuli za

mabepari. Mtu-Bint Nena anadhihirisha hili katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, “Kuombaomba ndiko kulikuwa maisha yao na mwisho kifo kikawa mkombozi wao.” (uk. 114). Mabepari hushamiri katika maeneo yanayotawaliwa na kifo. Hii ni kwa sababu, mabepari huzalisha maafa kupitia hulka ya kuyapujua mazingira halisi na unajisi wa ikolojia kwa ujumla. Hili linawiana na nguzo ya uwezo na kifo.

Mwito huu unaanzisha uhusiano mpya kati ya Wawalenisi na vifaa vyao vya uzalishaji mali, hasa ardhi. Mwito huu unawezesha utekelezaji wa msimamo wa chakula kwa wote ili kukabiliana na njaa. Udongo kwa Wachuna haukuwa chombo cha kuzalisha chakula ila rasilimali ya kuchezea kamari kwa minajili ya kupalilia ubepari, kupitia kujipatia utajiri wa kibinafsi kwa Wachuna wakiwa bado wamestarehe kitandani. Walivuna wakiwa kitandani kwa sababu walikuwa wamewaajiri watu kwenye mashamba yao ama kuyakodisha kwa aliyekuwa na fedha za kukodi. Kwa misingi hii, aliyelima hakuwa na shamba ilhali yule ambaye hakuwa analima alikuwa nalo. Hali hii ilipalilia mabepari. Kwa mfano, Mtu-Bint Nena katika *Walenisi* anaeleza kuwa, “Lao likawa ni kuchukua kodi tu na kunenepa kwa jasho la wengine.” (uk. 114). Mabepari humiliki na hudhibiti rasilimali za kiuchumi na kisiasa kwa manufaa yao wenyewe. Hakika huwa hawajali watu wengine wanaoangamia kutokana na maradhi, njaa na ukosefu wa maji kwa watu na mifugo.

Katika ubepari, kigezo muhimu na kikuu cha maendeleo ni ubaguzi. Dzombo anawaeleza wajumbe wa Kamati Kuu ya Kiwanda cha Trimi kuwa, kwao Duniani ni watu wachache sana na tena wa ngozi nyeupe tu ambao huwa na akili ilhali wananchi wengi huamrishwa tu kama wanyama. Waithiru (2019), Appel (2019) na Arboleda (2020) wanaeleza kuwa, ubepari hupaliliwa kwa kutiwa mbolea ya ubaguzi katika janibu zinazotawaliwa na mabeberu wa kisasa. Katika Duniani kwa akina Dzombo, viongozi weupe ndio huwatawala viongozi vikaragosi Waafrika na hivyo ndivyo pia huwa wataalamu wa kila jambo. Hili huwapa fursa nzuri vibaraka wao kujilipa malipo yaliyo zaidi ya maradufu ya wengi wa wafanyakazi katika kila kiwanda au mradi. Hili linawiana na kauli ya akina Smith (2007) na Waithiru (2019; 2020) kuwa, viongozi wengi katika mataifa fukara ya Afrika hasa wabunge hujitunuku mishahara mikubwa bila hata kulipa ushuru. Mtunzi Mkangi anaeleza kuwa ubepari hupalilia hali ya ulemavu wa kimawazo baina ya wananchi.

Kama zao la dhuluma na maonevu, ubepari unawafanya matajiri kuwanyanyasa na kuwadunisha maskini. Matope analiweka hili bayana anapodhihirisha athari hasi za mabepari katika *Mafuta*. Matope anakumbwa na njaa na kiu inayomsakata kama msumeno au kama kaa la moto kooni kutokana na kiu. Anaongeza kuwa njaa inayomkabili inamvunja mishipa na tumbo lake linashirai mfano wa liogopalo kuonekana. Kiu ya mate inamtesa mate yanapokauka na kufanya viungo vyake kushikamana. Matope anadokeza kuwa, njaa ile ya kisunzi humtoroka tu anapozirai lakini punde ajihisipo, kiu ya kifafa povu huwa afadhali kuliko uchungu utokanao na ile njaa. Kwa mfano, Matope anasononeka anaposhuhudia mwanawe akikukutaa kama kipungu. Kutokana na ubepari, matajiri wenye mahoteli makubwa wanayanunua masaza ili wawalishe nguruwe wao huku Matope akijitafutia chakula kwenye kidimbwi cha maji taka.

Aidha, matajiri na wakubwa wanaajiri askari wayalinde masaza na uchafu wa mahoteli haya ili wachochole wasinufaike nayo. Lakini katika mapipa-njaa ambayo hayakuwa chini ya ulinzi mkali wa polisi, Matope alipata ushindani mkubwa kutoka kwa panya, mbwa, nzi na kombamwiko. Kadhalika, kando na wanyama na wadudu, Matope anazozana na binadamu maskini wenzake. Wote kwa jumla, kutokana na athari hasi za mabepari – udhoofu wa njaa – huwa na ukali unaozidi wa mama simba. Katama Mkangi anaeleza katika *Mafuta* kuwa, "... kilichokukaribia ulikitupilia mbali kama jongoo na muaa wake! Masaza yenyewe ya kugombania basi!" (uk. 37). Matope anafafanua kuwa mifupa iliyobahatika kukwepa uma za matajiri, kingo za silesi, ugali mkavu, wali uliovunda na vyapati vilivyoungua ndivyo vilivyokuwa vipochopocho vya wachochole. Mwandishi anadhihirisha hali hii katika *Mafuta* anapoeleza kuwa, "... mabaki ambayo hata mbwa na paka hawahalisi kuyala. ... ndiyo tuliyogombania sisi, panya na wengineo." (uk. 37). Hali hii bado ingali halisi katika mataifa mengi fukara barani Afrika, hasa mijini ambapo familia kadhaa huzaliwa, huishi na hufia vichochoroni vya miji na kwenye mitaro ya maji taka. Mabepari huzalisha ufukara wa kiwango cha juu ambao halafu huuondoa utu wa binadamu na badala yake unyama hutawala.

Matajiri wakistarehe na kufaidi ubepari, wachochole wanavumilia dhiki na unyama wa hali ya juu. Kwa mfano, Matope anasadiki kuwa mainzi na makombamwiko pamoja na uvundo mkali si vikwazo katika usakaji wa angaa tonge la mlo. Hivyo, waduni wanakuwa na uelewano fulani ili kukabiliana na njaa. Dkt Charles anakiri

kuwa baadhi ya msingi mkuu na madhubuti unaoimarisha anthroposenia ni ukapitalisti au ubepari. Hili linasawiriwa na kobe anayeashiria bara la Afrika kwa ujumla, ambalo limekauka miti na linalogubikwa na kiangazi kutokana na mfumo wa kibepari wa maonevu na dhuluma tele. Mfumo huu unapindua falsafa ya wananchi wa Daluta ya umoja kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika istilahi ya kitafsida ya utandawazi.

Hali hii inadhihirishwa na mtunzi Mbogo kupitia mhusika Dkt Charles [taashira ya anthroposenia] anayemwonyesha Profesa Williams [taashira ya anthroposenia] kobe mkubwa [taashira ya bara la Afrika lililotafunwa na kugugunwa na mabepari] katika *Vipuli* kwa kueleza kuwa, "Kobe yule, kama mlima uliokauka miti na majani yake ya kiangazi na sasa yamebaki mawe na majabali." (uk. 138). Mvulana anayetoka kwenye dimbwi la kuogelea, akiwa na chupi huku maji yakimdondoka kichwani anaruka na kumkalia kobe mgongoni na ingawa kobe anasita kidogo, hatimaye, anaendelea kutambaa. Kobe akiashiria bara la Afrika, mvulana wa miaka mitano anaashiria mataifa tajiri ya Ughaibuni ambayo kwa karne nyingi yamekuwa yakiyanyonya mataifa fukara ya Afrika kwa manufaa yao wenyewe katika mfumo wa ubepari.

Ingawa mvulana anayemrukia kobe na kumkalia ni wa miaka mitano, kobe ana umri wa zaidi ya miaka mia tatu. Profesa Williams anadokeza hili anapomjibu Dkt Charles katika *Vipuli* kuwa, "... miaka mia mbili hamsini au mia tatu." (uk. 138). Hili linaashiria namna mataifa ya Ughaibuni yameyadhulumu mataifa fukara ya Afrika kwa miaka mingi, kiwango kwamba hata baada ya mataifa ya Afrika kupata uhuru, bado yanayabeba mataifa tajiri ya Ughaibuni ambayo kutokana na uwezo wao huweza kujijenga upya na kuwa machanga mithili ya mvulana wa miaka mitano. Dimbwi la maji ya kuogelea analoibuka mvulana yule wa miaka mitano linaashiria uwezo na rasilimali yalizonazo mataifa tajiri ya Ughaibuni ilhali mataifa makongwe na fukara ya Afrika yanaendelea kulawitiwa na kubakwa na anthroposenia kupitia mfumo wa dhuluma, ubaguzi na maonevu wa ubepari.

Ndiposa maji yanamdondoka mvulana yule kichwani kuashiria kutoka uongozi hadi kwa wananchi – miguuni – kutokana na wingi wa rasilimali na utajiri. Hali hii inashangiliwa na Dkt Charles anayepasua kicheko baada ya kushuhudia hali hii ikijidhihirisha mchana machoni mwake. Kwa misingi hii hii, ubepari unaisawiri anthroposenia kupitia ukatili unaotendewa sungura na Chatu kwenye kibanda chenye

ukuta wa mbao imara ambacho sungura hana njia anayoweza kutorokea. Ndani mwa kibanda hiki, chatu ametulia tuli ilhali kwenye kona, pembeni kidogo, sungura mweupe anatweta kwa woga huku macho yakiwa yamemtoka na sharubu zake ndefu zinamcheza akikondolea kifo macho. Hali hii inaambatana na nguzo ya nadharia ya uhakikimazingira ya kifo. Chatu anaashiria mataifa ya Ughaibuni yenye uwezo, utajiri na yenye mifumo imara ya kisiasa, demokrasia, kiuchumi na kijamii. Hii ndiyo sababu chatu ametulia huku mwili wake wote umejirunda pamoja na kufanya kichuguu hai cha mawimbi, kinachopumua kwa kupanda na kushuka .

Hali hii ni mithili ya kichuguu kinachoashiria chumi zinazojiweza katika riwaya ya *Mafuta*. Kichwa cha chatu nacho kimegota juu ya tofali la sementi huku macho yakitamani kitoweo kilichojikunyata kwa woga mbele yake. Mwandishi Mbogo katika *Vipuli* sawa na mtunzi Mkangi katika riwaya ya *Mafuta* wanaashiria kichuguu kama taashira ya chumi zinazojiweza na zilizoimarika ulimwenguni. Profesa Williams katika *Vipuli* anampambanulia Dkt Charles kuwa, sungura ni chakula chake chatu na ingawa ni ukatili unaoimarisha mabepari, anamkumbusha kuwa hata wao wenyewe wapo mjini Daluta kuiimarisha ubepari kupitia ukatili wa uvunaji na uuzaji wa vipuli vya figo na mioyo. Hili linawekwa bayana na mwandishi Mbogo katika *Vipuli* kupitia mazungumzo baina ya Dkt Charles na Profesa Williams yanayosema kuwa:

> “Huu ni ukatili. ... kumweka sungura yule humu ndani akiwa hai, katika mashaka, unyonge na matisho ya uhai wake. ... keshakata tamaa hana pa kukimbilia.” Profesa aliinama, kama tabia yake ..., “Umesafiri kilomita maelfu kuja kufanya hili hili!” (uk. 139).

Ingawa maangamizi hushamiri kupitia ubaguzi na maonevu, wanaopalilia hutumia hila kuwalaghai wenzao, wenyewe kwa wenyewe kupitia ubepari. Mfumo wa uchumi wa ubepari unapalilia anthroposenia kama anavyodhihirisha Emmanuel Mbogo kupitia majadiliano kati ya Dkt Charles, Profesa Williams na Balozi Suprano. Katika majadiliano yao kuhusu sanaa ya upachuaji na upachikaji wa vipuli vya binadamu inayosambaa katika sehemu nyingi ulimwenguni, wanaepuka kumvunja moyo Dkt Matoga kwa kumpa asilimia ndogo ya mgao wa mapato yao. Hata hivyo, sio utu unaowaongoza katika kumjali Dkt Matoga ila ni woga, asije akatafuta soko mahali pengine na wao wakose kuyafaidi maangamizi na hivyo wanauhimiza na kuulinda ubepari.

### 4.10 Utepetevu wa Binadamu

Utepetevu wa binadamu kupitia dini, matumizi ya moto, na utekelezaji hafifu wa sheria umechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika riwaya nne teule. Tafsiri potofu ya mafundisho ya kidini mara nyingi huwafanya watu kupuuza wajibu wao wa kutunza mazingira katika riwaya nne teule. Vivyo hivyo, matumizi ya moto katika kilimo, uchomaji wa taka, na uharibifu wa misitu yamekuwa chanzo kikuu cha uchafuzi wa hewa na upotevu wa bayoanuwai. Aidha, ingawa sheria za mazingira zipo, utekelezaji wake umekuwa dhaifu kutokana na rushwa, ukosefu wa rasilimali, na migongano ya kimaslahi. Ulinzi wa mazingira unahitaji mabadiliko ya kiitikadi, matumizi ya sayansi, na usimamizi thabiti wa sheria kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**i. Dini**

Dini ni imani ya kuamini kuwa yupo mungu au miungu (Wamitila, 2022; Ndalu na wengine, 2014; BAKITA, 2015). Michael (2009) anafafanua kuwa, dini ni jumla ya imani ya binadamu kadhaa pamoja na mafundisho wanayoshiriki na kueneza kuhusiana na masuala, maadili, desturi au itikadi wanazofuata na kuzisadiki, au mambo ya roho, kama vile suala linalofungamana na mungu, maisha au uumbaji wa maumbile yote. Nguzo zilizoongoza uchunguzi wa aina hii ya anthroposenia ni pamoja na uongozi mbaya, utamaduni na mazingira, binadamu dhidi ya maumbile, na utandawazi. Dini huweza kutumiwa na binadamu katika upujufu wa mazingira kama namna ya unajisi wa mazingira kutokana na utepetevu wa binadamu. Kutokana na utepetevu huu wa kidini, watu huyachafua na kuyaharibu mazingira. Katika riwaya ya *Walenisi*, Katama Mkangi anadhihirisha utepetevu wa binadamu kupitia dini kama aina ya anthroposenia. Kupitia mhusika Dzombo, anaeleza kuwa, kutokana na imani yenye misingi ya kidini, haamini ardhi inayomdhihirikia machoni kuwa imenakshiwa kila sehemu na binadamu. Hivyo, anadai kuwa ni kazi ya mungu. Mtu-Bint Fikirini anamsahihisha kwa kumjuza kuwa, ulimwegu ule ulikuwa umepangika kutokana na juhudi zao wenyewe. Thiong'o (1987) anasisitiza kuwa, binadamu hasa Mwafrika hupalilia anthroposenia kwa kutumia dini kama sabuni ya kujiondolea lawama ya utowajibikaji wake binafsi na jamii kwa jumla.

Mtu-Bint Fikirini anathibitisha hili katika *Walenisi* anapotaja kuwa ilikuwa imedhihirika hapo kabla kupitia ngano zao kuwa, kuliwahi kuwepo na watu waliokaa bila kuwajibikia wala kuyasikitikia: mazingira, uchumi, siasa, utamaduni, maradhi,

ulofa, vita vya wenyewe kwa wenyewe, mabadiliko ya hali ya hewa, ubepari, vurugu dhidi ya mazingira, na mengine mengi; huku wakiendelea kumsifu mungu kwa kila jambo, liwe nzuri au mbaya. Kwa mfano, Mtu-Bint Fikirini anataja katika *Walenisi* kuwa, "... kulikuwa na watu ... hawakuwa wakiacha kumsifu mungu kwa ziada zote walizojipatia kutokana na juhudi za wengine." (uk. 52). Kwa misingi hii, imani itokanayo na dini inadhihirishwa kama sababu kuu ya kuepuka wajibu wa kukabiliana na viongozi dhoofu na badala yake kuwapalilia kupitia lawama dhidi ya changamoto zitokanazo na utepetevu wao kama vile; ukame, uchafuzi na uharibifu wa mazingira, ulofa na ukoloni mamboleo.

Mtu-Bint Fikirini anaeleza kuwa, watu wanaoelezewa katika ngano zao ni kama vile Dzombo. Vilevile, anaongeza kuwa walikuwa na ulaghai mwingi sana. Aidha anataja katika *Walenisi* kuwa, "Ulaghai ndio uliokuwa taaluma yao." (uk. 52). Ulaghai hupalilia na huendeleza maangamizi kwa kukuza uongozi dhalimu, ufukara, ufisadi, tamaa, unajisi wa mazingira, maradhi na hatimaye maafa. Ulaghai ni kigezo kikuu ambacho kutumiwa na wanadini kuwapumbaza wafuasi bila pingamizi wala udadisi wa nafsi. Kutokana na uwezo wa dini kuathiri mila na desturi za jamii, hupelekea kuwahamasisha wanajamii kutumia rasilimali asilia vibaya kutokana na imani kuwa walipewa uwezo wa kuyatawala na kuyathibiti mazingira na vilivyomo. Utowajibikaji huu huzalisha vurugu dhidi ya mazingira kwa kiwango kikubwa sana. Hili linafungamana na kauli ya akina Njeru, Kobia na Musyimi (2022) kuwa, ingawa utamaduni wa binadamu umeshikamana na ulimwengu asilia na huathiriana moja kwa moja, binadamu kupitia dini ameunajisi kwa kutouwajibikia wala kuusikitikia.

Kupitia dini, viongozi wa nyakati zinazoelezwa na Mtu-Bint Fikirini kwenye ngano zao, waliwanyima haki wananchi kutokana na kutojua kwa wananchi na kushiriki imani kwa wananchi kwa njia pofu bila kudadisi ukweli. Hili linathibitishwa na Mtu-Bint Fikirini katika *Walenisi* anapomwambia Dzombo kuwa, "... wengi hawakuwa na kisomo, waliogopa kwa kirahisi na kudanganyika haraka. Na wale waliokuwa nacho, walinunuliwa kipumbavu kwa minajili ya ubinafsi wao wa kupindukia." (uk. 52). Hivyo basi, kinachodhihirika ni kuwa, upujufu wa mazingira hushamiri katika mazingira yenye ujinga, woga, ufisadi na ubinafsi. Kutokana na kutoelimika kwa wananchi, viongozi waliweza kuwadhulumu bila pingamizi, kwa kuwa wananchi wenyewe hawakujua gani ilikuwa haki yao wala wajibu. Hivyo, waliogopeshwa kupitia dini na walipolalamika kuhusu madhara ya tabianchi na mabadiliko ya hali ya

hewa, walifahamishwa kuwa ni mapenzi ya mungu wao kuwa maskini, kuangamia kutokana na maradhi na ukame kwa ujumla madhali msingi, viongozi wale walipewa uongozi na mungu mwenyewe. Hakika hii ndiyo taswira halisi katika mataifa mengi ulimwenguni hususan barani Afrika.

Dreyer (2007) anaeleza kuwa, uhusiano kati ya dini na hali ya ukoloni mamboleo barani Afrika ni wa kisimbiotiki. Kupitia mizizi iliyoimarishwa na wamishenari, dini imeendeleza ukoloni mamboleo kwa kuwapumbaza Waafrika wasidadisi sera na mifumo ya uongozi na utawala kwa jumla. Kwa upande mwingine, ukoloni mamboleo unaimarisha upujufu wa mazingira kutokana na athari hasi zake zinazopitishwa kupitia dini hadi kwa utamaduni wa Mwafrika na kusababisha udhoofu na uchafuzi wa tamaduni za kijamii, uchumi na miundo ya kisiasa iliyokuwepo kabla ya kipindi cha ukoloni mkongwe. Ufisadi, tamaa na ubinafsi pia vinachangia mabadiliko makuu ya tabianchi na hali ya hewa pakubwa. Vyote vinapaliliwa na dini moja kwa moja. Mtu-Bint Fikirini anakiri kuwa, ingawa dini iliwapofusha wananchi wale Wachuna, baada ya muda mrefu walizinduka na kushambulia wadhalimu. Anataja kuwa, Wachuna walishirikiana kuupalilia utu ili kuyadidimiza maangamizi na hivyo kudokeza mojawapo ya mbinu mwafaka na madhubuti ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira ilielezewa zaidi katika utafiti huu chini ya lengo la tatu.

Kadhalika, dini inasawiri anthroposenia kupitia mhusika Mtu-Bint Fikirini katika *Walenisi* anayetaja kuwa, "... viongozi wengi wa dini waliounga mkono upuuzi huo." (uk. 103). Hili linaashiria kuwa, kupitia dini, viongozi wa dini hudhihirisha na huchangia maendeleo ya upujufu wa mazingira ulimwenguni. Dzombo anathibitisha hili katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, "Jehanamu, tunaamini kama wao (Wachuna) ... viongozi wenu wa dini walivyofundisha." (uk. 103). Jehanamu ni duniani kwao Dzombo ambako maangamizi huabudiwa. Katama Mkangi katika *Walenisi* anasisitiza kuwa utepetevu wa binadamu kupitia dini ni aina ya anthroposenia. Kupitia mhusika Mama Mtu-Maanani, anaashiria kuwa dini humfanya binadamu kupalilia anthroposenia maishani mwake. Kwa mfano, Ibilisi ambaye anaabudiwa anachukuliwa kama mpaji wa yote mema na maovu. Hivyo, mja akipata mema humshukuru yeye na pia akipata maovu husema kuwa ni 'majaliwa' ya ibilisi. Kwa misingi hii, Ibilisi akaashiria kijisababu cha kutoyawajibikia mazingira na viumbe

vyote vilivyomo. Hili hupelekea binadamu kudharau thamani ya bioanuwai na umuhimu wa kudumisha usawa wa ikolojia.

Utepetevu wa binadamu kupitia dini kama aina ya anthroposenia unapalilia ubaguzi. Mtu-Makazi anafafanuliwa na Mtu-Dzombo katika *Walenisi* kuwa, Duniani dini zote zinafundisha kuwa mna baadhi ya watu wenye akili wanaostahili maisha bora kuliko wengine. Dini inakuza na kuendeleza kasumba ya kila siku katika *Walenisi* ikaririo kuwa, "... ingawaje mungu ametuumba sawa, usawa huu utapatikana tu baada ya kufa." (uk. 145). Hili linapalilia maangamizi aina aina madhali watu wanaendelea kuvumilia dhiki za; ulofa, ukosefu wa ajira, matumizi ya dawa za kulevya, unywaji wa pombe haramu, uchafuzi wa mazingira, ukosefu wa elimu bora, njaa, maradhi, vita vya kikabila, ubepari, ukoloni mamboleo na matatizo mengine chungu nzima, huku wakiamini kuwa kifo kitawaauni dhiki hizi zote. Kiuyakinifu, mwandishi Mkangi anadhihirisha kuwa utepetevu wa binadamu kupitia dini unatumia hila aina aina kupalilia mauti kupitia wahusika tofautitofauti. Wananchi, hasa katika mataifa fukara ya Afrika wanafundishwa kuwa na subira na kutowaonea ghere wenzao. Wanatishwa kuwa kufanya hivi ni dhambi na hivyo, waendelee kudumisha ulofa, maradhi na kuvumilia njaa ili wakiaga dunia waweze kunufaika pakubwa na kuwa watu wasiokosa hitaji lolote. Maajabu ni kwamba hata wanasiasa humaizi hili na wengi huutumia utepetevu huu kuwalaghai na kuwatuia wapiga kura kama shashi huku wakiyanajisi mazingira na uhai wao kila uchao.

Mathalani, Mtu-Bint Fikirini anamjuza Dzombo kuwa dini ilitumiwa na Wachuna kupalilia utumwa, utabaka na ubaguzi wa kimazingira. Anaeleza katika *Walenisi* kuwa hili lilifanikishwa na vitendo vya Wachuna kama vile, Wachuna walikuwa wakimgawa mungu katika vipande viwili. Walidai kwamba sehemu iliyokuwa hai ilikuwa yao wenye vyeo, nafasi na vyao ilhali iliyokufa ilikuwa ya wanyonge na vijakazi wao. Hii ni kwa sababu, Wachuna ambao ni taashira ya anthroposenia hasa barani Afrika walistarehe sana kabla ya mauti yao ilhali wananchi walitapatapa katika bahari ya ulofa. Wachuna waliwalaghai wananchi kwa kujifanya kutotilia maanani maisha yao ya raha mustarehe huku wakiwatia kasumba majeruhi wao kwa kutumia dini. Hili linawiana na kauli ya akina Moore (2015) na Ardoleda (2020) kuwa, katika maeneo yenye uonevu na ulofa uliokidhiri anthroposenia huimarika zaidi. Wachuna walitumia dini kueneza kasumba kuwa wananchi maskini wangeishi raha mustarehe baada ya kufa. Mtu-Bint Fikirini anasisitiza kuwa, wananchi walalahoi ndio tu

waliotumiwa kuyapalilia na kuyalinda madhara ya tabianchi kutokana na upofu na upuzi ulioenezwa na dini.

Dini kama aina ya anthroposenia inatumiwa na Wachuna kuwapumbaza wachochole ili kuendelea kuyafaidi maangamizi. Kupitia dini, wanyonge walizidi kutafunwa na njaa, wengine walizidi kujikunyata mapangoni kama wanyama au nje mithili ya miti pamoja na mateso na manyanyaso tele. Mtunzi Mkangi anathibitisha hili katika *Walenisi* anapotaja kuwa: "“Subira baba yenu aliye mbinguni atawatimizia yote huko Akhera,” dini iliwaliwaza na wakaliwazika." (uk. 192). Aidha, kupitia dini wanyonge waliendelea kujitosa kwenye ujinga na wakasusia kabisa kuwa watu. Pia, ili kuikaza imani ya dini kuwa anthroposenia ni sehemu ya maisha ya binadamu katika istilahi ya kitafsida ya ulofa, na kuwa hana budi ila kuukabili kupitia bahati nasibu, Wachuna wakatawanya michezo ya bahati nasibu tele. Hili linafungamana na kauli ya Oliver (2016) kuwa, ulofa ni ‘mungu’ ambaye huabudiwa bila hiari ila mja hujipata tu, lakini katika janibu za mataifa fukara pekee, hasa ya Afrika. Katama Mkangi anaongeza katika *Walenisi* kuwa, “Walipumbazwa na kupumbazika na akili zikawaganda, na ndivyo werevu Wachuna walivyoendelea kuipalilia hali hii na kuendelea kuvuna maridhawa ...” (uk. 192). Vifo vingi barani Afrika huwa tokeo la utepetevu wa binadamu kupitia dini. Wengi huyapuuza mabadiliko ya hali ya hewa, uharibifu wa maji na mchanga, umwagaji taka zenye kemikali sumu kwenye mito na bahari, pamoja na ufyakeji wa miti ovyo ilmuradi wasiwakasirishe viongozi wao wa kidini.

Mbeyu anaeleza kuhusu baba na mama katika hadithi yake inayoashiria ubaguzi na maonevu katika misingi ya dini. Kwa mfano, baba watoto anajivunia kuwanyanyasa wafungwa. Mateso yenyewe anayafanikisha kwa kutumia pini kuwadunga kwenye vidole na pia kuwachoma viungo vya mwili vya uzazi kwa kutumia moto wa sigara na ule wa spaki. Kijumla, moto unaashiria mangamizi. Hivyo basi, kwake huyu baba watoto kujisifu kwa kusema kuwa alitunukiwa kazi hii ya dhuluma kwa binadamu wenzake na mungu kunasawiri na kuthibitisha upaliliaji na ukuzaji wa mauti kupitia dini. Baba watoto anakariri katika *Mafuta* kuwa, “... ni mungu mwenyewe ndiye aliyemtunukia.” (uk. 67). Hakika, utepetevu wa binadamu kupitia dini unawapotosha watu kuhusu athari za shughuli za binadamu kwake, kwa mazingira na afya ya viumbe hai.

Kwa njia hii hii, mkewe na mama wa watoto wake pia anaendeleza maafa. Kwa mfano, Mbeyu katika *Mafuta* anataja kuwa, "... walikuwa hawaachi kusisitiza kwamba walikuwa wakitimiza utumwa wa mungu tu." (uk. 67). Walikuwa wakijisemea kuwa, hawangekuwa wakizifanya kazi zao isingekuwa ni ile haja yao ya kutaka kutimiza matakwa ya mungu. Mbeyu anasema kuwa katika jamii ile, mungu alisisitizwa sana sana. Ingawa wasichana wengi anaowatoa mimba ni wa tabaka la juu kama yeye, anatumia dini kama kigezo kikuu cha kutakasa na kuifaulisha kazi yake. Wasichana wote wanaofika mwake zahanatini wanaogopa kuwa na mimba ya aibu ila si sababu nyingine yoyote ya msingi. Wazazi, au hata marafiki wa wasichana wale wanamlipa mama huyu kuwatoa mimba wasichana wao. Baba na mama hawakukoma kutoa ushuhuda kuwa walikuwa wanatimiza tu mapenzi ya mungu. Hili linathibisha kuwa utepetevu wa binadamu kupitia dini unapalilia mauaji pakubwa madhali wengi wanaitumia kama kisingizio cha kutowajibikia kazi zao, maisha yao wenyewe na ya wengine, utu wao na wa wengine pia mazingira kwa jumla.

Hili linadhihirisha uwezo wa dini kuendeleza maangamizi bila vikwazo katika jamii kwa kuchelea kumuudhi au kumkosea mungu. Aidha, dini imetumiwa na wengi kuwaogofya watu wasije wakadadisi ukweli wa mambo. Jambo hili hukuza unafiki ndani ya uongo na woga na hatimaye, mauti hunawiri na kupevuka hasa katika mataifa mengi fukara barani Afrika (Walter, 2013, Iheka, 2015 na Waithiru, 2022a). Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa Mbeyu, kila siku, mtoto mmoja kati ya wale saba alikuwa akibuni sala kabla ya kula. Mara nyingi sala iliyobuniwa ilipalilia ubaguzi na maonevu pakubwa, katika misingi ya dini. Mathalani, mna siku mtoto mmoja alitunga sala iliyomsawiri mungu kama kiumbe anayebagua, anayepalilia dhuluma na anayeunga mkono uavyaji mimba – mauaji ya watoto na mijusi. Hali hii inazidisha usawiri wa maangamizi. Mtoto anapoomba anasisitiza shukrani kwa mungu kwa kumtoa mwana wake awatoe kwenye baa la njaa. Swali linaloibuka ni je, ikiwa kweli aliwapa wao shibe, ndiye pia kawanyima wanaoangamia kutokana na baa lile lile la njaa?

Mtoto yule anaongeza kuwa chakula kile ni mwili na damu ya mwana wa mungu na hivyo, anaomba kiwashibishe kimwili na kiroho. Hili linadhihirisha mungu mwenye ubaguzi anayepalilia maonevu na maangamizi kwa kwango kikubwa sana. Kadhalika, mtoto bila kufahamu anamshukuru mungu kwa kuwateua wazazi wake na kuwatunuku kazi zao ili wao wapate chakula kile cha kifahari. Ikizingatiwa kuwa kazi

zao ni za mateso, dhuluma na maafa kwa wengine, hali hii inaashiria kuwa matajiri huyafaidi mauti ya wanyonge, huku wanyonge wakiteseka, kuumia na hatimaye kuangamia. Haya yote yanafanikishwa na dini. Kauli ya mwisho ya mtoto inadhihirisha nguzo kuu ya anthroposenia, kati ya nyingi, ambayo ni ubaguzi. Mtoto anamshukuru mungu kwa kuwapa nafasi yeye na familia yao kukila chakula kile kwa niaba yake mungu, mwanae na roho mtakatifu. Hili linamaanisha kuwa, wanyonge huwa hawana chochote wanachopewa na mungu kama chakula na hivyo hubaguliwa.

Dini huendeleza imani hii ambayo huyahifadhi na kuyalinda maonevu na maangamizi. Kwa misingi hii hii, kila mtoto aliyepewa fursa ya kubuni sala aliusifu ubaguzi moja kwa moja na wazazi wake wakamfurahia kwa kuiviringa na kuifinyanga sala yenye 'baraka' tele. Wazazi hawa walifurahia namna kila mmoja wa watoto wao alivyokuwa na ucha mungu mwingi, hadi ilipofika siku ya saba ambayo ilikuwa zamu ya kitinda mimba wao kuiviringisha zaidi sala ya jioni. Ukweli ni kwamba, watoto wengine wote isipokuwa kitinda mimba walikuwa wakiwadanganya wazazi wao kuwa sala ile ilikuwa ya kubuni, ilhali ilikuwa inakaririwa kutoka kitabuni. Ingawa wazazi hawa waliwasifu watoto wao kwa ubunifu wao, hawakutambua kuwa kila sala ilikuwa sawa kila siku kutokana na upofu wa kiimani kuwa wao ndio wanaofaa kuliko wengine. Chanzo katika *Mafuta* anaamua kuficha ule uongo wa ndugu zake na kubuni sala inayosema, "Tunatoa shukrani kwa wafanyikazi wote waliohusika na uzalishaji wa chakula hiki; pia Baraka ya Mama Ardhi isifiwe; Amen." (uk. 69). Uhifadhi wa mazingira unatiliwa mkazo katika sala hiyo. Ingawa hili linafaa kuwa jambo la busara watu wengi hulipuuza na badala yake kushabikia upujufu wa mazingira.

Ulaghai wa kidini unapokabiliwa na ukweli hutetemeka. Hili linadhihirishwa na wazazi wake Chanzo ambaye baada ya kubuni sala hii alikaripiwa na wazazi wake vikali. Babake alimkemea Chanzo kuwa ni mpumbavu huku mamake akimfahamisha kuwa zile akili za kubuni ushenzi kama ule hazikuhitajika mle. Chanzo naye akaendelea kusisitiza kuwa yeye pia anazo akili za kubuni, jambo ambalo dini huepuka. Hivyo, ili kuyalinda maangamizi, wazazi wake Chanzo wanamfukuza kutoka pale mezani upesi na kumfahamisha kuwa tokea siku ile angekuwa akila masaza pamoja na hao wafanyikazi awapendao. Ingawa dini inaendeleza mauti katika hila na woga, yenyewe huogopeshwa na ukweli, matumizi madhubuti ya akili na ujasiri. Hili linathibitishwa na kauli ya Msati katika *Mafuta* inayoeleza kuwa, "...

kuadhibiwa kwa Chanzo kulitokana na kutumia ubongo wake ulioagiza ulimi wake kusema yaliyo ya kweli." (uk. 70). Ulimwenguni kwa jumla, binadamu anaendelea kukabiliwa na mabadiliko ya tabianchi kama zao la utepetevu wake kupitia dini. Utepetevu huu huhusishwa moja kwa moja na haki za binadamu na mazingira.

Ili kukabiliana na utepetevu huu, dini zinahitaji kufanya tathmini ya kina na ya kujikosoa kuhusu athari za imani na matendo yao kwa mazingira na kushirikiana na jamii ya ulimwengu ili kuchangia katika kutafuta suluhisho la changamoto ya uharibifu wa mazingira ulimwenguni. Dini huwafanya watu wajione kuwa na haki ya kutawala na kutumia mazingira kwa manufaa yao wenyewe, bila kujali madhara kwa viumbe wengine, bila kujali madhara kwa viumbe wengine. Hakika dini inafaa kuwa chanzo cha uangalifu na uwajibikaji kama itawafanya watu wajione kuwa sehemu ya mazingira na wajibu wa kuyatunza na kuyalinda kwa vizazi vijavyo.

**ii. Moto**

Kwa mujibu wa Ndalu na wengine (2014), Mdee na wengine (2015) pamoja na Wamitila (2022), moto ni mwako wa kitu kinachoungua au hamu ya kitu iliyokithiri. Katika *Walenisi* Katama Mkangi anadhihirisha utepetevu wa binadamu kupitia moto kama aina ya anthroposenia. Ikumbukwe kwamba, anthroposenia huchoma chumi, tamaduni, mifumo ya uongozi, pamoja na uhai wa binadamu (Clark, 2015; Sklair, 2022; Butler, 2024). Waandishi wa riwaya nne teule zilizochunguzwa wamedhihirisha utepetevu wa binadamu kupitia moto kama aina ya anthroposenia. Mihimili iliyoongoza uchunguzi wa aina hii ya anthroposenia ni uongozi mbaya, utandawazi, na utamaduni na mazingira. Joto linalomkumba Dzombo ghafla linatokana na moto. Hewa ya moto inampiga na kumwingia mapafuni na pia inamjaa matumboni na kumzuia hata kupumua. Ingawa anapochuchuma fahamu zinamrejea, pumzi zinamwangama. Kasi ya Trimi inazidisha joto. Kwa misingi hii, maafa yanaashiriwa na Trimi kwenda kasi ambapo maisha na uhai wa binadamu pia hukatishwa haraka na moto. Hii ni kwa sababu, moto huangamiza mazingira ya binadamu na hivyo kumwangamiza yeye pia kupitia ukame, maradhi na hatimaye maafa. Moto huharibu na hupunguza bayoanuwai ya mimea na wanyama hasa katika misitu na savana.

Simel (2015) akiyaunga mkono mawazo ya mtafiti anaeleza kuwa, kiangazi na ukame husababisha hali duni ya maisha na elimu kutokana na upungufu halafu ukosefu wa chakula. Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anaongeza kuwa, "Sasa, moto ulianza

kumwingia na kupumua kwake kukawa ni kwa taabu. Roho ilikuwa inamyeyuka na damu kumtoka." (uk. 53). Kwa misingi hii, Katama Mkangi anaashiria kuwa, moto humsababishia binadamu kiu ya ajabu, humfanya midomo kumkauka na ulimi kumgandama kaakaani. Dzombo anathibitisha hili anaposadiki kuwa, hufikia muda mate yakaadimika kinywani. Hata hivyo, moto humchoma binadamu bila kumchoma mwili ili iendelee kunufaika kutokana na mateso na maumivu unayomsababishia. Mwandishi anadhihirisha hili katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, "Moto huu ulimchoma lakini mwili haukuchomeka. Moto usioonekana aliusikia ukimshambulia bila kumtoa hata lengelenge." (uk. 53 – 4). Pia moto wa ubinafsi uliopindukia unaashiria maangamizi ya utu na maadili. Kutokana na ubinafsi uliopindukia, Wachuna wanapalilia maafa kwa karne nyingi ghaya. Hii ni kwa sababu, kutokana na utepetevu wa binadamu, moto huchangia uzalishaji wa gesi chafu, kama vile kaboni dioksidi na methani, ambazo zinaongeza joto la dunia na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Dzombo katika *Walenisi* anataja kuwa maangamizi hukuzwa na kuendelezwa kupitia moto. Anashikilia msimamo kuwa, kwao duniani, waliiteketeza misitu yao ya asili, yote, kwa moto. Mtu-Dzombo anamweleza Mtu-Bint Fikirini kuwa, ulofa, ubepari na hatimaye maangamizi vilikita kambi duniani mwao. Hii ni kwa sababu, duniani, watu wenye uwezo huwadhulumu na kuwanyanyasa walalahoi. Kwa mfano, badala ya wenye uwezo kusambaza stima kwa kila mwananchi, wanawasambazia wenzao wenye uwezo. Hili linasababisha uhaba wa stima kwa wengi, hasa walalahoi wa mashambani na mijini. Hili linafanikishwa na walalahai kupitia bei wanazopandisha kila siku na hivyo kuwabagua wengi kwa kuwanyima uwezo wa kugharamia moto na mahitaji muhimu ya maisha. Moto unaorejelewa ni ule utokanao na kawi ya stima.

Walalahai hawa, wanaingilia na kujihusisha na biashara ya makaa na kuni, huku wakiwauzia walalahoi ambao ndio wengi duniani. Ikumbukwe kwamba, ulofa hupalilia anthroposenia na kuitia mbolea madhubuti (Demos, 2017). Anthroposenia duniani huzalisha ufyekaji wa misitu na mapori na hatimaye husababisha upanuzi wa majangwa. Majangwa huashiria maangamizi kupitia ukame ambao huzalisha maafa katika mataifa mengi barani Afrika (Njeru, Kobia na Musyimi, 2022). Hivyo, mwandishi Mkangi anasawiri maafa kupitia moto. Moto wa marisau, wa ulevi na wa maradhi ya zinaa kama ukimwi na wa dawa za kulevya ni baadhi ya njia ambazo mwandishi ameisawiri anthroposenia kupitia moto. Moto husababisha uchafuzi wa

hewa, maji na ardhi, ambao unaweza kuathiri afya ya binadamu na viumbe hai wengine. Vilevile, huchangia udidimikaji wa rasilimali za asili, kama vile mbao, mazao na malisho, ambazo ni muhimu kwa uchumi na maisha ya watu.

**iii. Sheria**

Istilahi ya sheria huashiria dhana tofautitofauti. Lakini katika utafiti huu, neno sheria lina fahiwati ya kanuni zinazotungwa na bunge la nchi ili kusimamia taratibu ambazo hazina budi kufuatwa na kuelekeza adhabu zitakazotolewa kwa watakaokiuka kanuni zilizowekwa. Aidha, ni kaida zinazotungwa na chombo chenye mamlaka katika eneo fulani kama vile halmashauri iliyopewa mamlaka na bunge ili kusimamia taratibu za mahali husika kama vile, miji au kampuni. Kwa misingi hii, humaanisha kanuni zinazoendesha maisha ya waumini wa dini fulani au taratibu zinazotungwa na mamlaka yoyote yenye dhamana ya kusimamia eneo fulani kwa ajili ya kuleta nidhamu ya maisha katika eneo hilo (TUKI, 2013; 2014; Ndalu na wengine, 2014; Mdee na Wengine, 2015; BAKITA, 2015; Wamitila, 2022). Hivyo, kwa mujibu wa wasomi na watafiti hawa, sheria inafaa kukabiliana na unajisi wa mazingira ila si kuukuza.

Hata hivyo, hali hii ni kinyume kwani mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anausawiri unajisi wa mazingira kupitia sheria. Nguzo zilizoongoza uchunguzi wa sheria kama aina ya anthroposenia kutokana na utepetevu wa binadamu ni uongozi mbaya, uwezo na utandawazi. Mwandishi wa *Walenisi* analiweka hili bayana anapodhihirisha namna sheria inatumiwa kumhukumu Dzombo kwa kosa la kusingiziwa. Hii ni kwa sababu, kulingana na Katama Mkangi, katika mahakamani sheria zinafuatwa kwa mujibu wa kulinda au kutetea wenye vyao na vyeo ila si kudumisha haki za binadamu, na hivyo hupalilia maangamizi kupitia maonevu na dhuluma kwa wanyonge. Katama Mkangi anaongeza kuwa, sheria inatumiwa kumtia hatiani mtu yeyote anayepatwa na kisirani cha kushtakiwa. Dzombo katika *Walenisi* anashtakiwa na mwajiri wake kwa madai ya kuwachochea wafanyakazi wenzake ilhali alikuwa anawazindua kutoka kwenye upofu na ujinga wa ubaguzi. Hivyo, sheria inatumiwa na tabaka linalotawala kama chombo cha kuyalinda mauti kwa kuyalinda maslahi ya matajiri pekee. Sheria hulegeza viwango na vigezo vya ubora wa mazingira, kama vile kiwango cha uchafuzi wa hewa, maji na ardhi kinachoruhusiwa.

Emmanuel Mbogo kupitia hakimu mahakamani anadhihirisha anthroposenia kupitia sheria. Sheria anayonukuu hakimu kumhukumu Shipe inapalilia maonevu ingawa inajifanya kuwa inakabiliana nayo kwa kukemea ulozi na uchawi. Shipe anahukumiwa kifungo cha miaka saba gerezani, viboko saba pamoja na kazi ngumu. Hukumu hii inatokana na kosa analolifanya Shipe la kuwa mbunifu katika mbinu za kupambana na ulofa lakini badala ya kuelekezwa na kushauriwa, anahukumiwa kifungo cha ukatili na chenye adhabu kali hata kuliko kosa alilotekeleza. Hakimu katika *Vipuli* anataja kuwa, "Chini ya kifungu cha sheria nambari 9912931/18/3 cha mwaka 1959 kuhusu ulozi na uchawi, utafungwa jela miaka saba, viboko saba na kazi ngumu." (uk. 118). Hakika kwa kuzingatia muda na kipindi ile sheria ilipotungwa wa 1959, ni dhahiri kuwa mahakama hii inatumia sheria zilizotungwa na mbeberu kumtawala Mwafrika hata baada ya Daluta kupata uhuru. Kwa mujibu wa Wa Thiong'o (1987; 2009), hakuna wakati ambapo Afrika tutaweza kusuluhisha dhiki na matatizo yaliyozalishwa na mawazo ya mkoloni kwa kutumia mawazo yale yale, ila kwa kutumia mawazo ya Uafrika mamboleo unaohuluti tamaduni mbalimbali chanya wala sio ule ulionajisiwa na Mbeberu. Hili linadhihirisha dhuluma chini ya mfumo wa mabeberu wa kisasa. Hivyo, sheria huweza kuwa chanzo cha utepetevu wa binadamu kwa kuwapa watu uhuru na kinga ya kufanya shughuli zinazohatarisha mazingira bila kujali madhara kwa viumbe wengine.

### 4.11 Viongozi Wabaya

Viongozi wabaya huendeleza uongozi mbaya ambao huzalisha dhuluma na huwanyima wananchi sio tu haki zao za kimsingi ila pia utambulisho na utu wao (Thiong'o, 2009). Viongozi dhoofu kupitia uongozi mbaya kama aina ya anthroposenia hufanikisha hali hii kupitia uwezo wao wa kupalilia ulofa ulimwenguni. Emmanuel Mbogo katika riwaya ya *Vipuli* anadhihirisha namna ulofa unavyochangia kuwepo kwa makahaba na wanyonge ombaomba mjini Daluta. Ufukara unawavaa hadi uongozi ambao umewazalisha unawaona kama uchafu. Majadiliano kati ya wananchi yanadhihirisha kuwa malaya na waombaji hulileteа taifa aibu na fedheha kuu. Uongozi mbaya unazalisha mazingira na mifumo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa inayopalilia ulofa, unaopalilia na kuzalisha mauti. Hii ni kwa sababu, mtunzi Mbogo katika *Vipuli* anasema kuwa, "Halmashauri ya jiji ikiusafisha mji leo, baada ya wiki tu wanaanza kurudi tena." (uk. 175). Mihimili

iliyoongoza uchunguzi wa viongozi wabaya kama aina ya anthroposenia katika riwaya nne teule ni pamoja na uongozi mbaya, uwezo na kifo.

Ingawa malaya na ombaomba wanadhihirisha kuwepo kwao kwa akili moja na vichwa vigumu kama kamongo, ukweli ni kuwa ni uduni na changamoto za maisha ambazo ni zao la uongozi mbaya zinazowalazimisha kurejea mjini na kuendelea kuuchafua wao wenyewe. Ulofa huu unadhihirishwa na kauli ya wananchi katika *Vipuli* kuwa, "Ile ni mikahawa yetu, yahe! Tukiwa na kiu na njaa tutakula wapi?" (uk. 175). Kando na njaa ya kimapenzi, wengi wa wananchi hawana uwezo wa kununua chakula katika mikahawa kikubwa ya kifahari, na hivyo hukimbilia vibanda na vioski, ambapo wana uwezo wa kumudu bei hata wanapokula wakibishania mlo na nzi. Baada ya uongozi mbaya kuzalisha ufukara nao ufukara unazalisha kifo kinachokuwa hatima ya binadamu na mazingira yake kwa jumla.

Kwa mfano, Dkt Matoga anadhihirisha hili katika mkutano mfupi kati yake, Nyau, Shipe na Kipanga. Dkt Matoga anawashauri kuwa ni vyema kuepuka mji kwanza hasa katika maeneo yenye malaya. Hii ni kwa sababu, hata baada ya maskini, viwete na malaya kutoweka jijini katika hali inayotatanisha, vyombo vya habari na wananchi kwa jumla wanatambua tu ukosefu wa malaya wale kumi na wawili pekee. Gazeti la Daily Echo pamoja na lile la Mageuzi katika *Vipuli* yanaipa habari ya kupotea kwa malaya kumi na wawili kimiujiza katika eneo la Sokota, kipau mbele. Hili linaonyesha ukubalifu wa uongozi dhalimu baina ya wananchi katika mataifa mengi barani Afrika kwa mfano. Kauli ya Dkt Matoga inathibitisha hili katika *Vipuli* inaposema kuwa, "... dafina .... za vipuli kwa wakati ule iwe mochware ..., Magereza na maskini ombaomba waliokuwa wametapakaa na kulala ovyo katika mitaa, vichochoro na mageto ... ya jiji lile." (uk. 192). Hakika, ufukara mara nyingi husababisha waduni kuweka shinikizo zaidi kwenye mazingira, jambo ambalo huchangia ongezeko la watoto kwenye familia hivyo ongezeko la watu duniani. Hili hutokana na hali ngumu ya maisha kwa ujumla. Ulofa huchangia utupaji taka za binadamu usiofaa unaosababisha hali mbaya ya kuishi, shinikizo kubwa kwenye ardhi dhaifu kutosheleza mahitaji yao, uharibifu mkubwa wa rasilimali asilia na ukataji miti zaidi.

Hakika, kinachowapa ari kuu ya kuendeleza maangamizi ni uongozi mbaya, madhali siku yale magazeti yaliepuka kutaja lolote kuhusu kuadimika kwa akina yahe, hadi

siku hiyo, bila minong'ono kuwahusu walofa na walemavu, akina Dkt Matoga walichukulia suala lile kama bahati kubwa sana kwao kuliko mtende mwenyewe. Kadhalika, Jaji Mkuu Sekwao anapalilia uongozi mbaya unaokuza maangamizi. Katika juhudi za kuyalinda maonevu na ubaguzi, Jaji Mkuu, Sekwao, anaamrisha mkuu wa polisi, Bwana Radhani kuwachunguza vikali viongozi wa upinzani na kisha kuwatia kizuizini bila hatia yoyote, wakiwa wangali washukiwa. Jaji Sekwao anadhihirisha itikadi, hulka na mchango wake katika kupalilia maonevu, hasa katika janibu za Afrika kupitia uongozi mbaya katika *Vipuli* anaposema kuwa, "Hawa watu wanasikia nchi nyingine za Ulaya zinaanzisha vyama vingi, ... wao bila kujali historia yetu, mazingira yetu yaliyojaa ukabila, wanakimbilia hilo ..." (uk. 204). Hakika, uongozi mbaya unaweza kuongeza athari hasi za uchafuzi wa mazingira kwa maskini, walemavu na makahaba. Aidha, viongozi waovu hupelekea ukosefu wa uwajibikaji, udhaifu wa utekelezaji wa sheria na kanuni za mazingira, usimamizi mbaya wa rasilimali asilia na kushindwa kushughulikia sababu za msingi za umaskini na ukosefu wa usawa.

Ramadhani anafanikisha uongozi mbaya kwa kuwaamrisha polisi kupitia Inspekta Poponda. Mazingira anamotumia kuupalilia udhalimu kupitia uongozi mbaya ni kupitia shimo lililo chini ya ardhi ya jengo la Makao Makuu ya Polisi. Shimo hili ambalo ni jela kubwa ni siri ambayo raia wengi hawana habari kulihusu. Isitoshe, uongozi mbaya unazalisha ubinafsi, tamaa na ubepari kwa jumla. Dkt Matoga kupitia nadharia yake anasisitiza kuwa, ulimwengu unatawaliwa na hali ya kuchimbana na kulana wenyewe kwa wenyewe. Hali hii huifanya siasa kuwa muhimu sana kwa walinzi wa viongozi dhoofu. Hii ni kwa sababu, Dkt Matoga akiwa mmoja wao wa walinzi na wakuzaji wa viongozi wabaya anataka kufaulu katika siasa na kuwa kiongozi ili siasa iwe buruji imara la kuzilinda haja zake binafsi, usalama wake na utajiri wake pekee, bila kuwajali wananchi. Viongozi wabaya huzuia ushiriki na uwakilishi wa makundi yaliyotengwa katika utawala na sera za mazingira na kupuuza mahitaji na haki zao katika mipango na hatua za mazingira.

Vilevile, uongozi mbaya unazalisha upujufu wa mazingira anamoishi binadamu pamoja na viumbe vyote. Mwandishi wa *Vipuli* anadhihirisha hili anapoeleza hali ambapo wanafunzi wa Chuo Kikuu wanapogomea masomo na kufanya maandamano kuupinga uamuzi wa serikali yao wa kutenga asilimia kubwa ya bajeti ya nchi yao kuangazia uundaji wa silaha za kinuklia. Silaha hizi huwa na athari za maangamizi

dhidi ya mazingira, viumbe hai, maumbile na kila kitu ulimwenguni kwa jumla. Hili linawiana na kauli ya akina Maathai (2009), Curry (2011), Iheka (2015), Nkonge (2014), Mwirabua (2014) na Waithiru (2019) kuwa uongozi mbaya huchangia uharibifu wa mazingira, hupalilia ulofa, huimarisha maradhi, hutawaliwa na maafa ya wananchi huku viongozi wakinenepa na kukinai na hatimaye huimarisha udhalimu, hasa katika mataifa fukara ulimwenguni.

Msemaji wa serikali anazidi kudhihirisha kuwa uongozi mbaya hupalilia maonevu na ubaguzi kwa kudidimiza demokrasia. Kwa mfano, anasisitiza kuwa uundaji wa chama cha True Democratic Tigers pale Daluta ni kinyume cha katiba ya nchi, ambayo inapinga vikali kuwepo kwa vyama vya upinzani. Kusudi la Dkt Matoga la kujiunga na True Democratic Tigers limegubikwa na tamaa, hila na ubinafsi-uchoyo. Hili linawekwa bayana na mwandishi anapofafanua katika *Vipuli* kuwa, lengo lake Dkt Matoga la kujiunga na chama cha True Democratic Tigers ni aweze kuwa kiongozi mwanasiasa mkubwa katika serikali mpya baadaye kwa kukwea cheo kwenye chama. Hii ni kwa sababu, hii ndiyo njia ya pekee yake ya kujihakikishia usalama wa utajiri wake. Emmanuel Mbogo anasema katika *Vipuli* kuwa:

> "... yaani majumba yake, mashamba yake na hususani madola yake aliyoyakimbiza huko Ulaya na Marekani. Madola yaliyotokana na uhai wa mioyo na figo za maskini, vipofu, Malaya, vichaa, wafungwa waliohukumiwa kunyongwa, wenye kupatwa na ajali, vilema, ... waliozagaa na kutapakaa katika vichochoro, mitaa na mageto ya jiji la Daluta." (uk. 241).

Ulemavu huongeza udhaifu wa watu kwa hatari za mazingira kama vile, mafuriko, ukame, maporomoka ya ardhi na uchafuzi wa hewa. Watu wenye ulemavu hukabiliwa na vikwazo vya kupata habari, huduma na rasilimali ambazo zingeweza kuwasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira. Aidha, hukabiliwa na ubaguzi na unyanyapaa unaopunguza ushiriki na uwezeshaji wao katika maamuzi na hatua za mazingira. Ukahaba huweza kuwa sababu na matokeo ya uharibifu wa mazingira. Baadhi ya watu wanaweza kujihusisha na ukahaba kama mkakati wa kukabiliana na kuishi katika mazingira yaliyoharibika, ambapo wana fursa na rasilimali chache. Ukahaba pia unaweza kuchangia uharibifu wa mazingira, kwani unaweza kuhusisha shughuli zinazozalisha taka, uchafuzi na gesi chafu kama vile usafiri, hoteli matumizi ya dawa za kulevya.

**Hitimisho**

Kwa kutamatisha sehemu hii ya uchunguzi wa aina za anthroposenia zinazosawiriwa na waandishi wa riwaya nne teule, utafiti huu umedhihirisha paruwanja aina zote za anthroposenia zilizosawiriwa kifasihi na Katama Mkangi na Emmanuel Mbogo. Mosi, wamemsawiri binadamu kupitia shughuli zake za kiuchumi na utabaka kama aina ya anthroposenia, kisha wamemsawiri kupitia utovu wa utu na maadili, kupitia teknolojia na maendeleo na hatimaye, kupitia utumwa wa kimawazo na kiutawala. Isitoshe, wamefanikiwa kuwasawiri kupitia ajenti wa uharibifu wa mazingira kama vile wanyama na wadudu mbalimbali pamoja na vifaa vinavyotumiwa na binadamu kama vile; fedha, simu na tarakilishi, pamoja na kitanda na mafuta kisanaa. Kadhalika, aina zingine za anthroposenia ambazo wamefanikiwa kuzisawiri ni kama vile; vurugu dhidi ya mazingira, jiografia ya binadamu, wafisadi, mabeberu wa kisasa, mabepari, utepetevu wa binadamu kupitia; dini, moto na sheria; na viongozi wabaya. Nguzo zilizoongoza uchanganuzi wa data kwa kila aina zilielezwa katika kila kisehemu cha uchanganuzi mintarafu ya lengo la kwanza la utafiti.

# SURA YA TANO

# UCHANGANUZI WA MBINU ZINAZOSAWIRI ANTHROPOSENIA

## 5.1 Utangulizi

Uchanganuzi wa data katika sehemu hii ulifanywa mintarafu ya madhumuni ya pili ya utafiti na kuongozwa na baadhi ya nguzo kuu za nadharia ya uhakikimazingira. Kwa mujibu wa madhumuni ya pili ambayo yalikuwa kuhakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni (2002), Vipuli Vya Figo (1996), Mafuta (1984) na Walenisi (1995)*, mtafiti alihakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia karika riwaya hizi nne teule za Kiswahili. Mintarafu nadharia ya Uhakikimazingira, nguzo kuu kama vile; lugha na mazingira, haki na maadili ya kimazingira, uwezo, utandawazi, na utamaduni na mazingira ziliongoza katika uhakiki wa mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule. Mathalani, baadhi ya mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia zilizohakikiwa ni kama vile; taashira, taswira, ishara, majazi, tashtiti, na tashihisi. Hivyo basi, data ilikusanywa na kuchanganuliwa kutoka katika riwaya nne teule za Emmanuel Mbogo na Katama Mkangi.

## 5.2 Taashira

Qiping na Quan (2022) wametumia nguo kitaashira kuashiria uwezo wa mataifa tofautitofauti ulimwenguni katika udadisi wao wa uhusiano kati ya mama na msichana wake katika riwaya ya Amy Tan, katika upeo wa karne ya ishirini. Uwezo ni mojayazo ya nguzo kuu za nadharia ya uhakikimazingira iliyoongoza uhakiki wa namna taashira ilivyotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule za Kiswahili, kando na nguzo za lugha na mazingira, haki na maadili ya kimazingira, pamoja na nguzo ya maumbile. Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 208), "taashira ni aina ya tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumiwa kuwakilisha kitu kamili au kingine kinachohusiana nacho." Waithiru (2019: 4) anaeleza kuwa, "taashira hutoa ujumbe zaidi ya kile kilichoandikwa au maelezo ya chombo, kama vile, meli, nahodha, bahari, dau, au mabaharia. Waithiru (2022a) anaongeza kuwa, taashira huwa na uwezo wa kukipa kifaa, hali, jambo, viumbe hai na au visivyo hai na pia hisia, fahiwati zenye kina, uketo na au huweza kupanua fahiwati na dhana za kawaida. Kadhalika, huweza kuzipa maana maalum istilahi zilizoandikwa, ambazo ni tofauti na zile zinazofahamika katika hali ya kawaida na kuzifanya ziwe ala zenye

uwezo na umadhubuti katika kuwasilisha ujumbe lengwa kwa hadhira lengwa upesi na kwa njia nyepesi. Katika utafiti huu, dhana ya taashira iliangazwa katika misingi ya namna ilivyotumiwa na waandishi kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule. Hata hivyo, taashira ilidhihirika katika vipengele aina aina kama vilivyohakikiwa katika sehemu hii.

### 5.2.1 Taashira ya Mahali

Katika utafiti huu, istilahi ya mahali ilitumiwa kuelezea eneo au nafasi ambayo kitu au mtu huweza kukaa au kuishi, kufanya kazi, kutengeneza bidhaa, kutupa taka, kuabudu au hata kuwazia kwenye ubongo (Collins, 2014; Waithiru, 2019). Hivyo, istilahi hii ilivuka mipaka ya maana yake ya kawaida katika utafiti huu na kuhusisha dhana zingine tofauti kwa kuzirejelea kama dhana moja sawa yenye maana sawa. Mathalani, mwandishi wa *Bustani* anaashiria athari hasi pamoja na maangamizi yanayozalishwa na shughuli zinazopalilia maendeleo endelevu kama vile, viwanda. Viwanda kando na kutoa nafasi za ajira kwa vijana na wananchi kwa jumla, huendeleza maendeleo endelevu. Hata hivyo, katika harakati za kuendeleza shughuli za viwanda za kila siku, takataka mbalimbali na hatari kwa maisha ya binadamu huzalishwa. Mathalani, kiwanda cha *Saga Saga Chemical Industry* kinazalisha na kutupa unga wa kemikali pamoja na mafuta ya dizeli pale kwenye dampu la Siza. Jonalisti alipokuwa pale kwenye dampu la Siza, mwandishi anaeleza kuwa, baada ya kuweka kamera begani, alipiga hatua na kuvuka nyasi fupi zilizoliwa na unga wa kemikali na mafuta ya dizeli. Nyasi zile zinaashiria jinsi mazingira huharibiwa na kunajisiwa na uchafu kutoka viwandani ambavyo waasisi, wafadhili na manahodha ni binadamu. Hususani binadamu wenye uwezo wa kiuchumi ambao huyachafua mazingira yao bila kutarajia na ya wanyonge kwa kukusudia.

Dampu la Siza linaashiria utowajibikaji wa viongozi na binadamu kwa jumla katika uhifadhi wa mazingira. Kwa mfano, athari hasi za uchafuzi wa mazingira zinadhihirika pale ambapo mwandishi Mbogo katika *Bustani* anaeleza kuwa, "Moshi uliotokana na vibiwi vichache vya takataka zilizounguzwa ulifuka, ukajisokota na kusambaa sehemu zote za eneo la dampu lile. Jonalisti alipiga chafya na kusonga mbele." (uk. 24). Kule kupiga chafya kunaashiria athari hasi za kiafya dhidi ya binadamu. Hili dampu la Siza linaashiria viongozi wengi barani Afrika ambao huwa hawayawajibikii mazingira. Hivyo, wao huchangia utupaji taka ovyo bila kuzingatia mazingira safi. Zile takataka zinapotupwa ovyo, mazingira huathirika na huweza

kusababisha maradhi mbalimbali kwa binadamu. Hali hii inafungamana na nguzo ya uongozi mbaya.

Shamba la Edeni la Matope – Pipajaa la mama Fofi – ni taashira ya maeneo yanayopalilia utegemezi na ulofa. Mhusika Matope katika *Mafuta* anadhihirisha hili kupitia ufafanuzi wake kuwa, akina mama Fofi walikuwa wanambakishia makombo ya heshima kupitia sahani-sahani za vidohodoho vitamu pamoja na vinywaji vya soda na hata vikali. Pipa-jaa hili linaashiria mataifa fukara ya Afrika, ambapo watu duni kama vile walinzi na mbwa huishi maeneo sawa. Kwa mfano, pipa-jaa hili lipo nyuma ya nyumba za watumishi karibu sana na kijumba cha jibwa mlinzi. Aidha, seng'enge za miba pamoja na kucha za tai ni taashira ya anthroposenia na athari zake hasi, hasa dhidi ya wachochole na mataifa fukara ulimwenguni. Ndiposa mgongo wa Matope unadondoka damu baada ya yeye kujipenyeza katikati mwa seng'enge ili kulifikia pipa-jaa lile. Hili linawiana na nguzo ya uwezo ambapo wenye uwezo huwadunisha waduni na hatimaye kuwaangamiza. Hakika udhalilishaji huu wa ubinadamu husababisha madhara kwa maisha ya watu na mazingira yao kwa jumla.

### 5.2.2 Taashira ya Vifaa

Kifaa ni kitu chochote ambacho hutumiwa kwa minajili ya kutekeleza kazi au shughuli fulani (Waithiru, 2019; Waithiru na wengine, 2021), pia hurejelewa kama chombo. Magari yale ya *Town Council* yanaashiria ala za uharibifu wa mazingira zinazotumiwa na binadamu katika anthroposenia. Mathalani, katika dampu la Siza mlikuwa na maji machafu ambamo miguu ya Jonalisti iliweza kukanyaga. Maji yale yalikuwa yamemwagwa pale na moja ya magari ya *Town Council*. Hili linaashiria vita dhidi ya mazingira vinavyoendelezwa na binadamu katika anthroposenia. Kadhalika, kamera yake Jonalisti ni taashira ya ala zinazotumiwa na binadamu katika anthroposenia kupigana na unajisi wa mazingira. Hili hufanikishwa kupitia video na picha zinazonaswa na hatimaye kutumiwa kuwahamasisha wanajamii dhidi ya athari hasi za uchafuzi wa mazingira na pia kuwaelimisha njia na mbinu mbadala za uhifadhi na utunzaji wa mazingira katika anthroposenia. Hivyo, kando na binadamu kupalilia anthroposenia huwa anakabiliana na anthroposenia kwa njia madhubuti namna anavyoweza.

Mhusika Jonalisti kwa kutumia kamera yake, aliwapiga picha wanawake wawili waliokuwa wameinama wakiokota mabonge ya ugali na kuyatia kwenye vikapu vyao. Hili linadhihirisha kuwa uharibifu wa mazingira huzalisha ulofa na hasa njaa katika

anthroposenia. Vilevile, alipiga picha lundo la sindano za hospitali, madawa ya aina tofautitofauti yaliyokuwa ndani ya chupa, pamoja na pamba na mabendiji yaliyochanganyika na damu. Hakika, kupatikana kwa uchafu wa aina hii kunadhihirisha uongozi mbaya pamoja na kutowajibika kwa wizara, idara na wafanyikazi kwenye hospitali za umma na za kibinafsi katika mataifa mengi barani Afrika katika anthroposenia. Katika mazingira chafu, binadamu anasahau ustaarabu na kujidunisha kiwango cha mnyama. Aidha anajikosea heshima, utu, na staha kwa kujiweka kiwango sawa na mbwa, ndege na nguruwe ambao huvinjari na kuzozania mabaki na uchafu, hasa uchafu ambao huwa hatari kwa afya ya mwanadamu. Hili linadhihirika pale ambapo, watu kama sita hivi wanapofika kwenye lundo lile la sindano za hospitali, madawa, pamba na mabendiji yaliyochanganyika na damu, wanalivamia lile lundo.

Wanazozana na mtafaruku pamoja na tafrani ya kugombea uchafu, taka hatari na vifaa vyenye virusi unazuka. Mtafaruku ule ulipokuwa unaendelea, Jonalisti alishuhudia na kupiga picha kadhaa. Mwandishi Mbogo kwa kinaya anarejelea uchafu ule hatari kama almasi, dhahabu na lulu za dampu. Hili linaashiria namna binadamu amejidunisha kutokana na ulofa, kiwango kwamba anaweza kugombana na mwenzake dhidi ya takataka na kuzichukulia zile taka kwa heshima na taadhima. Hivyo, kamera ni ala inayotumiwa kupigana na unajisi wa mazingira. Kwa mfano, Jonalisti katika *Bustani* anachukua picha kwa minajili ya kuweka bayana utepetevu wa utawala wa mji wa Siza, hasa katika utupaji taka. Mathalani, mtunzi Mbogo katika *Bustani* anaeleza kuwa:

> "Jonalisti alirudi nyuma – furaha usoni si ya moyoni, kuwa amepata picha nzuri ambazo zingekuwa kielelezo kizuri cha wakuu wa Town Council na serikali walivyokuwa wanalea uchafu ule uliowasababishia wananchi madhara makubwa." (uk. 25).

Mkono wa binadamu unaopatikana na mmoja wa wale watu sita ni taashira ya maangamizi na ufukara yanayonawiri na kushamiri kama zao la anthroposenia. Ingawa mna wale wanaoshtushwa na hali ya mambo, wengine wamezoea dhiki, maafa na uozo wa maadili na wa uongozi na utawala, kiwango kwamba hawaoni la ajabu wakati watu wanaangamia na pia maiti za wafu zinapokosa kuheshimiwa. Katika kipindi cha mabadiliko makuu hasi ya mazingira, mizoga ya maiti inatupwa

ovyo kutokana na wingi wa maafa, hivi kwamba baadhi ya watu wakiangamia haijulikani na maiti hutupwa ovyo. Hili linaashiria maafa na uozo wa hali ya juu. Kwa mfano, ule mkono wa binadamu uliopatikana kwenye lile lundo la pamba na mabendiji yaliyochanganyika na damu, ulikuwa mzima. Aidha ulianzia begani, kiwikoni hadi kwenye kiganja. Mtu wa kwanza kuuona alipiga yowe lakini mwingine jasiri alichukua mti na kuurusha mahali peupe zaidi ambapo wote waliweza kuuona. Ulikuwa umekwishaanza kuoza na vidole viwili tayari vilikuwa vimedondoka na kupotelea kwenye taka au kuliwa na mbwa au nguruwe waliotamalaki dampu la Siza kila uchao.

Mtunzi Mbogo katika *Bustani* kupitia mhusika Jonalisti anadhihirisha vitabu kutoka kwenye maktaba ya Wilaya kama ala ya kupigana na uharibifu wa mazingira kitaashira. Hivyo basi, anaweka bayana kuwa, katika anthroposenia, vitabu vina nafasi kubwa katika kuwahamasisha wanajamii dhidi ya athari hasi za uchafuzi wa mazingira na haja ya kudhibiti anthroposenia. Hata hivyo, vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira vinahitaji ukakamavu, ushupavu na kujitoa mhanga. Mathalani, mkutubi wa kuazima vitabu pale maktabani anazembea kazini na kisha baada ya kuona vitabu alivyoagiza Jonalisti, anasinya. Hili linadhihirishwa pale ambapo anamkejeli Jonalisti katika *Bustani* kwa kumwambia kuwa, “Wenzako wanasoma novo, hadithi za kusisimua, wewe unasoma,” alisinya macho yake. “Nini?! *Pollution!* Mghuja!” (uk. 29). Hakika vita hivi vinakumbwa na vikwazo humu barani Afrika kutoka kwa Waafrika wenyewe, ambao ndio wameathirika zaidi kutokana na uchafuzi na uharifu wa mazingira ikilinganishwa na Ulaya, Uropa, Marekani na mataifa mengine tajiri. Hali hii inawiana na nguzo ya uwezo.

Aidha, mikate, mayai ya kukaanga, mvinyo na gari pia havijasazwa katika kusawiri anthroposenia kitaashira. Hii ni kwa sababu, misokoto myeusi ya moshi iliyochimbuka kutoka kiwanda cha Sagasaga ina kemikali sumu ambazo zinaliwa na kuhifadhiwa na mimea. Mimea ile kutokana na kemikali inadidimia kiukuaji na kikiwango. Kwa mfano, nyasi alizokanyaga akivuka Jonalisti pale kwenye dampu la Siza zilikuwa fupi kutokana na kemikali na mafuta ya dizeli. Gari nyeupe linaashiria namna anthroposenia inakamafleji ili isibainike kwa urahisi na badala yake ionekane kuwa takatifu. Benzi lake Bwana Abdula ni la rangi ya maziwa, kuashiria utakaso. Gari lenyewe linaguruma kwa chini kabisa kuashiria kuwa linahifadhi mazingira ilhali ni kinyume, ndilo linalopalilia na kusambaza kemikali hewani. Linatoa moshi mdogo

sana mweupe kupitia eksosi kuashiria usafi ilhali linahifadhi uchafuzi wa hewa. Tofauti na wananchi hohehahe, matajiri wanaopalilia uchafuzi wa hewa wanakamafleji kwa kuosha magari yao. Bwana Abdula ana mtumishi, Juma ambaye kazi yake ni kuyasafisha magari ya ukoo wa Bwana Abdula.

*Jabali la Magonjwa* sawa na *Jabali la Ujinga* ni taashira ya anthroposenia. *Mtambo-Mtu* anamjuza Dzombo kuwa, umbali wa *Jabali la Magonjwa* linapomkabili ni sawa na ule ule uliokuwa wa *Jabali la Ujinga*. Bunker na Ciccantell (2005), Musembi (2019), Gill (2016), na Moore (2018) wanapambanua kuwa, anthroposenia hunajisi ethnografia asilia ya jamii hasa katika mataifa ya ulimwengu wa tatu kutokana na hila na unafiki ambavyo huitawala na kuiendeleza anthroposenia ulimwenguni. Mwandishi wa *Walenisi* anasisitiza kuwa, ingawa anthroposenia hujidhihirisha kupitia miundo tofautitofauti, kunayo miundo itishayo na kuvuma zaidi kuliko mingine. Mathalani, lile la magonjwa lilitisha na kuvuma zaidi kuliko lile la Ujinga. Hii ndiyo sababu, *Jabali la Magonjwa* lilionekana kufura kila nukta kutokana na athari zake hatari na tena za maangamizi. Hili linafungamana na nguzo ya haki na maadili ya kimazingira.

Hata kama anthroposenia hutatiza na kuchukiza kando na kuangamiza, kuna miundo yake ambayo hakika hukirihisha. Kadhalika, anthroposenia hupaliliwa na kuendelezwa na uchafuzi wa mazingira. Kwa mfano, Dzombo anakiri kuwa, *Jabali la Magonjwa* linanuka na kuvunda kweli. Dzombo katika *Walenisi* anafafanua kuwa:

> "… halikupendeza kamwe, aliweza hata kuhisi kunuka na kuvunda kwake kwa kule kuliangalia lile umbo lake tu pale kiooni! Hata yale maumivu yaliyokuwa ndani ya Jabali hili, yaliweza kutanabahika kwa namna ya vile lilivyoumbika! Kutisha kwake hakuelezeki." (uk. 23).

Ikumbukwe kwamba, maradhi hushamiri katika mazingira chafu. Kunuka na kuvunda kwa Jabali hili kunaashiria uchafuzi wa hali ya hewa na dalili ya maafa. Kadhalika, maumivu yanayotanabahika kutoka ndani ya Jabali lile kutokana na jinsi lilivyoumbika, yanaashiria dhiki, mateso na dhuluma zitokanazo na anthroposenia katika maisha ya binadamu. Kadhalika, changarawe za ndui na za tetemaji, magondolea ya matumbwitumbwi, kimbunga cha mbuba, upele na mafunza ni taashira ya anthroposenia. Kohozi la kifaduro, homa ya minyoo, baridi yabisi, safura, macho, masikio, na kichocho pia vyaashiria anthroposenia. Aidha, katika

anthroposenia nishati za nuklia hushamiri. Dzombo anathibitisha hili anapotaja katika *Walenisi* kuwa, "… zilikuwa zikitumia nishati ya kinuklia." (uk. 24). Bila mipango na uratibu madhubuti wa uhifadhi na matumizi na pia namna ya kutupa taka zake, nuklia hupalilia anthroposenia pakubwa na hatimaye, huzalisha maafa yasiyomithilika yakiwa ni pamoja na ya uhai wa mazingira, viumbehai na viumbe visivyohai kimwavuli kwa miongo mingi. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo na kifo.

Miamba ya kitabaka na harufu inayotoka kwenye miamba hii ni taashira ya anthroposenia. Harufu inayotolewa na miamba hii ni ya sumu kali ambayo yeyote ainusaye kwa wingi huweza kudhoofika kimawazo daima. Hii inadhihirisha athari hasi na hatari kwa binadamu, kutoka kwa anthroposenia izalishayo njaa na maafa. Sumu yenyewe inazalishwa na ukosaji wa lishe bora hasa kwa walio ndani ya tabaka la chini. Katika utabaka, ufukara na uchafuzi na uharibifu wa mazingira hushamiri. Hata hivyo, wanaoathirika sana ni wale wa tabaka la chini ambao hubeba uzito wa tabaka la kati lililo juu yao. Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anathibitisha hili anapoeleza kuwa, "Kwa wale wapagazi, sumu hii haiachi kutiwa ukali kila nukta na ushuzi utokao kwenye hilo paa zito la wachache lililo utosini mwao." (uk. 25). Ikizingatiwa kwamba watoto ndio huendeleza kizazi cha binadamu, wanapoumizwa na kuangamizwa kutokana na utabaka na ubaguzi, hili linaashiria maangamizi ya binadamu. Hakika hili linafungamana na nguzo ya uwezo ambapo wenye nguvu huwanyanyasa wanyonge pamoja na na mazingira yao mtawalia.

Kadhalika, anthroposenia kupitia udhibiti wa utawala na uongozi huuhanithi na kuufanya udongo kuwa chombo cha biashara na kamari. Kwa misingi hii, udhibiti wa utawala na uongozi hueneza mila, desturi, utamaduni na sheria zinazosaidia kuukuza na kuuendeleza udhibiti wa utawala na uongozi wa mataifa duni. Udhibiti huu unaashiriwa na falme, dola na himaya mbalimbali zinazoupalilia kila wakati. Hivyo, miungu, lugha, mawazo na hata ndoto zisizopalilia udhibiti huu zinaanguka na kufifia. Mwandishi Mkangi anadhihirisha hali hii katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, "… wale waliotawaliwa, vyote vyao vilipuuzwa na kuitwa vya kishenzi. Si tamaduni zao wala lugha zao. Dini, sheria, desturi, mawazo, maendeleo na hata majina yao – vyote hivi, vilidharauliwa na kuitwa vya kishenzi." (uk. 171). Udhibiti wa utawala na uongozi kutoka kwa mataifa tajiri dhidi ya yale fukara unaangamiza kila kitu kinachoupinga. Katika jamii ya Wachuna kwa mfano, lililotambuliwa na watawala ni lile lililokuwa

likidumisha dhuluma, maonevu na ulofa ila si kwa kuwa ndilo lililostahili. Hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya.

Afya kama chombo cha biashara ni taashira ya anthroposenia. Ingawa inatarajiwa kuwa afya bora ni haki ya kila mtu, madhali kifo huwapata watu wote, Wachuna wanabidhaisha afya na kuifanya huduma ambayo ingempata aliyeweza kuinunua. Mwandishi anadhihirisha hili katika *Walenisi* anaposema kuwa, “Aliyebahatika kupata kitanda, ilimbidi kuzaa kwa makofi na matusi ya wauguzi na wakunga.” (uk. 179). Kama vile tu anthroposenia huwafaidi matajiri wachache huku wananchi wengi fukara wakiangamia, Wachuna wanajipa makao safi na salama pamoja na hospitali zenye vifaa tele, dawa za kutosha, madaktari na wauguzi wa kutosha waliohitimu, wasaidizi wanyenyekevu wengi na hivyo hayakuwa na misongamano ya wateja wenye maradhi tofautitofauti. Aidha, kila Mchuna alikuwa na daktari wake binafsi aliyekuwa akimtibu na kumhudumia akiwa kwake nyumbani au hospitalini. Kwa upande mwingine wananchi fukara wanateseka mumo humo. Ikiwa mama angefika hospitalini kujifungua, mara nyingi wamama walijifungua wakiwa bado wamesimama wakingojea kuhudumiwa. Ingetokea kwamba mama mjauzito angelalamika kutokana na maumivu, alikemewa, alizabwa makofi na alidhulumiwa bila kikomo. Hakika hili linawiana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo viongozi hupalilia ulofa na maangamizi ya viumbe na mazingira yao kwa jumla. Vifo vinavyotokana na utepevu na utelekezaji wa uongozi pamoja na sera dhoofu huchangiwa na umaskini wa viongozi na uongozi katika maeneo ambapo vifo vinavyoweza kuepukika huwakumba watu kama jambo la kawaida.

Ubidhaaishaji wa afya bora, unapalilia anthroposenia kwa kuongeza maafa. Baada ya wamama maskini kujifungua kwa dhiki na mateso, uzazi wao ulikuwa unatolewa bila wao wenyewe kujua, kufahamishwa au hata kupewa fursa ya kujiamulia wenyewe. Utasa huu uliosababishwa na wauguzi na madaktari Wachuna kwa wanawake maskini unadhalilisha utu na uhai wa binadamu na kukuza unyama. Mbinu hii ya utasa ilitumiwa na Wachuna kwa lengo la kupunguza ongezeko la watu duni katika ulimwengu wa Wachuna. Ingawa ongezeko la watu ulimwenguni husababisha ongezeko la uharibifu na uchafuzi wa mazingira kimwavuli (Morton, 2015; Arboleda, 2020; Frantzen na Bjering, 2020; Sritama, 2022), mauaji ya kizazi cha kesho ni maangamizi kamili ya ulimwengu na mazingira yake pia katika mfumo wa kisasa wa kapitalosenia ambao ni zao la anthroposenia (Moore, 2016, 2017, 2018; Simon na

Mark, 2018; Appel, 2019). Hili linafungamana na nguzo ya uwezo na kifo ambapo wenye nguvu huwadhulumu wanyonge na hatimaye huwaangamiza pamoja na mazingira yao.

Visibo vya soda vinavyotumiwa kama pesa na Zuka na wenzake katika riwaya ya *Mafuta* ni taashira ya sarafu ya mataifa fukara ya Afrika. Sarafu hii hudharauliwa na mataifa tajiri ya Ulaya, Uropa, Marekani, na mengine mengi hivyo, baada ya kuyakopesha mikopo yenye riba ya juu mataifa fukara ya Afrika, hudai yalipwe kupitia sarafu yao. Sarafu yao inaashiriwa na kunazi. Zuka na Kazamoyo wanaashiria mataifa fukara ya Afrika ambayo hujipata katika dimbwi la madeni ambayo hushindwa kuyalipa kama zao la anthroposenia. Kwa mfano, mwandishi anaeleza katika *Mafuta* kuwa, "Zuka na Kazamoyo … hawakuweza kushangaa ni kwa namna gani madeni yao ya visibo … yatakuwa ya kunazi! … Lililokuwa dhahiri kwao ni kwamba hawangeweza kulipa madeni yao … muda ulikuwa hauruhusu." (uk. 2). Hali hii inaashiria anthroposenia katika misingi ya nguzo ya uwezo ambapo mataifa ya Afrika yanadanganywa na kutumikishwa katika utumwa wa madeni. Mataifa ya Afrika huwa machanga na yenye uwezo wa kuzalisha mali kutokana na rasilimali zao asilia pamoja na nguvu yaliyonayo ya rasilimali ya wafanyakazi (Waithiru, 2019). Hivyo, anthroposenia huzalisha mabadiliko ya unyanyasaji, dhuluma na maonevu. Zuka na Kazamoyo wanadhihirisha hili wanapokanganywa na mageuzo ya kukopeshwa visibo vya soda kisha wanalipa madeni yao kwa kutumia kunazi.

Vidole vya viganja, majembe na fahali wawili zizini ni taashira ya anthroposenia. Baba mmoja katika riwaya ya *Mafuta* mle mahakamani anafafanua kwa ngurumo ya kutisha kuwa, visa vya vita vya vidole vya viganja vijinawishapo ni vita vya undugu. Vidole vinavyorejelewa ni aina ya anthroposenia – binadamu ambao hupigana wenyewe kwa wenyewe – na huendeleza vurugu dhidi ya mazingira, pamoja na ubidhaaishaji wa ubepari katika juhudi za kufaidi uongozi dhalimu, ubaguzi, ufisadi na uharibifu wa mazingira. Ikizingatiwa kwamba watu hawa hupalilia uongozi mbaya na ubaguzi huunganishwa na lengo moja la kuendeleza dhuluma na maonevu, basi hamna yeyote ambaye humuumiza mwenzake wala kumdhuru, ila wanyonge hukanyangwa na kutumiwa kama mbolea kunawirisha uongozi dhalimu, siasa za ulofa, uchafuzi na uharibifu wa mazingira pamoja na maangamizi kupitia jasho, damu na uhai wao. Hali hii inafungamana na nguzo za uongozi mbaya na utandawazi.

Mtunzi Mkangi kupitia baba mmoja pale mahakamani katika *Mafuta* anathibitisha hili anapoeleza kuwa, “Hakuna kidole hata kimoja kilicho na meno na ambacho kinaweza kudhuru wenzake … na hii ni kawaida kwani majembe hayaachi kugongana yakiwa pamoja.” (uk. 23). Majembe yanayorejelewa ni taashira ya anthroposenia na athari zao hasi dhidi ya uhai wa binadamu. Kule kugongana kwa majembe kunaashiria athari hasi za vikaragosi wa viongozi wa mataifa tajiri ya Ughaibuni katika kuyabadilisha mazingira na maisha ya viumbe hai na visivyohai. Nao fahali wawili zizini wanaashiria viongozi dhalimu katika mataifa fukara hususani ya Afrika katika janibu zinazoihifadhi na kuilinda anthroposenia. Hivyo, vita vya fahali hawa wawili zizini linakuwa tukio la ajabu na linalochipuka kama kesi ya jinai. Hii ni kwa sababu, ni kinaya kupata viongozi dhalimu wakiathirika na athari zao wenyewe. Hakika hili linakinzana na nguzo ya uongozi mbaya lakini linashabihiana na nguzo ya utandawazi katika mataifa yanayojinyonyoa manyoya dhoofu yanayoyazuia kupaa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Athari hizi hasi zinadhihirishwa na mhusika Matope anayelala, kuamka na kuishi kwenye bahari ya ulofa, njaa, maradhi na ubaguzi tele maishani mwake, ambazo ni athari hasi za uongozi dhalimu unaopalilia ufukara. Matope anaeleza katika *Mafuta* kuwa:

> “Tumezaliwa matopeni, tumezaana matopeni, tumekufa matopeni na tutazikana matopeni. … Mmefanya uongo ukawa ukweli na ukweli, uongo … Mmepindua hata sheria za maumbile ili kumamatia enzi yenu … Unyama wenu ndio utu na utu wetu ndio unyama. … Tutazuka basi na Maji tuyakomboe.” (uk. 40 – 1).

Matope ni jina la kimajazi linaloashiria taswira halisi inayopaliliwa na kuendelezwa na viongozi dhalimu na visesere vya mataifa ya Ughaibuni, hususan katika nchi fukara za Afrika. Ni kutokana na kushindwa kustahimili athari hizi anapoyatumia maji kukabiliana na wabaguzi, wafisadi na watesi wake. Matope analalamika kuwa, viongozi dhalimu huubadili uongo kuwa ukweli na hubadili sheria kwa manufaa yao wenyewe. Uadimikaji huu wa utu baina ya viongozi wa Afrika unapalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Hili linawiana na nguzo za utandawazi na uongozi mbaya.

Tonge linalorejelewa na mama Fofi linaashiria anthroposenia kamili katika mviringo wao. Mdee na wengine (2015) na BAKITA (2022) wanaeleza kuwa, tonge ni donge la

chakula kama vile, ugali au wali lililomegwa na kuviringwa kwa mkono. Hivyo, anthroposenia huwafaa matajiri, viongozi pamoja na wenye vyeo na vyao ambao humomonyoa uhai wa wanyonge mithili ya mafuriko yamomonyoayo udongo. Lakini, hata kabla ya mama Fofi kulimeza tu, Matope anaangamiza ulaghai na dhuluma kwa kuyatumia maji ambayo yanaashiria maangamizi ya ulaghai, maonevu na maafa na kutanguliza uchipuzi wa uhai kamili bila anthroposenia. Hili linaashiria matumaini ya kukabiliana na anthroposenia ulimwenguni.

Harufu itokayo kwenye mapipa-jaa ni taashira ya anthroposenia kupitia uduni. Hii ndiyo sababu mseto wa masaza, uozaji wake na uvundo kwa jumla hutoa harufu ya kuridhisha kwa Matope na wachochole wenzake. Ingawa ni harufu ya kughasi, kwao ni dalili ya shibe. Ndiposa Matope anapata uzoefu wa kung'amua pipa-jaa lenye vinono kwa kufuata harufu tu. Mathalani, harufu ya kakasi inamjuza kuwa mabaki yale ni ya chakula kisicho na bizari na ambacho hakijaiva vizuri. Matope anathibitisha uhitaji, ufukara na ukame anapotaja kuwa, "Mlo upatikanao kwenye mapipa-jaa haya hutupunguzia kuendesha kwa siku haba hivi." (uk. 38). Harufu ya jasho la makwapani nayo inatangazia waduni kuwa mabaki yale ni ya chakula kilichochacha kabla ya kutupwa jaani. Isitoshe, harufu ya kidonda kibichi inawajuza kuwa masaza yake yako shwari na yamenoga ladha, uhondo na virutubishi kemkem. Lakini harufu iliyopiku harufu zote na kuashiria shibe na raha, ni ile harufu ya marashi yaliyovunda kwa kuwa mwenye kujipaka amesusia kuoga. Harufu hii iliashiria kuwa makombo yaliyomo mle ni mlo wa maana na hadhi kuu, madhali hayakutiwa dawa ya kunguni au hata kukojolewa na wenye mali. Hili linawiana na nguzo ya uongozi mbaya na ile ya uwezo.

Sanamu kubwa iliyopo karibu na lango la kuingilia hoteli kubwa ya kitalii – Village Inn – inaashiria anthroposenia. Sanamu yenyewe imesaniwa kwa madini ya shaba. Rangi yake nyekundu inaashiria hatari. Hii ni kwa sababu, sanamu inaonyesha mnyama ambaye ni nusu shetani. Hali hii inaashiria anthroposenia, ambapo binadamu amekuwa nusu shetani na kupalilia maangamizi hadi katika maeneo ya starehe na burudani. Village Inn ni taashira ya mataifa mengi barani Afrika ambayo huwa na amani na utulivu. Hata hivyo, watu wametamalaki unyama na kuuepuka utu. Hawa ndio wanaosawiriwa na sanamu hii kama wenyewe ni nusu binadamu na nusu shetani. Sanamu hii inaashiria zimwi-mtu. Hivyo, linaashiria hali ambapo binadamu yule yule anayumba kimsimamo na kuwa na vichwa viwili. Vichwa hivi vinaashiria mvutano

kati ya utu na anthroposenia. Mwandishi wa *Vipuli* anathibitisha hali hii kupitia swali la Angela kuwa, "Maana yake nini? Kuwa; binadamu ni zimwi au zimwi ndiye binadamu?" (uk. 63). Ndiposa sanamu ile yenye umbo la zimwi-mtu inampa Angela hali ya unyonge na msisimko kwa wakati huo huo katika nafsi yake. Hili linalandana na nguzo ya uwezo na utandawazi.

Geti la Ubalozi wa Osantonio ni jeusi na limejengewa nembo ya tai mkubwa. Rangi nyeusi na nembo ya tai ni taashira ya anthroposenia. Waithiru (2022b) anadokeza kuwa, waandishi katika kazi za fasihi hutumia rangi kuashiria dhana tofautitofauti kiishara na kitaashira. Lundberg (2019) anaongeza kuwa, rangi nyeusi huwa taashira ya laana, huzuni, maafa, shetani au maradhi kutegemea utamaduni wa jamii husika. Katika riwaya ya *Vipuli*, mtunzi Mbogo ametumia geti jeusi kama taashira ya anthroposenia. Kwa mfano, anapambanua kuwa:

> "… geti jeusi lililojengewa nembo ya tai mkubwa anayetua toka mbinguni, domo lake imara na macho yake makali, yamelenga shabaha chini ardhini, mbawa zake zilizopetuka … zilielekea juu, miguu yake mikubwa yenye makucha makali ilitazama chini ikilenga windo lake tayari kulikwepua." (uk. 110).

Nembo ya tai inaashiria viongozi dhalimu katika mataifa fukara ya Afrika. Nembo hii ya tai mkubwa inamsawiri tai anayetua kutoka mbinguni. Mbinguni ni taashira ya mataifa tajiri ya Ulaya yenye uwezo wa kuyaangamiza mataifa fukara ya Afrika kwa mkupuo mmoja kupitia anthroposenia na athari zao hasi. Domo la tai huyu imara pamoja na macho yake makali yanayolenga shabaha chini ardhini vinaashiria namna anthroposenia ina uwezo wa kuyadonoa mataifa fukara ya Afrika kutoka duniani na kuyameza. Dunia inaashiriwa na ardhini katika misingi hii. Mbawa zake kubwa zinaashiria anthroposenia kupitia uwezo wa mataifa tajiri ya Ughaibuni wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo ya Nadharia ya Uhakikimazingira. Miguu yake mikubwa yenye makucha makali inayotazama chini inaashiria namna anthroposenia huyavamia mataifa ya Afrika vikali na kwa ushabaha wa hali ya juu.

### 5.2.3 Taashira ya Viumbe

Kimsingi, kiumbe ni kitu chenye uhai ambacho kibayolojia huwekwa kwenye kategoria ya ufalme wa wanyama ila si wa mimea (TUKI; 2006; 2013; 2014; BAKITA, 2015; 2022; Wamitila, 2022). Kwa mfano; binadamu, wanyama, samaki, ndege na wadudu ni viumbe (Ndalu na wengine, 2014; na Mdee na wengine, 2015). Mandhari ya dampu la Siza yanaashiria mazingira katika mataifa mengi barani Afrika, ambapo watu na wanyama huzozania uchafu na huharibu mazingira bila simile, hususani katika anthroposenia. Mathalani, nguruwe ambao ni taashira ya watu walafi wasiojali wengine, katika anthroposenia. Nguruwe ni taashira ya uchafuzi wa mazingira na pia ajenti wa uharibifu wa mazingira. Kwa mujibu wa Waithiru (2019, uk. 65), "nguruwe ni mnyama mnene na mfupi afugwaye, mwenye pua kubwa na ndefu, miguu mifupi na mkia mfupi ambaye Waislamu hawali nyama yake kwa kuwa ni haramu." Kadhalika, anafafanua kuwa, nguruwe huhusishwa na uchafu, kutoshiba kwa urahisi, kukoroma, kubugia kila kinacholika bila ubaguzi, tamaa na unono wa aina yake.

Katika anthroposenia, nyama ya nguruwe inaendeleza uchafuzi wa mazingira kwa kuwachafua binadamu na kemikali. Mazingira wanayoyavinjari nguruwe yana uchafu hatari. Mwandishi wa *Bustani* anasisitiza kuwa, kulikuwapo majimaji, miozo ya mabaki ya mafuta machafu pamoja na miozo ya mabaki ya nyama iliyotoa mijifunza mikubwa. Mtunzi Mbogo ameashiria mwanamke kama ajenti wa uchafuzi wa mazingira katika anthroposenia. Hili analiafiki pale anapopambanua kuwa, "… matambara ya sodo, watoto walioharakisha kuingia duniani kabla ya wakati wao …" (uk. 26). Hili linaashiria maangamizi, sio tu ya mazingira ila pia ya binadamu katika anthroposenia. Moshi uliofuka na kuzagaa pale kwenye dampu la Siza ni taashira ya athari hasi dhidi ya binadamu zitokanazo na uharibifu wa mazingira katika anthroposenia. Ikizingatiwa kwamba nguruwe wanaashiria viongozi fisadi, binafsi na wachoyo katika mataifa mengi barani Afrika, uchafuzi wanaoendeleza unaashiria uchafuzi wa viongozi kwa mataifa yao duni. Kadhalika, mintarafu ya mhimili wa uwezo, utupaji wa taka na uongozi wa jiji unaashiria uchafuzi wa mazingira ya mataifa duni ya Afrika kutoka kwa yale yenye uwezo na rasilimali kama vile magari ya Halmashauri ya mji wa Siza. Hali hii inafungamana na mhimili wa maadili ya mazingira ambapo binadamu anasutwa kutoyanajisi mazingira hata kama ana mamlaka juu ya mazingira yenyewe (Howarth, 1996).

Mathalani, katika *Bustani* Jonalisti anapotoka mle kwenye dampu, anakohoa, huku machozi yakimtoka kutokana na moshi, kiwango kwamba anatoa kitambaa na kujifuta michirizi ya machozi. Watoto wale wawili waliokuwa wa kama miaka minane hivi anaokutana nao Jonalisti, yaani Franco na Kidonda Zambarau ni taashira ya mataifa changa barani Afrika, ambayo yananyongwa na uchafu katika mazingira yaliyonajisiwa pakubwa. Mataifa haya yanaugua nduli tofautitofauti kutokana na unajisi wa mazingira. Mathalani, punde tu Jonalisti anapokutana nao mara ya kwanza, mmoja wao – Kidonda Zambarau – alikuwa na donda moja kichwani lililoonekana kutoa usaha na majimaji. Isitoshe, donda lenyewe lilikuwa na rangi ya zambarau. Katika mkono wake wa kulia, Kidonda Zambarau alikuwa amepakata chupa ya dawa na kushoto sindano za kutibia wagonjwa hospitali. Hili linaashiria maudhi yaliyo katika mataifa changa barani Afrika, yatokanayo na maradhi ambayo huzalishwa na mazingira chafu katika anthroposenia. Tajiri mwenye nguruwe anayerejelewa na Jonalisti ni taashira ya viongozi wa mataifa tajiri ya Uropa na Ulaya ambao hutawala na huongoza mataifa fukara barani Afrika kupitia viongozi fisadi, binafsi na wenye tamaa ambao huwa vikaragosi vyao. Vikaragosi hawa wanaashiriwa na mtunzi Mbogo kupitia nguruwe wanaopiga mbio kuelekea katikati mwa lile dampu la Siza bila kujali. Nguruwe wenyewe ni wachafu na walionona kupindukia. Hili linaashiria viongozi katika mataifa mengi barani Afrika ambao hutawaliwa na ubinafsi-uchoyo, tamaa na ufisadi, bila kujali mataifa yao yaliyobadilishwa kuwa majaa ya taka na mataifa ya Ulaya na Uropa katika anthroposenia. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo ya nadharia ya Uhakikimazingira.

Majoka yanayorejelewa na Pasta Yona ni taashira ya maangamizi. Kimsingi, anthroposenia huangamiza jamii kupitia njia nyingi tofauti. Ndoto yenye joka kubwa aliyoiota Pasta Yona ni taashira ya maangamizi. Hii ni kwa sababu, joka lile kando na kuwa na miguu miwili tofauti na joka la kawaida ambalo hutambaa bila miguu, lilikuwa na ndimi saba. Miguu inaashiria uwezo wa kutembea kama binadamu ilhali ndimi zile saba zinaashiria ukamilifu wa maangamizi kutokana na anthroposenia. Nambari saba huashiria dhambi saba kuu, matunda saba au vipawa saba vya roho mtakatifu, maadili saba, sanaa na sayansi saba pamoja na vipindi saba vya binadamu. Kadhalika, huashiria siku saba za wiki, rangi saba za msingi pamoja, na hivyo, ukamilifu na dhamana kwa kila jambo (Waithiru, 2019). Hili linaashiria kuwa, anthroposenia isipokabiliwa ipasavyo, ina uwezo wa kuangamiza ulimwengu kwa

jumla na kikamilifu. Pasta Yona anadhihirisha na kukariri katika *Bustani* kuwa, “Majoka yale hewani yalionekana mara yakikumbatiana na kurambana ndimi kwa usuhuba; mara yagombane na kutemeana cheche za moto zilizolipuka, toka kwenye ndimi zao sabasaba.” (uk. 35). Nyoka ni taashira ya anthroposenia na hivyo, mayai yake yanaashiria mwendelezo na ukuaji wa maangamizi kwa binadamu duniani. Hii ndiyo sababu Baba Adamu anashangaa kuwa kila walipoenda waliyaona mayai ya nyoka yameatamiwa.

Bwana Abdula kama kiumbe ni taashira ya anthroposenia. Kupitia Bwana Abdula, mtunzi Mbogo anaashiria matajiri barani Afrika ambao huendeleza na kupalilia upujufu wa mazingira kwa manufaa yao binafsi bila kujali wananchi wengine. Mathalani, kutokana na uraibu wake wa kuvuta sigara mchana kutwa, anamsababishia mkewe Zaituni matatizo ya vichomi vya kifuani. Kwa upande mwingine, kiwanda chake, ingawa yeye anaishi kilomita sitini kutoka kwenye kiwanda hadi kwake, wanaokizingira hawaepuki athari hasi za kiwanda kile cha Sagasaga Chemical Industry. Yusuf anaeleza katika *Bustani* kuwa, “siku hizi maradhi hapa Siza hayana mmoja. Unamwona mwenzako huyo … kukohoa hakumwishi. Mimi nitazame … Nitazame shemeji. Kitazame kichwa changu. Vipele hivi sijui vinatoka wapi? Nimepaka kila dawa, wapi! Maradhi ni mengi.” (uk. 4). Aidha, kutokana na mivuke ya kemikali sumu inayohanikiza kwenye mazingira ya Mji wa Siza inachafua hewa pakubwa. Baadhi ya wenyeji wanaoathirika na kiwanda hiki ni pamoja na Yusuf anayeugua vipele kichwani, mkewe naye, Zubeda anakohoa bila kikomo.

Kadhalika, Bwana Abdula ni taashira ya anthroposenia inayohanikiza uvundo kwake na kwa wengine. Kwa mfano, mdomo wake na pumzi zake vilitoa harufu kali ya sigara. Sigara ni taashira ya mizizi ya anthroposenia ambayo huathiri watu kupitia hewa. Kwa kushirikiana na matajiri wengine kama vile, *The Trans-American Chemical Products* wanaendeleza uchafuzi wa mazingira na hususani hewa. Staftahi ya Bwana Abdula, ambaye ni taashira ya anthroposenia inasheheni taashira zinazoashiria utunzaji na upaliliaji wa maradhi na uharibifu wa mazingira. Mathalani, nyama ya nguruwe imetokana na nguruwe ambao wanasambaza maradhi kwa watu. Mwandishi Mbogo anadhihirisha hili katika *Bustani* anaposema kuwa, “Nguruwe, kama zilivyo tabia za uchafu na ulafi wa kula ovyo, walipendelea zile takataka zilizovunda.” (uk. 26). Kwa misingi hii hii, maziwa yanayosemekana kuwa freshi ya ng’ombe si freshi vile. Hii ni kwa sababu, Jonalisti anakiri kuwaona ng’ombe, mbuzi

na nguruwe wakiwa wameinama wakila takataka za kila aina. Hili linafungamana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo njia binadamu anazoingiliana na kuhusiana na mazingira zinahitaji kutathminiwa.

Matajiri wanaoshirikiana na Bwana Abdula kuendeleza uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni taashira ya walowezi barani Afrika. Bwana Abdula anakiri hili anapowaza katika *Bustani* kuwa, "Lakini Bwana Abdula alijua wazi kuwa bila msaada wa matajiri wake:- *The Trans-American Chemical Products* – yeye peke yake asingeshinda vita ile." (uk. 48 – 9). Ikizingatiwa kwamba Bwana Abdula ni taashira ya maangamizi kwa mazingira basi matajiri wenzake pia ni taashira ya maangamizi kwa mazingira kwa sababu wanamsaidia katika vita vya kuuimarisha na kuulinda uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika mataifa fukara ya Afrika. Bwana Kimondo Makamu wa Mkurugenzi wa Sagasaga, Bwana Abdula na mwanawe Lyakati ni taashira ya uharibifu wa mazingira pia. Wote watatu wanaketi mle ofisini mwa Bwana Abdula kujadili namna ya kuilinda anthroposenia na kuipalilia isinyong'onyee. Hili linaashiria namna ambavyo matajiri na viongozi barani Afrika wanavyojitolea kuuendeleza uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Hakika hili huwa wanalifanikisha kupitia ufisadi, utawala mbaya, ubaguzi na maonevu. Hali hii inawiana na nguzo ya uongozi mbaya.

Bwana Abdula anadhihirisha kuwa anthroposenia hushamiri katika mazingira inamokaribishwa na kupaliliwa kwa ujasiri na hudidimia ikikemewa na kukatwa mizizi na wananchi wazalendo na wenye haki na usawa. Mathalani ingawa Bwana Abdula alikabiliwa na tisho la waandishi wa habari, tisho la waziri wa viwanda, Pasta Yona wa Yona na halafu lile la wakili Mwaka pamoja na wafanyakazi walioumia katika kiwanda chake cha kemikali cha Sagasaga; aliashiria ujasiri kwa kuudhibiti woga wake barabara mbele ya mwanae na Makamu wa Mkurugenzi wa Sagasaga Bwana Omondo Kimondo. Bwana Abdula na mwanae Lyakati wanamlinganisha Pasta Yona wa Yona na Mahatma Gandhi. Mahatma Gandhi anajulikana sana kama mwanzilishi wa migomo na maandamano ya amani dhidi ya utawala wa kimabavu wa kikoloni. Alikuwa mmoja wa wanaharakati ambao waliongoza vita vya kupigania uhuru wa taifa la India kutoka kwa utawala wa kikoloni wa Uingereza. Hivyo, inabainika kuwa suluhu dhidi ya dhiki zinazosababishwa na anthroposenia hupatikana katika mazingira yale yale yanayochafuliwa na kuharibiwa ila si kutoka ng'ambo.

Mahatma Gandhi alikuwa mtetezi wa haki za wananchi wa India dhidi ya Mbeberu Mwingereza. Hivyo, kumlinganisha Pasta Yona wa Yona na Mahatma Gandhi wa India kunaashiria uzalendo wa Pasta kwa mji wa Nomila, mji wa Siza na taifa lake kwa jumla na kwa jumla ukakamavu wake katika kukabiliana na dhuluma, maonevu,utumwa na uchafuzi na uharibifu wa mazingira yao. Kwa stihizai, Bwana Abdula katika *Bustani* anauliza ikiwa, "Enhe? Mnasemaje? Tumfanye nini huyu Mahatma Gandhi?" (uk. 53). Bwana Omondo Kimondo ni taashira ya wasaliti wanaopalilia udhalimu wa kila hali katika nchi za Afrika. Hajali Waafrika wenzake wala taifa lake. Aidha, anashadidia kauli kuwa hamna tatizo Pasta Yona wa Yona akikata roho. Anashangili kifo cha Pasta Yona wa Yona anayekabiliana na uchafuzi wa mazingira kwa hali na mali. Hili linafungamana na nguzo ya kifo ambapo wanaoyachafua mazingira huwa tayari kuwaangamiza wasiowaunga mkono. Hili linaashiria kuwa maandamano ni ala inayosaidia kufifisha uongozi mbaya, dhuluma, uharibifu na uchafuzi wa mazingira usiweze kukomaa wala kuimarika. Isitoshe, Pasta Yona wa Yona ni taashira ya viongozi wa dini wazalendo na wenye msimamo dhabiti. Bwana Abdula anakiri na kudhibitisha hili anaposema katika *Bustani* kuwa, "… Mahatma Gandhi hahongeki, hanunuliki." (uk. 53). Ukweli huu unajulikana na Bwana Kimondo anayesisitiza kuwa angetia bidii kuibuka na mbinu mbadala na madhubuti ya kumnyamazisha Pasta Yona. Anasisitiza kuwa kila mtu huwa na udhaifu mahala fulani, kama vile; mwilini, akilini, moyoni au hata katika uhai na maslahi ya wale wanaomhusu. Hili linaashiria kiwango ambacho taashira za dhuluma, maonevu, unajisi wa mazingira na manyanyaso ziko tayari kutenda maovu kuhakikisha uhai na maendeleo ya anthroposenia hasa katika mataifa ya Afrika.

Kitabu anachosoma Pasta Yona cha Mwanzo, sura ya kwanza na ya pili kinaashiria kusudi la Mungu la kuumba ulimwengu bila ubaguzi, dhuluma, maonevu, uchafuzi wala uharibifu wa mazingira. Bustani ya Edeni inaashiria ulimwengu ambao ulinuiwa bila kunajisiwa na yeyote wala chochote. Kitabu hiki kinaangazia kuumbwa kwa dunia pamoja na kuumbwa kwa mtu aliyewekwa kwenye Bustani ya Edeni. Hili linaashiria kusudi la kuwepo kwa ulimwengu bila anthroposenia. Ndiposa Pasta Yona anaeleza kuwa, kabla ya majilio ya anthroposenia ulimwenguni, dunia ilikuwa na uzuri wa ajabu. Hii ni kwa sababu, dunia ilikuwa na miti, maua, mabonde na milima ya kupendeza binadamu. Kadhalika, ilizagaa wanyama, ndege na wadudu wa kuvutia machoni mwa binadamu. Hata hivyo, shughuli za kila siku za binadamu zinaendelea

kuzalisha uchafuzi na uharibifu mkuu kupitia aina mbalimbali kama vile, vurugu dhidi ya mazingira, mabepari, wakoloni wa kisasa, jiografia ya binadamu na mawakala wa anthroposenia.

Haya yameshamiri kutokana na haja, tamaa, ubinafsi na ufisadi wa binadamu bila kuwajibikia wala kusikitikia mazingira yao. Pasta Yona anawauliza waumini ilikoenda dunia nzuri waliyowahi kuzawadiwa wazazi wao wa awali na pia waliyoirithi kutoka kwa wahenga wao. Hii ni kwa sababu, Bustani ya Edeni ni taashira ya ulimwengu na hivyo, kutoweka kwake kunaashiria kuchipuka na kunawiri kwa uharibifu na unajisi wa ulimwengu na vilivyomo. Pasta Yona anadhihirisha hili anapofafanua kuwa bustani yao ya Edeni haipo tena. Sababu kuu ikiwa, imekumbwa na mdudu anayeitwa maendeleo. Baadhi ya mhimili wa Nadharia ya Uhakikimazingira ni ule wa maendeleo endelevu unaofungamana na hali hii. Hivyo, mhimili huu unaashiria chimbuko la maangamizi ya ulimwengu ila si maendeleo endelevu yenyewe. Pia analaumu mdudu anayeitwa sayansi na teknolojia. Wadudu wanaolaumiwa na Pasta Yona ni taashira ya uharibifu ulimwenguni.

Hata hivyo, anawaeleza kuwa, chanzo kikuu cha uharibifu huo sio wadudu aliowataja ila ni binadamu mwenyewe. Mathalani, kwa hasira na sauti ya juu, Pasta Yona katika *Bustani* anaeleza kuwa, “Ninyi … ninyi. Wewe na wewe … na wewe na mimi. Ninyi. Ni sisi tunaoiharibu Bustani ya Edeni kwa kisingizio cha hawa wadudu niliowataja.” (uk. 76). Makosa yanayorejelewa na Pasta Yona yanaashiria upaliliaji wa uharibifu kama zao la shughuli za kila siku za binadamu. Vunjajungu anayeibuka na kusimama juu ya kivuli cha kichwa chake Bwana Abdula pale ndani ya kioo ni taashira ya uharibifu kupata ukomavu wa aina yake. Kwa kawaida, vunjajungu ni mdudu aina ya panzi mwenye kiuno chembamba na macho makubwa na hula wadudu wadogo (BAKITA, 2015). Hili linaashiria kuwa, uharibifu unapokomaa humeza hadi wale wanaoupalilia na kuulinda, kama Bwana Abdula, waziri wa viwanda, inspekta wa polisi na viongozi wengine tofautitofauti. Ikizingatiwa kuwa, panzi ana uwezo wa kupaa na kuruka kutoka sehemu moja hadi nyingine, hali hii inaashiria uwezo wa uharibifu wa kusambaa upesi na kwa wepesi. Bwana Abdula anajaribu kumpangusa vunjajungu yule lakini hakumwona. Hali hii inafungamana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira.

Baada ya kushindwa kumpangusa anakikabili kioo ili ahitimishe kuchana nywele ili pamoja na watoto wake waende kumtembelea Zaituni hospitali ya Aga Khan. Hata hivyo, roho karibu imtoke alipoona kuwa vunjajungu hayupo tena lakini mahala pake palichukuliwa na chura mkubwa. Chura aliyempa kiwewe Bwana Abdula ni mnyama mdogo mwenye damu baridi anayeweza kuishi nchi kavu na ndani ya maji ambaye ana ngozi ya mabaka na hurukaruka (TUKI, 2013; 2014; BAKITA, 2022; Wamitila, 2022). Hata hivyo, chura anayemwona Bwana Abdula ni mkubwa kupindukia. Mtunzi Mbogo katika *Bustani* anaeleza kuwa Bwana Abdula hakuwahi kuona chura mkubwa ajabu namna ile. Mathalani, anataja kuwa, "… hajapata kuuona ukubwa wake; kavimbiana utadhani kameza kitu au ana mimba." (uk. 79). Chura yule ni taashira ya uharibifu uliokomaa na kuimarika. Umbo lake linaashiria kuwa uharibifu hasa wa mazingira ni wa kiwango kikubwa na unaendelea kusambaa kila uchao.

Aidha, uharibifu huu unameza kila kiumbe na pia maumbile kama maziwa, bahari, mito na mimea aina aina. Ukweli ni kwamba hata wale wanaoashiria na kuupalilia uharibifu huu hawako tayari kuingiliana na kutagusana na nao. Bwana Abdula ako mstari wa mbele kupalilia, kukuza, na kuendeleza uharibifu na uchafuzi wa mazingira na vilivyomo lakini anapotazamana nao uoga unamvaa, kiwango kwamba anakurupuka hadi nje ya chumba chake. Uoga alionao unadhihirika hadi na mpishi wake – Nasoni. Mwandishi anaeleza katika *Bustani* kuwa, "Nasoni alikuja mbio. Alimkuta bwana mkubwa wake rangi usoni imembadilika, macho kayatoa pima." (uk. 79). Hili linalandana na nguzo ya kifo ambapo baada ya binadamu kuyapujua mazingira yake na vilivyomo huishia kujiangamiza mwenyewe. Hili analielewa bayana na ndiposa uharibifu ule ule anaopalilia ukimkabili anajawa na wasiwasi.

Kimsingi, uharibifu unaashiriwa na nyoka katika *Bustani* tangia mwanzo hadi tamati mwa kazi ile. Hata hivyo, taashira zingine zinaibuliwa kuashiria maangamizi ya mazingira. Hizi ni kama vile, vunjajungu, chura, na kinyonga. Kinyonga ni taashira ya uharibifu na uchafuzi inayolandana sana na sifa za maonevu, duluma na manyanyaso, maadamu kinyonga kama ajenti wa maangamizi huweza kubadili rangi ya kukamafleji ili kuimarika na kuendelea katika mazingira na hali tofautitofauti. Hili linadhihirishwa na Bwana Abdula anapomwambia mpishi wake – Nasoni – kuwa, "Wewe huna macho? Huoni yule chura – ee! Hapana sio chura ni kinyonga – wewe huoni huyo kinyonga. Hoo! Hapana sio kinyonga. Sasa ni nyoka. Sema!" (uk. 79). Kwa mujibu wa mwandishi wa *Bustani*, mna matumaini kuwa uchafuzi na uharibifu

kwa jumla unaweza kuthibitiwa. Hii ni kwa sababu, baada ya Bwana Abdula kutokwa na jasho jingi, anajifuta na kitambaa cheupe na kupata utulivu. Rangi nyeupe ni taashira ya unadhifishaji na utakaso wa uchafuzi na uharibifu.

Uchafuzi na uharibifu kwa jumla ni athari hasi kwa binadamu na hivyo Bwana Abdula ana sababu za kutosha kuiogopa. Kwa mfano, kutokana nao, Zaituni anaugua saratani. Hili linadhihirishwa na Dk. Silika anapomwambia Bwana Abdula kuwa, "Tumetazama zile X-ray tatu tulizompiga. Mkeo ana uvimbe kwenye pafu lake la kushoto." (uk. 81). Kwa mujibu wa Dk. Silika, Zaituni anaonyesha dalili ya moshi mapafuni mwake. Chanzo cha moshi ule ni sigara anazovuta kila wakati Bwana Abdula. Dk. Silika katika *Bustani* anafafanua kuwa, "… Zaituni wako ana kansa! … Na chanzo cha kansa hii ni sigara. Moshi wa sigara." (uk. 81). Sigara anayovuta Bwana Abdula inaashiria uchafuzi hewa na chanzo cha maradhi hatari kwa binadamu na viumbe wengine. Dk. Silika anamkumbusha Bwana Abdula kuwa, ingawa mtu havuti sigara anaweza akapata kansa kwa kuvuta moshi tu wa yule anayevuta sigara – Bwana Abdula. Ukweli huu unamfanya Bwana Abdula akumbuke taashira zilizombainikia kwake chumbani asubuhi ile kupitia viumbe aina aina. Hali hii inwiana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo njia tunazotumia kuingiliana na mazingira zinafaa kupigwa msasa kwani tusipotahadhari mazingira hujitetea kwa njia ambazo huishia kumwangamiza binadamu.

Kando na Bwana Abdula kuwa taashira ya uharibifu na uchafuzi, anaziona taashira zingine za uharibifu mawazoni mwake. Anaporejesha mawazo yake nyuma, anapata taswira ya taashira za uharibifu kama vile, chura, kinyonga, nyoka, na vunjajungu wakiwa pale mezani kwake nyumbani wakihudumiwa na mtumishi wake, Nasoni. Nasoni anaonekana akiwakirimu kwa vyakula, vipochopocho na glasi za mvinyo kupalilia anthroposenia. Hili linaashiria namna binadamu huukirimu na kuutunza uharibifu na uchafuzi kupitia vitendo vyake vya kila siku.

Njiwa wawili weupe wanaotua juu ya mwembe wanaashiria matumaini ya kushinda vita vya kukabiliana na uharibifu na uchafuzi kwa jumla. Taashira hii inampa Pasta Yona utulivu na anamwita Mama Esnati awashuhudie njiwa wa kawaida. Mama Esnati anasema kuwa, "Mm! Kwa kweli pamoja na ukubwa wangu huu sijapata kuwaona. Ni wakubwa kidogo kuliko njiwa wa kawaida." (uk. 85). Kadhalika, anasadiki kuwa weupe wa njiwa wale si wa kawaida, kuashiria matumaini katika

ukombozi kutoka kwenye giza la anthroposenia. Rangi nyeupe huashiria utakaso, amani na mabadiliko mema (Smith, 2019 na Waithiru, 2022b).

Ingawa binadamu amekuwa ajenti mkuu wa kuendeleza na kukuza uchafuzi na uharibifu wa mazingira, ameathirika sana na uchafuzi na uharibifu huu. Hii ndiyo sababu, mwandishi kupitia wahusika Baba Adamu na Mama Hawa katika *Bustani* anaeleza kuwa, "Tangu juzi tumeizunguka dunia tukiikagua bustani tuliyozawadiwa siku ile ya kwanza. Tumeona nini? Tumeona nyuso za huzuni zilizozungukwa na harufu mbaya, uozo wa taka, moshi wa kila aina." (uk. 37 – 8). Mtumishi wake Bwana Abdula ana miaka hamsini hivi na hivyo amekomaa. Mzee huyu – Nasoni – anaashiria watu wanaoendelea kuyachafua na kuyapujua mazingira kwa sababu hawana njia nyingine ya kupigana na ufukara. Hili linaonyesha kuwa, ufukara hushamiri uchafuzi na uharibifu wa mazingira ukishamiri. Mzee Nasoni anamtayarishia Bwana Abdula staftahi ya kifahari. Hili linaashiria jinsi watu wengi hupalilia anthroposenia katika harakati za kujiendeleza ili wafutilie mbali ulofa. Mavazi ya Nsoni yanaashiria watu wasioathirika na ufisadi, ubinafsi na tamaa katika uharibifu na uchafuzi hata kama huwa wanalea dhuluma, chuki, manyanyaso na maonevu ya kila aina. Mavazi yake ni sare inayohusisha koti, shati na kofia na vyote ni vyeupe kuashiria utakaso au udhu. Kutokana na ulofa watu kama hawa wenye udhu huchunga na kuingiliana na viongozi dhalimu, matajiri na wafisadi kwa adabu na heshima. Staftahi anayotayarishiwa Bwana Abdula inahusisha; mayai ya kukaanga, mikate, nyama ya nguruwe iliyosagwa, sharubati freshi ya maembe, maziwa freshi ya ng'ombe na chupa ya mvinyo. Staftahi yenyewe inaashiria upaliliaji wa waharibifu, wanajisi, wadhalilishaji na waonevu wa mazingira na vilivyomo kwa jumla – Bwana Abdula.

Mtoto Metu alipokuwa malishoni alijishughulisha na uwindaji wa ndege kama njiwa, kasuku, au nomvi. Katika harakati zake za uwindaji alikumbana na chatu aliyekuwa amejinyonganyonga chini ya mbuyu mkubwa. Kitaashira mbuyu huashiria laana au bahati mbaya. Waithiru (2019), BAKITA (2015) na Mdee na wengine (2015) wanaeleza mbuyu kama mti mkubwa na mnene sana ambao shina lake lina nyuzinyuzi na huzaa tunda lenye kokwa nyingi ndani. Mtoto Metu alipatwa na mkongoto alipomuona yule chatu. Chatu ni mnyama ambaye huashiria maangamizi kwa binadamu na kwa misingi hii ni taashira ya anthroposenia. BAKITA (2015), Mdee na wengine (2015) na Wamitila (2022) wanafafanua kuwa, chatu ni aina ya

nyoka mkubwa anayeweza kumeza mtu. Chatu aliyekuwa pale chini ya mbuyu alikuwa na macho yaliyong'aa na ngozi yake ilikuwa na madoa ya kuvutia. Hili linadhihirisha kuwa, maangamizi huwalaghai watu kuwa ni ya kuvutia ilhali ni ya kudhulumu, kutesa, kudhalilisha na hatimaye kuua. Mwandishi wa *Bustani* anaongeza kuwa, "Alikuwa chatu mkubwa aliyeweza kummeza mbuzi ama kondoo." (uk. 95). Mara Metu alimwona dudumizi, akajaribu kumlenga lakini akaambulia patupu. Dudumizi ni taashira ya huzuni na majuto. Kulingana na Mdee na wengine (2009), dudumizi ni mdudu mdogo mweusi anayeharibu nafaka au ndege mwenye rangi ya hudhurungi na wa ukubwa wa njiwa na anayelia kwa kugugumia.

Dudumizi anayeonekana na Metu ni aina ya ndege mwenye rangi ya hudhurungi. Maiti ya Pasta Yona inaliwa na tai na kunguru wanaopaa hewani wakiwa wameshikilia minofu ya nyama midomoni mwao. Hili linadhihirisha namna uharibifu na uchafuzi wa mazingira unavyowaangamiza wale wanoutisha au kujitahidi kukabiliana nao. Macho yake Pasta Yona yalikuwa yamekwishadonolewa na kuliwa na tai. Nguo zake zilikuwa zimetapakaa damu na mavi ya ndege. Metu anaisikia sauti ya mlafi fisi ikilia. Fisi ni taashira ya maonevu, ufisadi, uongozi mbaya na ukoloni wa kisasa ambapo mazingira hunajisiwa kila uchao. Hivyo, tama, uchafuzi na ubadhilifu – unaoashiriwa na fisi (Waithiru, 2019; 2022d) – unaimarisha ubinafsi, woga, ulafi, uchoyo na utovu wa utu baina ya uhusiano kati ya binadamu na mazingira yake. Hali hii inazua haja ya nguzo ya haki na maadili ya mazingira. Aidha, inawiana na kauli ya Garrard (2023), Hujibens (2023) na LaMothe (2024) kuwa, binadamu anafaa kusutwa namna anavyoingiliana na kutagusana na mazingira yake katika harakati za kujiendeleza kimaisha kwa jumla.

Moto anakata vijiti viwili na kukiita kile kikubwa 'mama' ilhali kile kidogo anakiita 'baba'. Anakiweka kijiti mama chini na kwa kutumia kijiti baba anapekecha matundu mengi. Kitendo hiki kinaashiria jinsi maonevu na ubaguzi huutoboa ulimwengu kiuchumi, kijamii, kisiasa, kimaumbile na kwa kila hali. Kwa mfano, Moto anasadiki katika *Walenisi* kuwa, "Alichokisikia kwa ghafla, kilikuwa ni kuchomeka na kuona moshi ukifusika." (uk. 155). Ikizingatiwa kwamba, moto ni aina ya maangamizi ambayo huuchoma na kuumaliza ulimwengu kupitia njia mbalimbali, basi ni dhahiri shahiri kuwa, moto unaovumbuliwa na Moto ni taashira ya maangamizi ya mazingira na uhai wa binadamu kwa jumla. Utafiti wa Dzombo kuhusu moto katika *Walenisi* unathibitisha hili anapoeleza kuwa,

> “Huku akitetemeka kwa hofu, cheche hiyo ikaanza kusambaa. Ilijieneza kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Sasa ikawa imepata nguvu na kuwa tsanzala ambayo ilienea kwa upesi na kumeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake. Kuangalia hivi, akajiona amesimama peupe!” (uk. 155).

Moshi nao unaashiria athari hasi za maangamizi aina aina – moto. Kutokana na moshi macho ya Moto yanaonekana mekundu mno. Kiwiliwili chake Moto kinaonekana kikiyumbayumba nyuma ya miale ya moto, kuashiria uwezo wa maangamizi wa kuyumbisha maisha ya binadamu na viumbehai pamoja na visivyohai ulimwenguni kote. Hali hii inawiana na nguzo ya uwezo na kifo.

Tai ni istilahi yenye dhana mbalimbali. Lakini katika utafiti huu, tai anasawiri uwezo, mamlaka, utawala na uongozi dhalimu unaoshibishwa na uhai wa wananchi duni. Kwa misingi hii, tai anayerejelewa kiuyakinifu ni ndege mkubwa mwenye mdomo uliopinda nchani, kucha ndefu zilizokunjika na kali ambaye hula mizoga na wanyama wadogo kama panya (BAKITA, 2015; 2022; Mdee na wengine, 2009). Tai ni mnyama mwenye ugwe wa neva mgongoni na hulandana na vipanga. Kucha zake ndefu humfaa sana kukamata uwimbo na mdomo wake huwa umepinda nchani ili kumfaa kupapura nyama. Isitoshe, tai huwa na uwezo wa kuona kwa kiwango cha juu zaidi akilinganishwa na ndege na wanyama wengine. Hii ni kwa sababu, huweza kutambua windo lake likiwa mbali sana. Tago la tai hujengwa juu ya miti mirefu au kwenye magenge marefu kuashiria mamlaka na uwezo. Mtunzi Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* ametumia tai kama taashira ya uharibifu na utawala dhalimu. Hakika hili linashabihiana na nguzo ya uwezo ambapo mataifa yenye uwezo huyatumikisha yale duni kwa kila njia.

Ukoo wa Moto unabadili jina na kuibua jina jipya linaloendeleza uhifadhi wa maangamizi. Kando na kuhifadhi jina hili la ukoo wa Tai linazalisha ukoo mwingine wa udhalilishaji kupitia Wachuna. Mwandishi anathibitisha hili anapoeleza katika *Walenisi* kuwa, “Hivi ndivyo basi ukoo mmoja wa Kichuna ulivyozuka na kujipatia utukufu, uwezo na hekima kwa kutumia hila zilizoweza kuwapa utawala juu ya wenzao na kuwala jasho lao.” (uk. 158). Kwa misingi hii hii, Wachuna wa ukoo wa Uganga uliotoa mtu aliyejulikana kwa jina la Mchawi ni taashira ya uharibifu na uchafuzi.

Majoka mawili yanayopindana mle juu ya mti matagaani yanaashiria maangamizi kwa binadamu kutokana na sumu yao. Mzozano kati ya majoka – bafe na chatu – mawili unaashiria namna utawala dhalimu na wa maonevu huzozana wenyewe kwa wenyewe ili wenye sumu kali na mbinu madhubuti za kuangamiza ulimwengu na vilivyomo kutawala pekee ulimwenguni. Ndiposa bafe na chatu wanapingilishana katika vita vya kumalizana. Bafe kwa kuogopa kuangamizwa na matiko ya chatu anaruka huku na huko, huku akizika machonge yake ya sumu hatari mwilini mwa chatu kila alipopata fursa. Naye chatu anajipinduapindua mithili ya pweza aliyejipalia makaa akisaga fursa ya kumzonga bafe kikamilifu. Mwandishi wa *Walenisi* anasawiri vita vya wenyewe kwa wenyewe baina ya maangamizi yenyewe na uharibifu wenyewe kwa wenyewe. Bafe ananaswa kati ya matiko yake na chatu lakini mti uliokuwa kati yao unamwokoa. Hili linaashiria namna nguzo kuu ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya maumbile inavyoshamiri katika vita dhidi ya maradhi, njaa, ulofa na maangamizi.

Nayar (2010), Garrard (2023) na Filipova (2023) wakikubaliana na mawazo ya mtafiti wanasisitiza kuwa, katika harakati za maingiliano na mahusiano kati ya binadamu na mazingira, binadamu huweza aidha kushamiri na kukomaa au kudidimia na halafu kuangamia. Baada ya bafe kunusurika maafa kutokana na maingiliano na mahusiano yake na mti, anazidisha ushambulizi kwa kumsukumia chatu sumu yake kwa wingi. Hakika, kama alivyotarajia bafe, chatu anazidiwa na ukali wa sumu na kujinyoosha twaa na kutulia kama gogo. Lakini, badala ya bafe kumwacha chatu anaamua kumwangamiza mwenzake kabisa. Hali hii inaashiria haja ya uharibifu, maonevu na utawala dhalimu kuangamiza sio tu viumbe vilivyohai, visivyohai na maumbile kimwavuli, bali pia uharibifu mwingine shindani. Hali hii inawiana na nguzo ya uwezo ingawa katika uwanda tofauti ambapo kando na mataifa tajiri kuyanyanyasa mataifa duni, yanadhulumiana yenyewe kwa yenyewe. Hili husababishwa na ubinafsi na tamaa ya kuwa na mamlaka na uwezo zaidi kuliko taifa linguine lolote ulimwenguni.

Kwa lengo na makusudi bayana, bafe anatia na kuyatumbukiza meno yake kichwani mwa chatu na kumtapikia sumu yake yote. Hili linazidi kuashiria namna uharibifu hufaidi wenyewe kutokana na maangamizi ya viumbe na maumbile aina aina. Mwandishi anathibitisha hili anapoeleza kuwa, “Bafe alikuwa akitaka chatu asikie maumivu yasiyoelezeka, naye chatu akasikia hivyo. Ule uchungu aliousikia, ndio

uliomfanya hata akajifyatua kwa ghadhabu ya mwisho." (uk. 159). Hata hivyo, hata baada ya juhudi kubwa za bafe kunuia kumwangamiza chatu, pale alipokuwa ametulia chatu kama gogo, anafyatua mkia wake kama umeme na kumzonga bafe katika matiko yake na kumsaga hadi akawa kima kweli. Baada ya kumwangamiza bafe, chatu anachimbua mizizi ya mti, anaivunja na kuimeza. Kadhalika, anabambua magamba na majani ya mti huo, anayakata kisha kuvimeza. Halafu baada ya kumeza vyote, chatu anatulia kitambo kiasi kabla ya kutoweka kwa mwendo wa kasi akiwa buheri wa afya. Kitendo hiki cha kumeza mizizi, magamba na majani kinaashiria namna uharibifu na uchafuzi hujivumbua upya kwa kutumia rasilimali asilia zinazopatikana kwa urahisi ulimwenguni. Hili linalandana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo ingawa binadamu ana uhuru wa kudhibiti ulimwengu, pia ni wajibu wake kuyalinda.

Ukoo wa Wachuna wa Uchawi ili kuendeleza maangamizi kujikita na kujilinda, wanageuza jina la mwanzilishi wao "Mchawi" na wakajiita wa ukoo wa "Nyoka". Nyoka sawa na Mchawi ni taashira ya maangamizi. Mabavu, kama lilivyofafanuliwa kwenye sehemu ya mbinu ya majazi inayosawiri maangamizi katika riwaya nne teule ni taashira ya dhuluma na maafa. Kwa kutumia hila, Mabavu anamuoa Kadzo baada ya kumwonea gere Dutu. Dutu anapokea athari hasi za ubinafsi, maonevu na ubaguzi moja kwa moja. Ananyang'anywa ulimwengu wote baada ya kupokonywa Kadzo – ishara ya ulimwengu (Nayar, 2010). BAKITA (2015) wanataja kuwa, dutu ni kilima kidogo au kichuguu au hata kipele kidogo kiotacho usoni, yaani chunusi. Ndiposa Mabavu anakifinya na kukiangamiza kwa kutumia ghiliba. Udhalimu na maonevu hushamiri kwa kujikita katika hila na usaliti.

#### 5.2.4 Taashira ya Udhalimu

*JABALI LA UDHALIMU* katika *Walenisi* ni taashira ya udhalimu, uongozi mbaya, unajisi wa mazingira na utovu wa utu na maadili baina ya watu. Kupitia mwandishi Mkangi inadhihirika kuwa maangamizi humkumba binadamu bila kumpa hata nafasi ya kujiandaa kuyakaribisha wala kuyakemea. Sauti zinazojaa na kubishana kwa sauti ya kutisha mle ndani ya *Sayari* zinaashiria athari hasi za udhalimu, uongozi mbaya na ufisadi dhidi ya uhai wa mwanadamu bila ubaguzi. Mathalani, Mwanamke anapiga nduru na kulalamika kuwa ulofa na maradhi yanayoweza kuepukika yanamuumiza. Mkristo naye anapokea makumbo kutoka kwa ubaguzi na utawala dhalimu, hadi analia kuwa inamtoa roho. Uharibifu na uchafuzi wa kila namna unamrejelea

Mwanamke kama *kelb* na Mkristo mnafiki. Hili linaashiria kuwa, katika utawala na uongozi dhalimu Wanawake wanachangia sawia na Wakristo waliojaa unafiki. Hata hivyo, ingawa uharibifu na uchafuzi hadi wa nafsi unasisitiza wafe, wanasusia kuaga. Naye Mwislamu anatolewa utumbo na ulofa, udhalilishaji na uharibifu wa kila hali kutokana na athari za uongozi na utawala dhalimu. Yeye pia anapokea vita vikali lakini anadinda kuangamia anapoamrishwa na dhuluma afe. Hali inalandana na nguzo ya kifo ambapo baada ya binadamu kuingiliana na mazingira kwa njia za maonevu na manyanyaso hatimaye huangamia mwenyewe na viumbe hai vilivyomo.

Mprotestanti pia hajasazwa. Dhuluma na maonevu zinampiga vita huku zikimtoa ini kutokana na lawama kuwa hana adabu. Uchafuzi na uharibifu kwa jumla hushibishwa na maafa ya binadamu na hivyo unamlazimisha afe lakini anakataa kata kata. Mkatoliki bila kutarajia anajipata akitolewa mapafu na utawala na uongozi dhalimu. Matokeo ya udhalimu huzalisha uchafuzi wa hali ya hewa, mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la joto duniani, ukame, ufukara, kufifia kwa maliasili, tamaa, ubinafsi, ubepari, uongozi mbaya, ukoloni mamboleo na maafa (Coughlin na Gephart, 2020). Hii ndiyo sababu udhalimu unamshtumu Mkatoliki kuwa utaing'oa miguu yake maadamu huwa anaabudu vinyago jambo ambalo ni kinaya. Kadhalika, Pagani Mwafrika analia kwa maumivu yanayozalishwa na maonevu. Udhalimu unaendelea kumshika bila kumwacha aende Myahudi. Kinaya ni kuwa unamshtumu kuwa ni mlaghai. Kwa jumla, udhalimu kupitia uchafuzi na uharibifu unawataka watu wote wafe ili unufaike, madhali hushibishwa na mauti. Hii ni kwa sababu, baada ya kuwatesa wanadamu kutoka kila kona ya ulimwengu huwa unawaangamiza. Kifo, kando na kuwa nguzo kuu ya nadharia ya Uhakikimazingira (Robert na Christine, 2016) huwa zao la mwisho kwa binadamu baada ya kumnyonga kiuchumi, kisiasa na kijamii (Clark, 2015).

Mhindi mwizi naye anashongolewa kwa kupigwa kwa tako la bunduki na kusukumiwa kifo. Mhindi mwizi pamoja na hanithi msomi wakiwa na mkosa dini Mkomunisti wanasusia kifo kutoka kwa udhalimu. Msomi anawekwa bayoneti makalioni na kujuzwa kuwa hatimaye atalipuliwa ubongo wake. Hanithi Mkosa dini Mkomunisti naye anatiwa moto wa spaki uzazini na kuongezwa murututu. Haya yote yanaashiria athari hasi za udhalimu ambazo hasa zimezalishwa na uongozi mbaya katika mfumo wa ukoloni mamboleo. Kwa mfano, katika ukoloni mamboleo, wananchi katika nchi za Afrika huvunjwa mbavu, hupigwa kwa tako la bunduki,

hutiwa bayoneti makalioni ili kulipuliwa, hutiwa moto wa spaki uzazini, hutolewa damu, hutolewa utumbo na kuteswa bila kikomo kwa lengo la kuwaangamiza (Thiong'o, 1987).

Watson na Watson (2007) wakikubaliana na mawazo ya mtafiti wanaeleza kuwa, ingawa utumwa wa kiuchumi, kisiasa na kijamii hutesa na kuchukiza kweli, utumwa utokanao na anthroposenia hunyanyasa na kutesa zaidi. Hii ni kwa sababu, dhuluma zitokanazo na anthroposenia hudhaniwa kuwa matokeo ya kiasilia ya ulimwengu, jambo ambalo si kweli. Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* kupitia mhusika Dzombo anaashiria dhuluma kama chanzo cha maradhi ya mapafu, maafa, na uchafuzi wa nafsi na mazingira ya binadamu. Anafafanua kuwa,

> "… Dzombo alijikuta ameshaingizwa ndani ya wingu la damu. Damu hii ilikuwa imechanganyikana na makohozi, matapiko, nyute, kinyesi, mate na mikojo na kufanya kuonekana uchafu wa kutisha na wa kuchafua roho." (uk. 33).

Kimsingi, udhalimu hushamiri katika maeneo chafu (De Christofaro na Cordle, 2018). Hivyo, Jabali hili linapalilia anthroposenia kupitia uchafuzi wa afya ya binadamu. Kiuyakinifu, *JABALI LA UDHALIMU* linaashiria anthroposenia ambayo inaashiriwa kupitia udhalimu tofautitofauti. Kwa mfano, inadhihirika kuwa udhalimu huashiriwa kupitia unyanyasaji wa wanawake, pale mwanamke anapopiga nduru kutokana na mateso na manyanyaso. Pia, inadhihirika kupitia udhalimu wa kidini, ambapo udhalimu unaendelezwa pale Uislamu unapogonganishwa na Ukristo. Vilevile, mivutano ya madhahebu ya kidini inaashiria udhalimu. Hatimaye, ubaguzi wa rangi, mvutano kati ya wasiosoma na waliosoma na pia vita vya kiitikadi ambapo ukomunisti unagombana na ubepari ni baadhi ya njia ambapo uchafuzi na uharibifu unadhihirika. Ikizingatiwa kwamba Mkangi anadhihirisha uchafuzi na uharibifu katika *Walenisi* kupitia uchafu, kama vile; makohozi, matapiko, nyute, kinyesi, mate na mikojo; basi ni bayana kuwa uchafuzi na uharibifu hasa wa mazingira ni tatizo kuu linaloyakabili maisha ya binadamu popote walipo na kwamba kuwepo kwao ni tisho kwa wanadamu wote. Hivyo, ni suala linalotishia sio tu jamii moja finyu ila pia jamii pana ya ulimwengu mzima. Hali hii inafungamana na nguzo ya kifo.

Umalaya unaosawiriwa na Dzombo unaashiria unajisi wa ulimwengu kutokana na dhuluma za kiuchumi na za mifumo ya kijamii. Maafa anayoyaona yakiwakondolea

macho Tsuma, Munga na Chai yanaashiria athari hasi za udhalimu kwa vijana, hasa katika mataifa fukara ya Afrika. Joka ni taashira ya udhalimu na manyanyaso. Mwandishi Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* sawa na Mbogo katika riwaya ya *Bustani* anaashiria joka kama udhalimu dhidi ya mazingira kimwavuli. Mtu-Bint Hekima anasisitiza katika *Walenisi* kuwa, "Utokako, binadamu ndio maibilisi kwa kuwa hawana utu sawa na vile Wachuna walivyokuwa hapa kwetu." (uk. 130). Mzee Mtu-Mwenzio anadokeza kuwa Jehanamu – Duniani anakotoka Dzombo – ni janibu zinazotawaliwa na majoka, yaani falme za udhalimu. Mtu-Bint Fikirini naye anaongeza kuwa, Ibilisi ni joka lisilo na utu linaloashiria udhalimu baina ya watu. Kwa mshipa huu huu, Mama Mtu-Maanani anatonesha katika *Walenisi* kwa kukariri kuwa, joka linaloashiria udhalimu linasawiriwa na binadamu asiye na utu ulimwenguni. Mfano mzuri ni viongozi na matajiri barani Afrika.

Hili linathibitisha kuwa binadamu ni asili ya udhalimu ulimwenguni, hasa katika nchi za Afrika. Wachuna wanaashiria Waafrika wabinafsi, wenye tamaa na ufisadi tele, na ambao hawana utu. Ikizingatiwa kwamba ulimwengu unanasibishwa na mwanamke ulimwenguni (Nayar, 2010), basi kitendo kile cha wanaume kumkanyaga mke ama zulia kinaashiria namna udhalimu unavyoufinyanga ulimwengu kwa mateso, dhiki, dhuluma, maradhi, ufukara, na ubidhaaishaji wa kibepari (Coughlin na Gephart, 2020). Mtunzi Mkangi anaashiria ulimwengu katika *Walenisi* kupitia mwanamke na unajisi wa ulimwengu kupitia mwanamume. Hivyo, Hani na wanawake wengine wanaashiria ulimwengu ilhali Dzombo na wanaume wengine wanaashiria udhalimu dhidi ya ulimwengu na vilivyomo. Kwa misingi hii, udhalimu huuchukulia ulimwengu kama embe lililoiva, ukilila huwa koka ya kutupiliwa mbali au hata ndizi, ukilila huwa ni ganda la kutupiliwa jaani. Pia dunia kwa udhalimu kimwavuli ni hindi ambalo likishatafunwa huwa gunzi au mua ambao ukishafyonzwa huwa ni ganda la chungu. Kadhalika, udhalimu unamumunya ulimwengu shinani kama nanasi ila nchani kuliko na kakasi unadhoofisha pia. Vilevile, udhalimu unauchukua ulimwengu kama dau ambalo ukishalitumia kuvuka lakuwa gogo au hata samaki ambaye huwa unamla lakini harufu huitaki. Hivyo, udhalimu unaashiriwa kupitia wanaume wenye unafiki tele.

Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anadhihirisha kuwa, Uchuna ambao ni uhusiano ni taashira ya aina mbalimbali za udhalimu, kama vile; ubepari, ukoloni mamboleo au utandawazi, ulofa, uongozi mbaya, ubidhaaishaji wa ubepari, vurugu dhidi ya

mazingira, na aina nyingine nyingi. Wachuna nao ni taashira ya binadamu ambao wanaashiria wadhalimu. Wachuna walitawaliwa na ubinafsi, tamaa, ufisadi, unyama, hila, uzandiki, utubinafsi na ubaguzi wa aina aina. Kivuli cha mbuyu nacho ni taashira ya ulaghai ambao hutumiwa kuwapofusha watu wasione athari hasi za udhalimu ulimwenguni ambazo huzalisha mabadiliko makubwa hasi ulimwenguni.

Wachuna wa koo, mbari na milango tofautitofauti wanaashiria udhalimu. Wachuna wanaotumia hila kugeuza mchanga ukawa chuma, wacheza ramli, masonara na wengine wengi wanaotumia tambo za kila aina ni taashira ya anthroposenia. Kiuyakinifu, mwandishi Mkangi katika *Walenisi* anadhihirisha na kuthibitisha kuwa, ulaghai ni nguzo kuu ya kuhimili udhalimu. Hii ndiyo sababu, Wachuna wanaoashiria udhalimu wanaghilibu kuhusu asili zao. Aidha, wanalaghai kuwa asili zao si za kibinadamu, na wengine wanasisitiza kuwa damu zao ni za rangi ya buluu ila si nyekundu. Aidha utamaduni unaozalishwa kutokana na najisi ya udhalimu unaashiria maangamizi kwa jumla. Kwa mfano, Wachuna baada ya kujipa sifa za kimiungu wanaanzisha tafrija, nderemo, tamaduni, mila na desturi ambazo zina lengo moja la kuwatenganisha binadamu ili wasidadisi ukweli wa mambo.

Nywele na kucha ndefu za Wachuna zinaashiria athari za udhalimu kwa ulimwengu na hususani binadamu. Mtunzi Mkangi kupitia taashira ya mazimwi anadhihirisha kuwa, udhalimu hushamiri katika janibu zinazotawaliwa na woga. Wachuna wanatumia hofu na woga kama ala madhubuti kupalilia na kukuza udhalimu. Mathalani, mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anataja kuwa, "Nao kwa kutumia woga na hofu hii, wakaweza kuzika makucha yao zaidi kwa wenzao ili kuzidisha urundikaji wa ziada." (uk. 167). Kwa misingi hii, mungu wa Chuma ni taashira ya udhalimu na manyanyaso. Wafua vyuma wanawalaghai watu wengine kuwa chuma hakingeweza kupatikana bila utoaji kafara wa binadamu. Hivyo, watu wakaanza hulka ya kutoa kafara ya machipukizi wawili bikira kila mwaka kwa mungu wa chuma. Utamaduni huu unasababisha maangamizi ya watu badala ya kuhifadhi uhai wao.

Wachuna wanatumia hila hizi kuendeleza utawala mbaya ambao unakuza udhalimu. Jinsi tu udhalimu humkama nguvu binadamu, Wachuna waliwakama wananchi wao. Zaidi ya hayo, Wachuna wanajenga magereza ili kupalilia utumwa, udhalimu na manyanyaso kupitia utawala wa kimabavu. Meno yao pamoja na magereza ni taashira ya utawala dhalimu. Sheria, dini na mabavu ni taashira ya mbinu dhalimu za uongozi

na utawala. Wachuna wanawafuga mabarubaru ambao kazi yao kuu ni kuhakikisha kuwa amri na sheria za maonevu za Wachuna zinaogopwa na kufuatwa kikamilifu. Kwa misingi hiyo hiyo, Wachuna wakaanza kutumia njaa na shibe kama ala ya kuendeleza uongozi mbaya. Mtunzi Mkangi anaeleza katika *Walenisi* kuwa, "Kwa kuwashibisha wachache, Wachuna wakawa wameshagundua vipi njaa na shibe ni fimbo na silaha kwao." (uk. 168). Hakika hizi ni mbinu ambazo viongozi wengi barani Afrika hutumia kuwadhulumu watawaliwa na kudumisha uongozi wao dhalimu kupitia siasa za umaskini. Hili linfungamana na nguzo ya uwezo ambapo watawala huwadhalilisha watawaliwa pamoja na mazingira yao kwa jumla.

### 5.2.5 Taashira ya Ulofa na Ndwele

Kwa mujibu wa utafiti huu, ulofa ni hali ya mtu kukosa mali (TUKI, 2013; 2014; BAKITA, 2022; Wamitila, 2022); kupungukiwa na uwezo wa kiuchumi (Maathai, 2009; Garrard, 2007); na kupungukiwa na uwezo wa kufikiri kwa urazini (Bladow na Ladino, 2018). Ndwele ni maradhi ya aina yoyote kwa binadamu; au ugonjwa (Ndalu na wengine, 2014; Mdee na wengine, 2015; BAKITA, 2015). Kwa mfano, katika anthroposenia, ufukara, maradhi, na maafa, yote yanashamiri na kukita mizizi barani Afrika. Mhusika Franco katika *Bustani* alikuwa anatokwa na kamasi kila wakati na mwili wake ulikuwa unamwasha. Hili linaashiria kuwa, katika anthroposenia, changamoto na dhiki zinazoyakumba mataifa changa ya Afrika, zinaathiri Waafrika wenyewe ila si watalii. Mathalani, wananchi wa mataifa haya hula chakula kisichowafaa kwa lolote. Hata hivyo, hukichangamkia na kukifurahia kwa kukosa kingine.

Jonalisti katika *Bustani* alipochukua kopo moja ya ile mikebe waliyokuwa wanatoa na kula nyama ya bifu, alibaini kuwa, nyama ile haikuwafaa kiafya. Anakiri kuwa, alipolisoma alipata moja ya kopo lile likiwa limeandikwa, "… DELICIOUS BEEF. Upande wa pili Uliandikwa: EP 1980." (uk. 26). Ingawa aliwafahamisha kuwa nyama ile ilikuwa hatari kwa afya zao, walipuuzilia mbali kauli yake. Hali hushuhudiwa mara nyingi katika janibu ambazo umaskini hutawala na dhiki, maradhi, siasa mbaya, miundo msingi dhoofu na uongozi dhoofu kwa jumla huzagaa. Hili linawiana na kauli ya Ballard (2023) kuwa, ingawa anthroposenia ni zao la shughuli za kila siku za binadamu za kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kisiasa, hushamiri sana katika maeneo ambayo ni fukara kama tokeo la uongozi mbaya. Hili linashabihiana na nguzo ya uongozi mbaya.

Vijana wale walidai kuwa Jonalisti alikuwa anafanya mchezo na kuwa alichekesha, ila hawakutambua na au hawakujali hatari iliyowakondolea macho. Hili linaashiria jinsi wananchi hasa vijana katika mataifa mengi barani Afrika walivyotamauka na kukata tamaa ya maisha kutokana na ufukara. Inadhihirika kuwa, mataifa haya hayana budi ila kukila chakula kisichowafaa. Kijana Franco anashadidia kauli hii katika *Bustani* anapochota konzi la nyama toka koponi na kulipeleka kinywani na bila kungoja kuimeza, anadai kuwa, "Huoni? Tamu hii mzee. Bila hii, sisi zamani "tumeishakufa"." (uk. 27). Hili linaashiria kuwa, kutokana na umaskini mataifa changa ya Afrika hayana uhuru wa kuchagua na kutofautisha kizuri kutoka kwa kibaya, kwani wana kilichooza pekee. Hali hii inafungamana na mhimili wa uwezo unaosisitiza kuwa, athari za mataifa yenye uwezo za kuyapujua mataifa duni na changa ni ufukara usiomithilika (Quick, 2004; Tan, 2019; Moore, 2015; 2016).

Katika anthroposenia, ndwele za kila aina zinashamiri na kuwalemea wakaaji wa Mji wa Siza. Baadhi ya wengine ambao hawakusazwa na umaskini na maradhi aina aina ni vijana wale wawili waliokuwa mle kwenye dampu la Siza. Mmoja alikuwa na donda moja kichwani lililoonekana kutoa usaha na majimaji. Jonalisti aligundua kwamba lilikuwa na rangi ya zambarau. Wa pili alikuwa anatokwa na kamasi saa zote na mwili wake ulikuwa unamwasha. Kila wakati, mtoto yule aliyapangusa makamasi kwa mkono mmoja na wa pili ulishughulika na ugonjwa wa Franco. Aidha, alijikwangua kwa makucha yake meusi, mara ubavuni, mara tumboni, mgongoni, kichwani na bila haya wakati mwingine viungo vya siri vya mwili hadharani. Uharibifu na uchafuzi wa maeneo unadidimiza bahari kwa sababu moshi unaofuka umejaa kemikali za maangamizi. Hivyo, ulofa unaposhamiri maradhi na njaa zinakuwa hadithi za kila siku kwa watu. Ingawa hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya linawiana na utepetevu wa elimu bora barani Afrika ambayo huwatayarisha Waafrika kutegemea kuajiriwa badala ya kujiajiri na kujitosa katika bahari la uvumbuzi na uzinduzi. Hadi wa leo, elimu hii hutumiwa na mataifa tajiri kuendelea kuyafukarisha mataifa ya Afrika kiwango kwamba Waafrika wengi wanakumbwa na ufukara wa kimawazo.

Watoto wa Zaituni nao wanaashiria uzalishaji na uendelezaji wa umaskini. Majina yao yanaashiria utandawazi katika maeneo fukara ulimwenguni. Mwangaza anaozungumzia Maskini Jeuri unaashiria uchumi hafifu na dhoofu. Mwangaza wenyewe unatumiwa na viongozi kuwapumbaza wananchi. Waithiru (2019)

akikubaliana na mawazo ya mtafiti anafafanua kuwa, viongozi katika mataifa mengi barani Afrika hutumia pombe haramu, dawa za kulevya na ufukara kama ala za kuwapumbaza wananchi ili waendelee kudumisha siasa za umaskini. Maskini Jeuri anaeleza katika *Walenisi* kuwa, punde tu anapokunywa chang'aa na kulewa, huusahau ulofa wake na matambara yake huyaona kama suti. Ikumbukwe kwamba, anthroposenia hushamiri katika mataifa fukara zaidi kuliko mataifa tajiri. Hii ni kwa sababu, sera na mifumo ya uongozi katika mataifa fukara hupalilia umaskini zaidi, ukame, uchafuzi na uharibifu wa mazingira, uraibu wa dawa za kulevya na pombe haramu, ukoloni mamboleo, ubepari, maradhi na maafa ya wananchi. Hili linawiana na kauli ya Moore (2017; 2018) na Chandler, Grove, na Wakefield (2020) kuwa, ndiyo viongozi wa mataifa tajiri katika mfumo wa kapitalosenia wameyaharibu na kuyachafua mazingira ya mataifa fukara kwa kuyafanya kama dampu la kutupa taka hatari lakini viongozi wa mataifa haya fukara, hususani ya Afrika wamechangia uchafuzi na uharibifu huu kwa kuendeleza mbinu zinazopalilia ulofa na utegemezi za uongozi. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo.

Hivyo, mwangaza anaourejelea Maskini Jeuri ni taashira ya uongozi dhoofu katika mataifa fukara ya Afrika ambao hutumiwa na wanasiasa wakati wa kutafuta kura lakini wakichaguliwa hali huendelea kuwa vile vile au hata huzorota zaidi. Maskini Jeuri anafafanua katika *Walenisi* kuwa, akiwa mlevi huwaka na kitandani, gugumu la mke wake pamoja na kikwapa chake kitoacho uvundo huwa havisikii kamwe. Ingawa ni kujidanganya, huwa anajihisi mwenye siha njema kuliko ngamia na nguvu zake humzidi msemaji bikira. Kifantasia, elimu yake huzidi ya maprofesa wote duniani na matatizo yote maishani humwia vijidudusi tu. Anathibitisha hili anapofafanua katika *Walenisi* kuwa, "Ulevi huwa umenipa nuru nyingine tofauti kabisa; na kwa watu kama sisi, hii ndiyo taa yetu ambayo hata watawala wetu wanaipendelea sana kwa kuwa inatung'arishia nuru yake ya kiza." (uk. 74). Hivyo, ulevi kwa jumla unaashiria upofu unaoenezwa na viongozi ili kuwapumbaza wananchi kupitia pombe haramu, dawa za kulevya na ahadi za uongo ili kuendelea kudumisha uongozi dhalimu na wa kudhalilisha utu na haki za wananchi, hasa katika jamii za Afrika.

Kwa upande mwingine, Jehanamu ni taashira ya mataifa chafu na fukara ambapo uchoyo, ubinafsi na tamaa zimezagaa. Mkewe Dzombo, Hani ni taashira ya mataifa fukara yanayogugunwa na kunyofolewa rasilimali asilia na viongozi wa Ughaibuni kisha kutupwa yakiwa hindi bichi. Katika anthroposenia, ulofa unashamiri na

kupevuka. Ulofa huyafanya mazingira ulimwenguni kuparara. Watu ulimwenguni kwa akina Dzombo, huishi ndani ya vibanda vya kuvuja na kula kwa nadra, huku wakifanya kazi za sulubu. Hivyo, ulofa unaashiria na kuiimarisha anthroposenia.

Dzombo anakisia kuwa mkewe na watoto walikwishafukuzwa na bwana mwenye kibanda kwa kukosa kulipa kodi. Aidha, utovu wa maadili unapalilia uzembe na ufukara kwa jumla. Dzombo anawaona mkewe na watoto wake mawazoni mwake wakiteseka. Anawaona binti zake Chizi na Umazi wakilazimika kufanya kazi ya umalaya ili kujitafutia riziki huku wakinyiririkwa na michirizi ya machozi na huzuni zisizoisha nyoyoni mwao. Vilevile, alimwona Hani akiteseka kwa kuuza chang'aa na kutembea na walevi walalahoi. Hivyo, ulofa na utovu wa maadili, maradhi na kifo ni vyambajengo vyenye uhusiano wa kisimbyotiki. Mwandishi wa *Walenisi* anathibitisha hili anapoeleza kuwa:

> "Aliwaona wavulana wake Tsuma, Munga na Chai wakipevuka kuwa wevi, watumishwa, majangili, magaidi, magawadi na wazururaji malofa. Watu ambao miili yao itakuja kuwa chakula cha marisasi ya wenye mali …" (uk. 127).

Utabaka hasa kwa kuangaza wanyonge unaashiria tofauti za kiuchumi na kwa jumla tofauti kati ya waduni na walalahai. Ubaguzi wa maeneo nao unaashiria ulofa kwa kuwaonyesha wanyonge kama uchafu ulimwenguni. Kwa mfano, mijini wanakoishi Wachuna kunaashiria maeneo ambapo waduni huchukuliwa kama vifaa visivyofaa ila si kama wanadamu. Maskini wasiopalilia anthroposenia ila huishibisha, wanatengwa na kuishi maeneo yasiyo na miundo msingi imara – mashambani. Mtunzi Mkangi anathibitisha haya katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, "Jamii ikawa sasa imejigawa vipande viwili: mji na shamba. Tabaka mbili: mla na mliwa. Daraja mbili: akili na tani." (uk. 168). Ukabila unaozalisha kabila la tajiri na la maskini unapalilia umaskini zaidi. Kabila la tajiri linakuza anthroposenia kwa kulila kabila la maskini. Mtunzi Mkangi anaeleza katika *Walenisi* kuwa, tajiri anakuwa mlaji, mwenye akili na anayeishi mjini ilhali maskini anakuwa mliwa mwenye tani na anayeishi mashambani. Mgao huu wa dunia unazalishwa na viongozi dhalimu na matajiri ili waweze kuutawala utu na uhai wa wananchi maskini kwa jumla.

Dini inatumiwa na mtunzi Mkangi kuashiria umaskini kama kigezo kikuu cha kuiendeleza. Wachuna wanalalamika kuwa, sio mapenzi yao kuzaliwa na akili nyingi

kuwazidi wenzao ila ni kudra zake mungu mwenyewe. Hakika dini imetumiwa na viongozi dhalimu kuwapumbaza na kuwatumikisha wananchi kwa kuitumia kama kisababu cha udhaifu wao na changamoto zinazowakumba wananchi kila uchao. Aidha wananchi wengi hufanywa kuamini kuwa umaskini na utakatifu ni masuala sawia na pacha ilhali viongozi wa kisiasa na kidini wanafaa kuishi kama wafalme katika kasri zao huku wakilindwa na kuhifadhiwa na wanyonge 'watakatifu'. Wanasisitiza kuwa binadamu hawakuumbwa sawa na kuwa wako tofauti kama vidole vya mkono. Wanatumia hila hizi za utawala ili kwa mabavu na njama waendeleze uongozi na utawala dhalimu nchini mwao. Wao tu ndio walionufaika na uongozi na utawala dhalimu bila kujali athari zake hasi kwa ulimwengu na watu wale wengine. Ubinafsi, tamaa na ulaghai ndizo nguzo zinazowaongoza Wachuna katika utawala wao. Hivyo, wanagogomeza anthroposenia kwa mabavu katika ulimwengu. Kadhalika, wanashikilia msimamo kuwa, bila wao kutekeleza kazi yao ya ubongo, basi ulimwengiu ungesimama na hakuna chochote kingeweza kutendeka.

Mtunzi Mkangi anafafanua katika *Walenisi* kuwa, "Kazi ya ubongo – yaani kazi yoyote iliyofanywa na Wachuna, ikawa na heshima na thamani zaidi kuliko kazi ya tani – yaani za mikono za waja wao." (uk. 169). Hivi ndivyo malipo yalivyodidimizwa pia. Kwa mfano, ukulima ulianza kuleta mapato duni na wengi wakauambaa, jambo ambalo lilipalilia njaa na ufukara kwa jumla. Kuraruka kwa gora la jamii katika vipande viwili kunaashiria jinsi anthroposenia inavyorarua ulimwengu na utu wa binadamu katika vigae vidogo vidogo. Jinsi anthroposenia inavyozidi kuota mizizi kupitia umaskini katika jamii ya ulimwengu mzima ndivyo utu unavyoendelea kufifia kila uchao. Hili linawiana na kauli ya White na Whitlock (2021) na Waithiru (2022d) kuwa, wenye uwezo hutumia dini kama kigezo cha kuueleza na kuufafanulia ufukara na hatimaye kama kigezo cha kuhalalisha uchafuzi, uharibifu na maangamizi ya watu kama jambo la kusherehekewa na kudumishwa, hususani baina ya waumini.

Vilevile, umaskini unachangia ugawaji wa ardhi kama vile nyama ya Moto ya kulungu. Hivyo, kiuyakinifu, Wachuna ni taashira ya matajiri wenye hushabikia ulofa ili kuendelea kuwatala na kuwathibiti watawaliwa. Katika mataifa mengi barani Afrika suala la ugawaji wa ardhi katika visehemu vidogo vidogo liliasisiwa na Mkoloni kabla ya kung'atuliwa mamlakani enzi za ukoloni mkongwe. Lengo la mkoloni huwa kulifanya bara la Afrika hafifu kwa upande wa ukulima hivi kwamba linayategemea mataifa yale yale yaliyowahi kulitawala. Mashamba yanapogawika

katika visehemu vidogo ukulima hushuka na mazao hupungua kwa kiwango kikubwa na hili huimarisha njaa na umaskini kwa jumla. Mathalani, mwandishi Mkangi katika *Walenisi* anaeleza kuwa:

> "Wachuna waliigawa nchi:
> Vipande – vipande karatasini.
> Nayo njaa kajaza nchi:
> Vipande – vipande vya maiti!" (uk. 170).

Kutokana na umaskini unaoashiriwa na mabarubaru wanaotumia mabavu kuwanyanyasa wananchi, vita vya wenyewe kwa wenyewe vinaibuka na kupevuka. Kwa mfano, vita vya upanuzi vya wenyewe kwa wenyewe pamoja na ugomvi wa kivolkeno ni taashira ya madhara ya ulofa baina ya wananchi hususani barani Afrika. Hall (2010), na Morton (2007; 2010) wanaeleza kuwa, kanoni za anthroposenia huzalisha vurugu dhidi ya mazingira kutokana na athari hasi za ukoloni mamboleo, hasa katika maeneo ambayo yaliwahi kudhibitiwa na wakoloni. Kwa mfano, wanadokeza kuwa, vurugu dhidi ya mazingira za kikoloni, kwa kiwango kikubwa huhusishwa na malengo yaliyowekwa na mkoloni katika koloni mbalimbali za hapo kabla, ambapo hadi leo malengo yale yanatawala paruwanja kupitia vikaragosi wa wakoloni wale wale.

Mwandishi anadhihirisha kuwa, umaskini huwaangamiza walalahoi zaidi kuliko walalahai anapotaja kuwa, "… ndwele hii ilikuta na kuenea zaidi kati ya wanyonge." (uk. 190). Umaskini hurutubisha anthroposenia na kwa misingi hiyo hiyo, anthroposenia hukuza ufukara. Hivyo uhusiano kati ya anthroposenia na ufukara ni wa kisimbiotiki. Mtunzi Mkangi anathibitisha uhusiano huu anaposawiri hali ambapo wanyonge walipandwa na mori wa ulafi. Mori huu ulikuwa unachochewa na kutiwa chokochoko na Wachuna ambao walikuwa wakiwarushia wachochole vijipande vya nyama mithili ya kuku wanaorushiwa punje za mahindi, wasiokuwa na budi ila kuzingoja punje zile kwa hamu na kuzidaka hewani. Smith (2007) na Waithiru (2022a) wanataja kuwa, viongozi wengi barani Afrika hudumisha siasa za umaskini ili kuweza kuwadhibiti wananchi kupitia ulofa na hususani njaa. Wachuna walikuwa wanawatupia waduni vijipande vichache na hili likawalazimisha walalahoi kupapurana, kukatana meno, kupigana miereka na kutiana makucha wakipigania

makombo yale haba. Hali hii inaashiria ulofa unaoashiria anthroposenia moja kwa moja.

### 5.2.6 Taashira ya Hali za Maumbile

Kwa mujibu wa Waithiru na wengine (2021: 48), "hali za maumbile huwa anuwai." Mathalani, Serikali ama Fyanduzi katika *Walenisi* ni taashira ya anthroposenia. Wachuna ambao kwa jumla ni taashira ya anthroposenia wanaimarisha utawala na uongozi dhalimu kwa kumiliki tambo za uchawi, moto na mabavu na kuzifanya tambo moja katika mfumo unaoashiria udhalimu. Tambo hili katika istilahi ya kitafsida linarejelewa kwa Fyanduzi au Serikali. Hii ni kwa sababu, tambo la Uchawi linaashiria utawala na udhibiti dhalimu ambao unapaliliwa na mambo kadha wa kadha. Mambo haya ni yakiwemo uganga, dini na sayansi. Hivyo, uchawi unaimarisha utawala dhalimu kupitia uganga, dini na sayansi. Kama ilivyotajwa awali katika sehemu hii, moto ni taashira ya maangamizi. Mtunzi Mkangi anasisitiza kuwa, ufundi, uhandisi na teknolojia ni baadhi ya virutubishi vya maafa kupitia moto. Kile anachosisitiza mwandishi wa riwaya ya *Walenisi* ni kuwa, ubunifu, uumbaji na uvumbuzi wa binadamu kupitia ufundi, uhandisi na teknolojia, ndio uumbaji na uharibifu wa maangamizi hasa, kama zao la udhalimu wa kila namna.

Kadhalika, tambo ya Mabavu linaivisha jungu la uwezo, nguvu, vyeo na madaraka. Kwa jumla, tambo la Mabavu ni taashira ya utawala wa kidikteta linaloimarishwa na uwezo, nguvu, vyeo na madaraka. Hali hizi tofauti zinaungana na kupatana katika kuzalisha anthroposenia kwa jumla. Smith (2007), Mukherjee (2010) na Waithiru (2022c) wanasisitiza kwamba, kando na serikali, watu wenye uwezo, nguvu, vyeo na madaraka kurutubisha uchafuzi na uharibifu aina aina huzalisha na hupalilia utawala dhalimu kwa lengo la kuendeleza ulofa hivyo kudumisha ubepari, utabaka, ubinafsi na ubaguzi katika mataifa mengi ulimwenguni. Kwa mujibu wa mwandishi Mkangi katika riwaya yake ya *Walenisi*, mafiga matatu yaliyooteshwa nyoyoni na akilini mwa wananchi wa taifa la Uchuna, ni taashira ya udhibiti wa nafsi za watu na utu wao kwa jumla. Mtunzi Mkangi anafafanua kuwa, Wachuna waliilinda na kuitunza anthroposenia kwa kuimarisha mizizi ya utawala wao dhalimu. Uongozi mbaya huchangia pakubwa katika ukuuzaji, utangazaji na mauzo ya anthroposenia hasa katika mataifa fukara ya Afrika (Moore, 2017, na Coughlin na Gephart, 2020).

Wachuna walibaini hili hivyo waliweza kupalilia udhibiti wa kimawazo kupitia Figa la Uoga, Figa la Ulafi, na Figa la Ujinga. Kama tu Jabali la Ujinga, mafiga haya yalijiunganisha na kukamilishana, kiwango kwamba ilikuwa muhali kutambua lipi ni lipi, ndani ya utando wa anthroposenia. Hili linathibitishwa na utaratibu waliouzingatia Wachuna kuimarisha ubaguzi na dhuluma. Figa la Uoga ndilo lililotangulia kukitwa nyoyoni za Wachuna. Waithiru na wengine (2021) wakiyaunga mkono mawazo ya mtafiti wanasisitiza kuwa, uoga sio tu silaha mwafaka ya kupalilia uongozi mbaya ila pia ni mbinu madhubuti na ya kutegemewa katika kuimarisha ukoloni mamboleo kwa lengo la kuuendeleza udhalimu. Moto aliutumia uoga vyema kuwafanya wenzake wazingatie sheria zake za maonevu na unyama. Figa la uoga lilipalilia udhibiti wa utawala na uongozi katika nchi ya Wachuna kwa mafanikio kutokana na ujinga waliokuwa nao wananchi. Ujinga huwapumbaza watu na kuwapofusha dhidi ya kutambua ukweli wa mambo.

Hata hivyo, baada ya uoga kutoweka punde tu ujinga ulipoyeyuka na kutoweka, Wachuna walitumia Mabavu kuuendeleza udhalimu na maonevu. Mabavu yenyewe yalifanikishwa na Wachuna kupitia ubunifu na uundaji wa silaha za kila aina za maangamizi. Mathalani, uvumbuzi wa bunduki ulirahisisha mauaji kwa kuokoa muda na wafanyikazi wauaji. Hii ni kwa sababu, mtu mmoja anaweza akatumia bunduki moja kuwaangamiza maelfu ya watu bila kuchafua wala kubomoa majengo na mali. Hivyo, uvumbuzi wa bunduki ukawa kilele cha uimarishaji wa maangamizi katika istilahi ya maendeleo endelevu. Ikumbukwe kwamba, utafiti huu uliongozwa na baadhi ya nguzo kuu za nadharia ya Uhakikimazingira. Hili linawiana na kauli ya Waithiru (2022a) kuwa, binadamu hawezi akapiga hatua bila kuyahusisha na kuyawajibikia mazingira yake katika harakati za maendeleo endelevu. Kwani bila kufanya hivyo, binadamu atayaangamiza mazingira yake mwenyewe pamoja na yeye mwenyewe mumo ndani katika mfumo wa kujiua kimazingira. Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anaongeza kuwa, maendeleo endelevu yanayoendeleza utabaka, maonevu, uoga, chuki, utandawazi na ubepari hupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira ulimwenguni. Mtunzi Mkangi anadhihirisha ukweli huu pale anapotaja kuwa:

> "Kubuniwa kwa bunduki hii pamoja na silaha nyingine, kama vile mabomu ya kutoa machozi na huku yakianzisha mtetemo wa ardhi, kulikuwa na lengo moja tu: nalo lilikuwa ni kuwatia wadhalilishwaji uoga ili wasiweze hata kuota kujikomboa." (uk. 188).

Wachuna walipalilia na kuulinda uongozi mbaya kupitia vikosi mbalimbali walivyoviunda kwa lengo hilo tu. Vikosi vyote vilikabidhiwa silaha za kutisha na kuwezeshwa kuangamiza yeyote na chochote kilichotishia uhai wa utawala dhalimu. Kwa mfano, wenyeji waliojaribu kusimama kidete kukabiliana na uongozi dhalimu hawakubahatika kwani, katika hiyo hali yao ya uduni waliuliwa kinyama. Kikosi kama cha "HFFU" – "Hebu Fanya Fujo Uone" – kililinda uongozi dhalimu kwa jino na ukucha. Vikosi hivi, pamoja na silaha zao, vinaashiria walinzi wa anthroposenia katika mataifa mengi barani Afrika. Hili linawiana na kauli ya Smith (2007), Mwirabua (2014) na Waithiru (2019) kuwa, vikosi vingi vya usalama barani Afrika hutumiwa na viongozi dhalimu kuimarisha ufisadi katika mfumo wa ukoloni mamboleo kwa minajili ya kuendeleza ubepari, ubidhaaishaji wa binadamu na utu, vurugu dhidi ya mazingira, utabaka, ulofa, maradhi, ukame na hatimaye maafa ya bayotiki.

Kwa misingi hii, figa la uoga likafanikiwa sana katika taifa la Uchuna. Mtunzi Mkangi anaongeza kuwa, hulka ya unyama huimarika huku utu ukididimia katika mazingira chafu. Hulka hii ya unyama inadhihirika pale ambapo baadhi ya Wachuna walalahai wanawakebehi na kuwakejeli wenzao walalahoi. Haya yote yanafanikishwa na hofu inayozidi kunogeshwa na kukolezwa zaidi kwa mabavu yanayozalisha kaida. Kaida zenyewe nazo zinazaa magereza. Hivyo, mabavu, kaida za magereza ni taashira ya utumwa hasa kwa binadamu. Kwa mkondo huu, uchawi, dini na Jehanamu ni taashira ya utumwa. Kama ilivyotajwa hapo awali, uchawi na dini kando na kuwa taashira za ala ya kupalilia umaskini ni aina za utumwa ulimwenguni, zinazostawishwa na kigezo kimoja kikuu – uoga. Hili linathibishwa na mwandishi wa *Walenisi* anapofafanua kuwa:

> "Kwa nini? Ili kushindilia zaidi figa la uoga kwa kuwapumbaza na tamaa za baadaye. … tamaa hizi zilikuwa vichwani mwa wachochole. Wasiobahatika ambao walitii kwa kuwa lijamu hii ilikuwa imegongomewa mwao akilini na ikajigeuza na kuonekana kama tabia zao za kikawaida. Kwa kweli wakaishia kuwa magofu tu basi." (uk. 188).

Tangu enzi za Mbeberu, utawala dhalimu umekuwa ukishamiri katika utawala wa kuwagawa na kuwatawanya binadamu (Thiong'o, 1987). Mtunzi Mkangi anathibitisha hili anaposisitiza kuwa, viongozi Wachuna walihakikisha kuwa

binadamu hawajashikamana na badala yake wametawanyika na kutawaliwa na ulofa, njaa, maradhi na mateso bila kikomo. Wachuna walifanikisha hali hii kwa kuyafanya mambo msingi kuwa bidhaa za kununuliwa tena kwa gharama ya juu. Mathalani, mambo kama utu, ubinadamu, maadili, heshima, nafsi na amani yalipigwa mnada na kunajisiwa hadhi yao paruwanja. Aidha, Wachuna walibuni madanguro ambapo wanawake na wanaume walifurahishia wateja wao kwa kucheza uchi. Uchafuzi huu wa maadili ulizagaa hadi kwa uongozi na mazingira kimwavuli.

Hali hii ilipalilia na ingali inapalilia utawala dhalimu pakubwa. Kutokana na ulafi wa wenye uwezo wa kiuchumi wakichelea kuvikosa baadaye, walivinunua kwa wingi na kujirundikia wenyewe bila kuwajali wanyonge. Hivyo, ulafi pia unaimarisha na kuashiria ubaguzi na utabaka ulimwenguni. Mtunzi Mkangi anakubaliana na ukweli huu anapotaja kuwa, “Ikiwa figa la uoga ndilo lililokuwa nguzo, basi lile la ulafi ndilo lililokuwa mwamba. Kutoka mwambani, pao la uchoyo-ubinafsi likateremka.” (uk. 189). Hivyo basi, uongozi mbaya na utawala dhalimu hupaliliwa na kutiwa mbolea na virutubishi na ubinafsi-uchoyo. Katika msemo wa, “Kila mtu peke yake na mungu awe wetu sote,” (uk. 189), utawala dhalimu na utamaduni ulionajisiwa unashamiri na kutapakaa kote ulimwenguni. Figa la pili lililokita nyoyoni mwa Wachuna ni lile la ulafi, ambalo liliwabadili watawala na watawaliwa kwa jumla kutoka kuwa binadamu hadi kuwa vyombo vya bishara vilivyopalilia ulofa na utawala dhoofu usiku na mchana.

Kinachodhihirishwa na Huggan na Tiffin (2010), Walder (2011), Morton (2012) na Moore (2017) wanashikilia msimamo kuwa, uchafuzi na uharibifu wa mazingira hushamiri katika mazingira ambamo utajiri wa mali na fedha huupiku uhai na utu wa binadamu. Mwandishi Mkangi anathibisha hili anapoeleza katika *Walenisi* kuwa, “… ulafi na nduguze ubinafsi na uchoyo wakapata nguvu na kutapakaa mpaka hali hiyo ikatambulikana kuwa ndiyo hali ya ustaarabu wa hali ya juu sana. … kitu cha thamani mno kuzidi hata uhai wa mtu.” (uk. 189 - 190). Mwandishi anasisitiza kuwa, chini ya ubaguzi na utabaka matajiri wachache huishi kama binadamu katika unyama wao huku wakiwalazimisha binadamu maskini wengi kuishi kama wanyama. Hali hii hufanikishwa na ulafi na pao zake. Hivyo, ulafi na pao zake ni taashira ya maangamizi ambapo hamna chochote kizuri cha ubinadamu huweza kuota. Hata hivyo, wanaoteseka na kuangamia katika mazingira fukara na chafu ni wachochole.

Kando na ujinga, ulofa, dini na ulafi kuwa taashira ya utawala dhalimu, mtunzi Mkangi anaashira lugha kama taashira ya ala ya kukuza na kupalilia dhuluma na utumwa. Hii ndiyo sababu, Wachuna walifanya juhudi ili wanyonge wasizinduke na kukabiliana na uongozi dhalimu. Hivyo, waliwapa watawaliwa elimu ya hekima ya kidundu. Elimu hii inaashiria utumwa madhali iliwafumba macho wanyonge wakakosa kuona ukweli wa kimazigazi. Hili lilisababisha maafa kwa yeyote aliyejaribu kuwaamsha wanyonge kwa kuwaelimisha kuhusu uongozi dhoofu na athari zake za utumwa kwa walalahoi. Mwandishi Mkangi anadhihirisha hali hii kupitia maelezo anayoyaeleza kuwa:

> "'Angalia washenzi wanavyofanyana? Hee … hee … heee …" Wachuna waliwacheka na kujitia kutoelewa chanzo cha tabia ya ushenzi wa wanyonge. Lakini walitambua kuwa walitawalika kwa urahisi baada ya kufuzu kwao katika ushenzi huo. … dini nayo wakapewa bure – jambo ambalo liliwapatiliza kwa kuwagongomeza zaidi ujingani. … Ulafi ukawa umewadidimiza ndani ya figa la Ujinga na likawa silaha kubwa mikononi mwa Wachuna. Walitambua … msemo uliosema: "Usimwamshe aliyelala ama utalala wewe." (uk. 190 - 191).

Nguzo kuu ya utumwa na udhibiti wa mawazo ya watu kama inavyoashiriwa na mwandishi wa *Walenisi* ni ujinga. Mathalani, Wachuna waliutambua na kuutegemea sana ujinga wa watawaliwa kwa minajili ya wao kuendelea kuufaidi uongozi na utawala dhalimu. Vilevile, uchawi, mashetani, majini, hirizi, maji matakatifu, misalaba, miujiza na waganga bandia ni taashira ya utumwa na uchafuzi wa mawazo na maadili kulingana na mtunzi Mkangi. Ukosefu wa utu baina ya matajiri pia unaashiria unyama. Hakika utumwa wa kimawazo na utabaka huzalisha umaskini kwa kiwango kikubwa. Wananchi wakiwa maskini huwa rahisi kutawaliwa na viongozi dhalimu.

Baada ya akina mama Fofi katika *Mafuta* kutambua kuwa mabaki ya makombo yalimfaa sana Matope, wanalitia pipa-jaa maji hadi pomoni, kiwango kwamba inambidi Matope kutumia mshipi na ndoano kuvua tinyango za nyama, samaki wa kupaka na mapochopocho mengine mengi. Matajiri wanawadunisha maskini kiasi kwamba wanayadhalilisha maisha yao. Kwa mfano, akina mama Fofi wanakitia chakula sumu ya panya na hatimaye kukipulizia dawa ya kunguni juu yake kama

mchuzi. Hili linaashiria upaliliaji wa maafa ambapo wachochole wanahiari kufa kuliko kuishi. Mtunzi Mkangi anadhihirisha hili katika *Mafuta* kupitia mawazo ya Matope anasema kuwa, "… ni afadhali kujitoa katika hali hii ya unyonge na utesaji pengine huko ahera huenda nikaonewa huruma." (uk. 40). Ukosefu huu wa utu hushamiri kiwango kwamba imekubalika na wengi kama hulka ya jamii. Hali hii huwafanya watu kukubali uchafuzi na uharibifu kama jambo linalokubalika na wanajamii hususani katika mataifa maskini.

Baada ya Matope kutendewa uhasidi na familia ile ya matajiri, anajisweta pale seng'engeni na huku damu ikimtiririka mgongoni anarudi kwake kwenye kidimbwi cha matope. Mwandishi wa *Mafuta* anataja kuwa, "… nilijirudisha pale pangu kidimbwini nikiwa majeruhi ya hulka ya jamii." (uk. 40). Aidha, matajiri wameubadili unyama wao na kuufanya utu na utu wa wachochole wakaufanya unyama ili kudumisha na kuimarisha utajiri ndani ya ubaguzi na ulaghai tele. Ndiposa matajiri wanawaona walalahoi kama nzi ambaye kufia kidondani – maafa ya wanyonge – si hasara. Kuthibitisha kuwa ukosefu wa utu unapalilia unyama, mwandishi wa *Mafuta* anaeleza kuwa, "Ikawa sasa ni mashindano ya yupi angeweza kuja na utesaji … wa kubuni … kabisa. … alijitokeza … akamlaani kwa kubwata: "Mtu weee …!""'(uk. 41 – 2).

Mbwa ni taashira ya watu duni hasa katika mataifa fukara ulimwenguni. Ti amewazoea mbwa wala watu ambao hufungwa na cheni na kufungiwa vizimbani vyao. Huwa hawatangamani na mabwana zao wala watu wengine. Mbwa hawa dhima yao kuu ni kushindishwa njaa ili wawe tayari kumla yeyote anayejaribu kuyaiba mali ya kuporwa. Hali hii inaashiria ubadhilifu wa mali ya umma hasa katika kipindi cha baada ya usasa. Kwa misingi hii hii, vita vya nyani na chui vinaashiria hali halisi ya uhusiano dhalimu baina ya viongozi na watawaliwa. Chui anaashiria watu dhalimu kupitia matajiri, viongozi na wenye uwezo katika jamii ilhali nyani ni taashira ya wananchi wanyonge. Chui na nyani wanapopanda mti wa mfune ili watizame kama kulikuwa kukija vita, chui anamtia makucha nyani. Nyani anatiririkwa damu huku chui akiiramba tu kwa furaha na alivyozidi kuiramba ndivyo alizidi kuyazika makucha yake mwilini mwa nyani. Walipofika kileleni, chui alitaka kujua vita vilikuwa vikitoka wapi na nyani katika *Mafuta* akamjibu kuwa, "… vita havikuwa vikitoka nje, bali ndani!"(uk. 78). Hali hii inasawiri namna utawala dhalimu huwanyonya damu wanyonge kupitia maradhi, ulofa na dhuluma chungu nzima.

Uongo na unafiki huwa vigezo vikuu vya kuendeleza udhibiti wa watu, uchumi wao, siasa zao, utamaduni na nafsi zao. Mbinu hizi za uongo, unafiki na kuogofya zinathibitishwa na mawazo ya Mtue kufanikisha umaskini. Mtue anashuku kuwa atachomwa na moto wa spaki uumeni, adungwe na sindano vidoleni na atoswe mapipani yaliyojaa maji machafu. Lengo kuu likiwa kuogofya. Kadhalika, anaogopa asije akarushwa kwenye shimo la majoka au hata kupelekwa msituni huku akiwa amefungwa kidato. Anahofia kutishwa na mabastola, kukemewa, kukaripiwa, kupondwa na matako ya mabunduki na kudhulumiwa kwa njia mbadala, kama vile; kusukumwa, kutukanwa, kudadisiwa, kufyandwa au hata kudungwa.

Chui Football Club ni taashira ya vijana wanaoshiriki hila na uzandiki katika fukara ya Afrika katika misingi ya ulaghai na uchawi. Kabla ya mechi, wachezaji wa klabu hii hugangwa na Gwiji ambaye ni mchawi anayesifika na ulogi wake wa kuaminika. Mmoja wa wachezaji anadhihirisha hili katika *Vipuli* anaposema kuwa, "“Blaza, ule uganga ulikuwa babu kubwa.” Mwenzake naye anajibu kuwa, “Sana. La sivyo Mehala ingetutoa.”" (uk. 237). Uganga huu huu ndio unaowapa ushindi dhidi ya Nigeria Morning Stars na katika mechi zingine zote wanazocheza. Sala ya Gwiji katika *Vipuli* inathibitisha hili inayosema kuwa:

> “Wewe golikipa wa Nigeria
> Tumekupofua macho
> Giza limekwingia
> Huna unaloweza
> AMINA.” (uk. 31).

**5.3 Taswira**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 225), “taswira ni dhana ya kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji”. Kuna taswira za kimaelezo ambazo huunda picha za kiishara zinazoashiria jambo fulani au zinazoficha ujumbe mwingine. Wamitila anaonyesha uhusiano uliopo baina ya taswira na jazanda kwa kusema kwamba jazanda ni neno ambalo hutumiwa kurejelea ile hali ya kutumia picha au taswira katika kazi ya kifasihi (Wamitila, 2010). Mtafiti alitambua kuwa jazanda na taswira ni kama ndugu, kwa sababu huhusu picha ambazo zimetumika kuashiria kitu fulani katika kazi ya kifasihi. Jazanda za kitaashira huwa na picha au taswira yenye ujumbe. Khamis (2004) anapambanua kuwa, taswira hurejelea

matumizi ya lugha kuwakilisha vifaa, matendo, hisi, mawazo, dhana, hali ya mawazo pamoja na tajriba za viungo vya kuwaza. Kuhusiana na taswira, Khamis anataja vipengele vinne vya taswira ambapo utafiti huu ulichunguza mojayazo ambayo ni ile ya mazingira asilia; kama vile, taswira za bahari, maziwa, mito, misitu, vichaka, wanyama, jangwa, milima, bonde, mawingu, mawimbi, volkanos mafuriko na nyingine nyingi.

Taswira hufanikisha lengo la mwandishi wa kazi ya kifasihi kutokana na uwezo wake wa kuchukuana na mazingira na wakati husika (Timammy, 2020). Musembi (2019) anaeleza kuwa, mtunzi Mkangi ametumia taswira katika kazi zake kwa lengo la kuyafumbika masuala nyeti na kuwasilisha ujumbe nuiwa vyema zaidi na kwa njia nyepesi na madhubuti. Hii ni kwa sababu, taswira alizozitumia mtunzi Mkangi kusawiri uongozi mbaya, dhuluma na maafa katika *Mafuta* na *Walenisi* zina uwezo mkubwa wa kuzifanya zinate na zigande mawazoni mwa msomaji ili aweze kufahamikiwa na uhalisi wa athari hasi za uongozi dhoofu, ulofa, maradhi na ndwele na kwa wakati huo huo apate ari na mshawasha wa kutaka kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika mazingira yake.

Mwandishi wa *Bustani* amesawiri uchafuzi na uharibifu wa mazingira na uhai wa binadamu kupitia taswira. Anasawiri mle kiwandani anapoeleza kuwa, Jonalisti alimotoka mle chooni, alielekea sehemu ya kuchemshia madawa. Aliifuata korido huku akipishana na wafanyakazi wengine. Alipofika tamati aliteremka kupitia ngazi zilizoteremsha hadi chini, ardhini. Hapa aliyapata madumu makubwa yaliyokuwa yamesimamishwa ukutani yakichemka. Mabomba membamba na mapana yalipita juu ya vichwa vya wafanyakazi waliokuwa wanaendeleza kazi zao kwa uangalifu mkubwa. Taswira huhusiaha matumizi ya maneneo kuelezea dhana au hali mbalimbali. Husaidia kuumba mandhari, kuimarisha muktadha na kuonyesha mhusika wa kazi ya kisanaa paruwanja, mandhari humchorea msomaji taswira pendwa, na ya kuvutia na nyepesi kujinasibisha nayo na kuitambua. Waandishi hutegemea taswira kuwapa wasomaji dhana, jumbe, na hali za kile wanachonuia kuashiria. Hufanikisha hili kwa uchaguzi mwafaka wa maneno yanayotumiwa kuwasilisha ujumbe lengwa kwa hadhira lengwa kwa njia nyepesi na madhubuti (Ngugi na Nabea, 2011).

Mtunzi Mbogo anaeleza katika *Bustani* kuwa, Jonalisti alikanyaga na kuvuka nyasi fupi pale jaani. Nyasi zenyewe zilikuwa na unga wa kemikali na mafuta ya dizeli.

Vibiwi vichache vya takataka vilivyounguzwa vilikuwa vinafuka moshi uliokuwa unajisokota na kusambaa sehemu zote za janibu la dampu lile. Moshi ule ulimwathiri Jonalisti na kumfanya apige chafya. Anasawiriwa akipiga hatua pale anapokanyaga maji machafu yaliyokuwa yamemwagwa pale na moja ya malori ya utawala wa kaunti ya Siza. Kadhalika, anasawiri aina mbalimbali za uchafu hatari pale kwenye jaa la taka. Mathalani, watu walikuwemo kwenye vikundi vya aidha wawili wawili, watatu watatu, wanne wanne au hata zaidi. Jonalisti aliweza kuwaona wanawake na wanaume wa umri tofautitofauti pamoja na watoto waliojizatiti kuchakurachakura takataka ili wapate 'almasi' kama walivyoiita au 'mali'. Hili linaashiria ufukara katika jamii kama zao la mazingira chafu na tasa.

Aidha, Jonalisti anawapiga picha wanawake wawili waliokuwa wameinama wakiokota mabonge ya ugali na kuyatia vikapuni. Hili linaonyesha kuwa, katika anthroposenia, kuna wale walio na shibe kiasi kwamba wanatupa chakula na kwa wakati huo huo kuna wale maskini hohehahe wasio hata na tonge la kumega. Upande mwingine mkabala na wanawake wale wawili mlikuwa na lundo la sindano za hospitali, madawa ya aina mbalimbali ndani ya chupa, pamba na mabendiji yaliyochanganyika na damu. Hili linadhihirisha kuwa, katika anthroposenia, uongozi mbaya unashamiri. Waithiru (2019, 2022a, na 2022c) anafafanua kuwa, uongozi mbaya huzalisha ufisadi, ubinafsi na utowajibikaji wa viongozi baina ya masuala mengine mengi hasi.

Kutokana na kutowajibikia wananchi, uongozi mbaya unapelekea matumizi mabaya ya madawa ambayo ni adimu kwa wagonjwa wengi katika hospitali nyingi mjini Siza. Kadhalika, wanaofaa kuwajibikia na kusikitikia mazingira wanapotupa taka, hawawajibiki. Katika anthroposenia, sindano za hospitali zinatupwa ovyo, madawa ambayo yangewafaa wagonjwa na yaliyowagharimu wananchi kodi ya juu yanatupwa ovyo na pia taka kama bendiji zinatupwa ovyo. Hili linatishia uhai wa binadamu kutokana na maradhi yanayomkumba pamoja na ufukara. Aidha maafa ni mojawapo ya mazao ya anthroposenia. Mbogo anasawiri jinsi watu wanapoona viungo vya maiti wanavyocheka kutokana na hali ya kawaida ya watu kufa katika anthroposenia hadi watu wakazoea. Jonalisti alipokuwa akipiga picha katika maeneo tofautitofauti ya lile jaa la taka, alishangaa kuwaona watu kama sita hivi wakiivamia ghafla sehemu ile, yenye sindano za hospitali, madawa ndani ya chupa, pamba na mabendiji yaliyochanganyika na damu. Mtafaruku na tafrani ya kugombea almasi, dhahabu na

lulu za dampu ukachipuka na kushamiri kati ya watu wale. Hili linaashiria athari za uongozi mbaya ambao hushamiri katika mazingira chafu na tasa kutokana na kunajisiwa na kemikali. Watawaliwa hujipata wakifukarika zaidi, wakiugua maradhi yanayoangamiza, na chuki na uhasama huzaliwa.

Siundu (2011), Foucault (2017) na Waithiru (2019), wakipambanua kuhusu uchafu wa uongozi uliooza wanaeleza kuwa, viongozi waovu hukosa tofauti kati ya uchafu na wananchi. Wananchi nao hufikia upeo wa kukubali hali hii hasa katika mazingira yaliyochafuliwa na kuharibiwa. Katika *Bustani* tunasawiriwa jinsi serikali ya Siza inavyolea uchafu unaowasababishia wananchi madhara makubwa. Jonalisti pamoja na watu waliokuwa pale waliona mkono wa binadamu baina ya takataka kwenye jaa. Mkono wenyewe ulikuwa mzima, tangia begani, kiwikoni hadi kiganjani. Ingawa ulikuwa umekwishaanza kuoza, mmoja wao alichukua mti na kuurusha mkono ule mahali peupe zaidi na ukaonekana vyema. Tukio hili badala ya kuwashtua au kuwashangaza linawaburudisha na wanacheka. Hali ya hewa inayosawiriwa kwenye ja lile la taka, si mwafaka kwa binadamu. Ndiposa Jonalisti anapogeuka kuondoka baada ya kupiga mkono ule picha tatu anakohoa. Mathalani, mwandishi wa *Bustani* anadhihirisha hili anapoeleza kuwa: “Jonalisti alikohoa Khoo! Khoo! Khoo! “Ee! Nimerudi.” Machozi yalikuwa yanamtoka – moshi. Alitoa kitambaa akajifuta.” (uk. 26). Hii ni baada ya yule mtoto mwenye kidonda cha zambarau kichwani kumuuliza ikiwa alikuwa ametosheka na dampu, ndiposa akarejea kuchukua pikipiki yake. Hakika mazingira chafu na yaliyoharibiwa yana ukuruba wa karibu sana na umaskini wa aina aina ulimwenguni kwa jumla.

Jonalisti aliwaona nguruwe wakila takataka zilizovunda pale kwenye jaa. Mlikuwamo majimaji, miozo ya mabaki ya mafuta machafu na miozo ya mabaki ya nyama iliyotoa mijifunza mikubwa. Kadhalika, mlikuwa na matambara ya nguo na ya sodo pamoja na watoto walioharakisha kuwasili ulimwenguni kabla ya siku yao ya kuzaliwa kuwadia miongoni mwa takataka zingine tele. Mwandishi wa *Bustani* anaendelea kusawiri mazingira dhoofu kupitia usawiri wa janibu na viumbe anavyotagusana navyo Pasta Yona katika safari yake ya kuelekea kwenye kilele cha mlima kuongea na Mungu. Pasta Yona alichukua fimbo ndefu kutoka pale kwenye kona sebuleni, kisha akaelekea kwenye kilele cha mlima. Alipotoka nje alikumbana na giza lililokuwa limetanda huku hali ya hewa ikiwa ya baridi. Katikati ya makaburi ya Wakristo, Pasta Yona alitembea taratibu huku akiifuata njia ile ya mkato. Akiwa

hatua kadhaa pale makaburini, alikutana na Kanoni Lunga ambaye alimsabahi, lakini Pasta Yona hakumjibu. Alipiga hatua na kupita katikati ya uwanja wa mpira na kushika njia iliyopita katikati mwa shamba la kanisa hadi shuleni. Kile kimya katika shule ya misheni kuanzia darasa la kwanza hadi la saba kinaashiria namna binadamu anavyonyamaza huku uchafuzi na uharibifu wa mazingira ukinawiri badala ya kuung'oa mizizi.

Mtunzi Mbogo katika *Bustani* anasawiri mazingira chafu na yaliyoharibiwa na binadamu pale mjini Siza. Anafafanua kuwa, Pasta Yona aliposimama kidogo kuipumzisha miguu yake, aligeuka na kutazama Mji wa Siza. Mji wenyewe uliwaka taa za umeme, hususani katika maeneo ya madukani. Pasta Yona katika *Bustani* anasawiri taswira ya uharibifu wa mazingira kwa jumla anapoeleza kuwa: "Aliyatuliza macho yake, akaitazama misokoto myeusi iliyopaa juu kimbagombago na ghafla moshi ule uligeuka kuwa majoka makubwa meusi." (uk. 34). Katika sehemu za wananchi wa kawaida moto wa kawaida ulionekana. Ikumbukwe kwamba moto ni mojayazo ya aina za anthroposenia zilizochunguzwa katika utafiti huu. Kadhalika, mazingira chafu na tasa huathiri kwa kiwango kikubwa wananchi wa kawaida ambao huzingirwa na ulitima. Wanaopalilia uharibifu na uchafuzi ni matajiri ilhali wanaoumia kutokana na athari zake hasi na hatari ni wananchi wa kawaida fukara. Mathalani, kiwanda cha Sagasaga kilitema moshi uliofuka kutoka kwenye ncha za mabomba yaliyochomoza juu ya majengo ya kiwanda.

Mwandishi Mbogo amesawiri mazingira chafu na dhoofu, aina zake na athari zake kimwavuli katika riwaya ya *Bustani*. Mathalani, anaeleza kuwa, siku moja asubuhi iliyokuwa na ukungu na manyunyu, Bwana Abdula alitoka kitandani na kuelekea bafuni. Ingawa mja hukoga na kuacha uchafu bafuni, Bwana Abdula kama aina ya anthroposenia alichangia anthroposenia pakubwa. Mathalani, yeye ndiye chanzo cha mkewe Zaituni kulazwa hospitali ya Aga Khan kutokana na vichomi vya kifuani. Kando na uharibifu wa hewa ulioendelezwa na kiwanda chake Bwana Abdula cha Sagasaga, yeye mwenyewe alikuwa anavuta paketi mbili za sigara kutwa. Watoto wake walikuwa wanapiga kelele kweli wakati mayaya walikuwa wanawatayarisha ili waende shuleni. Bwana Abdula alikuwa katunukiwa aina zingine tisa za anthroposenia – watoto wake. Mmoja wa wanawe – Lyakati – alitumia weledi wake wa shahada ya Sheria kuendeleza na kupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira,

hususani hewa kwa kukilinda na kukitetea kiwanda cha babake cha Sagasaga kisheria mara tu kiliposhitakiwa.

Aidha, katika mazingira chafu na dhoofu utandawazi unashamiri. Kwa mfano, baadhi ya watoto wa Bwana Abdula waliosomea Nomila International School ilhali Lata na Shaira wanasomea shahada zao Marekani. Mavazi ya Bwana Abdula yanafafanuliwa kusawiri jinsi anthroposenia inavyotunzwa badala ya kudhibitiwa katika mataifa mengi barani Afrika. Kwa mfano alivaa suti ya rangi ya bluu ya thamani kubwa, kiatu cheusi alichokinunua Roma, miwani yake ya mihimili ya dhahabu iligota juu ya pua lake na alikuwa na nywele nyeusi za singa zilizochungulia mbele juu ya panda la uso wake. Mwenyewe alikuwa ajenti wa uendelezaji wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Ndiposa mwandishi wa *Bustani* anaeleza kuwa, "Mtu aliyevuta paketi mbili za sigara kutwa, meno yake hayakuepuka mabadiliko ya rangi na kuwa ya kahawia." (uk. 41). Ikizingatiwa kwamba anthroposenia hutambulishwa na mabadiliko makubwa katika historia ya binadamu, Bwana Abdula ni wakala wa ukuzaji na uendelezaji wa anthroposenia. Hili linawiana na nguzo ya uongozi mbaya utandawazi.

Kimwavuli, mwandishi wa *Walenisi* amefanikiwa kumsawiri mwanaharakati na mwanaukombozi kupitia mhusika Dzombo. Anthroposenia huzalisha maonevu, chuki, ukiukaji wa haki msingi za binadamu na hatimaye maafa (Allen, 2011; Clark, 2015; Moore, 2015; Angus, 2016; na Gill, 2016). Haja na msukumo wa mtunzi Mkangi kumsawiri Dzombo kama mwanaharakati anayetawaliwa na hamu ya kuona usawa, uhuru na ukombozi unatokana na athari hasi za uongozi dhoofu katika kipindi cha uongozi na utawala alichoiandikia kazi yenyewe ya *Walenisi*. Hivyo, ingawa Mkangi aliandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* alipokuwa kizuizini (Wamitila, 1988; Chacha, 2003; Vonyoli, 2004; na Kwambai, Chai, Nabea na Bowen, 2018) na kwamba uandishi wa kazi hizi uliathiriwa pakubwa na tajriba yake ya miaka miwili kizuizini (Wamitila, 2003); ni dhahiri kuwa mazingira yale makali ya kisiasa nchini wakati ule pamoja na kule kudhibitiwa kwa uhuru wa kujieleza na kuukosoa uongozi na utawala kimwavuli, uliokuwa mamlakani, kulichangia katika usawiri wa anthroposenia kupitia mbinu ya taswira. Katika harakati za kukabiliana na anthroposenia zinazosawiriwa na mhusika Dzombo, inadhihirika kuwa historia ya Wachuna inasawiri historia ya binadamu pamoja na ukuuzaji na uendelezaji wa mfumo wa utawala dhoofu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa ujumla.

Katama Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* anasawiri anthroposenia kupitia taswira. Mathalani, anadhihirisha kuwa anthroposenia huzalisha ufukara wa kiwango cha juu zaidi kupitia wananchi ambao wanakosa nyumba za kuishi na badala yake huishi kando mwa barabara na majumba mijini. Kupitia mhusika Dzombo anaeleza kuwa, "Walizaana, kuishi na kufa barabarani. Hao, mbingu ndiyo iliyokuwa paa maishani mwao, na ardhi, godoro la fomu. Miili yao ilikuja kujua wororo wa mambo pale mchanga hafifu ulipotupiwa maiti zao wakizikwa." (uk. 176). Aidha, Katama Mkangi anasawiri watu ambao wanafaidi dhiki na mateso ya waduni kwa kila hali. Mathalani, anawasawiri Wachuna namna wanavyokuza udhalimu, ubaguzi na utawala dhalimu kwa jumla kupitia utawala wa kimabavu, maonevu na machukizo ilhali wanayafaidi kila uchao. Kwa mfano, wakati akina yahe wengine walikuwa na vazi moja tu la kila shughuli, huku wengine waliokosa cha kujifunika uchi wao wakiitwa wenda wazimu na wenye vichaa, Wachuna wana mavazi ya kila aina na kila shughuli.

Mwandishi Mkangi katika *Walenisi* anawasawiri Wachuna kama waliokuwa na mavazi aina aina, kama vile; magwanda, viatu, shanga, vipuli, manukato ya kila aina na hali, mikoba, na nguo za kupendeza kweli. Pia walikuwa na mavazi ya kazi na ya starehe; ya kulala na ya kuamkia; ya kutembelea na ya gumzo; ya safari na ya nyumbani; ya usiku na ya mchana; ya baridi na ya joto ya fukara na ya huzuni ya kuogelea na ya kuzikiwa; ya kuchezea na ya kukimbilia; ya kupikia na ya kulia; ya kutafuta mimba na ya kubebea mimba na mavazi mengine mengi. Hili linaashiria tofauti zinazopaliliwa na anthroposenia kati ya walalahai na walalahoi kwa minajili ya kuidumisha anthroposenia yenyewe. Hata hivyo, mtunzi Mkangi anasawiri athari inayowasawazisha tajiri na maskini. Athari hii ya uongozi na utawala dhoofu ni kifo. Kifo hakikuwabagua matajiri wala maskini. Watoto wa maskini wakifa kutokana na njaa, wa matajiri waliaga kutokana na ulafi. Maskini walipoaga kutokana na uchovu wa utumwa, matajiri walikufa kwa sababu za starehe za ulevi na ukahaba. Hivyo, kifo kikawasawazisha wote bila ubaguzi. Uongozi na utawala dhalimu hufaidi sio tu maangamizi ya wanadamu na wanyama ila ya viumbe vyote kwa jumla.

Mwandishi Mkangi kupitia kisa cha Metabu na Tabu wake pale Nokolani anasawiri maonevu, ubaguzi na dhiki kuu peupe. Medza baada ya kufika pale Nokolani huku akiwa amechoka na kujaa matapishi na kinyesi kwenye mbeleko mgongoni, anangonjea huduma kwa utulivu. Akiwa pale kwenye ubao, anawatazama waduni wengine waliokuwamo. Sakafu ilikuwa imejaa wagonjwa wengi ambao baadhi yao

walikuwa wamelala kwa maumivu. Wauguzi, madaktari na wasaidizi wote waliwazidishia wagonjwa hali ya kutamauka na maisha. Hii ni kwa sababu, wote walikosa nidhamu na moyo wa utu kimwavuli. Tabu anatapika hadi anakosa cha kutapika akiwa tu bado kwenye safu ya kungoja huduma na uchunguzi. Baada ya matapishi kumwisha, mwandishi anafafanua katika *Walenisi* kuwa, "Kilichokuwa kikimwandama kikawa ni fufutiko la kigegezi ambalo lilifanya mbavu zake changa kubenuka kwa uchungu mwingi uliozidishwa na kutokwa kwa nyute zikiwa na nyongo." (uk. 183). Hakika hili linadhihirisha namna ubaguzi, dhiki na mateso huwadunishia watu utu wao katika maeneo tofautitofauti ulimwenguni. Hili linafungamana na mhimili wa uwezo. Kwa upande mmoja tunasawiriwa madhara ya ubaguzi, machukizo na umaskini mkuu na wa pili tunasawiriwa namna matajiri na wenye mamlaka na nafasi kwenye jamii hujibarizi huku wengine wakiangamia.

Baada ya daktari kumpokea Tabu majira ya jioni, ngozi yake Tabu ilikuwa imebadilika na kuonekana kama ya kizee. Daktari kwanza anadhani kuwa ni kipindupindu lakini anaghairi na kuchunguza zaidi. Kwa sababu kingekuwa kipindupindu, tayari Tabu angekuwa ameaga dunia kabla ya jioni. Anamfinyafinya tumbo lake ndogo lililokuwa karibu kushikana na mgongo na kuhisi li tupu. Anatazama viganja vyake, anatazama ndani na chini ya mboni za macho yake na pia anakagua vijiguu vyake vikonde kuliko ngonda. Hapa ndipo inambainikia kuwa Tabu anaugua tengo ya kwashiokoo na marasimi. Maradhi ya Tabu yalisababishwa na ulaji wa tunguja – mwitu punde tu njaa ilipokosa kuvumilika tena. Kama kawaida ya dhiki, dhuluma na manyanyaso kukamilisha mchakato wao kwa maangamizi, Tabu anakufia mgongoni mwa mamake Medza. Baada ya kukosa nafasi ya kulazwa na Medza kukosa fedha za kumnunulia mwanawe dawa, daktari na muuguzi wanamkusanyia mwanawe kwenye matambara yanayovunda na kumpa. Mwandishi wa Walenisi anataja kuwa, "Akiwa njiani usiku huo akirudi nyumbani peke yake, alimsikia Tabu akikata roho mgongoni mwake." (uk. 185). Hali hii inasawiri namna wanyonge katika mataifa fukara ulimwenguni huupungia ulimwengu mkono kutokana na dhiki na dhuluma zinazowakumba katika mazingira mwao. Hili linawiana na nguzo za uwezo na uongozi mbaya.

Mwandishi anazidi kusawiri anthroposenia kupitia kidundu. Elimu ya hekima ya kidundu wanayoitumia Wachuna kuupalilia udhalimu na utawala wa kimabavu inaashiria utumwa wa kimawazo na kiutamaduni kwa jumla. Kwa mujibu wa Katama

Mkangi katika *Walenisi*, "Kidundu ni mdudu mdogo mweusi mfano wa mbung'o."(uk. 191). Mtunzi Mkangi anazidi kuisawiri anthroposenia kupitia kidundu anapofafanua kuwa, ni mdudu ambaye huweza kubeba matonge yanayomzidi mara tatu ya ukubwa wake. Hili linaashiria jinsi utawala wa kimabavu huweza kupuuzwa ulimwenguni hadi athari zake hasi zinaposhamiri na kupevuka na kuzalisha maafa yasiyoelezeka. Hili linawiana na kauli ya Angus (2016), Gill (2016), na Coughlin na Gephart (2020) kuwa, anthroposenia kwa ujumla isipotatuliwa kwa njia mwafaka na madhubuti inaweza kusababisha maangamizi kwa binadamu.

Kadhalika, kidundu kando na kuweza kuburura matonge makubwa makubwa ya mavi ya mbuzi, au ya kondoo, au hata ya ng'ombe, huweza pia kuyabingirisha kinyumenyume ili kuyakuza. Hili linaashiria hali ambapo anthroposenia inavyoendelea kukua katika mataifa tofautitofauti ulimwenguni, ndivyo inavyojizatiti kuathiri binadamu na mazingira yake. Huggan na Tiffin (2010) na Simon na Mark (2018) wakiyaunga mkono mawazo ya mtafiti wanataja kuwa, kadri binadamu anavyoendelea kujizatiti katika shughuli zake za kila siku bila kuyasikitikia mazingira yake ndivyo anavyoendelea kupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira yake kwa ujumla. Kadiri tonge linavyozidi kukua, ndivyo nacho kidundu huzidi kujizoazoa na kutia bidii zaidi za mchwa kulivingirisha nyuma aendako na ambako huwa hakuoni. Hili linaashiria hali ambapo uchafuzi na uharibifu wa mazingira unapoendelea kukua ulimwenguni ndivyo binadamu anavyozidi kudorora kiuchumi, kisiasa na kijamii huku akitapatapa katika giza la kujipalia makaa mwenyewe bila kufahamu.

Katama Mkangi katika riwaya yake ya *Mafuta* anasawiri maangamizi kupitia mbinu ya taswira. Anaeleza kuhusu pande la mtu linaloashiria maangamizi. Analisawiri kama linalometameta kama jongoo; lenye mashavu makubwa na ya kuvimba; lenye tumbo kubwa la kutondoroka na la kufura. Jitu hili limefura tumbo kama kwamba limebeba mimba nne. Hali hii inasababishwa na nguzo kuu ya maangamizi ambayo ni ulafi na ubinafsi-uchoyo. Anasisitiza kuwa kizingiti cha shingo lake kimepakata kichwa cha kusangika utosini kama uwanja wa ndege. Taswira anayosawiri mama Fofi pia inasawiri uhalisi wa hila, ubaguzi na dhuluma. Sifa, mumewe mama Fofi alizaliwa kwenye mazingira ya ulofa. Mavazi aliyoyavaa yalikuwa yametengenezwa kwa ngozi ya mbuzi. Nyumba yao ya nyasi haikuwa na dirisha hata moja. Mlango ulikuwa mmoja uliotumiwa na kila kitu kuingia na kutoka. Watu, mbu, moshi, kuku, inzi, uvundo, marashi, watoto, hewa na kila kitu kwa jumla, kiliingia na kutoka

kupitia mlango ule ule mmoja. Kazi za sulubu zinasawiri umaskini na uhitaji unaozalisha ubinafsi-uchoyo.

Kwa mfano, shughuli za kuchunga mbuzi na kondoo, kwenda shambani kama mkazi wa ndugu wadogo, kulima tumbo likiwa na njaa kamili, na kuhitimu kuwa wakulima halisi kama somo la lazima katika mazingira yaliyotawaliwa na ukame. Njeru, Kobia na Musyimi (2022: 184) wanafafanua kuwa, “Ukame ni hali ya hewa ya sehemu fulani inayofanya pakose maji ya kutosha kwa muda mrefu.” Hali hii huzalisha ukosefu wa chakula kwa viumbe hai vyote katika mfumo mzima wa ikolojia. Katika mazingira kama haya, wakulima ambao hutegemea maji ya kunyunyiza kama nguzo kuu na chanzo cha maji ya mimea, chemchemi za maji yale vikikauka kutokana na vurugu dhidi ya mazingira kama zao la ufukara na mabadiliko ya tabianchi, ukame hushamiri.

Kando na ukosefu wa maji kuhatarisha uhai wa mimea na wanyama humzalishia binadamu njaa, maradhi na hatimaye maafa (Riccardo, 2017). Njiru (2015), Simel (2015), Alia (2017), Gichure (2017), Magharibi (2017), Tan (2019), pamoja na Njeru na wengine (2022) wanaeleza kuwa, ukame huwa na madhara tele kama vile ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiafya na pia huzalisha athari hasi. Athari zinazozalishwa na ukame zinashabihiana na kunywea kwa mimea, ulofa, upungufu wa mlo, kudhoofika kwa maliasili kama vile udidimiaji wa maji, madini na misitu, na hatimaye ukame hudhoofisha shughuli za masomo na upataji elimu bora kwa jumla katika janibu zinazoathirika. Mtunzi Mkangi anathibitisha hili anapofafanua kuwa, madhara ya mabadiliko ya tabianchi kupitia ukame husababisha chumi dhoofu, hutinga elimu bora na hupalilia ulofa katika kila hali na nyanja zote za maisha.

Mtunzi Mkangi anaendelea kusawiri anthroposenia kupitia ubaguzi unaodhihirishwa na hali inayotawala kuzaliwa kwa Sifa tofauti na inayotawala kuzaliwa kwa Mama Fofi. Kupitia mama Fofi, mwandishi wa *Mafuta* anaeleza kuwa, Sifa alizaliwa katika mazingira ya ukame na ulofa tele ilhali mama Fofi alizaliwa katika mazingira ya shibe na utajiri. Ubaguzi ni mojawapo ya mazao ya anthroposenia. Watson na Watson (2007) wanataja kuwa, kando na ubaguzi wa kila aina kuwa msingi wa utumwa, huwa kisababishi kikuu cha mabadiliko ya tabianchi. Tofauti na Sifa aliyegonjeka na kukaribishwa duniani na njaa na dhiki kibao, mama Fofi alizaliwa godoroni la usufi na moshi wa uvumba na manukato ndiyo yaliyomlaki na kumkaribisha duniani.

Tofauti hizi huzalishwa na ubaguzi, ufisadi na ukosefu wa usawa katika utoaji huduma kwa umma katika mfumo wa uongozi na utawala dhalimu.

Ikizingatiwa kwamba matope yanasawiri maisha ya ulofa, dhiki, mateso, dhuluma na maonevu, taswira anayosawiri matope inasawiri umaskini wa kifedha na kimawazo barani Afrika. Kwa misingi hii hii, Matope anaashiria mataifa fukara barani Afrika kutokana na athari hasi za umaskini kama zao la uongozi mbaya. Mtunzi Mkangi anayasawiri matope namna yalivyokuwa yamemvaa na kumgubika Matope sawa tu na namna udhalimu huugubika ulimwengu bila kubagua. Mathalani, matope yamemtapakaa Matope mwilini, makavu na yaliyomkauka. Nywele zake zina muundo wa vilima vingi vidogo vidogo vya udongo mkavu, vilivyosawiri kichuguu kichwani mwake. Shingoni michirizi ya matope ilijisambaza huku kifuani matope yanamvaa kama fulana; tumboni yako kama ukumbuu; kiunoni, kibobwe, miguuni, mlongi na pia nyayoni yanamvaa kama ngozi ya pili au sapata anapotembea. Suruali ya Matope imebaki mararuraru ambayo inaonekana kusitiriwa na ukambaa unaomwingia matakoni na kujitokeza mbele kinenani. Kinenani napo pananing’inia kibambu cha nguo kinachomhifadhia heshima Matope. Matope anasawiriwa kama mpokezi wa athari hasi za anthroposenia ulimwenguni. Katama Mkangi katika *Mafuta* anasawiri hali duni inayozalishwa na mabadiliko ya tabianchi, utawala dhalimu na ubaguzi wa mazingira hususani katika mataifa yanayoendelea. Anadhihirisha hali hii anapoeleza kuwa:

> “… ulipofikia pipa-jaa tu, na kutupa macho ndani, mainzi yalijitupa nje kwa haraka sana huku yakikuachia nafasi … wewe u mheshimiwa! Kijiti mkononi na pakacha kulikwepa, utaanza kuchakurachakura kujitafutia vinono hata kwenye masaza! Hapo avingirishapo donge la sima, ama shondea la wali, au jiwe la mfupa, utakuwa makombamwiko purukushani mawindoni pia. Wakuonapo tu, nao pia hukupa nafasi kwa kwenda pembeni, mwa pipa-jaa kwa haraka sana kana kwamba wanakufanyia gwaride la heshima!” (uk. 37).

Hakika hili linaadhiria ubaguzi wa mazingira na wanyonge ulimwenguni. Pipa-jaa zinaashiria mataifa duni yanayotupwa taka na mataifa tajiri ya Ughaibuni. Waduni hula kwa macho tu huku wenye uwezo wakibarizi vinono, vipochopocho aina aina na hali bora ya maisha katika mazingira safi. Heshima inayodumishwa kati ya wadudu

na maskini inasawiri uhusiano uliopo kati wanyonge wenye mawazo mema na wale wenye umaskini wa kimawazo.

**5.4 Ishara**

Mpemba (2016), Yegon (2016), Mosha (2017), Waithiru (2019) na John (2022) wanafafanua kuwa, ishara huumbwa na msanii kupitia tamathali ambazo huwasilishwa kupitia mbinu tofautitofauti za kisanaa kama vile, jazanda, sitiari, tashihisi na nyingine nyingi. Waithiru (2019: 2 – 3) akimnukuu Madumula (2009) anasema kuwa, "neno ishara kama istilahi ya kifasihi, ni lile lililo sawa na kitenzi chenye maana ya 'tupia pamoja' na nomino yake huwa na maana ya 'alama', 'nembo' au 'dalili' au 'ishara'."

Watunzi Mbogo na Mkangi wamefanikiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya zao kupitia mbinu ya ishara. Mathalani, Mbogo ametumia ishara kusawiri anthroposenia katika riwaya ya *Bustani* kupitia mhusika Doricas na Mama Mohamed. Doricas pamoja na Zubeda wanafafanua kuhusu ishara ya kinyonga. Walipokuwa njiani wakielekea hospilini kumwona Eliya, Doricas alikuwa karibu kumkanyaga kinyonga aliyekuwa akikatisha njia. Ingawa Mama Mohamed aliruka pia, hakumaizi kilichosababisha mchupo ule. Walipogeuka na kumtazama kinyonga akienda kwa mwendo wa taratibu huku tayari akiwa amebadili rangi ya ngozi yake na kuichukua ile ya vitenge vya Doricas, Mama Mohamed alicheka, ilhali Doricas alifadhaika. Mfadhaiko wa Doricas ulitokana na mawazo yake yaliyokuwa mbali na kumfanya amdhanie kinyonga kuwa nyoka. Hili linaashiria kuwa, katika mazingira chafu na duni binadamu huwaogopa baadhi ya viumbe kama vile nyoka. Kiishara kinyonga ni ishara ya bahati nzuri.

Mama Mohamed anakiri katika *Bustani* kuwa, "Kinyonga, katika kabila letu, ni mnyama wa bahati." (uk. 12). Hata hivyo, tofauti na imani ya kabila la akina Mama Mohamed, kabila la kina Doricas wanashikilia msimamo kuwa kwao kinyonga ni ishara ya nuksi au bahati mbaya. Tofauti hizi za kiishara zinadhihirisha tofauti za imani zinazozunguka tamaduni tofautitofauti katika usawiri wa anthroposenia. Paa anayerejelewa na mwandishi wa *Bustani* ni mnyama wa porini mwenye muundo unaolingana na ule wa mbuzi. Kimsingi paa huashiria ishara mbalimbali. Baadhi ya ishara zinazoashiriwa na paa ni uwezo wa kuwaza kwa haraka na wepesi, uwezo wa kuchagua maneno ya busara, watu wenye moyo wa amani, watu wenye makini ya hali ya utu, watu wenye kupitisha mawasiliano kwa wepesi na pia watu wenye uwezo wa

kuona na kutambua hatari kwa haraka. Paa aliyemtokea Pasta Yona akiwa njiani kuelekea kwenye kilele cha mlima kunena na Mungu, aliashiria ujumbe maalumu. Ujumbe aliopitisha kwa Pasta Yona ni ule wa kutahadhirisha asije akakabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira yao. Uchafuzi na uharibifu wa mazingira unapigana vita kuhakikisha kuwa umenawiri. Uchafuzi na uharibifu huu umeashiriwa kupitia ishara zenye ushawishi na upole lakini pia zenye unafiki mwingi.

Kwa upande mmoja, punda huashiria unyenyekevu na huhusishwa sana na dini ya Kikristo katika Biblia. Kwa upande mwingine, punda huashiria unafiki, kwani, ingawa punda huwa ametulia akionekana, ukimkaribia kutoka nyuma, mashuzi huyarusha kweli. Zile rangi za pundamilia miguu sita pamoja na ubawa mkubwa upande wa kulia ziliashiria ishara zilizonuia kumkanganya na kumuogofya Pasta Yona ili asiweze kuendelea kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira lakini hakutetereka. Aidha, yule paa mwenye umbo la ajabu anaashiria mabadiliko ya tabianchi kama zao la mazingira chafu. Ndiposa mtunzi Mbogo katika *Bustani* anamsawiri kiishara na kukiri kuwa, “Alikuwa na rangi za pundamilia, miguu sita na ubawa mkubwa upande wa kulia. Mdomo wake mweupe ulidonoa chini, ukawa unakula punje za nafaka zilizofanana na kitabu kidogo cha rangi nyekundu.” (uk. 34). Miguu sita na ubawa mmoja ni ishara ya kutokamilika. Mdomo mweupe unaashiria amani lakini katika mfumo kamili wa unafiki. Hii ni kwa sababu, nafaka unazobugia, kutafuna na kumeza zinafanana na kitabu ambacho ni ishara ya vita dhidi ya anthroposenia na hivyo mdomo ule uliubusu unajisi wa mazingira na kuunawirisha badala ya kuukemea.

Kwa upande mwingine, Pasta Yona ni ishara ya wananchi wazalendo wanaopigana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kila uchao, kwa ujasiri na ukakamavu. Baada ya kuona yule ndege–mnyama, Pasta Yona alikohoa na yule kiumbe akashtuka na akaruka. Pasta Yona anapohisi kuwa mtu wake wa nje kafa na pahala pake roho ikatamalaki, mliibuka ishara mbalimbali. Ishara ya mtu inaashiria jamii; maiti inaashiria kuangamizwa kwa jamii na mabadiliko ya tabianchi; ilhali ufufuo unaashiria matumaini ya kushinda vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Kule kutoka kwa kichwa kwenye kaburini kuelekea duniani kunaashiria kuwa, ingawa uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaangamiza binadamu pole pole, itawadia siku na binadamu na mazingira yake atafufuka na pia mazingira yatafufuka kutoka kwenye mabadiliko ya tabianchi.

Kaburi ni ishara ya maangamizi na hatma yake dhidi ya ulimwengu. Shamba la Edeni linaashiria ulimwengu katika uchafuzi na uhabifu wa mazingira. Baba Adamu na Mama Hawa wanaashiria wanadamu na kwa jumla jamii katika mazingira yaliyonajisiwa. Maua yaliyorembesha joho refu la mama Hawa yanaashiria rasilimali asilia zitakazo ulimwenguni na ambazo zinaendelea kuharibiwa katika mazingira chafu. Bustani ya Edeni linasheheni ndege, mimea, maua na wanyama tofautitofauti. Bustani ya Edeni hivyo, laashiria dunia ilivyokuwa kabla ya kuchafuliwa na kuharibiwa na binadamu. Hili linawekwa bayana na Mama Hawa anaposhangaa katika *Bustani* na kuuliza kwa sauti iliyofurika simanzi kuwa: “Jana tu! Jana tu tulikwenda kulala na sasa leo? Siku ya pili kumekuwa hivi? Ama Mwenyezi Mungu katuhadaa?” (uk. 36). Mshangao na simanzi zinatokana na kutoamini baina ya Mama Hawa na Baba Adamu, mabadiliko yaliyozalishwa na tabianchi. Mabadiliko yenyewe yalichukua muda mchache mno kwa sababu binadamu naye amekuwa akipalilia mabadiliko ya tabianchi kwa bidii za mchwa. Mama Hawa anaashiria binadamu wanaokataa tamaa ya maisha kutokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira, na kwa sababu wengi hawataki kuwajibika, wanalaumu hadi muumba wao.

Ingawa Baba Adamu anamkaripia mkewe na kughadhabishwa na swali lake anafadhaishwa pia na mabadiliko makuu na makubwa ya bustani yao ya Edeni kutokana na anthroposenia. Ikizingatiwa kwamba bustani ya Edeni inaashiria ulimwengu, ni dhahiri kuwa mabadiliko yanayozalishwa na tabianchi ulimwenguni yana uwezo wa kumfanya mwanadamu akate tamaa maishani. Ndiposa anamtazama mkewe kwa masikitiko mengi. Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha mabadiliko makubwa ulimwenguni. Mathalani, mtunzi Mbogo anapambanua katika *Bustani* kuwa:

> “Wote wawili wanaikumbuka ile mito ya Havala iliyotiririka ikiyakumba mawe ya dhahabu kuelekea baharini. Wote wanaukumbuka Mto Gihoni uliosafiri ukichukua tope na udongo wenye rutuba, ukafurika majira ya masika, ukamwaga mbolea kandokando ya mabonde ya Edeni, mabonde yaliyootesha mimea ya matunda, miti, maua na vyakula vilivyoshibisha macho na hisia za binadamu.” (uk. 36).

Kumbukumbu za Baba Adamu na Mama Hawa zinaashiria mabadiliko makubwa ambayo yamefanyika katika ulimwengu wa sasa kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Kabla ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira, ulimwengu uliweza kuotesha mimea ya matunda, miti, maua na vyakula chungu nzima. Vyakula hivyo vilimfaa binadamu vikamshibisha na kumtosheleza. Ingawa mito ilifurika kabla ya mabadiliko ya tabianchi, haikusababisha maafa, ila ilimwaga mbolea kandokando ya mabonde mbalimbali abamo binadamu alilima ulimwenguni. Aidha, udongo wenye rutuba na tope ulikuwa asilia bila kemikali na kuchangia pakubwa uzalishaji wa mimea na vyakula tele. Ikizingatiwa kwamba anthroposenia ni kipindi cha historia ya binadamu kinachotawaliwa na mahitaji ya binadamu yanayoendelea kuzalisha mabadiliko makubwa; mabadiliko makubwa katika bustani ya Edeni yanaashiria uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla. Baba Adamu alipomtazama mkewe kwa masikitiko, alielewa fika kuwa, kama yeye mwenyewe, mkewe alikuwa na sababu tosha za kufadhaishwa na mabadiliko yale makubwa ya bustani yao ya Edeni.

Baadhi ya mabadiliko yaliyodhihirika hadharani ni kutoweka kwa mito ya Havala iliyowahi kutiririka huku ikiyakumba mawe ya dhahabu kuelekea baharini na pia kutoweka kwa Mto Gihoni uliokuwa unasafirisha tope na udongo wenye rutuba huku ukiwa umefurika majira ya masika na halafu kumwaga mbolea kandokando ya mabonde ya Edeni. Mabonde yale yaliotesha mimea ya matunda, miti, maua na vyakula vilivyoshibisha sio tu tumbo za binadamu ila pia macho na hisia zao. Kadhalika, Mto Hedekeli ulikauka, mto uliokuwa ukitembea kwa madaha, huku ukiinyonga kiuno chake kizuri na ukapita mbele ya Ashuru. Baba Adamu anakiri kuwa waliupenda sana kutokana na mambo kama; fuko na pwani zake zilizotandikiwa mchanga wa fedha, nyasi kijani kibichi, maua ya kila rangi yaliyowakumbatia Baba Adamu na Mama Hawa kwa uturi na manukato yasiyo kifani. Baba Adamu anakiri katika *Bustani* kuwa, “Bustani ya Edeni haikuwapo tena. Uzuri wa ardhi haupo tena. Maua, mito na maziwa ya maji safi tuliyozawadiwa havipo tena. Mazingira yote yamebadilika.” (uk. 37). Aidha, kulingana na Baba Adamu na Mama Hawa, walikuwa wanajitandaza juu ya mchanga ule wa fedha nyakati za jioni huku wamekumbatiana pamoja. Hili linaashiria kuwa uharibifu wa mazingira unasababisha utengano badala ya utangamano.

Zaidi ya hayo, ndege wa kila rangi walioruka juu ya vichwa vya akina Baba Adamu huku wengine wakidiriki kutua juu ya vichwa na mabegani mwao waliadimika baada ya uharibifu wa mazingira. Wadudu, kama vile, vipepeo, panzi, nyuki na wengine waliokuwa wakihanikiza ndani na nje ya Bustani walikosekana kabisa. Maanguko

makuu yaliyosababisha mungurumo mkubwa pia yalifikia kikomo baada ya Mto Frati uliowahi kukimbia kasi huku ukivuka milima na kuiparamia milima ya mawe kukauka. Haya ni baadhi ya mabadiliko makubwa yanayoashiria uharibifu wa mazingira duniani.

Pasta Yona alipokuwa kanisani kwenye madhabahu alishtuka ghafla baada ya kuiona ishara ya ajabu ikielea juu ya vichwa vya waumini. Ingawa ni yeye pekee aliyeweza kuyaona maono yale, alisimama, akatazama pale hewani. Alistaajabu kumwona mwanamke aliyevikwa jua, ilhali mwezi ulikuwa chini ya miguu yake. Mwanamke aliyekuwa anaonekana na Pasta Yona pekee mle kanisani ndani ni ishara ya ulimwengu. Nayar (2010) anasisitiza kuwa, kati ya karne ya kumi na nane na ile ya kumi na tisa, maendeleo endelevu yalifungamanishwa na mazingira katika misingi ya ukoloni na ubepari. Ingawa yote miwili ilichanganua ulimwengu kama kifaa cha kutumiwa na binadamu ilihusisha ishara na taashira za uumbaji wa viumbe, maumbile na diskosi moja kwa moja na ulimwengu kama mwanamke.

Sababu kuu ya kumrejelea mwanamke kama ulimwengu ni kwa sababu ulimwengu kama mwanamke humpatia binadamu uhai pamoja na mimea na wanyama wote kwa jumla. Hivyo, ishara ya mwanamke aliyevikwa jua na mwezi ukiwa chini ya miguu yake ni ishara ya sayari. Mwanamke yule alikuwa na taji na nyota kumi na mbili juu ya kichwa chake. Taji hili linaashiria maumbile yanayouzingira ulimwengu. Mwanamke yule alikuwa na mimba lakini alikuwa anatiririkwa na machozi yaliyotokana na uchungu na maumivu yaliyosababishwa na kuzaa kwake. Uchungu na maumivu ya kuzaa yalimliza machozi kweli. Hata hivyo, alipokuwa anazaa, mlitokea joka kubwa jekundu. Ikumbukwe kwamba, ingawa kuzaa humsababishia kiumbe anayezaa maumivu na uchungu halafu humsababishia furaha mzazi. Kitendo cha kuzaa ni ishara ya ulimwengu kupata ukombozi, mwanzo mpya na nguvu mpya baada ya kupigana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mtoto anayezaliwa wa kiume ni ishara ya shujaa wa kukabiliana na maangamizi. Joka kubwa jekundu ni ishara ya maangamizi. Joka lile lilikuwa na vichwa saba na pembe kumi na juu ya vichwa vyake vilemba saba. Ikizingatiwa kwamba nambari saba ni ishara ya ukamilifu, vichwa saba vinaashiria ukomavu wa maangamizi ambayo mihimili yake ni pembe kumi. Rangi nyekundu nayo ni ishara ya hatari, inayoashiria hatari inayozalishwa na maangamizi ulimwenguni kutokana na athari zake hasi. Mkia

wa joka lile ulikuwa unakokota theluthi ya nyota za mbinguni huku ukiziangusha ulimwenguni. Theluthi ya nyota za mbinguni ni ishara ya athari hasi za maafa dhidi ya mbingu. Zile nyota zina moto unaochoma ulimwengu na moto huzalisha maangamizi mengi na makubwa. Hivyo, kuziangusha nyota zile nchini ni ishara ya maangamizi yanayotokana na anthroposenia ulimwenguni. Nyoka yule alisimama mbele ya yule mwanamke katika *Bustani*, aliyekuwa tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake.

Hii ni ishara ya jinsi uchafuzi na uharibifu wa mazingira hutafuna ulimwengu na vilivyomo, viwe hai au visiwe hai. Hili linathibitishwa na nyoka ambaye baada ya mwanamke kumzaa mtoto wa kiume, anamla. Kitendo hiki ni ishara ya namna mabadiliko ya tabianchi hutafuna binadamu kupitia maradhi kama ya saratani, hutafuna mazingira kupitia kemikali na gesi na maangamizi yote kwa jumla dhidi ya ulimwengu. Hata hivyo, mna matumaini kuwa binadamu anaweza kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira hata kama athari zake zitaishi kwa muda mrefu. Hili linaashiriwa na kuyeyuka kwa ishara ile ya joka jekundu juu ya vichwa vya waumini. Kadhalika, ishara ile inampa Pasta Yona tahadhari dhidi ya kuzungumza tena mbele ya makachero wa serikali na Abdula ambao ni ishara za wanajeshi wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira wanaoilinda na kuitunza kwa manufaa yao binafsi bila kuwajali wananchi wenzao.

Neno analosoma Pasta Yona baada ya kutoka hospitalini alikokuwa amempeleka mke wake akajifungue mtoto linaashiria changamoto zilizokuwa zimemkondolea macho Pasta Yona. Ndiposa Wakili Mwaka anafika pale uwanjani mapema na kuinua bango lililoandikwa: "ABDULA MUUAJI WA WATOTO WETU." (uk. 87). Pasta Yona ni ishara ya wanajeshi wanaokabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kila njia. Hivyo, wanaopalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira wanamchukulia kama adui wao mkuu. Hii ndiyo sababu, polisi wengi wakiwa na silaha wanalizunguka eneo lote la Sagasaga. Hii inaashiria namna serikali ya Siza inavyojitolea kuyalinda maangamizi.

Nyimbo anazozisikiliza Dzombo katika *Walenisi* zinaashiria ubaguzi, maonevu na manyanyaso. Akiwa ndani ya *Sayari* anafinya kizibo kinachosema 'muziki' na punde tu wimbo wa *Matatizo Tumeyazoea* unapasua hewa. Dzombo anathibitisha kuwa, dhiki, mateso na dhuluma kwa jumla si masuala ambayo binadamu anaweza kuzoea

na badala yake anafaa kuyatatua. Mathalani, anaeleza katika *Walenisi* kuwa, "Hakutaka kuusikiliza mpaka mwisho kwa kuwa matatizo hayazoeleki! Matatizo ni yatatuliwe wala si yazoeleke!" (uk. 22). Hivyo, anausitisha na kufinya tena kizibo cha muziki na punde wibo wa *Mambo bado* unavurumishwa. Angaa huu unampa taswira halisi kuwa manyanyaso ya kimazingira bado yako hai na makali. Miamba ya kasumba iliyomo ndani mwa Jabali la Magonjwa ni ishara ya maangamizi. Kadhalika, nondo anaashiria binadamu huku mdudu chotara akiashiria zao la athari hasi za maafa. Miamba ya kasumba inamvutia Dzombo kwa lengo la kumuumiza jinsi nondo huvutiwa na mwangaza kisha hatimaye huchomeka mbawa na kuwa mdudu chotara. Miamba ya kasumba inawaka mataa ndani ya giza la lile Jabali. Jambo hili linamvutia mithili ya nondo na taa uwakao. Ingawa Dzombo anajaribu kujizuia kutazama mataa yale, mataa yenyewe yalikuwa yanajigeuza rangi mara kwa mara na kutoa umbo la visiki vya namna namna vya kuvutia na hivyo kumtia kwenye jaribio. Hili linaashiria majaribio ambayo huwatosa watu katika bahari la maangamizi kutokana na kutojua.

Hili linaashiria kuwa, binadamu hujitosa katika kasumba za uongozi mbaya, ubepari, vurugu dhidi ya mazingira na kasumba zingine tele kutokana na kutofahamu ukweli wa mambo. Mathalani, Dzombo anafafanua kuwa nduli ziletwazo na miamba ya kasumba huwa na ishara tofautitofauti na za kujificha zisije zikabainika. Ishara hizi hupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa. Hujifisha kwa kupendeza ingawa huwa vinaficha vidudu vikali vya mauti. Hivyo, kufichua uchafuzi na uharibifu si jambo rahisi kwani zile rangi za kuvutia za visiki vina uwezo wa kunasa yeyote yule. Kwa mfano, mna ishara ya kifafa cha kutojijua ambayo humpa mtu hali ya kujitusi bila yeye mwenyewe kujifahamu kuwa anajitusi. Maradhi haya hutatiza kweli, madhali mgonjwa huyachukulia kuwa yenyewe ni dawa kwake. Hili linadhihirisha kiwango ambacho upofu dhidi ukweli huweza kujikamafleji ili tu ushamiri ulimwenguni. Kwa mfano, mja anapodhani kuwa hana dini, hujisota kwenye dini ya mwingine akitafuta suluhu na pale hujipumbaza zaidi. Katika mataifa mengi barani Afrika, dini imekuwa ikitumika kama dawa ya kulevya ambapo wanyonge wengi hufukia dhiki zao na kuzisahau huku wakitumainia kuwa zitatuliwa na nguvu za kiajabu au za kimazingaombwe za waganga. Hali hii huwafanya watu kutobuni wala kuzindua kwa kuimarisha fantasia na utegemezi kutokana na imani zinazotwaza uvivu na kutweza ukakamavu, ushupavu, uhalisia na uasilia katika ubunifu. Hili linawiana na nguzo ya utamaduni na mazingira.

Uvivu, utegemezi na utumwa wa kuomba na kutegemea misaada na mikopo hubatizwa na kupata jina jipya, katika pensili ya imani mpya na hata kufanywa mlaji wa nyama na mnywaji wa damu ya binadamu. Haya yote humpelekea kuzorota zaidi kwa kifafa, kumpooza ubongo wake na athari zingine nyingi hasi ilhali moyo wake u bado unapiga. Hivyo, maangamizi hujidhihirisha kwa kukamafleji kupitia njia tofautitofauti kwa lengo la kumuumiza binadamu. Ingawa hali ya kutojitambua hugeuzwa kuwa ya kawaida, kifafa kinapochukuliwa kumaanisha hali halisi, ukweli ni kwamba hili hutokana na upofushaji wa ubepari kwa binadamu. Kwa mfano, mwandishi anathibitisha hili anapofafanua katika *Walenisi* kuwa, kifafa humpoteza fahamu razini mja na akaanza kudai kuwa na pesa kwa mfano, ilhali mbinu za pesa zenyewe hazijui ziliko. Hii ni kwa sababu, katika utando wa utumwa wa kimawazo, kiuchumi, kijamii na kisiasa, binadamu kifedha huagizwa kile atapanda, nini atanunua na nini asinunue na hatimaye, hulipwa. Huu ni utumwa wa kiuchumi unaoashiria ukoloni mamboleo kadamnasi katika mataifa mengi barani Afrika.

Katika utumwa huu, kuagizwa huwa hakuishi ilhali utampata mtumwa yule akizidi kujinaki kuwa pesa bado ni zake tu. Kifafa, kuomba na majipu ni ishara ya anthroposenia. Pia mabendiji ya matibabu ya misaada, pamoja na kijiti cha kumwongoza mgonjwa ni ishara ya anthroposenia. Mwandishi wa *Walenisi* anaeleza kuwa, kifafa husababisha majeraha ya kuomba kusikoisha kwa lengo la mgonjwa kujitibu maradhi yake. Katika ukoloni mamboleo, anthroposenia hushamiri kupitia mikopo na msaada katika nchi za Afrika inayokopwa na kuombwa na viongozi wa Afrika kutoka mataifa tajiri ya ughaibuni. Lengo kuu huwa kukabiliana na athari hasi za anthroposenia kama vile ulofa, maradhi na madeni lakini matokeo huwa kinyume. Uombaji huu huwasababishia wananchi majipu ya kuombaomba kutokana na utumwa unaotokana na uombaji wenyewe. Utumwa huu hutokana na masharti, riba ya juu na muda mrefu unaowekwa wa kuyalipia madeni ya mikopo yanayotolewa na mataifa tajiri ya Uropa, Marekani, Mashirika ya Kimataifa, na mengine mengi. Kule kupachikwapachikwa mabendiji ya matibabu ya misaada kunaashiria ulemavu wa kiuchumi barani Afrika kutokana na mikopo yenye riba ya juu zaidi.

Mabendiji yanakazwa machoni na kuachiwa mdomo kwa sababu, ingawa Mwafrika hupofushwa huwa huru kuzungumza apendavyo. Njia moja madhubuti ya kunena dhidi ya mabendiji ya vidonda na majeraha ya mazingira ya binadamu ni kupitia fasihi. Mtunzi Mkangi anatashtiti ukoloni mamboleo katika *Walenisi* kiishara katika

kupalilia uchafuzi na uharibifu kwa ujumla anapotaja kuwa, wakati wote ule, Mwafrika katika utumwa wa mazingira chafu na tasa husema kuwa, “Mimi niko huru. Mimi niko huru. Mimi niko huruuu,” kama sahani ya santuri iliyokwama, …” (uk. 27). Jinsi uchafuzi, uharibifu na dhuluma zinavyozidi kushamiri, mtu huendelea kupotoka. Mtunzi Mkangi anatoa ishara ya uchafuzi na uharibifu kimwavuli kama binadamu mwenyewe, hasa Mwafrika. Anaeleza kuwa, kadri ishara ya kifafa cha kutojijua inavyozalisha matatizo pamoja na dalili za kisonono cha kuiga ndivyo binadamu huendelea kutojithamini yeye mwenyewe pamoja na jamii yake kwa jumla. Uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa jumla humpofusha na kumlemaza binadamu kimawazo, kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Aidha, binadamu hukosa thamana ya jina lake, utamaduni wake, ustaarabu wake, na kila kitu hukikosea thamana. Hii inadhihirisha namna Mwafrika katika nchi za Afrika huabudu utamaduni na kila kitu cha Mzungu kutokana na elimu dhoofu; mifumo dhoofu ya uongozi na utawala; imani na desturi potofu za kulema; yote aliyoyarithi kutoka kwa mkoloni, na kupelekea kujidharau yeye pamoja na utamaduni na jamii yake. Jambo hili huwapelekea Waafrika kukosa ujitambuzi hivyo utamaduni wao hunajisika. Huu ni uchafuzi wa mazingira ya utamaduni. Hili linawiana na kauli ya akina Morton (2015), Davis na Heather (2015), Frantzen na Bjering (2020) Slovic na wenzake (2020) na Filipova (2023) kuwa, uchafuzi wa mazingira huchangiwa pakubwa na tamaa, ubinafsi-uchoyo na ufisadi wa binadamu. Mwafrika hupofushwa na haja ya maendeleo endelevu, kiwango kwamba, yeyote ambaye hujaribu kumkosoa au kumzindua huwa mzushi, mchawi na asiyetosheka na majina kadhaa ya matusi humiminiwa yeye, pindi tu anapojaribu kumkosoa mgonjwa huyu wa kujiangamiza mwenyewe. Hii ni kwa sababu, maangamizi kupitia ukoloni mamboleo humfanya Mwafrika kinyago tu kwa kumfanya aige yale maovu pekee kwa kutokuwa na uwezo wa kuchuja mema kutoka kwa mabaya. Lugha ni ishara ni mojawapo ya njia ambazo unajisi wa kimazingira kwa jumla hutumia kujipenyeza barani Afrika. Hali hii inafungamana na nguzo ya maendeleo endelevu.

Katama Mkangi katika *Walenisi* anataja kuwa ndwele ya lugha imkumbapo Mwafrika, humfanya akose kukumbuka lugha yake ya kwanza. Anasisitiza kuwa, “Utamwona akitapatapa kujitafutia hewa ya kuweza kujieleza kinaganaga kwa kutumia lugha hii ya mtawala wake!” (uk. 28). Dzombo alishangaa alipoikuta miamba ya kasumba ndani ya ukungu wa Jabali la Magonjwa. Sababu kuu ikiwa, aliyeshikwa

na kisonono cha kuiga kwa kukosa ulimi wa kuzaliwa nao, aliyaeneza na kuwaambukiza watoto wake na hivyo kurithisha njia za kupanda na kupalilia utumwa wa kila aina. Jambo hili lilifanya tukio lenyewe kukomaa kuwa dalili na kuwa bato la kizalia. Bato hili ni ishara ya maangamizi ya mazingira na uhai wa binadamu. Hili huyafanya maafa kuenea katika nchi za Afrika na kuwa sehemu ya ustaarabu wa Mwafrika. Ulofa, dhiki na mauti huwavutia wengi kwa sababu ya haja ya kuwanyonya na kuwatumia tu bila kujali matokeo. Ndiposa yale mataa katika *Walenisi* yalijigeuza rangi muda baada ya muda mithili ya kinyonga kushiria namna maafa hujibadili namna ya maangamizi ingawa hatima huwa moja - kifo. Hili linawiana na nguzo ya kifo.

Makero ya dhuluma yanayofuatwa na mayowe ya wanaodhulumiwa katika Jabali la Udhalimu yanaashiria maafa. Giza tupu lililopo ndani ya Jabali hili ni ishara ya umaskini na mauti. Hili linaashiria kuwa, umaskini na mauti huwapofusha wananchi kutokana na dhuluma wanazokumbana nazo maishani. Kwa mfano, Dzombo anashinikizwa afe na ishara ya mauti lakini anakataa, pale anapojibu katika *Walenisi* kuwa, "Kufa! Mwanaharamu wee!" "Sifi, ng'o!"" (uk. 32). Magereza ni ishara ya utumwa wa kimawazo na utu kwa jumla, hasa katika mataifa fukara ya Afrika. Kallman na Dini (2017) wanaeleza kuwa, 'gereza' ni ishara inayotumiwa na watawala, hata wa kiutandawazi kama namna kuu ya kuwadhibiti wananchi na kuwaogofya pamoja na kuwaweka katika hali ya kuchunguzwa kwa kila namna. Lengo kuu huwa kuulinda na kuutunza utumwa. Wachuna katika Walenisi wanajenga na kuimarisha magereza kwa kusudi la kuimarisha mauti. Ufunguo anaotumia Dkt Matoga katika *Vipuli* kati ya kitita kikubwa cha mafunguo unaashiria maafa yanapotangulizwa na kukaribishwa katika mataifa duni na viongozi wa mataifa husika wenyewe. Anawajuza Nyau, Shipe na Kipanga kuwa, baada ya wao kuleta maiti za kuzoa vipuli vya figo na mioyo, wanapitisha gari kupitia lango lile analofungua ili kuzipakua na kuzipasua maiti. Kabla ya mauti kuuangamiza uhai wa binadamu huuangamiza utu wake kikamilifu. Hali hii inafungamana na nguzo za haki na maadili ya mazingira na kifo.

**5.5 Majazi**

Mtunzi Mbogo katika *Bustani* ametumia majazi kupitisha ujumbe wake kwa kuisawiri anthroposenia. Majazi ni hali ya kumpa mtu, mahali au hali au jina kulingana na maumbile au sifa fulani. Mathalani, kiwanda cha *Sagasaga Chemical Industry* kina

jina la kimajazi. Ikizingatiwa kwamba kiwanda hiki kinaashiria maangamizi kwa kuyapalilia, kuyaimarisha na kuyaendeleza, jina lake linathibitisha sifa na maumbile yake, sio tu kwa wafanyakazi ila pia kwa jamii na mazingira yanayokizingira. Jina hili linahusisha maneno kama saga saga, ambayo hurejelea hali ya kupondaponda nafaka au mhogo kwa kutumia aidha jiwe au mashine na kuifanya ungaunga. Kadhalika, ni kusababisha kitu kiishe polepole kwa kusuguana na kitu kingine (TUKI, 2006; Mdee na wengine, 2015; BAKITA, 2015; Wamitila, 2022).

Kutokana na kile kiwanda, wakaaji wa eneo la Siza wanapondwapondwa kiafya kupitia maradhi mbalimbali. Hii inachangiwa pakubwa na ukiukaji wa sheria na masharti ya Shirika la Afya Duniani kuhusu namna ya viwanda ya kuwalinda wafanyakazi, wenyeji na mazingira kilichomo kwa jumla. Mathalani, Eliya alikuwa na kikohozi kisichokwisha na ugonjwa wa kuwashwa na ngozi ulimwandama pia bila kikomo. Zubeda kwa upande mwingine anakohoa bila kikomo. Yusuf mumewe Zubeda, naye ana vipele kichwani ambavyo amejaribu kupaka dawa aina aina bila kupata nafuu. Hili linadhihirisha kuwa unajisi wa mazingira huzalisha maradhi mengi tofauti yasiyo na tiba. Kupitia kiwanda cha kemikali cha Sagasaga, Yusuf kama mfanyakazi anapondwapondwa kiafya na kiuchumi. Kiafya anapata ndwele tofauti zisizotibika kutokana na athari za dawa wanazotengeneza na kupakia bila vifaa vya kujikinga, ilhali kiuchumi anafanyishwa kazi ya sulubu kwa malipo duni. Mwandishi anadhihirisha ukweli huu katika *Bustani* kupitia mhusika Yusuf anapoeleza Doricas kuwa:

> "... Aaa! Siku hizi maradhi hapa Siza hayana mmoja. Unamwona mwenzako huyo ... kukohoa hakumwishi. Mimi nitazame ... Nitazame shemeji. Kitazame kichwa changu. Vipele hivi sijui vinatoka wapi? Nimepaka kila dawa, wapi! Maradhi ni mengi." (uk. 4).

Hali hii inasawiri uhalisia ulio katika mataifa mengi ulimwenguni ambapo wananchi hukesha kwenye zahanati na hospitali tofautitofauti wakitafuta matibabu kutokana na kuugua ndwele aina aina. Ndwele hizi ambazo huwakumba wananchi kila uchao huwa zao la mazingira chafu na yaliyoharibiwa na binadamu hususani matajiri, katika shughuli zake za kujiendeleza kiuchumi, kisiasa na kijamii za kila siku. Hali hii inafungamana na nguzo ya maendeleo endelevu ambapo binadamu huyapujua mazingira katika harakati zake za kujiendeleza kiuchumi. Hili linawiana na kauli ya

Garrard (2023) kuwa, binadamu huishia kuyadidimiza maendeleo ya uhifadhi wa mazingira katika harakati zake za kuyaimarisha maendeleo endelevu mintarafu ya malengo ya kitaifa, kimataifa na milenia na hatimaye hujiangamiza mwenyewe.

Eliya anadhihirisha kuwa mabadiliko makubwa ya tabianchi huchangiwa pakubwa na binadamu kama aina ya anthroposenia. Binadamu katika harakati za kutekeleza shughuli zake za kila siku, huimarisha mabadiliko makuu ya tabianchi. Kiwanda cha *Saga Saga Chemical Industry* kimesababisha maradhi mengi ya kiajabu kwa wenyeji wa Siza. Maradhi haya mengi yamekuwa donda ndugu kwa wakaaji kwani hamna dawa inayotibu mengi ya maradhi haya. Jina lake Ntanaeli linageuzwa mintarafu ya sifa na uraibu wake wa kuchapa mtindi na kulivuta ganja au bangi. Pombe na bangi ni baadhi ya bidhaa zinazopalilia maafa kupitia udhibiti wa mawazo ya binadamu. Hivyo, jina lake jipya la ukepteni linashika kani na kuashiria utawala dhalimu huku lile la Natanaeli likikufa. Hili linaashiria uwezo wa dhuluma na utwala dhalimu kuangamiza lugha katika jamii kutokana na athari zake hasi. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo.

Wenyeji wa Siza waliurejelea ugonjwa wa kujikuna kama ugonjwa wa Franco. Ugonjwa huu ulipata jina hili kutokana na jinsi mtu alivyokuwa akijikuna mwilini kama anayeimba na kucheza muziki. Jina Franco huhusishwa na mwanamuziki maarufu kutoka taifa la Congo. Wamitila (2003: 106) anaeleza dhana ya majazi kuwa: "Ni mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi au yanatuelekeza kwenye wasifu wa tabia zao. Jina la mhusika linakuwa kielelezo cha tabia yake." Katika riwaya ya *Walenisi*, mtunzi Mkangi ametumia jina la mhusika – Maskini Jeuri – kusawiri umaskini, dhuluma na madhara ya utawala dhoofu. Maskini Jeuri anapompa Dzombo chang'aa, ananuia waweze kuinywa ila si kutia kwenye kibatali kama mafuta ya taa. Hivyo, ananyamaza anapomuona Dzombo akiitia kwenye kibatali na kuakisha utambi kwa kutumia mshale wa kiberiti uliokuwa unawaka. Mawazoni mwake anadhani kuwa Dzombo anatafiti ili akina yahe kama yeye na wengine wanufaike na wapungie mkono matatizo yasiyoisha ya ukosefu wa mafuta ya taa. Maskini Jeuri anapalilia umaskini na utabaka bila hiari yake, ila kutokana na ukosefu wa namna. Kutokana na utabaka unaotenganisha walalahai na walalahoi kama bingu na ardhi, maonevu na maafa yanapaliliwa.

Maskini Jeuri anamsisitizia Dzombo katika *Walenisi* kuwa, taa kwa walalahoi kama wao ni ulevi. Hili linachangia maafa kwa sababu ulevi huendeleza ulofa ambao huendeleza maangamizi. Hii ndiyo sababu alidhani Dzombo alielewa kuwa, alipomwambia kuwa wakaiwashe, kwamba Dzombo alielewa kuwa alimaanisha wakaiwashe taa ya rohoni mwao, yaani ya mwao akilini kupitia unywaji wa chang'aa. Maskini Jeuri anasisitiza katika *Walenisi* kuwa, "… kwetu sisi watu duni, ulevi ndio taa yetu. Ukishawaka chang'aa ama busaa, au waragi, hata na pia chibuku, ama piwa au … muratina ama kwa tembo la mnazi, mtu haachi kuona mwangaza mpya maishani mwake." (uk. 74). Kutokana na ufukara, wananchi wengi katika mataifa ya Afrika hujifukia lepe la kujisahaulisha dhiki na matatizo wanayokumbana nayo. Lepe hili husababishwa na uraibu wa dawa za kulevya, pombe haramu, michezo ya kamari, elimu ya kupofusha, ukame na maradhi chungu nzima. Haya yote hufanikishwa na viongozi wa mataifa tajiri ya Ughaibuni ambao huyanyonya, huyanajisi na huyahanithisha mazingira ya Afrika ili yawe tasa na yasiweze kuyatosheleza mahitaji ya Waafrika. Hili linawiana na nguzo ya uwezo na kifo.

Jina moto limetumiwa kimajazi kuashiria anthroposenia. Moto ndiye aliyeuvumbua moto kwa kutumia vijiti viwili. Kimajazi, moto huashiria mabadiliko, hususani katika mazingira kwa namna mbalimbali. Ingawa moto huwa sehemu ya maumbile, huchangia pakubwa katika uumbaji na uumbuji wa ikolojia kwa kuhudumu kama wakala wa mabadiliko (Saha, 2019). Kadhalika, moto huweza kuwa hatari kwa kuharibu vifaa, kuunguza porini, kuchoma mimea na kuchafua hewa kwa kutoa moshi ambao huwa na athari hasi kwa binadamu. Hivyo, moto huingiliana na kuathiriana na viumbe hai na visivyo hai, mazingira vilivyomo na ikolojia kwa jumla katika mfumo mpana wa ikolojia. Hii ni kwa sababu, moto ni mwako wa kitu kinachoungua (TUKI, 2014).

Moto anathibitisha kuwa jina lake ni la kimajazi anapovumbua moto na kuuwasha kwake nyumbani. Hili linaashiria juhudi za binadamu za kuvumbua, kuzalisha na kuendeleza maangamizi. Mathalani, wanakijiji wanaposimama karibu na moto unaowaka, Moto anawaambia katika *Walenisi* kuwa, "Mimi ndimi Mootoo …; naivisha na kuunguza. Nateketeza na naoteka. Anitakaye nitakuja kwake na nimpe uwezo huu wangu …" (uk. 157). Maangamizi huogofya, madhali Moto anapoupulizia moto, unaalika kwa moshi na cheche nyingi zinazowafanya wanakijiji wenzake warudi nyuma kinyumenyume kwa woga. Moto anawalaghai wenzake badala ya

kuwajuza ukweli kuhusu chimbuko la maangamizi yale yaliyojidhihirisha kwao machoni kupitia moto. Moto anawadanganya wenzake kuwa chanzo cha moto kilikuwa malaika aliyemtunukia uwezo wa kuzalisha moto. Anawavutia na kuwatia kwenye utando wa mauti kwa kuwagawia sehemu ya nyama ya kulungu iliyokuwa imeivishwa na moto barabara.

Kila mtu alikubali kuwa ile nyama iliyochomwa ilikuwa tamu ghaya. Moto kando na kuwaonjesha utamu wa nyama choma, anawatia hofu ili wasiweze kudadisi asili na athari halisi za anthroposenia – moto. Kwa mfano, anawatia hofu katika *Walenisi* kwa kusema kuwa, "Hizi ndizo nguvu za Mooootoo … Mimi ndimi Mooотoo … nijieni niwageuzie maisha yenu …" (uk. 157). Hakika, anthroposenia iliwageuzia watu maisha kwa sababu, baada ya watu kukumbatia moto kwa kuchukua kila mmoja kaa na kupeleka makwao; tamaa, ubinafsi, ufisadi na ubaguzi yanavumbika ulimwengu mzima kutoka kila pembe ya dunia. Na kama mwamba ngoma kila mwanakijiji alivuta kwake. Hivi ndivyo maangamizi yalivyoasisiwa na kusambazwa kote ulimwenguni. Kutokana na hila za moto, maangamizi yalipata mashiko na yakaota mizizi, sio tu ulimwenguni bali hadi kwenye nafsi na utu za watu, hasa Wachuna. Baada ya Moto kuwalambisha wanakijiji kaa la moto kila mmoja, watu walianza kuuzoea moto na wengi wakawa wanaenda kwake Moto kupata 'moto mpya'. Hali hii ilimpa Moto fursa nzuri ya kutoa masharti ili kuwafanya watu watumwa wa anthroposenia. Moto hakutaka moto uenee shaghalabaghala. Hivyo, aliweka masharti mawili yaliyoelekeza kuwa, moto ungepatikana kwake Moto tu kila jioni na pili, moto ulihitajika kuzimwa punde tu baada ya matumizi. Kutokana na woga aliokuwa amewauzia wenzake hapo kabla, hakuna aliyedhubutu kuvunja kanuni zake Moto. Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anathibitisha hili anapofafanua kuwa:

> "Masharti haya yalifuatwa, naye akawa mgawaji wa moto wa pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa – na punde si punde za utukufu pia! Sasa watu wakawa bila moto, hakukuliwa kitu na basi kumtegemea yeye kukazidi." (uk. 157).

Moto anaendelea kusawiri maangamizi kupitia ubatizo wa moto ulioitwa Moto Mtakatifu. Kwa kutumia hila, uzandiki na vitisho, Moto alifanikiwa kuwashawishi watu wote wawe wakimgawia chakula chao ili naye pamoja na familia yake azidi kuuhifadhi Moto Mtakatifu. Ili usife. Kimsingi, na kimakusudi, Moto akakuza na

kuhifadhi mauti. Hivyo, kitendo kile cha kila mtu kumpatia Moto theluthi ya chakula chake kinaashiria jitihada za wanadamu kuyalisha na kuyashibisha mauti ulimwenguni, kupitia shughuli zao za kila siku. Mwandishi wa *Walenisi* anathibitisha hili anapofafanua kuwa, "… mkewe na watoto wake wakawa hawana haja ya kufanya kazi. Hali watu hawakukoma kumpatia "kodi ya moto", ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi kujiepusha na kufanya kazi, huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha "Utukufu wa Moto"." (uk. 158). Hali hii ndiyo iliyoasisi maafa, hasa katika mataifa mengi barani Afrika. Hali hii inafungamana na nguzo ya kifo ya Nadharia ya Uhakikimazingira. Hili linawiana na kauli ya akina Morton (2015), Demos (2017), Moore (2017), DeLoughrey (2019), na Frantzen na Bjering (2020) kuwa, binadamu alivumbua anthroposenia kiajali lakini akaihifadhi na kuiendeleza kimakusudi na tena kwa malengo ya milenia pamoja na ya maendeleo endelevu katika janibu tofautitofauti ulimwengunni, hasa katika nchi za Afrika.

Kwa misingi hii, anthroposenia imeendelea kupevuka, kusambaa na kujilinda kwa kila namna. Mathalani, anthroposenia hujidhihirisha kupitia majina aina aina lakini kusudi la anthroposenia huwa moja na bayana ulimwenguni: kunyanyasa, kuonea, kutesa, kudhoofisha na hatimaye kuangamiza na kisha kurudia mchakato huu huu kwa nguvu mpya (Moore, 2017; 2018). Mchawi ana jina la kimajazi linaloashiria na kusawiri maangamizi katika riwaya ya *Walenisi*. Mdee na wengine (2009) wanafafanua kuwa, mchawi ni mtu anayewaroga watu; yaani mtu anayewadhuru watu kwa njia za kishirikina ilhali mganga ni mja anayewatibu wagonjwa na kuwapa dawa. Mchawi alikuwa ametoka kwenye jamii ya Wachuna wa ukoo wa Uganga. Kupitia Mchawi inadhihirika kuwa, maangamizi huzalisha mabadiliko ya maisha ya wanajamii kwa jumla. Kabla ya uchipuzi wa maangamizi ya kimazingira duniani, maeneo mengi yalikuwa tulivu na mwafaka kwa uhai wa binadamu (Moore, 2017; Filipova, 2023). Mathalani, Mchawi anachagua pahali penye kivuli, nafasi ya wazi yenye miti mikubwa na midogo iliyokuwa imeshikamana juu matawini, na pia pazuri pa kupumzikia. Lakini majilio ya maangamizi kupitia nyoka yanamkatizia hadi choo chenyewe alipokuwa akijisaidia.

Baada ya kuhakikisha kuondoka kwa chatu, Mchawi alikimbia hadi kwenye shina lile lile la mti alimojigangia chatu na bila kupoteza muda, akachimbua mizizi, akabambua magamba na akachuma majani ya mti ule. Vyote akavitia bindoni na kuelekea kwake nyumbani bila kujali choo kilichokuwa kimempeleka pale kabla ya mzozano wa chatu

na bafe. Kwa upande mmoja, mauti yanawalaghai watu kuwa yanawafaa ilhali yanawanyonya damu kiuchumi na kijamii. Hapo kabla kwa mfano, Mchawi anamganga jirani yake, ambaye alikuwa ameumwa na bafe na watu walikuwa wamekwishaanza kuchimba kaburi huku wengine wakimshawishi atoe wosia wake asije akaacha vita na mizozano ya kifamilia baada ya mauko yake. Mchawi anatumia mizizi na magamba anayoyasaga unga na kuuchanganya na majani. Kisha anautia unga ule pamoja na majani kwenye chungu chenye maji na kuyakoroga.

Katika harakati za kumtibu jirani yake, anaigiza kelele za chatu na bafe. Hili linaashiria namna mauti hujiendeleza katika maisha ya viumbe-hai. Mchawi anamnywesha upawa mzima wa dawa yake na ghafla, mgonjwa akaanza kuangaza macho na kisha akaketi. Mabadiliko haya yanawapa watu matumaini ya uhai bila kujua kuwa, Mchawi alikuwa na hila zake humo ndani. Badala ya Mchawi kuwafichulia siri yake ya asili ya dawa yake anarembua macho na kuwachekelea tu. Kutokana na ufanisi wa kumtibu jirani yake, sifa za uganga wa Mchawi zilienea kote na kusababisha watu kumiminika kwake wakimletea wagonjwa. Mwanzo waliwaleta wagonjwa waliokuwa wameng'atwa na nyoka lakini hatimaye walimletea wagonjwa wa kila maradhi. Mchawi naye kwa hila na kubahatisha, alizidi kuyachanganya mavuo yake na miti shamba mingine na kuwatibu baadhi huku wengine wakijifilia. Watu kwa sababu ya kupofushwa na dhiki na manyanyaso tele hawakumlaumu Mchawi kwa wale wagonjwa walioaga dunia. Kwa kauli moja walikariri katika *Walenisi* kuwa, "Mchawi amejaribu kila alichoweza, lakini kwa bahati mbaya tu." (uk. 161). Hili linadhihirisha kuwa, bahati nasibu ni nguzo kuu ya maangamizi ambayo hushamiri sana, hasa katika janibu za Afrika. Hili linalandana na nguzo ya kifo.

Bitanihirwe na wengine (2022) wanataja kuwa, pingu za michezo ya bahati nasibu zimelemaza chumi nyingi barani Afrika na kuwafanya vijana watumwa wa kimawazo huku ulofa, uongozi dhalimu na maafa yakinawiri kila uchao. Kama Moto, Mchawi anawalaghai watu kujilimbikizia mali kwa kuwatisha. Kwa hofu, watu wanamuomba Mchawi asisitishe kutoa huduma zake za matibabu wala asirejee kwao makondeni. Hivyo, watu wanamlisha na punde si punde, Mchawi anatajirika na kupata hisia za kifalme, utukufu na mjuaji kweli. Ili kupalilia ulofa na utegemezi, kuulinda na kuuhifadhi, Mchawi kama Moto, anawalisha kiapo wanawe wa kiume baada ya

kuwarithisha siri ya utumwa na maangamizi ili usije ukajulikana na wananchi wengine wala taifa lingine barani mwao.

Mabavu ni jina la kimajazi linalosawiri maangamizi. Mabavu anaasisi maangamizi kupitia hila zake za kimabavu. Mabavu ni nguvu itumiwayo kufanya jambo bila idhini ya mtu au watu wanaohusika (BAKITA, 2015 na Mdee na wengine, 2015). Kwa mfano, Mabavu anatumia nguvu kumteka nyara Kadzo huku akiwa amevalia ngozi ya simba na kunyatia kama simba bila idhini ya Kadzo. Anamficha kwenye pango na kumwacha mle. Baada ya wanakijiji na mashujaa wote kukata tamaa, wazazi wa Kadzo wanamwendea Mabavu kwa unyenyekevu na huzuni tele na kumsihi aende akamwinde na amwangamize simba yule. Kwa kujifanya, Mabavu akajitayarisha kwa ngao, assegai mikononi, njora, alani, uta mabegani, fumo mgongoni na mishale ziakani na kisha akaondoka kwenda kumwinda 'nunda' aliyemnyakua Kadzo kutoka nyumbani kwao usiku uliokuwa umetangulia.

Hakika kabla ya jua kutua, Mabavu alirejea na ngozi ya simba dume mabegani pamoja na Kadzo akiwa mzima kabisa. Ingawa watu hawakusadiki video iliyojidhihirisha machoni mwao paruwanja, wazazi wake Kadzo hawakuwa na lingine isipokuwa kutimiza ahadi yao kwa Mabavu, na hivyo ndivyo Kadzo aliolewa na Mabavu. Wazazi wake walikuwa wamemwahidi Mabavu kuwa wangemwoza binti yao kwake ikiwa angefanikiwa kumwangamiza nunda aliyeshukiwa kumteka nyara Kadzo. Mabavu hivyo, anaashiria utawala wa kimabavu na utumwa, hasa katika mataifa mengi barani Afrika, ambamo walalahai na watawala hutumia hila kupalilia uongozi na utawala dhalimu. Huufaidi utawala na uongozi dhalimu katika uhusiano wa unyonyaji, dhuluma, maonevu na ukiukaji wa haki za kibinadamu (Moore, 2017; 2018; Head, 2028). Kwa kutumia hila, Mabavu anaendelea kujipatia wasichana wote warembo. Nguzo kuu inayoendeleza na kuhimili dhuluma na unyanyasaji katika misingi hii ya hila, dhuluma, maonevu na ukiukaji wa haki za binadamu ni hofu.

Kutokana na hofu watu wanamjia Mabavu awasaidie bila wao kudadisi mambo yanayotokea wala kutathmini uhalisia wa kila tukio. Mabavu anawalaghai watu na kupalilia utumwa hadi watu wanabadili jina lake na kumwita simba. Kule kuua simba katika eneo lile naye Mabavu, kunaashiria athari hasi za dhuluma na mateso zinazotishia uhai wa viumbe, hasa wanyama. Lara na wengine (2018) pamoja na Coughlin na Gephart (2020) wakikubaliana na mawazo ya mtafiti wanataja kuwa,

anthroposenia huunyonya uhai wa viumbe vyote vyenye uhai duniani. Simba ni taashira ya anthroposenia pia. Hili pia ni jina la kimajazi linalosawiri maangamizi, hususani kwa wananchi wa kawaida katika mataifa fukara ulimwenguni. Ikizingatiwa kwamba ulimwengu hunasibishwa na ishara za mwanamke (Nayar, 2010), basi Kadzo na wasichana wote wanaoozwa kama makafara kwa makeke makuu wanaashiria ulimwengu unaonajisiwa na kudhibitiwa na viongozi dhalimu wenye uwezo na utajiri unaoashiriwa na Mabavu au Simba. Hili linafungamana na nguzo ya uwezo na kifo.

Mdee na wengine (2009) wanafafanua kuwa, simba ni mnyama pori wa jamii ya paka lakini mkubwa kuliko wote wa jamii hii mwenye manyoya ya rangi ya majani makavu na ambaye hula nyama. Simba kwa tamaa, ubinafsi na unafiki anajitia inda ya kuvaa ngozi za wanyama hatari. Mathalani, anavaa ngozi ya simba na kuketi juu ya kichwa cha simba huku akivyoga ngozi ya chui. Kifuani anakangamwa na mkumbuu wa ngozi ya chatu. Kwa jumla, mavazi haya yaliwaogofya watu kwa hofu na unyenyekevu. Kama tu maangamizi ambayo hufaidi na kushamiri katika woga, Simba alishibishwa na hofu ya wanakijiji na akajitwika jukumu la kuwabikira wasichana wote ili tu wazazi wao wapate ulinzi wake. Simba anawalazimisha watu kukubali sheria zake akiwa amewalaza kifudifudi mavumbini huku wakiwa wameyabwaga macho. Katama Mkangi katika riwaya yake ya *Walenisi* anathibitisha hili anapoeleza kuwa, “Hivi ndivyo tambo la Mabavu lilivyozua Wachuna waliojipa ufahari wa simba na mwishowe wakajipa ufirauni wa chapa ya “Simba”, kama kitambulisho cha utawala wa nasaba yao.” (uk. 166). Simba anaendeleza maangamizi kupitia hila, maonevu na utawala wa kimabavu. Aidha, anatunga kaida ambazo anawalazimisha watu kuzikubali bila hiari yao. Hili linawiana na nguzo ya uwezo na kifo.

### 5.6 Tashtiti

Dhihaka ni kisawe cha kinaya, kejeli na kwa kiwango fulani tashtiti ambayo uwezo wake mkubwa hudhihirika kupitia nguvu za kibalagha (Wamitila, 2010). Kiuyakinifu, tashtiti hukusudia kufichua uozo, uovu au ubaya kwa matumizi ya mchanganyiko wa ucheshi na dhihaka. Wamitila (2003) anafafanua kuwa, tashtiti ni ‘kilengwa cha shambulio’ ambacho hupatikana katika mazingira maalum ya kihistoria, kibinafsi, au hata ya kijamii. Kilengwa hiki cha kushambuliwa ni cha lazima kiasi kwamba ikiwa kitakosekana huenda tusiweze kuzungumzia suala la tashtiti katika mazingira

yanayohusika (Simpson, 2021). Katika utafiti huu, kilengwa ni njia zinazopalilia anthroposenia kimwavuli pamoja na hali zinazotawala na kuidhibiti anthroposenia.

Kwa mfano, katika anthroposenia, viongozi ndio wanaoongoza kuvunja sheria za kulinda mazingira, ambamo wao ndio wanaotarajiwa kuhakikisha kuwa kaida zinazingatiwa kikamilifu. Mathalani, Jonalisti alipokuwa anatoka dampu la Siza alikumbana na kibao kikubwa kilichokuwa kimewekwa na Halmashauri ya Mji wa Siza. Jonalisti alikiri kuwa maandishi yale yalikuwa kejeli na mzaha wa wakuu wa Halmashauri ya Mji wa Siza. Hii ni kwa sababu kibao chenyewe kando na kutengenezwa na mbao kilikuwa kimekitwa ndani ya uozo wa taka za dampu. Mbao zilizokitengeneza zilitokana na miti iliyokatwa ovyo. Maandishi yaliyoandikwa yalikuwa dhahiri na yaliandikwa kuwa:

*MUNICIPAL COUNCIL OF SIZA WARNING*
*NO DUMPING*

HALMASHAURI YA MJI WA SIZA ONYO
USITUPE TAKATAKA HAPA:
UKITUPA UTASHTAKIWA
**BY ORDER: TOWN CLERK** (uk. 28).

Mwandishi wa *Bustani* anasawiri vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kitashtiti. Baada ya umati wa watu kupiga yowe na kulikemea dampu la Siza, nguruwe waliokuwa wamejiinamia wakiufaidi uhondo wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira wanashangazwa na ukemeaji ule. Mbogo anaeleza katika *Bustani* kuwa, "… hawakuamini kuwa binadamu (ati yule anayewafuga) alikuwa na akili chache vile … akaacha kazi zake na kuandamana akikilaani chakula chao cha dampu ambacho wao walikiona kama mlo kamili." (uk. 92). Hili linawiana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo binadamu hutathminiwa namna anavyoingiliana na kutagusana na mazingira.

### 5.7 Tashihisi

Kwa mujibu wa TUKI (2014), tashihisi ni usemi wa kukipa kitu kisicho uhai sifa ya kitu chenye uhai. Mtunzi Mbogo anatumia uhuishaji kuashiria jinsi maangamizi yanavyomkabili mwanadamu. Mathalani, ardhi yenyewe inainuka na kujaribu kudidimiza vita dhidi ya unajisi wa mazingira kupitia maombi ya Pasta Yona.

Mwandishi wa *Bustani* anataja kuwa, "Kutokea hapo sasa upandaji wa kilima ulikuwa mgumu zaidi, ardhi iliinuka juu ghafla." (uk. 34). Pasta Yona alipofika kileleni cha mlima, alilikuta jiwe kubwa lililokaa juu ya jiwe jingine likimtazama. Eneo lile ndilo alilotulia na kunena na mungu kama kawaida yake. Maombi yake yalilenga kukabiliana na mauti yaliyotisha kuwaangamiza yeye na wafuasi wake pamoja na wakaaji wa Mji wa Siza. Karibu na lile jiwe lililomtazama alipiga magoti na kuanza kuyaleta na kuyaelekeza mawazo yake pamoja kabla ya kumwomba mungu. Viungo vyake vya mwili vinatubu, kuabudu na kusujudu kwa unyenyekevu.

Mto Gihoni ulisafiri huku ukichukua tope na udongo wenye rutuba katika bustani ya Edeni. Mtunzi Mbogo katika *Bustani* kupitia mhusika Baba Adamu anaeleza kuwa, Mto Hedekeli ulitembea kwa madaha huku ukinyonga kiuno chake vizuri. Kwa mfano, anasema katika *Bustani* kuwa, "Wote bado wanaukumbuka Mto Hedekeli uliotembea kwa madaha, ukinyonga kiuno chake kizuri …" (uk. 36). Fauka ya hayo, anaongeza kuwa, "Walikuwa bado wanaukumbuka Mto Frati uliokimbia kasi, ukavuka milima na kuiparamia milima ya mawe …" (uk. 37). Mazingira ambamo kasri la Abdula lilimo yamepewa uwezo na sifa za kuwa na uhai. Mwandishi Mbogo katika *Bustani* anaeleza kuwa, kasri la Abdula lilikuwa limesimama pwani. Kasri la Abdula sio tu ishara ya anthroposenia ila malezi hasa ya anthroposenia. Ni kasri ambalo husitiri aina kadhaa za anthroposenia, kama vile Abdula na familia yake. Mbogo anaendelea kueleza kuwa udongo uliokuwa umefunikwa kwa majani ya rangi ya kijani kibichi ulianzia pale ukutani mwa nyumba kisha ukateremka umbali wa mita hamsini kuelekea mashariki.

Bwana Abdula anaongeza kuwa majani yale yalihusiana na mchanga wa fedha wa Bahari ya Hindi ulioendelea huko mashariki hadi ukagusana, ukakumbatiana na maji ya chumvi. Maji yale ya Bahari ya Hindi yalikuwa yakikupwa majira machanga, na kasha halafu, yalijaa tena siku ilipokomaa na kuzeeka. Aidha, ua lilipochomoza alfajiri na kuwaka zaidi nyakati za mchana, liliufanya mchanga ule wa fedha ucheze na kuchekacheka kwa furaha kama nyota mbele ya macho ya familia kubwa ya Bwana Abdula.

**Hitimisho**

Kwa kutamatisha sehemu hii ya uhakiki wa mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni*, *Vipuli vya Fifo*, *Mafuta* na *Walenisi*, utafiti huu umedhihirisha wazi wazi mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia na waandishi wa kazi hizi nne za waandishi Mbogo na Mkangi. Kwanza kabisa, waandishi hawa wamefanikiwa kutumia mbinu ya taashira kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule. Mbinu hii wameitumia kupitia vipengele tofautitofauti vya taashira. Vipengele hivi ni pamoja na; taashira ya mahali, taashira ya vifaa, taashira ya viumbe, taashira ya ulofa na ndwele na pia taashira ya hali za maumbile. Kadhalika, walifaniwa kutumia mbinu ya taswira, ishara, majazi, tashtiti na tashihisi kusawiri anthroposenia katika nne teule zilizotajwa katika sehemu hii. Nguzo zilizoongoza uhakiki wa data kwa kila mbinu zilifafaliwa katika kila kisehemu cha uhakiki mintarafu ya lengo la pili la utafiti huu.

# SURA YA SITA

# UCHANGANUZI WA RAI ZA WAANDISHI WA RIWAYA NNE TEULE

## 6.1 Utangulizi

Uchanganuzi wa data katika sehemu hii ulifanywa mintarafu ya madhumuni ya tatu ya utafiti na kuongozwa na nguzo kuu za Nadharia ya Uhakikimazingira. Kwa mujibu wa madhumuni ya tatu ambayo yalikuwa kutathmini rai za waandishi wa riwaya teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni (2002), Vipuli Vya Figo (1996), Mafuta (1984) na Walenisi (1995)*; mtafiti alitathmini rai walizozitoa waandishi kuhusu namna aina aina za kukabiliana na anthroposenia katika riwaya hizi. Uchanganuzi wa rai za waandishi ulitekelezwa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. Kwanza ni ushahidi wa maandishi ambao hujumuisha kauli za moja kwa moja za wahusika, maoni ya mwandishi au vipengele vya ishara vinavyoonesha ujumbe wa mwandishi. Pili, uandishi wa wahusika ambapo uchambuzi kuhusu jinsi wahusika katika maandishi wanavyoakisi au kuhimiza suluhu dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Vilevile, kuchunguza imani, matendo na motisha za wahusika. Tatu, nia ya mwandishi ambapo uchambuzi wa filosofia, maarifa kuhusu uzoefu wa kibinafsi wa mwandishi, muktadha wa kitamaduni na muktadha wa kihistoria ulitekelezwa. Nne, uchambuzi wa mada ambapo mada kuu au vichocheo ndani ya maandishi ili kufahamu ujumbe uliojificha wa mwandishi ulitekelezwa. Mintarafu ya Nadharia ya Uhakikimazingira, nguzo kuu kama vile; jinsia na historia za jamii, maumbile, haki na maadili ya kimazingira, uwezo, utandawazi, na utamaduni na mazingira ziliongoza katika uchanganuzi wa sehemu hii kwa kuangaza mtazamo wa mwandishi.

## 6.2 Vyombo vya Habari na Uhamasishaji wa Uendelevu

Vyombo vya habari ni teknolojia ambayo kusudi lake kuu ni kuwasilisha ujumbe au kupasha habari kwa hadhira kubwa au watu wengi zaidi (Mitchell, 2007). Nadharia ya Uhakikimazingira huhimiza kaida za kimazingira ambazo hunuia kuimarisha masuala ya mazingira kwa ujumla. Moja ya kanuni zake kuu ni kukuza uhifadhi wa mazingira kwa kuhamasisha uelewa na kuhimiza mbinu endelevu. Aidha, nadharia hii inakuza ekosentriki ambapo thamani ya ndani ya viumbe vyote na mifumo ya ikolojia inatambulika. Kwa kupinga mitazamo ya anthroposentriki, uhakikimazingira hukuza mtazamo wa kina zaidi na unaoelekea kwenye kuyasikitikia na kuyawajibikia mazingira kwa kuyahifadhi. Waandishi wa riwaya nne teule wametumia aina tofauti

za vyombo vya habari kuwahamasisha, kuwazindua na kuwashajiisha watu kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.

### 6.2.1 Vyombo vya Habari vya Chapa na Ufanisi wa Mazingira

Mtunzi Mbogo kupitia mhusika Jonalisti anawasisitizia watu haja ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kutumia magazeti yaliyotolewa kila siku kwa lugha ya Kiswahili, JAMII YETU na la Kiingereza, OUR SOCIETY. Hili linadhihirisha kuwa, magazeti kama chombo cha habari cha chapa yanaweza kutumiwa kuwahamasisha wananchi dhidi ya njia mwafaka za kuyahifadhi na kuyanawirisha mazingira kwa kuwahamasisha watu. Ikizingatiwa kwamba gazeti kama chombo cha habari chapa kilikuwa kifaa madhubuti cha kuwafikishia wananchi ujumbe, waandishi wa riwaya teule wanatoa rai kuwa gazeti ni mwafaka katika kukashifu uchafuzi wa mazingira kwa jumla kwa kuwafafanuliwa wananchi kuhusu madhara ya kudumu ya mazingira chafu. Hakika, uhamasishaji kabambe hupalili uelewa wa kina zaidi wa umuhimu wa kuhifadhi rasilimali asilia, kulinda bioanuwai na kudumisha usawa wa ikolojia. Hukuza wazo kwamba uhifadhi wa mazingira sio tu muhimu kwa wanadamu bali pia ni muhimu kwa ustawi wa sayari yote.

Mwandishi Mbogo kupitia mhusika Pasta Yona wa Yona anatumia vitabu kuwahamasisha watu kuhusu njia za kukabiliana na unajisi wa mazingira. Anaonyesha nafasi ya vitabu katika vita dhidi ya uharibifu wa mazingira. Vita hivi vinafanikishwa kupitia uhamasishaji wa watu dhidi ya madhara ya uchafuzi wa mazingira kwa uhai wa viumbe. Isitoshe, anasisitiza kuwa, viongozi wa dini wawe mstari wa mbele katika vita vya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kutumia kitabu kitakatifu – Biblia kukashifu uchafuzi wote. Kupitia magazeti na vitabu mtunzi Mbogo anatoa rai kuwa vina nafasi muhimu ya kutoa taarifa muhimu zinazosaidia kuwajibisha mashirika na serikali. Hili linawiana na kauli ya akina Angus (2016), Moore (2017; 2018) na Feder (2021) kuwa, vitabu vina nafasi kubwa katika vita vya kudidimiza na hatimaye kuuangamiza uchafuzi na unajisi wa mazingira. Wanasisitiza kuwa, ingawa lengo kuu la ubepari – ambao ni aina ya anthroposenia ambayo hupalilia kapitalosenia – ni kulimbikiza mali na utajiri bila kujali athari za ulimbikizaji wenyewe, huchangia pakubwa katika kuimarisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira ulimwenguni. Hivyo, juhudi za kudidimiza uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kutumia vyombo vya habari kuwashajiisha watu wahifadhi mazingira; zitazalisha ufifiaji wa maradhi tofautitofauti; uhifadhi wa misitu

ambayo huzalisha oksijeni ambayo binadamu na wanyama hupumua, ujenzi wa mifumo kabambe ya kiikolojia, pamoja na usafishaji wa maji, hewa na mchanga ambavyo vimenajisiwa na utupaji taka ovyo kutoka kwenye viwanda mbalimbali.

Isitoshe, mtunzi Mbogo anapendekeza kuwa uandishi na uchapishaji kwenye gazeti kuhusu unajisi wa mazingira unaotekelezwa na mashirika makubwa, viwanda, matajiri na asasi za kiserikali ni ala kabambe ya kukabiliana na unajisi wa mazingira. Lengo kuu la kuandika kwenye gazeti ni kuwahamasisha wananchi kuhusu athari hasi za mazingira tasa na haja za kuzikabili kwa ujasiri. Hakika mabadiliko ya tabianchi yaweze kutatuliwa na binadamu punde tu aelewapo madhara yamkubayo kama vile, maradhi, njaa, maudhi na maafa. Aidha, mabadiliko haya yanapalilia ulofa, uongozi mbaya, maafa na madhara mengine mengi.

Mwandishi Mbogo katika *Bustani* anapendekeza matumizi ya magazeti kama mbinu ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kuwahamasisha wananchi dhidi ya unajisi wa mazingira. Kwa mfano, vichwa vya habari vya gazeti la *Our Society* na lile la *New Era* vinampa kiwewe Bwana Abdula punde tu anapovitupia jicho kuvisoma. Ikizingatiwa kwamba Bwana Abdula ni taashira ya watu na ajenti wanaoyachafua na kuyaharibu mazingira, hasa katika mataifa mengi duniani, kuchefuka kwa mtima wake ni ishara tosha kuwa magazeti ni mbinu mwafaka ya kukabiliana na wachafuzi wa mazingira. Kupitia magazeti haya mzozo wa kiwanda cha Sagasaga na uchafuzi wa mazingira ya mji wa Siza ulikuwa umeangaziwa upya kwa ari kubwa. Kwa upande mmoja, gazeti la *Our Society* liliandika kwa hati iliyokolezwa rangi kuwa: *LEAKAGE OF SULPHURDIOXIDE IN SAGASAGA CHEMICAL FACTORY* ilhali kwa upande mwingine, gazeti la New Era lilikuwa limerembesha anwani kwa maneno kuwa: *SAGASAGA CHEMICAL INDUSTRY MUST GO – Priest* Yona wa Yona. Hali hii inawiana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo binadamu huhamasishwa kushiriki katika juhudi za uhifadhi wa mazingira.

Umwagikaji wa *Sulphurdioxide* unaashiria ueneaji wa uharibifu wa mazingira ulimwenguni kote, madhali ni kemikali ambayo huwa sumu na hupatikana katika volcano na pia katika petroli inayoungua. Kemikali hii huwa chanzo cha mvua yenye asidi. Hivyo, ni kemikali hatari kwa maisha ya viumbehai na baadhi ya viumbe visivyo hai na pia mimea. Umwagikaji wa kemikali hii katika kiwanda cha Sagasaga

ni thibitisho tosha kuwa kiwanda hiki ni taashira ya chanzo cha uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa jumla. Pasta Yona wa Yona naye anaashiria watu wanaokabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa udi na uvumba ili kupunguza makali ya mabadiliko ya tabianchi dhidi ya maisha ya binadamu na viumbehai pamoja na mimea na maumbile. Katika gazeti la *New Era*, Jonalisti ambaye ni mmoja wa wanaharakati wakuu wa kukabiliana na tabianchi amefanya kazi kubwa na murua. Mathalani, chini ya anwani la gazeti, kushoto, aliiweka picha ya ajenti wa kupiga vita unajisi wa mazingira – Pasta Yona wa Yona. Upande wa kulia, chini kidogo, alikuwa amepachika picha ya chumba cha Sagasaga kulikotokea ajali ya akina Eliya na Baba Samsoni. Uhamasishaji huu unawafanya watu kuona haja ya kuyahifadhi mazingira yao kwa ujasiri na kwa kujitoa kafara.

Mtunzi Mbogo anasisitiza kuwa, katika mazingira chafu, malezi ya watoto yanatatizwa na afya ya viumbe hai inadorora. Kwa mfano, kupitia mhusika Jonalisti katika ukurasa wa pili wa gazeti *New Era* anaeleza na kuambatanisha maelezo yake na picha ya Eliya akiwa ametundika mguu juu ya kitanda kule hospitalini, huku akionekana akimpa mkono mwanawe Samsoni. Hili linaashiria kuzorota kwa afya ya jamii na changamoto zinazozalishwa na mazingira chafu na dhoofu katika malezi ya watoto katika jamii ulimwenguni. Mwandishi Mbogo anapendekeza haja ya kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa mazingira safi pamoja na kuwaanikia uchi wa madhara ya mazingira chafu kupitia maandishi na picha gazetini.

Kupitia picha na maelezo kwenye gazeti, mtunzi Mbogo anawaonyesha paruwanja wenyeji wa Siza namna ufukara huwafanya wananchi kukumbatia utumwa, uchafuzi wa mazingira na hatimaye maafa. Anafanikisha hili kupitia picha inayoonyesha wafanyakazi wa Sagasaga wakipakia madawa ndani ya gari bila kuwa na mipira ya kujikinga dhidi ya madhara yake. Hali hii inawiana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo binadamu anapoingiliana na mazingira kwa njia zisizo na maadili husutwa na mazingira yenyewe kupitia ukame, mafuriko, kiangazi na maafa ya mimea, wanyama na watu kwa ujumla.

Inadhihirika kwamba matumizi ya magazeti kuwaanika wachafuzi wa mazingira huwaogopesha na kuwapunguzia ari na juhudi za uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Mwandishi anadhihirisha hili kupitia mhusika Bwana Abdula ambaye, kinachompigisha mshipa ni maandishi aliyoyaandika Jonalisti chini ya picha ile.

Katika ukurasa wa tatu wa gazeti lile la *New Era*, Jonalisti anaendeleza maelezo yake huku akiambatanisha na picha tatu zinazosawiri hali halisi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Picha ya kwanza inalionyesha dampu la Siza. Hili linadhihirisha kuwa picha ni njia nzuri ya kuihamasisha jamii dhidi ya uchafuzi wa mazingira kama aina ya vyombo vya habari ya chapa. Hili linawiana na kauli ya akina Davis na Turpin (2015) kuwa, picha kando na kuvutia na kumpendeza mtazamaji kutegemea ladha ya mtazamaji huwa ala mwafaka ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kumtia binadamu ari ya kuyahifadhi mazingira.

Hii ni kwa sababu, ikizingatiwa kwamba binadamu ndiye asili ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira pia ndiye anayepokea athari hasi za uchafuzi na uharibifu huu moja kwa moja, huweza kujihamasisha kuhusu mbinu mwafaka za kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kupitia picha. Hii ni kwa sababu, ubongo wa binadamu huchanganua masuala yanayowasilishwa kwa picha kwa njia ya kiasili, haraka na huwa rahisi kwa binadamu kuikumbuka picha kwa wepesi. Chini ya picha ile mwandishi kupitia mhusika Jonalisti anasisitiza madhara ya utepetevu wa uongozi na utawala katika kuruhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika mataifa mbalimbali. Picha hii inawapa wanajamii wa Siza njia mbadala ya kusawiri uchafuzi wa mazingira na kupambazukiwa na ukweli kuhusu madhara ya mazingira chafu na tasa kama zao la athari za shughuli za binadamu za kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa ujumla.

Aidha, mwandishi Mbogo anatumia picha kusawiri madhara ya mazingira chafu kwa binadamu kupitia minofu ya mifugo wanaochinjwa katika maeneo tofautitofauti. Kwa mfano, picha ya pili inaonyesha nguruwe na ng'ombe wakiwa wameinamia taka huku wakizimega kwa bashasha. Hili linawapa wananchi walaji nyama jicho jipya la kutazama na halafu kuwazia nyama wanayonunua ya nguruwe na ng'ombe. Hii ni kwa sababu, mhusika Jonalisti anaeleza wazi katika *Bustani* kuwa, wakwasi ambao hula nyama ya nguruwe hunogeshewa ladha na zebaki na makemikali mengine ya Sagasaga. Vilevile, mtunzi anawadhihirishia watu kupitia picha kwenye gazeti madhara ya kuyanywa maziwa ya ng'ombe wanaokula taka kutoka kwenye dampu la Siza. Wanapokunywa maziwa hayo, wakaaji wa Siza pamoja na wana wao wanakumbwa na maradhi ya saratani.

Mwandishi kupitia mhusika Jonalisti anadhihirisha ufukara kama zao la mazingira chafu na hivyo kusisitiza haja ya kuyanadhifisha mazingira kama njia ya kupambana na umaskini. Kwa mfano, katika ukurasa wa nne wa gazeti lile la *New Era* Jonalisti anaweka picha ya watu wanaogombania kuokota sindano za hospitali na chupa za madawa katikati mwa mchafukoge wa taka za hospitali katika dampu la Siza. Ugomvi huu unaonyesha hali ya ufukara baina ya wanajamii katika mazingira chafu. Katika mazingira chafu na yaliyoharibiwa, maisha ya binadamu yanahatarishwa. Utowajibikaji wa hospitali ya Wilaya ya Siza unadhihirisha uongozi mbaya katika mazingira chafu na yaliyonajisiwa. Hakika hili linashabihiana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo uongozi huruhusu asasi, idara, wizara na sekta mbalimbali za kiserikali kuyapujua mazingira bila kuyawajibikia wala kuyasikitikia.

Halikadhalika, mwandishi anawazindua watu kuhusu haja ya kupalilia uongozi unaoyapa mazingira kipao mbele. Mathalan, kupitia *Bustani* anasawiri uongozi mbaya kupitia Halmashauri ya Jiji la Siza. Inadhihirika kuwa uongozi mbaya hupalilia uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Kupitia mhusika Jonalisti anaonyesha kibao cha Halmashauri ya Jiji chenye maandishi ya kutahadharisha wenyeji dhidi ya umwagaji taka kwenye dampu la Siza. Kwenye picha hii anaiunganisha picha ya kibao kile na picha ya gari la taka la Halmashauri ya Jiji likitapika takataka kwenye sehemu ile ile iliyokuwa na bango la onyo kali. Ndiposa Jonalisti anatashtiti uongozi mbaya wa mji wa Siza anapouliza kibalagha chini ya picha ile kuwa, “Je, Wazee na Waheshimiwa wa Halmashauri ya Jiji wanasemaje kuhusu mambo haya? “ (uk. 44). Aidha, magazeti ni ala muhimu ya kuwahamasisha wanajamii kuhusu haja ya kukabiliana na mazingira chafu. Mwandishi analithibitisha hili kupitia mhusika Pasta Yona anayeeleza katika gazeti la *New Era* kuwa, ilibidi kiwanda cha Sagasaga kifungwe na kutimuliwa kutoka kwenye mji wa Siza ili hewa iwe safi.

Isitoshe, kwa kuwa gesi inavuja mara kwa mara katika kiwanda cha kemikali cha Sagasaga, mwandishi kupitia mhusika Jonalisti anafafanua kuwa, inasababisha uzorotaji wa afya baina ya wanajamii, kama vile wafanyakazi wengi wa Sagasaga. Hii ni kwa sababu, wengi wao wana vidonda, wanapunyuka nywele, wana vikohozi na mafua bila kikomo, na wengine wana maradhi ya kuwashwa ngozi. Kupitia mhusika Jonalisti, mwandishi anawazindua watu kuhusu athari za mazingira chafu na tasa kwa jamii nzima. Ndiposa mwandishi anataja kuwa, madhara ya Sagasaga yameenea kwa

wakazi wengi wa Wilaya ya Siza bila ubaguzi. Kwa mujibu wa mtunzi Mbogo, gazeti ni ala mwafaka ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

### 6.2.2 Vyombo vya Habari vya Kielektroniki na Ufanisi wa Mazingira

Mwandishi Mbogo katika *Bustani* anatoa rai kuwa, teknolojia ya kisasa inafaa sana katika kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Anadokeza kuwa, pale hospitalini kwa mfano, mmoja wa watu kadhaa waliokuwa wamesimama pale kwenye Mapokezi alikuwa amevaa mshipi uliokuwa na kamera. Lengo kuu la kuwa na kamera ni kukusanya ushahidi katika harakati za kukabiliana na wachafuzi na wanajisi wa mazingira ya Siza, hasa sana katika kuukosoa uongozi dhalimu. Watu wanapohamasishwa dhidi ya athari hasi za mazingira chafu, tasa na hatari wanakuwa katika nafasi nzuri ya kuyakabili yote. Hili linawiana na kauli ya akina Watson na Watson (2007), Huggan na Tiffin (2010), Moore (2016) na Coughlin na Gephart (2020) kuwa, binadamu wakimaizi mambo hasi yanayozalishwa na mazingira dhoofu, wataweza kuyamakinikia na kuyasikitikia mazingira.

Katika kipindi cha miaka ya 1980 ambapo riwaya ya *Mafuta* ilichapishwa, majanga ya mazingira pamoja na maendeleo katika teknolojia ya setelaiti yaliruhusu ufuatiliaji na uchambuzi bora wa mabadiliko ya mazingira na uchafuzi. Kipindi cha miaka ya 1990 - *Walenisi* na *Vipuli vya Figo* – na 2000 – *Bustani ya Edeni* – ambapo riwaya tatu teule ziliandikwa kilishuhudia kuibuka kwa mtandao wa intaneti na vyombo vya habari vya kidijitali ambavyo vilichangia pakubwa katika harakati za mazingira kwa ujumla. Ndiposa Mtunzi Mbogo kupitia mhusika Bwana Abdula anadhihirisha kiwewe ambacho huwakumba waharibifu na wachafuzi wa mazingira wanapokisia kuwa shughuli zao zinaweza kuanikwa peupe kupitia vyombo vya habari. Hili linadhihirisha kuwa, vyombo vya habari vina mchango mkubwa katika kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira pamoja na utawala dhalimu kwa ujumla.

Ingawa uchafuzi na uharibifu wa mazingira ulikuwepo kabla ya vyombo vya habari vya kisasa, unaweza kudhibitiwa kupitia matumizi ya vyombo vya kisasa vya habari. Binadamu ameweza kupuuza chimbuko la uchafuzi wa mazingira na michakato inayolitambulisha lakini kupitia matumizi ya vyombo vya habari unaweza kudhibitiwa kwa ufanisi (Bladow na Ladino, 2018; Coughlin na Gephart, 2020). Mathalani, mtunzi Mbogo katika *Bustani* anapendekeza matumizi ya picha kama ala ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwa kuwahamasisha wananchi. Mtunzi

Mbogo kupitia mhusika Jonalisti ambaye alipiga picha nzuri zilizokuwa kielelezo kizuri cha kuwakashifu wakuu wa mji wa Siza na serikali kimwavuli, dhidi ya hulka yao mbaya ya kulea uchafu, ambao uliwasababishia wananchi madhara mengi na makuu anawakemea wachafuzi na kuushabikia uhifadhi wa mazingira.

Halikadhalika, mtunzi Mbogo katika *Bustani* anasisitiza kuwa vyombo vya habari vya kielektroniki anavyovirejelea kama mashine vinafaa kutumiwa kama ala mwafaka na madhubuti katika vita vya kukabiliana na uharibifu wa mazingira. Kupitia mhusika Baba Adamu, mwandishi Mbogo anapendekeza kuwa maendeleo na mashine ni ala nzuri ya kukabiliana na tabianchi anapoeleza katika *Bustani.* Punde tu mtunzi Mbogo anapopendekeza matumizi ya maendeleo na mashine kama ala ya kukabiliana na unajisi wa mazingira anasisitiza haja ya watu kuhimizana umuhimu wa kuudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira kupitia maendeleo na mashine, hasa ya mashine za vyombo vya habari.

### 6.3 Kupambana na Uchafuzi: Nafasi ya Ukakamavu katika Ulinzi wa Mazingira

Uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni suala linalohitaji ukakamavu na kujitolea kwingi. Mwandishi Mkangi amesawiri safari ya mhusika Dzombo kama ya mja anayepania kuyahifadhi mazingira. Mwandishi Mbogo katika Bustani amemsawiri mhusika Pasta Yona wa Yona kama mwanaharakati wa masuala ya mazingira ambaye hatimaye anaangamizwa na wachafuzi wa mazingira. Safari ya Pasta Yona wa Yona inaonyesha ukakamavu wa kipekee katika mchakato wa kuhifadhi mazingira. Mwandishi anaonyesha namna Pasta Yona wa Yona anavyokabiliana na changamoto kama vile, wachafuzi wa mazingira, uchafuzi wa hewa, upinzani wa uongozi na utawala, ufukara na mengine mengi. Hata hivyo ana azma ya kulinda mazingira asilia na hili linampelekea kuangamizwa na uongozi ili asishiriki maandamano ya kupinga unajisi wa mazingira unaowasababishia wakaaji wa Siza maradhi aina aina. Mwandishi Mbogo anasawiri safari ya mhusika huyu kwa maelezo yanayosisitiza jinsi ukakamavu unavyohitajika katika mapambano dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira na jinsi mhusika pamoja na wahusika wengine kama vile Jonalisti, Pamela na Wakili Mwaka wanavyokua na kupata nguvu kutokana na mapambano haya.

Mtunzi Mbogo kupitia mhusika Jonalisti anadhihirisha nafasi ya ukakamavu na kujitolea kwa binadamu katika vita dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Baada ya Jonalisti kurejea nyumbani hoi; kula; kuoga; na kisha kuingia kwenye

chumba cha malazi, usingizi unamchukua mara moja. Hii ni kwa sababu alikuwa na uchovu si haba maanake utafiti wa habari za Sagasaga na uchafuzi wa mazingira ulikuwa umemshughulisha siku nzima. Kujishughulisha huku ni tokeo la kujitolea na ukakamavu wa Jonalisti. Mwandishi Mbogo anahimiza watu wajitolee katika juhudi za uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Mwandishi Mbogo kupitia mhusika Pasta Yona wa Yona katika *Bustani* anadhihirisha bayana kuwa, suluhu dhidi ya mazingira najisi litatokana na ukakamavu, kujitolea na kujitoa kama kafara kwa Waafrika hasa, kuchukua hatua wao wenyewe bila kungoja uongozi na utawala usiowajali. Hili linawiana na kauli ya akina Moore (2017; 2018), Garrard (2023) na Filipova (2023) kuwa watu wote kwa jumla bila kuangaza uongozi pekee wana jukumu la kuyawajibikia na kuyasikitikia mazingira kwa njia moja au nyingine bila kutarajia malipo yoyote. Aidha, Waithiru (2022d) anaongeza kuwa, binadamu ana wajibu wa kuyatunza na kuyahifadhi mazingira yake kwa njia madhubuti zenye haki na usawa kwa mazingira kwa ujumla. Kutokana na kauli za wataalamu hawa mtafiti katika utafiti huu alitambua kuwa, hakika bila binadamu kujitolea na kujitoa mwenyewe, itakuwa vigumu kwa ulimwengu kumudu mabadiliko ya tabianchi bila uhai wa viumbe kuhatarishwa.

Mwandishi kupitia mhusika Pasta Yona wa Yona kwa mfano, anaapa kuwa ikiwa serikali haitachukua hatua kali dhidi ya kiwanda cha kemikali cha Sagasaga basi yeye atafunga kula na kunywa na hatimaye, kuitisha mgomo na maandamano ya wananchi wote wa Siza kukemea na kukashifu uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Kujitolea kwa mhusika Pasta Yona wa Yona ni kiini cha mafanikio katika juhudi za uhifadhi wa mazingira. Mwandishi Mbogo anatumia mifano ya kujitolea kwake kwa shughuli za uhamasishaji wa umma kuhusu madhara ya mazingira chafu na dhoofu, kampeni za usafi hasa pale hotelini, na elimu ya umma ili kuonyesha mafanikio ya juhudi zao wote. Kujitolea huku kunawawezesha wahusika wengine na jamii kuungana katika juhudi za uhifadhi, na mwandishi anasisitiza kwamba bila kujitolea, harakati za kuhifadhi mazingira haziwezi kufanikiwa. Hakika bila ukakamavu na kujitolea kwa kila mja, mazingira chafu yataendelea kuyadidimiza maisha ya viumbe kutokana na maradhi aina aina yanayotokana na mazingira yaliyonajisiwa.

Mwandishi Mkangi katika riwaya yake ya *Mafuta* anapendekeza juhudi za binadamu, kujitolea na kujitahidi kama mbinu kabambe ya kukabiliana na wanaoyachafua na kuyaharibu mazingira kwa ujumla. Kupitia juhudi za mhusika Sifa katika *Mafuta*

anaweza kukabiliana na ufukara, mazingira chafu na ya kubagua pamoja na hali ngumu ya maisha. Kwa mfano, Sifa anatia bidii peke yake na anakusanya mbawa nyingi zaidi za gredi wani. Mbawa hizi zinamwezesha kupata ziada ya kutosha kuwaajiri watu wengine kama vibarua. Hili linasaidia kudidimiza umaskini. Biashara yenyewe ilipanuka na Sifa akafanikiwa kukabiliana na mazingira chafu kupitia vita dhidi ya ukame na uhitaji. Hatimaye, Sifa anajinunulia kichuguu chake mwenyewe. Uchumi imara husaidia katika uhifadhi wa mazingira kuliko uchumi duni. Hili linawiana na kauli ya Falola (2024b) kuwa, uchumi wa Afrika hutaimarishwa na Waropa ambao lengo lao ni kuunyonya uchumi wa Afrika bila kuliendeleza bara la Afrika. Hivyo, ni wajibu wa Waafrika kuyalinda mazingira yao na kuimarisha chumi zao.

Waandishi Mbogo na Mkangi wametumia ufananisho na taswira ili kuimarisha ujumbe wa ukakamavu na kujitolea kwa binadamu katika harakati za uhifadhi wa mazingira. Matahalani, ufananisho wa miti inayokauka katika *Walenisi* na mazingira duni katika *Mafuta* inaonyesha haja ya ukakamavu na kujitolea katika juhudi za kuyatunza mazingira. Taswira ya joka kubwa katika *Bustani* inaonyesha uthabiti wa asili na umuhimu wa kulinda misingi ya mazingira dhidi ya uharibifu. Hili linawiana na taswira za wanyama zinazosawiriwa na Momanyi katika *Nakuruto* walioko hatarini na mazingira yanayoharibiwa zinaonyesha haraka na umuhimu wa kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira. Hizi taswira zinaongeza nguvu ya maelezo na kuhamasisha wasomaji kuchukua hatua.

Waandishi hawa wawili wanadhihirisha jinsi ukakamavu na kujitolea vinaweza kubadilisha mtazamo wa kitamaduni na kijamii kuhusu uhifadhi wa mazingira. Mwandishi Mbogo anaonyesha jinsi jamii ya Siza katika Bustani ilivyokuwa ikipuuza mazingira hapo awali na jinsi juhudi za mhusika Pasta Yona wa Yona zinavyobadilisha hali hii. Kwa kuonyesha mabadiliko haya, mwandishi Mbogo anasisitiza kwamba uhifadhi na utunzaji wa mazingira ni jukumu la pamoja linalohitaji ukakamavu wa pamoja na kujitolea kutoka kwa kila mwanajamii. Kupitia mtazamo wa watunzi Mbogo na Mkangi, sifa za ukakamavu na kujitolea zinaonekana kama nguvu za lazima katika kukabiliana na changamoto za kimazingira. Waandishi wanawatia moyo wasomaji kuelewa na kuthamini umuhimu wa kujitolea na ukakamavu katika juhudi za kuhifadhi mazingira, akisisitiza kwamba ni kupitia hatua hizi tu tunaweza kuhakikisha dunia yenye siha kwa viumbe hai wote.

### 6.4 Nafasi ya Utu katika Uhifadhi wa Mazingira: Sauti ya Mwandishi

Ingawa inadhihirika kuwa mataifa changa barani Afrika yananyongwa na maradhi, ufukara, na chakula hatari kwa afya ya wananchi katika mazingira chafu na yaliyoharibiwa, Swaleh na Timammy (2019) wanapendekeza kuwa suluhu lipo barani Afrika na ulimwenguni katika misingi ya utu. Maathai (2009) anapendekeza kuwa, ushirikiano, utu na huruma ni mambo yanayoweza kusaidia pakubwa kukabiliana na uchafuzi na unajisi wa mazingira kwa ujumla. Aidha, fasihi mara nyingi hutumia kaulimbiu za utu ili kuangazia masuala muhimu ya kijamii na kimazingira. Uchambuzi wa kipengele hiki ulizingatia jinsi mwandishi anavyoonyesha dhana ya utu katika muktadha wa uhifadhi wa mazingira. Hivyo, iliangazia jinsi utu unavyofanikisha uelewa wa kina wa wajibu wa binadamu katika kulinda na kuhifadhi mazingira. Waithiru (2022d) anaongeza kuwa, utu huwa kigezo kikuu cha nguzo ya utamaduni wa mazingira ya Nadharia ya Uhakikimazingira.

Mathalani, mwandishi Mbogo kupitia mhusika Jonalisti anaonyesha mchango wa utu katika ujenzi wa ubinadamu kwa ujumla. Jonalisti baada ya kushuhudia Franco na Kidonda Zambarau wakila chakula kilichoharibika pale kwenye dampu la Siza, anawapa kila mmoja noti ya shilingi mia mbili. Mwandishi wa *Bustani* anapendekeza kuwa, utu ni mbinu mwafaka katika kukabiliana na uchafuzi na udhoofishaji wa mazingira. Mtunzi Mbogo kupitia utu wa mhusika *Advocate* Mwaka anaonyesha mchango wa utu katika kukabiliana na wachafuzi na wanajisi wa mazingira. Bwana Abdula – mchafuzi wa mazingira – alimjua *Advocate* Mwaka na pia jiji lote la Nomila lilimfahamu vyema. Hii ni kwa sababu, *Advocate* Mwaka hakuwa tu wakili wala mtetezi tu wa wanyonge, ila alikuwa Profesa wa Sheria katika Chuo Kikuu cha Nomila. Alifahamika kutokana na utu wake wa kujitolea kwake kwa kila mara kuwatetea mahakamani wafanyakazi na wakulima wa kiwanda waliokuwa, aghalabu, wakinyanyaswa na kunyimwa haki zao na matajiri kama vile Bwana Abdula ama hata na serikali. Hakika hili linafungamana na nguzo ya uwezo ambapo mataifa tajiri na yenye uwezo huyadunisha na kuyapujua mazingira ya mataifa duni uliwenguni.

Katika mazingira duni, chafu na tasa, viongozi na matajiri hawawasikitikii wala kuwajali wananchi. Kulingana na mtunzi Mbogo kupitia mhusika Baba Mohamed katika *Bustani*, katika kiwanda cha kemikali cha Sagasaga wafanyakazi hawana vifaa vya kutosha vya kujikinga na madhara ya gesi na makemikali mengine mengi. Anapendekeza haja ya kuwepo kwa utu baina ya waajiri ili kuwapa sare wafanyakazi

wote inayosaidia kuwalinda. Katika mazingira duni wafanyikazi hutagusana na kemikali bila kujilinda wala kuyasikitikia mazingira yenyewe kutokana na ukosefu wa utu. Uhusiano kati ya waajiri na waajiriwa huwa wa maangamizi ila si wa utu. Njia anazotumia mwanadamu kuingiliana na mazingira bila utu zinazalisha uharibifu wa mazingira zaidi kuliko uhifadhi wa mazingira.

Kwa mujibu wa waandishi Mkangi na Mbogo mabadiliko ya tabianchi hunawiri katika mazingira yenye ukosefu wa ajira, yenye ufisadi na ufukara tele kama zao la ukosefu wa utu. Mwandishi Mkangi anamwonyesha mhusika Dzombo jinsi anavyokua kupitia kujifunza umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Mhusika huyu pamoja na watu wengine duniani walianza na mitazamo ya ubinafsi, lakini kupitia safari zao za kibinafsi na mapambano na uharibifu wa mazingira, wanaanza kuelewa na kuthamini utu na umuhimu wa kujali dunia yote. Katama Mkangi anaonyesha mabadiliko haya kwa kutumia maelezo ya kina ya hisia na hatua za wahusika, akisisitiza jinsi utu unavyoweza kuleta mabadiliko chanya katika juhudi za uhifadhi. Kuijtolea kwa wahusika katika kuhifadhi mazingira kunachochewa na hisia za kina za utu na huruma. Mtunzi Mkangi kupitia mhusika Dzombo katika Walenisi anaonyesha jitihada za binadamu wanaopanda miti, kuendesha kampeni za usafi, na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa mazingira, ili kuonyesha jinsi utu unavyoweza kuwa chanzo kikuu cha msukumo wa kuhifadhi mazingira.

Mtunzi Mbogo anapendekeza utu kama mbinu nzuri ya kuhimiza uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Kupitia mhusika Doricas anaeleza kuwa, tangia hapo mwanzo pale Siza watu walipinga sana suala la kuweka kiwanda cha kemikali cha Sagasaga mahali salama kwa afya ya viumbe na mazingira kwa jumla lakini viongozi wakawasaliti kutokana na ukosefu wa utu. Kupitia mhusika Pamela anathibitisha kuwa, ingawa wananchi wengi walipinga kiwanda cha Sagasaga kinachoendeleza unajisi wa mazingira pale Siza, viongozi wa siasa waliziona pesa bora kuliko uhai wa watu. Hili linafungamana na nguzo ya maendeleo endelevu ambapo kutokana na tamaa na ukosefu wa utu, binadamu huelendea kuyanajisi mazingira yake katika harakati za kujiendeleza kiuchumi. Mwandishi Mbogo ameonyesha jitihada za wahusika za kiutu katika harakati za uhifadhi wa mazingira. Kwa kuonyesha jitihada hizi, mwandishi Mbogo anasisitiza kwamba kuhifadhi mazingira ni tendo la kiutu linalotegemea kujali na kujitolea kwa wengine.  Mwandishi Mbogo katika *Bustani*, kupitia mhusika Jonalisti anadhihirisha kuwa, watu wanafaa kuwajibikia vita dhidi ya uchafuzi na

uharibifu wa mazingira kwa hiari yao bila kungoja viongozi wengine wazalendo wanaopata vikwazo kutoka kwa viongozi fisadi, dhalimu na binafsi barani Afrika. Emmanuel Mbogo katika *Bustani* anapendekeza matumizi ya mipango madhubuti ya kukemea unajisi wa mazingira na ongezeko la tabianchi ulimwenguni kwa kujikita kwenye utu.

Mtunzi Mkangi kupitia mhusika Dzombo katika *Walenisi* anadhihirisha kuwa, utu ni ala mwafaka ya kukabiliana uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya binadamu. Hii ni kwa sababu, utu unatatua asilimia kubwa ya mabadiliko ya tabianchi, hewa chafu, mchanga ulionajisiwa na kemikali pamoja na utupaji taka na umwagaji maji na kemikali sumu na hatari kwa uhai wa binadamu ovyo katika maeneo yasiyoruhusiwa hasa katika mito, maziwa na bahari. Katama Mkangi katika *Walenisi* anadokeza kuwa, utu unaondoa umaskini na utegemeaji wa aidha taifa kwa lingine au hata mtu kwa mwingine. Kutokana na utu wananchi wana makao; uzinzi huna nafasi; majaa ya takataka yenye uvundo na inzi chungu nzima ni safi na ya kuvutia; hamna watoto chokora mijini na mitaani; watu wamejiweza kiuchumi hawapatikani wachoma mihogo na mahindi njiani na mengine mengi mazuri. Hakika hili linadhihirisha kuwa utu husaidia sio tu kuyahifadhi mazingira ya binadamu bali pia utamaduni, maadili, historia na itikadi za jamii ulimwenguni kwa ufanisi mkubwa kuliko mbinu nyingine mbadala. Ikumbukwe kuwa utu ni kigezo cha nguzo ya utamaduni na mazingira katika harakati za uhifadhi wa mazingira.

Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa, uchoyo unadidimizwa, uvivu unakemewa na kutoweka, dhuluma zinaangamizwa na kusahaulika, yote kutokana na utu. Anasisitiza kuwa utu hudidimiza uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya binadamu kwa ujumla kwa kiwango kikubwa sana. Anadhihirisha na kuthibitisha hili kupitia mhusika Dzombo anapoeleza kuwa, utu unahifadhi vijiji, miji, mashamba, viwanda, mbuga, misitu, mabonde, pamoja na vilima na milima. Hili linadhihirisha uwezo wa utu kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa aina aina maadamu utu unahifadhi viziwa na maziwa; mito na vijito pamoja na bahari na pwani. Haya yote yanashuhudiwa na Dzombo katika safari ya utu. Utu unazalisha uhifadhi na unakuza mabustani yenye matunda mengi ya kila aina. Mtunzi Mkangi anasisitiza kuwa, utu unapalilia uhifadhi wa Bustani ya Edeni ambayo haijanajisiwa na shughuli za kila siku za binadamu za kujiendeleza ambazo huyapujua na kuyanajisi mazingira kwa ukatili mkuu. Katika Bustani ya Edeni, kila aina ya maembe, mananasi, machungwa, machenza, mabibo,

mapera, matomoko, mafenesi, na mengine mengi yamezagaa. Hakika utu unapalilia uhifadhi wa mazingira kwa kiwango kikubwa sana. Hali hii inawiana na nguzo ya utamaduni na mazingira.

Zaidi ya hayo, mtunzi Mkangi anaeleza katika *Walenisi* kuwa, utu unapalilia uhifadhi na utunzaji wa mbuga zinazosheheni vilima ambavyo katikati vijito vya maji safi meupe vinatiririka. Dari ya mawingu tofautitofauti inajitandaza juu ya Bustani ya Edeni. Upepo wa kuburudisha na mwororo unapepea mazingira yasiyochafuliwa na shughuli za binadamu za kiuchumi. Taswira na ufafananisho zimetumiwa n waandishi wote wawili kwa ustadi ili kuimarisha ujumbe wa utu na umuhimu wake katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Mathalani, taswira ya Bustani ya Edeni inayotunzwa vizuri katika *Bustani* na *Walenisi* kama mfano wa ulimwengu unaohitaji uhifadhi na utunzaji, inaonyesha jinsi utu unavyohitajika katika kila hatua ya uhifadhi. Mtunzi Mbogo anaonyesha ufananisho wa dunia kama mama anayehitaji ulinzi na upendo wa watoto wake katika *Bustani* unaoongeza kina cha maelezo na kuhimiza wasomaji kuchukua hatua za kuhifadhi kwa misingi ya utu.

Hili linawiana na kauli ya akina Watson na Watson (2007) kuwa, utu ni ala mwafaka na madhubuti ambayo hutakasa na kutawaza ulimwengu kutokana na najisi ya mazingira na maadili dhoofu. Kwa mujibu wa Katama Mkangi, utu ni mapenzi yaliyokita nguzo katika nidhamu na nidhamu yenyewe iwe chemichemi yake ni akili ya ufafanuzi-tambuzi. Utambuzi kuwa mazingira chafu na yaliyoharibiwa huwafunga watu kwenye utumwa wa kimawazo, kihisia, kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa jumla na hivyo kudidimiza utu huku dhuluma, maonevu, maradhi na maafa yakishamiri. Ndiposa Katama Mkangi anaeleza kuwa utu huwapa watu ufunuo wa utambuzi pamoja na ushirikiano. Riwaya zake za *Mafuta* na *Walenisi* zinachunguza namna utu unavyoweza kubadilisha mtazamo wa kitamaduni na kijamii kuhusu mazingira. Kwa kuonyesha jinsi wahusika wanavyobadilika kutoka kwa ubinafsi hadi kwa jamii inayoyajali mazingira, mwandishi Mkangi anaonyesha kwamba utu unaweza kuwa na athari kubwa katika mabadiliko ya kijamii na kimazingira. Mwandishi Mkangi anaonyesha kwamba wakati jamii inapoongozwa na utu na huruma, inaweza kufanikisha malengo makubwa ya uhifadhi.

Katama Mkangi kupitia dibaji ya kijitabu cha maelezo anachopewa mhusika Mtu-Dzombo anaangaza ujumla wa uchumi-jamii wa jamii ya Walenisi ambao msingi wao

mkuu ni utu. Utu unawawezesha Wawalenisi kutambua ya kwamba, Walenisi ni nchi yao na hivyo hata uchumi ni wao. Utu unawawezesha kuondoa ubaguzi baina yao, ukabila na ubepari. Utu unawafanya wote wawe sawa na hivyo kuweza kukabiliana na uongozi dhalimu, ukoloni mamboleo, uchafuzi na uharibifu wa mazingira pamoja na ufukara kwa ufanisi. Hili linawiana na kauli ya Waithiru (2022c; 2022d) kuwa, utu humsaidia binadamu kujinyonyoa ubawa wa kudhibitiwa na mkoloni chini ya mfumo wa ukoloni mamboleo ulimwenguni. Utu unawapambanulia kuwa kile wapandacho ni chao; kile wavunacho ni chao; kile wavumbuacho ni chao; na kile walishacho ni chao pia. Hivyo, utajiri wote wa mali yote ni yao wao Wawalenisi kama umma. Utu unawafafanulia kuwa, kila mmoja ni umma. Hivyo, yeyote yule Mwalenisi anayepuuza mali ya umma, basi wa kwanza anayepuuza na kumzorotesha ni yeye binafsi. Aidha, utu unawatahadharishia Wawalenisi kuwa wasije wakageuzwa kuwa watumwa na vyombo vyao vya utaalamu. Hii ndiyo sababu, maendeleo yao yamejikita kwenye ukweli kuwa, wavitumie na wavitawale vyote waviumbavyo na wavibunivyo, madhali ndilo shina la maendeleo na ustaarabu wao, kurahisisha maisha ya kila Mwalenisi bila ubaguzi.

Hivyo, mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa, utu ni kipengele muhimu kinachoweza kuhamasisha na kuleta mabadiliko ya kudumu katika uhifadhi wa mazingira. Tofauti na Walenisi, Duniani hamna utu ila ubaguzi, manyanyaso, udhalilishaji, ukoloni mamboleo, uongozi na utawala dhalimu, utumwa pamoja na unajisi wa mazingira na vilivyomo – anthroposenia kwa kijumla – , matendo na matukio ambayo huwafanya wananchi hasa katika mataifa fukara ya Afrika kuwa watumwa katika taifa lao (Huggan na Tiffin, 2010).

Waandishi Mkangi na Mbogo wanasisitiza kuwa, katika mazingira yanayotawaliwa na udhalimu, maonevu na manyanyaso, watu wanaumizana, wanachukiana, wanatesana, wanamalizana, wanachinjana ingawaje hawalani nyama wanadumisha ulofa. Hakika rai ya mwandishi Mkangi ya kutumia utu kukabiliana na unajisi wa mazingira kama ala mwafaka na madhubuti inatiwa uzito na nguzo ya utamaduni na mazingira ambapo kila utamaduni huhimiza maadili na utu kama kigezo msingi na thabiti cha kuzihifadhi chemichemi za maji, mito, maziwa, bahari, misitu, milima na katika kutathmini njia anazotumia binadamu kutagusana na mazingira. Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa, tukiwa na utu kama binadamu tutatambua kwamba ubinadamu wetu ni wa thamani kuliko vyombo vya mikono yetu, madhali vinafaa

kurahisisha, kudumisha na kustarehesha maisha yetu, ila si vya kututawala sisi wanadamu. Kimsingi, anasisitiza kuwa utu ukiondoa upofu ulimwenguni giza litatokomea mbali na kupelekea kufifia kwa ufukara, uongozi na utawala dhalimu na dhuluma za kila aina duniani. Mtunzi Mkangi anadhihirisha kuwa, uchafuzi na uharibifu wa mazingira unafaa kukemewa na kila kiumbe. Hii ni kwa sababu, athari zake hasi huviathiri viumbe vyote, hai na visivyohai.

Mathalani, kupitia mhusika Dzombo, mwandishi Mkangi anafafanua kuwa, anthroposenia ni kiza kikuu ambamo binadamu huishi. Katika mfumo wa uongozi dhalimu na ukoloni mamboleo binadamu anakumbana na dhuluma kati ya binadamu wenyewe pamoja na uvundo wa maradhi ya kitabaka kati ya watu. Isitoshe, udhalimu na unajisi wa mazingira hutawaliwa na mayowe ya njaa na ufukara na hatimaye maafa. Hivyo, binadamu hana budi ila kuukumbatia utu. Mwandishi anafafanua kuwa, vita dhidi ya udhalimu ambao uliashiriwa na Wachuna katika *Walenisi* havikufaulu kwa kuwa umma ulikuwa unapigana na mtu bali vilifua dafu madhali vilikuwa vita ya utu dhidi ya udhalimu.

Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa, utu ulipalilia ukweli, mapambazuko na ufahamu ilhali udhalimu ulipalilia unyama, hila na giza. Utu ulizalisha mapambazuko mapya yaliyoasisi ujenzi wa ulimwengu mpya usio na ubaguzi, ufukara na unajisi wa mazingira. Utu unachomoza jua la ufahamu unaozidi kuangaza na kuwapa watu ufunuo. Ufunuo huu unawasaidia kutambua hila na unyama uliokuwa ndani ya jina la ulimwengu wao. Jina lile lilikuwa WALENI lililomaanisha kuwa "Wale ni Waliwe". Utu uliwasaidia kuligeuza likawa WALENISI. Hili nalo likamaanisha kuwa, "Wale ni Sisi na Sisi tu WALE." Hivyo, utu ulizalisha umoja usiobandukika uliodidimiza uharibifu wa mazingira, maonevu, ubaguzi na dhaluma nyingi. Hii ndiyo sababu, Wawalenisi walianza kuitana *Mtu* kabla ya kutaja jina la mhusika kwa minajili ya kusisitiza utu kati yao. Kupitia utu mwandishi Mkangi anadhihirisha kuwa, uongozi mbaya ambayo ni nguzo ya Uhakikimazingira unaweza kutatuliwa na utu ili kujenga mazingira safi ya kizazi cha leo na kesho.

Kwa misingi hii, mwandishi Mkangi kupitia mhusika Mtu-Dzombo wa Bedzombo anasisitiza umuhimu wa utu kama ala mwafaka ya kukabiliana na mazingira chafu, uongozi dhalimu na maonevu na manyanyaso baina ya binadamu na kwa mazingira. Ndiposa anasisitiza kuwa, kupitia utu, kila mja anafaa kutia juhudi kila siku, awe na

Juma la Mwangaza, Mwezi wa Ufahamu pamoja na Mwaka wa Usawa katika ulimwengu wa Walenisi usiokuwa na hata chembe ya dhuluma. Hivyo, utu ni namna mwafaka na madhubuti ya kukabiliana na dhuluma anazokumbana nazo mwanadamu pamoja na udhalimu dhidi ya mazingira kwa ujumla. Hali hii inafungamana na nguzo ya uongozi mbaya pamoja na ile ya utamaduni na mazingira ambapo maadili ya binadamu hususani anavyoshughulikia uhifadhi wa mazingira hupigwa msasa.

Mwandishi Mkangi kupitia Thome Kuu katika *Walenisi* iliyomo Mapenzoni, anataja kuwa ina lengo moja tu. Tofauti na serikali ambayo kazi yake kuu ni kukana na kuficha tofauti zilizopo kwa kuubatilisha na kuuhepesha ukweli, Thome Kuu jukumu lao kubwa ni kufichua, kuzikubali na tena kuzikabili tofauti zilizopo, kwa minajili ya kuzitatua. Hivyo, lengo kuu la Thome hili Kuu ni kuuimarisha utu wa Wawalenisi. Utu unapewa hadhi na nafasi thamani sana madhali ndio uliowasaidia kuudidimiza udhalimu kwa mkupuo mmoja. Wachuna waliokuwa wakiupalilia udhalimu waliendeleza ubaguzi uliopungukiwa na utu na hivyo udhalimu ulidumu kwa kuwabagua watu kisiri na kwa hila za kila namna. Hakika, utu hutukumbusha kuwa kila spishi, hata ile dhaifu ina jukumu muhimu katika kudumisha usawa wa mazingira. Hili linawiana na kauli ya Filipova (2023) kuwa, binadamu anapopoteza bioanuwai anavuruga uwiano kati ya spishi aina aina na uhifadhi wa mazingira. Hili linafungamana na nguzo ya maumbile ambapo msisitizo wa urari wa viumbe hutiliwa mkazo.

Mwandishi Mkangi kupitia Thome Kuu ya Wawalenisi anahimiza kuwa, utu humhimiza binadamu kushughulikia mabadiliko ya tabianchi kwa dharura. Ongezeko la joto, matukio ya hali ya hewa kali na kuyeyuka kwa barafu kunachangiwa zaidi na uozo wa utu wa binadamu, ambaye huivuruga mifumo ya mazingira kiholela. Hakika tukichukua mtazamo wa utu, tutatambua kuwa matendo yetu yanawaathiri sio tu kizazi cha leo ila cha kesho pia. Hivyo, ni wajibu wetu kuupalilia utu ili kuweza kuhusisha na kushirikisha jamii pana ya ulimwengu, kuweza kuheshimu maarifa ya kienyeji na kuwawezesha watu kuwa walinzi wa mazingira yao. Juhudi za uhifadhi wa mazingira zinafaa kuzingatia mila, maarifa ya ikolojia ya jadi pamoja na mipango inayoongozwa na jamii. Hali hii inafungamana na nguzo ya utamaduni wa mazingira ambayo huhimiza jamii iwajibikie mazingira bila ubaguzi.

Kulingana na mwandishi Mkangi, utu huwasaidia watu kupiga hatua mbele katika nyanja za ufundi, uhandisi, teknolojia na sayansi kimwavuli. Hivi husaidia sana katika harakati za kuzalisha usawa, mapenzi na ufanisi baina ya wanadamu. Hili linalandana na kauli ya akina Watson na Watson (2007) kuwa, utu ni kigezo kikuu katika mchakato wa kukabiliana na udhalimu na utumwa, sio tu baina ya binadamu na binadamu ila baina ya binadamu na mazingira yake. Hakika utu huimarisha uhusiano kati ya watu na hususani kati ya binadamu na mazingira yake. Isitoshe, utu kwa mujibu wa nguzo ya maendeleo endelevu huwa msingi katika kupalilia uhifadhi wa mazingira katika harakati za kuafikia malengo endelevu. Ingawa hili ni kinyume na nguzo hii inayosisitiza kuwa, kama binadamu huwezi ukahujumu kiumbe kimoja kisha ukadai kuwa unajiendeleza, utu unapenyeza usawa kati ya viumbe vyote na mazingira yao kwa ujumla bila kuangazia mazingira ya matajiri pekee na kuyapuuza ya wanyonge. Hali hii inawiana na nguzo ya uwezo inayodokeza kuwa, mazingira ya matajiri hutunzwa kwa ungalifu katika shughuli za kuzalisha maendeleo kwenye taifa husika huku ya wanyonge yakitumiwa kama dampu la kusombea taka za kila aina.

Mwandishi Mkangi kupitia wimbo wanaouimba Wawalenisi wote wakiwa wameshikana mikono wakiwa kwenye duara katika *Walenisi*, unamfanya Mtu-Dzombo wa BeDzombo kudondokwa na machozi ya furaha baada ya kugundua Utu wake. Kupitia mhusika Mtu-Dzombo anayekumbuka ubaguzi ulio duniani mwandishi anatuonyesha haja ya utu katika kuimarisha usawa wa kimazingira. Mwandishi anasisitiza kuwa, uchambuzi wa kina wa utu katika fasihi huonyesha tofauti katika athari hasi za mazingira. Uongozi duni mara nyingi unasababisha ubaguzi pamoja na ukosefu wa haki za mazingira. Jamii katika maeneo yaliyotengwa huteseka zaidi kutokana na uchafuzi wa mazingira, ukosefu wa maji safi na usimamizi duni wa taka. Anahimiza kuwa utu husaidia kutambua tofauti hizi jambo ambalo ni muhimu kwa mabadiliko yenye maana.

Waandishi Mkangi na Mbogo wanahimiza haja ya kuwepo kwa utu kwa kila mmoja. Kulingana nao, utu una uwezo wa kukabiliana na vijenzi vya udhalimu kwa jumla; kama vile; ubaguzi wa kijinsia na wa kidini, ulofa, watoto na familia za mitaani na vichochoroni, dawa za kulevya, pombe haramu, dhuluma na unyanyasaji, ufisadi, uongozi mbaya, unyakuzi wa mali ya umma, tamaa na ubaguzi wa kila aina. Hivyo, utu kwa kuimarisha usawa huweza kukabiliana na udhalimu kikamilifu. Mwandishi Mkangi anaendelea kusisitiza haja ya kutumia utu kukabiliana na ubinafsi-uchoyo

kupitia safari ya utu katika *Walenisi*. Dzombo katika *Walenisi* anasafiri safari ya kiutu kwa kutumia Trimi mle Walenisi ilhali katika *Mafuta*, Ti anasafiri safari ya utu kwa kutembea na kulala ndani ya kidimbwi kwa zaidi ya juma zima. Anapofika kwa akina Msati, Ti hana tofauti na wenyeji wa mji wa vidimbwi vya matope. Mathalani, anaizoea baridi ya matope, rinda lake linakukutaa kwa kuishi matopeni, ngozi yake inashirai kwa kukosa mafuta na nywele zake zinakuwa timutimu. Hali hii inawiana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo binadamu anasutwa namna anavyotagusana na binadamu mwenzake na mazingira kwa jumla.

Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa, utu huhimiza kilimo endelevu na mifumo ya chakula. Ili kuepuka ukame, binadamu hana budi kuzitema faida za muda mfupi na kuweka kipaumbele cha usalama wa chakula kwa muda mrefu. Mazoea ya kilimo endelevu, upandaji miti pamoja na mtandao wa chakula wa ndani huchangia utu kwa kuhakikisha kuwa vizazi vya leo na vijavyo wanapata lishe bora. Safari inayosawiriwa na mwandishi Mkangi ya Ti kumwona Msati inakuwa kama ubatizo mpya kwake Ti. Ubatizo huu mpya unampa Ti uvumbuzi wa utu wake na hivyo anatambua namna ya kukabiliana na ubaguzi, ubiafsi-uchoyo, ubepari na unajisi wa mazingira. Utu unaangamiza maonevu kikamilifu.

Hakika utu huimarisha nguzo ya utamaduni na mazingira ambapo maadili yanayosisitiza uhifadhi wa mazingira yanapewa kipao mbele. Hili linawiana na kauli ya Philips (2003) kuwa, utamaduni wa kila jamii huna budi kuangazwa katika misingi ya kimazingira, kwa sababu vyote viwili huchangiana na kukamilishana. Utamaduni wa kila jamii hupalilia utu kwa lengo la kuuhifadhi uhusiano wa haki na usawa kati ya binadamu wenyewe kwa wenyewe na kati yao na mazingira yao ila si wa maonevu, ubaguzi, machukizo na manyanyaso. Hivyo, waandishi wa riwaya nne teule wametoa rai kuwa, utu ni ala mwafaka ya kukabiliana na anthroposenia kwa njia madhubuti, nyepesi, mahususi na inayopatikana na yeyote kwa upesi na urahisi. Aidha, wanahimiza kuwa, utu hulingana na kanuni za uchumi wa mzunguko. Hivyo badala ya mfumo wa ‘chukua-tengeneza-tupa,’ binadamu anafaa kujihamasisha kuhusu utumiaji tena, upya na kupunguza taka. Wanahitimisha kuwa, kuchukua mtazamo wa utu, binadamu anaweza kuunda mustakabali endelevu ambapo haki za kijamii na usawa wa mazingira utaongoza kila jambo.

### 6.5 Ushirikiano na Ujasiri katika Uhifadhi wa Mazingira: Mtazamo wa Mwandishi

Kimsingi, uwajibikaji katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za jamii na nchi yoyote ile ni suala msingi. Kwa mujibu wa Seif (2022), viongozi wa jamii yoyote ile wanafaa kuungana na kushirikiana kwa hali na mali katika mambo yote ya kijamii na kimaendeleo, madhali umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Mwandishi Mbogo anasisitiza kuwa watu ndio silaha kuu ya kukabiliana na anthroposenia kupitia umoja, ushirikiano na ujasiri. Mintarafu ya malalamishi ya mhusika Bwana Abdula na wasiwasi wake, inabainika kuwa, watu wakiungana pamoja wana uwezo wa kuutisha na kuudidimiza uchafuzi na uharibifu wa mazingira pamoja na wachafuzi kwa mkupuo mmoja. Kupitia mhusika Abdula mtunzi Mbogo anadhihirisha hili pale ambapo anawaza katika *Bustani* kuwa, "Alifikiri, tufani hii itakuwa si nyingine bali ya hawa watu wanaokipiga vita kiwanda chake cha Sagasaga." (uk. 41). Kimbunga kinachompa kiwewe Bwana Abdula kinaashiria silaha yenye nguvu dhidi ya unajisi wa mazingira ya wanyonge hasa. Bwana Abdula na kiwanda chake cha Sagasaga ni taashira ya wakala wa uharibifu wa mazingira katika mataifa fukara ulimwenguni hivyo mwandishi anatoa rai kuwa watu washirikiane kwa ujasiri kama njia mwafaka ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mwandishi Mbogo anadokeza kuwa, watu wana nguvu dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira, mithili ya upepo unaovuma au kuzunguka kwa nguvu sana, yaani dharuba kali dhidi ya upujufu aina aina. Hivyo, rai kuwa ushirikiano na ujasiri husaidia katika uhifadhi wa mazingira ina mashiko. Vita dhidi ya kiwanda cha Sagasaga vinaashiria vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla. Ingawa binadamu ndiye chimbuko la upujufu wa mazingira, mwandishi wa *Bustani* anaamini kuwa binadamu yuyu huyu ndiye mwafaka katika kukabiliana na upujufu uu huu kupitia ushirikiano baina ya watu kwa ujasiri. Mwandishi Mbogo anasisitiza kuwa, kwa kushirikiana, jamii, serikali na mashirika yanaweza kuleta pamoja maarifa, fedha na teknolojia kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira. Isitoshe, ushirikiano unaweza kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mwandishi Mbogo anahimiza kuwa, kupitia mikakati ya pamoja, tunaweza kufadhili miradi ya kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa na kuzuia athari zake kwa mazingira.

Mwandishi Mbogo katika *Bustani* anasisitiza rai kuwa, umoja na ushirikiano wa kila mja kwa ujasiri ni njia madhubuti na inayohitajika katika harakati za kukabiliana na

uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, ingawa Pamela ni mbishi, anawalazimisha wanawake wenzake washiriki katika majadiliano ya kutafuta suluhu dhidi ya unajisi wa mazingira. Kupitia mhusika Pamela mwandishi Mbogo anaeleza kuwa, madhara ya mazingira chafu na tasa hayabagui wake au waume ila yanaathiri wote kwa pamoja. Ukweli huu unadhihirishwa na Pamela na punde tu baada ya Mama Mohamed na Doricas kupambaukiwa na ukweli huu, wanajiunga na majadiliano. Mwandishi kupitia mhusika Pamela anasisitiza kuwa:

> "Wanawake! Wanaume! Kitu gani hiki, ee! Haya mambo yanatuhusu sote. Hayo madawa ya kemikali ya kiwanda cha Sagasaga yanachagua, ee? Watu wote tunaathirika – kama ni mafua, vikohozi, kupunyuka nywele na saratani bila shaka zinatusubiri. Mungu apishilie mbali." (uk. 65).

Mwandishi Mbogo anatoa wito wa ujasiri na ushirikiano katika kupambana na uchafuzi wa mazingira. Kwa kuchukua hatua za kuzuia na kutoa adhabu kwa wachafuzi, mataifa mengi yanaweza kulinda chimbuko la maji, ardhi na bioanuai. Maradhi kama mafua, vikohozi, kupunyuka nywele na saratani yanashamiri katika mazingira chafu na yaliyoharibiwa kweli. Maradhi ya mafua hutokana na binadamu kupumua hewa chafu na yenye kemikali sumu. Vikohozi zisivyowakoma wenyeji wa Siza katika *Bustani* vinasababishwa na hewa chafu pamoja na dampu la Siza linalofuka moshi kila wakati, usiku na mchana. Katika mataifa mengi ulimwenguni, hususani barani Afrika, matajiri pamoja na viongozi binafsi na waharibifu hujenga viwanda ambavyo huwa vinakiuka sheria na masharti yaliyowekwa na Shirika la Afya Ulimwenguni kwa lengo la kuyahifadhi na kuyalinda mazingira. Hili linawiana na kauli ya Thiong'o (1987) kuwa, mataifa tajiri hujenga viwanda vinavyozalisha kemikali hatari katika mataifa ya Afrika kwa sababu hawana hasara yoyote wakiwaangamiza maelfu ya Waafrika tofauti na wanavyohuzunika wanapowazika wenzao. \

Mwandishi Mbogo anadokeza kuwa, madhara ya mazingira yaliyoharibiwa na chafu husababisha kupunyuka nywele pamoja na maradhi ya saratani jambo ambalo huzalisha maafa kwa kiwango kikubwa. Hali hii huwa ya kawaida katika mataifa fukara kwa sababu matibabu ya saratani hugharimu fedha nyingi ambazo huwa muhali kupatikana miongoni mwa wanyonge. Hivyo, kutokana na ulofa wengi huangamia kutokana na saratani bila hata kufahamu kinachowaangamiza kwa sababu

hata kufanyiwa majaribio na vipimo huwa vigumu kwao. Hii ndiyo sababu, mtunzi Mbogo anatoa rai kuwa ushirikiano na ujasiri ni ala mwafaka na madhubuti, si tu katika kukabiliana na madhara ya mazingira chafu na yaliyoharibiwa ila pia katika kudidimiza vyanzo vya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kimwavuli. Aidha, anahimiza ujasiri katika kubadilisha mifumo ya uwekezaji. Hili anapendekeza kuwa, viongozi wa mataifa mengi ulimwenguni yanafaa kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi ili kufadhili miradi ya mazingira. Hii inahitaji kuboresha mifumo ya uwekezaji na kuonyesha fursa za kibiashara zitokanazo na uhifadhi wa mazingira.

Kulingana mtunzi Mbogo kupitia mhusika Doricas katika *Bustani*, umoja na ushirikiano baina ya wanajamii utachangia pakubwa katika kukabiliana na upujufu wa mazingira. Kwa mfano, baada ya kumpa Samsoni titi anyonye, anawaeleza wote waliokusanyika pale kuwa mna mambo matatu makuu ya kuzingatia katika kukabiliana na unajisi wa mazingira. Kwanza, anataja kuwa suala la uchafuzi uliokuwa unaendelea na maradhi yaliyokuwa yanazidi kuenea miongoni mwa wanajamii lilihitaji litafutiwe ufumbuzi madhubuti. Hata hivyo, anasisitiza kuwa ufumbuzi madhubuti au ufumbuzi wowote ule hauwezi kupatikana bila umoja na ushirikiano baina ya wanajamii. Kwa mfano, anafafanua katika *Bustani* kuwa, "Na ufumbuzi hatuwezi kuupata kama hatuna umoja. Ndiyo maana tumekutana hapa leo." (uk. 65). Mtunzi Mbogo kwa kupitia wahusika akina Jonalisti, Wakili Mwaka, Baba Mohamed, Kepteni, Samsoni, Eliya, Doricas, Pamela, na Mama Mohamed anaashiria wanajamii wanaokabiliana na upujufu wa mazingira kila uchao. Uvumbuzi huwa silaha mwafaka katika kudidimiza upujufu wa mazingira ulimwenguni. Hivyo, rai kuwa umoja na ujasiri hupalilia uvumbuzi ni kweli na inayoendeleza uhifadhi na ukuuzaji wa mazingira safi na yanayonawiri.

Jambo muhimu na la maana katika kukabiliana na unajisi wa mazingira ni ushirikiano na ujasiri. Mwandishi Mbogo kupitia mhusika Pamela anasisitiza umuhimu wa ushirikiano anapoeleza katika *Bustani* kuwa, "Kuna haja ya sisi sote kuungana – la sivyo matajiri wa Sagasaga watatumaliza." (uk. 65). Ushirikiano katika vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira unafanikisha shughuli hii. Hii ndiyo sababu, watu wengi wanashirikiana kwa ujasiri katika maandamano yanayonuia kukemea upujufu wa mazingira kwa sauti na kauli moja yenye nia safi juu ya mazingira.

Katika maandamano, watu walikuwa wengi. Watoto wengine walianguka kisha wakasimama tena. Wengine walianguka wakaumia lakini palitokea mtu akawasaidia. Mwandishi anaeleza katika *Bustani* kuwa, “Wimbi lile la watu lilikuwa kama kitu kimoja, ndugu mmoja na damu moja. Maandamano sasa yalifika karibu na Dampu la Siza. Watu walipiga yowe na kulikemea dampu lile.” (uk. 91). Ushirikiano na ujasiri katika maandamano unaibuka kama ala mwafaka na madhubuti ya kuukemea uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Katika mataifa mengi fukara ulimwenguni, maandamano hutumiwa na wananchi kama njia ya kujieleza kwa kuonyesha kutofurahishwa au kutopendezwa na jambo fulani. Hivyo, ushirikiano kwa ujasiri katika maandamano dhidi ya unajisi wa mazingira ni njia inayodhihirisha ukomavu katika kukabiliana na madhara ya mazingira yaliyopujuliwa.

Kwa mujibu wa mtunzi Mkangi katika riwaya ya *Walenisi*, ujasiri ni ala mwafaka ya kukabiliana na ufukara, ubaguzi, dhuluma na utasa wa kimazingira. Anadhihirisha hili kupitia mhusika Dzombo anayeeleza kuwa, hatua thabiti ya kijasiri ilimfaa sana katika kulishinda *Jabali la Magonjwa* ambalo linaashiria mazingira gonjwa na dhoofu yanayotawaliwa na ndwele aina aina. Hivyo, kwa mujibu wa waandishi Mkangi na Mbogo, ushirikiano na ujasiri ni njia mwafaka ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Mathalani, kijana Mtu-Wazo anaeleza katika *Walenisi* kuwa, “... ulichukua muda mrefu ... kabla ya wao kutambua kwamba adui wao alikuwa mmoja na hawakuwa na budi bali kufungamana kwenye nia moja na kuwa na lengo moja.” (uk. 53). Ingawa mtunzi Mbogo katika riwaya yake ya *Vipuli* anaisawiri hali ya Eliza kama ya kutamausha kupitia sauti ya mtoto Eliza inayosema kuwa, “Mamaa! Nakufaa!” (uk. 121), anadokeza kuwa kuna matumaini ya mataifa ya Afrika kuweza kuukabili unajisi wa mazingira kupitia ushirikiano wa mataifa jirani ya Afrika.

Mwandishi Mbogo anadhihirisha hili katika *Bustani* kupitia mpangaji jirani anayezisikia sauti za yowe za Eliza na kuja mbio kumnusuru kutoka mikononi mwa simba-mwitu – Nyau – ambaye anaashiria namna mataifa yenye uwezo huyanajisi mazingira ya mataifa duni. Zainabu aliyekuwa amelala kwake, aliamka ghafla usingizini na kukimbia na kuugonga mlango wa Nyau kama askari jela. Hatimaye, watu tele, wengine wakiwa na marungu, wengine nyundo au mitaimbo walifika na wakafanikiwa kumnusuru Eliza na kumpeleka hospitalini. Ingawa Eliza alikuwa amezirai huku damu zinamtoka, Zainabu na watu wengine wanamkimbiza hospitalini bila kusita. Hali hii inaashiria kuwa, pakiwemo na ushirikiano na nia njema, bara la

Afrika linaweza kujikomboa kwa kuukabili unajisi wa mazingira unaosababishwa na matajiri kutoka Afrika na wanaotoka Ughaibuni kikamilifu.

Halikadhalika, mtunzi Mbogo anasisitiza umuhimu wa thamana ya umoja kama mbinu madhubuti ya kukabiliana na dhuluma na unajisi wa mazingira katika riwaya ya *Vipuli*. Hili analifanikisha kupitia kinyago cha mpingo kilichopo pale nje ya Panama International Hotel upande wa nyuma. Dkt Charles anadai kuwa kinyago kile kinadhihirisha watu wanaoonekana kama wacheza sarakasi au wanaocheza ngoma za kitamaduni. Hili linaashiria kuwa, katika umoja, utamaduni kama kitambulisho cha jamii unaweza kutumiwa kukabiliana na udhoofishaji wa mazingira. Kupitia mhusika Profesa Williams mwandishi Mbogo anapambanua kuwa, taashira ya kinyago kile, pamoja na ishara na taswira zake zote si mchezo na kuwa sanamu haionyeshi sarakasi ila sanamu yenyewe inadhihirisha falsafa au itikadi kuhusu maisha ya wananchi wa Daluta. Katika sanamu ile, Profesa Williams anamfafanulia Dkt Charles kuwa, namna watu wanavyoshikana; namna nyuso zao zinavyoonyesha huzuni inayotokana na maisha magumu; na dhiki za kila wakati; namna sanamu yenyewe ilivyo kwa jumla inasawiri falsafa ya wenyeji wa Daluta ya umoja. Mtunzi Mbogo anadhihirisha kuwa, kupitia umoja binadamu anaweza kuikabili na kuisuluhisha anthroposenia kwa wepesi na haraka. Hili analithibitisha kupitia ufafanuzi wa Profesa Williams katika *Vipuli* kuwa:

> “... falsafa yao ni kuwa: ili waweze kuyakabili na kuyadhibiti maisha yao, huzuni na ndoto zao, lazima waishi kikoa; lazima wakamatane, wawe kitu kimoja. Wana msemo usemao: Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.” (uk. 137).

Hakika umoja unadhihirika kuwa mbinu mwafaka katika kuyatatua matatizo yanayosababishwa na mazingira chafu na tasa. Bila ushirikiano, inabainika kuwa hatima ya wanyonge wengi ulimwenguni, hususani barani Afrika itakuwa kifo. Hili linawiana na nguzo ya Nadharia ya Uhakikimazingira ya kifo, ambapo baada ya binadamu kuingiliana na kutagusana na mazingira kwa njia ya maonevu na manyanyaso, mazingira yanamsababishia binadamu ndwele za maangamizi na ukame kutokana na kiangazi au mafuriko. Haya yote huzalishwa na mabadiliko ya hali ya anga ambayo huzalishwa na upujufu wa mazingira kwa ujumla. Upujufu wa mazingira husababisha mabadiliko makuu ya tabianchi ambayo hatimaye hupelekea

mmomonyoko wa udongo, mafuriko, kiangazi, ukame, njaa na halafu maafa ya mimea, mifugo na hatimaye watu. Hili linawiana na kauli ya Wamitila (2010), Njeru na wenzake (2022) na Garrard (2023) kuwa, mabadiliko ya tabianchi yanasababishwa na ufyekaji wa miti na uchafuzi wa mazingira na binadamu bila kujali madhara yake kwa kizazi cha kesho. Hivyo, ushirikiano na ujasiri ni ala muhimu katika vita dhidi ya upujufu wa mazingira.

### 6.6 Matumizi Madhubuti ya Rasilimali Asilia: Mtazamo wa Waandishi

Kupitia wahusika mbalimbali watunzi Mbogo na Mkangi wanatoa rai kuwa, matumizi ya vifaa asilia katika mazingira asilia vinavyopatikana kwa urahisi ni mwafaka, faafu na madhubuti katika harakati za kukabiliana na unajisi wa mazingira. Kwa mfano, majivu toka jikoni yanamwagwa kuzunguka shimo la choo kuondoa harufu harufu na kuwafukuza nzi. Mbinu hii ni ya kitambo lakini umadhubuti wake pamoja na wepesi wa kupatikana huifanya njia kabambe ya kukabiliana na uchafuzi wa hewa, hususani msalani au mahala panapofuka harufu mbaya. Baadhi ya rai walizotoa ni pamoja na matumizi endelevu ya maji na maumbile ili kushughulikia uchafuzi wa mazingira.

#### 6.6.1 Thamani ya Maji katika Ustawi wa Mazingira

Katama Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* anatoa rai kuwa maji ni ala nzuri ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla. Tafakari za Katama Mkangi zinaonyesha kujitolea kwake binafsi kwa uhifadhi na matumizi sahihi ya rasilimali asili. Maji ni kiowevu kinachopatikana kwenye mito, bahari au maziwa na wakati mwingine hutokana na mvua ambacho viumbe hunywa na watu hupikia, huogea au kufulia (Mdee na wengine, 2009; TATAKI, 2013; BAKITA, 2015; Wamitila, 2022). Maathai (2006) anasisitiza kuwa, maji huzalisha mali na chakula cha kutosha na hivyo mna haja ya kuhifadhi chemchemi za maji, misitu, na kuwajibikia utumiaji maji mwafaka. Ikizingatiwa kwamba moto unaashiria uharibifu wa mazingira uzimaji wa moto unaashiria uhifadhi wa mazingira. Mwandishi anasawiri hali hii pale moto unaoashiria uharibifu wa mazingira mtawalia na unaomshambulia Dzombo bila kumtoa hata lengelenge, unazimwa na maji. Hili linaashiria kuwa, maji yana uwezo wa kukabiliana na uharibifu wa mazingira kikamilifu. Njiru (2015) na Simel (2015), wakiyaunga mkono mawazo ya mtafiti wanaeleza kuwa, maji kando na kuosha, na kutakasa, kukuza mimea na chakula, kukata kiu kwa binadamu na wanyama; maji ni uhai. Maji humpa binadamu, mnyama na mmea uhai kwa kukata

kiu na kusaidia kusafirisha viritubishi mbalimbali katika sehemu tofauti za mwili au mmea.

Katama Mkangi kupitia mhusika Dzombo katika *Walenisi* anadhihirisha kuwa maji kando na kukata kiu ni chimbuko cha uhai. Anasisitiza kuwa maji yana nafasi mwafaka katika vita vya kukabiliana na athari hasi za mazingira dhoofu kama vile uchafu, kiu na njaa. Katika riwaya ya *Mafuta* mwandishi Mkangi anatoa rai kuwa, matumizi ya maji ni njia mwafaka na madhubuti ya kukabiliana na utawala mbaya, dhuluma na uchafuzi wa aina aina kwa jumla. Kupitia mhusika Mama Fofi anasisitiza uwezo wa maji wa kukabiliana na dhuluma, machukizo, ubaguzi na manyanyaso baada ya kumwagiliwa maji na Matope na punde uteule ukamtoroka na kumkimbia kuliko janga. Ikizingatiwa kwamba uteule unaashiria unafiki na ulaghai unaogubika na kuulinda ukatili, dhuluma na ubaguzi ulimwenguni, uwezo wa maji wa kudidimiza uteule unaashiria uwezo wa maji wa kukabiliana na dhuluma na maonevu ya kila aina. Hivyo, maji yana uwezo wa kutakasa mazingira tasa na yaliyogubikwa na uchafu wa ubaguzi, maonevu na utabaka.

Kupitia mhusika mama Fofi mwandishi Mkangi anafafanua kuwa, maji hudidimiza na kuuangamiza ubaguzi na utabaka kikamilifu na tena kwa njia nyepesi na rahisi. Katama Mkangi anaendelea kudhihirisha kuwa maji ni ala nzuri ya kukabiliana na dhuluma anaposawiri kitaashira kuwa, maji ni taashira ya ukweli, uhalisia na haki dhidi ya mateso, ubaguzi, utabaka na dhuluma dhidi ya mazingira. Kwa kawaida maji safi huwa na uwazi na pia hutumika kuneemesha na kuwatakasa watu, wanyama, majumba, maeneo mbalimbali, na hata mimea, iwe ni kwa kuoga au kunywa au kubatiza. Hii ndiyo sababu, wateule waliweka mila, desturi na itikadi kuwa, endapo mtu yeyote yule ameoshwa na maji kabla ya kukilalia kitanda, basi milele hangepata fursa ya kukilalia kitanda au kuufaidi utabaka, ubaguzi wala maangamizi. Kwa jumla, maji yametumika na mwandishi kuashiria usoshialisti ambao ni adui ya ubaguzi, ubepari na maangamizi ya watu na mazingira yao. Matajiri wanaichukulia hali hii kama mauti kwao kutokana na tamaa, ubinafsi na unafiki walionao. Mtunzi Mkangi anasisitiza umuhimu wa kuhifadhi makazi ya asili na kutumia maji kwa njia endelevu ili kupunguza uchafuzi na kulinda bioanuwai.

Kwa misingi hii hii, mwandishi kupitia mhusika Ti anasisitiza haja ya kuyatumia maji kupata utulivu na uhuru kwa kujiosha nafsi, mwili na mazingira yake kwa maji.

Mwandishi anaeleza kuwa, karibu machozi yamdondoke Ti anapojisafisha na maji, madhali hakutazamia ukarimu wa kutunukiwa maji ya kujisafishia matope. Baada ya kujiosha na maji na kujipanguza kwa kanga safi anawatambua waliokuwamo mle ndani. Hili linaashiria kuwa maji hutakasa unyama, maonevu na dhuluma na kumpa mtu uwezo wa kuona mambo kwa uhalisi wake ila si kupitia hila na unafiki. Mwandishi anasisitiza haja ya kutumia maji kwa njia ya haki na maadili.

Mwandishi anadhihirisha kupitia mhusika Ti kuwa maji yana uwezo wa kumtoa binadamu ujingani – taashira ya anthroposenia – na kuzalisha uhuru wa kimawazo, nafsi na kimazingira. Katama Mkangi anasisitiza kuwa maji tu ndiyo suluhu la unyama, utabaka, ubaguzi, maangamizi na ufukara kwa kuwa huzalisha utulivu na utu. Hili linadhihirisha kuwa maji ni ala mwafaka ya kukabiliana na unajisi wa nafsi na wa mazingira mtawalia. Hali hii inalandana na nguzo ya haki na maadili ya mazingira ambapo binadamu anahitajika kuingiliana na mazingira kwa mazoea endelevu na ya kimaadili. Mwandishi anasisitiza kuwa matumizi madhubuti ya maji katika mazingira husababisha mazoea endelevu katika kilimo, misitu, na usimamizi wa wanyamapori ambayo ni muhimu kupambana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Aidha, mtunzi Mkangi anaonyesha umuhimu wa kutumia maji kwa njia zinazodumisha usawa wa kimazingira kwa lengo la kuyahifadhi mazingira.

Mtunzi Mbogo anatoa rai kuwa maji ni rasilimali muhimu ya kunyunyizia miche ya miti ili kuongeza idadi ya misitu ulimwenguni. Katika *Bustani* anapendekeza mazoea endelevu kutokana na matumizi madhubuti ya maji yaliyomo ulimwenguni na ya mvua. Mazoea haya ni kama vile, mzunguko wa mazao, uhifadhi wa udongo na usimamizi wa chemchemi za maji – visima, mito, maziwa na bahari – kwa njia endelevu. Kutokana na maelezo yake katika *Vipuli* na *Bustani* anasisitiza kuwa, uwajibikaji katika matumizi ya maji tena ya kiuadilifu kwa mtu binafsi na kwa jamii pana kwa jumla ulimwenguni, huweza kupunguza uchafuzi na kuendeleza siha ya mifumo ya kimazingira. Kwa ujumla, waandishi Mkangi na Mbogo wanatoa rai kuwa, uhusiano wa karibu wa mifumo ya asili na misingi ya kimaadili ya uhifadhi na matumizi ya maji na vyanzo vyao kwa uwajibikaji huchochea kujitolea kwa kina kwa usimamizi wa mazingira. Wote wawili wanaonyesha umuhimu wa usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji na uhifadhi wao katika kushughulikia uchafuzi wa mazingira. Hakika, watu wakizingatia hili watajenga jamii yenye siha, shibe, utulivu na umoja katika siku zijazo endelevu. Hili linawiana na kauli ya Mostafanezhad na

Norum (2021) kuwa, matumizi madhubuti ya maji hujenga ramani ya kufikia usawa wa kimazingira na kupunguza uchafuzi katika anthroposenia.

### 6.6.2 Maumbile kama Msingi wa Mazingira Endelevu

Maumbile ni nguzo mojayazo muhimu iliyoongoza uchanganuzi wa data katika utafiti huu. Kama ilivyotajwa, mhimili huu husisitiza haja ya urari kati ya hali za kimaumbile. Katama Mkangi katika *Walenisi* anafafanua kuwa, maumbile yanaweza kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira yenyewe. Mathalani, kupitia mhusika Mtu-Nasi anaeleza kuwa, Trimi ni mitambo ambayo imeundwa kwa lengo la kujipeleka yenyewe kwa kutegemea kunyonya smaku inayozalishwa na Sayari yao. Mwandishi anakariri kuwa, smaku yenyewe ni nzuri kwa binadamu na mazingira yake. Kwa makini anataja katika *Walenisi* kuwa, smaku yenyewe inapatikana bure, haina kelele na haichafui mazingira. Hili linaashiria kuwepo kwa urari baina ya hali za kimaumbile katika harakati za kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Hili linawiana na kauli ya Amer (2022) kuwa, ulimwengu na maumbile kwa jumla huwasilisha dhana za kitamaduni kwa binadamu hasa kuhusu mazingira yake. Hili humuumba binadamu kimawazo, kihisia, kiitikadi, mielekeo na desturi chanya kuhusu maumbile na hivyo kuchukia na kukemea uchfuzi na uharibifu wa mazingira.

## 6.7 Nafasi ya Mashairi na Nyimbo katika Kuizindua Jamii

Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalum wa lugha ya mkato katika usemi unaoeleza wazo, hisi au tukio juu ya maisha au jambo na hufuata utaratibu maalum wa urari na muwala unaozingatia kanuni za utunzi wa mashairi husika, yawe huru au ya arudhi (Wamitila, 2022). Wimbo nao ni maneno na sauti zilizopangwa kimuziki na huambatana na mapigo ya sauti na ngoma aina aina (TATAKI, 2013; TUKI, 2014). Mwandishi Mbogo anawazindua wananchi kupitia mhusika Jonalisti anaposisitiza mbinu ya kuwahamasisha na kuwachochea wananchi wa Siza dhidi ya shakawa zinazozalishwa na mazingira chafu na dhoofu kupitia uandishi na uchapishaji wa ushairi kwenye gazeti. Mathalani, kupitia mhusika Pasta Yona anafafanua kuwa, kwa kuwaanika viongozi wanaopalilia uchafuzi wa mazingira, kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi wa Siza dhidi ya madhara ya kiwanda cha kemikali cha Sagasaga mazingira yanahifadhiwa kwa njia madhubuti. Mwandishi Mbogo kupitia mhusika Jonalisti anayoyatumia maandishi yanayozingatia urari na muwala – ushairi – kwa lengo la kuwahamasisha wananchi dhidi ya madhara ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaotekelezwa na kiwanda cha kemikali cha

Sagasaga. Ushairi huu unaibuka kuwa ala mwafaka ya kuyapigania mazingira na uhai wa viumbe. Hili linawiana na kauli ya Wamitila (2010) kuwa, fasihi ina nafasi kubwa katika kukemea uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Kulingana na mwandishi Mbogo, baadhi ya njia madhubuti katika kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni kama vile; mapambano ya kisheria, maandamano, barua za kushutumu serikali, propaganda magazetini, redioni, televisheni na vyombo vingine vya chapa na vya kielektroniki vya habari. Kiuyakinifu, njia hizi hufanikishwa kupitia matumizi ya mashairi na nyimbo kwa lengo la kuwahamasisha wananchi na kuwaelimisha kuhusu haja na umuhimu wa kuyatunza mazingira yao. Hili linawiana na kauli ya Sritama (2022) kuwa, mna haja kubwa ya binadamu kuzinduka kutoka lepe la mapuuza ya madhara ya shughuli zake dhidi ya mazingira yake kimwavuli. Butler (2024) anaongeza kuwa, binadamu akiendelea kuzika kichwa mchangani huku kiwiliwili kikiteketezwa na fukuto la mazingira chafu kutokana na anthroposenia hamtakuwa na ulimwengu wa kutunza wala wa kuyatunza kwani watakuwa wameangamia. Feder (2022) anasisitiza kuwa, anthroposenia inahitaji ukakamavu kutoka kwa kila mja kuikabili ikiwa binadamu atakuwa na kesho yenye matumaini, shibe na siha tele. Hakika, haya yote ni kweli na yatawezekana baada ya binadamu kumaizi na kupambaukiwa na madhara ya mazingira dhoofu bila kuyapuuza. Kupitia mashairi na nyimbo mwandishi Mbogo anamzindua binadamu na kumtia chonjo katika vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mbinu nyingine anayorai itumike kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni ile ya matumizi ya wimbo kuwahimiza wananchi kudumisha usafi wa hewa na mazingira kwa ujumla. Kwa mfano, kupitia ngoma ya mdundiko inayoambatana na wimbo wa Abdula na Cel katika *Bustani* unawasisimua wahusika wengi kama vile, Pasta Yona wa Yona, Pamela, Wakili Mwaka, na wengine wengi. Wengine wote wanajitupa uwanjani na kucheza huku wakikemea uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Wanaimba na kutaja kuwa, kutokana na unajisi wa mazingira, mazingira yamechafuka na vidonda vimo kichwani. Wanapotaja haya wanainua mikono juu kuashiria kutamauka na pia wanashika vichwa vyao kuashiria maradhi ya vipele vichwani, kutokana na hewa chafu.

Mwandishi Mbogo anasawiri madhara ya mazingira chafu kwa binadamu, wanyama na mazingira yenyewe kupitia maradhi na maafa yanayowakumba wakaazi wa mji wa Siza katika *Bustani*. Kwa mfano, anafafanua namna nywele za wenyeji wa Siza zinavyopunyuka kutokana na maradhi ya saratani yanayosababishwa na uchafuzi na uharibifu wa hewa na mazingira kwa jumla. Hakika maradhi ambayo husababishwa na mazingira chafu kama vile ya saratani huwalemea maskini zaidi kuliko matajiri. Hii ndiyo sababu wengi ambao huangamia kutokana na madhara ya mazingira chafu ni wanyonge huku matajiri wakihamia mataifa ya Ughaibuni na kupata matibabu ya kipekee. Aidha, uchumi wa mataifa fukara huendelea kudidimizwa na madhara ya mazingira chafu na dhoofu ulimwenguni. Hali hii inafungamana na nguzo ya uwezo na kifo ambapo mataifa yenye nguvu huyachafua mazingira ya mataifa duni.

Kupitia wimbo, mwandishi Mbogo anawahimiza wanajamii kuyasafisha mazingira na kuyalinda. Hili analifanikisha kupitia namna wananchi wanavyoimba huku wakiiga namna wagonjwa wa Siza wanavyopiga magita. Wanadhihirisha hili pale wanapojikuna mwili mzima. Kabla ya kuimba kibwagizo wanataja kuwa, katika mazingira yaliyonajisiwa, kamasi zinavuja puani na wanasisitiza hili kwa kupenga kamasi na kuzifutia unyayoni. Mwandishi anafafanua hili kupitia wahusika ili kudhihirisha changamoto, ndwele na matatizo yanayozalishwa na mazingira chafu na dhoofu. Lengo lao kuu la mwandishi Mbogo likiwa kuwahamasisha wanajamii kuhusu athari hasi za mazingira yaliyonajisiwa na binadamu kwa maisha na uhai wa binadamu.

Kulingana na mwandishi Mbogo, mashairi na nyimbo yana nafasi kabambe katika kuwazindua na kuwaelimisha wanajamii kuhusu haja na namna za kuyahifadhi mazingira. Nyimbo na mashairi ni zana zenye nguvu za mabadiliko ya kijamii na uhamasishaji. Ingawa muktadha wa kijamii unafafanuliwa katika misingi ya mtazamo wa mwandishi Mbogo kwenye uelewa wa kijamii, unaakisi nguvu ya mashairi na nyimbo katika kuyahifadhi mazingira. Hili linafanikishwa kupitia kuongeza uelewa na kuleta mabadiliko ya kijamii ulimwenguni kwa jumla. Hata hivyo, ni vyema kukumbuka kuwa, waandishi Mbogo na Mkangi wameweza kuathiriwa moja kwa moja historia yao, ushawishi kutoka kwenye mazingira walimokulia pamoja na ushawishi wa kisiasa wanaouandika. Mwandishi Mbogo anasisitiza kuwa nyimbo huwa njia mwafaka ya kuifikia hadhira pana hivyo ni madhubuti katika kuendeleza uzinduzi na uhamasihaji wa jamii pana kuhusu mbinu za uhifadhi wa mazingira.

Kwa mfano, kupitia wimbo wa Siza B katika *Bustani*, mwandishi Mbogo anakabiliana na unajisi wa mazingira kwa kuwaelimisha wananchi. Mtunzi Mbogo anadokeza kuwa, mavazi ya waimbaji wale wa Siza au Maleba yanaashiria vita dhidi ya uharibifu wa mazingira katika misingi ya utamaduni. Mathalani, wanawake wanavaa sketi na blauzi za vitenge, chini njuga na vichwani manyoya ya tausi. Tausi ni ndege mkubwa anayefugwa ambaye ana madoadoa ya rangi ya samawati na kijani anayetanua mkia wake kuonyesha urembo wake (BAKITA, 2015; Wamitila, 2022). Hivyo, wananchi wa Siza wanajivunia kukabiliana na wanaopalilia uharibifu wa mazingira. Wanaume walivaa hivyo hivyo pamoja na suruali na shati la kibuluu. Hili linaashiria utayari wao kukabiliana na wanaoyapujua mazingira mtawalia. Hili linafungamana na nguzo ya utamaduni na mazingira ambapo kila jamii huhusisha mbinu na imani za kuyahifadhi na kuyatunza mazingira yao. Hakika hili linawiana na kauli ya Momanyi (2009) katika riwaya yake ya *Nakuruto* kuwa, kila utamaduni wa jamii husika una nafasi kubwa katika uhifadhi wa chemchemi za maji ili kuulinda uhai wa jamii na mazingira yao.

Mwandishi Mbogo anasisitiza kuwa utamaduni wa jamii ya Siza katika *Bustani* na ile ya Daluta katika *Vipuli* unasaidia pakubwa katika uhifadhi wa mazingira. Kupitia jamii hizi anaihimiza jamii pana ya ulimwengu kupitia wahusika na maudhui katika riwaya zake mbili teule kuudumisha utamaduni unaopalilia uhifadhi wa mazingira. Waithiru (2022d) anaongeza kuwa, utamaduni kando na kuwa nguzo kuu ya Nadharia ya Uhakikimazingira huchangia pakubwa katika kusisitiza umuhimu wa kuyahifadhi mazingira kwa wanajamii tangia kuzaliwa hadi kuaga kwa binadamu. Wimbo ni ala mwafaka ya kupitisha ujumbe kwa wanajamii kwa njia nyepesi, upesi na madhubuti (Waithiru, 2022d) na ni bayana kuwa mtunzi Mbogo amefanikiwa katika matumizi ya nyimbo kuwahamasisha wananchi kuhusu haja ya kuyalinda na kuyatunza mazingira. Hili linafungamana na kauli ya Turner na Freedman (2010) kuwa, matumizi ya nyimbo katika elimu ya uhifadhi wa mazingira husaidia pakubwa kuwafahamisha wanafunzi kupitia dhana zinazojengwa kupitia urari wa kimuziki, huku zikiibua mvuto katika mada za kimazingira.

Rai za mtunzi Mbogo zinadhihirika kupitia wahusika, maudhui, falsafa yake pamoja na uchanganuzi wa lugha na toni aliyotumia katika kazi zake husika. Ikizingatiwa kwamba gesi, Abdula, Sagasaga, Dampu na Pesa zianaashiria ajenti za uchafuzi na uharibifu wa mazingira mtawalia, kuzikemea ni kuukemea unajisi wa mazingira

kupitia nyimbo. Hakika kama anavyokiri mwandishi, wimbo ni mbinu mwafaka ya kudhoofisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira ulimwenguni kwa kuwahimiza watu wadumisha usafi wa mazingira. Kwa kweli, nyimbo zinadhirisha ufanisi kama ala ya kuukemea uchafuzi na uharibifu wa mazingira na ndiposa mbinu nyingi za uhifadhi wa mazingira katika tamaduni mbalimbali huwasilishwa kupitia nyimbo kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Lugha inayotumika katika mabango kuwahamasisha wananchi dhidi ya kuukemea unajisi wa mazingira ni ya kishairi. Mtunzi Mbogo anarai kuwa, matumizi ya mabango ni mbinu mwafaka na madhubuti ya kuwasilisha hisia na maoni ya watu bila kujali tabaka, dini wala asili. Mathalani, mabango yaliyokuwa pale uwanjani yalisema kwa mfano katika *Bustani* kuwa: GESI YA SAGASAGA NI SUMU KWA MAISHA YETU. (uk. 89). Hii ni dhihirisho kuwa kemikali zinazotolewa na viwanda mbalimbali katika maeneo tofautitofauti ni hatari kwa maisha ya binadamu. Lingine lilisema kuwa: HATUTAKI TAKATAKA ZA NYUKLIA NCHINI MWETU. (uk. 89). Takataka za nyuklia ni mojayazo ya baadhi ya kemikali hatari kwa maisha ya binadamu kama zao la shughuli za binadamu za kuimarisha zana zao za vita. Bango hili lilipata mshawasha kutokana na habari kuwa mwezi mmoja uliotangulia, meli ya Wajerumani iliyokuwa imejaza mabaki hatari ya nyuklia ilikuwa imetia nanga katika Bahari ya Atlantiki ikisubiri kumwaga mabaki hayo ya nyuklia kandokando mwa Pwani ya Nigeria. Hivyo, mtunzi Mbogo anawahamasisha Waafrika na walimwengu kwa jumla kuyasikitikia na kuyawajibia mazingira kwa usawa bila ubaguzi.

Kwa mujibu wa TATAKI (2013), ushairi ni sanaa ya kutunga mashairi, tenzi, ngonjera au nyimbo. Katama Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* ametumia shairi kama mbinu kabambe ya kuwahimiza watu wakabiliane na upujufu wa mazingira mtawalia. Kupitia mhusika Dzombo anasana mashairi na nyimbo zinazokongolewa na vijana kwenye Trimi huku wakifanya kazi. Vijana wale walikuwa wakijihamasisha wao wenyewe kwa wenyewe, haja ya kukabiliana na wanajisi wa mazingira – Wachuna. Katama Mkangi anatoa rai kuwa, matumizi ya ushairi nyimbo pamoja na simulizi kukabiliana na upujufu wa mazingira ni mbinu madhubuti, nyepesi na mwafaka. Wamitila (2003: 318) anaeleza ushairi nyimbo kuwa, "... umetungwa kwa ajili ya kuimbwa," ilhali simulizi, "... huambatana na ala za muziki, mapigo ya ngoma, kupigwa kwa makofi pamoja na sifa nyingine." Hivyo, waandishi wa riwaya nne teule wamefanikiwa kudhihirisha ufanisi wa matumizi ya mashairi na nyimbo

katika kuwazindua watu kuhusu haja ya kudidimiza upujufu wa mazingira au waangamie kutokana na madhara ya mazingira yaliyopujuliwa. Hali hii inalandana na nguzo ya utamaduni na mazingira ambapo binadamu anahimizwa haja ya kuyahifadhi mazingira yake kwa kusudi la kuuhifadhi uhai wake.

Kupitia ushairi, mtunzi Mkangi anawahimiza watu wasusie uharibifu wa mazingira kwa kuwa mazingira chafu ni kupe ulimwenguni na hivyo uchafuzi unafaa kukemewa vikali na kuangamizwa kabisa. Kupitia mhusika Kijana wa kiume katika *Walenisi* mwandishi Mkangi anatumia ushairi kukashifu ubaguzi wa kimazingira na wa kiuchumi mtawalia. Mwandishi Mkangi anatahadharisha kuwa, mazingira chafu huzalisha ukame, udhalimu, ubaguzi na maonevu na hatimaye maafa na kuwaacha wananchi wakiwa vipande vya maiti katika taifa lao wenyewe. Hivyo, mwandishi Mkangi anaihamasisha jamii dhidi ya dhuluma, maonevu na ubaguzi na athari zake hasi kupitia ushairi na nyimbo. Matumizi ya mashairi na nyimbo yanadhihirisha ufanisi mkubwa katika kukabiliana na ukatili dhidi ya mazingira na dhidi ya maangamizi ya binadamu kwa ujumla kupitia uwezo wake wa kuwashaajiisha watu kuukemea upujufu wa mazingira. Katama Mkangi kupitia vijana anatumia ushairi kama ala ya kuwahimiza watu wakabiliane na udhalimu kwa jumla.

Katama Mkangi anadhihirisha kuwa, shairi ni ala madhubuti na mwafaka ya kuwazindua watu kukabiliana na ubaguzi, utabaka na dhuluma aina aina za kimazingira. Kupitia mhusika Mtu-Wazo katika *Walenisi* anafafanua kuwa, "Lakini siku walipozinduka! Babee! Mbona Wachuna walitafuta pakujificha na wasipaone!" (uk. 108). Ingawa vijana hawakupambaukiwa na kutumiwa kwao vibaya kwa makame na utumwa, hatimaye waligundua na kupitia ushairi wakajihamasisha wenyewe kwa wenyewe na kuudidimiza udhalimu na maafa kwa jumla. Vijana katika mataifa mengi barani Afrika wanatumia ushairi kama ala ya kuimarisha juhudi zao katika kukabiliana na udhalimu, uongozi mbaya na upujufu wa mazingira mtawalia. Hali hii inawiana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo viongozi huhalalisha hulka zinazozalisha unajisi wa maadili, wa mazingira na wa nafsi. Hata hivyo, waandishi Mkangi na Mbogo wanayatumia mashairi na nyimbo kuwazindua wananchi katika vita dhidi ya unajisi wa mazingira.

Matokeo ya juhudi za kukabiliana na unajisi wa utu na wa mazingira kutokana na ukakamavu unaozalishwa na uhamasishaji kupitia ushairi wa vijana yanadhihirikia

Wawalenisi paruwanja. Kwa mfano, mwandishi Mkangi kupitia mhusika Mtu-Bint Nena anamfafanulia Mtu-Dzombo kuwa, mashairi aliyoyasikiliza yalikuwa yametungwa na vijana walioasisi vyama vya ushirika ili kukabiliana na ukatili na unajisi ulionawirishwa na utawala dhalimu na wa maonevu wa Wachuna. Hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya ambapo mazingira na kesho ya vijana hunajisiwa na viongozi. Mwandishi wa *Walenisi* anasawiri matunda ya vita dhidi ya unajisi wa mazingira kwa kuwahimiza watu kupitia ushairi anapoelezea kuwa, baada ya kuyatunza mazingira, mashamba yalinawiri na hewa ikavutia. Mashamba yanasheheni mawimbi ya masuke na masuke ya wimbi, mtama, mpunga, mawele na ngano kwa wingi. Mahindi yalinawiri kwa mazao na afya tele. Nadharia waliyoitumia vijana Wawalenisi iliyosambazwa na kuelimishwa wengine kupitia ushairi inasaidia kudidimiza ukame, njaa na maafa.

Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa mna manufaa tele kuishi katika mazingira safi. Mathalan, kupitia mhusika Mtu-Bint Nena anaeleza kuwa, hamkuwa na Mwalenisi hata mmoja aliyekuwa analala njaa. Hivyo, udhalimu, unajisi wa mazingira na utu pamoja na ukatili wa binadamu vimechangia pakubwa katika kuuharibu utu na ulimwengu kwa jumla. Hali hii inafungamana na nguzo ya uongozi mbaya. Hakika hili linadhihirisha paruwanja kuwa mna haja ya binadamu kutumia mbinu zozote zile mwafaka kukabiliana na udhalimu hususani dhidi ya mazingira kwa jumla. Kwa mujibu wa waandishi Mkangi na Mbogo, matumizi ya mashairi na nyimbo yanaibuka kuwa faafu na madhubuti katika kuwahimiza watu washiriki vita dhidi ya unajisi wa mazingira bila kuviachia utawala na uongozi tu. Aidha mna haja ya kujitoa wenyewe ila si kujitolea tu kwenyewe ili kushinda vita dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla.

### 6.8 Mwandishi na Maandamano: Kutetea Uhifadhi wa Mazingira

Mbinu ya kutumia maandamano inaungwa mkono na wengi kama njia madhubuti ya kukabiliana na wanajisi wa mazingira kwa kukemea shughuli zao dhoofu na zenye kuzalisha mabadiliko ya kudumu ya tabianchi. Rai hii inatolewa na mwandishi Mbogo kupitia mhusika Pamela anayesema kuwa, pamoja na wazo la kuwahamasisha na kuwatia hasira wananchi wa Siza, anatoa rai kuwa wazo la Pasta Yona la kufanya maandamano kama mbinu mwafaka ya kuwahimiza wananchi kukabiliana na wapujufu wa mazingira.

Mwandishi anasisitiza kuwa wengi hukubaliana na mbinu hii ya kuwahamasisha watu dhidi ya unajisi wa mazingira. Ndiposa anasana wahusika Wote waliokuwamo wakiliunga mkono wazo la maandamano. Kupitia mhusika Pasta Yona wa Yona katika *Bustani* mwandishi anapendekeza kuwa, maandamano yanafaa yahusishe kila mja ili watu wote wahamasike kwa pamoja. Kwa mfano, anawahusisha watu wote kama vile, wafanyakazi, wakulima, watu wa dini na makundi mengine yote katika maandamano ya kukemea uchafuzi na uharibifu wa mazingira na kiwanda cha kemikali cha Sagasaga katika *Bustani*. Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa, maandamano yamekuwa njia muhimu ulimwenguni ya kufikisha ujumbe wa kijamii na kisiasa hivyo yanafaa zaidi katika uhamasishaji wa uhifadhi wa mazingira. Mwandishi anatumia maandamano kuwazindua watu juu ya umuhimu wa kulinda mazingira yao kwa ajili ya vizazi vijavyo. Anasisitiza kuwa maandamano yanaweza kuchukuliwa kama mwamko wa umma dhidi ya uharibifu wa mazingira.

Katika riwaya za *Bustani*, *Walenisi*, *Vipuli* na *Mafuta*, waandishi wanapendekeza maandamano kuchukuliwa kama mwamko wa umma dhidi ya uharibifu wa mazingira. Katika riwaya hizi zao wanaonyesha maandamano kama njia ya kuwaunganisha watu na kuwaelimisha juu ya athari za shughuli za kibinadamu kwa mazingira. Kupitia maandamano, waandishi wanatoa mfano wa namna jamii inaweza kushirikiana ili kupigania haki ya mazingira safi na salama. Katika *Bustani* mwandishi Mbogo anaeleza jinsi wakaaji wa Siza walivyokusanyika na kuandamana kupinga uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa hewa unaosababishwa na kiwanda cha kemikali cha Cel. Uchafuzi huu unatia hewa, vyanzo vya maji na mimea sumu. Katika *Vipuli* mwandishi Mbogo anafafanua namna utoaji leseni ovyo na uongozi unachipuza ujenzi wa viwanda vinavyotupa taka ovyo na kuichafua mito na bahari. Kupitia maandamano haya, mwandishi anahimiza haja ya kuwa naujasiri na ukakamavu baina ya wananchi pamoja na nguvu ya mshikamano wa jamii katika kupigania uhifadhi wa mazingira. Katika *Mafuta* na *Walenisi*, Katama Mkangi anatumia lugha yenye nguvu na taswira za maandamano kuashiria kutamauka na dhuluma wanazopitia watu kutokana na uongozi mbaya unaoyapujua mazingira kwa hiari. Anapambanua namna wanasiasa, mabeberu wa kisasa na wafanyabiashara wanavyopuuza kaida za mazingira hususan barani Afrika na kuchochea uharibifu zaidi wa mazingira. Maandamano yanakuwa sehemu, mkakati na harakati za kijamii

ambapo wananchi wanajifunza kuhusu haki zao na jinsi ya kuzitetea, hasa za kimazingira.

Kupitia mandhari ya maandamano, Katama Mkangi na Emmanuel Mbogo wanawafundisha wasomaji juu ya haja ya kuwa na uelewa wa kina kuhusu mazingira yao. Maandamano yanahimiza watu kuchukua hatua, kuelewa athari hasi za uharibifu na uchafuzi wa mazingira, na kushiriki katika juhudi za kuhifadhi mazingira. Isitoshe, waandishi wanadhihirisha kwamba elimu ni msingi wa maandamano yenye ufanisi. Kwa mfano, wakaaji wa Siza wanapata maarifa kutoka kwa wanaharakati wa mazingira na wataalamu wa sheria kama Jonalisti na Pasta Yona wa Yona katika *Bustani*; ambao wanawasaidia kuelewa umuhimu wa uhifadhi wa mazingira. Elimu hii kando na wanakamati kupitia sehemu zote husika wakiwaelimisha wananchi inafanikishwa kupitia magazeti ya New Era na Our Society kila siku kwa zaidi ya majuma mawili. Magazeti yalitilia mkazo habari ya Pasta Yona na maandamano ya Siza. Hii inadhihirika pale ambapo watu mitaani hawakuzungumzia lingine ila kuhusu maandamano ya Siza dhidi ya kiwanda cha kemikali cha Cel. Msingi wa himizo la waandishi hawa wawili linajikita katika mizizi ya nguzo ya haki na maadili ya mazingira ya Nadharia ya Uhakikimazingira.

Hili linadhihirisha kuwa maandamano ni njia mwafaka na madhubuti ya kuhimiza watu juu ya vita vya kukabiliana na upujufu wa mazingira. Hakika katika mataifa mengi barani Afrika, viongozi huyanajisi mazingira kwa kuikata miti; kutoa leseni za uchomaji makaa ovyo; kutoa idhini ya ulimaji ndani ya misitu na kando ya kingo za mito na visima; kutoa leseni za ujenzi wa viwanda vya kemikali bila kuzingatia sheria na masharti yaliyowekwa na Shirika la Afya Duniani na kuruhusu uagizaji wa mashine na magari kuukuu yanayotoa kaboni kupita kiasi hewani ambayo husababisha mvua ya asidi. Hivyo, mna haja ya maandamano ambayo kwa mujibu wa waandishi wa riwaya nne teule huwa njia madhubuti katika kuwasilisha malalamishi kwa serikali na utawala duniani, hasa barani Afrika kuhusu unajisi wa mazingira ambao huendelezwa na viongozi, utawala, wananchi na mashirika aina aina. Kulingana na waandishi hawa wawili, maandamano husaidia pakubwa katika kuwahamasisha wananchi ambao huhitaji tu kupewa motisha kiasi tu maanake dhuluma ambazo hupitia hutosha kuwapa nguvu na ukakamavu tosha kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Watunzi Mkangi na Mbogo wanadokeza kuwa, wananchi huandamana wakifika ukingo wa uvumilivu na matumaini. Mathalan, katika riwaya zote nne baada ya kutathmini vifo na madhara yasababishwayo na polisi wakizuia waandamanaji kuandamana ni hasara ndogo sana ikilinganishwa na maradhi, vifo na mateso ambayo husababishwa na mazingira chafu kama vile; saratani, njaa, mafuriko, kiangazi na maafa. Hiki ni kinyume na anavyobisha Harvey (2020) kuwa, binadamu kupitia asasi za utawala na vyombo vya dola hujisababishia maangamizi zaidi kuliko ukame na mafuriko. Katika utafiti huu ilibainika kuwa madhara ya mazingira yaliyonajisiwa hupiku madhara mengine yoyote ulimwenguni. Hivyo rai ya waandishi kuwa maandamano ni njia mwafaka ya kuwahamasisha watu kuhusu haja ya kuyahifadhi mazingira ni faafu.

Emmanuel Mbogo anasisitiza kuwa vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kupitia uhamasishaji wa elimu kupitia maandamano vinahitaji ukakamavu na msimamo thabiti. Kupitia mhusika Pasta Yona wa Yona hata baada ya kutishwa asitishe maandamano na wale makachero waliomsoza; wakamtupa kwenye chumba kisicho na kiti, kitanda wala mkeka, isipokuwa tundu ndogo ukutani lililowajibika kama dirisha aliendelea kusisitiza haja ya maandamano. Alifungiwa humo tangu saa nne asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni na hakusimama dede, ila alisimama kidete. Kupitia mhusika huyu, mwandishi Mbogo anaihimiza jamii kutumia maandamano kutetea haki za mazingira yao. Anapendekeza kuwe na ushirikiano na umoja wa kila mmoja katika harakati za kukabiliana na wanaoyachafua na kuyaharibu mazingira.

Mtunzi Mbogo anasisitiza kuwa, lengo kuu la maandamano huwa kuwahamasisha na kuwazindua wananchi ili wayatunze na kuyalinda mazingira yao. Mathalan, anafafanua katika *Bustani* kuwa, wananchi wa Siza hawakuandamana ili ati waharibu usalama, mali na maisha ya watu ila waliandamana ili waelekezwe kuhusu jinsi wanavyoweza kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira yao. Hii ni kwa sababu, anasisitiza kuwa maisha ya wananchi kama vile wa Siza huwa hatarini kutokana na mazingira yaliyopujuliwa. Hakika mazingira yaliyonajisiwa huwaangamiza watu wengi kuliko hata risasi. Hivyo, maandamano yanadhihirika kuwa mbinu mwafaka na madhubuti ya kuwaelimisha na kuwazindua watu. Maandamano kama yanavyoelezewa na waandishi katika riwaya nne teule yanakuwa ala yenye nguvu ya kuwaelimisha na kuwahamasisha watu kuhusu uhifadhi wa mazingira. Kupitia maandamano, waandishi wanatoa mwanga juu ya namna

wanajamii wanaweza kushirikiana katika kulinda mazingira na kuhakikisha kuwa rasilimali asilia zinadumishwa kwa ajili ya vizazi vijavyo. Maandamano yanabaki kuwa njia bora na madhubuti ya kuleta mabadiliko ya kijamii na kuwahamasisha watu kuchukua hatua kwa ajili ya mazingira yao. Mataifa mengi ulimwenguni hasa barani Afrika huzirai kutokana na kunyongwa kiuchumi, kijamii na kisiasa na mazingira yaliyopujuliwa. Ingawa hiki ni kinyume na nguzo ya maadili ya mazingira ni bayana kuwa kila mmoja ana wajibu na fursa murua ya kudidimiza uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kila namna.

### 6.9 Elimu kama Ala ya Uhifadhi wa Mazingira: Mtazamo wa Mwandishi

Kwa kiwango kikubwa, elimu huchangia katika kukabiliana na anthroposenia. Vermeulen (2020) na Reno (2022) wakiyaunga mkono mawazo ya mtafiti wanasema kuwa, elimu kupitia Fasihi Mazingira huchangia pakubwa katika kuwahamasisha wanajamii kuhusu haja na hitaji la kupunguza gesi sumu hewani, ambazo huzalisha mabadiliko ya hali ya hewa, kuraruka kwa ozoni na tabianchi kimwavuli. Wanasisitiza kuwa, ingawa taaluma hii ni changa, madhali inachipuka kama juhudi za karne za hivi karibuni za sanaa za kimazingira, inakoleza ladha na kunogesha vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira ulimwenguni. Ni taaluma inayoyapa mazingira nafasi pana katika matini yoyote ile ya kisanaa. Hivyo, kwa mujibu wa waandishi wa riwaya nne teule, mchango wa elimu kama njia ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi na utunzaji wa mazingira kiujumla hauwezi kupuuzwa. Katika fasihi ya Kiswahili, elimu imekuwa kipengele muhimu katika kuleta mabadiliko na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kijamii na kimazingira.

Waandishi wa riwaya teule zilizotafitiwa katika utafiti huu wametumia elimu kama njia ya uzinduzi na uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na jinsi jamii inavyoweza kuchukua hatua za kuzilinda rasilimali asilia kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho. Mathalani, ingawa Dkt Matoga anasawiriwa kama aina ya anthroposenia na mtunzi Mbogo, mhusika huyu anaelewa fika kuwa elimu ni njia nzuri ya kukabiliana na ufukara, uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Hii ndiyo sababu anawahimiza watoto wake watie bidii katika elimu. Mathalani, anamrai Kibao mwanawe katika *Vipuli* kuwa, “Lazima ukazanie masomo yako, ... elimu ni ngao ya maisha! Elimu ni mali! Elimu ni silaha!” (uk. 86). Isitoshe, mtunzi Mbogo anatoa rai kuwa, elimu ni mbinu madhubuti ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa kuwapa watu stadi za uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Mathalani,

kupitia mhusika Yusuf anamwambia mhusika Jonalisti katika *Bustani* kuwa, “Sisi wanyonge tunawategemea nyinyi vijana mliosoma. Hawa watu hawajali kutupa vifaa vinavyohitajika kwa usalama wetu dhidi ya madawa ya sumu.” (uk. 20). Hivyo, waandishi wa riwaya nne teule wahimiza kuwa elimu kwa ujumla ni ala mwafaka, madhubuti na sahili katika vita dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa jumla.

**i. Elimu ya Utafiti**

Elimu ya utafiti huwapa watu silaha ya ustahamilivu, uvumbuzi, uzinduzi, mabadiliko na raghba ya kujenga upya utamaduni, maadili na mazingira yao kwa jumla. Hili linawiana na kauli ya akina Reid na Scott (2008) na Stevenson na wenzake (2013) kuwa, utafiti katika elimu ya mazingira huimarisha maridhiano kati ya binadamu na mazingira kwa kumpa binadamu ustahamilivu na raghba ya kuyahifadhi na kuyajenga upya mazingira yake. Mtunzi Mkangi katika *Walenisi* anatoa rai kuwa, elimu ni mbinu mwafaka ya kukabiliana na unajisi wa mazingira hususani elimu ya utafiti. Mathalani, anataja kuwa *Jabali la Ujinga* linalosawiri anthroposenia barani Afrika linaweza kutatuliwa kwa kutumia elimu na werevu. Anadhihirisha hili anaposema kuwa, “... elimu na werevu angalau vilimwandaa vya kutosha, kuweza kujikinga na tofali zito la ujinga wa utotoni na ule wa kibaleghe ...” (uk. 13). Linalodhihirika hapa ni kuwa, pakiwemo na ufahamu na weledi tosha kuhusu chanzo na masuala yanayosababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira, basi binadamu anaweza kukabiliana na upujufu wa mazingira kimwavuli kwa nji madhubuti. Ufahamu na weledi huu hutokana na elimu. Hili linawiana na kauli ya Katama Mkangi kupitia mhusika Dzombo kuwa, alitatizika sana alipokabiliana na *Jabali la Ujinga* – linaloashiria unajisi wa nafsi, maadili na mazingira mtawalia. Hii ni kwa sababu, kama anavyotaja elimu ni ala muhimu katika kukabiliana na upujufu wa mazingira ya binadamu kwa ujumla.

Elimu ya utafiti inachukua nafasi kubwa katika kuongeza uelewa na kuhamasisha watu kuhusu masuala ya mazingira. Kupitia elimu ya utafiti, waandishi Mbogo na Mkangi wanaweza kuwafahamisha wasomaji wake kuhusu madhara ya uharibifu wa mazingira na njia bora za kukabiliana na changamoto hizi. Waandishi hawa wametumia wahusika, mandhari na matukio katika kazi zao kuonyesha umuhimu wa elimu katika juhudi za uhifadhi wa mazingira. Matofali yanayolijenga *Jabali la Ujinga* yanaashiria mbinu, miundo na mitindo tofautitofauti ya anthroposenia. Kupitia

mhusika Karani akimwambia mhusika Dzombo katika *Walenisi* tunajuzwa kuwa watapewa mkopo na marafiki zao ili nao waweze kuwakopesha akina Dzombo ili nao wawalipe deni lao ili mradi waendelee kulima kahawa, chai, katani, pareto, pamba na miwa. Jambo hili Dzombo analiona kama utumwa kwa viongozi, wananchi, utawala na utumwa wa fedha za kigeni. Ingawa karani anauona utumwa huu kama maendeleo, Dzombo anayaona maendeleo yale yakiwa maendeleo ya ujinga. Anapoachwa pale ofisini na karani, anabaki akikodolea macho meza iliyojaa makaratasi. Anapofungua kiganja chake na kukitazama kile kikaratasi alichokuwa amekuja nacho kudai malipo ya mavuno yake, aliiona kama pingu zilizokuwa zikimfyanda kutoka utosini hadi nyayoni.

Mtunzi Mkangi katika riwaya yake ya *Walenisi* anarai kuwa elimu ni njia mwafaka ya kukabiliana na upujufu wa aina zote kwa kuwaelimisha watu kuhusu njia bora za kukabiliana na upujufu wenyewe. Anadhihirisha hili kupitia mhusika Dzombo, pale Dzombo anapokitupa kikaratasi chini na kukisaga kwa kisigino na akakata shauri kwenda kusoma ili angalau aweze kuelewa utandu huu wa ujinga. Hivyo, elimu hususani ya utafiti ina nafasi kubwa katika kulitatua tatizo la uchafuzi na uharibifu wa mazingira, maadili, uongozi na utawala kwa jumla. Hili linafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile ambapo anaonywa dhidi ya kujipalia makaa kwa kuyanajisi mazingira yake kwa kisingizio ati ana mamlaka juu yake.

Kwa misingi hii hii, Katama Mkangi anarai kuwa utafiti ni njia mwafaka ya kukabiliana na changamoto na dhiki aina aina. Kupitia Dzombo, anasisitiza kuwa, anthroposenia inahitaji kutafitiwa kiini, misingi yake na kile kinachoipa uhai ili kuweza kukabiliana na chanzo badala ya dalili. Dzombo anadhihirisha kuwa changamoto na matatizo yatokanayo na dhuluma na unajisi dhidi ya mazingira sio ya kawaida hivyo yanahitaji utafiti wa kimakusudi, kina na madhubuti. Kwa mfano, mwandishi anadokeza katika *Walenisi* kuwa, “Na kwa kawaida, utafiti huanzia mizizini kuelekea matagaani. Kwa kutegemea nadharia hii kama mwongozo, Dzombo aliamua kupambana ...” (uk. 22). Katama Mkangi anasisitiza umuhimu wa utafiti katika kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Anathibitisha hili katika *Walenisi* anapotoa kauli kuwa, “Ilikuwa wazi kwake kwamba, bila ya utafiti ule, basi *Jabali la Magonjwa* lingemla.” (uk. 23). Maadamu, baada ya Dzombo kukazana na utafiti bila kukata tamaa na kwa kumakinika kweli, kule kutisha kwa Jabali lile kukaanza kudidimia. Ukungu mzito mweupe unaosheheni Jabali hili unamdhihirikia

Dzombo baada ya utafiti. Hivyo, kwa mujibu wa mwandishi Mkangi, utafiti ni ala madhubuti ya kutatua sio tu matatizo ya kimazingira ila yanayomkabili binadamu kwa ujumla. Elimu ya utafiti huwa kiambajengo muhimu na msingi katika mhimili wa maendeleo endelevu wa Nadharia ya Uhakikimazingira.

Mtu-Dzombo anavutiwa na kupendezwa na namna utaalamu wa utafiti wa vijana wa Wawalenisi unavyotumiwa kukabiliana na madhara ya mazingira chafu na yaliyoharibiwa. Baadhi ya tafiti zilizodhihirisha ufanisi dhidi ya upujufu wa mazingira paruwanja ni utafiti juu ya hali ya anga, udongo, na maradhi mbalimbali ya mimea. Majibu na matokeo ya tafiti hizi yalitumika moja kwa moja na kupelekea mabadiliko makubwa chanya kwa Wawalenisi. Kiu cha elimu ya utafiti kama njia mwafaka ya kukabiliana na unajisi wa mazingira na utawala kinawasukuma vijana wengi kufanya utafiti kwa minajili ya kuwapanulia elimu na ujuzi wao katika nyanja hizi ila sio kwa kuwa ati walikuwa wakufunzi wa nyanja hizi za masomo. Katama Mkangi anasisitiza katika *Walenisi* kuwa, "... utafiti ndiyo njia ya kipekee iliyoko imwezeshayo binadamu kuyahama maumbile kwa manufaa yake." (uk. 117). Huku kuyahama maumbile kunaashiria vita dhidi ya anthroposenia ulimwenguni. Hili linathibitishwa na akina Mtu-Bint Hekima wanapomtembeza Mtu-Dzombo kwenye mabonde ya vyakula vilivyokuwa vikinawiri kwa unyunyizaji maji. Hali hii inafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile.

Wachuna walikuwa wanatumia uhaba na ukosefu wa chakula kama chombo cha biashara na fimbo ya utawala dhalimu kwa kuwafanya watu kuwa watumwa wa maumbile. Hapo kabla, katika enzi ya Wachuna, wakulima walitia bidii za mchwa katika kilimo lakini mavuno yalikuwa katiti ghaya kwa sababu ya utegemezi wa mvua pekee. Hili lilizalisha ukame, madhali udongo yabisi uliibuka kuwa tasa. Hii ni kwa sababu, mvua huja kwa misimu isiyoaminika. Wachuna walitumia njaa nchini mle kujinufaisha wao wenyewe zaidi. Hata hivyo, baada ya elimu ya utafiti, vijana wa mwamko waliichukulia mvua kama bakshishi, madhali utegemezi wao wa maji ya ukulima ulikuwa yale ya kunyunyizia kutoka kwenye mabwawa, hifadhi mbalimbali za maji na mito. Inabainika kuwa, kando na utafiti wa kuyatumia maji kwa unyunyizaji haukuwa wa bei ghali ukilinganishwa na miradi ya kishenzi iliyowaunufaisha wachache, ilizalisha mageuzo makubwa na adui njaa akatokomea kwenye kaburi la sahau na husikika tu kwenye hekaya tu. Hakika suluhu kama hizi ndizo zinazohitajika katika mataifa fukara ulimwenguni na hasa ya Afrika ambapo

wananchi wengi huangamia kutokana na njaa. Hili litafanikishwa na elimu ya utafiti. Ingawa hali hii ni kinyume cha mhimili wa maendeleo endelevu na uongozi mbaya, inasawiri suluhu halisi, sahili na zinazowezekana katika Ulimwengu wa Tatu.

Elimu bora huwa zao la utafiti kwa jumla ambapo wananchi wenyewe wanapewa fursa ya kuchangia mahitaji yanayofaa kutimizwa na elimu kwao kama jamii. Waandishi wa riwaya teule wametumia elimu bora kutokana na utafiti wa nyanjani na kwenye maabara kwa lengo la kuudidimiza ujinga, dhiki, changamoto za kimaisha, ufukara, dhuluma aina aina na kuimarisha mbinu bora za uongozi na utawala zinazokiuka kaida za ukoloni mamboleo, hasa barani Afrika. Hili linawiana na kauli ya akina Issberner na Lena (2018) na LaMothe (2024) kuwa, elimu bora na inayotimiza mahitaji ya wanajamii husika ndiyo tu ala sahili na madhubuti ya kukabiliana na madhara makuu ya anthroposenia ulimwenguni kwa jumla bila kuipalili. Hivyo, elimu bora kama zao la utafiti huchangia pakubwa katika kusuluhisha dhiki, maradhi, ufukara, uongozi mbaya, utawala dhalimu, mbinu bora za ukulima, mbegu bora za upanzi, uvumbuzi na uzinduzi wa chanjo bora katika maeneo husika na mbinu bora za uhifadhi wa mazingira.

Kwa mfano, mwandishi Mkangi, anafafanua katika *Walenisi* kuwa, elimu bora kupitia utafiti wa upana na kina hudidimiza Figa la Uoga na kuzalisha Ujasiri. Ujasiri huudidimiza uongozi na utawala dhalimu pamoja na ukoloni mamboleo kwa upesi na wepesi. Vilevile, kupitia utafiti elimu bora huangamiza Figa la Ulafi na badala yake kuvyaa Ukinaifu. Ukinaifu huunyima uongozi dhalimu, ubaguzi na ufukara uhai. Kadhalika, elimu bora huufukuza upao wa Ubinafsi na kuuchipuza ujamaa na pia huukemea upao wa Uchoyo na badala yake kuzalisha ukarimu. Ujamaa na Ukarimu huwa adui wakubwa wa ubaguzi, utabaka, ulofa, uongozi dhalimu na dhiki zingine nyingi zisababishwazo na unajisi wa mazingira. Kwa misingi hii hii, elimu bora hukausha mizizi ya Figa la Ujinga na badala yake kunawirisha ufahamu. Ingawa hapo kabla, miale ya mapambazuko ya ufahamu ilionekana hafifu sana, mwandishi Mkangi anakiri kuwa baadaye ililiamsha jeshi la wanyonge ulimwenguni kote wakaweza kuumaizi unyama na uchafu wa udhalimu uliokuwa miongoni mwao. Hali hii inafungamana na nguzo ya uongozi mbaya.

Mwandishi anathibitisha hili katika *Walenisi* anapoeleza kuwa, “... ndivyo dhoruba ya ufahamu ilivyoshtukia pazia za giza la ujinga na kuzipasulia mbali; kuyeyusha barafu

za uoga, kumulika mapango ya ulafi na kuteketeza magugu ya ubinafsi-uchoyo." (uk. 193). Hivyo, kupitia elimu bora baada ya utafiti, binadamu hupata ufahamu unaowafunua macho wakaweza kuona unyama wote unaowazingira. Kutokana na ufahamu huu binadamu huweza kukabiliana na unajisi wa mazingira, utawala dhalimu, njaa, kiangazi na ukosefu na uhaba miundomsingi na mbinu bora za ukulima wa kisasa. Hili linafungamana na kauli ya akina Pedersen na wenzake (2024) kuwa, udhalimu hujidhihirisha na hujiendeleza kupitia unyama wa wachache kushiba ilhali wengine wengi wakiaga kutokana na njaa; unyama wa wachache kuwatawala wengine wote kwa mabavu; unyama wa maonevu; unyama wa dhuluma, ulofa na unyama wa kila aina. Inadhihirika kuwa, baada ya kupata elimu bora kupitia utafiti, binadamu wanaweza kuutatua unyama wa ulofa unaostarehe mivunguni mwao, hususani barani Afrika. Hili linawiana na nguzo ya maendeleo endelevu ambapo binadamu anatahadharishwa kuyatunza mazingira katika juhudi zake za kujiendeleza kiuchumi.

Mathalani, Wawalenisi katika riwaya ya *Walenisi* waliweza kukabiliana na anthroposenia iliyojidhihirisha kupitia unyama wa wizi barabarani na vichochoroni vyao; uchafu wa rushwa na riba vyooni mwao; unyama wa maangamizi na manyanyaso madarini mwao; uchafu wa ubarakala na unafiki kwenye maeneo yao; uchafu wa ufukara, uzururaji, ukiwa na uombaji masebuleni mwao; unyama wa maradhi, uchi na uulevi misalani kwao; uchafu wa kutojiamini rohoni mwao pamoja na uchafu na unyama wa kila aina. Hakika, uongozi dhoofu husababisha dhiki tele kwa watawaliwa hususani katika janibu zinazotawaliwa na ufukara wa kila aina. Hali hii inawiana na nguzo ya uongozi mbaya na ile ya binadamu dhidi ya maumbile.

Aidha kutokana na elimu bora kama zao la utafiti, ufahamu unawafunulia Wawalenisi utu wao. Utu huu unachipuka, unamiminika, unastawi, unapanuka, unaenezeka na unaongezeka na kukita mizizi kukabiliana na anthroposenia katika taifa la Walenisi. Katama Mkangi anadhihirisha hili anapopambanua katika *Walenisi* kuwa, "Sasa utu wao ukawa ni mseto wa ujasiri, ujamaa, umoja, udugu, na ukarimu. Tofauti zao kama hizi za jike na dume, ama za mla samamki na za mla panya ... ambazo Wachuna ... hawakusahau kuzivivia, zikatoweka." (uk. 194). Tofauti zilizokuwa zimedumishwa na Wachuna kupitia ukabila, dini, ubinafsi, tabaka, lugha, asili, rangi, usomi, miji, na mashambani; udhalimu huo ukavunjiliwa mbali. Hii ni kwa sababu, watu, kupitia elimu bora walitambua utu wao na kuukemea unyama. Kupitia matukio mbalimbali,

kama vile kampeni za usafi, upandaji miti, na matembezi ya mazingira, waandishi Mbogo na Mkangi wanaonyesha jinsi elimu ya utafiti inavyoweza kuhamasisha jamii kuchukua hatua za kulinda mazingira yao. Kupitia wahusika, waandishi wanasawiri kuwa, watu wanaposhiriki shughuli hizi, wanapata uelewa wa kina kuhusu changamoto za mazingira na namna wanavyoweza kuzitatua. Hivyo, kupitia elimu ya utafiti, mwandishi anatoa mwanga juu ya umuhimu wa kumaizi na kuchukua hatua za kulinda mazingira yetu. Waandishi wanatumia wahusika, mandhari na matukio katika riwaya zao kuashiria namna elimu ya utafiti inaweza kubadilisha jamii na kuhamasisha watu kuchukua hatua za uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya uhai wa viumbe wote.

**ii. Maarifa ya Teknolojia**

Maarifa ya teknolojia huyapa mazingira mshipa mpya wa uhai pamoja na viini vipya, virutubishi na ustahamilivu katika ulimwengu ambapo binadamu hujizatiti kila uchao kuyanajisi na kuyaangamiza mazingira kwa jumla. Hili linawiana na kauli ya akina Koci na wenzake (2017), Fulekar na wenzake (2018) na Mark (2023) kuwa, maarifa ya teknolojia na uvumbuzi huwa ya raghba kwa wasomi na wataalamu wanaofanya kazi katika nyanja za viwanda; utawala na ulingo wa elimu ya maji na udhibiti wa taka; uzalishaji wa kawi; uzalishaji na matumizi ya mafuta ya dizeli, petroli na gesi; ulinzi wa rasilimali asilia; uhifadhi wa ikolojia; uhifadhi wa afya ya binadamu pamoja na utengenezaji wa sera za kimazingira. Hakika, maarifa ya teknolojia huchangia pakubwa katika kubuni na kuzindua suluhu sahili dhidi ya mazingira na zinazotumia rasilimali asilia zinazopatikana kwenye mazingira kwa urahisi. Huwa sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote ile, hali inayofungamana na nguzo ya utamaduni na mazingira.

Waandishi Mkangi na Mbogo wanapendekeza maarifa ya teknolojia kama njia kuu ya kuwahamasisha na kuwaelimisha wanajamii kuhusu uhifadhi wa mazingira. Waandishi hawa katika riwaya nne teule wanaonyesha jinsi wahusika wanavyotumia maarifa ya teknolojia katika harakati za kulinda vyanzo vya maji, misitu na wanayama pori. Kwa mfano, kutokana na kifaa cha kutabiri upepo kilicho mle ndani ya *Sayari*, Dzombo anaweza kufahamu ulikotoka na ulikokuwa ukielekea upepo. Mwandishi anarai kuwa, ili kukabiliana na anthroposenia inayopaliliwa na utabaka kinachohitajika ni kujiondosha ili kusababisha kuporomoka kwa ghafla kwa lile paa la utabaka linalowaangamiza hasa watoto. Hata hivyo, anaonya kuwa, kuondoka huku

kunaweza kuwa kwa manufaa tu pale ambapo jamii itaimaizi kwanza unakotoka upepo uvumao wa kitabaka na unaelekea wapi. Uelewa huu unasababishwa na kufanikishwa na maarifa ya teknolojia. Dzombo anataja katika *Walenisi* kuwa, "Bila kujua hiyo, basi kujiondoa kwa ghafla kibinafsi hakuleti mabadiliko yoyote." (uk. 25). Katama Mkangi anadhihirisha kuwa mna matumaini chanya ya kuweza kukabiliana na ufisadi na ubaguzi wa kimazingira. Hii ni kwa sababu, anaeleza kuwa, Dzombo baada ya kuonyeshwa ulikotoka na ulikokuwa ukielekea upepo wa utabaka na kile kitabiri, anajua namna ya kuutega. Utegaji huu unampeleka upande ule miamba ile ilikokuwa na hivyo anaweza kuikwepa kwa urahisi na kujinusuru kutokana na sumu kali ya maafa.

Mwandishi Mkangi anadhihirisha hali ambapo binadamu kupitia mhusika Dzombo anakutana na maradhi ya watoto ya marasimi na kwashiakoo yatokanayo na ukosefu wa lishe bora. Ili kukabiliana na tatizo hili mtunzi Mkangi anatoa rai kuwa maarifa ya teknolojia ya kilimo bora ni msingi na madhubuti katika kuangamiza maradhi na maafa kwa ujumla. Mathalan, faida ya ziada iliyotokana na kilimo iliwawezesha Wawalenisi kukita misingi ya kuasisi na kupanua viwanda kama vile cha Trimi. Mwandishi anaongeza kuwa, kwa kutumia maarifa ya teknolojia, maji yalivumbuliwa chimbuko na chemchemi tofautitofauti. Mathalani, anaeleza katika *Walenisi* kuwa, "Hawa, kwa kutumia maji ambayo yalikuwa yamejaa tele mitoni, maziwani na hata kuzimu, kwa kilimo, wakawa wameweza kujinasua kutokana na kutegemea maumbile na masharti yake." (uk. 118). Kwa kutumia maarifa ya teknolojia kukabiliana na kiangazi na ukosefu wa maji, matokeo ya ufanisi kama vile shibe, lishe bora na afya njema yanadhihirika. Hili linadhihirisha kuwa, vijana, hususani barani Afrika wanaweza kutoa suluhu dhidi ya dhiki zinazolinyofoa bara hili bawa za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hili linawiana na kauli ya Waithiru (2022d) kuwa, vijana barani Afrika wana uwezo wa kuzalisha; nafaka, mali ghafi kwa viwanda, matunda; kufuga wanyama wa nyama na wengine kujiajiri kwenye mitandao. Hakika unajisi wa mazingira na utawala ukididimia, shibe hushamiri. Hii ndiyo sababu Wawalenisi katika *Walenisi* walikuwa na maghala ya vyakula kwa kila idadi ya raia elfu moja katika majimbo yote.

Hakika maarifa ya teknolojia huzalisha vifaa vinavyorahisisha maisha ya binadamu na kuchangia maendeleo endelevu ulimwenguni. Kwa mfano, kwenye Kreshi pale kiwandani cha Trimi, Dzombo anawapata watoto wachanga wakiwa wamelazwa

kwenye kitanda kimoja kirefu na kipana na wadogo wa kutambaa pamoja na wale wa miaka mitatu. Wale wachanga walikuwa wanagusana na kuchekeleana kwa furaha. Wale waliotambaa walikuwa wakichezacheza na vidubwasha vya kuvutia kwa macho, harufu, sauti na mapasho chini ya waangalizi maalum. Nao wale wa miaka mitatu walisaidiwa kufanya lolote linalonasa fikira zao na hivyo kukuza uhuru wa kimawazo. Haya yote yanafanikishwa na maarifa ya teknolojia ianyochangia uvumbuzi na uzinduzi. Uvumbuzi na uzinduzi huchangia suluhu kwa karibu changamoto zote katika maisha ya binadamu, hususani Waafrika badala ya utumwa wa utegemezi kwa mataifa tajiri ya Ughaibuni. Hili linawiana na kauli ya Maathai (2009) kuwa, changamoto kubwa barani Afrika ni ule utumwa wa utegemezi wa kimawazo baina ya mataifa duni ya Afrika kwa yale tajiri ya Magharibi. Hivyo, maarifa ya teknolojia hutoa suluhu kwa changamoto hizi.

Maarifa ya teknolojia inawawezesha Wawalenisi kubuni na kujenga Kreshi, ambapo wazazi huwapeleka watoto wao na kuwaacha chini ya uangalizi wa waangalizi waliofuzu katika kazi ya kuwatunza watoto wa umri huo. Wazazi baada ya kupata hakikisho kuwa watoto wao wako salama, nafsi zao huwa huru na kule kutokuwa na jambo lolote linalowakera huwawezesha kuwa madhubuti katika shughuli zao za kila siku. Umadhubuti huu hudidimiza ulofa, udhalimu na uongozi dhoofu na badala yake hupalilia utu. Isitoshe, kutokana na maarifa ya teknolojia, watoto hulishwa chakula bora na kuvishwa na kutunzwa kwa hali ya kisasa kabisa. *Nakolani* ambayo ni zao la elimu ya teknolojia inajishughulisha na siha ya wafanyakazi wote kiwandani. Pia, hujihusisha na siha pamoja na tiba za ndwele za watoto wadogo. Hivyo, maarifa ya teknolojia hudidimiza udhalimu kwa kudidimiza uhusiano katika maeneo ya kazi wa paka na jibwa.

Maarifa ya teknolojia ni tisho kubwa kwa utumwa na udhalimu kwa sababu, humpa binadamu nafasi ya kuchagua, kuchunguza na kudadisi na hatimaye, kuelewa kwake humpa uhuru kamili bali si kumfanya kuwa kinyago cha umaskini, maradhi na maafa. Aidha, maarifa ya teknolojia inaangazia ulemavu wa kimawazo na kuzidisha mwangaza wa ufahamu kuhusu mbinu mbalimbali za kukabiliana na ufukara, uongozi mbaya na maafa kwa jumla. Waandishi Mbogo na Mkangi wanaonyesha wahusika wakuu katika riwaya nne teule wakiwa wanaharakati wa mazingira na waoelewa umuhimu wa maarifa ya teknolojia katika kuboresha mazingira yao. Wahusika hawa wanajitolea kusambaza maarifa ya teknolojia kwa jamii kupitia mikutano ya wanajii,

magazeti, runinga, redio na hata maandiko ya kifasihi kama mashairi na nyimbo. Hakika mchango wa maarifa ya teknolojia katika maendeleo endelevu na kuimarisha uongozi bora ulimwenguni si wa kupuuzwa.

#### iii. Elimu ya Haki za Kijinsia

Mwandishi Mkangi kupitia mhusika Dzombo anasawiri ufanisi dhidi ya anthroposenia utokanao na elimu ya haki za kijinsia ambao huimarisha, sio tu uhusiano kati ya vijana wa kike na wa kiume ila pia maendeleo endelevu. Uongozi mbaya unaotawaliwa na maonevu, chuki na ubabedume hutinga na kukwamiza hatua za maendeleo endelevu kwa kuchangia mabadiliko makubwa hasi katika mazingira (Clark, 2015; Chandler na wenzake, 2020; Mostafanezhad na Norum, 2021). Miongoni mwa Wawalenisi, usawa wa kijinsia unazalisha kazi sawa kwa mke na mume. Aberbach (2018) anafafanua kuwa, jamii nyingi zimeukubali ufukara kama suala la kiasilia lakini sio Biblia. Suala la kuuangamiza ufukara huanza kwenye Biblia katika ushawishi wa kupunguza bonde kati ya matajiri na maskini. Hakika kwa kiwango kikubwa, Biblia huyaona maisha ya binadamu, hususani historia ya usasa na maendeleo endelevu kupitia jicho la maskini. Aberbach anapendekeza kuwa, ingawa ni kinyume na baadhi ya maelezo ya Biblia, elimu ya usawa wa kijinsia ni muhimu katika kukabiliana na unajisi wa mazingira, uongozi na utawala kwa jumla.

Mathalani, kupitia mhusika Dzombo mwandishi Mkangi anakiri katika *Walenisi* kuwa, aliduwaa alipowaona wasichana na wavulana wakitekeleza majukumu sawa. Hivyo basi, kwa Wawalenisi, haki za kijinsia zinawapa mwanga kuwa, sio tu jukwaa la kumnyanyasa mtoto wa kiume, ila siri ya umoja wa ushirikiano wao katika kukabiliana na ufukara, utawala na uongozi dhalimu. Hata hivyo, mwandishi Mkangi anasisitiza haja ya usawa unaojikita katika misingi ya uelewa na uwajibikaji ila si wa lazima kwani utazaa utumwa badala ya mtu huru. Usawa wa kijinsia baina ya Wawalenisi unatokana na kuelewa kwao kuhusu haki za kijinsia kuwa, siri ya mtu kutaka kujua kule atokako; utamaduni wake; kule aendako; maisha yake na hatimaye kile akitakacho, ndoto na ruwaza zake, ambako kuko ndani huimarisha ushirika baina ya watu. Wawalenisi baada ya kupambaukiwa na haki za kijinsia wanasisitiza kuwa, ni ndani ya mwanamke ambamo siri ya uhai hutungwa, kuota na halafu kuzaliwa. Hivyo, wanashikilia msimamo kuwa, mwanamke ni kitovu cha hekima ulimwenguni. Hili linawiana na kauli ya Nayar (2010) kuwa, mwanamke sawa na ulimwengu

huhifadhi uhai ndani yake na hutambuliwa na ishara za kuzalisha uhai ila si maafa ulimwenguni.

Kupitia mhusika Mama Mtu-Maanani mwandishi Mkangi anadhihirisha kuwa, kabla ya majilio ya haki za kijinsia, wanawake walikuwa wakitukanwa ama kutaabishwa kwa kumeza tembe, kupigwa sindano au hata kushindiliwa vijiti kwenye viungo vyao vya uzazi ilimradi wasiweze kutunga mimba. Hii ni kwa sababu, wakati huo wa enzi ya Wachuna, mwanamke alichukuliwa kama kifaa cha kumburudisha na kumliwaza mwanamume ila si kama binadamu. Hivyo basi, alipohitajika kuzaa alizaa kama mtambo na alipokanywa kuzaa, basi pale mataambisho ya tembe, sindano na vijiti yalitekelezwa. Hili linaashiria unajisi wa ulimwengu kutokana na shughuli za kila siku za binadamu (Nayar, 2010). Hii ni kwa sababu, binadamu baada ya kuutawala ulimwengu alizalisha ubaguzi kati ya maskini na tajiri, kati ya wanawake na wanaume na kati ya binadamu na mazingira yake. Hivyo, unajisi dhidi ya ulimwengu unaashiria unajisi wa mazingira kwa jumla.

Wanawake wengi walifanywa tasa kutokana na mifereji yao ya mayai ya uzazi kukatwa na kutiwa matanzi huku wengine wakitolewa uzazi wao kikamilifu katika *Walenisi*. Ingawa Wachuna walisingizia kuwa hizi zilikuwa jitihada za maendeleo, ukweli ni kuwa zilisababisha kuvyazwa kwa mwanamke na kutasiwa. Hili linadhihirisha upaliliaji wa maangamizi ulimwenguni (Clark, 2015; Moore, 2017). Anthroposenia huchangia pakubwa katika kuufanya ulimwengu tasa kiwango kwamba unashindwa kuwahifadhi wanadamu, wanyama na maumbile mengine mengi (Moore, 2018). Hivyo, mna thamana kubwa na manufaa tele katika kuimarisha haki za kijinsia hasa barani Afrika kama mbinu madhubuti ya kukabiliana na anthroposenia. Hakika inadhihirika kuwa mna haja ya kutumia elimu ya haki za kijinsia kama njia mwafaka ya kukabiliana na unajisi wa mazingira, uongozi na utawala dhalimu mtawalia kwa lengo la kuzalisha amani, utulivu na uhuru wa mawazo, uzalishaji wa lishe bora, maisha bora, afya bora kwa wote na malezi bora ya watoto. Hili linafungamana na nguzo ya jinsia na historia za kijamii ambapo Glotfelty na Fromm (1996) wanasisitiza kuwa, shughuli za jana za jamii huchangia uundaji wa mifumo ya kesho ya mazingira kwa kuzingatia jinsia zote sawa bila ubaguzi katika mazingira yenye usawa.

Waandishi Mkangi na Mbogo wanasisitiza haja ya kuwepo kwa usawa wa kijinsia kama haki msingi ya kijinsia. Usawa ni hali ya kulingana au kuwa bila ya tofauti ilhali jinsia ni hali ya kuwa kiume au kike (Wamitila, 2022). Hivyo, usawa wa kijinsia ni kusudi la juhudi za kuibua na kuimarisha usawa kati ya jinsia za kike na za kiume na kuepushana na manyanyaso aina aina ya jinsia moja dhidi ya nyingine yaliyotawala jana ya binadamu (Larsen na wenzake, 2023). Mwandishi Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* anatoa rai kuwa, usawa wa kijinsia ni mbinu mwafaka ya kukabiliana na anthroposenia. Anadhihirisha hili anapoeleza kuhusu mshtuko wa Dzombo alipobaini kuwa Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda kikubwa ni Mtu-Bint Fikirini. Kiwanda hiki na uvumbuzi wa Wawalenisi ulichangia uhifadhi, utunzaji na ulinzi wa mazingira safi, ya kupendeza na yenye kusheheni mimea aina aina yenye manufaa tele kwa viumbe vyote. Kupitia mhusika Dzombo, Katama Mkangi anadhihirisha hili katika *Walenisi* anapoeleza kuwa:

> “... alikuwa amekaa ukingoni mwa kijito cha maji meupe – kijito kilichotiririka katika imani isiyoisha. Kingoni pia kulikuwa na nyasi za ukoka zikifuatiliza hicho kijito. Nyuma ya nyasi hizi kulionekana msitu wa mihepe, mikayamba, mivuli, mishomoro na miaaoini. Hapa na pale mivinje ilisikika ikilia upepo ulipovuma. Na kwa mbali mibuyu, mikwaju, mifune, mivule, na miti mingi mikubwa ya kiasili, ilisimama ikijua usalama wao unahifadhiwa na wala hautakiukwa kamwe. Juu mbingu zilikuwa za nili hafifu ya kuvutia.” (uk. 96 – 7).

Mwandishi Mkangi anaeleza kuwa, manufaa ya kiwanda cha Trimi yalikuwa tele hasa kwa mazingira. Hivyo, mwanamke kuwa Mkurugenzi mkuu lilikuwa jambo na jukumu kubwa. Hasa ikizingatiwa kuwa aliwaongoza wanaume, lile linaashiria usawa wa kijinsia ambapo mwanamke au hata mwanamume habaguliwi kwa vyovyote. Usawa wa kijinsia unachangia mazingira safi na ya ufanisi. Hakika usawa wa kijinsia huchangia pakubwa katika ujenzi wa jamii mpya, mazingira safi na uongozi bora. Hili linawiana na maoni ya Doherty (2022) na Waithiru (2022b) kuwa, suala la usawa wa kijinsia katika kukabiliana na anthroposenia linafaa kuangazwa katika fasihi ya watoto ili kujenga msingi thabiti baina ya watoto katika kuulinda ulimwengu wao dhidi ya unajisi. Hili linafungamana na nguzo ya jinsia na historia za kijamii ambapo mwanadamu anafaa kuzingatia hulka na tabia zinazopalilia uhifadhi wa mazingira tangia kuzaliwa kwake bila kubagua jinsia yake.

Mwandishi Mkangi anaeleza kuwa, tofauti na maeneo ambapo dhuluma, uongozi mbaya, ubaguzi na uchafuzi na uharibifu wa mazingira hupaliliwa, mle kiwandani wafanyikazi walivaa sare iliyofanana bila ubaguzi wa kijinsia. Kupitia mhusika Dzombo anashuhudia usawa wa utu, jinsia na maisha kwa jumla baina ya wafanyakazi. Tofauti na dunia ya Dzombo ambamo mtu aliweza kujulikana hali yake ya kimaisha, kama vile, chakula alichokula, mshahara aliokuwa akipokea, mtaa alioishi na tabaka na mawazo yaliyomtawala, mle kiwandani mavazi yaliwasawazisha kila mtu na pia wote walikuwa na umilisi sawa wa utaalamu. Utaalamau ulidhihirika kupitia ustadi na uthabiti waliokuwa nao wafanyakazi. Hivyo, usawa wa kijinsia huzalisha utafiti wa kina, dhati na mwafaka kwa maendeleo endelevu katika taifa lolote lile. Ingawa hili ni kinyume na nguzo ya maendeleo endelevu inadhihirika kuwa usawa wa kijinsia huchangia uhifadhi wa maadili na mazingira mtawalia. Hili linawiana na kauli ya mwandishi Mkangi katika *Walenisi* kuwa, ni baada ya kudidimiza ubaguzi wa kijinsia, uliokuzwa na kuendelezwa na Wachuna, ndipo utafiti kwa dhati ulifanywa na ukatumiwa ipasavyo kwa manufaa ya kila mwananchi.

Mwandishi Mkangi anahimiza kuwa, mna haja ya usawa wa kijinsia ili kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wanapata fursa sawa katika maendeleo. Anasisitiza kuwa, elimu ya haki za kijinsia huwawezesha wake kwa waume kuelewa masuala ya uhifadhi na kuchangia katika sera na mikakati inayolenga kulinda mazingira yenye usawa na uendelevu. Mwandishi Mkangi anasisitiza umuhimu wa usawa wa kijinsia kama mbinu madhubuti ya kukabiliana na dhuluma, ubaguzi na manyanyaso aina aina. Mathalani, katika Kamati Kuu ya Kiwanda cha Trimi, wajumbe wa kike na wa kiume wako sawa. Wajumbe wanafafanua katika *Walenisi* kuwa, "Akili na mikono ndizo sawa. Haiwezekani mmoja kumzidi mwingine kwani ukizitenganisha, basi hakutakuwa na chochote kitakachoweza kufanyika." (uk. 143). Katika usawa huu, ubaguzi unadidimizwa na hivyo anthroposenia inafifia. Mwandishi Mkangi kupitia wajumbe anasisitiza kuwa, kuzalisha watoto na kuzalisha mali ni shughuli muhimu katika ujenzi wa taifa ambavyo vinahitaji ushirikiano sawa kati ya mke na mume.

Ushirikiano huu unawafanya Wawalenisi kuwa na usawa na hivyo hawaachani, iwe ni kitandani au makazini mwao. Usawa wa kijinsia unawapa utambuzi kuwa mahitaji yao wote yako sawa. Hivyo, nafasi na mchango wa usawa wa kijinsia katika kusuluhisha dhiki, mateso, ulofa, uongozi na utawala dhalimu hauwezi ukapuuzwa kamwe. Ili ulimwengu uweze kutimia kilele cha demokrasia, uvumbuzi, uzinduzi na

ushirikiano wa ukweli na haki bila uzandiki, basi usawa wa kijinsia lazima upewe kipao mbele na mikakati ya kuufanikisha itiliwe mkazo hata kwenye mgao wa bajeti za mataifa mbalimbali, hasa ya Afrika [ambapo ubabedume, manyanyaso ya mvulana pamoja na tamaduni zinazodumisha udhalilishaji wa kijinsia zingali zinashamiri].

### 6.10 Matumizi Pevu na Madhubuti ya Akili katika Uhifadhi wa Mazingira: Sauti ya Mwandishi

BAKITA (2015; 2022) na Wamitila (2022) wanaeleza akili kama dhana ya uwezo wa kujifunza, kuelewa na kufikiri kwa mtiririko wenye urazini na mantiki. TATAKI (2013) wanaongeza kuwa, akili ni uwezo wa kuelewa kitu au jambo; werevu; ujanja; maarifa na kadhalika. Kwa mujibu wa waandishi Mkangi na Mbogo, matumizi pevu na madhubuti ya akili ni njia muhimu ya kufikisha ujumbe na kuhamasisha jamii kuhusu masuala muhimu kama uhifadhi wa mazingira. Katika kazi zao wanasisitiza kuwa, matumizi ya akili huweza kuchukuliwa kama mbinu ya kufikiria kwa makini na kwa undani kuhusu masuala ya mazingira. Mwandishi anapotumia akili katika kuelezea athari za uharibifu wa mazingira na umuhimu wa uhifadhi, anawawezesha wasomaji wake kuelewa kwa kina na kuchukua hatua sahihi. Akili inahusisha utafiti, uchambuzi na uwasilishaji wa hoja zenye mantiki ambazo zinashawishi wasomaji kuchukua hatua hasa za utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Katika riwaya ya *Walenisi*, mtunzi Mkangi anatoa rai kuwa matumizi mwafaka, rahisi na madhubuti ya akili ni njia madhubuti ya kukabiliana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Kwa mfano, mhusika Mtu-Bint Fikirini anafafanua kuwa, "... tuna zaidi ya silica; ... tuna bongo kubwa kuwazidi ... Tuna akili tena za utambuzi, hali hawa wenzetu hawana uwezo huu." (uk. 104). Kupitia mhusika huyu, mtunzi Mkangi anasisitiza kuwa, binadamu ana maarifa zaidi ya wadudu, wanyama, ndege, samaki na viumbe vingine na hivyo, viumbe hawa wakishindwa kusonga mbele wala kurudi nyuma, binadamu huwapiku kiakili. Kutokana na uwezo huu wa binadamu wa kiakili anafaa kuzitumia akili zake kukabiliana na changamoto anazokumbana nazo kwenye mazingira yake. Hali hii inafungamana na nguzo ya binadamu dhidi ya maumbile ambapo binadamu asipoweza kuyatunza mazingira yake basi yatamwangamiza upesi.

Katika maeneo yanayotawaliwa na ufukara, viongozi, hasa katika nchi za Afrika huupalilia ujinga na kuueneza ili waweze kutawala kwa karne nyingi. Wao huwakuza wanyama, wadudu na ndege huku wakiwadhalilisha wanadamu. Pia huwapa

wanyama, wadudu na ndege ubinadamu na wanadamu huwapa ududu na unyama. Hulka hii ya kiududu na kiunyama hupalilia anthroposenia pakubwa (Moore, 2018 na Coughlin na Gephart, 2020). Mwandishi Mkangi anasisitiza kuwa, viongozi huwavika wanyama utu na binadamu huwavua utu wao na kuwavika unyama. Hivyo mtunzi Mkangi anahimiza kuwa, mna haja ya binadamu kutumia akili zake madhubuti kukabiliana na uongozi dhalimu, ubaguzi wa kimazingira na manyanyaso aina aina. Matumizi haya yanachangia ubunifu na ujenzi mpya wa ulimwengu mpya usio na dhuluma, ubaguzi, utabaka, maradhi na ufukara. Hili linawiana na nguzo ya utamaduni na mazingira ambapo kutokana na uhifadhi wa mazingira binadamu huishi kwa amani na ufanisi.

Katama Mkangi anasisitiza kuwa, Wawalenisi waligundua siri ya kukabiliana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira ni kutumia akili ila si kushiriki imani za maonevu, manyanyaso na dhuluma chungu nzima. Kupitia mhusika Mtu-Makazi mwandishi Mkangi anakiri kuwa, Wawalenisi waligundua kuwa Mungu ni mapenzi na hivyo, katu hawezi kuwabagua wanadamu aliowaumba mwenyewe. Wanasisitiza kuwa, hakuna sababu tosha ya Mungu kuwafanya wengine tajiri na wengine fukara wa kulishwa na kuvishwa na tajiri wakiwa hai, ati watalishwa na kuvishwa na Mungu wakiaga. Hivyo, wanaamini kwamba uongozi dhalimu, tamaa, ubaguzi, utabaka na ulofa ndivyo husababisha ubaguzi huu ambapo binadamu wengine wanataabika katika uhai wao na halafu hulishwa na kuvishwa baada ya kufa kwao. Hivyo, rai kuwa matumizi mwafaka na madhubuti ya akili katika kukabiliana na hali hii inayoendeleza dhuluma ni ya kweli. Matumizi mwafaka na madhubuti ya akili husaidia binadamu kutambua na kumaizi ulaghai unaoendelezwa na uongozi na utawala wa maonevu na ubaguzi ili kuukuza na kuuendeleza ufukara, utegemezi na utumwa wa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hili linafungamana na nguzo ya uongozi mbaya.

Kwa kutumia akili, Wawalenisi wanaweza kukabiliana na upofu utokanao na uongozi mbaya na mazingira tasa. Hili linathibitishwa na mtunzi Mkangi kupitia mhusika Mtu-Makazi katika *Walenisi* anapotaja kuwa, viongozi hawawezi kuwapumbaza wananchi kila wakati. Mwandishi Mkangi kupitia mhusika Mtu-Bint Fikirini anadhihirisha kuwa, ingawa dini huendeleza utumwa, ubaguzi, ufukara na uongozi dhalimu; kwa kutumia akili inaweza ikadhibitiwa kikamilifu kwa kusudi la kuidhibiti na kuitawala anthroposenia, badala ya anthroposenia kuutawala ulimwengu kwa jumla. Hakika uhuru wa kimawazo humkomboa mwanadamu kutoka kwenye utumwa

wa kimawazo na hususani ule wa ukoloni mamboleo. Hili linawiana na kauli ya akina Curry (2011), Njiru (2015), Moore (2016; 2017), na Alia (2017) kuwa, binadamu atajikomboa kikamilifu kutoka kwenye minyororo ya anthroposenia punde tu atakapoliangaza suala la anthroposenia kwa urazini na uhuru wa kimawazo. Hili linawiana na nguzo ya haki na maadili ya kimazingira.

Aidha, matumizi madhubuti ya akili na binadamu huzalisha ushirikiano ambao huwa muhimu sana katika harakati za kukabiliana na anthroposenia. Mathalani, mwandishi Mkangi anafafanua katika *Walenisi* kuwa Wawalenisi wote walishirikiana pamoja kukabiliana na uongozi mbaya na udhalimu wa kila aina baada ya kutumia akili zao vizuri bila kutia kasumba, imani wala hisia zozote zile. Wake kwa waume, vijana na wazee, wataalamu; waliosoma na wale ambao hawakuwa wamesoma, mafundi; mijini na mashambani, wakulima na wafanyakazi ofisini au kwenye viwandani; wote waliwajibika na kusikitikia hali yao ya maisha na kwa pamoja wote wakawaza na kubuni mbinu mwafaka katika ushirikiano wa kufaana za kukabiliana na ufukara, mazingira tasa na dhuluma aina aina kikamilifu na hatimaye walifanikiwa. Mwandishi Mkangi kupitia mhusika Mtu-Nasi anasisitiza kuwa, kiuyakinifu, Ulimwengu wao wa Wawalenisi ulipata jina la Walenisi kwa minajili ya kusisitiza ukweli kuwa, maslahi ya kila Mwalenisi hayatofautiani kamwe.

Mwandishi Mkangi anahimiza kupitia Wawalenisi kuwa, matumizi mwafaka na madhubuti ya akili ndicho kigezo kikuu ambacho mungu alimpa binadamu ili kuweza kujitatulia mengi ya matatizo akumbanayo nayo kama vile mazingira chafu na tasa, mafuriko, ukame, ujinga, uongozi dhoofu, ufukara, utumwa na ubaguzi wa kila aina kwa ushirikiano, ubunifu na usawa. Mwandishi wa *Walenisi* kupitia mhusika Dzombo anathibitisha kuwa, matumizi madhubuti ya akili yanasaidia pakubwa kukabiliana na kasumba inayopaliliwa na dini kwa minajili ya kuukuza na kuuendeleza utumwa na ufukara. Dini kupitia kasumba ati binadamu ataepuka manyanyaso Mbinguni ni potofu na ya kulemaza juhudi za binadamu za kukabiliana na maonevu, dhuluma na ubaguzi. Katama Mkangi kupitia mhusika Dzombo anashauri ulimwengu na kiuyakinifu binadamu kuzitumia akili zake razini vyema ili kukabiliana na unajisi wa maadili na mazingira akiwa bado hai ulimwenguni. Mathalani, Wawalenisi walifahamu ukweli huu, na walidhamiria kuutekeleza kila siku. Kwa kutumia akili vyema waliweza kupalilia utu, wakaweza kushirikiana na hivyo wakaweza kuishusha Mbingu katika ulimwengu wao ambapo kila Mwalenisi alifanikiwa si tu kuiona

pekee, ila pia kuionja na kuifurahia pia. Hakika mwanadamu akizingatia matumizi madhubuti ya akili ataweza kujikomboa kutoka kwenye minyororo ya utumwa, ufukara, maradhi, ukame, ukoloni mamboleo na maafa mtawalia. Hili linafungamana na nguzo ya utamaduni na mazingira.

Katama Mkangi anafafanua kuwa, halikuwa jambo rahisi kuung'oa upuzi na upofu uliopaliliwa na dini wa kuimarisha utumwa, utegemezi na ukoloni mamboleo, kutoka mawazoni na fikira za wananchi fukara. Ingawa wananchi wawa hawa walidhulumiwa kila uchao, ndio walioulinda utumwa, ufukara na ukoloni mamboleo. Ingetokea manabii waliotabiri kuwa utumwa, ufukara na maafa yalikuwa yakiwacheza shere na 'imani' iliyokuwa yao bandia, hapo kabla, ni wananchi wale wale duni waliokuwa wakiwaapiza, wakiwashutumu na kuwachukulia kuwa walikuwa maadui wakubwa wa Umma. Mtunzi Mkangi anadokeza kuwa, upofu na upuzi huu ulitatuliwa kwa kutumia akili kwa njia pevu na madhubuti. Hata hivyo, halikuwa jambo rahisi. Ilifikia muda na Umma ukajigawa na kuangamizana wenyewe kwa wenyewe. Hili linawiana na kauli ya akina Waithiru na wenzake (2021) na Waithiru na wenzake (2023) kuwa, Waafrika fukara katika mataifa duni ya Afrika hupigana wenyewe kwa wenyewe kuulinda ufukara, uongozi dhalimu na vikaragosi vya mkoloni; utumwa wa ukoloni mamboleo, wanajisi wa mazingira na maangamizi kwa ujumla.

Kupitia mhusika Mama Mtu-Pendo mwandishi Mkangi anadhihirisha na kuthibitisha kuwa, kwa kutumia akili, Wawalenisi wanamfanya binadamu kuwa lengo na kiini cha jitihada zao baada ya kutumia akili kwa upevu na umadhubuti. Hili linadidimiza unyama na maafa, huku utu na uhai vikishamiri. Mhusika Dzombo anakiri katika *Walenisi* kuwa, "Maendeleo yao yametengwa katika mfumo wa kuendeleza uhuru wa binadamu katika kila mianya ya mazingira na mazingara yake." (uk. 149). Mwandishi Mkangi anafafanua kuwa, kwa kutumia akili Wawalenisi waliweza kukabiliana na maangamizi na badala yake maendeleo endelevu, uongozi bora na haki za mazingira yakashamiri kote nchini Walenisi. Hili linafungamana na nguzo ya haki na maadili ya kimazingira lakini ni kinyume na nguzo ya uongozi mbaya.

Mwandishi Mkangi katika *Mafuta*, kupitia mhusika Ti anasisitiza haja ya matumizi ya akili ili kuivumbua siri ya maafa iliyojikita katika hila, ujinga na giza tele. Ti baada ya kukubali kutumia akili yake binafsi vikwazo vya woga kumhimili kimawazo anajiona

ng'andu za miaka zikianza kumyeyuka. Anakubali ukweli ujidhihirishe kwake na pale anapata uvumbuzi unaompapatisha roho namna ya ndwele ya safura. Kule kutoweka kwa uvimbe wa kutofahamu kunamfanya ajigaragaragaze kitandani kwa maumivu. Ute unamjaa kinywani, mikojo mikali inamjia kwa kasi na anajicheka, madhali anavumbua kuwa, kwa muda mrefu amekuwa akitawaliwa na ujinga na utumwa maishani mwake. Ti baada ya kutumia akili yake barabara anatambua kwamba, wengi wa wateule huzaliwa ujingani, hukulia ujingani, huishi ujingani, hula na hunywa ujingani na hatimaye huaga ujingani. Kwa njia hii, maangamizi yanavuliwa nguo kupitia matumizi ya akili na Ti anaamua kuyakabili vilivyo. Hivyo, ujinga unaibuka kuwa kigezo kikuu cha kuyaendeleza maangamizi ya binadamu na mazingira yake.

Matumizi pevu na madhubuti ya akili, kama yanavyoonyeshwa na waandishi Mkangi na Mbogo katika riwaya nne teule zao, ni chombo chenye nguvu cha kuhamasisha, kuzindua na kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira. Kupitia matumizi ya akili, waandishi hawa wanatoa mwanga juu ya umuhimu wa kufikiria kwa makini na kuchukua hatua sahihi za kulinda mazingira yetu. Waandishi hawa wametumia wahusika, mandhari na matukio katika riwaya zao kuonyesha jinsi akili inaweza kubadilisha jamii na kuhamasisha watu kuchukua hatua za uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya kesho yenye siha, shibe, utulivu na amani kwa viumbe hai vyote.

**Hitimisho**

Kwa kutamatisha sehemu hii ya kutathmini rai za waandishi wa riwaya teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni* (2002), *Vipuli Vya Figo* (1996), *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Utafiti huu umedhihirisha baadhi ya njia madhubuti zinazoweza kutumika kukabiliana na anthroposenia ulimwenguni katika misingi ya fasihi na waandishi Mkangi na Mbogo. Mosi, wametoa rai kuwa binadamu kwa kutumia vyombo vya habari, utu, ukakamavu na kujitolea kwake anaweza kukabiliana na anthroposenia kikamilifu. Kisha wametoa rai kuwa ushirikiano na ujasiri, matumizi madhubuti ya rasilimali asilia, uzinduzi wa jamii kupitia mashairi na nyimbo, pamoja na utekelezaji wa maandamano ni njia mwafaka za kukabiliana na anthroposenia. Isitoshe, wamefanikiwa kusisitiza rai kuwa, elimu na matumizi pevu na madhubuti ya akili yana nafasi kubwa katika vita dhidi ya udhalimu, utumwa, ubaguzi, maonevu, uchafuzi na uharibifu wa mazingira pamoja na maangamizi. Nguzo zilizoongoza uchanganuzi wa data kwa kila rai iliyotolewa na watunzi wa kazi husika zilielezwa katika kila kisehemu cha uchanganuzi mintarafu ya lengo la tatu la utafiti.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.1 Utangulizi

Katika sehemu hii, mtafiti alishughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti mintarafu ya madhumuni ya utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti za siku za usoni. Kila kijisehemu kilidandavuliwa mintarafu ya madhumuni ya utafiti kwa kujikita katika dhana kuu. Dhana kuu iliyotawala kazi nzima ni ile ya anthroposenia katika riwaya teule za Kiswahili za *Bustani ya Edeni, Vipuli vya Figo, Mafuta* na *Walenisi*.

## 7.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameratibiwa mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu. Matokeo haya yalitarajiwa kujibu maswali ya utafiti na hivyo yametolewa kwa mpangilio sawa na maswali hayo ambayo ni: Je, aina za anthroposenia zinazosawiriwa katika riwaya nne teule ni zipi? Je, mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule ni zipi? Je, rai za waandishi wa riwaya teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya za *Bustani ya Edeni, Vipuli vya Figo, Mafuta* na *Walenisi* ni yapi?

### 7.2.1 Aina za Anthroposenia

Kutokana na utafiti huu, imethibitishwa kuwa binadamu ndiye chanzo kikuu cha anthroposenia kupitia maingiliano na mahusiano yake na mazingira kwa jumla. Binadamu amefanikiwa kuafikia hili kwa kujiponza kiafya, kiuchumi na kijamii. Hili amelifanikisha kupitia shughuli zake za kiuchumi na utabaka. Katika harakati zake za kiuchumi, binadamu hujenga viwanda ambavyo mifumo yake ya utawala hubuni sera zisizoyasikitikia mazingira kamwe. Mathalani, ilibainika katika utafiti huu kuwa viwanda vingi katika mataifa fukara huchakata taka kwa njia inayosababisha uharibifu mkuu wa mazingira. Kemikali zinazozalishwa na viwanda zinaingia kwenye mito, maziwa, bahari na visimani na kuharibu viumbe hai na mifumo ya ikolojia. Pia uzalishaji wa viwandani katika *Bustani* husababisha uchafuzi wa hewa kupitia utoaji wa gesi chafu.

Kutokana na tamaa na ubinafsi pia kupitia utovu wa utu na maadili, binadamu ameendeleza ufyekaji wa misitu kwa ajili ya kilimo katika *Walenisi* ambapo Dzombo

anafyeka miti kwa nia ya upanzi wa pareto, pamba, kahawa na mimea mingine yenye manufaa kwa mataifa ya Ulaya. Hili linasababisha kupotea kwa makazi ya wanyama, kupungua kwa utoaji wa oksijeni na kuongezeka kwa joto ulimwenguni. Kilimo cha kisasa kinachosisitiza matumizi ya mbolea za kemikali na dawa za kuua wadudu husababisha uchafuzi wa maji na ardhi. Utupaji wa taka ovyo unasababisha uchafuzi wa hewa, maji na ardhi hususan pale kwenye dampu la Siza katika *Bustani*. Taka za plastiki na karatasi za sandarusi zimekuwa donda ndugu katika mataifa mengi ulimwenguni. Katika mataifa ya ulimwengu wa tatu hasa, matumizi ya nishati kutoka kwenye vyanzo visivyo vya kijani kama vile makaa ya mawe na mafuta ya petroli husababisha uchafuzi wa hewa na kuongeza joto duniani kutokana na utoaji gesi chafu. Wanyama na wadudu waliibuka kuwa wakala wa anthroposenia. Madhara ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira huweza kuwa kubwa zikijumuisha mabadiliko ya tabianchi, kupungua kwa bioanuai na kuathiri afya ya binadamu. Hii ni kwa sababu binadamu amezidisha vurugu dhidi ya mazingira.

Wafisadi, mabeberu wa kisasa, mabepari na viongozi wabaya huchangia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kupitia njia aina aina zilizodhihirika katika utafiti huu. Viongozi wabaya wanaweza kupuuza au kubadilisha sheria na kanuni za mazingira ili kuruhusu uchimbaji wa rasilimali bila kujali athari za kimazingira. Mabepari hukosa kuwajibika kwa vitendo vyao, wakificha ukweli kuhusu athari za mazingira kutokana na miradi yao na kuepuka hatua za kurekebisha hali. Mabeberu mara nyingi wanafanya shughuli za uchimbaji madini, ukataji miti na uzalishaji wa viwanda kwa wingi bila kujali madhara yake kwa mazingira. Viwanda vingi hasa barani Afrika [ambavyo humilikiwa na mabepari] hutoa gesi chafu na taka za kemikali ambazo huchafua hewa na maji, kuathiri afya ya viumbe hai na mazingira kimwavuli. Imedhihirika katika *Bustani, Walenisi, Vipuli* na *Mafuta* kuwa, viongozi wabaya na mabepari hupuuza kanuni za maendeleo endelevu kwa kutanguliza faida za kiuchumi juu ya mazingira, bila kuzingatia athari za muda mrefu. Kigezo kikuu ambacho huimarisha viwanda hivi ni ufisadi. Katika mataifa mengi, ufisadi huruhusu mashirika makubwa ya kimataifa kuvunja sheria za mazingira kwa kuwahonga viongozi ili kutoa leseni za ujenzi wa viwanda vinavyokiuka sheria za ulinzi wa mazingira.

### 7.2.2 Mbinu Zilizotumiwa Kusawiri Anthroposenia

Waandishi Mbogo na Mkangi wametumia mbinu za taashira, taswira, ishara, majazi, tashtiti na tashihisi kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule. Matokeo ya

namna taashira imetumiwa na waandishi ili kumfanya msomaji asawiri kwa kina na uangavu masuala ya anthroposenia kupitia riwaya ya Kiswahili yameelezwa katika sehemu hii. Waandishi hawa wamefanikiwa kutumia mbinu ya taashira kuonyesha madhara ya ya uchafuzi wa mazingira na kuhamasisha wasomaji kuchukua hatua za kulinda mazingira. Wametumia maneno ambayo yana maana yenye uketo zaidi ili kusisitiza umuhimu wa kushughulikia masuala ya mazingira. Maeneo kama vile ya kiwanda cha kemikali cha Siza, Dampu la Siza na shamba la Edeni la Matope katika *Mafuta* yamesawiriwa kitaashira kusawiri anthroposenia katika riwaya za *Bustani* na *Mafuta* mtawalia. Waandishi wametumia uchafuzi wa maadili kuashiria uchafuzi wa mazingira ulimwenguni kwa ujumla. Taashir ya vifaa pia imetumiwa kusawiri anthroposenia kupitia kamera ya Jonalisti, mzoga wa mkono wa binadamu, jabali la magonjwa na la ujinga na visibo vya soda. Taashira zingine ni kama vile; ya viumbe kama vile, nguruwe, majoka, Bw Abdula, moto, dudumizi, tai, ukoo wa moto na ukoo wa Wachuna. Taashira ya udhalimu pia haikusazwa kupitia jabali la udhalimu na mhindi mwizi. Taashira za ulofa na ndwele pia kama vile; Jehanamu, kijana Kidonda Zambarau, familia ya Dzombo na makazi yao pamoja na dini zimetumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya teule baina ya zingine.

Kwa upande mwingine, waandishi wametumia majazi kufikisha ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa hadhira. Kwa mfano, mwandishi Mbogo ametumia kiwanda cha Sagasaga kuashiria namna shughuli za kiwanda hiki zinavyochangia kusaga mazingira ya mji wa Siza. Hali hii inaashiria namna uchafuzi na uharibifu wa mazingira unavyopaliliwa na binadamu katika harakati zake za kujiendeleza kiuchumi. Mji wa Siza unawakilisha ulimwengu kwa jumla hususan miji tofautitofauti katika mataifa yanayoendelea ulimwenguni. Wanyama kama vile kinyonga na nyoka wametumiwa na mwandishi Mbogo katika *Bustani* kama ishara za kuashiria hali na viumbe kama vile viongozi na matajiri wasaliti ambao huchangia unajisi wa mazingira. Moshi unaotoka kiwandani cha kemikali cha Sagasaga unaashiria uchafuzi wa mazingira. Moto katika *Walenisi* pia unaashiria uharibifu wa mazingira. Waandishi Mbogo na Mkangi wametumia taswira kusawiri anthroposenia. Hili wamelifanikisha kupitia hali ambapo uharibifu wa mazingira kama vile misitu iliyokatwa kwa kuchomwa makaa na utengenezaji wa mbao, mito iliyokauka na yenye maji machafu pamoja na moshi mzito kutoka viwandani unaochafua hewa. Taswira hizi wamezitumia kwa ufanisi kumhusisha msomaji kihisia ili kumfanya

awajibikie na ayasikitikie mazingira yake katika juhudi za uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Mbinu hizi za kifasihi zimetumiwa na waandishi Mbogo na Mkangi kufikisha ujumbe lengwa kwa ufanisi. Mbinu hizi zinawasaidia wasomaji kuelewa madhara ya uchafuzi wa mazingira na umuhimu wa kuchukua hatua za kulinda mazingira kwa ujumla.

### 7.2.3 Tathmini ya Rai za Waandishi wa Riwaya Teule Kuhusu Jinsi ya Kukabiliana na Anthroposenia

Tathmini ya rai za waandishi Mbogo na Mkangi kuhusu namna ya kusuluhisha changamoto zitokanazo na anthroposenia ilifanywa kwa kuchunguza baadhi ya njia wanazopendekeza zitumike na binadamu. Waandishi wamehimiza matumizi madhubuti ya vyombo vya habari vya chapa na vya kielektroniki katika kuwahiza watu haja ya uhifadhi wa mazingira. Wameendelea kusisitiza kupitia sauti zao kuhusu umuhimu wa ukakamavu katika juhudi za uhifadhi wa mazingira, umuhimu wa utu pamoja na haja ya ushirikiano na ujasiri baina ya wanadamu. Isitoshe, wanahimiza matumizi madhubuti ya rasilimali asilia kama vile maji na maumbile kama msingi wa mazingira endelevu; haja ya uzinduzi wa jamii kupitia mashairi na nyimbo, maandamano na elimu aina aina. Matumizi pevu na madhubuti pia yamehimizwa na waandishi kama mbinu madhubuti ya kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Kupitia wahusika na hadithi ndani ya hadithi, waandishi Mbogo na Mkangi wamefanikiwa kusisitiza kwamba mna njia mwafaka na madhubuti kama zilizotajwa katika sehemu hii ambazo ni muhimu katika juhudi za kudumu za kuhifadhi mazingira. Tathmini ya data ya sura ya sita inaonyesha kuwa, kwa kutumia fasihi, wasomaji wanaweza kufahamu na kuthamini umuhimu wa kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira kwa misingi ya mazingira endelevu. Hili husaidia sio tu uendelevu wa mazingira bora ila pia kuhakikisha dunia bora kwa vizazi vya leo na vya kesho. Waandishi wameweza kudhihirisha kuwa watu wanaweza kubadilisha maoni yao na kuchukua hatua za pamoja za kuhifadhi mazingira. Hii ni dhihirisho tosha kwamba waandishi wa kazi za fasihi wana nafasi mwafaka ya kuimarisha mbinu za utunzaji wa mazingira kwa kuboresha uhusiano wa kijamii na mazingira kwa ujumla.

## 7.3 Mahitimisho

Katika tasnifu hii, mwanya wa kiakademia uliozibwa ni kuongeza tahakiki kuhusiana na jinsi fasihi inashughulikia anthroposenia. Utafiti umechunguza aina za anthroposenia katika riwaya nne teule kwa kuongozwa na nguzo kuu za nadharia ya Uhakikimazingira. Baadhi ya aina za anthroposenia ambazo zimechunguzwa ni pamoja na binadamu, mawakala ya anthroposenia, matumizi ya vifaa na binadamu, vurugu dhidi ya mazingira na jiografia ya binadamu. Halafu mtafiti amehakiki mbinu zilizotumiwa kusawiri anthroposenia katika riwaya nne teule. Isitoshe, amehakiki mbinu kama vile taashira, taswira, ishara, majazi, tashtiti na tashihisi. Hatimaye, ametathmini rai za waandishi wa riwaya nne teule kuhusu jinsi ya kukabiliana na anthroposenia katika riwaya nne teule. Rai ambazo zimetolewa ni pamoja na matumizi ya vyombo vya habari, ukakamavu na kujitolea kwa binadamu, matumizi ya rasilimali asilia kama vile maji na maumbile, matumizi madhubuti ya mashairi na nyimbo, maandamano, elimu na usawa wa kijinsia.

## 7.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Kwa kuangazia mapendekezo ya utafiti wa hapo baadaye, katika mchakato wa utafiti huu, masuala kadhaa yaliibuka kutokana na baadhi ya changamoto zilizotokana na utafiti huu. Mtafiti anapendekeza kuwa utafiti kuhusu taswira na ufananisho wa anthroposenia katika kazi za fasihi unaweza kufanywa katika misingi ya kimazingira. Suala la wahusika na maadili ya mazingira linafaa kutiliwa maanani katika tafiti za hapo baadaye kwa lengo la kuonyesha jinsi maendeleo ya wahusika yanavyoonyesha mabadiliko ya kijamii na kimazingira. Mikakati ya uhifadhi wa mazingira na athari zake kwa wasomaji zinafaa kutathminiwa. Baadhi ya kaulimbiu za kijamii na kisiasa kuhusu mazingira zinafaa kutathminiwa katika misingi ya kimazingira. Uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi na fasihi ya kipindi kinacholandana na anthroposenia unafaa kuhakikiwa. Ushirikiano wa binadamu na mazingira katika anthroposenia unaweza kukadiriwa athari zao kwa mazingira. Uchunguzi wa njia za uendelevu na matumizi ya kazi za kisanaa katika kuimarisha weledi kuhusu anthroposenia unafaa kumulikwa. Isitoshe, maadili ya uhifadhi na masuala ya kijamii bila kusahau uanaharakati wa kazi za kisanaa ya anthroposenia yanafaa kuchunguzwa. Kimwavuli, mna mengi kuhusiana na anthroposenia hivyo haya ni mapendekezo tu ya kutoa mwanga ila si kwamba utafiti wa halafu umefungwa nayo.

## MAREJELEO


Aberbach, D. (2018). *The Bible and the 'Holy Poor' From the Tanakh to Les Miserables (1st ed.)*. Oxford: Routledge.

Ahmandi, M. (2024). *Towards an Ecocritical Theatre Playing the Anthropocene (1st ed.).* Routledge.

Albert, O. I. & Lawanson, T. (Eds.). (2019). *Urban Crises and Management in Africa: A Festschrift for Akin Mbogunje*. Pan-Afrcan University Press.

Alia, A. (2017). 'Ecocritical Post-Colonial Studies on Humans, Land and Animals.' Unpublished Masters Thesis (MA): University of Nothern Iowa.

Allen, R. C. (2011). *Global Economic History*. Oxford: Oxford University Press.

Amer, S. E. (2022). Literature and Ecology: Promoting an Eco-Consciousness through Children Literature. *International Journal of Language and Literary Studies*. 4(3), 192 – 201. http://doi.org/10.36892/ijlls.v4i3.933

Andermahr, S., Lovell, T. & Wolkowitz, C. (1997). *A Glossary of Feminist Theory*. London: Edward Arnord.

Angus, I. (2016). *Facing the Anthropocene*. New York: Monthly Review Press.

Appel, H. (2019). *The Licit Life of Capitalism: US Oil in Equatorial Guinea*. Durham: Duke University Press.

Arboleda, M. (2020). *Planetary Mine: Territories of Extraction Under Late Capitalism*. London: Verso.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi, Kenya: Longhorn Publishers.

BAKITA (2022). Kamusi Kuu ya Kiswahili (3rd ed.). Longhorn Publishers.

Ballard, S. (2023). *Art and Nature in the Anthropocene Planetary Aesthetics (1st ed.).* Routledge.

Bardhan, P. (2017). Corruption and Development: A Review of Issues. In Heidenheime, A. J. & Johnston, M. (Eds.), *Political Corruption Concepts and Contexts* (p. 321-338). University of California, Berkeley: Routledge.

Bergthaller, H. & Horn, E. (2020). *The Anthropocene: Key Issues for the Humanities (1st ed.)*. Routledge.

Bernard, T. O. (2002). *Research Methods in Anthropology: Qualitative and Quantitative Methods* (3rd Ed.). California: Alta Mira Press, Walnut Creek.

Bertens, H. (2024). *Literary Theory: The Basics (4th ed.)*. Routledge.

Bitanihiriwe, B. K. Y., Adebisi, T., Bunn, C., Ssewanyana, D., Darby, P. & Kitchin, P. J. (2022, Octomber, 7th). Gambling in Sub-Saharan Afrika: Traditional Forms and Emerging Technolojies. *Current Addiction Reports 9(1), 373 – 384, Springer Nature Article*.https://doi.org/10.1007/s40429-022-00449-0

Bladow, K. & Ladino, J. (Eds.). (2018). *Affective Ecocriticism: Emotion, Emdodiment, Environment*. Lincoln: University of Nebraska Press Lincoln and London.

Buell, L. (1996). "The Environmental Imagination: Thoreau, Nature Writing, and the Formation of American Culture". Cambridge. MA London, England: Havard University Press.

Buell, L. (2005). *The Future of Environmental Criticism: Environmental Crisis and Literary Study*. Malden: Malden Blackwell Publishers

Bunker, S. G. & Ciccantell, P. S. (2005). *Globalization and the Race for Resources*. Baltimore: Johns Hopkins University Press.

Burdon, P. D. (2023). *The Anthropocene: New Trajectories in Law (1st ed.)*. Routledge.

Burdon, P. D. & Martel, J. (Eds.). (2025). *The Routledge Handbook of Law and the Anthropocene (1st ed.)*. Routledge.

Butler, D. R. (Ed.). (2024). *The Anthropocene (1st ed.)*. Texas: Routledge.

Canty, J. M. (Ed.). (2025). *Ecological and Social Healing Multicultural Women's Voices (2nd ed.)*. Routledge.

Carvalho, V. M. & Gavioli, N. (Eds.). (2020). *Literature and Ethics in Contemporary Brazil*. Routledge.

Chacha, L. M. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi, Kenya: Africawide Network.

Chandler, D., Grove, K. & Wakefield, S. (Eds.). (2020). *Resilience in the Anthropocene: Governance and Politics at the End of the World (1st ed.)*. London: Routledge.

Clark, T. (2015). *Ecocriticism on the Edge The Anthropocene as a Threshold concept*. UK, London: Bloomsbury Academic An imprint of Bloomsbury Publishing Plc.

Claser, M. (2002). *Human & Nature Interaction in the Anthropocene. Potential of Social- Ecological Systems Analysis*. Makala kutoka http://www.oekm.de

Cohen, M. P. (2004). Blues in the Green: Ecocriticism Under Critique. *Journal Article of Environmental History 9(1) pp. 9-36*. Oxford University Press.

Collins, J. J. (Ed.). (2014). *The Oxford Handbook of Apocalyptic Literature*. New York, USA: Oxford University Press.

Coughlin, M. & Gephart, E. (2020). *Ecocriticism and the Anthropocene in Nineteenth –Century Art and Visual Culture*. New York, NY and London: Routledge Taylor & Francis Group.

Cox, C. R. (2015). Faulty Presuppositions and False Dichotomies: The Problematic Nature of 'the Anthropocene'. *Telos* 2015: 59 – 81, https://doi.org.10.3817/0915172059

Creswell, J.W. (2014). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches (4th ed.)*. United States of America: SAGE Publications, Inc.

Crutzen, P. (2008). *Geology of Mankind. The Anthropocene*. Nature 415: 23. Makala kutoka http://www.oekm.de

Curry, P. (2011). *Ecological Ethics: An Introduction*. (2nd ed.). Cambridge, UK & Malden, MA: Polity Press.

Davis, H. (2015). Life and Death in the Anthropocene: A Short history of Plastic. In: Heather, Davis and Turpin, Etienne (Eds.). *Art in the Anthropocene:*

*Encounters Among Aesthetics, Politics, Environment and Epistemologies.* London: Open Humanities Press, pp. 347 – 358.

Davis, H. & Turpin, E. (Eds.). (2015). *Art in the Anthropocene Encounters Among Aesthetics, Politics, Environments and Epistemologies*. Open Humanities Press.

De Cristafora, D. & Cordle, D. (2018). Introduction: The Literature of the Anthropocene. *C21 Literature: Journal of 21st – century Writings*, 6(1): 1. Pp. 1 – 6, DOI: https://doi.org/10.16995/c21.73

DeLoughrey, E. (2019). "Towards a Critical Ocean Studies for the Anthropocene." *English Language Notes* 57(1): 21 – 36. https://www.muse.jhu.edu/article/724603

Demos, T. J. (2017). *Against the Anthropocene: Visual Culture and Environment Today*. Berlin: Sternberg Press.

Doherty, P. (2022). Reading Children's Literature in the Anthropocene: the Representation of 'nature' in Ursula K. Le Guin's Earthsea Fiction. *Children's Literature in Education* 55, 248 – 262. https://doi.org/10.1007/s/0583-022-09490-2

Dreyer, J. S. (2007). Religion and State in Postcolonial Africa: Challenges and Opportunities. Reserchgate. https://www.researchgate.net/publication/237404462 Accessed on 10/10/2022

Dyke, V. F. (2025). *Conservation in the Anthropocene Reshaping Interaction with Nature (1st ed.)*. Routledge.

Economides, L. (2025). *Wild Anthropocene Literature and Multispecies Justice in Deep Time (1st ed.)*. Montana: Routledge.

Ellis, E. C. (2018). *Anthropocene A Very Short Introduction*. Oxford: United Kingdom. Oxford University Press.

Estock, S. C. (2001). *A Report Card on Ecocriticism*. AUMLA.

Estock, S. C. (2005). *Shakespear and Ecocriticism: An Analysis of 'Home' and 'Power'* in Lear.

Falola, T. (2024a). *Daily Life in Colonial Africa (1st ed.).* Bloomsbury Publishing.

Falola, T. (2024b). *Decolonizing African History*. African Books Collective.

Feder, H. (Ed.). (2021). *Close Reading the Anthropocene (1st ed.)*. Routledge.

Filipova, L. (2023). *Ecocriticism and the Sense of Place (1st ed.)*. Routledge.

Fiedorczuk, J., Newell, M., Quetchenbach, B. & Tierney, O. (Eds.). (2023). *The Routledge Companion to Ecopoetics (1st ed.)*. Routledge.

Franklin, M. I. (2012). *Understanding Research: Coping with the Quantitative-Qualitative Divide*. London and New York: Routledge.

Frantzen, M. K. & Bjering, J. (2020). Ecology, Capitalism and Waste: From Hyperobject to Hyperabject. *SAGE Journal of Theory, Culture & Society*, 37(6), 87 – 109.

Fuchs, C. (2023). *Media, Economy and Society: A Critical Introduction (1st ed.).* Routledge.

Fulekar, M. H. & Pathak, B. (2018). *Environmental Nanotechnology (1st ed.)*. CRS Press.

Garrard, G. (2004). *Ecocriticism*. New York, USA: Tylor & Francis Group, Routledge.

Garrard, G. (2007). Ecocriticism and Education for Sustainability. *In Pedalogy: Critical Approaches to Teaching Literature, Language, Composition & Culture*, Vol. 7(3): 359 – 386. Duke University Press.

Garrard, G. (2023). *Ecocriticism (3rd ed.)*. Routledge.

Gee, J. P., & Handford, M. (Eds.). (2012). *The Routledge Handbook of Discourse Analysis*. New York, NY: Routledge.

Gichure, R. W. (2017). 'Effects of Drought on Crop Production and Coping Mechanisms Undertaken by Small Scale Farmers: A Case Study of Makueni

County, Kenya.' Unpublished Masters Thesis (MA). University of Nairobi.

Gill, B. (2016). *Race, Nature and Accumulation*. PhD Dissertation, University of Toronto.

Glotfelty, C. na Fromm, H. (Eds.). (1996). *Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*. Athens and London: The University of Georgia Press.

Gregory, T. (2021). *Pornography, Indigeneity and Neocolonialism (1st ed.).* Routledge.

Hall, M. (Ed.). (2010). *Restoration and History: The Search for a Usable Environment Past*. New York and London: Routledge.

Head, L. (2018). *Hope and Grief in the Anthropocene: Re-conceptualising human -naturerelations (1st ed.)*. Routledge.

Heise, U. K. (2006). *Greening English:Recent Introductions to Ecocriticism.* Contemporary Literature.

Heise, U. K. (2008). *Sense of Place and Sense of Planet: The Environmental Imagination of the Global*. New York, NY: Oxford University Press.

Heise, U.K. (Mh.) (2016). *Literatures, Cultures and the Environment*. Palgrave: Macmillan.

Horacio, D. C. (May, 2015). Environmental Violence and Its Consequences. *Latin American Perspectives Journal*. DOI:10.1177/0094582x15585116

Howarth, B. R. (1996). Climate Changes and Overlapping Generations. *Journal of Contemporary Economic Policy, 14(4). Pg. 100-111*. https://doi.org/10.1111/j.1465-7287.1996.tb00637.x

Huggan, G. & Tiffin, H. (2010). *Postcolonial Ecocriticism: Literature, Animals, Environment*. London and New York, NY: Routledge.

Hujibens, E. H. (2023). *Developing Earthly Attachments in the Anthropocene (1st ed.).* Routledge.

Hupkens, P. & Durbeck, G. (Eds.). (2023). *Narratives of Scale in the Anthropocene Imagining Human Responsibility in an Age of Scalar Complexity (1st ed.).* Routledge.

Iheka, C. N. (2015). 'African Literature and the Environment: A Study in Postcolonial Ecocriticism'. Unpublished PhD Thesis: Michigan State University.

Issberner, L. R. & Lena, P. (Eds.). (2018). *Brazil in the Anthropocene: Conflicts between predatory development and environmental policies (1st ed.).* Routledge.

John, B. N. (2022). Usawiri wa Lugha ya Ishara Iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani. Jarida la Fahari ya Kiswahili,* 1(1), 66 – 76.

Kallman, M & Dini, R. (2017). *A Macat Analysis of Michael Foucault's Discipline and Punish.* London: Routledge.

Kesting, S., Negru, I. & Silvestri, P. (Eds.). (2022). *The Gift in the Economy and Society: Perspectives from Institutional Economics and Other Social Sciences (1st ed.).* Routledge.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Kenya. Vide-Muwa Publishers.

Khamis, S. A. M. (2004). Images of Love in the Swahili Taarab Lyrics: Local Aspects and Global Influence. *Nordic Journal of African Studies*, 13(1), 30 – 64.

Kobia, J. (2007). 'Tumbombele Mla Misitu', katika Mbatiah, M. (mh) uk. 137 – 153. Nairobi: Focus Publishers Limited.

Koci, V., Rumi, T, Dao, P. & Duc. P. (Eds.). (2017). *Environmental Technology and Innovations Proceedings of the 1st International Conference on Evironmental Technlogy and Innovations (Ho Chi Minh City, Vietnam, 23 – 25 November, 2016) (1st ed.).* CRC Press.

Kumar, R. (2014). *Research Methodology*. (4th ed.). London, Thousand Oaks, New Delhi: India. Sage Publications.

Kusserow, K. (2018). "Welcome Remarks." *Picture Ecology: Art and Ecocriticism in Planetary Perspective Symposium*. Princeton University: Princeton University Press, December 7.

Kwambai, M., Chai, F., Nabea, W. Na Bowen, D. (2018). Uwakilishi na Uamilifu wa Utopia katika Riwaya za Mkangi: Walenisi na Mafuta. *Coretrain Journal of Social Sciences, Education and Humanities,* Vol. 1(1), pp. 237 – 252. ISSN: 2363 – 2470.

LaMothe, R. (2024). *A Political Psychoanalysis for the Anthropocene Age The Fierce Urgency of Now (1st ed.*). Routledge.

Lara, S., Peta, T. & Denise, V. (Eds.). (2018). *Feminist Ecologies: Changing Environments in the Anthropocene*. Cham: Switzerland. Palgrave Macmillan Publishers.

Larsen, E., Moss, M. S. & Skjelsbaek, I. (Eds.) (2023). *Gender Equality and Nation Branding in the Nordic Region (1st ed.)*. Routledge.

Larsson, et al. (2019). Legal Definitions of the Environment and of Environmental Damage. Research *Gate: Stockholm Institute for Scandinavian Law 1957 -2009*. https://www.researchgate.net/publication/336315959

Lundberg, A. (2019). Color Meanings and the Art of Using Color Symbolism. *WWW-sivusto. Saatavissa: https://99designs.com/blog/tips/color-meanings/[viitattu 23.3.2022].*

Maathai, W. (2009). *The Challenge for Africa*. Britain: William Heineman.

Magharibi, L. (2017). *Athari za Ukame*. Available at https://sw.eferrit.com/athari-za-ukame: Accessed on 13/11/2022

Maier, D. S., Donhauser, J. & Weber, M. (Eds.). (2025). *Disruptive Innovations and the Environmental Crisis; Ethical, Practical, and Sociopolitical Concerns (1st ed.).* Ohio: Routledge.

Makokha TKS, Kahaji, E., & Dipio, D. (Eds.). (2011). *In East African Literature: Essays on Written and Oral Traditions*. Logus Verlag Berlin.

Mark, K. (2023). *Research Methods for Environmental Studies A Social Science Approach (2nd ed.)*. Routledge.

Mbatiah, M. (2019). "Dhima ya Fasihi katika Mshikamano wa Kitaifa: Tathmini ya Tungo za Tom Olali" katika *Mwanga wa Lugha*. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur. 1 – 14.

Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*. Nairobi, Kenya: Marimba Publishers.

Mbogo, E. (1996). *Vipuli Vya Figo*. Nairobi, Kenya: East African Educational Publishers.

Mbogo, E. (2002). *Bustani ya Edeni*. Nairobi, Kenya: Longhorn Publishers (K).

Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A. (2015). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Kenya. Longhorn Publishers.

Mdee, S., Shafi, A., Kiango, J. Na Njogu, K. (2009). *Kamusi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya. English Press.

Mhango, P. na Bulaya, J. (2022). Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili. *MULIKA Na. 38*, uk 105 – 125.

Michael, S. (2009). *Conteporary Theories of Religion*. Roultledge.

Mitchell, S. (2007). *The History of News (3rd ed.).* Oxford University Press.

Mkangi, G.C.K. (1984). *Mafuta*. Kijabe Street, Nairobi, Kenya: Heinamann Educational Books (East Africa).

Mkangi, G.C.K. (1995). *Walenisi*. Nairobi, Kenya: East African Educational Publishers.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi, Kenya: Sasa Sema Publishers.

Moore, J. W. (2015). *Capitalism in the Web of Life. Ecology and the Accumulation of Capital*. London: Verso.

Moore, J. W. (Eds.). (2016). *Anthroposecene or Capitalocene? Nature, History, and the Crisis of Capitalism*. Oakland, CA: USA. KAIROS PM Press.

Moore, J. W. (2017). The Capitalocene, Part I: On the Nature and Origins of Our Ecological Crisis. *The Journal of Peasant Studies*, 44(3), 594 – 630, https://doi.org/10.1080/03066150.2016.1235036

Moore, J. W. (2018). The Capitalocene Part II: Accumulation by Appropriation and the Centrality of Unpaid Work/Energy. *The Journal of Peasant Studies*, 45(2), 237 – 279 https://doi.org/10.1080/03066150.2016.1272587

Morton, T. (2007). *Ecology Without Nature: Rethinking Environmnetal Aesthetics*. United States New York, NY: Havard University Press.

Morton, T. (2012). *The Ecological Thought*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Morton, T. (2013). *Hyperobjects: Philosophy and Ecology after the End of the World.* Minneapolis: University of Minnesota Press.

Moseley, W. G. & Otiso, K. M. (Eds.). (2023). *Debating African Issues: Conversations Under the Palaver Tree*. USA: New York (NY), Routledge.

Mosha, D. (2017). Lugha ya Ishara katika Dhifa za Jikoni Nchini Tanzania katika *Kioo Cha Lugha*, 15(1), Dar es Salaam: TUKI.

Mostafanezhad, M. & Norum, R. (Eds.). (2021). *Anthropocene Ecologies: Entanglementsof Tourism, Nature and Imagination (1st ed.)*. Routledge.

Mpesha, T. (2016). Nadharia za Tafsiri katika Jilala, H, (Mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing.

Mukherjee, P. (2010). *Postcolonial Environments: Nature, Culture and the Contemporary Indian Novel in English*. UK: Palgrave Macmillan.

Musembi, N. N. (2019). "Taswira kama Kurunzi ya Kuangazia Uozo katika Jamii ya Kisasa:Mfano kutoka Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*" katika *Mwanga wa Lugha*. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur. 93 – 104.

Mvumbi, F. N. & Ngumbi, E. K. (2015). *Companion to research methodology: focus on humanities, education and social science.* Nairobi: CU

Mwaniki, J. M. (2019). 'Athari za Mtagusano kati ya Jamii na Ekolojia Katika Ushairi wa Kithaka Wa Mberia: Bara Jingine na Rangi ya Anga'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mwirabua, A. (2014). 'Ukoloni Mamboleo na Utandawazi Katika Tamthilia Teule'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Nabea, W. & Ngugi, P. (2012). Kiswahili Poetic Aesthetics: From the General Identities to the African Prodigy. *Journal of Literary Studies; Routledge,* 28(2), 83 – 98. ISSN 0256-4718

Nabea, W. (2021). The Role of Prostitutes in the Political Economy of Corruption in Ben Mtobwa's *Pesa Zako Zinanuka* and *Dares Salaam Usiku*. *Journal of Literary Studies; Routledge*, 37(4), 1 – 13. ISSN 0256-4718

Nanda, V. P. (2011). *Climate change and environmental ethics*. New Jersey: Transaction Publishers.

Nayar, K. P. (2010). *Contemporary Literary and Cultural Theory: From Structuralism to Ecocriticism*. Delhi, India: Longman.

Ndalu, A. E., Babusa, H. & Mirikau, A. S. (2014). *Kamusi Teule ya Kiswahili: Kilele cha Lugha*. Nairobi, Kenya: East African Publishers.

Ngugi, P. & Nabea, W. (2011). Children Literature in Kiswahili: A Stylistic Approach. In J.K. S. Makokha, E. Kabaji & D. Dipio (Eds.)., *East African Literature: Essays on Written and Oral Traditions* (pp. 223 – 244). Logos Verlag Berlin.

Njeru, M. K., Kobia, J. M. & Musyimi, D. M. (2022). Motifu ya Ukame katika Tamthilia za Janga la Werevu (Mohamed, 2011) na Majira ya Utasa (Arege, 2015). *East African Journal of Swahili Studies,* 5(1), 183-195. https://doi.org/10.37284/eajes.5.1.733.

Njiru, H. M. (2015). 'Eco-Techno-Cosmopolitanism: Education, Inner Change and Practice in the Contemporary U.S. Eco-Disaster Novel.' Unpublished PhD Thesis: Miami University.

Njogu, K. na Chimerah, R; (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Nkonge, E. (2014). 'Ujumi Mweusi Katika Tamthilia za Nitaolewa Nikipenda na Mukwava wa Uhehe'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Swahili hub.

Ogude, J. & Mushonga, T. (Eds.). (2023). *Environmental Humanities of Extraction in Africa Poetics and Politics of Exploitation (1st ed.).* Routledge.

Okuku, W. M. (2010). "Uchanganuzi wa Kiisimu wa Baadhi ya Matini za Kiswahili: Mtazamo wa Pragmatiki Leksika." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Oliver, L. (2016). *The Postcolonial Intellectual: Ngugi wa Thiong'o in Context*. New York, NY: USA. Routledge Taylor & Francis Group.

Omolo, K. (2002). "Political Ethnicity in the Democratisation Process in Kenya." *AfricanStudies*, 61(2), pp. 209 – 221.

Onchangu, R. N. (2013). "Mtindo Katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ong, M. J. & Whittle, M. (2024). *Global Literature and the Environment (1st ed.).* Routledge.

Ong'utte, N. R. (2014). 'Uhakiki wa Suala la Uhifadhi wa Mazingira Katika Tanzu Teule za Fasihi ya Kiswahili ya Milenia Mpya'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno (Haijachapishwa).

Ong'utte, N. R. na Nabeta, S. N. (2014). 'Literary Environmentalism: An Ecocritique of Kiswahili Literature'. *International Journal of Ecology and Ecosolution,* Vol. 1 (2), pp. 29– 41, August 2014 Review.

Outka, P. (2013). *Race and Nature from Transcendentalism to the Harlem Renaissance*. United States, New York, NY: Palgrave Macmillan.

Palys, T. (2008). *Purposive Sampling, the Sage Encyclopaedia of Oualitative Research Methods*. Sage Publications.

Paszkiewicz, K. & Ruthven, A. (Eds.). (2025). *Cinema of/for the Anthropocene Affect, Ecology, and More-Than-Human Kinship (1st ed.)*. Balearic Islands: Routledge.

Pedersen, H., Windsor, S., Knutsson, B., Sanders, D., Wals, A. & Franck, O. (Eds.). (2024).*Education for Sustainable Development in the 'Capitalocene' (1st ed.).* Routledge.

Pentreath, R. J. (2021). *Nuclear Power, Man and the Environment (1st ed.).* Routledge.

Philips, D. (2003). *The Truth of Ecology: Nature, Culture, and Literature in America*. Oxford: Oxford University Press.

Qiping, L. & Quan, Z. (2022). The Agentic Force of Clothing in Amy Tan's *The Valley of Amazement. Journal of Language, Literature and Culture*, Vol. 69(1), 19-33, https://doi.org/10.1080/20512856.2022.2071812

Quick, P. S. (2004). 'An Ecocritical Approach to the Southern Novels of Cormac Mccarthy.' Unpublished PhD Thesis: University of Georgia.

Reid, A. & Scott, W. (Eds.). (2008). *Researching Education and the Environment Retrospect and Prospect (1st ed.)*. Routledge.

Reno, S. T. (Ed.). (2022). *The Anthropocene Approaches and Contexts for Literature and the Humanities (1st ed.)*. Routledge.

Riccardo, R. (2017). *Ukame-Wikipedia, Kamusi Elezo Huru*. Available at https://sw.wikipedia.org/wiki/ukame: Accessed on 7/12/2022.

Roberts, L. D. (2015). Ethical issues in conducting qualitative research in online communities. *Qualitative Research in Psychology*, 12, 314–325.

Robert, T.T. & Christine, M. B. (Eds.). (2016). *Ecocriticism and Geocriticism: Overlapping Territories in Environmental and Spacial Literary Studies*. New York, NY: Palgrave Macmillan.

Rueckert, W. (1978). Literature and Ecology: An Experiment in Ecocriticism. *Lowa Review* 9, 71-86.

Rueckert, W. (1996). Literature and Ecology: Experimental Ecocriticism. In Glotfelty, C. and Fromm, H. (Ed.), *Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology* (pp. 105-124) Athens and London: The University of Georgia Press.

Sabula, A. M. (2014). 'Nafasi ya Wanawake katika Uhifadhi wa Mazingira katika Riwaya ya Nakuruto: Mtazamo wa Fasihi ya Ufeministi wa Ekolojia'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Said, A. M. (1988). *Kiza Katika Nuru*. Oxford: Oxford University Press.

Said, A. M. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi, Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.

Scott, K. (2012). *Ecopoetics: The Language of Nature, the Nature of Language*. Massachusetts: University of Massachusetts Press.

Secretan, D. (2019). *Classicism (1st ed.).* Routledge.

Seif, D. G. (2022). Nyimbo za Kiasili Zinavyoimarisha Mafunzo ya Jadi Nchini Tanzania. *Jarida la Fahari ya Kiswahili,* 1(1), 34 – 53.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi, Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: Kampuni ya Utamaduni na Uchapishaji.

Sidang', A. (2023). *Parliament of Owls*. East African Educational Publishers.

Simel, A. (2015). 'The Effects of Drought and Famine on Agricultural Production, Living Standards and Education, Status of the People of Kitui County, Kenya.' Unpublished Masters Thesis (MA): University of Nairobi.

Simon, L. L. & Mark, A. M. (2018). *The Human Planet How We Created the Anthropocene*. A Pelican Book. Penguin Books Publisher.

Simpson, S. (2021). The Year's Work in Stylistics. *Language and Literature: International Journal of Stylistics,* 29(4), 454 – 479.

Siundu, G. (2011). Metaphor and the Economy of Hope in Jared Angira's *Lament of the Silent & Other Poems* (2004). In J.K. S. Makokha, E. Kabaji & D. Dipio

(Eds.)., *East African Literature: Essays on Written and Oral Traditions* (pp. 245 – 258). Logos Verlag Berlin.

Sklair, L. (Ed.). (2022). *The Anthropocene in Global Media: Neutralizing the risk (1st ed.).* Routledge.

Slovic, S. (2009). *A Booklist of International Environmental Literature*. World Literature Today Online. Oklahoma State University, Oklahoma.

Slovic, S., Rangarajan, S. & Sarveswaran, V. (Eds.). (2020). *Routledge Handbook of Ecocriticism and Environmental Communication (1st ed.)*. Routledge.

Smith, J. D. (2007). *A Culture of Corruption: Everyday Deception and Popular Discontent in Nigeria*. New Jersey: United Kingdom. Princeton University Press.

Smith, A. J. & Wilson, A. (2024). *Radical Ecology in the Face of the Anthropocene Extinction A New and Urgent Philosophy for Complexity in the Social Sciences (1st ed.).* Routledge.

Sritama, C. (2022, Nov. 16th). Off-Shore Aesthetics and Waste in the Ship-Breaking Literature of Bangladesh. South Asian Review Article. Taylor & Francis Group. https://doi.org/10.1080/02759527.2022.2145745

Stevenson, R. B., Brody, M., Justin, D. & Wals, A. E. J. (Eds.). (2013). *International Handbook of Research on Environmental Education (1st ed.)*. Routledge.

Swaleh, A. & Timammy, R. (2019). "Literature as Medium for Moral Instruction: A Swahili/Islamic Analysis of Ahmad Nassir's Utenzi wa Mtu ni Utu" katika *Mwanga wa Lugha*. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur. 17 – 30.

Tan, C. (2019). 'An Ecocritical Study of J. G. Ballard's Climate Fiction Novels.' Unpublished PhD Thesis: Pamukkale University.

TATAKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.

Thiong'o, N. (1987). *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Timammy, R. (2020). “Tamathali za Usemi na Taswira katika Utenzi wa UKIMWI wa Zimwi” katika *Mwanga wa Lugha*. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur. 15 – 32.

TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary*. (3rd ed.). Mauritius. Book Printing Services.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Kenya. Oxford Press.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (3rd ed.). Nairobi: Kenya. Oxford University Press.

Turner, K. & Freedman, B. (2010). Music and Environmental Studies. *The Journal of Environmnetal Education,* 36(2004), 42 – 52. https://doi.org/10.3200/JOEE.36.1.45-52

Vermeulen, P. (2020). *Literature and the Anthropocene (1st ed.)*. Routledge.

Vonyoli, A. J. (2004). “Hadithi kama Chombo cha Maudhui katika Fasihi. Uchanganuzi katika Riwaya za Mkangi, Mafuta (1984) na Walenisi (1995).” Tasnifu ya Uzamili (M.A.) Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wa Thiong’o, N. (2009). *Re-membering Africa*. Nairobi: Kenya. East African Publisher.

Waithiru, A. K. (2019). ‘Matumizi ya Taashira Kuangaza Jiografia na Utandawazi Katika Tamthilia za *Zilizala* na *Sudana’*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Laikipia (Haijachapishwa).

Waithiru, A., Onyango, J., & Wendo, N. (2020). Tathmini ya Kipengele cha Taashira za Wahusika katika Tamthilia ya Kimani Njogu: Mfano wa Zilizala. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*. ISSN: 2663-9289

Waithiru, A. K., Nabea, W. K., na Onyango, J. O. (2021). “Uamilifu wa Taashira Katika Tamthilia za *Zilizala* na *Sudana”* katika *Mwanga wa Lugha*. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur. 43 – 54.

Waithiru, A. K. (2022a). Symbols of the Sentient House of Usher: An Ecocritic Approach *EastAfrican Journal of Education Studies*, 5(2), 369-376. https://doi.org/10.37284/eajes.5.2.812.

Waithiru, A. K. (2022b). An Evaluation of Environmental Symbolism used in Children Literature: Case Study of *Kijiji Cha Ukame* and *Mazingira Maridadi*. *East African Journal of Education Studies*, 5(3), 1-10. https://doi.org/10.37284/eajes.5.3.846.

Waithiru, A. K. (2022c). Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya *Sudana*. *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), 124-130. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010.

Waithiru, A. K. (2022d). "Tathmini ya Binadamu na Mazingira katika Riwaya ya *Nakuruto*" katika *Mwanga wa Lugha: Juzuu la 7(2).* Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur. 163 – 171.

Waithiru, A. K., Wandera, S. S. na Onyango, O. J. (2023). "Tathmini ya Anthropomofiki katika Riwaya ya Shamba la Wanyama" katika *Mulika: Juzuu la 42(2).* Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 217 – 237.

Walder, D. (2011). *Postcolonial Nostalgias: Writing, Representation, and Memory*. New York: Routledge.

Wallenhorst, N. & Wulf, C. (Eds.). (2023). *Handbook of the Anthropocene Humans between Heritage and Future (1st ed.)*. Springer Publishers.

Walter, J. (2013). *River of Dark Dreams*. Cambridge, MA: Havard University Press.

Wamitila, K. W. (1988). "Towards Unlocking Katama Mkangi's *Walenisi*. A Case of Parabolic Narrative?" katika *Kiswahili Juzuu* (61)1999, Jarida la TUKI, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.

Wamitila, K.W. (2002).*Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publisher.

Wamitila, K. W. (2022). *Kamusi Pevu ya Kiswahili (3rd ed.).* Nairobi: Vide-Muwa Publisher.

Watson, N. R. & Watson, R. (2007). *Back to Nature: The Green and the Real in the Late Renaissance*. Pennsylvani: University of Pennsylvania Press.

White, J. & Whitlock, G. (Eds.). (2021). *Life Writing in the Anthropocene (1st ed.)*. Routledge.

Yegon, M. C. (2016). 'Uwasilishaji wa Ufeministi Kinzani katika Kiswahili kupitia Tafsiri: Tathmini ya Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*.' Tasnifu ya Umahiri Chuo Kikuu cha Nairobi.

Yin, K. (2014). *Case study research: Design and methods*. Thousand Oaks: Sage Publications.

(10)

# LAIKIPIA UNIVERSITY

P.O. Box 1100-20300,
NYAHURURU,
KENYA

TEL: +254-(0) 20 2671779, 20-2671771;
Cell: +254 0729285902, 0729281902
bpgs@laikipia.ac.ke; www.laikipia.ac.ke

**OFFICE OF DIRECTOR**
**GRADUATE SCHOOL**

REF: MDK32/2614/20

31st May, 2023

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: ANTONY KAGO WAITHIRU – REG. MDK32/2614/20**

The above mentioned is a Postgraduate student of Laikipia University undertaking a Doctor of Philosophy (Kiswahili and Communication Studies ) degree at the Department of Literary and Communication Studies, School of Humanities & Development Studies. His Research Proposal entitled, **ANTHROPOSENIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI ZA BUSTANI YA EDENI, VIPULI VYA FIGO, MAFUTA NA WALENISI**, has been Examined and Accepted by the Board of Graduate School and is hereby authorized to conduct her research.

Any assistance accorded to her will highly be appreciated.
Thank you.

Prof Felicia Yieke, PhD
**Director – Graduate School**

*Vision: A University for Valued Transformation of Society*
*Mission: To serve students and society through research, education, scholarship, training, innovation, outreach and consultancy*
Laikipia University is Certified to ISO 9001:2015 and ISO/IEC 27001:2013

LAIKIPIA UNIVERSITY
P.O. Box 1100-20300,
NYAHURURU,
KENYA
TEL: +254-(0) 20 2696596;
Cell: +254 713-552761/
lu-ierc@laikipia.ac.ke; www.laikipia.ac.ke

# INSTITUTIONAL SCIENTIFIC ETHICS REVIEW COMMITTEE

Ref: LU/APP/40/2023 6th July, 2023

Antony Kago Waithiru
P. O. 120 – 20115,
**EGERTON**

Dear Mr. A. Kago,
**RE: Anthroposcnia katika Riwaya teule za Kiswahili za *Bustani ya Edeni, Vipuli vya Figo, Mafuta* na *Walenisi***
This is to inform you that Laikipia University Institutional Scientific Ethics Review Committee (LU-ISERC) has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **LU/APP/40/2023.** The approval period is **6th July, 2023 – 5th July, 2024.** This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used;
ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by Laikipia University Institutional Scientific Ethics Review Committee;
iii. Death and life-threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to Laikipia University Institutional Scientific Ethics Review Committee within 72 hours of notification;
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to Laikipia University Institutional Scientific Ethics Review Committee within 72 hours;
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions;



*Vision:* *A University for Valued Transformation of Society*
*Mission:* *To serve students and society through research, education, scholarship, training, innovation, outreach and consultancy*
Laikipia University is ISO 9001:2015 and ISO/IEC 27001:2013 Certified

vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal and

vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to Laikipia University Institutional Scientific Ethics Review Committee.

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://research-portal.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely

Prof. Charles Nguta PhD

**Chairman - Laikipia University Institutional Scientific Ethics Review Committee**



***Vision:*** *A University for Valued Transformation of Society*
***Mission:*** *To serve students and society through research, education, scholarship, training, innovation, outreach and consultancy*
Laikipia University is ISO 9001:2015 and ISO/IEC 27001:2013 Certified

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **211065**

Date of Issue: **12/December/2023**

# RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Mr.. ANTONY KAGO WAITHIRU of Laikipia University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in on the topic: ANTHROPOSENIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI ZA BUSTANI YA EDENI, VIPULI VYA FIGO, MAFUTA NA WALENISI for the period ending : 12/December/2024.**

License No: **NACOSTI/P/23/31712**

**211065**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**

Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

## CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
   i. Endanger national security
   ii. Adversely affect the lives of Kenyans
   iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
   iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
   v. Adversely affect the environment
   vi. Adversely affect the rights of communities
   vii. Endanger public safety and national cohesion
   viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke